MASHAURI
juu ya
MALEZI
katika
KARNE YA KIDIGITALI

KUZAA NA KULEA

ANGALIA VITABU VINGINE VYA KISWAHILI KWENYE WEBSITE

MAARIFAMTANDAONI.COM

ASANTE KWA MWENYEZI MUNGU NA WASOMAJI, WAANDISHI, WAHARIRI, WAHAKIKI, WAHAMASISHAJI, WASHAURI NA WANAUFUNDI

Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani
Daniel Masaka-Kisii, Kenya
Bettie Magesa -Muasya-Nairobi, Kenya
Suzana Nyakrere-Rorya, Tanzania
Stephen Letta-Masasi, Tanzania
Kwandu Kasiri-Kibaha, Tanzania
Mbusi Mpagalushu-Bariadi, Tanzania
Innocent Wayoga-Dar-Es-Salaam, Tanzania
David Masaka-North Carolina, USA

–ALFABETI ZA MALEZI YA WATOTO au mzazi wa karne ya 21
(Tusaidie kuedit zaidi, tunahitaji Msaada -asante)

1. (The main thing, is to keep the main thing, the main thing)

JAMBO MUHIMU NI KUFANYA, JAMBO MUHIMU KUWA JAMBO MUHIMU

2. MTOTO AKIWA TUMBONI MWA MAMA
3. HATUA ZA KUKUA ZA MTOTO
4.WATOTO KATIKA BIBLIA
5.MAZIWA YA NG'OMBE AU MAZIWA YA MAMA
6. MTOTO SHULENI
7. KWANINI MUNGU ALITUPATIA WATOTO
8. UGUMU WA KAZI YA UZAZI
9. ELIMU YA NGONO KWA VIJANA
10. MAOMBI YA NYUMBANI (IBADA)
11 TARATIBU NYINGINE ZA NYUMBANI
12.MAWASILIANO NA WATOTO
13.NDOA TAKATIFU
14.TALAKA NA MATOKEO YAKE
15.MABIBI NA MABABU NA WALEZI WENGINE
16.KUWEKA VIWANGO KWENYE FAMILIA (FAMILY VALUES)
17 . WATOTO AMBAO NI WATU WAZIMA
18.KUKATA KITOVU CHA MTOTO
19. WATOTO AMBAO NI WATU WAZIMA NA WANAISHI NYUMBANI
20. AFYA YA WATOTO
21. WAKWE NA WAZAZI WENZA (afya)
22. BABA NA MALEZI YA WATOTO
23. MAMA NA MALEZI YA WATOTO
24. KUCHAGUA MWENZI WA MAISHA
25. BURUDANI, MICHEZO, NA MARAFIKI
26. MAGONJWA YALETWAYO NA FASHENI (IKKCW)
27. KUADABISHA
28. UMASIKINI NA MAZINGIRA MAGUMU YA MTOTO
29. KUSAIDIA KAZI, KUHUDUMIA NA KUFUNDISHA USTADI NA UJASILIAMALI
30. UNYANYASAJI WATOTO (IKKCW)
31. MUZIKI, UCHAWI NA MENGINEYO
32. WATOTO NA VYOMBO VYA HABARI NA TEKNOLOJIA (IKKCW)
33.WAZAZI SOLEMBA (Single parenting).
34. KUFUNDISHA, WATOTO NYUMBANI
35. MIFANO YA KAZI AMBAZO UNAWEZA KUWAPA WATOTO KUTOKANA NA UMRI
36. NENO LA MUNGU
37. MAOMBI
38. a. MAMBO zaidi ya 101, TUNASHAURI UFANYE NA WATOTO WAKO
    b. Mambo 20 yanayosaidia Tabia njema kwa watoto

39. AFYA YA wazazi
40 KUKUZA MTOTO WA KIUME AWE KIONGOZI
41.KUKUZA MTOTO WA KIKE KUTOKANA NA MITHALI 31 (IKKCW)
42. HITIMISHO LA JAMBO MUHIMU LA MALEZI YA WAZAZI.

A. Maswali na majibu ya wazazi au watoto

B.Dondoo za Huduma mbali mbali

Kwa kutumia saa moja kila siku kujisomea mtu binafsi, siku saba kwa juma, siku 365 kila mwaka, mtu anaweza kujifunza kwa kasi ile ile kama mwanafunzi aliye shuleni muda wote. Na kwa kutumia saa moja kila siku kwa kujifunza, mtu anaweza kuwa mtaalamu kwa somo lolote alilolichagua katika muda wa miaka mitatu hadi mitano. Hebu somo letu liwe Neno la Mungu maana ndiyo kitabu kikuu cha malezi ya watoto. Watoto hutofautiana sana hivyo tunavyolea mtoto mmoja ni tofauti kwa kiasi fulani na mtoto mwingine kutokana na haiba na karama zao kuwa tofauti. Hebu tuchukue muda kusoma na kutenda malezi mema ya watoto, maana hakuna aliyefika kila mtu ana masumbuko ya aina fulani na fani hiyo. Mtu mwingine amefanunua kulea (parenting) ni mwenye dhambi mmoja kumlea mwenye dhambi mwingine. Nia ya mzazi ni kumwezesha mtoto kuishi bila yeye, ajitegemee kwa mambo yahusuyo mwili, roho, akili, jamii, na hata uchumi.

Dibaji

Dunia ni ngumu. Pambano kuu baina ya Shetani na Mungu au ubaya na wema linaendelea masaa 24 ya kila siku na siku zote 7 za juma. Shetani alipoingia kibaruani (punch in) hajatoka (punch out). Katika kushughulika na wanadamu shetani hajawaacha watoto. Ameendeleza mikakati ya kuwaharibu watoto kama ambavyo amefanya na kwa watu wazima. Sasa ana muda mfupi sana kutoka na unabii wa Neno la Mungu wa Danieli 2, 7, 8 na 9 ni wakati wa kujitayarisha. Si wakati wa kuwa hofu, kwa taratibu tunamkabidhi Mungu kila kitu

Kuna makundi matatu ya watoto. Wale wa mazingira magumu sana wanasumbuliwa na kunyanyaswa na utawala mbaya wa wazazi walezi au jumuiya (hawa wanatutia huzuni) na wale wanaodeka na ubinafsi, kujifikiria wenyewe, kusumbua, au kutawala wazazi, na kutaka wazazi wawatii. Utii ndiyo somo la kwanza la muhimu kwa mtoto, na kisha hufuata ratiba, mpangilio, kuhudumia, kutawala nafsi, kuwa na kiasi, kazi na usafi. Upendo, nidhamu na kumpa mamlaka na majukumu mtoto polepole anapokua, ndiyo mahitaji ya mtoto yaliyo muhimu kutoka kwa mzazi. Upendo hutoa muda na huvumilia. Ombi letu ni kufanya jambo muhimu liwe jambo muhimu (the main thing is to keep the main thing the main thing). Lililo muhimu kwa malezi ni tabia njema na kumtii Mungu. Nasema hili kwa vile najua Waafrika wanamjali Mungu sana. Hili linaakisiwa kwenye nyimbo zetu za taifa, mila na desturi. Mungu tu ndiye msaada kwa makuzi bora na tabia njema. Sisi wenyewe hatuwezi lolote. Mwenyezi Mungu ndiye Mzazi mkuu. Wazazi tupunguze shughuli na kutenga muda wa kulea, ili tuwe mifano kwa matendo, Kuadilisha na kufanya watoto wetu wanafunzi. Hakuna aliyefuzu malezi, ila tumeona hitaji la kuwa kitabu cha kiswahili cha malezi ya watoto. Kwenda semina na kusoma vitabu vya malezi ya watoto iwe kipaumbele. Watu wengi wakitueleza yao tunaweza kufikiri tumeachwa na basi! Usidanganyike, kila familia ina mizoga yake!. Mbinguni hatutaenda na masanduku, majumba, magari, chakula na vinginevyo. Tutaenda na tabia na watoto wetu tu. Miaka saba ya mwanzo tabia ya mtoto imejengeka. Ila Mwenyezi Mungu ni mwenye rehema kama tumekosea tuungame kwa dhati. Bado tuna nafasi kwa watoto, wajukuu au watoto wa jumuiya kuwasaidia. Wakina baba na mama wengi wamekesha na kuhangakia watoto

kwa namna mbali mbali. Mzazi kwa kawaida humpenda mtoto kuliko mtoto anavyompenda, hebu Mungu awalipe jitihada zenu. Mtoto anakuwa mshindi kwa kujikana nafsi na kutawala nafsi. Kila mzazi/mlezi ana bustani! Bustani yako ni mtoto. Kila siku unapanda mbegu kwenye bustani. Jambo kubwa kupita yote ni kumsaidia mtoto wako kuishi bila wewe! Hebu tumwombe Mwenyezi tukishirikiana naye atoe magugu mabaya.

Ukurasa wa Nyuma

Grace momadi Masaka: Anasema fundisho kubwa kuwapa watoto wetu ni kuwasaidia waishi bila sisi wazazi kisha hatimaye wapate uzima wa milele. Waweze Ana watoto wawili daudi na Paulo ambao wapo shule ya msingi. Ameolewa na Daniel Masaka ambaye ni mkemia wa kiwandani, NJ. Grace anafanya kazi vituo vya kutunza wazee marekani, na kufundisha watoto wake wapo shuleni. Amesomaea fani ya aualimu wa biolojia, kemia, dini, na uuguzi.

Daniel Masaka ni Mkemia wa viwandani. Anasisitiza mchango wa kina baba kwenye malezi ya watoto, hasa katika ulimwengu wa leo ni muhimu sana. Baba yetu wa imani, Ibrahimu Mungua alipendekeza kwa kusema “Kwa maana nimemjua kwamba atawaamuru wanawe na nyumba yake baada yake waishike Njia ya BWANA wafanye haki na hukumu”. Hebu tumwombe Mungu tuwe kama Ibrahimu. Hata Nuhu naye aliingia kwenye safina na familia yake. Hebu tufuate mifano ya baba hawa. Hata kama hatuwezi kuingia mbinguni na kila mtu, basi tuingie na familia zetu. Yeye amesomea Veterinary (Mifugo n atiba kwa wanyama), Kemia, na Biolojia

Bettie Magesa Muasya ni mwalimu wa shule ya Advent Hill, Nairobi: amesomea fani za hesabu, dini na ualimu, ana watoto watatu ambao ni Naomi, Alvin na Anita na wajukuu watatu. Ameolewa na mch Paul Musyoka Muasya ambaye ni Mchungaji Kenya. Bettie, Amehusika na makongamano mengi ya malezi ya watoto na wakina mama wa viongozi wa dini (shepherdess). Anasema Danieli aliyekuwa mtoto mdogo tu “aliazimu moyoni mwake” kumweheshimu Mungu japo itamgharimu. Hata leo Mungu atawasaidia watoto wetu. Yeye amesomea hesabu, Ualimu na Biblia

Sura ya 1

JAMBO MUHIMU NI KUFANYA JAMBO MUHIMU LIWE JAMBO MUHIMU.

Jambo muhimu katika maisha yetu ni lipi? Ni muhimu sana kila mmoja ajiulize swali hili. Ni kitu gani ambacho ni muhimu katika maisha yako? Je ni mali, elimu, mitindo (hasa kwa

wanawake), mume/mke, watoto, vyeo? Biblia inatuambia hivi, katika kitabu cha Mathayo 6:33; “Bali utafutateni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.” Kuutafuta kwanza ufalme wa Mungu wapendwa, ndiyo jambo muhimu, na mengine yote hufuata baadaye.

Kuutafuta ufalme wa Mungu ni kufanya yote uwezayo ili kuwa tayari kumlaki arudipo. Pia ni kuwaandaa wengine, wakiwemo marafiki, ndugu na jamaa na hasa watoto. Katika kitabu cha Yeremia 13:20 kuna swali ambalo tutaulizwa: “....liko wapi kundi lako ulilopewa, kundi lile zuri?” Swali hili linaweza kuulizwa kwa viongozi wa kiroho au wa kiserikali, lakini pia tutaulizwa sisi kama wazazi kuhusu watoto tuliopewa. Hivi tutajibuje wapendwa, kama tuliachilia watoto wetu wakaangamia kwa sababu ya malezi yetu mabaya sisi wazazi? Kitabu hiki kina lengo la kujibu swali hili, ili tutakapooulizwa tuseme ‘Tuko hapa Bwana pamoja na kundi dogo la watoto uliotupatia.’

Watoto ni thawabu toka kwa Mungu, (Zaburi 127:3). Tunapopewa zawadi na mtu, huithamini na kuitunza sana. Niliwahi kumwomba rafiki yangu kitu fulani, akakataa akisema ‘nilipewa kama zawadi, siwezi kuigawa.’ Rafiki yangu mwingine anayejulikana kama mama Mwangi (Rachel Mutero) alinifundisha somo la maana sana kuhusu namna alivyothamini zawadi ndogo sana niliyokuwa nimempatia.

Tulikuwa na mchezo wa urafiki wa kisiri (secret friend) kanisani kwetu Karura. Kwenye mchezo huu unachagua karatasi yenye jina, na unamwombea mtu huyo hadi siku ya kutambuana. Siku hiyo watu wanawaletea marafiki zao zawadi, kulingana na uwezo wa kila mtu. Mimi nilikuwa nimemchagua mama Mwangi na nikawa nimemletea kitambaa cha kichwani cha bei nafuu sana. Ingawaje alikuwa na vitambaa vingine vizuri na vyenye thamani kubwa, alifurahia sana nilipompatia kitambaa kile, na akawa anakivaa kwenye matukio maalumu kama kanisani n.k.; Siku moja alipokuwa amesafiri, aliibiwa mizigo yake, likiwemo begi ambalo lilikuwa na kitambaa hiki. Alisikitika akaniambia kwamba aliibiwa kitambaa chake ambacho nilikuwa nimempatia kama zawadi!!! Mama huyu alikuwa amepoteza nguo zake za thamani, lakini alisikitikia kitambaa chenye thamani ndogo sana kwa sababu kilikuwa zawadi, aliyoithamini sana. Je, tungethamini na kuitunza kiasi gani zawadi hii ya watoto tuliyopewa na Mungu?

Katika siku hizi za mwisho, shetani ameingilia watoto, na anajua kabisa kwamba akiwanasa watoto atakuwa ameliangamiza kanisa na taifa la kesho. Watoto wetu wamekuwa balaa badala ya kuwa mbaraka kwetu. Sisi tunaosoma Neno la Mungu tunafahamu kwamba unabii unatimia katika maisha yetu. Je, tutamwachia shetani aangamize watoto wetu katika anasa, madawa ya kulevya na mitindo ya dunia hii? Je, tutafanyaje tuokoe watoto wetu? Je, kuna tumaini lolote?

Katika Biblia, tunasoma kuwa Musa na kaka yake Haruni walipokwenda kwa Farao kule Misri, wakitaka awaruhusu kwenda jangwani kumuabudu Mungu wao, Farao aliwaambia, “Nendeni, mkamtumikie BWANA, Mungu wenu, lakini ni kina nani watakaokwenda?” Musa akamjibu, “Tutakwenda na vijana wetu na wazee wetu, na wana wetu, na binti zetu...” Kutoka 10:8-9. Hali kadhalika, na sisi, kama Musa, lazima tuazimie kwenda mbinguni pamoja na watoto wetu, kwa maana, Mungu ameahidi kuokoa watoto wetu kama ilivyoandikwa kwenye katika kitabu cha Isaya 49:25; “ kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe, nami nitawaletea wana wako wokovu.”

Wazazi wengi baada ya kupata mtoto wamejiuliza mioyoni ‘nitamleaje mtoto huyu?’ Swali hili alililiuliza pia Manoa katika kitabu cha Waamuzi. Tunachukua muda kusomea mambo mengi

ila hatuna maarifa na elimu ya kulea. Jambo hili limekuwa tatizo hasa katika kizazi hiki, kwani miaka ya zamani mama alikuwa na marafiki, shangazi, jirani, dada, mama na bibi waliomzunguka na kumpa ushauri. Walikuwa hawana vitabu, na hata hivyo hawakuvihitaji sana kwani walikuwa na mila na destruri zilizowapa dira. Walikuwa na majibu, kwa maswali karibu yote! Japo mengine hayakuwa sahihi, bado walikuwa tayari kushirikiana na wengine kutafuta majibu sahihi zaidi ya malezi. Mama huyu mpya alikuwa na wanawake watu wazima waliomsaidia katika mawaidha ya kulea watoto.

Joto hili la upendo limeanza kupotea! Watu wengi wamekuwa katika kuhama hama na majirani wamekuwa na sura ngeni kila mara. Mama na shangazi zao wamehamia miji mingine mikuu kama Nairobi, Dar, Bujumbura, Goma, Jinja na Kigali. Na hata kama wasingekuwa wamehama, pengine wasingekuwa na ushauri mzuri kiasi cha kutosha. Kutawanyika na upweke huu, kumefanya wazazi wengi wawe na hofu kutokana na wengi wao kutojua mengi kuhusu malezi.

Ni kweli mamilioni ya wazazi hawana msaada, na pia hawana itikadi, mila, desturi, dira, au filosofia yoyote ile ya kufuata katika kulea. Changamoto na maswali mengi huja kwa haraka kuliko tunavyoweza kuyatatua. Tumekuwa tukidai kwamba sheria za zamani ziondolewe na kuwe na mapinduzi yatakayotoa nafasi kwa mambo mapya ya kileo. Wakati wasiwasi na hofu vikizidi kuongezeka kwa wazazi, kumeibuka wana taaluma wa saikolojia, walimu na madaktari wa watoto, wakijaribu kujibu maswali ya malezi. Hivi sasa watoto wengi wa nchi za magharibi wanalelewa na falsafa hizo. Je hawa watu wa magharibi wamefanikiwa na falsafa za wanataaluma wao katika kulea? Kwa kweli falsafa zingine za wanasaikolojia kama Freud zimeonekana kama zina kuchanganyikiwa. Mfano wamekuwa na mashauri mengi ambayo hawayafuati, au yanaonekana yana walakini. Nafikiri binadamu yoyote aweza kumshauri mtu kitu, ila ni vyema kwa wakati mwingi kuangalia maadili ya mshauri.

Mtu aweza kutegemea kwamba akili za watoto hawa wa magharibi na tabia zina mvuto mzuri sana! Kuna mazuri machache na mabaya mengi! Hili si kweli, watoto walio jela wameongezeka. Matumizi ya madawa ya kulevya, pombe, mimba mashuleni, magonjwa ya akili, na kujiua kumezidi kuongezeka kwa watoto. Kwa kweli shughuli ya uzazi imezidi kuwa ngumu kuliko wakati ule mabibi na mashangazi walipokuwa wakitoa ushauri. Hatuwezi kuwalaumu washauri wote wa taaluma wa magharibi ila tunachosema ni kuwa watalaamu wao wengi wamemwacha Muumba katika mashauri yao. Hawajachukua historia ya miaka 6,000 na kuona jinsi mafanikio ya kulea watoto yalivyokuwa. Kila mwanasaikolojia ametuuzia bidhaa yake kana kwamba ni ukweli mtupu.

Falsafa hizi, zimedai kwamba kumpenda mtoto kwa kumwadabisha ni makosa, na kwamba kutumia mamlaka kwa mtoto ni hatari, na kumfundisha mtoto kuhusu Muumba ni vibaya. Mambo haya yamevuka mipaka hadi kufikia kwenye hatua ya kufundisha mashuleni kwamba ushoga ni sawa na kwamba kuna ngono salama nje ya ndoa takatifu. Ubora wa tabia ambao hauna viwango, heshima au thamani za tamaduni zetu, unajitumikia tu bila kumtumikia Mwenyezi Mungu na umeleta shida. Hatuna majibu ya maswali mengi katika kulea ila yale tunayoeleza yamethibithishwa kupitia vizazi vingi na Yeye Aliye mzazi na Mlezi mkuu kupita wote. Usafi wa moyo, maneno na matendo ni muhimu katika malezi ya mtoto (purity).

Tunaamini kwamba mpango wa kulea unaanza na ndoa takatifu. Ndoa hiyo iwe na uaminifu, kuheshimiana, na kulindana ambapo mke atamtii mume na mume atampenda mke.

Watoto ni urithi toka kwa Mungu na hivyo wanapaswa kuwa waaminifu (integrity), kuchukua majukumu, kujibidisha katika usafi wa moyo, kuwa na juhudi kazini, kujikana nafsi, kunyenyekea na kuwa na imani.

Ibilisi anapambana nasi wazazi kwani anatambua akiwapata watoto wetu wakiwa wadogo watamtumikia yeye tu na si Mungu. Farao, Rameses na Herodia mkuu, kama tusomavyo kwenye Neno Takatifu, walitoa amri kwamba watoto wa kiume wauawe wakiongozwa na Ibilisi. Siku hizi pia anaendelea na azma hiyo hiyo. Anaitekeleza kwa mbinu na mitindo mbali mbali kutegemeana na wakati katika historia na mahali. Katika wakati wetu hapa Afrika roho hii inaendelea kutenda kazi. Mwandishi Daktari Mbennah anasema kwamba wakati akitembelea Tanzania na kuendesha semina kwenye wilaya moja, aliona Kituo cha Afya cha Wilaya ambacho wauguzi na wahudumu wake walikuwa wanatumia muda mwingi kujizungusha na kuchelewa kutoa huduma. Watoto walikuwa wakifariki kwa kiwango na katika hali ya kutisha na isiyotarajiwa. Katika juma moja, walikufa hadi watoto watano wakati kama wangepata huduma iwapasayo maisha yao yangenusuriwa. Ibilisi anawalenga watoto kupitia kwetu. Hebu tuwe watu wa maombi. Mzazi lazima awe na malengo kwa mtoto wake, hata kabla hajazaliwa, na kumwomba Mungu ayafanikishe.

Watoto wetu siku hizi wanajifunza uchoyo kutoka kwetu. Zamani wazazi waliweza kumwomba mtoto kitu walichompatia katika hali ya kumjaribu kama angeweza kukitoa alichopewa. Lakini siku hizi tuna shughuli nyingi kiasi cha kushindwa kufuatilia kama mtoto amepata masomo haya ya ukarimu anavyostahili na tunaishia katika kubabaisha tu. Watoto wangu wawili walipata mapera mawili kila mmoja, na yule mdogo wa miaka sita alikuwa na rafiki, ila hakutaka kumpa pera! Na yule mkubwa naye hakutaka kumpa kwani alisema ssi rafiki yake bali rafiki wa mdogo wake, wakaendelea kucheza, nikawakuta wanakula na mwenzao anawatazama! Nikawaambia sasa nitachukua mapera yote na kumpa huyu mtoto. Kila mmoja akatoa moja yule mtoto akapata mawili. kila mmoja alihitaji somo la kutoa. Kutoka siku ile wakiwa na kitu wanasema “Mama chukua na wewe hiki, au mega hapa.” Wape watoto nafasi za kutoa vitu. Wakikupa kitu usikatae pokea kwa upendo wajifunze kutoa.

Wazazi, watoto wenu wakiwagundua kuwa ni wachoyo watawaiga na kufanyia mazoezi katika nyumba zao wakati watakapokua. Ikiwa mwanao atakua akiwa na tabia ya uchoyo na tabia hiyo imejengeka itakuwaje? Hakikisha wanao wanakuwa tayari kugawana na wale wanaocheza nao. Najua kutokana na tamaduni za kule tulikotoka, baadhi yetu ni wabahili kuliko wengine ila kila tamaduni ina la kujifunza, kwa kuwa kila mtu ana mapungufu fulani na Neno la Mungu ndiyo kigezo cha kujifunzia. Ukiwa na kitu, wapelekee jirani zako, au wahitaji barabarani na uwape. Hata kwenye ibada usiende na mikono mitupu kama pesa unayo. Toa sadaka, kwa kuwa wanao hawatajifunza kutoa zaka na sadaka kama wewe hutoi! Ukiitwa kusaidia mahali, mfano kuvuna mahindi, nenda na watoto ili wajifunze. Jirani yangu alisafiri na kuomba nimwagilie nyanya zake maji. Sikuwa na nafasi bali niliona itakuwa wakati mzuri watoto wangu kusaidia jirani. Niliamua kwenda nao wafanye kazi hii, ili iwe sehemu ya maisha yao, huduma za jamii. Wasipoona nasaidia wengine, wao itakuwa vigumu zaidi kusaidia.

Mchungaji na rafiki yetu Mlenzi toka Kongo ambaye aliishi kwenye watoto wengi masikini alikuja kututembelea Marekani mwaka 2010. Kijana wangu wa miaka tisa alinunuliwa rubberband za kuvaa mkononi (sillyband), nikawambia kwa vile ana nyingi kama,

thelathini hivi, ampe mchungaji wa Kongo michache ili akawape watoto masikini Kongo watafurahi. Alikataa, akalia machozi kabisa. Kesho yake aliamka na kusema “mama zile sillyband ni bei gani?” nikwambia ni dola moja akajibu “Hiyo tu! Kwa nini sikuzitoa jana? Basi nitampa zote”. Mioyo yetu inashindana na uchoyo kila kukicha, hebu wasaidie watoto kujua kwamba ukarimu ni tabia ya mbinguni na itaanzia hapa hapa duniani. “Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa, kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwa sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile mpimiacho watu, ndicho mtakachopimiwa” (Luka 6:38)

Napenda kusema kwamba mifano yetu sisi wazazi ndiyo inalea watoto hata kuliko maneno yetu, nimesikia mtoto wangu wa miaka kumi akiniambia; “Mama wewe ni mnafiki; ulituambia tusikatishe kwenye majani yanakufa mbona wewe unakatisha!”. Baba yangu alikunywa pombe na alitupa tunywe pia, nikiwa na miaka sita aliniambia “Onja.” Nilipoonja nikasema moyoni: “Hivi pombe ni chungu hivi, kwa nini watu wazima wanajisumbua kunywa visivyo vitamu? Nikamwuliza baba kwa nini hanywi soda?” akajibu “Soda inajaza tumbo na kwenda kwenda chooni kila mara.”.

Wakati huo baba na mama walikuwa wakinywa. Mdogo wangu alionjeshwa, naye na alipokuwa na umri wa miaka mitatu tulimwona anaimba na kuzunguka zunguka kumbe tuligundua amelewa! Na mpaka leo ana miaka arobaini na mitatu, hajitegemei; anasaidiwa na mahitaji yake. Baba alikuwa mtu ambaye anategemewa nasi na ndugu zake na aliyawezea majukumu yake hata akinywa, ila mtoto amemharibikia. Ikiwa mtoto atakuwa amejifunza tabia mbaya kwenye mazingira yaliyo nje ya nyumbani ni kitu kingine ila kama amejifunza kwako inaleta huzuni. Jambo baya mzazi ukilifanya na kumfundisha mtoto, yeye anabobea kwa kina zaidi yako. Nimeona wazazi wanaokunywa pombe ya ndizi na ulezi (mbege) wakimnywesha mtoto pombe hiyo ili alale asiwasumbue wakifanya shuguli zao. Pombe inaingia kwenye damu na mtoto hawezi kuiacha. Wengi wananiambia walionjeshwa wakiwa wadogo na wanashindwa kuiacha mpaka Mungu aingilie kati. Natilia mkazo: Wazazi, matendo yenu maovu yana mvuto mkubwa siku zote kwa mtoto kuliko mazuri!

Tuna pambano kuu linaendelea kati ya Mungu na Shetani. Usibweteke na kujisahau kwamba upo vitani kila dakika! Mara nyingi, kibinadamu, inaonekana kana kwamba shetani anashinda, ila tunajua shetani hajui mawazo yetu, ana vidokezo tu kwa matendo yetu na hivyo tukiwa magotini kwa sala tutashinda kwa neema ya Mungu. Hata hivyo, mzazi usijidanganye kufanya uovu fulani tu, na ukataka mtoto wako asiufanye. Mtoto kushindwa kwake vishwawishi ni rahisi sana zaidi yako, na unajua ni kwa sababu gani! Hata hivyo wewe kama mwalimu ukimfundisha mtoto akafuzu hata kukupita wewe si ndiyo umeliwezea somo? Kina baba wengi siku hizi wameacha kwenda kwenye nyumba za ibada ila utawasikia wakihimiza “Musa mbona huendi ibadani!” wakati yeye mwenyewe anashinda nyumbani miaka yote.

Wazazi ufuatiliaji wa majukumu ni muhimu. Usimpe mwanao kazi kama hauko tayari kuifuatilia. Itafanyika kwa kulipua na vibaya vibaya na kisha atajenga tabia ya kufanya kazi kwa uhafifu. Mtoto apewe kazi ya kufanya kila siku na uikague. Hata akiwa ana umri wa miaka miwili anaweza kumenya maharage, na kufuta vijiko. Zipo kazi nyingi unazopaswa kufikiria kumpa mwanao na ndiyo maana mama anayekaa nyumbani ni mbaraka ikiwa atakuwa mfuatiliaji. (Angalia sura ya orodha za kazi). Yale ambayo mtoto anafanya ili kujenga ustadi

yafuatiliwe. Kuna yaya gani au shangazi gani atatilia maanani haya? Kama yupo ni nadra sana. Hata mara nyingi nilipokuwa nimetingwa kibaruani na kuweka mtu aniangalilie wanangu nimekuwa nikiwaza, “Hivi sijui kwa nini sisi wanawake tungali bado tunazaa kama hatuko tayari kukaa na watoto wetu!” Naona wanawake wa kihindi wanakaa na watoto wao hata walio na mashahada ya chuo kikuu mazito mazito. Na nimeona kama New Jersey tukiishi na wahindi na waarabu wote watoto wao wana adabu, wanajua lugha ya walikotoka vizuri, wanakula chakula cha utamaduni wao, na wanafanya vizuri mno darasani, wakiongoza hata watoto wa Kimarekani. Karibu wote wanapata ufadhili wa masomo kwenye vyuo vinavyoongoza nchini Marekani kama vile Harvard, MIT, Yale na kadhalika. Sisi wengine Waafrika tuna watoto wenye shida hapa na pale, hawataki kula ugali au chakula cha Mwafrika ila junk food ya Wamarekani. Lugha wanayoijua hakuna zaidi ya Kiingereza. Akija nyumbani anashindwa kuzungumza na bibi na babu, hawezi kula chakula ambacho shangazi amepika! Na sisi tunaona ni maendeleo eti!

Tusiache watoto wetu wawe kama vimwinyi au vichifu fulani hivi. Sisi tufanye kazi, wao wasifanye, wakati nasi kwa wazazi wetu tulifanya, je hii ni huruma ya kweli? Na wakienda kuishi kwenye ndoa si itawashinda, maana kila mtu anataka kuwa Bwana na mwingine awe mtumwa, itawezekana kweli? Niliona vijana wetu wengine wa kisasa wakigombana kwenye ndoa “ameosha kijiko kimoja nami kimoja nataka tuwe sawa bin sawa”. Heshima itakuwa ngumu kwenye ndoa hiyo. Kwa mtoto wa kike, yapasa ajue mwanamume anapaswa kuheshimiwa ni agizo la Neno la Mungu. Na mtoto wa kiume kumpenda mke wake, hivi wanajifunza nyumbani. Kila mwanamke hapendi kabisa mtoto wake wa kiume aoe mwanamke anayemkosea adabu, japo yeye aweza kukosa adabu kwa mume, lakini asingependa kuwa na mkamwana wa namna ile.

Lingine ni la kusaidiana. Ukiona mtoto wa mwenzako au jirani yako ana kosa fulani shuleni, msaidie yule mtoto. Ila kama unaona kwamba haiwezekani mwambie mzazi wake ili kusudi alishugulikie. Haisaidii kumsema mtoto kijiji kizima na hujamwambia mwenye mtoto. Pengine ni jambo ambalo hata mtoto mdogo hajajua kwamba ni baya, na mzazi hajajua kinachoendelea. Ila ukimwambia kwa upendo naye akakasirika na kuona wewe ndiyo mbaya wake, basi utakuwa umefanya sehemu yako. Ila mtu mzima anayependa watoto, watu na Mungu hatakaa kimya mambo yakiharibika. Tusiposaidia watoto wa wengine pia itaturudia, kwani wakiwa wezi au waharibifu watasababisha madhara hayo nyumbani kwetu pia. Na ndiyo sababu naona umuhimu kwa wale wenye uwezo kuwasaidia watoto wa wengine kwenda shule. Ni mbaraka mkubwa wa kuendeleza jamii. Najua siku hizi si kama zamani. Ulipokuwa unatenda kosa uliadhibiwa na jirani yoyote na ukienda kulalamika kwa wazazi wako uliongezewa kipigo, na hiyo ikawafanya wengi kuona bora kunyamza!

Mtoto ajue yeye ni nani? Yupo duniani kwa sababu gani? Na anaelekea wapi? Malengo yake ni yapi duniani? Yanapita mawimbi ya wanafalsafa na sayansi nyingi kama uibukaji. Hebu mweleze mtoto wako yeye ni nani. Kwa mujibu wa mila zetu sisi Waafrika hatukuwa tunawafundisha watoto wetu upuuzi huo “Wewe ulitoka kwa nyani.” Hata nyani wenyewe hawataki tuwe familia moja nao! Alituchekesha Mchungaji Bulengela akisema alisikia nyani mmoja akimwambia mwenzake “Hawa binadamu tabia yao ngumu bwana! wanachafua mazingira, wanaweka moshi mdomoni, na kila mara wanagombana. Sisi nyani hatuna hayo, wakae huko huko. Wasiseme walitoka kwetu”.

Hata kama wewe si mhandisi wa roketi huwezi ukagundua kwamba ulitoka wapi na ujithamini? Nikiwafundisha watoto wangu nauliza, “Wewe ni nani?” Anajibu jina lake. “Uko hapa kwa ajili gani?” anajibu “Nimeumbwa na Mungu na baada ya maanguko ya binadamu Edeni niko kwenye ukarabati ili niwajulishe wengine, nami nijitayarishe.” Unaenda wapi?” Anajibu “Naenda mbinguni niishi na Mungu milele zote.” Kumbuka wewe hukuumbwa Sokwe na hutaendelea kubadilika kuwa kitu kingine! Umeumbwa kwa mfano wa Mungu kwa makusudi maalumu ya utukufu, jifunze kiundani hayo, maana Mungu ana nafasi ya kukueleza. Katika simu ya sala unayompigia, hakuna usemi tuliouzoea kwenye simu wa “Mpendwa mteja...simu uliyopiga haipatikani kwa sasa!”

Watoto wengi wa kike wamekuwa na kutojithamini siku hizi. “Sijui mimi ni nani, nimepotea, wacha niende nikajihoji mimi ni nani.” (I do not know who I am, I am lost. I am going to find myself). Wengi husema vitu Kama nywele zangu ni mbaya za kipilipili, miguu yangu siyo mizuri, masikio yangu makubwa NK. Mungu Ndiye aliyetuumba, kama alituumba hivyo, na sisi hatuna jinsi ya kujibadilisha, Naye ni Baba Mwema, je si Yeye basi Ndiye mwenye Kigezo cha uzuri ni nini? Mungu hakusema nywele za aina fulani ndiyo nzuri na za aina fulani ni mbaya. Tusijilinganishe na watu wengine tafadhali! Thamani yetu inahusu na Kuumbwa na Mungu na Kukombolewa Naye. Hakuna mtu Mwenye thamani mwenyewe, Hakuna anayeweza kuumba au kumkomboa mtu.

Mzazi ye yote au mtu mzima kwenye jumuiya, ni mbaraka wa kusaidia watoto wengine. Wanapokuja nyumbani kwako hebu waonyeshe maadili mema, namna ya kufanya kazi na adabu njema. Watoto waruhusiwe kucheza. Kucheza kwa mtoto kulivyo ni kama kufanya kazi kwa mtu mzima (play is to children, what work is to adults. Wao hufanya mazoezi ya maisha halisi. Watoto wanahitaji kurudia rudia na wawe na ratiba itakayowasaidia kujifunza. Mfano rahisi, mtoto mdogo aliyezaliwa awe na ratiba ya kunyonya, kila baada ya masaa 3. Akilia kabla ya hapo waweza kumpa maji ya kunywa. Baada ya juma tu atazoea. Itamsaidia kuwa na mpangilio wa tabia, kuwa na kiasi na kuushinda ulafi, nawe pia itakusaidia kupumzika na kufanya kazi nyingine au kupata usingizi. Ni ukatili kumwacha mtoto afanye anachotaka. Tabia, afya na mahusiano yake yatakuwa mazuri akiwa na ratiba.

Wazazi tumetelekeza watoto kwa njia nyingi. Wazazi tumetokomea. Kuna mama mmoja alisema, “Kijana wangu amekuja na mwenzake wa darasa la tisa wa shule ya bweni na wala wazazi wa yule kijana hawamtafuti! Baada ya mimi kuwapigia simu wamesema sawa akae tu huko kwako!” Yule kijana, kwa msaada wa ile familia alimaliza shule na kuwa kijana safi mwenye adabu na kazi nzuri tu, kumbe masikini alikosa msaada. Kuna watoto wengi wakipata mahali penye maji na rutuba wananawiri na kuwa watoto wema tu ambao wanasaidia familia, jumuiya na taifa kwa ujumla. Mzazi ambaye una mfano bora, nyumba yako ni taa kama ile ya bandarini inayofanya meli zisipotee au kuzama (lighthouse). Nawasihi wale wenye uwezo msisaidie watoto wenu tu kwa elimu na maarifa, saidia na watoto wengine pia hata kama inabidi ujitoe mhanga kidogo. Hata kuwapa moyo watoto wa jirani ni jambo kubwa. Hili nimeliona magharibi; wazazi wanajua kuwatia moyo watoto, na kujihatarisha kuliko sisi, na hii inasaidia sana mtoto. Mtoto aachwe huru kidogo kujifunza vitu fulani, usimkemee kila mara; “Usijifunzie baiskeli yangu, utaiharibu!” Najua vitu ni aghali ila mtoto atajifunza lini?

Kwa wale ambao hawakujaliwa kupata watoto, kuna watoto wengi wanaohitaji uongozi na malezi. Omba Mungu akuonyeshe, kama ni fungu lako kusaidia yatima au watoto wasio na

makao. Dini ya kweli ni kusaidia yatima na wajane na kujilinda na mawaa. Kumbuka hata watu wabaya husaidia wa kwao, kwa hiyo huna la ziada ulilofanya ukijilinganisha na wabaya. Kumbuka kusaidia familia na jamaa zako ni jukumu lako ila kusaidia masikini usiyemjua ni kazi ya Mungu Mwenyezi mwenyewe na ni mbaraka kwani amesema, "Amsaidiaye masikini humkopesha Bwana, naye atamlipa kwa tendo lake jema." Je, umeshawahi kumkopesha milionea au Rais wa nchi yako? Mimi sijawahi! Sasa Mungu mwenyewe anakukopesha! Mbona hata nasikia kutetemeka! kinyangarrika kama mimi kumkopesha Mungu Mwenye Enzi!! Ni ombi langu kuwa kitabu hiki kikusaidie kukupa kanuni za kulea na uzidi kumwomba Mungu akuongoze na kukufunulia mengi zaidi. Uwe huru kutuandikia ushauri wako ukieleza yale uliyojifunza, ili nasi tubarikiwe. Email yetu na anuani yetu ipo hapa.

SURA YA 2

MTOTO AKIWA TUMBONI MWA MAMA

Biblia yasema "Maana wewe Ndiwe uliyeniumba mtima wangu, uliniunga tumboni mwa mama yangu, nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu na ya kutisha.... mifupa yangu haikusitirika kwako, nilipoumbwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi... macho yaliniona kabla sijakamilika..." Zaburi 139. Watoto ni ahadi ya tumaini katika kila kizazi. Kila kizazi kinakusudiwa kuwa na mchango wake katika imani, utimilifu na historia. Mungu Anawatumia watoto kutimiza makusudi yake maalum mfano Musa, Yusufu, Yeremia.

Ni kwa ajili ya ulimwengu uliovunjika na mahusiano kusuasua ndiyo maana watoto wengi wanazaliwa katika mazingira magumu kama ya kukosa wazazi wote au mmoja, kunyanyaswa, na umasikini unapita kipimo. Mtoto ni mtu kamili kwa kuwa ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Ila kutokana na kuwa amezaliwa katika dunia yenye dhambi hivyo hata naye kibinadamu anamhitaji Mungu kama tulivyo sisi watu wazima. "Wote wamepotoka na wamekosa." Wanahitaji wokovu wa Mungu. Kila mtoto ana makusudi ya kutimiza kwa mpango wa Mungu. Yeye anawapenda watoto. "Waacheni watoto wadogo waje kwangu wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa Mungu ni wao."

Mtoto ni zao la yai la mama na mbegu toka kwa baba. Zote zina nyuzinyuzi za urithi (genes-chromosomes) ambazo ndani yake kuna kitu kijulikanacho kama DNA deoxyribonucleic acid. Hiki kina sifa za kipekee za urithi wa mtu mmoja mmoja na kumfanya awe wa aina yake pekee kabisa na mtu au kiumbe kingine. Mwanadamu ana chromosomes 46, ila yai lina 23 na mbegu za kiume 23 na hilo linafanya mtoto awe na 46 kama ilivyo kwa kila mwanadamu ili asiwe na maradufu ya viungo yaani mikono 4 miguu 8 n.k. Kila sehemu ya mwili wetu ina chembe hai. Yai na mbegu ya kiume ni chembe hai za uzazi (reproductive cell) zisizoonekana kwa macho. Tuna chembe hai ya misuli ya nyama, ya moyo, chembe hai za ubongo, chembe hai za mifupa, kuna chembe hai za aina tofauti 13 hivi kwa binadamu. Labda tutoe mifano ya chembe hai kubwa

kupita zote ambazo zinaoonekana kwa macho, mfano: mbegu ya kiume ya nyangumi ni kilo 8. Nazi pia ni chembe hai kubwa ya mimea.

Seli zinatofautiana kwa kiasi fulani, na ndiyo maana mfupa ukatofautiana na jicho kwa sababu chembe hai zake zimekuwa na tofauti kidogo ya maumbile kwa maana ya rangi, umbo, ukubwa, vitu vilivyomo n.k). Ila chembe hai zote ndani zina vitu vya kufanana kabisa. Mfano chembe hai ya jani ina Kroloplasti za kijani ili kutengeneza chakula kutokana na jua, bali chembe hai ya kiazi, haina rangi ya kijani kama ya jani yaani Kloroplasti. Chembe hai nyingi zinafanya tishu. (Mfano misuli, mifupa), na tishu nyingi zinafanya viungo mfano moyo, au ubongo. Na viungo vingi ndiyo tunapata mwili. Chanzo cha uhai cha mtoto tuseme Baraka ni pale mbegu ya baba au chembe hai ya uzazi ya mume inapoingia ndani ya yai la mkewe.

Mimba hupitia hatua tatu za maisha. Wakati wa kujaamiiana mbegu moja ya baba kati ya mamilioni ya baba ikiingia ndani ya yai mimba inakuwa imetungwa na uhai wa kiumbe kipya unakuwa umeanza. Ndiyo sababu kutoa mimba (isipokuwa kwa sababu ya hatari za afya ya mama) ni dhambi; maana kiumbe kamili mbele za Mungu. Mama mmoja anayesaidia kushauri wasichana wasitoe mimba, mwaka huu 2013 alisema kwa miezi minne, toka Januari mpaka Aprili, wamarekani laki tatu na watu 12 milioni duniani wametoa mimba. Hebu tuwe washauri na kusaidia vijana wetu pale tunapoweza, na pia tuweke mifano mizuri. Kutoa mimba si njia ya uzazi wa majira, au furaha, bali kuua kiumbe ambacho Mungu anakithamini kupita vyote.

Mara moja mwili wa Baraka unaanza kuumbika na kukua kutokana kwa kugawanyika kwa chembe hai (cell). Kiumbe huyu ni duara na anasafiri kupitia mirija ya uzazi na kukaa kwenye mfuko wa uzazi. Seli za Baraka zinaanza kuunganika na mishipa ya damu na kupata lishe na baadaye kondo hutengenezwa na kuendelea na lishe toka kwa mama. Baada ya majuma matatu mpaka manne mviringo wa Baraka unagawanyika katika sehemu tatu; ile ya ya juu iitwayo ectoderm inayounda ngozi, nywele, makucha na mfumo wa fahamu. Ile ya ndani iitwayo endoderm huunda mapafu, ini, tezi zote, tumbo, kongosho, nyongo na ile ya kati iitwayo mesoderm iundayo misuli, mifupa, mfumo wa mkojo, uzazi, damu nk. Moyo wa Baraka unaanza kudunda sasa. Katika juma la 5/6 pua na uso, miguu na via vya uzazi vya Baraka huonekana. Juma la 7/8 mdomo na ubongo hugawanyika kulia na kushoto na moyo na figo zinakuwa bayana. Na baraka anaanza kujisogeza hapa ndiyo ujumbe wa DNA utaamua mtoto kuwa wa kike au kiume.

Miezi 3-9 kondo linaumbwa vizuri, Baraka anaonekana sasa kama mtoto mchanga. Baraka anaweza kuonyesha hisia zake kukiwa na mwanga. Mwezi wa nne Baraka anaanza kujisogeza na mwezi wa tano na wa sita Baraka anaanza kuwa na ngozi, na kuanza kuhisi sauti. Kina baba wengi wamezungumza na watoto wao katika hatua hii. Na baada ya kutoka tumboni watoto wameweza kutambua ile sauti! Miezi mitatu ya mwisho Baraka aongezeka uzito mara mbili na mafuta, nywele, na uwezo wake wa kusikia na kukumbuka unaanza kufanya kazi vizuri. Mtoto ana hatari mbali mbali kabla hajazaliwa kama vile matumizi ya tumbako, vileo, madawa ya kulevya, madawa ya hospitali, shida za kurithi (genetically), mateso au kujeruhiwa kwa mama kimwili au kihisia na magonjwa ya mama. Mama epuka kuvuta vileo kabisa, na jaribu kuwa na mazingira yasiyo na vita kwa mtoto. Na kama unatumia dawa zozote za hospitali mwone mganga wako akushauri kwanza.

Mtoto anazaliwa muujiza wa ajabu. Mungu Ametukirimia kushiriki uumbaji naye! Jukumu hili kubwa lisipunguzwe thamani yake, hapa tunaacha urithi mkubwa kupita yote. Mtoto unayemwangalia unaaanza kujiuliza atakuwa nani? Watu mashuhuri duniani walizaliwa wote kwa njia hii. Mtoto ni mtu kamili na hata ukiwa peke yako na mtoto mdogo hauna ukiwa! Waweza kuanza kuzungumza naye! Mfano na maelekezo na mvuto wako ndiyo utakaomjenga kuwa mbaraka au laana ukisaidiwa na Mwenyezi Mungu. Unafikiria jinsi ya kumtimizia mahitaji yote ya lazima. Piga magoti usali kuwezeshwa kufanya kazi hii, si ndogo eti.

Mtoto analia kwa vile hawezi kujieleza. Ni wajibu wako kukagua kama ni njaa, mkojo, baridi nk. Kama umechoka tafuta msaada. Usiwe na hasira na kumdhuru mtoto. Zungumza na mtoto japo hakujibu, anasikia na anafurahi. Tabasamu naye! Unapowasiliana na mtoto, mkumbatie ili kumfanya awe karibu nawe. Chukua picha zake akiwa mtoto kwa ukumbusho. Anakua haraka utapenda ukumbuke! Yaweke mazingira ya mtoto salama mfano ngazi, na kupanda madirishani. Mtoto awe katika utulivu na usalama, sauti au magomvi zipunguzwe. Usifanye kitu kinachofanya mtoto akuogope. Wewe ndiye unamwakilisha Mungu kwa mtoto wako.(soma afya ya mtoto uk.). Kila mtoto ni tofauti. Jifunze mtoto wako anapendezwa na nini, na anasikia na kuwa na nidhamu ukifanya jambo gani.

Mwite mtoto wako jina la kumfaa, la kumpa matumaini. Watu wanaompenda Mungu wametoa majina ya kusaidia hata tabia za watoto mfano Furaha, Baraka, Tumaini, n.k. Usitoe jina la mtoto bila kufikiri. Mwaka huu nilitembelea ziwa Victoria nikasikia majina ya watoto ya ajabu kama Mkojo, Fisi, Taabu, Shida, Mjinga, Hafai, Kibiriti, Difficult, Masikini, Fukara n.k. Tafadhali nakusihi usimpe mtoto majina ya kukatisha tamaa kama haya, au ya kufanya auishi uhalisia wa jina lake. Chagua jina ambalo lina thamani. Maneno ni muhimu sana katika maisha yetu. Tafadhali kama hata mtoto wako amekuwa mkubwa bado una nafasi ya kubadilisha jina lake, na kumwita jina la matumaini, faraja na upendo. Mjumuishe mtoto katika kazi, mfano wakati unapopika n.k.

Kama una watoto wengine, ni vyema uwatayarishe kimawazo kwamba utapata mtoto mwingine ili wasione wivu. Mchunge mtoto aliyezaliwa kwani watoto wadogo hawajui usalama. Waweza kumlisha chakula wakifiiri ni kitu cha kawaida, kama wanavyowalisha wanasesere (dolls) wao, au kumpiga kwa wivu. Inabidi uchukue muda na mtoto mkubwa ili asione amesahaauliwa. Nilikuta mtoto wangu wa miaka minne akijaribu kulala na mtoto kwenye kitanda kidogo! Usimtelekeze mtoto. Kuwa na muda na mtoto ni muhimu kuliko vitu. Siku hizi wengine wanashindwa kihali, au kimali kulea. Ikifikia hatua hii, kuna wengi hawana watoto, tafuta njia ya kumpeleka kwenye ustawi wa jamii kwa ili kupata mtu wa kuishi naye. Hili litakuwa jema kuliko kumdhuru mtoto, zungumza na mwenzi, au wazazi wako kwa hili.

Kunyonyesha pia ni muhimu (angalia sura ya kunyonyesha) endelea kumsomea hadithi. Usikazane sana kufanya masomo rasmi. Mwache mtoto awe huru hata mpaka miaka saba acheze na umfundishe kazi hiyo ndiyo muhimu. Watoto wengine ni rahisi kusikia maagizo, na kusahihishwa na kujadili nao (A-compliant) na wengine wana mawazo yao tofauti, na wapenda kupinga pinga (B-strong willed). Tabia hizi zote mbili zina ubaya

na uzuri wake. Jua tabia ya mtoto wako ili umsaidie. Mfano usiwe ukimwambia yule wa B kila mara atoe haki zake ili mambo yawe rahisi. “B tafadhali mpe kiti A ili tusiwe na muda mrefu wa kubishana wewe ni mtoto mzuri hupendi ugomvi!” Baada ya muda yule wa A atachukia na kutaka aasi.

Watoto wengine wanahitaji adhabu kidogo sana na kukosolewa kwa nadra. Wengine kila siku wahitaji adhabu au kukosolewa na wanataka wapate (attention) au umakini wako kila mara. La muhimu, usitelekeze jukumu lako kama mzazi ili kuonyesha kwamba wewe ndio mwenye mamlaka na neno la mwisho. Jifunze tabia za watoto ili uwasaidie. Napenda kusema kwamba tabia za watoto hazibakii hapo hapo zingine zinabadilika wakikua. Aweza kuwa alikuwa A akabadilika kuwa B.

Mtoto akizaliwa kichwa chake chaonekana kikubwa sana kuliko mtu mzima kwa uwiano na anazidi kukua ubongo kwa haraka kwa mwaka wa kwanza akizaliwa. Jaribu kusisimua ubongo wa mtoto na kumwelezea hadithi inatatanua ubongo wake katika kufikiri. Muziki mwororo wa sauti ya chini unaliwaza mtoto. Msomee mtoto hadithi, kila siku mwimbie nyimbo. Msaidie pole pole kukariri mafungu na nyimbo inatanua ubongo! Rafiki yangu mmoja aliweka mkanda wa Neno la Mungu wakati mtoto amepumzika, alimsaidia mtoto kukariri mafungu vizuri alipokuwa mkubwa na kulipenda Neno hili. Neno la Mungu, likitoka halitarudi tupu. Mtoto anayesomewa kila siku, japo mchanga, atajua kusoma mapema, na kuelewa mambo.

Mtoto aweza kuzaliwa na shida za mtindio wa ubongo (phenylketonuria), ukosefu wa damu (sickle cell), damu kutoganda (hemofilia), matatizo ya misuli (Huntington), kudhoofika misuli (duchennes) tafadhali mwone mganga akushauri kuhusu upungufu wowote. Ila chukua muda usome zaidi kuhusu jambo hili, maana nimeona marafiki wengi waliojitahidi kufundisha watoto hata wale wenye shida (autisim, Down syndrome) na wakaweza kuendelea vyema, ukilinganisha na wale ambao wazazi walikata tamaa na kuwaacha wakae tu bila msaada wowote.

Nchi zetu zina shida ya walimu wa Special education, au walimu wa watoto wenye shida za kujifunza, ni maombi yangu kwamba siku za mbeleni taifa litachukua muda kusaidia watoto wenye changamoto hizi, na hawa wale ambao ni viziwi, vipofu, bubu n.k. Ukisoma Historia, watoto wengi kama Helen Keller, Fanny Crosby na wengineo, waliokuwa na shida fulani, walijifunza mengi na hata kusomea shahada na kutembea dunia nzima kutoa hotuba za kusaidia watoto wenye mahitaji maalumu (special needs children). Mzazi na hata mwalimu aweza kumpa mtoto moyo wa namna hii, kama vile mwalimu Ana alivyompa Helen Keller matumaini na akafanya mambo makuu ambayo hata walio bila vilema, hawakuyafanya!

Magonjwa mengine ya zinaa kama kaswende, kisonono, Herpes simplex, ukimwi au surua yana hatari kwa mtoto. Ni vyema upimwe ili usimwathiri mtoto.

Anza kujenga tabia ya kumsomea mtoto mdogo, Neno la Mungu na vitabu vingine. Kuwa na vitabu kunajenga tabia na kumfanya mtoto avithamini vitabu. Hata kama hujui kusoma na kuandika angalia jinsi ya kufanikisha zoezi hili!
Wazazi wengi wa magharibi wanalala vyumba tofauti na watoto wao. Waafrika wengi walioishi magharibi wanafikiri tabia hii inafanya mtoto na mzazi wasiwe karibu, na hivyo

kumfanya mtoto akimbie nyumbani mapema na kwenda kujitegemea! Kwa upande wangu naona ni tabia nzuri inayojenga kujitegemea ila ina hatari kama mtoto anaumwa au ana shida fulani. Ni vyema mtoto awe karibu.

Hata hivyo watu wengi wa Afrika tulizoea kulala na ndugu kwenye nyumba zetu. Hata wale wanaoishi wenyewe wana woga wa kulala wenyewe kwenye vyumba vyao wakiwa na umri mdogo au hata mkubwa! Nafikiri kama mama halewi au hana ugonjwa si vibaya akilala karibu na mtoto pengine kwenye kitanda chake au kando na mtoto mwenye kitanda chake. Mama mwingine mzungu nilivyomwambia hivi alisema "Pengine kwa sababu huko Afrika watu wananyonyesha watoto wao na ni rahisi kwa mama kumnyonyesha mtoto." Wengine wanasema mtoto mdogo awe na kitanda chake ili asipate magonjwa ya watu wazima. Nafikiri kama ni magonjwa atapata tu maana wakati wote unamshika na kuwa naye hata mchana. Nafikiri hapa utaona kile kinachofaa kwako. Wanaume wengine wamekataza wake zao kunyonyesha pia. Hapo nafikiri binadamu aliumbwa anyonye maziwa ya mama na si haki mtoto kunyimwa faida hii.

SURA YA 3

HATUA ZA KUKUA ZA MTOTO.

UTOTO (EARLY CHILDHOOD) – MIAKA 1 – 6

Miaka 1 –6 ni kipindi cha shughuli nyingi kwa mtoto. Uliwahi kushangaa jinsi chakula kidogo tu anachokula mtoto kinampatia nguvu za kuruka, kucheza na kufanya shughuli hizi zote siku nzima? Shughuli au michezo na watoto wenzake ni muhimu sana, ingawaje pia hupenda kukaa nyumbani na mama, kuhakikisha tu kwamba mama yupo karibu. Mtoto wa miaka mitano anaweza kuvaa mwenyewe, kufunga kamba za viatu, kupiga mswaki na kufunga vifungo vya nguo. Anaanza kupenda kupekua vitabu, hasa vya picha.

Mtoto huyu anaishi katika ulimwengu usio halisi, (make-believe world), yaani ulimwengu wa ndoto. Muda fulani anaweza kujifanya chura, farasi au hata injini ya gari ya zimamoto. Hawezi kutofautisha kati ya vitu vya kweli na vya kufikirika tu. Kwa mfano, anaamini kwamba

paka mkubwa mweusi ni dubu. Wakati huu mtoto anauliza maswali mengi sana, kama 'kwa nini?' 'Ni ya kufanyia nini?' n.k.

Kipindi hiki pia ni cha kuiga sana. Mtoto ataiga maneno, lugha au tabia mbaya bila kujali umuhimu au maana yake. Anapenda san kucheza, hata akiwa peke yake. Wakati huu hadithi za kurudia rudia (jingle and rhyme) zinamvutia sana. Anawaamini sana wazazi na kila kitu wanachomwambia. Wakati huu mtoto anatakiwa kujua ratiba (program) yake. Anatakiwa ajue anachotakiwa kukifanya. Mtoto asiyekuwa na sheria anakuwa hana ulinzi (secure) na atajisikia kuwa hapendwi na halindwi. Mtoto hawezi kufundishwa kwa kushauriana (reasoning) wakati huu. Anategemea sana wazazi ili kumpa mwongozo. Pia anahitaji sheria za kufuata, na huchanganyikiwa anapoombwa ushauri, au anapohusishwa kwenye majadiliano.

Kiroho, mtoto mwenye umri huu hupenda sana hadithi za Biblia, ingawaje wakati mwingine huogopeshwa na mawazo ya kwamba Mungu huona kila kitu anachokifanya. Mzazi ampeleke mtoto ibadani, japo mara nyingine wazazi wamechoshwa na yanayoendelea kwenye nyumba za ibada. Kama vituko au habari fulani ni muhimu, wasome Neno la Mungu na kuchagua ushirika unaofuata Neno la Mungu na maadili yaliyo bora. Kumbuka kama Nuhu angesema "safina inanuka na mavi ya simba humu, wacha nitoke" angepata shida. Aliishi mle karibu mwaka, hata kama kulikuwa na uvundo. Ila jitahidi uingie ushirika unaojifunza Neno la Mungu kwa ukweli, na kutekeleza. Twajua kwamba hakuna mtu mwenye kweli yote, ila msingi wa Ushirika uwe neno la Mungu na si mapokeo, au mawazo ya watu. Ukweli wa Neno la Mungu pia ni endelevu, tunazidi kufunuliwa tunaposoma.

Hii ndiyo miaka ya kujenga tabia ya mtoto. Hakuna wakati mzuri wa kufundisha utiifu kama wakati huu. Hivyo mzazi shika usukani mapema. Hata waswahili wanasema "samaki mkunje angali mbichi." Tunawalaumu sana vijana wa siku hizi, eti hawafanyi hiki au kile, hawana adabu, wanapenda anasa, wanavaa visivyo, hawapendi mambo ya kiroho, n.k. Kama hatupendi haya yatokee kwa watoto wetu, basi tuanze kuwafundisha mapema. Hasa kwa maisha yetu na lugha yetu pale nyumbani, hivi vitamuathiri mtoto sana.

Katika kitabu cha Learning to Live, Lora Clement anasimulia hadithi ya kweli ya mtu mmoja ambaye alijenga hoteli yenye ghorofa tatu. Kwa muda mrefu hii hoteli ilikidhi mahitaji ya mji huo mdogo. Siku moja mafuta yaligunduliwa karibu na mji huo. Biashara ikavuma sana, na hiyo hoteli moja tu katika mji ikawa inafurika kila siku. Mwenyewe akaamua kupanua hoteli yake. Akamwita mjenzi mashuhuri akamwambia aongezee ghorofa ya nne. Mjenzi akakubali, "Lakini lazima nione msingi." "Msingi wa nini!" Mwenye hoteli alishangaa! "Nataka uipandishe juu, siyo chini. Hebu twende kwenye paa nikuonyeshe." "Ndiyo, nafahamu. Lakini kabla sijaongeza ghorofa nyingine, ni lazima nione kama msingi ni imara, kiasi kwamba utaweza kustahimili uzito wa ghorofa nyingine." Akachukua vifaa vyake akapima upana na kina cha msingi. Kisha akatikisa kichwa kwa huzuni akasema, "Nasikitika. Huu msingi hauwezi kustahimili uzito wa ghorofa ya nne."

Mwenye hoteli alishikwa na butwaa kwa muda, asijue la kusema! Alikumbuka alipokuwa akijenga hoteli hii, mjenzi alimsihi ajenge msingi imara, "Kwa sababu, nani ajuaye, labda utahitaji kupanua hii nyumba baadaye." Akakumbuka alivyomjibu; "Siwezi kupoteza hela zangu, eti kwa ajili ya upanuzi wa baadaye, ambao, nani ajuaye kama utahitajika!"

Sasa upanuzi ulihitajika. “Je, unaweza kuufanya msingi uwe imara?” “Ndiyo, naweza. Lakini itakugharimu hela nyingi sana sasa, kuliko ambavyo ungeujenga tangia mwanzo.” Alimjibu.

Huu ndio wakati wa kuweka misingi mizuri ya tabia za watoto wetu. Wengi wetu tunafikiria watoto bado ni wadogo. Wataadabika wakikua. Si kweli. Wanahitaji wawe na msingi wa malezi bora wakingali wadogo. Miaka saba. Hebu tutumie wakati huu vizuri, tuwafundishe maadili mema, ya kumpendeza Mungu na wanadamu. Ndipo wataweza kustahimili uzito wa mambo mengi atakayopambana nayo maishani. Ni vigumu sana kurekebisha tabia wakiwa wakubwa. Kumbuka waswahili walisema, samaki mkunje ukingali mbichi.

MIAKA YA KATI YA UTOTO 7 - 9 (MIDDLE CHILDHOOD)

Umri huu pia ni wa shughuli nyingi, lakini hizi zinakuwa na malengo. Mtoto ana hamu ya kujua mambo, na ni mdadisi, hivyo anauliza maswali mengi. Ni vizuri kuyajibu maswali haya kwa uwazi na ufupi. Kwa mfano, ukiwa unakula, unaweza kumtuma mtoto chumvi au maji, na atauliza ‘ni ya nini?’ Usije ukawa mkali na kumkaripia mtoto, kwamba, “Huoni kwamba ninakula, kwani chumvi huwa ni ya nini!” Mjibu tu kwa upole kwamba, “Ninataka kuongezea kwenye chakula.” Akiuliza, “Kwa nini?” Mwambie, “Kwa sababu haitoshi.” Akiongezea, “Kwa nini haitoshi?” Mwambie, “Kwa sababu aliyepika hakuunga ya kutosha.” Hata akiendelea kuuliza kwamba kwa nini hakuunga ya kutosha, usimwambie hutaki au umechoshwa na maswali.

Hebu soma hadithi hii ya kweli. Mtoto mmoja wa miaka saba, alimuuliza mama yake: ‘Mama, hivi sisi tunatoka wapi?’ Mama yake alikuwa amejua kwamba mtoto akiuliza swali ni lazima ajibiwe kwa uwazi. Basi akafikiria sasa wakati umefika wa kuelezea mtoto mambo yote yanayohusu mfumo wa uzazi (reproduction). Akaanza kuelezea hiyo sayansi ya mfumo wa uzazi, jinsi yai la mama na mbegu ya baba vinavyokutana wanaposhiriakiana kimwili. Jinsi mtoto anavyokua tumboni hadi miezi tisa ndipo anazaliwa. Alielezea kwa muda wa kama dakika ishirini hivi, hadi mtoto akachoka. Alipomaliza, mtoto akiwa na uso wa kutoridhika na mshangao, alimwambia, ‘Mama hujajibu swali langu, nimekuuliza, sisi tunatoka wapi? Kama rafiki yangu Daudi anatoka Musoma, Je, sisi tunatoka wapi?’ Kwa hiyo ujibu maswali yote kwa uwazi na kwa ufupi tu, ukizingatia umri wa mtoto.

Mtoto huyu bado anapendelea hadithi lakini siyo za kufikirika tena. Anapenda hadithi za matukio halisi. Mara nyingi anauliza kama hadithi ni ya kweli. Sasa anataka awe injinia na siyo injini. Pia anapenda kucheza na watoto wengine na siyo peke yake. Muda wake wa kuzingatia mambo (attention span) ni mfupi, hivyo anahitaji kubadilishiwa matukio.

Mtoto wa miaka sita anaanza kujifunza kusoma na kuhesabu. Akifikia miaka saba atakuwa anaweza kuchora na kuandika vizuri. Mungu ni wa muhimu sana katika maisha ya mtoto huyu. Anategemea maombi yake yajibiwe mara moja jinsi alivyoomba. Bado anapendelea hadithi za Biblia na hufikiria sana kuhusu Mungu na mbingu. Mashujaa wa Biblia ni watu halisi kwake, na hupenda sana hadithi zao. Anapenda sana atambuliwe (approval) na wenzake. Pia anapenda mashindano na wenzake, mradi tu yeye ndiye awe mshindi. Kiroho, wanaanza kuuliza maswali mengi ambayo alikuwa wameyaamini zamani. Anaweza kujisomea Biblia na kuishi jinsi Biblia inavyoshauri. Anaona maana ya kuwa wakili (steward) mwema.

MIAKA 10 – 12 (PRE-ADOLESCENCE)

Kipindi hiki ni cha kelele na shughuli nyingi. Watoto wana afya ingawaje wanakua polepole. Hata hivyo wasichana wanakua haraka kuliko wavulana kimwili, kiakili na kihisia (emotionally). Wasichana huanza kuota matiti na nywele za sehemu za siri, pia wengi huanza kuona damu ya hedhi wakati huu. Pia hufikia asilimia tisini ya kimo chao. Wakifikia miaka kumi na miwili ndipo wavulana wanaanza kuwafikia wasichana. Wanalingana wanapofikia umri wa miaka kumi na minane hadi kumi na tisa.

Kiakili, wana uwezo mkubwa wa kukariri mambo waliyojifunza au kusoma. Ni wakati mzuri sana kuwapa mafungu ya kukariri kutoka katika Biblia. Wnafurahia sana kazi za kanisani, hasa wakiwa katika vikundi. Ni muhimu sana kuwasajili katika chama cha Skauti, au Watafutanjia (Pathfinders) ambako watafundishwa kufanya mambo mbalimbali katika vikundi vya madarasa yao. Mafungu niliyokariri nilipokuwa katika umri huu, bado nayakumbuka hadi leo! Wanahusudu sana watu waliofanikiwa na kufanya mambo makubwa. Wanaanza kufikiria kazi atakayoifanya baadaye.

Kiroho: Kipindi hiki ni muhimu sana, kwani watoto wana hamu sana na mambo ya kiroho na ya dini. Wanataka kujitoa maisha yao kwa Yesu na kuishi kwa ajili yake. Wengi wanajitoa ili wabatizwe katika kipindi hiki, hasa wenye umri wa miaka kumi na miwili. Ni wakati mzuri wa kuwafundisha mambo ya kiroho, kwa sababu wakati huu wanahusudu sana watu waliofanikiwa. Hivyo ni vizuri kuwapa mifano ya watu waliofanikiwa na mashujaa katika Biblia, k.m. Yusufu, Daniel, Esther n.k.

Kijinsia (social): Wavulana bado hawana haja sana na wasichana, na hata wasichana hawana haja sana na wavulana, hasa wa miaka kumi. Akimgusa kidogo, hata kwa bahati mbaya, ataenda kumsema kwa mwalimu. Wavulana wanapenda kuwa/kucheza peke yao, na wasichana pia. Nilipokuwa ninafundisha watoto wenye umri huu, walikuwa wanakataa kushikana mikono. Kama tungefanya mduara kwa kushikana mikono, wangeacha pengo kati ya mvulana na msichana.

Kiakili (mental): Watoto wa umri huu hupenda kuchunguza sana. Wanatoa (dismantle) vitu ili waone jinsi vilivyotengenezwa, kisha wanavitengeneza tena. Wanapenda hadithi sana na kusoma vitabu vizuri. Wana hamu sana ya kukusanya vitu. Wataalam wanasema asilimia tisini ya watoto wa umri huu wanakusanya kitu kimoja au kingine kwa wakati mmoja. Utakuta mtoto ana makopo, vyuma, vifuniko vya chupa, nyaya, nyuzi n.k. mifukoni. Ni wakati mzuri wa kusoma nishani (honours) katika chama cha Skauti au Watafutanjia (Pathfinders), ambako wanafundishwa kusoma na kukusanya vitu mbalimbali kama maua, miti, sarafu/stempu za nchi mbalimbali, wadudu, mbegu n.k. Hali yao ya usikivu bado ni ya chini. Mtoto anapenda kubadilishiwa matukio, hasa ambayo hayana shughuli nyingi.

Kimwili (Physical): Hiki ni kipindi ambacho mtoto ana afya nzuri sana. Anapenda kufanya mazoezi ya kukimbia sana. Anapenda lugha ya siri, lugha ambayo wazazi au waalimu hawaelewi, hata wakiwasema wakiwepo hawataelewa kwamba wanasemwa wao. Wanawapatia watu (hasa walimu) majina bandia. Huu ni umri wa kuhusudu, kiasi cha kuabudu mashujaa (hero au stars worship). Ni lazima wawe na watu mashujaa wanaowahusudu, kwa

hiyo ni vizuri kuwapatia mashujaa hawa, hasa wa biblia, manake usipowapatia, watatafuta wa kwao.

MIAKA 13 – 15 (EARLY ADOLESCENCE)

Kipindi hiki, watoto hukua kwa kasi sana kiasi kwamba viungo vingine vya mwili vinakua haraka kuliko vingine. Kwa mfano pua, mdomo au miguu inaweza kurefuka kuliko sehemu nyingine. Wanakuwa na hofu kwamba labda watabakia vile vile. Siyo vizuri kuwatania, au kuwatukana 'miguu mirefu kama swala, pua ndefu au ona anavyofanana!' Kijana huyu yuko macho lakini anaota mchana (day-dream); akiwaza na kuwazua atakavyokuwa katika siku za usoni. Anajifunza mambo mapya kwa kasi kubwa.

Kwa kawaida, mtoto wa umri huu, afya yake ni nzuri sana. Anapenda kula sana. Ni vizuri kuwa na chakula kingi wakati huu. Usimpimie chakula na usimseme kwa kumuabisha anapokula sahani mbili au zaidi. Sehemu za uzazi za mtoto zinaimarika. Wasichana wanakuwa warefu kuliko wavulana na wananza kusoma vitabu vya mapenzi. Mzazi, huu ni wakati wa kuangalia kwa makini. Vitabu vinavyosomwa viwe vya kusaidia maisha, na maadili. Wavulana wanapendelea zaidi michezo na mazoezi ya kimwili kama kukimbia. Matiti ya wasichana hujaa. Wote huanza kuasi wazazi. Wakifika umri wa miaka 12 – 13, wanaanza kuvutiwa na wale wa jinsia tofauti kwa kiwango cha chini, wakiwa na woga mwingi.

Huu ni wakati wa kuabudu vikundi (gangs), wakiogopa kuwa tofauti. Wanathamini sana marafiki zao, na hawataki kuwa tofauti au kupingana nao. Kijana anakuwa na malengo halisi na hupangia maisha yake yajayo. Hali (mood) yake inabadilikabadilika. Wakati mmoja anafurahi, na mwingine amekasirika na kununa bila sababu. Wakati fulani anapenda chakula fulani, wakati mwingine hakipendi. Wasichana wanapenda kuchekacheka (giggle) ovyo hata bila sababu. Katika miaka hii wavulana wanavutiwa na wasichana, na wasichana pia wanavutiwa na wavulana. Huu ni wakati wa hatari kwani watoto wanaweza kujaribiwa kuanza uhusiano wa kimapenzi wakati ambao ni wadogo na hawako tayari kuchumbiana. Hivyo waalimu na wazazi wa watoto wa umri huu wawe waangalifu sana. Wasiwaache peke yao bila mtu wa kuangalia shughuli zao.

Mambo ya kiroho hufifia wakati huu, lakini hutegemea marafiki zao wako upande gani. Wakiwa watu wa kiroho atawafuata, wasipopenda kwa mfano, kwenda kanisani, atawaiga. Kama tulivyosema awali, asilimia kubwa wanapenda kubatizwa wakiwa na umri wa miaka kumi na miwili. Kundi linalofuatia ni watoto wa miaka kumi na mitatu, nao hupenda kubatizwa katika wakati huu, na asipobatizwa wakati huu, baadaye hali ya kupenda mambo ya kiroho hufifia. Wengi wanachagua kazi watakazozifanya baadaye, wakati huu.

MIAKA 16 – 17 (MIDDLE ADOLESCENCE)

Katika kipindi hiki, wengi wao wanakuwa wamekomaa kimwili. Wavulana wamekomaa kimchezo na wasichana wanaanza kuumbika vizuri na kupendeza. Wengine wanaanza kuwa na chunusi, hivyo ni vema kula chakula bora ili wawe na nguvu, pia ngozi ya kupendeza. Mfano: Vitu vya sukari, kama peremende vinaongeza chunusi.

Kijana anafikia asilimia themanini na tano (85%) ya kimo chake katika kipindi hiki. Anaanza kujitambua na kujizatiti. Anataka vitu vilivyohakikishwa (proof) vya kila kitu kabla hajaamini. Anapenda sana wasomi na ataamini kila kitu ambacho mtu 'mwenye jina' au msomi atakachokisema. Ana mipango na malengo ya juu ya maisha yake, na anaweka mikakati ya jinsi ya kufikia malengo haya. Anapenda sana mazoezi ya kimwili. Sehemu za uzazi zinakomaa.

Anapenda marafiki wa kipekee (special). Yuko makini sana, na anafuata mawazo au mapendekezo ya rafiki zake. Yuko wazi kiasi cha kutojali hisia za wengine. Anawaza pia jinsi ya kupata fedha, na hata wengi wanaweza kuacha shule waanze biashara ili wapate fedha, hata kama ni biashara ya kuuza pipi.

Kiroho: Akiwa na marafiki wanaopenda mambo ya kiroho ataendelea, lakini hamu ya mambo ya kiroho na kwenda kanisani hupungua akikosa marafiki wazuri. Kama hakuwa na msingi bora, inakuwa vigumu kumfundisha kitu kipya wakati huu. Anaanza kufikiria dini itakayomfaa mwenyewe, na siyo lazima iwe ile ya wazazi. Wataalam wanasema kwamba, ni vigumu kufanya kwa watoto katika siku za usoni, kile ambacho hujakijfanya katika wakati huu. Mtoto alivyo sasa, ndivyo atakavyokuwa kitabia, atakapokuwa na miaka sitini! Hili linaniogopesha sana, ila kwa wanaomwamini Mungu, tunafahamu kwamba kwa rehema za Mungu Anaweza kubadilisha mioyo migumu ya mawe akaifanya ya nyama, wakati wo wote tunapojitoa kwake.

MIAKA 18 – 24 (LATER ADOLESCENCE)

Katika kipindi hiki, kijana anakua polepole kimwili, ili afikie kimo chake, yaani asilimia kumi na tano (15%) zilizobaki. Waliochelewa kukua huwa wanawafikia wenzao katika kipindi hiki.Tabia imeimarika wakati huu. Mwelekeo wa kijana hueleweka karibu na kila mtu, kwamba ni mcha Mungu, mlevi, mgomvi, mcheshi, mkarimu, mwadilifu, n.k. Kila mtu atamfahamu kwa tabia hiyo. Ni kipindi cha kutafuta mwenzi wa maisha na kufikiria kujenga unyumba.

SURA YA 4
WATOTO KATIKA BIBLIA

Biblia ina mifano ya watoto wengi waliofanya makuu Mfano Yeremia aliitwa akiwa mdogo sana, na hata MUNGU alimwambia asisiseme kwamba yeye ni mdogo. Hata watoto wachanga MUNGU huwaita. Tutazungumzia kuhusu watoto wachache katika Biblia. Samuel alikuwa mtoto wa nadhiri. Mama yake alimwomba kwa Mungu, na akatoa nadhiri kwamba angemtoa kwa Mungu milele. Katika 1Samuel 1:10-11 tunasoma; "Naye huyo mwanamke alikuwa na uchungu rohoni mwake, akamwomba BWANA akalia sana. akaweka nadhiri, akasema, Ee BWANA wa majeshi, ikiwa wewe utaliangalia teso la mjakazi wako, na kunikumbuka, wala usinisahau mimi mjakazi wako, na kunipa mimi mjakazi wako mtoto mume, ndipo mimi nitakapompa BWANA huyo mtoto siku zote za maisha yake...."

Imani ya mama huyu ni ya pekee. Hakuwa na mtoto ye yote. Alimwomba Mungu ampatie mtoto mume, na aliamini kabisa kwamba Mungu atampatia. Mtoto wake pia akawa wa pekee (kuhani, nabii na 'Rais' wa nchi) kwa sababu ya imani na malezi ya mama yake. Kwa miaka michache tu (3-4), Hana alimfundisha mtoto wake kumcha Mungu kama yeye, na akawa mbaraka mkubwa katika taifa zima la Israeli. Mungu alizungumza na huyu mtoto mdogo tangu akiwa mdogo hadi maisha yake yote. Hana aliitilia maanani kazi yake ya malezi. Alihakikisha kwamba Samueli alijua (hata akiwa mdogo) yeye ni nani, kwa nini alizaliwa, na madhumuni yake ni kumtumikia Mungu. Alipokuwa anamtembelea kila mwaka alimkumbusha kwamba yeye ni nadhiri ya Mungu.

Jamani, hapa tuna changamoto kubwa!!! Huwa tunafikiria kwamba mtoto wa miaka mitatu hadi mitano ni mtoto mdogo hajui cho chote. Hapa tunaona kwamba huo siyo ukweli, maana Samueli alikaa na mama yake kwa miaka michache tu, na aliweza kumsimamia na kumtumikia Bwana kwa miaka yake yote. Hata Mungu akamtumia kutangaza hukumu kwa nyumba ya kuhani Eli! Wataalam wanasema kwamba tabia ya mtoto inaimarika katika miaka sita ya kwanza. Hebu tutumie miaka hii kuwafundisha lengo lao katika maisha, ambalo ni kumtumikia Mungu.

Mfano mwingine katika Biblia ni wa mtoto Musa. Musa alizaliwa Misri wakati wana wa Israeli walikuwa wanateswa na amri ya kuuawa kwa watoto wa kiume ikiwa imetolewa na mfalme Farao. Mama yake alimficha kwa muda wa miezi mitatu (Kutoka 2) na alipokuwa hawezi kumficha tena, alimtengenezea kisafina cha nyasi akamtia ndani, akakiweka katika majani kando ya mto. Binti Farao alipokwenda kuoga, akakiona, akasema; "Mchukue mtoto huyu, ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako. Yule mwanamke akamtwaa mtoto, akamyonyesha. Mtoto akakua, naye akamleta kwa binti Farao, akawa mwanawe." Kutoka 2:8-10.

Wataalamu wa Biblia wanasema kwamba Musa alirudishwa kwa binti Farao akiwa na umri wa miaka kumi na miwili tu!! Na hiyo ilitosha kabisa kumfanya ajue nia (purpose) yake ya kuishi, kwamba ni kumtumikia Mungu. Musa alisomeshwa katika shule za kifahari za misri, ambako watoto wa ikulu walisomea. Alipata elimu ya juu sana, akiandaliwa kuwa mfalme wa Misri baadaye.

Wapendwa, miaka kumi na miwili tu ilitosha kumfanya Musa afanye maamzi makubwa kama tunavyosoma katika Waebrania 11:24-27; "Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri,....."

Inawezekana kabisa hata leo kuwafundisha watoto wetu, waone kwamba kumtumikia Mungu ni bora kuliko kujifurahisha na anasa za dunia hii, ambazo ni za kitambo kidogo tu. Shetani anajua muda wake ni mfupi sana, tena sana. Ndiyo maana ameleta anasa nyingi za kufumba watoto wetu macho, ili wajitose ndani na kusahau kujiandaa kwa ajili ya ufalme. Hebu mfano wa Musa ututie moyo watu wa Mungu, kwa sababu kama ni anasa na vitu vya kuburudisha, hakuna vinavyozidi vile vya ikulu. Unaagiza tu vinaletwa, unakohoa tu unahudumiwa, lakini Musa aliyaona hayo yote kuwa ni ubatili na ni ya muda kitambo.

Hadithi ya Yusufu ni ya ajabu. Kijana aliyezaliwa katika familia kubwa ya wake na watoto wengi. Familia hii ilikuwa na vituko vingi, kama mitara yenye wivu wa ajabu, kijana Reuben kulala na mama yake wa wakambo, ulaghai wa baba, mama kuiba vinyago aviabudu, kaka Yuda kumchukua Kahaba, Kaka wakatili kuua kijiji kizima, dada kubakwa, mjomba Labani kutolipa mishahara vizuri, baba na Esau jiko lao, mama na Yakobo jiko lao na mengineyo. Mama ya Yusufu alimuonea dada yake Lea wivu sana, maana alikuwa anazaa na yeyé alikuwa hana mtoto. Baadaye ndio Mungu alimbariki akazaa Yusufu na nduguye Benjamini. Ndugu zake, wa kambo, walimuonea wivu sana kiasi cha kutaka kumuua. Baadaye waliamua kumuuza kwa wafanya biashara Waishmaeli, waliomchukua Yusufu hadi Misri; (Mwanzo 37:27-28). Huko Misri alinunuliwa na Potifa, akida wa Farao. Mke wa Potifa alipomtamani akamlazimisha azini naye, Yusufu alimwambia hivi; "....tazama bwana wangu (Potifa) hajui kitu kilichowekwa kwangu nyumbani, na vyote alivyo navyo amevitia mkononi mwangu. Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuilia kitu cho chote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkosee Mungu?" Mwanzo 39:8-9.

Mama yake Yusufu, Raheli alikufa wakati Yusufu alipokuwa kijana mdogo sana. Hii ina maana kwamba Yusufu aliona mfano mzuri kwa baba yake Yakobo ambaye aliishi maisha ya kumcha Mungu. Maombi na kafara za kila siku, pamoja na hadithi alizomsimulia Yusufu kuhusu maisha ya baba yake Isaka na babu yake Ibrahimu, zilimvutia sana Yusufu mpaka akatamani kumtumikia huyu Mungu wa baba na babu zake.

Je, maisha tunayoishi, kama wazazi, yanastahili kuigwa na watoto wetu? Je, tunafanya ibada za asubuhi na jioni nyumbani mwetu? Je, tunawasimulia juu ya makuu ambayo Mungu ametufanyia katika maisha yetu, kiasi kwamba watoto wetu wamtamani huyu Mungu tunayemwamini? Je, inawezekana tuwe na watoto kama Yusufu leo? Wapendwa inawezekana. Kuna vijana wengi waliokwenda nchi za ng'ambo na wamesimama imara kama Yusufu, wanang'aa na kumuangazia Mungu wao. Hawafanyi vituko kwa sababu wako mbali na wazazi au washiriki wanaowafahamu. Wanamcha Mungu wakijua kwamba yeye peke yake ndiye anajua "kila neno la siri, likiwa jema au baya." Mhubiri 12:14.

Baadaye, wakati ndugu zake Yusufu walipokuja kununua chakula Misri, waliogopa sana na kuingiwa na hofu kuu, hasa Yusufu alipojitambulisha kwao! Walijua huo ndio utakuwa mwisho wao, kwa sababu Yusufu alikuwa na uwezo mkuu. Alikuwa kama makamu wa Raisi au Waziri Mkuu wa leo. Angeamrisha askari tu, na mara moja wote wangeangamizwa. Lakini aliwaambia hivi: "Karibuni kwangu,....Mimi ni Yusufu, ndugu yenu ambaye mliniuza kwenda Misri. Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku; maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu,.....na kuwaokoa ninyi kwa wokovu mkuu. Basi si ninyi mlionipeleka huku, ila Mungu;.....naye ameniweka..... kama mtawala katika nyumba yote ya Misri." Mwanzo 45:4-8. Ndiyo, tukiwafundisha watoto wetu kumtanguliza Mungu kwa kila jambo, hawatalipiza kisasi. Watawapenda hata wanaowachukia.

Kuna hadithi nyingine ya msichana mdogo katika kitabu cha Wafalme wa pili sura ya 5. Msichana huyu, ambaye jina lake halikutajwa, alichukuliwa mateka kutoka katika nchi yao ya Israeli kwenda katika nchi ya maadui wao ya Shamu. Angekuwa na sababu zote za kukata tamaa, na kudhani kwamba akiwa mbali katika nchi ya ugenini, kati ya watu wasiomcha Mungu, hakuna kitu ambacho angeweza kufanya.

Kama Yusufu, alifanya kazi yake kwa bidii na kwa uaminifu, la sivyo asingepelekwa kufanya kazi kwa kamanda na jemedari mkuu wa jeshi la mfalme wa Shamu. Hata hivyo msichana huyu hakusahau kwao, na hasa Mungu wake. Wala hakuwa na kinyongo na hawa aliowafanyia kazi kwa sababu ya kusambaratisha taifa lake. Aliwapenda, alimhurumia na alimwombea Naamani ili apone. Akamwambia mke wake, " Laiti bwana wangu angekuwa pamoja na yule nabii aliyeko Samaria! Maana angemponya ukoma wake." 2Wafalme 5:3. Alikuwa na imani kwamba nabii Elisha angeweza kumponya. Ingawaje ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya, na haukuwa na tiba, lakini msichana huyu alikuwa amefundishwa na wazazi wake kwamba hakuna kisichowezekana kwa Mungu.

Wazazi walikuwa wamefanya kazi yao ya malezi vizuri. Matokeo yalikuwa huu ushuhuda wa ajabu kutoka kwa msichana huyu mdogo, juu ya Mungu wa kweli katika nchi ambayo ilikuwa hata haimtambui. Naamani alijifunza kwamba kuna nguvu zinazaoshinda nguvu za majeshi yote ya binadamu, kwa sababu ya wazazi waaminifu waliokuwa mbali, waliofundisha mtoto wao kumpenda na kumwamini Mungu.

Kisa hiki kinanifanya nifikirie kina mama tunaoweka mayaya nyumbani, ili watusaidie kulea watoto na kufanya kazi za nyumbani. Wengi wetu hatuwathamini dada hawa. Tunawatesa na kuwadharau na kuwakejeli. Hatuli nao mezani, kwa mfano, ila tunangoja tukishamaliza kula tuwaite watoe vyombo, na kula mabaki. Wengine hata wanakula chakula tofauti na cha hao mabinti. Wakila nyama/samaki, wao wanakula mboga za majani. Wakikosea kidogo, tunawabandika matusi kibao! Ndiyo maana kuna hadithi nyingi sana kuhusu wasichana wa kazi, wanaoshirikiana na majambazi, kwa kuwafungulia mlango, wawaibie mabwana zao ili wawakomeshe na kuwalipizia kisasi! Wengine wanawatesa watoto, wanawanyima chakula, au kuwapatia chakula kichafu. Msichana mmoja alikuwa anatemea chakula cha mtoto mate, kabla hajampatia, ili kumkomesha mama wa mtoto!

Ninaamini mke wa Naamani hakumtendea hivyo huyu msichana, na kama alimtendea hivyo, (kwa sababu watumwa walikuwa na hadhi moja kama wanyama wa kufugwa) na bado aliwahurumia akawaambia siri ya uponyaji mahali iliko. Kwa kweli, msichana huyu alikuwa wa pekee sana kama Yusufu. Hakupenda kulipiza kisasi. Haya yote ni matokeo ya malezi mazuri. Tuwe na wakati na watoto wetu, wanapokuwa wadogo, na kuwafundisha maadili.

Ninaamini kwamba, inawezekana kabisa kuwa na mtoto kama huyu msichana. Inawezekana kuwa kama Yusufu, Musa, Samuel, Daniel, Esther, leo hii, hata wakiwa katika nchi za mbali. Je, unaniunga mkono? Itategemea tu, na muda tulionao wa kuwafundisha wakiwa wadogo, na pia mfano wa maisha yetu tunayoishi. Methali 22:6 inasema, "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee." Hili fungu tutalirudia mara kwa mara, kwa maana ndilo 'JAMBO MUHIMU.' Baadaye tutaona hii 'njia impasayo' ni ipi. "Naam hamkupata kusoma kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa"

Katika Yohana 6, twasoma kisa cha mikate mitano na samaki wawili. Kristo alishirikisha watoto katika huduma yake. Tusihudumie watoto kwa kuwa tu wengine nao wanafanya hivyo au kwa kuwa twapata faida au huruma, maana huruma yaisha. Moyo wa Mungu kwa watoto ni wa ajabu. Ishmaeli, mtoto wa Hajiri alikuwa amepoteza matumaini. Ishmaeli alikuwa na maumivu ya kufa Mwanzo 21:17 'Mungu akasikia sauti ya kijana 'nitakufanya kuwa taifa

kubwa'. Taifa kubwa ni baraka, ikiimanisha watu wanaojiamini, wabunifu, wenye kuheshimiwa na kutambulika duniani kote.

Hajiri huwakilisha wanawake wengi duniani wanaopewa mimba na kuachwa wametelekezwa, wakihangaika na watoto peke yao. Wajane wengine, wameachwa na mali ambazo zilinyang'anywa na ndugu, na hivyo kupoteza matumaini kwa kuwa hawana chakula cha kuwanusuru watoto wao. Hajiri anasikia uchungu na kuyatambua maumivu ya Ishmaeli, ambaye anawakilisha watoto wengi wanaoachwa kwa maumivu na hata kufa na kuharibika bila uhakika wa kuwa na chakula cha kufaa wakati wote na hawana uhakika wa kupata matibabu. Wengi wanaachwa na uangalizi wa TV na dhana potofu. Hawana faraja au kwenda shule. Watoto wengi wameachwa na familia zao, shule zao, siasa zao, serikali na makanisa yao. Wengi wako mitaani wakipambana na hatari nyingi. Mungu husikia kilio chao katika mazingira magumu. Zab 139:13-16 Zab22:9-11 Yak 1:27 Zab 68:5,6 Mith 22:6 ef 6:2 Wal 18:21 Kut 22:21-23 ab 72:4 Mat 18:6 lam 2:19 deut 6;6-9. Mafungu haya yanatuelekeza tufundishe watoto wasitangetange. Hajiri anakuwa mtu kwanza kuandikwa kwamba alikutana na malaika! Kweli MUNGU huona, husikia na ana huruma na hufariji katika shida zetu wazazi.

Kama vile Ishamaeli, watoto wengi wanasafiri na kukosa matunzo kwa shida za talaka! Sisi tumkabidhi Mungu watoto wetu, mimi nami nimempa. Uwe na mategemeo makubwa yatamsaidia mtoto kufikia malengo makubwa.

Wanafunzi waliwafokea (Math 18:1-5) wakina mama waliokuwa wanaleta watoto kwa Yesu, kwa madai kuwa "ana kazi nyingi mno" lakini Yesu bado alikuwa na muda nao. Watoto wakiimba Hosana na kupunga matawi ya mitende, walipigwa marufuku kuleta kelele, bali Kristo alisema "endapo hawa watanyamaza kunisifu, mawe yatapiga kelele". Hata leo twaona mawe mengi ya Radio na TV yakipiga makelele.

Agizo ni enendeni 28:19,20 Enendeni ni agizo, siyo ushauri, pendekezo, jambo zuri, au atakayejisikia au linalokubalika. Neno 'Mkawafanye' humaanisha kutia bidii. Hata watoto wanapaswa kuwa wanafunzi wake!

Mwanadamu aweza kuwa na akili sana (very intelligent) na kubuni mengi, hadi kwenda kwenye mwezi, ila asipomtii Mungu, hatima ya mataifa huwa katika mapungufu.

SURA YA 5

MAZIWA YA NG'OMBE AU MAZIWA YA MAMA?

(Kuchagua maziwa ya makopo au ya mama).

Kazi za mama ni nyingi na kunyonyesha ni mojawapo. Mungu alijua mwanamke akijifungua atakuwa na shuguli nyingi na atapumzika tu wakati akinyonyesha! Wakina mama wangapi waweza kufanya kazi nyingine wakinyonyesha? Ni vigumu sana, inabidi watulie mahali pamoja. Huu ni wakati wa mama kuendelea kula vyakula bora. Mama mja mzito huambiwa na watu ale chochote ambacho ana hamu nacho! Ushauri huu ni potofu. Maisha yake na ya mtoto yanamtegemea katika kipindi cha ujauzito na kipindi cha kunyonyesha. Yapaswa awe na kiasi (self control) kwa kile anachokula. Asifanye kazi kupita kiasi. Mchoko wa mama au msongo vinaathiri ubora wa maziwa na uchangamfu/haiba ya mtoto. Mama awe mcheshi maana haiba yake inaakisiwa na mtoto. Hebu mume wake awe mfariji na kuonyesha upendo wakati huu, ili ucheshi wa mama uwe rahisi kuonekana kwa mtoto.

Chakula bora kwa mtoto aliyezaliwa ambacho kimetolewa ni maziwa ya mama. Ndiyo maana tuliumbwa nayo. Matiti ya mwanamke yana kazi mbalimbali kama vile urembo, na kutoa vichocheo vya kike (womenhormones). Ni ukatili wa mama, kwasababu ya furaha au shuguli zake aache kunyonyesha (Convenience and social enjoyment). Mama anayemruhusu mtu mwingine ampe mtoto wake chakula, ajue kwamba huyo anayemkabidhi jukumu hilo, ndiye atakayemvuta mtoto kitabia. Kumfundisha mtoto chakula bora ni muhimu kwa mama, na hili linapaswa kuanza kutokea mwanzo.

Mtoto mdogo ajue anakula ili aishi na siyo anaishi ili ale. Mafunzo yaanze utotoni, akiwa mkononi. Mtoto awekewe masaa ya kula. Kwa mtoto mdogo anyonye kila baada ya masaa matatu. Mama wengi wakiona mtoto analia anapewa ziwa kama kitulizo. Watoto wengi wamekuwa walafi kuanzia utotoni kutokana na tabia hii. Ni vile chakula si kingi mahali pengi, tungekuwa na watu wengi ambao ni wanene kama nchi zingine zenye chakula kingi. Hali ya ulafi ikiendelea inamfanya mtoto asishinde vishawishi au majaribu kwa urahisi. Tabia njema yatokana na kujikana nafsi, kutawala nafsi, kutii na kuwa na mipango.

Mtoto anyonye maziwa kwa miezi 4-6 bila chakula kingine isipokuwa maji. Mtoto asipewe peremende au vitu vitamu vya aina hiyo au chakula cha watu wazima ambacho tumbo lake halitayeyusha. Ni ahadi ya Mungu, "Mlee mtoto katika njia impasayo naye hataiacha mpaka atakapokuwa mzee". Kunyonya ni haki ya mtoto, asinyimwe hii kama afya ya mama inaruhusu. Jinsi mtoto anavyokua, hatua na umakini uchukuliwe kuwafundisha ladha na tamaa ya chakula. Mtoto asiwe akila kila ovyo ovyo; atafikiria kwamba mlo ndiyo kilele cha maisha yake hapa duniani.

Ulafi unaleta magonjwa mengi hasa siku hizi. Wazazi wazifunze ndimi za watoto wao kufurahia ladha za vyakula vya afya. Vyakula hivi ni vile vya asili, tulivyoumbwa tuvile. Tusichukue muda mwingi kubuni mapochopocho ambayo yanachukua muda na kuharibu chakula cha asili. Nimeona watu wakipika nyama na kuweka sukari na mananasi! Watu wengine wanasema wao hawali nyama ila wanakula mifano fulani ya soya au

magome iliyowekwa kemikali nyingi na kukobolewa kwa kutisha. Usilazimishe kwa nguvu watoto kula vile ambavyo vina ladha isiyokuwa nzuri. Watavizoea wakikua, mfano mgagani, uyoga, beet root, na maparachichi watoto wengi huchukua muda kuvizoea. Ila mengi ya chakula yahitaji hekima, maana mtoto asikatae kila kitu, kuna vitu vya muhimu kula!

Wazazi wengi wenye watoto wadogo wa miezi, badala ya kuwabebea watoto matunda wanabeba vyakula ambavyo hata kwa sisi watu wazima ni sumu. Mfano chips, nyama za kukaanga, keki, bisukuti, mchele uliokobolewa, coca cola, mikate myeupe, maandazi meupe n.k. Watoto ni watu kamili, wana uchaguzi wa vyakula, na kama havipingani na bajeti au kanuni za afya, wape! Lakini usifanye mtoto awe kisultani kidogo, ukiwa na watoto watano, na kila mtu anataka kitu tofauti, na baba pia, utachanganyikiwa! Ni vyema mtoto ale mboga na matunda kila siku. Nimeona watoto wengine ukiwapa mboga hawali, ila nyama wanaibugia hapo hapo!. Mtoto asile katikati ya milo. Inaharibu afya na kisha wakati wa kula anakuwa hana hamu ya chakula.

Kina mama ambao hawajali tamaa za chakula za watoto wao, watavuna baadaye. Ulafi wa chakula (no self control) unaathiri dhamira na mafikara ya watoto tunajua “bustani ya Eden ilipotea kwaajili ya chakula na itarudishwa kwa kutawala tamaa ya chakula”. Watoto wasione kwamba wanajitoa mhanga kwa kukosa kile wanachotaka ila wanafanya kile ambacho kitakuwa kizuri kwa afya. Watoto wengi wameugua kwaajili ya kula ovyo au kutovaa vizuri wakati wa baridi. Hebu wazazi watafute sababu ili waweze kuwasaidia watoto hawa. Malezi bora si kitu cha kubahatisha bali ni mipango.

Faida za mama kunyonyesha mtoto ni nyingi kama vile:

1. Mama na mtoto wawe karibu zaidi.
2. Kuongeza kinga ya mwili ya mtoto – kukinga maradhi na alergy
3. Maziwa yanakuwepo wakati wote yana joto la kufaa na hayana vijidudu vyovyote (sterile).
4. Maziwa ya mama yanayeyushwa kirahisi tumboni na yana wanga, mafuta, vitamini, madini na protini inayoenda sambamba na mahitaji ya mtoto. Maziwa ya ng’ombe yanapaswa kutiwa maji, maana lishe yake ni kwa ajili ya mtoto wa ng’ombe ambaye anatembea siku hiyo hiyo
5. Mtoto anakuwa na michubuko michache ya mkojo.
6. Kunamfanya mama kuondoa uzito usiotakiwa ambao aliupata wakati wa ujauzito
7. Ni njia ya uzazi kupanga uzazi wa majira. Anaponyonyesha huwa hapati ujauzito mwingine.
8. Mwili unatumia kila kitu bila kubakisha makapi mengi.
9. Kinyeshi cha mtoto hakina harufu au gesi au matumbo kuumauma.

MAZIWA YA NGOMBE

Katika wanyama wote duniani ni binadamu tu anayekunywa maziwa ya wanyama wengine. Wanyama wengi wana maradhi mengi, ndiyo sababu wanapewa madawa ya kuua vijidudu (antibiotic), pesticides (dawa za kuua wadudu ili kupunguza inzi au mbung’o), dawa za chanjo na vichocheo ili kufanya wakue haraka na kutoa maziwa mengi (hormones). Imefika wakati wa kujiuliza kama ni muhimu kunywa maziwa? Tamaa ya pesa kuliko utu katika biashara nyingi imejitokeza. Magonjwa mengi kama kifua kikuu (brucellosis), anthrax (kimeta), ndigana na kuru. Ugonjwa wa kuru (Jacob Krustfield) na

mengine yameua wengi. Kuru ilitokana na kulisha ngombe na mifugo mingine kama kondoo na kuku ili wakue haraka.

Mfumo wa uyeyushaji wa mwili wa wanyama hawa unaathiriwa na nyama, kwani wameumbwa kula majani. Inasemekana kwamba wafugaji wengine wanawapa kuku dawa za ukimwi ili wanenepe haraka!. Wanyama wanaokula mimea (vegetarians) wakila nyama hupata maradhi ya ubongo na kuwaambukiza watu wanaokula nyama hizo. Mamilioni ya ng'ombe kule Uingereza waliuwawa, na chakula cha wanyama hao kiliteketezwa. Hata hivyo wapo wanaosema kwamba chakula hicho kilibadilishwa kwenye mifuko mingine na kutumwa kwa mifugo ya nchi nyingine.

1. Maziwa yana bakteria wengi kama Salmonella, E .coli. kwajili ya lishe iliyopo.
2. Maziwa yana mafuta mengi kuliko mwili unavyohitaji. Mafuta mengi kwenye mwili hufanya watu wanenepe, huongeza kisukari, na kuziba mishipa ya fahamu.
3. Kwa miaka mingi tuliambiwa kwamba maziwa ya ng'ombe ni mazuri kwa kuimarisha mifupa ya watu wazima na ya watoto. Utafiti mwingi wa karibuni umevumbua kwamba watu wenye mifupa migumu kupita wote duniani ni wabantu chini ya jangwa la Sahara. Cha kustaajabisha ni kuwa watu ambao wanakunywa maziwa mengi duniani, wanatoka kwenye nchi zenye maziwa, ambazo hazina wabantu. Nchi za Skandinavia kama vile Denmark, Sweden, Norway na Finland na zingine za Magharibi zinaongoza kwa unywaji wa maziwa. Wanawake wa nchi hizo wanashida ya mifupa kujengeka kuliko nchi nyingine. Kwa kawaida wanawake ndiyo wana shida ya mifupa kuliko wanaume. Mifupa inakuwa myepesi na kuvunjika kirahisi (osteoporosis). Sababu zilizotolewa juu ya uimara wa mifupa ya Wabantu ni kuwa wanabeba mizigo mizito, wanakula mboga za majani na wanapata jua kwa mwaka mzima. Wazazi wanapaswa kuishi kwa ajili ya watoto wao zaidi ya marafiki zao na jumuiya.
4. Sehemu ya maji ya maziwa inaitwa whey na ile ya kuganda inaitwa casein. Hii casein inaleta (mzio) allergy kwa watu wengi. Ukiwa na magonjwa ya mapafu kama asthma, kukohoa au mapafu acha maziwa ni adui yako. Ukitokewa na vipele na vivimbe jaribu kuacha maziwa. Maziwa, mayai na nyama kama vile za kondoo zina mzio (allergy) mkubwa kuliko mimea.
5. Maziwa yamekuwa biashara kwa watu wengi na itakuwa vigumu watu kukubali kwamba ni wakati wa kuacha maziwa. Wale ng'ombe wa kienyeji walitoa lita tatu hivi kwa siku za maziwa. Yalikuwa na ladha nzuri bila madawa au vichocheo.
6. Siku hizi mambo yamebadilika.
Kumekuwa na watu wengi wanalangua maziwa na kuuza kiasi kwamba mengine yanaozea njiani kirahisi.

Rafiki anayefanya kazi kwenye kiwanda cha maziwa aliniambia maziwa haya yanawekwa dawa ili kuyafanya yasigande haraka. Dawa hizi zingine zina madhara na sumu kwa binadamu. Dawa hizo ni kama vile formaldehyde, sodium hyroxide au boric acid. Kweli twapaswa kuchemsha tu maziwa "pasteurization" na si halali kwa yeyote kutumia haya madawa. Ila ni nani kweli atakuwa polisi wao kila siku? Kwa tarifa yako tu formaldehyde hutumiwa kutunza maiti ili isiharibike. Japo wanaweka kidogo kwenye hayo maziwa, lakini bado ni sumu. Nchi nyingine za Magharibi pia zinaweka dawa hiyo kwenye nyama ili isharibike kirahisi. Nafikiri wameruhusiwa kwa uchache.

7. Mara baada ya ng'ombe kukamuliwa kuna bakteria 10,000 kwa mililita ya maziwa na baada ya masaa matano wanafika milioni moja! Kama watu wanakunywa maziwa hapo hapo hatari hupungua na hivyo formaldehyde na hydrogen peroxide huwa haina haja ya kuwekwa.

8. Maziwa yanafanya makamasi kuwa mengi kwenye mfumo wa kupumua na kuongeza gesi na shida za tumbo. Kama una allergy au asthma au sinus, ni bora uache maziwa kabisa. Ngombe nao wanaongezeka kuwa na magonjwa kwa ajili ya unene. Hukaa mahali pamoja wakila na kunywa kwenye uchafu mwingi bila kusogea na wengine hawana mwanga wa kutosha

9. Tumeshaambiwa mara nyingi kwamba maziwa ni kitu cha asili na kila mtu anayahitaji. Kitu cha ajabu ni kuwa, maziwa haya si yale ya asili kwani yana bakteria wengi na yanahatarisha maisha. Ng'ombe hawa wanakuwa na misongo na kutoa vichocheo vya cortisol ambavyo si vizuri viingie katika mwili wa bindamu.
10. Watu wengi wazima – takribani 75% hawawezi kuyeyusha vizuri maziwa (digestion).
11. Tujue kwamba ng'ombe anaweza kuwa mzima asubuhi na kufa jioni. Pia watu wanaokamua wanaweza kutumia dawa kwa matiti ya ng'ombe kupungua mastitis.
12. Maziwa yameonekana pia kuwa na aina ya sumu zinazotokana na fungus zinazoitwa aflatoxins. Fungus hizi zinakuwa kwenye chakula wanacholishwa ngombe. Hizi zaweza kuharibu ini, figo, na mfumo wa kupumua. Utafiti wa mwaka 2005 kwenye nchi moja ya Afrika Mashariki ulikuta 44% ya maziwa yana aflatoxin. Na hii siyo shida tu Afrika hata nchi nyingine za Magharibi zinakuwa mpaka 25% na hii shida ipo kwenye nafaka zake. Kuna teknolojia inayoitwa mycosorbs ya kunyonya hizi sumu za fungus ila asilimia 50% ya wenye maziwa hawatumii kwa vile ni ghali sana.
13. Jibini (cheese) nayo ina shida nyingi japo hapa kwetu hatuitumii. Kutengeneza jibini mara nyingine hutumia rennet ambayo ni kichocheo (enzyme) kinachotoka kwenye tumbo la ndama au mtoto wa nguruwe. Hii inavunja protein ya maziwa na kuibadilisha. Yasemekana ili Swiss cheese itengenezwe ni lazima kuwa na rennet. Ganda lile la cheese laweza kuwekwa mafuta ya taa au mafuta ya mimea na rangi ya chakula ya njano. Jisomee zaidi jinsi jibini inavyotengenezwa. Hata cheese inayoitwa cottage si salama siku hizi. Angalia jinsi ya kutunza, isiharibike na mambo mengi ambayo huwekwa. Jibini ya kijani inaozeshwa kabisa na fungas na wanatumia bakteria kuozesha. Bakteria ni wengi sana kwenye jibini, mpaka milioni mbili kwa gramu moja.

14. Wakati mwingine pareto inawekwa ili wadudu (mites) wasiingilie na kuila. Jibini ni maziwa yaliyooza yenye bakteria na mafuta mengi ambayo yatazidi kuongeza mafuta ya cholestrol kwenye damu. Maziwa yanatoka kwa ng'ombe wengi ambao wanaumwa. Kama unaweza kuiepuka fanya hivyo.

SURA YA 6
MTOTO SHULENI

Elimu au shule ya mtoto huanzia nyumbani, kwani ndiyo shule ya kwanza ya mtoto. Shule hii ndiyo itamfundisha mifumo na kumpa miongozo atakayoifuata katika maisha yake yajayo. Miongozo hii ni pamoja na mahusiano na Muumba, heshima, utii, uadilifu, upole, kujizuia (self control), upendo, na unyenyekevu, ambavyo hufundishwa nyumbani, kwa mifano na matendo. Masomo haya ndiyo yatamfunulia ujuzi wa kujua mema na mabaya. Mtoto asipopata mfunzo haya nyumbani, shetani atamfundisha mengine baadaye. Baba na mama ndiyo waalimu wa kwanza wa mtoto, kazi ambayo ni muhimu sana kuliko ya mwalimu. Wazazi wote washirikiane kufanya kazi hii. Kama nilivyosema awali, miaka saba ya kwanza ya maisha ya mtoto ndiyo ya muhimu sana, kwa maana ndiyo inayojenga tabia ya mtoto. Hivyo ni muhimu sana wazazi kutilia maanani kazi hii ya kufundisha watoto nyumbani. Kama methali isemavyo: “Mtoto umleavyo ndiyo akuavyo.”. Mtoto atanufaika zaidi akifundishwa nyumbani kwa miaka minane ya awali, yale yote ya muhimu, kabla ya kwenda shule. Mambo haya ni kama kutii, adabu njema, upendo, usafi na mambo yahusuyo mwili, ikiwamo na kujisafisha baada ya kutumia choo, kuoga na kwenda chooni kwa wakati,, furaha, kazi, kujua herufi na namba.

Ulimwengu umejaa vikwazo vingi, na shetani amewalenga watoto na vijana. Wengi wamevutwa na mitindo na maisha ya ubinafsi na kupenda anasa. Kwa kuingilia tamaa za mwili, nguvu za kimwili na kiroho zinapungua. Wazazi wanahitaji hekima toka kwa Mungu, ili waweze kufanya kazi hii muhimu ya kwalea watoto kwa “njia iwapasayo,” ili wawe wa manufaa katika maisha haya na yajayo. Kwa maombi na sala, wawaweke watoto mikononi mwa Mungu kila siku. Yesu aliwaombea wanafunzi wake (hata sisi) kwamba “.....usiwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu.” Yohana 17:15-17.

Baba na mama wote lazima washirikiane. Utafiti mmoja ulionyesha kwamba tabia ya mtoto inachangiwa kwa asilimia 40% toka kwa mama, 20% toka kwa baba. Hii inajumlisha asilimia 60% toka kwa wazazi! Mtoto akipata asilimia sitini katika somo, tuseme la hesabu, atakuwa amefaulu huo mtihani. Hivyo mtoto huyu pia akipata asilimia sitini toka nyumbani ataweza kumudu maisha kitabia na atasimama imara. Asilimia 40% zilizobaki zinagawanywa

hivi:10% ya tabia yake ataipata shuleni/marafiki, asilimia 10% toka kanisani, 10% toka katika mazingira anayoishi na asilimia 10% ni mchango wa mtoto mwenyewe.

Mama una jukumu kubwa hapa. Asilimia zako arobaini ni nyingi kumpa mtoto msingi wa maisha. Mfunze mtoto katika njia za Bwana, katika hali ya upole. Sauti ya ukali na kukaripia wakati wote haifai. Mtoto atajifunza kuongea hivyo hivyo kwa ukali. Kutisha pia hakufai: yaani kusema 'nitakuchapa,' au 'ngojea nimwite mbwa aje akuume!' Baadaye atazoea vitisho na hatajali tena. Kama umeahidi kwamba utamchapa, basi mchape akikosea, isiwe ni vitisho tu. Wafundishe kwa upole na upendo. Ukifanya sehemu yako kwa uaminifu, Mungu naye atafanya sehemu yake. Mama White anasema, "Nyumbani kuwe ni mahali pa kupendeza sana kwa watoto na kuwepo kwa mama nyumbani kuwe na mvuto mkubwa kwa watoto."

Mtoto anapofikia umri wa kwenda shuleni, aende; maana atakuwa tayari sasa kukabili watu wengine wa nje ya jamii yao. Siku hizi watoto wanapelekwa shuleni wakiwa wadogo sana! Nimeona watoto wa miaka miwili wakipelekwa shuleni, eti darasa la watoto, (baby class). Jamani! Mtoto huyu anatakiwa awe huru, aruke huku na kule, achezee mchanga na kufinyanga vitu bila sheria zo zote. Shuleni kuna ratiba ya kufuata na pia aweza kupata mafundisho ambayo hayatamjenga kiroho. Miaka saba ya mwanzo ni muhimu tuwe na watoto wetu karibu. Yote niliyopaswa kuyajua nilijifunza kabla ya miaka sita. Ni kweli kwamba mama wengi siku hizi wanafanya kazi. Na mayaya aidha wamekuwa ghali, watundu sana, au hawapatikani. Wengine wanawatesa watoto wanapoachwa nao. Sasa mama anaona afadhali alipie mtoto shuleni na ampeleke akiwa umri mdogo, miaka miwili au mitatu!

Kwanza, shule hizi ni za biashara (business) na ni kusaidia kazi ya uyaya kwa mama asiyekaa nyumbani. Ugumu wa maisha umewafanya watu wabuni jinsi ya kupata hela, na wameanzisha hizi shule kwa minajili ya biashara. Wanazitangaza au kuzipigia debe wakitumia maneno matamu, eti ni kumzoeza mtoto tu, hakuna kusoma, n.k. Kuonyesha kana kwamba usipompeleka mtoto wako, utakuwa kana kwamba umeachwa na basi! Na unapompeleka mtoto kuanza chekechea au darasa la kwanza, unaulizwa kama mtoto alishapitia shule ya watoto, (baby class)? Ukisema ametokea nyumbani, shule nyingi zinamkataa. Sasa tutafanyaje? Uzoefu wetu wa watu mashuhuri kama Mwalimu Julius Nyerere, ni kwamba walienda shule baada ya miaka 10 na walimaliza chuo katika miaka ile tu wengine walimaliza!

Pili, licha ya kuwa na ugumu wa mayaya, umekuwa kama ni mtindo (fashion) kupeleka watoto wadogo shuleni. Kina mama tunapenda sana mitindo ya kisasa, hata kama ni ya kupeleka watoto shuleni mapema ili afahamu kuongea kiingereza na kusoma mapema, hasa katika shule za kifahari.

Tatu, tumetelekeza wajibu wetu kama wazazi. Wengi wetu, hasa wafanya kazi, hatuna muda wa kukaa na watoto. Hivyo tunaonelea afadhali kuwapeleka shuleni mapema watuondokee. Nilikuwa ninawaambia rafiki zangu fulani waliokuwa wanaangaika wakitafuta biashara ambayo itawaletea faida kubwa. Nikawaambia wajenge shule ya chekechea ya kulala (boarding). Ili mradi waajiri watu wa kutoa huduma maalumu kama mayaya wasomi na manesi wa kutibu na kulala na watoto usiku. Watu wengi watawaletea watoto wao, hata wa mwaka mmoja! Kumbuka miaka saba ya mwanzo ndiyo muhimu sana kwa mtoto kujifunza mambo yatakayokuwa muhimu katika maisha yote.

Nawasihi wapendwa, kwa kadri inavyowezekana, hebu na tuwafundishie watoto wetu nyumbani mwetu hadi angalau wafikie umri wa miaka sita hadi minane hivi ndipo waende chekechea. Kamwe usimpeleke mtoto wa umri wa miaka miwili au mitatu shuleni, maana atachoka baadaye, na kisha atakuwa na mafundisho ya watu wengine na si yako wewe kama mzazi! Mifumo yetu ya elimu ina mashindano (competition) makubwa. Watoto hawana hata nafasi ya kucheza! Waalimu wanang'ang'ania watoto wajue kusoma sentensi wakiwa chekechea (miaka minne), ili shule yao ipate sifa. Masomo kama ya maarifa ya nyumbani, elimu ya kazi ya mikono, na sanaa mbalimbali yamekuwa kama yamepitwa na wakati. Hebu tuache mtoto awe mtoto jamani. Mama White anasema, "Natamani Mungu angeongea na wazazi uso kwa uso kama alivyoongea na Manoa na mke wake, akiwaelezea jinsi ya kulea mtoto wao." Child Guidance uk. 30

Je, tutaifahamuje shule inayomfaa mtoto anapokuwa amefikia umri wa kwenda shule? Shule inayofaa ni shule ambayo inahimiza misingi ya Neno la Mungu, misingi inayowajenga watoto siyo kiakili tu, bali pia kimwili, na kiroho. Shule ambazo zitamwandaa mtoto kukabiliana na maisha haya na maisha yale yajayo. Shule ambazo zinafundishwa na waalimu wanaomcha na kumheshimu Mungu. HILI NDILO JAMBO MUHIMU. Neno la Mungu lasema, "utafaidi nini kupata ulimwengu wote na kuukosa uzima wa milele?" Ni hatari sana kumpeleka mtoto katika shule yo yote, hasa katika wakati huu wa mwisho. Shule ambazo hawatajengwa kiroho. Shule ambazo watafundishwa nadharia za uibukaji (evolution). Shule ambazo walimu na wafanyakazi hawamwamini Mungu. Aidha wanamdharau au kumkufuru Mungu mbele ya watoto wanaowaangalia kama mifano (model). Shule ambazo hazijali kama wanavuta sigara au kunywa pombe, ukiachilia mbali madawa ya kulevya yaliyosambaa siku hizi. Shule ambazo watoto wanaapa na kutumia lugha chafu. Shule ambazo wanasoma siku saba kwa juma, bila kuthamini siku takatifu ya kwenda kumwabudu Mungu. Mtoto asipoenda shuleni anaadhibiwa, hivyo inabidi mzazi ampeleke shuleni kwanza ndipo kisha aende kanisani. Mzazi anamwambia mtoto, "Soma tu, kwa sasa, utaenda kanisani ukimaliza shule, Mungu anaelewa." Hivi masomo yana mwisho kweli? Atamaliza shule lini? Kama nilivyokwisha kusema, hali ya kiroho ya mtoto inafikia kilele anapokuwa na umri wa miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu.

Mzee mmoja wa kanisa alikuwa akimpeleka binti yake shuleni kwanza, kisha anaenda kanisani. Siku moja binti akaja mapema, nafikiri kulikuwa na shida fulani shuleni, wanafunzi wakaruhusiwa kwenda nyumbani mapema. Badala ya mtoto huyo kumsubiri baba shuleni, aliamua kumfuata kanisani, maana kanisa lilikuwa karibu. Binti huyu akiwa amevalia sare zake za shule pamoja na begi lake la vitabu aliingia kanisani, akamtafuta baba yake, akamwona amekaa mbele kwenye viti vilivyotengewa wazee wa kanisa. Mtoto akamfuata baba yake hadi hapo mbele akakaa naye. Baba aliona aibu, akatafuta pa kutorokea asipaone.

Rafiki yangu mmoja, mke wa mchungaji, aliwaambia wazazi; "Tunalalamika kwamba vijana wa siku hizi, eti ooh; wako hivi na vile, wanapenda anasa na hawapendi kwenda kanisani. Sasa wangependaje kwenda kanisani wakati tulikuwa tunawapeleka shuleni siku ya ibada, badala ya kanisani?" Akaongezea; "Wanapokuwa wakubwa ndiyo tunakimbilia mchungaji, ooh, njoo umwombee kijana wangu hapendi kwenda kanisani, na hata maombi nyumbani hapendi, n.k." Akamalizia hivi: "Tafadhalini acheni kuwasumbua wachungaji eti waje kuwaombea watoto ambao nyie wenyewe mliwaharibu, kwa kuwaonyesha kwamba elimu ya dunia hii ndiyo bora kuliko Mungu."

Watoto hawa wanatuheshimu sana, maana wangetuuliza, “Hivi mama/baba, ulipokuwa ukinipeleka shuleni badala ya kunipeleka kanisani hapo zamani, ni kwa kuwa Mungu hakuwepo au hakuwa wa maana wakati huo?” Lakini cha kutia moyo ni kwamba, Mungu wetu hahukumu kama sisi tuhukumuvyo. Ana uwezo wa kutubadilisha, lakini hebu tusiwanyime watoto furaha na raha ya kumfahamu na kumtumikia Mungu wao wakiwa wadogo. Tukifanya hivyo Biblia inasema “Hawataacha hata watakapokuwa wakubwa.”

Wenzetu waislamu wametushinda katika hili, maana hawawasomeshi watoto wao kwenye shule za hivi hivi. Wana shule zao, ambako wanahakikisha mtoto amepitia ‘madrasa’ yote ndipo aende kusomea katika shule nyingine, pale inapolazimu sana. Hata akiwa huko, binti wa kiislamu lazima avae mavazi ya heshima, akifunika kichwa na miguu, kulingana na mila na itikadi za dini yao. Hali ya kuwa bikra hadi ndoa pia bado inathaminiwa sana na ndugu zetu waislamu.

Licha ya mzazi, mwalimu ni mtu muhimu sana katika maisha ya mtoto. Watoto wanawathamini sana waalimu, na hata wakati mwingine huwathamini kuliko wazazi. Wazazi wengine, hasa wa siku hizi, wameshindwa kuwadhibiti watoto wao, na wengi wamewaachia waalimu kazi hiyo. Mzazi mmoja aliniambia, “Mwalimu itabidi unisaidie, maana mtoto hawezi kufunga TV, afanye kazi ya nyumbani.” Nikashangaa sana, na kujiuliza kama nitakuwa ninaenda nyumbani kwake ili nifunge TV ili mtoto afanye kazi ya nyumbani!

Watoto wengi wanawaiga waalimu wanaowapenda. Wataiga lugha yao, wataiga hata miondoko, chakula na mavazi yao. Hata wengi wanaamua kutaka kuwa waalimu ili wawe kama waalimu wao. Kama mtoto anamhusudu mwalimu fulani, na huyo mwalimu anavuta sigara, akipuliza moshi juu, mtoto ambaye anafahamu kwamba sigara inaathiri afya ya mtu, atamuiga mwalimu. Kwa nini mwalimu wake anayefahamu mambo mengi hivyo, asifahamu kwamba sigara ina athiri afya zetu? Mwalimu ana uwezo mkubwa wa kuathiri tabia ya mtoto kwa upande wa chanya au upande hasi, milele. Mwalimu ni mzazi wa pili! Anaweza kumjenga au kumpotosha mtoto.

Mtu mmoja alikamatwa na polisi Nairobi, kwa sababu ya kuua watu, hasa wasichana. Alitangazwa kwenye runinga kwamba alikuwa ameua wasichana zaidi ya kumi na kuitupa miili yao! Alipohojiwa alisema alifundishwa (initiated) kwenye genge hili (sect) hili na mwalimu wake wa sekondari, alipokuwa katika kidato cha kwanza! Kama mwalimu ni mtu muhimu hivi katika maisha ya mtoto, je, umempelekea mwalimu wa aina gani mtoto wako?

Zamani wazazi wangeringia tabia za watoto wao. Nakumbuka nilipokuwa mdogo, mama alisisitiza sana utii na heshima kwa watu wote. Nilipokuwa mjeuri, aliniadhibu na kusema, “Unataka nipitie wapi humu kijijini?” Hii ilikuwa na maana kwamba, tabia yangu mbaya ingejulikana kote kijijini, na sifa hii mbaya ingemfanya aone aibu kuchanganyika na wanakijiji wenzake. Na kama watoto wangekuwa na tabia nzuri, basi sifa zao pia zingevuma kote kijijini, na wazazi wangesifiwa kwa malezi mazuri ya watoto wao. Lakini leo sifa ya wazazi inatokana na mali au utajiri walio nao. Je, wanaishi wapi? Mahali na nyumba yenyewe, gari/magari waliyo nayo; pia shule anayosomea mtoto wao. Lakini shule yenye maadili mazuri, siyo lazima iwe ya kifahari. Angalia sana shule anayosomea mtoto wako, na mwalimu wake.

SURA YA 7

KWA NINI MUNGU ALITUPATIA WATOTO

Mungu angeweza kutupatia watoto kwa kutumia njia tofauti na ya uzazi. Angeweza kuwafanya wakue kwa miezi michache au wiki chache na hata kwa siku chache tu. Wanyama na ndege wanakomaa kwa siku, juma, miezi au miaka michache tu. Lakini inawachukua watoto miaka mingi kukomaa, kimwili, kimawazo kiakili na pia kiroho. Mtoto anapewa wazazi kwa sababu mbili muhimu: Wamlee na kumtimizia mahitaji yake na pia wampe mwongozo.

Kumtimizia mahitaji yake ni pamoja na kumpa chakula kinachofaa na kwa wakati unaofaa. Siyo kumpatia kila kitu anacholilia. Siku hizi wazazi wanawaogopa watoto. Watoto wamekuwa kama 'visultan' vidogo. Wanaamrisha wazazi: "Nataka hiki, sipendi kile." Ataamrisha tangu chakula, mavazi, marafiki, miziki wanayoisikiliza, maeneo ya kutembelea na hata shule wanazozipenda! Cha kusikitisha ni kuwa, wazazi wengi hawawezi kutoa miongozo inayofaa kwa watoto, wakiogopa kupoteza uhusiano kati yao na watoto wao.

Mungu hakutupatia watoto ili tuwatimizie mahitaji yao tu, lakini pia kwamba tuwape mwongozo wa maisha. Tuwapende na kuwaadabisha. Kupenda bila kuadabisha ni hisia tu, Kuadhibu bila kupenda ni unyapara (tyranny). Je, tunawapenda watoto wetu? Kama

tunawapenda, basi tunaweza kuwaadabisha. Lakini ukijaribu kuwaadhibu pasipo upendo utaishia kuwa na watoto waasi (rebellious).

Tutafanyaje sasa? Uwe na msimamo (consistent). Usiwe kigeugeu. Sema unachomaanisha na maanisha unachokisema. Kama huna uhakika na kitu basi usikiseme. Kwa mfano, usiahidi zawadi ambayo unajua hautatoa, au kutishia kwamba utatoa adhabu na baadaye usahau.

Mfundishe mtoto kwamba kulilia vitu hakutabadilisha uamuzi wako. Kulia kwa hasira na kujigaragaza chini (tantrum) huwa ni makosa ya mtoto, akitaka kumjaribu mzazi, lakini baada ya hapo huwa ni makosa ya mzazi kumdekeza.

Usimrekebishe mtoto wako kila wakati. Mtume Paulo anasema katika kitabu cha Waefeso 6:4 kwamba, “Kina baba msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.” Tukiwakosoa sana watoto, watajidharau na kuwa na kujijengea hali ya kutojiamini. Hii itawafanya wachanganyikiwe. Mara nyingi wazazi hutegemea watoto wafanye mambo makuu, na hivyo tunawawekea sheria nyingi. Hebu wazazi tuweke sheria chache tu ambazo zitamsaidia mtoto kuzizingatia.

Fundisha watoto kwamba Mungu huadhibu pia (discipline). Wafundishe kuomba msamaha na hata wewe, kama mzazi ukiwakosea uwaombe msamaha. Kwa njia hii watajifunza kuomba msamaha kwa Mungu.

Watie moyo na uwasifu wanapofanya mazuri. Wajue kwamba unajivunia (proud) kuwa na watoto kama wao. Huwa wanajisikia vizuri sana wanaposifiwa na kutiwa moyo na wazazi. Hii itawafanya wajibidiishe kufanya mema zaidi. Kama mtoto anafeli mitihani shuleni, inabidi wewe kama mzazi uchukuwe jukumu la kujua ni kwa nini anafeli. Mzazi ukae na mtoto na kuangalia madaftari yake na kazi yake ya shuleni na ya nyumbani, (homework). Labda haelewi darasani, au labda haoni ubaoni, anahitaji miwani.

Binti yetu alikuwa na shida hii, alikuwa haoni ubaoni; na hatukufahamu hadi mwalimu alipotuambia. Hivyo ni muhimu kumtembelea mwalimu wa mtoto wako na kuzungumzia maendeleo ya mtoto wako darasani. Inawezekana hasikii vizuri, hivyo haelewi mwalimu anapofundisha. Haya yote ni baadhi ya majukumu yetu kama wazazi.

Ni lazima tuwatie moyo watoto wetu, tuwabariki na kuwatimizia mahitaji yao. Pia tuwaadabishe na kuwaadhibu wasipotii. Tuwape mwongozo wa maisha. Zaidi ya yote, tuwe mfano bora kwao. Wamwone Kristo katika maisha yetu. Mfano wa Kristo ndiyo elimu ya juu kupita zote, ambayo itampa mwelekeo mzuri maishani. Watoto wetu wanatufahamu sana. Wanafahamu kama tunampenda Yesu au la. Wanafahamu kama tu walafi au la. Wanatujua nje na ndani, na hivyo lazima tuwe waangalifu sana. Je, tunathamini vitu vya dunia hii kiasi gani? Kama unataka watoto wako wampende Yesu na kutamani ufalme wake, basi ishi maisha hayo. Udhihirishe upendo huo kwa Yesu na watu wengine. Watoto watakuiga. Je, unatoa zaka na sadaka?

Mwisho, wakinge watoto wako kutokana na anasa za dunia. Mara nyingi watoto wetu wanakulia kwenye nyumba na mazingira ya kikristo, ambako sheria ni “Usifanye hiki au

kile....." Baadaye tunawapeleka kwenye ulimwengu wenye giza bila kuwapa njia za kujifurahisha (recreation) ambazo ni salama. Baadaye tunabaki tumepigwa na butwaa, wanapotelekeza maadili waliyofunzwa nyumbani, na kuingilia anasa za ulimwengu huu. Hapa ndipo unaona faida ya kuwapeleka watoto katika shule na vyuo vya kanisa. Mahali ambako watapata maburudisho mazuri yanayomtukuza Mungu.

Je, tunafahamu mahali ambako watoto wetu wanatembelea na mambo wanayoyafanya wanapokuwa nje? Ni vizuri kufuatilia na kufahamu watoto wako wanatembelea wapi, na wanachokifanya wanapokuwa huko. Mwambie mtoto wako sababu za kufanya au kutofanya mambo fulani na pia faida na madhara yake. Ni vizuri kuwakinga wanao kutokana na uamuzi wanaochukua hasa wanapokuwa wadogo hadi watakapokuwa wamekomaa kuweza kufanya uamuzi unaostahili.

Kumbuka, kazi hii ni kubwa lakini lazima tuifanye. Lazima tushiriki na Mungu kikamilifu katika malezi ya watoto kwani Alitupatia ili tuwe mawakili tu, wa kuwalea na kuwafikisha mbinguni. Anawajali sana kuliko sisi wazazi tunavyowajali. Kama tunampenda Yesu na tunaishi kama watoto wake, watoto wetu pia watakuwa jinsi tunavyotaka, wataishi ndani ya Bwana wetu Yesu Kristo.

SURA YA 8
UGUMU WA KAZI YA UZAZI (THE DIFFICULT ART OF PARENTHOOD)

Vita kati ya vizazi siyo ngeni. Katika historia kumekuwa na vita hivi kati ya vijana (usasa) na wazee au kati ya mambo ya kisasa na yale yaliyopitwa na wakati, ambayo kwa wazee bado ni ya muhimu. Vijana kutowatii wazee kumekuwa kitu cha kujivunia kwao. Kama wazazi, ni muhimu tujue jinsi ya kupigana vita hivi. Kama mwanasosholojia Edgar Z. Friendenberg anavyosema: “Watoto hawapigani na wazazi wao, wanawaacha.” (abandon)

Wazazi wengi hawana taarifa ya kile ambacho watoto wao wanafikiria kwa sababu hawawapi nafasi ya kuwaambia mawazo yao. “Huoni nina kazi?” Ni jibu tunalowapa

watoto, hasa wale wadogo. Hii ni njia mwafaka ya kumfukuza mtoto. “Spend time not money;” anashauri Clark Kerr, ambaye ni mwalimu, akimaanisha “Tumia wakati siyo fedha”. Unapokuwa na mtoto wako na kuzungumza naye, utamfahamu mtoto na itakuwa rahisi kumsaidia. Njia nzuri ya kumsaidia mtoto ni kufanya mambo mazuri kwa pamoja kama familia. Kuwa mfano katika kucheza michezo pamoja na watoto, kutembea (hike) pamoja, kazi za kujitolea kanisani, kukambika na hata kazi za nyumbani.

Waalimu wengi wanakiri kwamba kazi ya ualimu imekuwa ngumu sana siku hizi. Nami nawaunga mkono kwa sababu nimekuwa mwalimu kwa muda mrefu. Kuna tofauti kubwa sana ya waalimu wa karne ya ishirini na moja na waalimu wa miaka ya nyuma kidogo. Mwalimu mmoja aliingia kwenye ofisi ya mwalimu mkuu akamwambia, “Nimechoka, ninaacha kazi.” Akasema kila anachofanya kujaribu kurekebisha wanafunzi wanaghairi na kudharau. Hawatii hata agizo dogo tu la kimsingi, na kwamba wazazi wa kisasa wanawaunga mkono kwamba wana haki zao za kufanya wanavyotaka.

Ukweli ni kwamba, watoto hawapendezwi na wazazi wanaowaachilia kufanya wanavyotaka; wanaona kwamba wazazi wao hawawajali. Wanapenda wazazi ambao wana ‘uti wa mgongo’ na uwezo wa kusimamia maadili ambayo wanajua yanawafaa watoto. Mara nyingi wazazi ambao hawana msimamo (permissive) wanaruhusu watoto wao wafanye wanavyotaka. Watoto wanajua hili, hivyo hawawezi kuheshimu wazazi wa aina hii. Usifikirie kwamba unamsaidia mtoto wako kwa kumruhusu afanye anavyotaka. Baba, hebu uwe baba, na mama hebu uwe mama, siyo rafiki. Watoto wana marafiki zao, wanachohitaji ni baba na mama wa kuwaongoza. Katika kitabu cha Methali 31, Biblia inazungumzia juu ya mke au mama mwema. Fungu la 28 linasema kwamba, “watoto humuita heri.” Mama atakayeitwa “Heri” na watoto siyo mama aliyewaachilia watoto wake kufanya wanavyotaka, kutembelea wanakotaka, kuvaa wanavyotaka, kula wanavyotaka, n.k. Huyu ni mama ambaye ametoa miongozo ya kufuata katika nyumba yake na kuisimamia vema, hata kufikia hatua ya kusifiwa na watoto kando ya mume wake, fungu la 29: “Mumewe naye humsifu na kusema, binti za watu wengi wamefanya mema; lakini wewe umewapita wote.”

Kulea watoto katika kicho cha kumcha Bwana kunahitaji mzazi anayeelewa; mwenye imani na uvumilivu wa hali ya juu. Yesu anatuvumilia sisi sote. Wazazi wazuri ni chumvi ya ulimwengu. Wanaheshimiwa na watoto wao. Wanasaidia sana kuboresha ulimwengu huu ulioharibika. Wanasaidia vijana kukua kama wanavyostahili.

Wazazi wazuri ni mawakili (mawakala) wa Mungu. Paul Rader anasema haya kuhusu baba yake; “Baba yangu alipokuwa karibu kukata roho, aliangalia mbinguni akatabasamu. Rafiki yake akamuuliza, “Rader, unawezaje kutabasamu hivyo wakati hakuna hata mtoto wako mmoja anayemtumikia Mungu?” Baba yangu akatabasamu zaidi, akamwambia kwamba hilo halikuwa jambo la muhimu wakati huo. “Niliwalea kama (Mungu) alivyoniagiza, atawarudisha yeye mwenyewe, kila mmoja wao.” Na kweli, kila mmoja wa watoto wake alimrudia Bwana.

Kila mzazi anayewaombea watoto wake, nakuhakikishia kwamba Mungu anasikia. Usikate tamaa. Watarudi. Methali 22:6 inasema, “Mlee mtoto kwa njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mkubwa.”

SURA YA 9

ELIMU YA NGONO KWA VIJANA

Elimu ya kijamii ni muhimu sana kwa mtoto. Mtoto anapozaliwa tu, kila mtu huwa anataka kujua ni wa jinsia gani: wa kike au kiume. Zamani watoto wa kiume walithaminiwa sana, (katika jumuiya fulani) kuliko watoto wa kike. Ilhali, watoto wa kike walithaminiwa sana kuliko watoto wa kiume katika makabila fulani, hasa kwa minajili ya malipo au mahari ambayo wazazi wangepata wakati mtoto huyu anapoolewa. Hivyo watu wengi huwa wanapenda kuwa na mchanganyiko wa wasichana na wavulana, hata kama uwezo huo ni wa Mwenyezi Mungu peke yake.

Watoto wa umri wa chini ya miaka mitano hadi miaka sita huwa wanashangaa walitoka wapi. Mtoto wangu wa miaka mitatu aliniuliza siku moja, “mtoto anaingiaje tumboni mwa mama, na anatokaje?”. Watoto Wanauliza maswali mengi yanayohusu jinsia ya watoto. Wanagundua kwamba wana tofauti. Mtoto wa kike wa miaka minne alimuuliza mama yake, “Mbona Jonny ana kitu kirefu cha kukojolea na mimi sina?” Pia wanapenda kuuliza walitoka wapi? Wakiona mnyama au kuku akimpanda mwingine anauliza, “ Hao wanafanya nini? Mbona anamuumiza mwenzake?” Huu ni wakati mzuri wa kuanza kufundisha elimu ya kijamii, ukijibu kwa kifupi tu maswali yanayoulizwa. Watoto wakiwa wadogo, mara nyingi wanafikiria kwamba tuliwatoa hospitalini, kwa kuwa wanaona picha zao wakiwa wadogo hospitalini, au wanasikia watu wakisema kwamba waliwaona walipozaliwa hospitalini. Kama mama aliyeelezea mtoto wake wa miaka mitano, (alipoomuuliza alitoka wapi), nadharia yote ya mfumo wa uzazi (reproduction), na mtoto akabaki akishangaa, kisha akamwambia, “nilikuuliza hivi, rafiki yangu Daudi anatoka Musoma, sisi tunatoka wapi?”

Mtoto anapofikia umri wa miaka saba anakuwa amefahamu tofauti za maumbile ya msichana na ya mvualana. Unaweza kuwaona wakishikashika sehemu zao za siri. Wakati mwingine wanaweza kuwashika wenzao matakoni au katika sehemu zao za siri, huku wakichekacheka.

Miaka tisa hadi kumi na mitatu ni miaka ya kujiandaa kwa ajili ya ujana. Ingawaje viungo vya uzazi huwa bado havijakomaa, wasichana wanaweza kuanza kupata hedhi yao. Pia huanza kujadili wanayoyajua kuhusu ngono pomoja na rafiki zao. Wengi wanakuwa wamesoma shuleni kuhusu mfumo wa uzazi, na wana hamu ya kujua zaidi. Wanapofikia umri wa miaka 11 hadi 14, wengi wanakuwa wana taarifa kamili kuhusu uzazi na ngono. Wanakuwa na hisia zinazowafanya washangae wasijue jinsi ya kuzitumia. Basi wanabaki wakitaniana tu kuhusu hisia zao.

Umri wa hatari sana ni wa kati ya miaka kumi na mitano na kumi na minane. Vijana katika umri huu wana mvuto mkubwa sana kwa vijana wa jinsia tofauti (opposite sex). Wazazi na waalimu wanahitajika sana kuwapa vijana hawa mwongozo na elimu ya kijamii (sex education) kuhusu hisia zao, ambazo zinachemka sana wakati huu, ilihali wangali wanganga, wanachanganyikiwa wasijue jinsi ya kujizuia. Wasichana wanavutiwa sana na wavulana, na pia wavulana wanavutiwa sana na wasichana, ingawaje bado hawapendi kuonekana hadaharani. Hivyo wakipata nafasi wakiwa peke yao wanaweza kuvuka mipaka kwa kufanya mambo yasiyofaa ili mradi kuweka kwenye vitendo na kukidhi haja ya hisia hizi. Inabidi kuwaambia vijana hawa kwamba hii ni hali ya kawaida ya kukua, na kwamba Mungu alitupatia uwezo wa kujizuia na kusubiri hadi hapo tutakapokuwa tayari kuchagua mmoja wa kuambatana naye katika ndoa.

Ni vizuri vijana waambiwe athari na hatari za kujihusisha na mambo ya ngono mapema. Athari kubwa muhimu ya kuwasisitiza ni kwamba hii ni dhambi mbele za Mungu. Jambo la dhambi tunamfanyia Mungu kwanza kabla ya watu. Yusufu alisema “Nitamfanyiaje ubaya huu Mungu” wakati mke wa Potifa alipotaka kulala naye. Wanaume wa siku hizi pia wanakabiliwa na wasichana ambao wako tayari kujitoa kwao na kulala nao. Hili halikuwepo zamani. Angalau wavulana ndiyo waliwaanza wasichana. Leo, mambo yamebadilika. Majaribu yako katika jinsia zote, na wakati wote. Tujifunze jinsi ya kutia nanga kwa Mungu, maana ndiye atakayetuokoa.

Pili, jambo hili laweza kukatisha masomo yake, kwa kupata mimba na mtoto ambaye bado hana uwezo wa kumlea. Mama asimpe binti yake dawa za kuzuia mimba. Mama wengine wanaona ni afadhali amkinge binti kupata mimba, kuliko amzalie hapo nyumbani.

Tatu, anaweza kuambukizwa magonjwa ya zinaa, yakiwemo ukimwi, ambao hadi sasa hivi hauna tiba. Kumfundisha binti kutumia mipira ya kondomu ili kuzuia mimba au magonjwa ni aibu kwako mzazi. Wazazi wengine, hasa mama wanawatafutia au kuwahimiza wasichana wao wawe na wachumba wakingali wadogo! Hii ni aibu kubwa. Kuna wakina mama wengine wamehusishwa kwenye kuwasaidia wasichana wao kutoa mimba, au kuingia kwenye uasherati. Iwe ni mwiko wewe kama mzazi kumwingiza mtoto katika dhambi hii.

Pia utashusha hadhi yako na utakuwa mtumwa wa kutumia mwili wako kwa kujifurahisha wewe mwenyewe kwa anasa na tamaa za kimwili. Enzi hizi za uhuru wa ngono (sexual freedom), eti ni kutimiza haja tu kama vile unavyokula ukisikia njaa, au kunywa maji unapokuwa na kiu. Katika enzi hii ya teknolojia ya kubonyeza (press button) tu na kupata unachotaka, iwe ni hela, chai au kahawa imetufanya tufikirie kwamba, hata ukisikia tamaa ya mwili, badala ya kuutawala mwili na kujizuia, basi ni lazima ujiridhishe hapo hapo. Ndiyo maana, ubakaji umekithiri siku hizi.

Kijana anapokuwa amefikia umri mzuri wa kutafuta mwenzi wa maisha, (mara nyingi vijana wanapata wachumba wanapokuwa vyuoni), ni vizuri pia wachumbiane katika hali ya kumcha Mungu na kujizuia hadi watakapooana. Mama White anasema kijana aombe maradufu anapofikia umri huu wa kutafuta mchumba na Mungu, kwa wakati ufaao, atakupatia.

Katika kipindi kimoja cha vijana, kijana mmoja alichangia akasema kwamba hakuna haja ya kungoja hadi waoane kama wameshahakisha kwamba wataoana, na hasa kama wameshatambulishana kwa wazazi wa pande zote mbili. Kwa kumjibu mchungaji alifungua

Biblia na kusema, “Nitawasomea fungu fulani na ninawaomba mniambie linatoka katika kitabu na sura gani katika Biblia.” “Msizini.” Alianza kusoma Biblia, “isipokuwa kama una mchumba wako ambaye mna hakika kwamba mtaoana, na mmeshatambulishana kwa wazazi wa pande zote mbili....” Vijana wachache walishabikia wakaanza kutafuta kitabu na sura inayosema hivyo kwenye Biblia, lakini wengi waligundua wakasema kwamba hakuna fungu kama hilo kwenye Bilblia. Wote walifurahia ubunifu wa Mchungaji huyu na wakakubaliana kwamba watafuata mwongozo wa Mungu ulioko katika Biblia. Na kwa neema yake watasubiri hadi waunganishwe katika ndoa takatifu.

Hebu neno la Mungu lizingatiwe, kwamba ngono nje ya ndoa ni dhambi, hata kwa vijana ambao hawajaoana, hata kama wanapendana kiasi gani. Shetani amedhalilisha ndoa, na hasa kushirikiana kimwili, limekuwa kana kwamba ni jambo la kawaida tu. Kama kukata kiu kwa kunywa glasi ya maji au soda. Au kula chakula unaposikia njaa. Unaangalia tu mgahawa ulio karibu unaingia na kuagiza chakula, unakula. Ukishiba unaenda zako. Kesho yake ukisikia njaa tena, utakula po pote tu, mradi ushibe, siyo lazima uende kwenye ule mgahawa uliokula jana yake. Hii ndiyo hali tunayoiona kwenye runinga na mtandaoni, kwamba uhusiano wa kimwili siyo lazima uwe wa kudumu, ni wa kujifurahisha kwa muda tu. Na mtu anajisikia zaidi anapokuwa na wenzi wengi.

Kulikuwa na kipindi ambacho kilikuwa kinaonyesha baba mmoja anatembea na mke wa kijana wake (mkamwana), na wote kijana na baba wakazaa na huyo binti, na wote wanajuana!!! Ubaya zaidi, wanaonyesha kwamba ni sawa kabisa, hakuna shida wala madhara yo yote. Ukipenda sawa. Pia kuna haya mazoea ya watu wengi, (nafikiria pia kutokana na runinga), kwamba wapendanao, lazima walale pamoja na kufanya ngono. Mtoto mmoja wa chekechea alikuja kushtaki akilia kwamba mwenzake amesema kwamba yeye ni rafiki (girlfriend) wa mvulana fulani mdogo kama yeye. Nikamuuliza, “Kwani kuna ubaya gani, ukiwa rafiki wa mvulana huyo?” Akasema, “Mimi silali naye!” Jamani!! Nani aliwambia hawa watoto wadogo kwamba ukiwa rafiki wa mvulana au msichana fulani ni lazima ulale naye? Haya ni mawazo ya mwovu shetani.

Wakati fulani tulikuwa kwenye makambi mahali fulani, nikahudhuria kipindi cha vijana. Mhubiri wao akawa anawafundisha somo la kuwa safi (pure) katika ujana wao. Akawauliza, “Je, inawezekana vijana wa kileo wajitunze (wawe pure) hadi waoe/waolewe?” Akaongezea swali la kutia changamoto sana, “Je. Yesu angezaliwa katika kipindi hiki, na malaika Gabrieli aje akitafuta msichana safi, bikra wa kumzaa Yesu, je, angepatikana?” Wavulana wengi, kama siyo wote waliokuwepo walijibu kwa kuzomea, “HAPANAAA!” Wasichana wachache sana walijibu kwa aibu, “Ndiyo, tupoo.” Mhubiri akawashangaa wavulana akawauliza wanajuaje kwamba wasichana wengi leo siyo bikra, na ni nani wahusika wakuu wa baya huo? Wakabaki kuchekacheka tu. Niliwasifu wasichana wachache walioitikia kwamba bikra wapo hata leo. Hebu tuwaambie wasichana wetu kwamba inawezekana kuwa bikra hadi siku ya kuolewa.

Mama mmoja aliwafundisha wasichana wake kwa kuweka nadhiri kwamba kwa neema ya Mungu watabakia kuwa bikra hadi watakapoolewa. Aliwapa ufunguo mdogo uliokuwa kwenye mkufu. Akawaambia kwamba wauvae siku zote, ili uwakumbushe kwamba wamefungwa hadi siku ya ndoa takatifu. Siku hiyo usiku, ndiyo ampatie mume wake huo ufunguo na kumwambia kwamba, “Nilijitunza kwa ajili yako, chukua huu ufunguo kama ishara ya kwamba

wewe ndiye unanifungua kwa mara ya kwanza leo!" Nilifurahia sana mfano huu. Inapotokea kwamba kijana ameteleza kidogo, basi tumfundishe kwamba Mungu anasamehe, na unaweza kuwa bikra mara ya pili. Yaani, kama uliteleza au kubakwa, usijidharau na kukata tamaa, na kuanza kuishi maisha ya kurandaranda ovyo ovyo. Jitunze.

Wazazi wenzangu, hebu tukemee dhambi hii ya uasherati. Hii ni dhambi hata tukiipamba kwa lugha gani. Biblia inasema wanzinzi wote hawataurithi ufalme wa Mungu. Tuwatie vijana wetu moyo kwamba inawezekana kuishi maisha matakatifu kama Yusufu. Haikuwa rahisi kwake kumkimbia mke wa Potifa, na kusema, "Nitawezaje kufanya uovu huu na kufanya dhambi mbele za Mungu?" Mwanzo 39: 9. Huwa ninawauliza vijana wanaobisha kwamba siku hizi hawawezi kujizuia hadi waoe, kwani enzi za zamani kulikuwa hakuna simu na mitandao, ilikuwa lazima watu waandikiane barua, ambayo ingemfikia mpenzi baada ya wiki kadhaa. Siku hizi ni ujumbe mfupi wa maneno tu na tayari mmeshaonana baada ya dakika chache tu. Huwa nawapa mfano wa Yusufu, kwamba naye alikuwa na hisia (emotions) kama wao, na alikuwa kijana kama wao.

Mambo mengine ya kuwafundisha watoto wanapoendelea kukua ni kuhusu kujisisimua kwa kushika sehemu za siri au punyeto (masturbation) na picha za umalaya (ponografia). Haya yote yanathiri afya ya mtoto au mtu mzima, kwani siyo mpango wa asili wa binadamu, na huleta hali ya dhamira kushitakiwa na kuharibikiwa na fikiri kwa namna fulani. Kulingana na mpango wa Mungu, hii ni dhambi pia, na kiafya ni madhara makubwa.

Siyo kwamba hisia za watu wa zamani zilikuwa zimepungua au zilikuwa kidogo kuliko zile za watu wa kisasa. Zote zilikuwa sawa. Tofauti ni katika hali ya kujizuia (self control). Kujizuia kunahitajika katika nyanja nyingi za maisha, kama mavazi, vyakula, hasira n.k. Danieli aliamua katika moyo wake kwamba "hatajinajisi na vyakula vya mfalme," Danieli 1:8. Kwa hiyo siri iko katika uamuzi. Bahati mbaya sana wengi wetu tunaishi kama bendera fuata upepo; hatuna maazimio yo yote katika maisha. Mungu alituumba ili tumtukuze Mungu kwa miili yetu, na kila tulitendalo, kwa nguvu za Mungu inawezekana wapendwa.

SURA YA 10

MAOMBI AU IBADA YA NYUMBANI (FAMILY WORSHIP)

Kuna shule muhimu tatu za kumfundisha mtoto. Shule ya kwanza ambayo ni ya muhimu sana ni ya nyumbani. Licha ya kumfundisha mtoto tabia ya utii, upole, upendo, heshima, uwajibikaji, n.k, jambo jingine la muhimu sana ni kumfundisha kumpenda na kumcha Mungu. Wakati mzuri wa kutoa mafunzo haya ni wakati wa ibada ya nyumbani. Ibada ya nyumbani ni muhimu sana. Jambo la kuhuzunisha ni kwamba nyumba nyingi, hata za wakristo, hazifanyi ibada au hata sala nyumbani. Siku moja niliwauliza wanafunzi

wangu kama walikuwa wanafanya maombi ya kifamilia asubuhi au jioni. Wawili tu kati ya watoto ishirini ndiyo waliosema kwamba walikuwa wakifanya sala jioni! Watoto, hata wa wazee wa kanisa na mashemasi walisema hawafanyi sala ya pamoja, isipokuwa tu wakati wa chakula!!!

Wengi wetu tunaomba maombi ya kibarua tu wakati wa chakula. Hata wakati mwingi hatufikirii tunachokisema isipokuwa maneno machache tuliyoyakariri tangu utotoni: 'Mungu tunajua kupika lakini hatuwezi kubariki, sasa tunaomba utubarikie chakula hiki kwa jina la Yesu, amina." Hilo ndilo ombi tunaloombea chakula cha asubuhi, mchana na jioni, Jumapili hadi Jumamosi, Januari hadi Desemba. Watoto wanaiga ombi hilo hadi watakapokuwa wakubwa wataomba na watoto wao hivyo hivyo, isipokuwa kutokee mwamko wa kiroho maishani mwao.

Kwa nini wakristo wengi hawafanyi ibada na sala nyumbani? Sababu nyingi zinazotolewa ni kama zifuatazo: Kwanza, ni ukosefu wa muda wa kufanya maombi. Kila mtu ana shughuli nyingi (busy). Hakuna muda wa kukaa chini, kusoma Biblia na kufanya maombi kama familia.
Pili, Ratiba za watu ni tofauti. Haiwezekani kuwakusanya familia yote kwa wakati mmoja ili kufanya maombi. Wengine wanafika nyumbani usiku sana, na ni vigumu kungojeana wote ili kufanya ibada ya familia. Tatu, Wengi hawaoni haja. Hawana hayo maono ya mibaraka na faida ya kuwa na maombi ya kifamilia. Mtu mmoja aliniambia, "Inatosha kwenda kanisani mara moja kwa wiki na kusali huko." Nne, wengine hawafahamu waanzie wapi na waishie wapi. Hawajui jinsi ya kuongoza ibada hii.

Sababu hizi zinaweza kuwa za kimsingi, lakini jamani, hivi tunamwelewa Mungu ni nani katika maisha yetu? Kwamba yeye ndiye anatuwezesha kufanya hizo shughuli zetu? Anatupatia afya, nguvu na uwezo wa kwenda huku na kule. Anasema katika kitabu ya Yohana 15:5 kwamba ".....pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." Ukimtegemea mtu, tuseme kwa chakula, karo, kodi ya nyumba na mahitaji mengine, bila shaka utamthamini sana mtu huyo. Utamtii na kufanya kila analokuomba.

"Sina wakati!" Huna wakati wa kufanya kile anachokihitaji Mungu? Hiyo ni hali ya kipau mbele. Kumbuka: JAMBO MUHIMU NI KULIFANYA JAMBO MUHIMU LIWE MUHIMU. Kumtanguliza Mungu kwa kila jambo ndilo jambo muhimu sana katika maisha yetu. Ndiyo maana hatuna nguvu (powerless). Nilisoma hadithi moja ya mtu ambaye alikuwa anafagia (vacuum) jumba kubwa la mkutano (hall), akitumia mashine kubwa ambayo inatumia umeme. Bahati mbaya, mtu huyu alikuwa kiziwi, na hivyo asingesikia mashini ikiunguruma. Akasukuma hiyo mashine bila kujua kwamba umeme ulikuwa umekatika! Maskini alichoka bure! Ndivyo na sisi tulivyo. Tunasukuma hili gurudumu la maisha peke yetu bila nguvu ya mbingu, na tunachoka bure.

Sababu ya ugumu wa kukusanya watu pamoja kufanya maombi ni tatizo la ratiba (scheduling). Pangia muda wa maombi na jaribu sana kuutunza. Mungu atakusaidia. Penye nia pana njia. Unapopanga muda wa maombi, ni muhimu kutia maanani mambo yafuatayo:
Umri wa watoto, (kama wapo); umri wa watu wengine unaoishi nao, kazi zao na muda wanaofika nyumbani.

Kukosa maono (vision) ndiko kunasababisha tusione umuhimu wa kuwa na kipindi muhimu cha ushirika na Mungu wetu. Je, ukiwa na mpenzi wako, utachoka kuzungumza naye? Je, utangojea mwonane mara moja tu kwa wiki, hasa akiwa anaishi karibu na wewe? Utatamani kuwa naye kila mara, na kama yuko mbali, utampigia simu mara kwa mara.
Kama shida yako ni kutojua jinsi ya kuongoza ibada ya maombi nyumbani (technique), basi soma vitabu, na umuulize mchungaji wako atakusaidia. Hapa kuna mawaidha machache:

Kwanza, kama una watoto wadogo, chagua muda ambao watakuwa hawajazidiwa na usingizi. Watoto wetu walipokuwa wadogo tulikuwa tunafanya maombi kabla ya chakula cha jioni. Watu wengi, hata watu wazima, wanashikwa na usingizi mara tu wanaposhiba. Kwa kweli hakuna sheria yo yote, ni vizuri kila familia ipange mpango wao kulingana na wanavyoona na wanavyopendelea. Pia jaribu kufupisha ibada kama watoto ni wadogo, lakini usiharakishe ili uangalie TV au ufanye jambo jingine. Ukifanya hivyo utawafundisha watoto kwamba maombi siyo ya muhimu sana.

Pili, uwe na utaratibu unaobadilika badilika. Hii inahitaji ubunifu (creativity) mkubwa na mipango. Watu wengi wanasema ibada yao ya nyumbani haivutiii, kwa sababu utaratibu ni ule ule, kila siku. Badilisha utaratibu, hasa ukiwa na watoto wadogo. Chezeni michezo ya Biblia. Choreni na kupaka rangi. Shindaneni kwa kukariri mafungu. Jifunze nyimbo mpya, na igizeni baadhi ya hadithi za Biblia n.k. Hii ni baadhi ya mifano michache tu. Kuna vitabu vingi vya watoto, vinunue vitakusaidia.

Tatu, wahusishe watoto (child centred). Hebu watoto wataje mafungu ya kukariri, waimbe nyimbo za pekee, watoe ushuhuda na pia waombe. Usifundishe lesoni ya watu wazima mkiwa na watoto. Tafuta muda wako usome lesoni yako. Watoto wana lesoni zao na ni nzuri sana. Zinafundisha hatua kwa hatua na zina shughuli za watoto za kila siku. Jitahidi angalao uwanunulie lesoni zao kulingana na umri wao.

Gawanya siku kulingana na mahitaji. Uwe na siku ya kuombea mahitaji ya familia, siku ya kuombea ndugu na jamaa, siku ya kuombea kazi ya Mungu, siku ya kuombea wachungaji na wamishonari n.k. Ombea uhuisho na uvuvio (Revival and reformation) nyumbani mwenu. Tukivuviwa nyumbani tutakuwa na kanisa lililo na mwamko pia. Unaweza kufuata utaratibu ufuatao, ingawaje unaweza kuongezea au kuubadilisha. Fanya mambo yawe na ladha na kutofautisha tofautisha mambo ili yasije kuwa mapokeo, mpaka waseme wameboeka! Lazima tuwe na ubunifu kwenye ibada zetu kwa namna fulani.

1. Sala: Wakati wa kuongea na Mungu
2. Biblia: Katika maombi tunaongea na Mungu lakini Mungu huongea nasi kupitia katika Biblia. Soma Biblia kulingana na umri wa watoto. Usisome tu ili mradi. Uifanye iwe na mvuto na maana kwa watoto hata wakiwa wadogo. Kama nilivyosema, hii inahitaji ubunifu na maandalizi makubwa.
3. Nyimbo: Watoto wetu leo wanapenda nyimbo zenye midundo. Ni muhimu kuwafundisha nyimbo (hymns) za sifa nyumbani na ambazo hazina mionjo ya dunia.

4. Vitabu: Tumia vitabu vya ibada (devotional books) vya aina mbalimbali, hata vya watoto. Hivi vinarahisisha kazi, kwa kuwa vimeandikwa kwa lugha inayoeleweka kwa watoto na vina hadithi nzuri za watoto.

Kadri unavyoweza, jaribu sana kuwa na ibada nyumbani angalau mara moja kwa siku. Ila mara mbili ndiyo bora zaidi: Asubuhi na jioni ni wakati ufaao sana. Nilipokuwa mdogo, baba yangu alikuwa anatuamsha asubuhi saa kumi na mbili kwa ajili ya sala. Angeanza kuimba wimbo wa "Bwana asubuhi kucha, nitakuinua....." Alitaka kabla ya kumaliza fungu la kwanza, tuwe tumeshafika. Tulikuwa tunakasirika, na tungejifunika na blanketi na kujifanya kana kwamba tumelala. Hutaamini kwamba nilipoolewa nilianzisha huo mtindo, na ninaamini hata watoto wangu wataiga mtindo huu.

Faida kubwa ya maombi ya pamoja kama familia ni kuwa na muda mzuri wa kuongea, kumsifu Mungu, na kumwambia kwa pamoja hoja za kifamilia na kumshukuru kwa maombi yaliyojibiwa. Watoto wanajifunza kuwa Mungu hujibu maombi. Rafiki yangu alikuwa ameomba na watoto wake kuhusu hitaji fulani la pesa. Walipomaliza tu, simu ililia, wakakuta ni ujumbe ambao ulikuwa unasema kwamba wametumiwa hela na mtu wasiyemfahamu, kiasi ambacho walikuwa wanahitaji! Rafiki yangu alishangaa sana, ndipo mtoto wake mdogo akamuuliza, "Baba, kwa nini umeshangaa hivyo, ilhali tumemaliza kuomba sasa hivi, si Mungu amejibu maombi yetu?"

Ibada ni kama majibu kulingana na jinsi Mungu alivyojidhihirisha kwako. Mungu alijifunua (revealed) kwetu, na ni wajibu wetu kuitikia.

SURA YA 11

TARATIBU NYINGINE ZA NYUMBANI (FAMILY RITUALS)

Ibada na sala nyumbani, ni utaratibu ambao kama wazazi tutauanzisha katika familia zetu utatupatia uhakika kwa watoto wetu kuwa "hawatauacha hata watakapokuwa wazee." Watauendeleza hata watakapokuwa wameondoka nyumbani na kuanzisha nyumba zao.

Taratibu zingine ni kuwa na siku au usiku wa familia (family night). Chagua siku moja ambayo mtafanya vitu mnavyovipenda kama familia. Labda mtapika chakula mnachokipenda wote,au mkaange bisi au karanga, mtaimba au kujifunza wimbo mpya kama familia, mtatoa ushuhuda wa kitu kilichokufurahisha au kukuhuzunisha sana katika wiki hiyo. Pia mtaulizana maswali ya Biblia (Bible trivia), na mtakariri mafungu. Nilipokuwa mdogo, baba alikuwa anafagia uwanja wa nyumba yetu hadi barabarani. Kisha anachukua nguo zetu za kuvaa kanisani anatunyooshea. Saa kumi na mbili tulikuwa tunapanga viti nje tunakaa wote na kuanza kuimba nyimbo za pekee za Sabato, za kwaya, na kusoma

neno. Hata wanakijiji walijua hilo, tusipoimba wangekuja kutuuliza, mbona hawakusikia tukiimba Ijumaa usiku.

Unaweza pia kuwa na utaratibu wa kupeleka watoto nje kuona maumbile ya Mungu, labda mara moja kwa juma. Watoto wetu walipokuwa wadogo, tulikuwa tunawapeleka kwenye mbuga za wanyama mara moja kwa mwaka. Tungeenda siku moja au tungepanga kwenda kupiga hema kwa siku mbili tatu tatu hivi, (weekend). Siyo lazima mkae hotelini. Tulikuwa tunaenda na mahema (camping) na tunajipikia au kuchoma viazi na mahindi kwenye moto wa kuni usiku. Tulifanya hivi kila ilipowezekana maana baadaye vijana wetu walienda kusomea shule za mbali. Hebu jaribuni hili. Watoto wanaoishi mjini, ambao hawajawahi kupika na kuni watafurahia jambo hili.

Pastor Joel Okindo, ambaye ni mkurugenzi wa idara ya uwakili katika Union ya Kenya alitufundisha juu ya utaratibu wa ajabu wa jinsi ya kufundisha watoto kutoa zaka. Alisema, kila nyumba iwe na kisanduku kidogo cha zaka na sadaka. Unaweza kukitengeneza au kukinunua. Kiwe na shimo juu, na kufuli. Kila siku wakati wa maombi ya jioni, kila mtu anatoa ushuhuda wa jinsi alivyobarikiwa. Kama alipata pato lo lote, anatoa zaka (asilimia kumi), anaweka kwenye kisanduku. Pia anaweza kutoa sehemu kwa ajili ya sadaka. Mara nyingi tunafikiria pato ni mshahara tu, na hata huo wengi wetu hatutoi zaka na sadaka kamilifu. Je, ukikutana na rafiki wa zamani akupe hela ya kunywa soda au kula chakula, hilo siyo pato?

Binti yetu alipokuwa mdogo alitushangaza sana, tulipokuwa tumeanzisha kisanduku hiki. Siku moja alipewa zawadi ya shilingi hamsini,na mwalimu wake, aliposhinda mtihani wake wa darasa la nne. Alikuja jioni akatoa ushuhuda, akiwa tayari ametafuta chenji, akaweka kwenye kisanduku shilingi tano za zaka, na nyingine tano za sadaka. Tulishukuru Mungu sana kwamba watoto wamejifunza funzo hili la kumtolea Mungu zaka na sadaka. Huu ni utaratibu ambao unaowafaa watoto tu, bali utatufanya hata sisi wazazi kuwa waaminifu katika matoleo yetu ya zaka na sadaka. Siku ya kusali ikifika, mnafungua tu kisanduku mnahesabu na kuweka kwenye bahasha, (kanisani kwetu tunatumia bahasha) mnaandika jina la familia. Ye yote hata mtoto anaweza kupeleka kanisani.

Je, umeshawahi kusikia usemi usemao kwamba “Nyumba inayosali pamoja hukaa pamoja?” (the family that prays together stays together). Huu ni ukweli kabisa, lakini pia imethibitishwa kwamba familia inayocheza pamoja hukaa pamoja, (the family that plays together, stays together). Nimeshataja kuhusu kucheza pamoja michezo ya Biblia. Hata michezo mingine pia ni muhimu, kama kukimbia, kutembea, kucheza mpira, kujificha na kutafutana (hide and seek), hasa kwa walio na watoto wadogo, wanaupenda sana mchezo huu.

Licha ya kufundisha watoto neno na Mungu na kuomba, ni muhimu kuwafundisha yafuatayo:

1. Utii: Kama nilivyokwishasema, utii liwe neno la kwanza ambalo lazima mtoto afundishwe na wazazi. Kutii bila kubisha au hata wakati mwingine, bila kuelewa. Raia wema hutii sheria za nchi kwa sababu ni sheria. Ibrahimu alimtii Mungu bila maswali hata ingawaje hakuelewa kwa nini Mungu alimtaka amtoe kafara mtoto

wake wa pekee Isaka. Wazazi lazima tuwe na tabia nzuri na pia tuwe mfano bora ili kuhimiza utiifu kwa watoto.

2. Watoto pia wafundishwe kufanya kazi. Kila mtoto awe na kazi ya kufanya nyumbani. Mama usione kana kwamba mtoto anakuchelewesha, anapoosha vyombo au kudeki polepole au vibaya. Vumilia. Hata kama itabidi urudie, utakuwa umemfundisha mtoto somo la maana sana. Biblia inasema kwamba "mtu asipofanya kazi asile." 2Wathesalonike 3:10.

3. Watoto wafundishwe kuwa wachangamfu bila kulalamika lalamika ovyo wakati wote. Wakina mama tuwe wachangamfu nyumbani. Mara nyingi tunakuwa wachangamfu kazini na kanisani lakini nyumbani tunanuna! Biblia inasema katika kitabu cha Ezekieli 16:44 kwamba "Kama mama ya mtu alivyo, ndivyo alivyo binti yake." Sikufahamu kwamba msemo wa "like father like son" ulitolewa kwenye Biblia, ila wakabadilisha badala ya mama wakaweka baba na badala ya binti wakasema mwana. Mama ndiyo mboni ya nyumba. "Kila mwanamke aliye na hekima hujenga nyumba yake, bali aliye mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe." Methali 14:1.
   Mama wapatie utaratibu wa kufuata nyumbani na jinsi ya kupanga vitu vyao vya kuchezea na vyumba vyao.

4. Watoto wafundishwe kuheshimu watu na vitu vya wenzao. Wafundishwe kusema samahami, asante, naomba/tafadhali n.k. Wafundishwe kuheshimu wakubwa na watu wa jinsia tofauti (opposite sex). Wafundishwe kuwapa wengine nafasi ya kwanza, kama Ibrahimu alivyofanya kwa Lutu. Hii inaondoa ubinafsi ambao umekithiri sana siku hizi.

5. Pia watoto wafundishwe jinsi ya kuishi kwa amani na wengine. Somo la kuomba msamaha hufundishwa nyumbani. Kupigana, kugombana au kutukanana kusiruhusiwe hata kidogo. Mwanafunzi wangu aliniambia kwamba mama yake huwa anamwambia kwamba "tit for tat is a fare game," eti lazima nijitee, nisije nikanyanyaswa na wengine. Mama unawezaje kumwambia mtoto hivyo? Hebu tuwafundishe watoto kuwa wapole na wavumilivu; na kwamba Mungu ndiye atatulipia kisasi. Wafundishe kugawana vitu vyao na watoto wengine. Wafundishe kuwaonea wengine huruma, kutetea haki na kuwa wakweli. Wafundishe kusamehe na kuomba msamaha.

Wazazi tuwe macho hapa kwa kuwa haya yote hufundishwa vizuri kwa mifano. Waone tukiwasamehe kwa kuwa watoto wadogo hufanya makosa mengi sana. Mikono yao michanga yaweza kudondosha vyombo na kuvivunja. Mikono hii pia yaweza kuiba. Ndimi zao ni changa zaweza kusema uongo mwingi sana na kusingizia.

Siku moja nilisikia kisa cha kusikitisha sana, kwenye redio. Mama aliyemlisha mtoto wa dada yake mavi kwa sababu aidha kweli aliiba au alipoteza chenji ya hela ndogo tu! Mwingine alimwiingiza msichana mdogo wa miaka sita kijiti kwenye sehemu zake za siri! Jamani! Huu si unyama tena ila ni ushetani! Hata kama mtoto amefanya kosa kubwa kiasi gani, hasitahili adhabu za kishetani kama hizi. Hebu fikiria tunavyomkosea Mungu kila sekunde; je, angetuadhibu hivyo tungekuwa hai kweli?

Wazazi tujue kwamba tabia hujengwa nyumbani kila siku, pole pole na kwa uvumilivu mkubwa.

SURA YA 12

MAWASILIANO NA WATOTO

Je, watoto wetu wanazoea mawasiliano gani wakuapo? Kuna jamii zingine ambazo mtoto hutakiwa kutomtazama mtu mzima machoni anapozungumza naye kama ishara ya heshima. Watoto waonekane tu nyuso zao ila sauti zao zisisikike (children must be seen and not heard). Wengine wanamkodolea macho mtu mzima kuonyesha umakini katika kile anachoambiwa! Je mawasiliano yako na ya mtoto wako ni yapi? Usizungumze bila kufikiri, au kutenda bila kufikiri mbele ya mtoto (carelessness)

Yale unayowafanyia watoto yanafikisha ujumbe. Je unakazana kuwanunulia watoto nguo tu na si vitabu? Hali hiyo itafanya watoto wako wathamini nguo zaidi ya vitabu. Je unatumia sauti kali kufoka, na kugomba nyumbani? Je unajionyesha kwa kufuja pesa na kununua vitu ambavyo havina maana? Tabia hii itajitokeza kwa watoto wako pia. Je una marafiki wabaya na unaishi maisha ya uzinzi au uasherati? Watoto wako watakuiga. Nilishangaa mtoto wangu mdogo kila mara akizungumza sauti ya juu nikagundua

ananiakisi mimi. Na kweli watu wengi waliniambia sauti yangu iko juu! Mtoto anahitaji maisha ya utulivu na si ya kelele ili ubongo ukue vizuri!

Watoto ni urithi toka kwa Bwana nasi tukumbuke kwamba ni mawakili tu kwa watoto hawa na wa jumuiya ambao ni yatima au wahitaji tunaowalea. Nyumbani ndiyo shule ya kwanza ya mtoto. Twaweza kuwa tunataka kuwasaidia ila mawasilianno yetu yakawa mabaya mpaka tukaharibu maisha yao na kuwa si mbaraka tena.

Mama alikuwa akiishi na binti yake aliyeachwa na mume ambaye alimtesa mno, hata huyu mama yake mzazi alipatwa uchungu na kumchukua na wajukuu wake awasaidie. Ikitokea mikwaruzo midogo midogo anamwambia binti yake “ndiyo maana uliachika!” Au huwafokea wajukuu akisema; “Ndiyo maana mpo hapa kwangu.” Napenda kushauri maneno haya kamwe yasitoke kinywani mwako. Hata kama ni mtoto, hahitaji viboko kwa njia ya maneno ya kumhuzunisha. Nani anataka maneno ya namna hii? Wewe? La! Mimi la hasha! Kwa nini tunayasema basi? Na kusema ulimi uliteleza na hata mara nyingine kusema watu hawasamehi, kumbe watu wametusamehe ila hawataki kusikia midomo yetu michungu. Tunayazoea wala hatuyaachi, tunabebana nayo tu. Tunatembea kama mabomu yaliyo tayari kuwaumiza watu na midomo yetu.

Tubadilike na kutoa maneno ya kutia moyo au kuhamasisha tabia na nidhamu ya mtoto kwa wakati unaofaa. Kuna wakati ambao ungepasa kumtia moyo au kumsifu mtoto na ukinyamaza unadumaza au kufifisha kitu ambacho kingemsaidia.

Mawasiliano kati ya wazazi na watoto ni ya muhimu sana. Mara nyingi wazazi wengine tuna haraka ya kutoa maneno makali kwa watoto wetu. Nilipokuwa nikitembelea nchi ya Tanzania hapa na pale, nilisikia mama mmoja akisema maneno kama haya “Nimekuita na unajibu kwa sauti ndogo kama jini, una mapepo wewe?”
“Una meno kama kenge wee!” “Ng’we!” Akang’aka wakati binti ameitikia bee!. “Mbwa wewe, kama baba yako!”

Baba mwingine alikasirika mtoto wake wa miaka mitatu alipojikojolea na kumpiga vibaya, na mtoto kufa pale pale. Mzazi huyu alikosa kujitawala nafsi. Anampiga mtoto mpaka anaua, na anategemea mtoto ajitawale nafsi. Baba mmoja akawa ameandaliwa kuku wa kukaanga. Mtoto akamkuta baba akila, akakimbia akachukua paja la kuku. Baba akakasirika akamshika na kuunganisha vimikono vyake na kisha akachukua panga akavikata akisema; Mikono hii haitawahi kuchukua kuku wangu tena!”

Baba mwingine nchi nayoishi aliyependa gari lake sana, alikuta mtoto analibonda bonda bati lake na jiwe, alikasirika akamkata vidole vyake vyote. Alipowekwa hospitali baba yule alimtembelea na mtoto akamkumbatia baba na kumwuliza “hivi vidole vingine vitaota lini?”. Baba yule kwa kukosa tumaini alienda na kujiua, alichomwa na yale maneno, na hasira zilikuwa zimeisha na akatambua gari ni kitu hafifu mno kulinganisha na mtu na hasa mtoto wake.

Kwa kweli tumekuwa na shida matendo na kauli zetu, na ndimi zetu kwa kuwa wengi wetu tumezitumia kulaani badala ya kubariki watoto. Pengine ni kwa ajili ya misongo ya uchumi, au kuishi mijini ambapo watoto na wazazi hawana shuguli za kutosha.

Wazazi wamesahau wao ndiyo waliwaleta watoto humu duniani. Hata kwa wale wasio na makosa makubwa wamepewa mizigo ya mawe ya maneno na adhabu kali.

Mama mmoja aliniambia “Nimerithi tabia hii kutoka kwa baba yangu; alikuwa na maneno makali kweli, alituita ‘mbwa nyinyi!’ na akawa anafadhili watu wengi na kuwapa maneno matamu watu wa mbali, ila sisi watoto na mama tulikemewa na kupewa mizigo ya kuni za maneno. Alipokuwa na maneno matamu kwetu na kutushugulikia ilikuwa wakati tunaumwa. Wakati huo alitafuta dawa, na kutoa maneno ya faraja. Nilifikiri hivi ni mpaka tupate shida ndipo tuumbe maneno ya kutia moyo kwa watoto wetu? Kuna kitu nimekichunguza kuhusu watu wa Magharibi – hasa wazungu. Wanajua kusifia watoto wao wadogo kuliko sisi.

Mama mmoja Mwamerika mweusi alimkemea kwa matusi mtoto wake wa kiume; kwa kubembea upande ambao walinzi walisema wasibembee. Kidogo akatokea mama mzungu na mtoto mdogo wa umri unaokaribiana na yule Mwamerika mweusi. Yule mama mzungu hakutoa yale matusi, bali alisema kwa upole; “Nicolas, tumeambiwa tusitumie bembea ya upande wa kushoto, hamia kwenye ile ya kulia.” Na mtoto akahama, bila jasho kumtoka au matusi. Yule mama Mwamerika mweusi alinitizama kwa jicho la aina fulani kana kwamba anataka kusema; “Sisi weusi tuna shida na watoto wetu wa kiume, ndiyo maana adhabu zetu kwao na maneno ni makali maana kuwa mwanamume mweusi nchini Amerika ni shida. Kila kitu unasingiziwa “suspect” na adhabu wanazopewa ni kubwa na kukaa jela bila sababu ya maana ni jambo la kawaida. Kwa hiyo najihami na kuwaadabisha watoto wangu wa kiume, kabla wengine hawajawadhuru.” Ni kweli pengine alikuwa na sababu na hata sisi wazazi huku Afrika tuna nia nzuri ya kusaidia watoto mpaka tunapita mpaka na kuharibu mambo kabisa.

Wakati huo huo kumsifu mtoto kupita kiasi, na kisha akaanza kujivuna, kunyanyasa, kubagua au kudharau wengine nayo pia ni shida kubwa. Ni lazima kuwe na mahali pa katikati. Nimesikia mtoto mdogo akimwambia mwenzake “Njoo nyumbani kwangu nitakulisha!” Niliwaza huyu mtoto wa miaka sita anajivuna! Kwanza hana nyumba wala chakula, naye ni “kupe.” Akiwa mtu mzima atawaambia watu masikini,“Mimi ndiyo nakulisha nisingekuwa mimi wala usingeishi.” Hiki ni kiburi na kudharau watu ambao Mungu amewaweka mapitoni mwako kukubariki na kufanya uwe na moyo wa shukurani. Wapendwa hakuna anayejua kukaa katikati, bali tukishuka magotini kila siku, BWANA atatupa hekima yake. Kama tulivyoona kwamba kulea ni kazi kubwa kwani ni mwenye dhambi mmoja anamlea mwenye dhambi mwingine, ataweza kweli pasipo Mwenyezi Mungu.

Mara nyingi wazazi wa siku hizi tumeingia majaribu ya kuwa na shughuli nyingi! Yaani tuna shuguli nyingi, hata tunaona kumfundisha mtoto ustadi kama wa kuvaa nguo zake au kwenda chooni unatuchukulia muda, na hivyo ni afadhali tumvalishe au kumwekea nepi. Zamani wakina mama wa Afrika waliweza kumtenga mtoto katikati ya miguu yao ili aende choo, na akafuzu akiwa na miezi michache tu! Leo nimekutana na kina mama wenye taaluma, wanaoshughulika na masomo shuleni, waliorudia elimu ya watu wazima na pia wanaofanya vibarua na ujasiriamali. Watoto wetu wanavaa pampasi mpaka miaka mitatu na tunajisifu kuwa ni maendeleo. Nilikutana na rafiki nikashangaa! Ana watoto mapacha wenye akili kweli kweli. Wana miaka mitano na wanajua kusoma; ila bado wamevaa nepi kwa vile hana muda wa kuwafundisha (potty training). Pampasi ni

aghali na zina madhara ya afya na pia ni uchafuzi wa mazingira. Kumbe kuwa na maendeleo na vitu vingi ni kupungukiwa katika vitu vinginevyo!

Watu husema sheria ya kwanza ya Mungu mbinguni ni mpangilio (order). Watoto wetu wana vitu vingi vya kuchezea. Wanasesere na vitu vingine vya kuchezea vimezagaa vyumbani mwao na kuachwa bila mpangilio maalumu. Mpangilio unaleta nidhamu na kujenga tabia. Hebu sisi wazazi tuchukue muda kuwafundisha watoto wetu.

Sisi si wataalamu wa kulea watoto. Lakini hiyo haimaanishi ya kuwa, hakuna aliyefuzu! Kila mtu ana mashimo mengi, anayoyaona na asiyoyaona, tunachotakiwa ni kujifunza pamoja. Kuandikwa kwa kitabu hiki kulitokana na kutembelea Afrika Mashariki na Kati kwa miezi tisa bila kuona kitabu cha kiswahili cha malezi ya watoto. Kuna watu milioni 100 wanaozungumza Kiswahii nchini Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo, Kenya na Tanzania. Hata kwenye lile Kongamano la Dodoma la maombi ya kitaifa la mwaka 2012, tulitafuta kitabu cha Kiswahili cha Malezi bila mafanikio na kuishia kuviona vya ndoa tu.

Nafikiri msingi wa ndoa bora unatokana na malezi bora, mara nyingi twapeleka watoto wadogo shule za bweni, nao hawana picha ya kuishi katika familia kwenye mabweni, na mwishowe wale “mashangazi” wa mabwenini wanawaita mama na “wajomba” baba. Matokeo yake sisi wazazi tunabadilika kuwa shangazi na wajomba.

Watu mashuhuri kwa ubaya au kwa wema duniani kote, wamejengeka kutokana na malezi. Mfano ni Thomas Edson aliyegundua taa ya balbu. Alikuwa akifundishwa na mama yake nyumbani kwa kuwa alikuwa mtoto mdadisi na mwalimu wake hakushughulika naye, akidhani kuwa akili yake ilikuwa duni. Mwalimu hakupenda kuulizwa maswali na Edson maana alikuwa akilisumbua darasa lote. Edison alipenda majaribio ya sayansi na alikuwa darasa la kwanza. Mama yake Edson alifanya majaribio ya sayansi na kumnunulia vifaa vya majaribio na akaendelea na utafiti wake. Yasemekana alifanya zaidi ya majaribio elfu moja kabla ya kuvumbua taa.

Hitler, yule fashisti wa kijerumani aliupata ukatili wake kutoka kwa malezi ya mama yake aliyekuwa na ukali wa kikatili. Watoto ni amana tuliyopewa, hebu tuwe wenye kujali na kutumia muda kwa ajili yao katika sala. Watoto ni kipimo ili tabia zetu zizae uvumilivu, na kutoa mikwaruzo ya uchoyo kwenye maisha yetu. Mtoto akilia sharti tuamke, na pia ni lazima tujinyime ili tuwe na chakula cha kumpatia mtoto.

Nilipokuwa mjamzito, nilikuwa na hofu mara nyingi kwamba je kiumbe aliye ndani ya tumbo langu atazaliwa mzima bila kilema? Yaani hatakuwa na kasoro kwenye pua, masikio, macho nk. Mtoto alipozaliwa nikaona ana viungo vyote kamili. Baadaye nilianza kufikiria tabia na malezi yake, je atayamudu masomo na ustadi (academic and skills)? Sasa hivi watoto hao wapo shule ya msingi na bado nafikiria; Je, watasoma vizuri wapate kazi na wajitegeme na pengine wanisaidie uzeeni? Je, watakuwa na tabia njema kwa kupenda watu na kubariki watu wengine kwa huduma na sadaka zao? Na zaidi ya yote, Je, watampenda Mungu maishani mwao na kumtumikia na mwishowe wapate ile thawabu ya paradiso ambayo ndiyo zawadi kubwa duniani kupita zote? Maana itamsaidia nini mtu kupata utajiri na umashuhuri wa duniani ila mwisho aende Jehanamu, au asiwe mbaraka kwa wazazi na jumuiya?

Inasemekana asilimia 75 ya watoto wote humwamini Mungu na kumtumaini na kumtegemea kama mwokozi wao, kabla hawajafikia umri wa miaka kumi. Asilimia 15 kabla hawajafikia umri wa miaka 15, kisha asilimia 7 kabla hawajafikia miaka 15-50, na baada ya miaka 50 ni asilimia 3% tu wanaofanya hivyo! Hii ina maana miaka ile kumi ya mwanzo na hasa sita ndiyo unaweka alama kwenye simenti ya ubongo wa mtoto. Hebu wazazi tuweke mkazo kwa watoto wakiwa wadogo.

Niliona kina mama wengi wa kizungu wanaacha kazi na kuirudia pale mtoto anapofikia miaka saba. Wanapunguza kununua vitu vingi, kama TV na makochi ili mshahara mmoja utoshe. Mama anabaki nyumbani kushugulika na watoto ili kuwajenga kwa tabia bora. Watoto wanaorudi nyumbani wasimkute mama wana upungufu fulani. Haya yameonekana katika nchi za magharibi ambako wenzetu waliyaanza maendeleo haya miaka zaidi ya 70 iliyopita na sasa athari zake zinaonekana wazi. Upo utafiti mwingi unaohusiana na jambo hili. Watoto wengi wamejifunza mabaya mengi kwa ajili ya kutokuwa na uangalizi. Wengine wameingia katika mazingira hatarishi.

Mtoto mmoja wa miaka sita wa Kimarekani alioneshwa kwenye TV miaka ya 1990, kwamba alimwua mwenzake wa miaka sita darasani. Kwa ajili ya wazazi kutokuwa nyumbani, alichukua bastola ya baba yake na kuanza kuitumia. Alipomwona mtoto mwenzake akimtania na kumkejeli kwa vile ni masikini na mweusi, alikuja nayo shuleni na kumfyatulia. Nina imani kama mama angekuwa nyumbani angepata vidokezo fulani, kwamba huyu kijana ana mpango wa kuchukua hii bastola.

Watoto wengi wameitwa watoto ufunguo (latch key kids). Wakifika nyumbani wana funguo zao wanafungua na kuendelea kujimiliki/kujitawala kwa masaa manne kabla mzazi mmoja hajatokezea toka kibaruani. Masaa haya manne mtoto mdogo wa msingi anafanya nini mwenyewe? Labda itakuwa ni runinga yenye mapotofu mengi, hasa pale kwenye chaneli nyingi. Watoto huenda kucheza na watoto wa majirani na kujiingiza kwenye mengi ambayo hayana uangalizi. Tulitembea mji unaoitwa Bunda Tanzania na mtoto wangu wa miaka sita aliniambia “Mama mbona hawa watoto wanamwambia mwenzao avue nguo awe uchi na akavua?” Walikuwa watoto wa kiume wawili wa miaka watano wakimwambia msichana wa miaka minne. Walikaa na watoto wangu kila siku kwa wiki mbili tulipokuwa kule. Wazazi hawakushugulika kuwafuata mpaka jioni, hata wale wenye watoto wa kike!

Hatuwezi kuzika vichwa vyetu mchangani kama mbuni na kujifanya hakuna shida kwetu, au kujifariji kuwa eti hizo ni shida za watu wa Magharibi tu. La, hasha! Hata huko Magharibi wana nafuu. Miaka thelathini iliyopita Tanzania ilipiga marufuku gazeti la Baraza kwa madai kuwa linaandika matusi, linaonesha watu waliovaa nguo fupi n.k. Ni kweli lilikuwa gazeti chafu. Ninachoshangaa siku hizi kuna magazeti yenye matusi kuliko lile la Baraza na yanaanikwa peupee! Nchi za Magharibi zinauza habari kama hizo kwenye shubaka la nyuma ya duka. Televisheni zinazomilikiwa na serikali hubeba pia picha nyingi za wasichana na wavulana walio nusu uchi. Mambo mengi yanayooneshwa kwenye televisheni hizo, ni vishawishi kwa ngono. Kwa kweli kuna machache yaliyo kwenye televisheni hizo ambayo ni ya kujenga.

Nilisafiri kwa basi kutoka Nairobi kwenda Mwanza katika miaka ya tisini. Basi lilikuwa na televisheni na mambo yaliyokuwa yanaoneshwa yalihusu ukatili wa mapambano ya silaha na urafiki wa ngono haramu. Mama mmoja wa watoto wa chini ya miaka kumi alisema “Baba kondakta, badilisha mkanda tuna watoto hapa.” Yule kondakta akajibu, “Waambie watoto wako watazame chini!” Nchi za magharibi hawawezi kuonesha haya hadharani, kwenye basi la jumuiya, kwa kuwa wenzetu wana uhuru wa kuchagua kile mtu binafsi anachotaka kuona. Ipo miziki, na matusi ya ajabu ambayo sitayatamka hapa, ambayo niliyasikia kwenye basi la KBS Nairobi.

Wengi wa watangazaji wa redio siku hizi, wanaiga matusi ya Kiingereza na wanachanganya na lugha za makabila yao au Kiswahili. Nilimwendea kondakta na nikamwambia, pengine wewe wataka kusikiliza matusi, ila hili ni basi la jumuiya silipi nauli yangu kusikia uchafu wa namna hii na nina watoto wadogo. Alisema atapunguza sauti kidogo! Haikusaidia maana nilikuwa nyuma ya dereva. Nikamwambia “Nina dhambi zangu kama binadamu lakini hiyo ya matusi, nimeishinda naomba usiniongezee zako maana endapo nitasikia maneno machafu, itakuwa vigumu kufutika kichwani mwangu, au kujifanya sikuyasikia.” Kwa kweli hata madereva wa matatu au daladala wana shida maana wanatoka nyumbani saa kumi alfajiri na kurudi saa sita ya usiku na hawakutani na watoto wao. Siku nzima wanasikiliza utumbo mwingi na hawaoni watoto na wanazidi kusomba uchafu huu tena.

Napenda kusema siku hizi kina mama wa Magharibi wanarudisha umakini wa kulea watoto wao, ila sisi Waafrika tunapungukiwa. Baba wengi wa nchi za Magharibi, wanashugulikia watoto wao kwa sababu hamna mayaya na wanajenga mahusiano na watoto. Ila kina baba wa nchi zinazoendelea wana shuguli nyingi, na hivyo kujenga mahusiano na watoto wao limekuwa jambo gumu.

Kila binadamu duniani anajua kile kilicho bora na kisichofaa. Hili niligundua nilipoeanda Dodoma Julai, 2012 kwenye kongamano la wanawake. Kauli mbiu ilikuwa ‘wanawake waliovuviwa kiroho wataupindua ulimwengu!’ Fursa ikatolewa ya wanawake waliokuwa wanahudhuria kongamano hilo, kwenda kuzuru bunge lililokuwa linaendelea na kikao chake hapo Dodoma. Kilichonishangaza ni kwamba maafisa wa bunge walituagiza wakisema ‘hakikisheni mmevaa nguo za heshima, zisizo fupi, za kubana au zenye mikono mifupi, siku mnapokuja kutembelea bunge!’ Jamani kumbe kuna kanuni za kuvaa na za kufundisha watoto wetu, ambazo dunia inazifahamu!

Hata ukienda nchi za Magharibi kwenye mahojiano ya kutafuta kazi (interview), ukiwa umevaa nguo za ajabu ajabu wajua huwezi kupata kazi? Sasa kwa nini uvae hizo nguo mbele ya mtoto wako na kujivunjia heshima? Hata mtoto anapaswa kuwa na somo la kuvaa nadhifu na kwa adabu, hasa watoto wa kike ambao ndiyo wanaojaribiwa zaidi kuvaa ovyo. Kuvaa ovyo kunanaathiri afya na maumbile lakini kwa bahati mbaya tunakosa masomo ya kutusaidia kujua pa kuanzia katika kuikabili hali hiyo. Tusipowapa mafunzo hayo watoto wetu kuna uwezekano wa kuhamishia tabia hizo kwa wajukuu zetu. Napenda kusema kwamba hakuna ambaye amefuzu malezi au aliye daktari wa malezi. Mwenye uwezo huo ni Mwenyezi Mungu peke yake! Sisi tunajaribu kudodosa dodosa kwa kutumia uzoefu mdogo tulio nao.

Binadamu amepewa uwezo mkubwa wa kufundishika na Mungu wetu. Ikiwa tunafundisha na kutiisha viumbe vingine ili viwe vya manufaa, Je, haipasi kushugulikia tabia za watoto wetu? Farasi anafundishwa, na mbwa anafundishwa. Nilifika uwanja wa ndege wa Ohare Chicago, nilishangaa nilipoingia nikaambiwa wasafiri wote tupange mstari na mizigo yetu. Baada ya hapo waliletwa mbwa wa polisi kukagua na kunusa ile mizigo. Nikauliza kwani kumekuwaje? Wakasema wanakagua madawa ya kulevya na vitu vingine. Mbwa wamefundishwa mpaka wanaweza kufanya kazi kwa ufanisi hivi! Haukupita muda na mara mbwa alinusa begi fulani na kisha kuanza kulinyanyua. Viumbe vinafunzwa, si kulea mtoto, kumpa chakula, malazi na mavazi tu bali pia kumfundisha ili tabia yake ifae, na kumlinda kutokana na mazingira yake.

Mama mmoja, tuliyekaa naye hotelini, alimwambia mtoto wake wa miaka sita aende chooni. Nikamwuliza anaenda mwenyewe? Akasema ndiyo! Nikwamwambia la hasha! Hapa si nyumbani kuna watu waovu msindikize. Mtoto mmoja wa kike wa miaka kumi alienda mwenyewe chooni akakutana na mwanamume mmoja mwovu akambaka. Mama alimngoja kama dakika ishirini, kisha akaenda akamwita mtoto wa kike. Mtoto wa kike aliitika huku akilia, kwa maumivu na majeraha mengi akielezea jinsi alivyotendwa. “Aliniambia nisitoke nikae humu humu” Yaonekana yule mtu mwovu alikimbia. Jua watoto wako walipo wakati wote.

Wachina wanasema ukitaka kuwa na furaha siku moja nenda kwenye hoteli nzuri na kula mlo mmoja, ukitaka kuwa na furaha ya mwaka mmoja panda miti na bustani (garden), na ukitaka kuwa na furaha maisha yako yote fanya tofauti katika maisha ya mtoto wako (make a difference in a life of a child). Natambua mtoto si mali ya mtu binafsi, bali ni wa jumuiya yote. Wengine miongoni mwa watoto hao, ni wapwa zetu wajukuu zetu, watoto wa majirani, walimu wa shule, viongozi wa mambo ya kiroho kwenye misikiti, makanisa na mahekalu. Watoto bora waliofundishwa vizuri hubariki wengi mara nyingi kuliko hata familia zao. Mfano mhandisi au tabibu atasaidia maelfu katika maisha ya watu.

Nyumba yenye nidhamu na mipango mizuri, huzungumza mengi kwa niaba ya Mungu kuliko mahubiri yote kibwetani. Nyumba yenye mafanikio ni yenye watoto ambao ni mfano kwa jumuiya. Watoto wenye adabu, upole, ukarimu, bidii, na kumcha Mungu wanahudumu na kuburudisha wenye dhiki. Shuguli yetu hapa duniani ni kurithisha watoto wetu dhahabu ya tabia njema. Wanahitajika watoto wema wenye hekima watakaokuwa mbaraka kwa ulimwengu kuliko wenye akili za darasani au kazi nzuri tu.

Usichukue muda mwingi kuhadithia ubaya wa watoto wako. Piga magoti uombe. Nyumbani ndipo ujenzi wa watoto bora ulipo. Si shuleni, kanisani, msikitini, hekaluni, au kwenye jumuiya. Mtoto toka akiwa mdogo unamjenga, na kumpa ujumbe fulani katika maneno yako. Mfano watoto wadogo wa kike wanavalishwa vikaputula vifupi na nguo za kuacha mikono na migongo wazi. Kisha akiwa msichana unataka avae “nguo ya heshima” itawezekana kweli? Kwa sababu ya mitumba nimeona watoto wetu wakivalishwa nguo zilizo kinyume cha tamaduni zetu maana zinaacha miili wazi. Mtoto wako nyumbani ndiyo anafundishwa kuvaa, usafi, adabu na mengineyo. Mtoto wangu wa kiume ana tabia ya kuvaa nguo ndani nje, na mbele nyuma. Nikiwa nyumbani nimekuwa nami na tabia hii naye ameiga! Sijaleta mvuto mzuri!

Tuepuke tabia ya kumsifia mtoto kupita kiasi, maana yaweza kumfanya ajivune na kumpa wakati mgumu katika kuishi na watu. Kila kitu kifanyike kwa kiasi. Ubunifu wa mtoto ni wa muhimu. Je utamsaidia kuwa mbunifu? Mpe uhuru na majukumu. Akicheza au akichora, ajieleze nia yake na anachotaka kuchora, kutengeneza au kuumba. Watoto wengi wa nchi za Magharibi wameweza kuvumbua vitu siyo kwa sababu wana utajiri, ila ni kwa sababu wazazi wamewaachia nafasi ya ugunduzi. Usimlinganishe mtoto wako na wa mwingine. Angalia usikazanie kutoa ushauri wako kila mara mpaka uone umehitajiwa. Mara zote uwe tayari kucheza na kuunda vitu na watoto wako kwa kutumia kazi za mikono au burudani. Utajua anachofikiri na kumwongoza vyema naye pia atajenga kukuthamini na kukuamini. Kumpa mtoto muda ni sawa na kumpa upendo wako! Jibu maswali yake, sikiliza anachosema, na uishi maisha ya uaminifu na ya mfano kwa maneno yako, kwa matendo yako, na kwa mawasiliano yako. Watoto wanahitaji kujenga imani kwako kwamba wewe unawajali, hivyo usiache kuwapongeza wakitenda mazuri. Maneno mazuri hujenga. Waambie maamuzi ya familia, na waambie kwamba wao ni sehemu muhimu ya familia na namna kuzaliwa kwao kwenye familia yenu kulivyoleta furaha. Watoto wangu wanataka niwahadithie hili tena na tena! Wanauliza, “Nilipozaliwa ulifikiriaje? Je nilikuwa na uzito gani? Nilikuwa nalia sana? Ilikuwa juma ngapi?” Huwa ninachoka kurudia rudia ila najikaza kwa kuwa natambua umuhimu wa maswali yao. Wazazi tujikaze!

Waambieni watoto wenu, jinsi nyie wazazi mnavyotaka kujua kinachoendelea katika maisha yao. Angalieni hasira isije ikaharibu mahusiano. Watoto wengine hawajazoea kutazama wazazi usoni kutokana na walivyolelewa. Mamlaka yanakuwa na umbali kiasi fulani. Hili laweza kuwa na athari hapo baadaye. Mfano marubani wa Korea wakati fulani walipokuwa wakiendesha ndege za kawaida za Boeing, ndege hizo zilikuwa zikianguka sana hata kufikia hatua ya kupigwa marufuku wasitue katika miji mingine. Watu wakashangaa inakuwaje Wakorea ambao ni watu makini katika shuguli zao zingine wanapoteza umakini katika kurusha ndege?

Mwanasaikologia mmoja alifanya utafiti wa mila, jadi kwa kutumia kisanduku chekundu (black box) na kugundua kwamba wanatii sana maagizo ya mamlaka hata kama kuna kosa kwenye maagizo hayo. Wakati wa ukaguzi wakigundua kwamba kuna kosa la kiufundi, na kisha wakimshauri mhandisi mkuu hufokewa na kuambiwa hamna shida hapo, nao hufyata mkia na kukubali kuondoka na ndege yenye matatizo. Hujikunyata na kutii kwa kutaka wasimkasirishe mkubwa hata kama wanajua wanaenda kupoteza maisha. Waliposahihisha hilo kwamba “kutokana na sheria zetu haijalishi wewe ni mkubwa au nani ukiwambia usitoe ndege kiwanjani”.
Jambo jingine kuhusu mawasiliano ni sisi wazazi. Je ninafoka nyumbani? Je ninaonyesha uasi na chuki kwa mke/mume wangu, bosi wangu, jirani au watoto wangu? Je, ni mtu mwenye uvumilivu, na upole kwa watu wengine?

Tujitahidi wazazi na watoto wetu, katika imani tutie wema, na katika wema maarifa, na katika maarifa kiasi, na katika kiasi saburi na katika saburi utauwa, na katika utauwa upendo.

SURA YA 13

NDOA TAKATIFU

Ndoa ni muhimu mno kwenye malezi ya watoto. Kwa mpango wa Mungu, mtoto ni tunda la ndoa. Ndoa itaathri maisha yako na ya mtoto hapa dunaniani na kwenye ulimwengu ujao. Ndoa ilianzia bustani ya Eden, ambapo Mungu mwenyewe aliisimika. Maisha ya upendo, usafi, staha, wajibu na ushirikiano kati ya mume na mke ni ya muhimu. Ndoa ni shule ya maisha yako yote. Ni vyema iwe ya watu wa imani moja, na ikiwezekana wa utamaduni mmoja. Hii inafanya amani na utulivu viwepo. Wachunguzi waligundua kwamba watu wanaoishi katika ndoa kwa muda mrefu duniani ni Wachina, kwa kuwa wana utamaduni na imani moja. Ingawa imani zao ukizichunguza hazimweki Mungu mbele, ila wakiwa na mambo mengi yakufanana na yamtizamo mmoja kama chakula, elimu, na mengineyo wanakuwa na mizozo michache. Watu wamegombania mambo madogo madogo mfano mhindi anaweka pilipili nyingi na mchina hapendi.

Ni muhimu unapochagua mwenzi, kufikiria kwamba huyu ndiye atakayekuwa baba au mama wa watoto wako, na kama umefanya kosa katika uchaguzi, usisite kusitisha uchumba huo, na kumwomba Mungu akuongoze, ili upate mke au mume mwema.

Nyumba ya mizozano inaleta huzuni kwako na kwa watoto pia. Hebu usije ukafanya kosa la kukutana na mtu usiyemjua vizuri barabarani, au kwenye mtandao wa kompyuta kisha mkafunga naye ndoa. Mara nyingi watu wasiofahamiana hujihami kwa kutoonyesha tabia halisi, na kwa hiyo ni vyema uchumba uwe angalau miezi sita mpaka miaka miwili, na ni vyema pia ukawa na tarifa za kutosha za mtu huyu kwa kumwona kabla hajawa mchumba au kwa kupata ushauri wa watu ambao ni wakweli na wanaompenda Mungu. Watu wengi siku hizi hutaka ndugu zao waoe au kuolewa japo

kuwa wana tabia ngumu, na kwa sababu hiyo wengi hujizuia kusema ukweli kuwahusu hawa ndugu zao.

Mchungaji mmoja na rafiki aitwa Absalomu aliniambia, “Siku hizi mtu akiniuliza tabia ya mtu anayetaka kuoa sitamwambia, maana nikisema navyoijua nitachukiwa, hivyo hata kama ni mchawi, nitasema sijui”. Nilimwuliza rafiki huyu, “Je, akiwa binti yako utajisikiaje?” Alijibu, “Kama ni binti yangu, hicho ni kitu kingine, ningependa kujua ukweli wote!” Wale waishio nje ya kwao ni vigumu kujua tabia za watu ambao hawakukua nao kijijini. Mfano ni wa watu watatu ambao kwa nyakati tofauti ndani ya miaka mitatu walikuja kuniposa. Kwa vile nilikuwa chuoni, niliwaambia kwa kweli sikupanga kuolewa wakati huo. Baada ya muda niligundua walikuwa na wake na watoto katika nchi zao walizotoka, na wale wake na watoto baadaye wakaja, na wawili kati ya hao walikuwa wachungaji. Ninachosisitiza hapa ni kuwa, ni “Mungu tu atakayekusaidia katika hili!”. Usichezee ndoa yako.

Uwe mwanamume au mwanamke! Mungu alimpa ndoa mwanadamu kukuza uhusiano wake kati yake na YEYE. Ndoa ni takatifu na inazo sheria kama serikali. Mungu hakuanzisha ndoa izae talaka ila kwa ajili ya dhambi jambo hilo lilitokea. Kwa mujibu wa Maandiko Matakatifu, talaka iliruhusiwa kutolewa kwa kosa la uasherati tu. Lakini si lazima ndoa ivunjike kwa kosa la usherati, kwani bado kuna mlango mpana wa msamaha kwa mkosaji. Msahemeane hata sabini mara sabini. Ndoa pia ilianzishwa ilete furaha na si huzuni. “Umfurahie mke wa ujana wako...uishi kwa furaha na mke umpendaye”. Mungu alimfanya mke toka kwa mume awe mwenziwe, awe msaidizi wake, wasitawalane, ila pawepo na upendo na utii. Msaidizi ni wa muhimu. Kama ilivyo kwa Roho Mtakatifu ambaye ni msaidizi na ana nafasi yake muhimu. Mungu alitaka Adamu na Hawa wafurahiane, watiane moyo, wafarijiane, wathaminiane, na wapendane. Hata kama huoni thamani ya ndoa kwa sasa kwa kuwa unaishi na mwenzi wako, siku utakapoishi upweke utatambua thamani yake.

Mama mmoja kabla mumewe hajafa alisema “mimi ni mjane tu, huyu mwanamume hafanyi chochote nyumbani ni mimi tu” baada ya mumewe kufa aliwashuhudia watu akisema, “sikujua mwanamume ana uzito kiasi hiki. Wafanyakazi wananidharau, hawanisikilizi nikiwatuma, wanawake wengine wananikimbia wakifikiri nitachukuwa waume zao, na marafiki wa mume wangu wakiniona wananikwepa wakifikiri nitawaomba msaada!’ Jiulize kama ndoa si muhimu, je ni kwa nini wanaoachika huenda kutafuta tena?

Mungu hakuanzisha ndoa ili awaweke mume na mke katika madaraja tofauti, bali alisema hao wawili watakuwa mmoja. “Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake na hao wawili watakuwa kitu kimoja, na kile ambacho Mungu alichokiunganisha Mungu Mwanadamu asikitenganishe”. Thamani ya Adamu na Hawa mbele za Mungu ilikuwa moja. Chochote alichokuwanacho Adamu, Hawa alikuwa nacho. Mila za kutisha zimezuka za kudhalilisha wanawake, na hata baadhi ya makabila au mataifa ya Afrika yanahesabu kuzaa mtoto wa kike ni mkosi. Kule China na India mimba za watoto wa kike zinatolewa, na hii imesababisha mamilioni ya Wachina kukosa wanawake wa kuoa! Mtoto ni mtoto. Makabila mengine yamezika mwanamke hai wakati mume wake alipokufa!

Biblia yasema “Mke ni kitu chema.” Mara nyingi wanaume tunathamini mama na dada zetu ila si wake zetu. Wote hawa ni wa Mungu! Mke ni mwenzi wa mume wake, na ndiye rafiki na jirani wa kwanza. “Mpende jirani yako kama nafsi yako.” “Mwanamke mwema ni taji ya mumewe. Mume wake hujulikana mlangoni aketipo pamoja na wazee wa nchi;” Methali 31:23. Mume au mke wako ni zawadi toka kwa Bwana, na ni mdhamini wa maisha yako ukiwa mgonjwa au katika shida yoyote. Kwa kawaida utaishi naye muda mrefu kuliko wazazi wako!

Mke na mume ni msiri na mshirika wa mwenzake katika mambo yao. Kama kuna kudharauliana au kudhalilishana kukome! Mko timu moja; mna ubia. Mwenzako akishinda nawe umeshinda, akishindwa umeshindwa. Kila mmoja lazima ajitoe kwa mwenzake asilimia 100 na si 50%. Kama ni hamsini kwa kila mmoja ni dhahiri ndoa itavunjika. Mara nyingi tumependa kutenga wenzi wetu tukidhani ndivyo tutafanikiwa na huku kila mtu anajifikiria mwenyewe. Mahali ambapo tungeshinda na kufanikiwa kidogo tungeshinda na kufanikiwa zaidi.
Nimesikia wanawake wakisema “mwanamume si ndugu yako eti!” kwa kweli kwa mpango wa Mungu mume alipaswa kuwa karibu na mke wake kuliko mwingine yoyote. Wanawake wengi wanasahau waume zao wanapozaa. Washauri wanasema “mfanye mume wako awe mtoto wako wa kwanza.” Ukimpenda na kumthamini naye akafanya vivyo hivyo mtaishi mbingu ndogo hapa duniani. Ni kwa vile umimi na ubinafsi unajiinua kichwa chake ndiyo maana kila mtu anajihami. Kuonyesha upendo kwa mke au mume wako si kuonyesha udhaifu wako, kujidharau au kutimiza matakwa ya Maandiko peke yake la! Ni kuongeza furaha yako. Onyesha upendo kwa kuzungumza na kwa kutenda utaleta furaha. Usiseme anajua ninampenda! Mume pia asiwe mtu anayetaka kuburuza, kunyanyasa au mwenye matakwa magumu kuyatimiza. Toa uhuru kwa ubavu wako naye atakufanyia vingi kwa upendo.

Ndoa aliyoianzisha Mungu, ni ya mume mmoja na mke mmoja. Mungu hakuumba Adamu na Hawa na Mariamu! Je wewe mume au mke unatajisikiaje endapo mwenzako ana ndoa ya watu wawili au zaidi? Nchi nyingine zina tofauti ya mitala, yaani mwanamke mmoja ana waume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja. Na watu wa Magharibi wana mitala ya mke mmoja kwa wakati mmoja, na kuachana bila sababu za maana. Mtu huyu aoapo mwingine yule aliyemwacha kisheria na kwa haki mbele za Mungu bado ni mke au mume wake. Hakuna mwanamke au mwanamume anayependa mitala kamwe, maana mitala ni shida tu. Wanawake wengi wanakaa kwenye mitala ya mume mmoja na wake wengi hapa kwetu Afrika ya Mashariki, ila nchi chache duniani, kama za Afrika Magharibi, mwanamke mmoja ana waume wawili kwa jadi zao!

Watu wengi hapa Afrika walitoa sababu zifuatazo za kuwa na mitara:
Wanaume ni wachache ukilinganisha wanawake ambapo kwa wastani wanaume ni asilimia 44. Sababu nyingine ya kuoa mitala ni kutafuta hadhi na misukumo ya kikabila. Mfano katika makabila mengine mwanaume asiye na mitala hubezwa na kuambiwa “kuwa na mke mmoja ni kama mtu mwenye jicho moja!” Mitala katika jamii zingine imetumika kama mbinu ya uzazi wa majira. Kutokuwa na kiasi na kushindwa kungoja mzunguko wa kike wa maumbile ambayo Mungu alitupangia. Mitala pia huchukuliwa kama njia ya kuzalisha mali kwa kuwa na watoto wengi.

Mitala wakati mwingine imetokana na kukosa watoto kabisa, na hivyo kuoa mke mwingine kwa matarajio ya kujipatia mtoto. Mitara pia huweza kutokea kutokana na kuwa na watoto wa jinsia moja na hivyo kujaribu kuoa mke mwingine kwa nia ya kujipatia watoto wa jinsia tofauti. Wengine huamua kuoa mitara kutokana na kuozwa mke ambaye si chaguo lake. Mitara pia hutokana na kutofautiana sana baada ya ndoa kwa ajili ya kutojiendeleza kwa mke, kielimu, au kimwonekano. Hata hivyo, tatizo kuu ambalo ndiyo shina la mitara ni kupungua kwa upendo! Watu wanaanza kutothaminiana na kuacha kuhudumiana ipasavyo na kuanza kuona wale wanaofanya nao kazi na kukutana nao kila siku ndiyo wa muhimu au wazuri zaidi. Wanaume wengine hufikiri kwamba wakiwa matajiri, kuoa wake wengi ni burdani ya kutumia mali zao.

Mitara ina matatizo mengi sana, hasa katika uleaji wa watoto. Tunayashuhudia haya kwa Ibrahimu aliyeingia katika mitara kwa kufuata ushauri wa mke wake. Kwanza wale wake wanaoneana chuki, na watoto wao wanajiunga na timu za mama zao. Japo Hajiri ambaye aliingizwa aliungama na kujinyenyekeza bado watoto wakaanza kudhihakiana. Mungu alinyamaza hakusema kitu ila wakati machafuko yalipozuka tena aliingilia kati na kumwambia "Ibrahimu sikiliza sauti ya mke wako, maana katika Isaka uzao wako utaitwa" Hivyo ilibidi Ibrahimu amwache Hajiri aende zake. Hata hivyo si kweli kuwa mume mwenye mitara huwapenda wake hao wote kwa usawa. Mungu aliumba mke mmoja na mume mmoja, wawe mwili mmoja na hivyo kuingiza mtu mwingine si ndoa ambayo Mungu aliikusudia, ila ni mipango mingine ya udhaifu na dhambi zetu kama binadamu.

Ndoa hizi pia zinaleta wasiwasi kwa mume kwamba pengine aweza kuwekewa sumu na wale wake wanaompa dawa ili wapendwe, au wake zake hawatoshelezwi na wataenda na wanaume wengine na kuleta magonjwa mengi ya zinaa. Ndoa hizi kiuchumi mara nyingi hazitoleshelezi mahitaji ya wake na watoto na kufanya wawe kama wajane au yatima. Mume ndiye anayekaa kama Sultani akitumikiwa. Wake wanashindana tu ili wamfurahishe mume, ili angalao wapendwe zaidi! Watoto hukua katika dhiki na kujenga chuki na baba zao na pengine wakasaidiwa na jamaa za mama zao au serikali katika kusomeshwa. Watoto pia hukosa upendo wa baba. Baba anakuwa katika mizunguko ya nyumba zingine, na kwa kuwa mtoto huhitaji upendo wa baba na mama mtoto hujikuta akipungukiwa na upendo wa baba. Baba huwa mgeni kila apitapo kwenye mizunguko ya familia yenye mitara. Watoto huishia kufanya vituko vya ajabu na kupungukiwa na hadhi.

Mfano ni nyumba ya mfalme Daudi ambayo watoto wake walifikia hatua ya mmoja kumwua mwingine na mwingine kumbaka dada yake.
Neno la Mungu linasema ilitokana na baba kushugulika na wanawake na kutotumia muda wake wa kutosha kuadilisha watoto kama baba. Hii inachangia ubaba uliopasuka na kuvunjika. Watoto wanakosa nidhamu mfano: Yakobo alikuwa na shida nyingi ya watoto wa mama mbali mbali kugombana na wake zake ambao walikuwa madada wa rika moja na wanawe wa kiume. Hata kijana wake wa kwanza Reuben akalala na Bilha mama yake wa kambo. Na vijana wa pili na tatu walikuwa na harara na kuua watu wengi wa Shekemu.

Napenda kusema kwamba ndoa iliyo bora ni ile inayomtanguliza Mungu mbele "Bwana asipoijenga nyumba waijengao wafanya kazi bure. Bwana asipoulinda mji yeye aulindaye akesha bure' zab 127:1

Ndoa ni shule ambayo hakuna anayeweza kusema amefuzu, wanandoa chukueni muda kujifunza na kusoma vitabu vya kuwasaidia hasa vile ambayo vinaongozwa na Maandiko ya Mungu. Hebu muwe watu wa kiasi katika mahusiano yenu. Angalia kwenye rejea (bibliography vitabu uvitumie, angalia kwenye compyuta). Ili kupata leseni ya gari lazima usome udereva kwenye kitabu na barabarani kwa miezi kadhaa. Ila kabla ya kuoa au kuolewa watu wachache sana wanasoma vitabu vya ndoa na malezi ya watoto. Wanategemea kwamba ndoa zao zitafanikiwa tu, eti kwa sababu wanapendana sana! Na malezi ya watoto kwamba yatafanikiwa tu! Usijidanganye anza kusoma neno la Mungu kila siku lina maelezeo mengi ya ndoa na malezi.

Kina mama msichukue muda mwingi kupamba nyumba na shuguli za nyumbani na mkasahau kusoma na mume. Anza kusoma kitabu cha Mithali. Kuna waandishi wengi pia wanaompenda Mungu walioandika mambo yenye manufaa sana. Chukua muda wa kusoma vitabu, kujifunza na kufanyia mazoezi uliyojifunza ili yakusaidie katika ndoa yako na hatimaye katika malezi ya watoto. Kuna falsafa nyingi za kujenga unyumba mwema, hizi nyingi hazifanyi kazi vizuri mara nyingi. Wengi niliokutana nao, wale ambao wana elimu ya ushauri na shahada kubwa, wamekuwa wakiongoza nyanja hiyo bila kujikita kwenye neno la Mungu. Wameachana mara nyingi (wamepeana talaka zaidi ya moja) na hata mara nyingine najiuliza: wanashaurije wengine ambapo wao hawakufaulu? Ila wengi wa taaluma hizo wamenieleza kwamba eti watu wakiachika ndiyo wanashauri vizuri zaidi kwa sababu walijifunza kutokana na makosa waliyofanya!

Ndugu msomaji utajaza jedwali mwenyewe unapotafuta mshauri kwa ajili ya ndoa yako. Sina maana kwamba mashauri ya viongozi, au wasomi yasisikilizwe, ila jitahidi kwamba watu hao wawe watu wenye hekima ya kiroho pia. Kumbuka, hata kama ni viongozi wa dini epuka kutoa siri za nyumbani kwako bila sababu. Uwe mwangalifu unapotafuta mashauri. Ndoa zote ni safari ndefu yenye milima na mabonde, tufani na mengineyo. Kiongozi mkuu katika safari hii awe Mungu Yeye atawasaidia, kuvumilia, kushirikiana, amani, upendo na jinsi ya kutatua matatizo. Jambo kubwa katika mioyo yenu ni kusema “Lolote litakalotokea Bwana ni rubani atatusaidia katika kutatua matatizo.” Lazima msimame dede pamoja, mkiwa timu moja kukabiliana na lolote lijalo.

Safari ya unyumba huanza na safari iitwayo marekebisho. Wakati wa fungate mke na mume huchukua muda kuonyeshana mapenzi na hisia zao, kufanya marekebisho, muda wa kupanga sura ya familia itakavyokuwa, na kufahamiana vizuri na kila mmoja. Jambo hili limeidhinishwa pia katika Neno la Mungu; “Mtu atwaapo mke mpya, asiende vitani pamoja na jeshi wala asipewe shuguli juu yake yoyote, akae faragha mwaka mmoja nyumbani mwake apate kumfurahisha mkewe aliiyemtwaa.” Kumb. 24:5.
Huu ni muda wa kujiweka katika mfumo mpya wa upendo na kufanya mambo pamoja. Lala, tembea, zungumza, starehe na cheka na mwenzi wako. Ni wakati wa kupata uzoefu wa kupembua na kumaliza tofauti endapo mmekwazana au kuhitilafiana katika mawazo. Muda huu wenzi hawa hugundua vile vinavyowapendeza na visivyowapendeza. Wenzi hawa na waweke kanuni za maisha ya familia zitakavyokuwa na kuziweka katika vitendo; kwa mfano wakati wa kuomba na kusoma Neno la Mungu, wakati wa kula, jinsi ya kuhusiana na wakwe, watoto wangapi wazaliwe na mengineyo.

Kipindi hichi cha faragha ndiyo muda unaofaa kufahamiana vizuri na kufunua utu wenu uliofichika. Mtagundua yale yanayompendeza mwenzi, udhaifu wake na uimara wake. Kwa jumla utagundua tofauti nyingi ndogo ndogo. Kujua haya kutasaidia katika ndoa na maisha yenu. Watu wengine huwa wanakata tamaa wakijua uhalisia wa mwingine. Hii si sawa, kwani hiyo inatusaidia kutafuta suluhu.

Kila binadamu anapoingia katika ndoa anakuwa na matarajio fulani kutoka kwa mwenzi wake. Matarajio hayo ni kama kupendwa kwa dhati, kuaminiwa katika kila jambo, kuheshimiwa mawazo yako, kupewa shukrani pale unapostahili, kufahamika na kueleweka nia yako, kutiwa nguvu kwa mambo ambayo una shauku nayo, kusaidiwa katika matatizo, kusaidiwa katika kuamua, kufurahia uwezo au vipawa vyako, kufanya ujisikie ni wa muhimu, kuondolewa upweke na mengineyo. Ingawa wengi hujitahidi kuwatimizia wenzi wao mambo haya, uhalisia, ubinadamu na hata wakati mwingine ubinafsi huingia.

Wapenzi wapaswa kuwa wavumilivu, wenye ushirikiano, hekima na maarifa katika kutafuta suluhu. Kila ndoa hupitia hatua hii na kama bustani yapaswa ipaliliwe mara kwa mara ili maua yake yashamiri na kutoa harufu ya manukato. Unapoona ndoa za kupigiwa mfano na kutamanika zimepita hatua hii, na kwa ushirikiano wapenzi wametafuta muafaka wa maisha mapya, ndipo utajua umuhimu wa kujifunza uvumilivu katika ndoa. Baada ya ndoa, kila mtu amkubali mwenzake kama alivyo na kuacha mazoea ya wakati wa ukapera. Fanyieni kazi tofauti za tabia zenu, uhusiano wa nje, tendo la ndoa, mawasiliano na matumizi ya fedha.

Jambo kubwa katika yote ni kujua kwamba “Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake na kuambatana na mke wake, na wawili watakuwa mmoja.” Ni jukumu lenu kutafuta jinsi ya kuishi pamoja bila kuzua matatizo. Watu wote wanatofautiana hata wawe ndugu waliozaliwa pamoja, au wazazi mkiishi pamoja na watoto wakubwa, na kushirikiana mambo mengi kwa undani kama vile mume au mke yabidi mujiweke sawa ili msizue mizozo. Msemo: “Mama nipe radhi kuishi na watu kazi,” ni kweli kabisa. Mizozo mingi huashiria kwamba ipo haja ya kurekebisha mambo ili uhusiano uimarike. Namna unavyomaliza mizozo na mke wako ndiyo uhusiano wenu unavyozidi kuimarika. Mizozo huzuka kutokana na maoni tofauti, na isiposhugulikiwa vizuri na mapema huweza kuzua ugomvi na kufanya wenzi wafarakane hasa pale mmojawapo anapojaribiwa kutumia mamlaka isivyo halali na kutoa kauli za ukali kama, “Upende usipende tutakaa na mama yangu.”

Ili uhusiano usiangamie yabidi hekima, uvumilivu na kuthaminiana viendelee kuwapo wakati mkipitia mabonde na milima ya maisha. Wale marafiki wa zamani wakitoa mashauri yao kwenu yabidi muwe waangalifu. Mungu awe mshauri wenu namba moja. Kwa maana, “Bwana asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure.” Watambulishe rafiki zako kwa mwenzi wako ili mwenzi wako asipate tafsiri potofu au kupata mashaka nao. Nimeona katika desturi za watu wengine, huwa hakuna kutambulishana. Unakutana na mtu mwenzako haumjui mnaingilia gumzo lenu na kumtelekeza (ignore) kabisa uliyekuja naye. Mnakuwa kama hampo safari moja. Mkimaliza na huyo wa barabarani ndiyo mnaokota uhusiano wenu na kuendelea nao tena!

Kama ulikuwa na mzazi mwenzio mwingine kabla ya kuolewa uyaweke haya wazi pia. Usionyeshe kumthamini yeyé kuliko mwenzi wako na uweke mpaka katika mahusiano yenu, mfano hata kama alizoea kuja chumbani kwako kabla hujaoa au kuolewa, piga marufuku kwa hilo.

Uwe mkweli na muwazi kwa mwenzi wako akikudadisi kuhusu watu fulani, barua, au SMS fulani.Ukipigiwa simu usiende kujibia chooni au chumba kingine. Hilo litafanya mwenzio akutilie shaka kwamba una siri fulani ambayo hutaki aijue. Usitoe maelezo ya kudanganya, maana akigundua hatakuamini nyendo zako. Maisha yahusuyo mahusiano ya zamani kama vile picha au barua na mengineyo yenye utusitusi yateketeze mapema kabla ya kuingia kwenye ndoa. Hebu pangeni matumizi ya pesa pamoja. Ni muhimu kuwa na bajeti ya familia ambayo wote mtashiriki kutoa mawazo. Mume au mke asishiriki mawazo potofu toka kwa wanaume wengine au wanawake wengine. Endapo makosa yatatokea hebu mume na mke wawe wepesi kuombana msahama na kujirudi. Maneno ya sumaku yanayonasa upendo na amani ni yale matano nayo ni "Tafadhali, asante, pole, nisamehe, na nakupenda." Yanapotumiwa huthibitisha ukweli wa kwenye Maandiko Matakatifu kuwa ndoa ni kitu cha furaha, amani na upendo.

Tuwe tayari kukiri makosa "Ungamianeni ninyi kwa ninyi". Hautadhalilika wala kujipunguzia hadhi. Tunyoosheane vidole. Jambo hili la kunyoosheana vidole limekuwa ni shida kubwa katika ndoa nyingi. Kumbuka Mungu alimwuliza swali Adamu; "Je umekula yale matunda?" Naye hakujibu alichoulizwa ila alisema "ni mke uliyenipa!" Lawana kamwe haijengi ndoa bora bali badala yake huhuzunisha watoto na kuwafanya nao wasikiri makosa yao wanapoyafanya.

Mungu hutusamehe tunapokiri makosa, kuungama na kuyaacha. Yeye ni Mwenye rehema. Jifunze kuungama unapomfanyia mwenzio makosa. Kiburi kiwe mwiko kwako kama unataka kujenga unyumba bora na kuwa mzazi bora. Watoto wako nao wakiona unavyonyenyekea na kuungama watafanya hivyo hivyo wanapokosa na kutatua matatizo yao. Watoto wanaangalia jinsi unavyomheshimu mume wako au kumpenda mke wako.

Jifunzeni kuzungumza lugha nzuri, na wala msitumie matusi. Watu hufikia misingi ya kuoana na kupendana kutokana na maneno! Mvulana humtafuta msichana na kumwambia nakupenda. Binti, kama naye anapenda, hufurahia na kusema maneno matamu ambayo wazungu huyaita "sweet little nothings." Mtu aweza kusema sili wala silali kwa kukufikiri, nakuota na mengine mengi! Maneno mengine matamu matamu yanatiririka kama vile, pole mpenzi, nakukumbuka na kadhalika. Hebu basi haya maneno matamu na tabasamu yaendelee maana ndiyo yatakayowapa furaha na kuwasaidia katika umoja wenu.

Msikashifiane. Mahaba yakipungua, yapalilieni. Hakuna mtu mzuri duniani utakayeridhika naye! Ukimtafuta wa aina hiyo utamkosa. Yule uliye naye ndiye mzuri. Mjenge basi kwa njia zote. Nafikiri mmesikia kwamba ndoa ya kwanza ina uwezekano wa talaka wa asilimia 50, wakati ndoa ya pili ina uwezekano wa 73%, na ndoa ya tatu 94%! Waweza kufikiri unatatua tatizo kwa kukimbilia ndoa yako na kumbe unazua matatizo mengin zaidi! Nimeona rafiki wakisema "Yule mume wa kwanza alikuwa mlevi ila alikuwa nafuu. Huyu ni bahili na msengenyaji afadhali ningeishi na yule mlevi!

Usimtukane mwenzi wako kwa maneno kama, “Una meno kama kenge.” Maana hiyo yaonyesha kuwa uchaguzi wako pia haukuwa mzuri kuolewa na kenge. Maneno huchochea chuki na hasira. Maneno mengine wazazi wanayoyatumia kwa watoto wakati wakigombana ni mabaya sana. Kusema “Mbwa wee, kama baba yako!” huonyesha kuwa umeathirika kimawazo kwani mbwa huzaa mbwa na kwa hiyo unachosema ni kuwa yule mume au mkeo aliyezaa huyo mtoto naye ni mbwa! Hebu tuchunge midomo yetu, maana wawili watakuwa mmoja.

Ulimi huwasha moto, Mithali 31:9. “Mwanamke mpumbavu hupiga kelele ni mjinga hajui kitu”. Hebu tujifunze kuondoa hasira maana haina utulivu au upole. Hasira huharibu nyumba nyingi. Mwombe Mungu atoe hasira yako kabla jua halijatua! Uwe unamchumbia mwenzio kila siku mtaishi kwa upendo mwingi. Akitoa jibu la ukali wewe poza kwa kutoa jibu la upole. “Jibu la upole hugeuza hasira bali neno liumizalo huchochea gadhabu.” Kuwa muwazi na kumpa mwenzako imani kwa kutokuwa na vitendo vinavyompa mwenzako hisia mbaya. Mfano kukaa na watu wa jinsia tofauti na kuwaonyesha shauku ambayo yapasa tu kuonyeshwa kwa mwenzi wako.

Pesa na mawasiliano ya kuitumia katika nchi nyingi ndiyo jambo linaloleta magomvi ya ndoa. Hebu mwanamke pia awe na sauti ya kuzungumza katika bajeti. Pesa ni za wote, mmekuwa mwili mmoja. Kufichiana mapato yanafanya msiwe mume na mke bali kama wapangaji katika nyumba moja. Mwe na mipango na malengo mamoja, msitawaliwe na pesa bali muitawale. Usitumie pesa kwa jambo ambalo hukulipangia. Keti na mwenzi wako mshauriane. Mkumbuke kutoa sadaka na zaka kwa Mungu wenu. Kama wenzi mshiriki pamoja mambo matakatifu kama kuomba pamoja, kusoma Neno la Mungu, kwenda kwenye ibada, kulala pamoja na kubadilishana mawazo. Msijifanye mna shughuli nyingi.

Watu wengine kwa kupanga, wanaazimia katika ndoa yao mwanamke atakaa kijijini na wazazi pamoja na watoto na mume atakaa mjini akifanya kazi. Hii si ndoa. Mke si mama yako kwamba mukae mbali mbali. Kama ni maswala ya dharura kama vile elimu na ugonjwa vinavyowafanya muwe mbali mbali, hebu na yawe ya muda mfupi tu. Lazima mwende sambamba kwa hayo. Kama mke anaenda ibadani na mume anaenda kuvua samaki je mtoto atafanya nini? Tumieni uhuru wenu vizuri, ndoa inakuwa na shida endapo hamko wazi japo mu huru. Kuwe na demokrasia ya kuruhusu kila mmoja wenu kutoa mawazo yake. Usiseme”mimi ndiyo mwanamume hapa, unaniuliza naenda wapi? Utajua safari za wanaume wewe mwanamke?” Narudia, Jifunzeni kusema maneno matamu na mazuri, si udhaifu la hasha, ni katika jitahidi za kupendezana. Mara nyingi twapendeza watu wa mbali ambao hawatatusaidia chochote na kutia huzuni wale wa karibu na hiyo huturudishia huzuni.

Si vibaya kabisa kumpokea mzigo mume wako atokapo kazini au mke atokapo sokoni. Kupeana zawadi za kufurahishana ni jambo la kawaida sana katika mahusiano ya ndoa, mbona mlifanya hivyo wakati wa uchumba? Je sasa zawadi imekuwa mwiko?mbona zitaleta furaha tu. Fanyieni ukarimu na kuruahiana na kushangiliana! Haya yote huamsha hisia za mwenzi na kumwelekeza katika upendo. Kipaumbile kiwe kila mtu amwelewe mwenzake; yaani atambue mabadiliko ya mwili na ya kisikolojia. Kila mtu akubali kuacha madai ya haki zake. Hakuna mmoja anayepaswa kushindwa kuridhisha hisia za

mwenzake ambazo zimetolewa na Mungu mwenyewe na kuweka ndoa yao katika majaribu.Usiwe mtu wa kukosoa wakati wote na kushindwa kushukuru pale unapoona umetendewa wema. Usitake kulazimisha mwenzi wako awe kama ulivyo wewe. Watu wana haiba tofauti.

Neno la Mungu linasema uzinzi ni kwa yule mtu aliyepungukiwa na akili (Mithali 9:13-17). Ili kuokoa janga la uzinzi linaloikumba nyumba yako mwombe Mungu awafunulie. Mfano magonjwa ya kiroho yaani kupungikiwa kwa imani ya mmoja katika dini yake ndiyo chimbuko hasa. Mengine ni kupungikiwa na nguvu za kiume au ugonjwa na kutomridhisha mwenzako. Kuchoka kwa mmoja kutokana na kazi na majukumu mengi aliyonayo. Kwa mfano mke huonekana amechakaa na kujiachia kutokana na kutingwa na kazi nyingi. Sababu zingine zinazochochea kuwepo kwa uzinzi ni pale mke anapokuwa jeuri asiye mcheshi. Kutumia madawa ya kulevya yenye kusisimua hubadilisha pia tabia ya mtumiaji. Kutengana kwa muda mrefu kimasomo na kikazi pamoja na umbea na uchochezi wa ndugu na marafiki navyo huchangia tabia ya uzinzi.

Lakini tukumbuke Mungu ameamuru “usizini” hivyo jaribuni kuziba nyufa ndogo ndogo za nyumba yenu. Ukiona makosa madogo madogo yanayojitokeza na mwenzako akakwambia ‘Mimi sifurahii jambo hili’ basi jitahidi ulimalize haraka iwezekanavyo. Mfano mke akizoea tabia ya kugombeza ndugu za mume bila sababu na kuwanyanyasa ni vyema mkae pamoja na kujadili, kuliko mwanamume afikie hatua ya kwenda kuoa mwanamke mwingine.

Kutoafikiana na uzazi na kulazimisha mume kuwa na watoto wengi, au mke kutakiwa kuzaa watoto wengi na mume au familia ya mume ni moja wapo ya mambo yanayoathiri ndoa. Kutoa siri za nyumbani kwa ndugu, marafiki au mtu ye yote ni jambo baya sana. Na pia wakwe ambao si wema wana tabia ya kutoa amri, “Fukuza huyu mke hakufai,” au “Huyu Bwana ni masikini sana mwache!” Usafi ni muhimu nyumbani, na wanawake wajifunze mapishi kuzipendeza familia zao na kulinda afya pia. Tukumbuke Bwana Asipoilinda nyumba, yeye ailindaye afanya kazi bure.

Ili kuimarisha nyumba yako yabidi ufanye mambo yafuatayo. Usikae na wazazi wako baada ya kuoa au kuolewa, na hata ndugu wengine wanakuwa kipingamizi cha ndoa yako. Si siri, ndugu wengi wameharibu ndoa za watu na hasa ulimwengu wa talaka nyingi. Inasaidia kueneza udhaifu wenu kwa watu wengine na kufanya gundi ya kuwa mwili mmoja isiwe na nguvu “Upendo husitiri wingi wa dhambi.” Onyesha dalili za kupenda mwenzi wako kama ulivyokuwa ukifanya wakati wa uchumba, na nyumba yako itakuwa na furaha ya kudumu. Usitosheke sasa kwamba umemkimbiza na kumweka kikapuni ukamsahau! Jikumbushe mambo yaliyokuvutia mpaka ukampenda.

Usianzishe mazungumzo kwa kufoka na lawama. Shaurianeni, na pendeni kufuatana pamoja kama vile mlivyofanya wakati wa uchumba. Heshimu nafasi ya mwenzako na mwombe Mungu akuongezee mapenzi kwa mwenzi wako. Mama utambue nafasi ya mumeo kama kiongozi, haidhuru ana elimu ya kiasi gani “mume ni kichwa cha mke.” Naye mume asimpe msaidizi wake majukumu mengi kiasi cha kumfanya awe mvivu. Inasemekana katika bara la Afrika, 90% ya shuguli za kilimo hufanywa na wanawake. Na kwa vile sasa tuna asilimia 70-80 ya wanawake waumini duniani, na wanaume wengi kutoshiriki kazi ya ukuhani wakiwaachia kazi hiyo wake zao, hata pengine wanaume

hawajibidishi kimaendeleo ila wanataka wategemee wake zao kwa kipato, inafanya mke kufanya wajibu ambao hakupewa na Mungu awali.

Ilikuwa mke akae na watoto na kupika nyumbani; na kuitunza familia. Mama alikuwa si wa kubeba mizigo mizito. Kila mmoja amshukuru mwenzake katika nafasi yake. Kila mtu aelewe majukumu yake katika ndoa. Ninyi ni mwili mmoja. Goli likifungwa na mguu, uso wa mtu ndio unapigwa picha ila mguu haulalamiki! Mwanamume endelea na utanashati, mipango, upole na utaratibu, na kuipatia familia yako mavazi, malazi na chakula. Mke itunze nyumba, choo, bafu na jiko lako vizuri. Jifunze mapishi usiwe msusaji. "Upendo hauhesabu mabaya." Jifunze upole; usimkosoe, usimtawale, usimlazimishe au kujaribu kumtengeneza mwenzako. Ni Mungu tu awezaye kuleta mabadiliko hivyo mwombee mtu huyo. Uwe mtu wa kiasi katika kila jambo. Kutenda mabaya kuwe mwiko na kutenda mazuri kufanywe kwa kiasi. Mfano ni mazoezi, kula chakula, tendo la ndoa n.k. (1 Wakorintho 7:5, na 1Wakorintho 9:25). Shetani ameleta mafundisho mengi potofu ya tendo la ndoa. Tendo la ndoa ni takatifu, na siyo dhambi ya kwanza ya Adam na Hawa.

Dhambi ya kwanza ilikuwa chakula ambacho kilihusu utii wa sheria zote za Mungu. Tendo la ndoa si tendo chafu au la anasa mbaya. Si jambo la aibu. Muwe na maongezi yenye mahusiano mema ili kila mmoja atake kushiriki tendo la ndoa. Muwe wachangamfu, wenye kujali mambo ya usafi. Mazingira yawe mazuri. Wengi wana chumba kimoja na sauti zao zasikika vyumba vingine hata kwa watoto. Jaribuni kuwa na faragha, huku mkichunga hisia zenu kutozimwa. Na matatizo yaletayo huzuni kama kukosa kazi yatokeapo, ni vyema mjaribu kuchangamshana mioyo yenu. Msiongezeane matatizo kwa kulaumiana na kudharauliana. Kila mtu ajirekebishe kwa dosari ndogo ndogo alizonazo.
Muwe pamoja katika kuadilisha watoto. Ukishikwa na hasira hebu hesabu namba moja hadi kumi nawe utaona hasira yako ikiyeyuka! Msigombane na kuonyesha tofauti zenu mbele ya watoto ili kusaidia kutunza nidhamu yao. Zungumzeni peke yenu. Muwe kitu kimoja katika kuadilisha watoto ili watoto wasiwachezee.

Sura ya 14
TALAKA NA MATOKEO YAKE

Katika dunia tunayoishi talaka imekuwa zaidi ya 50% ya ndoa zote. Hili ni jambo la kusikitisha sana. Wale wanaomwamini Mungu wameonekana kupunguza idadi ya talaka hasa kama wanasali pamoja kila siku, asubuhi na jioni. Ninaposema kusali, hizi si sala za kukariri, bali ni sala zenye kugusa mahitaji muhimu na mambo yanayotoka moyoni, ambayo tunamwambia Mungu. Utafiti wa Marekani wa miaka ya 80 uligundua kwa wale wanaosali pamoja na kwenda ibadani ni ndoa moja tu kati ya 1,050 hutengana! Talaka ulikuwa si mpango wa Mungu, ilikuja kwa ajili ya dhambi. Na hata hivyo kuna nafasi ya kusameheana.

Katika ndoa za kiafrika hapakuwa na mwanya wa talaka kabisa. Jambo hili lilikuwa zuri mara nyingi, úseme ubaya ulikuja mara chache pale yule aliyeolewa au kuoa mtu mkatili alipata shida hadi kifo. Nafikiri hili ndilo lililosababisha ndoa kuitwa pingu ya maisha. Siku hizi unakuta mtu anasema, "Naenda kwetu, naweza kuendelea na maisha bila wewe," hata kwa makosa madogo madogo tu! Upendo umepungua sana.

Kabila fulani la kiafrika walinyoa nywele chache za mke na mume wakazichanganya. Siku ya arusi zililetwa na mke na mume waliulizwa, "Je, waweza kuchambua nywele zako tu uzitoe?" Wanaposema hawawezi kuzijua, wanajibiwa na viongozi wa jamii, "Kama mmeshindwa kuzitenganisha nywele zenu, hivyo hivyo msitengane milele." Katika makabila mengi watoto walikuwa mali ya baba, na hiyo ikawa njia ya kumfanya mwanamke kuvumilia akae kwenye ndoa, kwa kuwa hakuna mwanamke ambaye angewaacha watoto wake wakiteseka, hasa wale wadogo.

Kuna talaka chache sana ambazo haziwezi kuzuilika. Hebu kwa wale ambao hawajaoa au kuolewa watumie muda mwingi kuombea ndoa zao kuliko michango na sherehe kubwa kubwa za maonyesho ya uzuri, pesa na mavazi. Siku hizi watu huweza kufanya sherehe hadi tatu kwa arusi moja.Wengi wetu tuna jamaa waliopata talaka na tumeshuhudia matokeo yake katika kulea watoto na jamii nzima. Cha ajabu ni kwamba kabla ya kuvunjika kwa ndoa hizo wanandoa walifikiri si muhimu kuishi katika ndoa. Baada ya kukaa kidogo tu waliingia tena katika ndoa nyingine. Hii inatoa fundisho kuwa ndoa ni kitu muhimu. Watafiti husema kwamba ndoa ya kwanza ina hatari ya kuvunjika kwa 50%, wakati ile ya pili ina hatari ya kuvunjika kwa 70%, na ya tatu ina hatari ya kuvunjika kwa 90%.

Si kweli kwamba mtu fulani atakuwa mwema sana kuliko yule uliye naye. Mvumilie yule unayeishi naye kwa kuwa hakuna aliye mwema hata wewe mwenyewe si mwema ni vile tu yule unayeishi naye pia anakuvumilia. Zimwi likujualo halikuli likakwisha. Mke na mume siku hizi wana mahangaiko mengi sana kiasi kwamba hawali mlo hata mmoja kwa siku wakiwa pamoja. Kila mmoja huamka na ajenda zake na kufanya shughuli zake bila kumshirikisha mwenzake. Hakuna anayeichunguza na kuijali ndoa yake. Endapo wote wanandoa tungeamka asubuhi na kuomba pamoja maombi ya dhati, tukijua BABA yetu wa mbinguni anashugulika na magumu yetu yote na kwamba mwenzi wangu ni mtu wa thamani na tukienda kulala usiku tukaomba pamoja kwa dhati na kusoma NENO la MUNGU tungeepuka talaka nyingi. Wakina mama wale ambao wana hekima toka kwa MUNGU hawaoni kwamba kusoma kwao au kuwa na kibarua ni sababu ya kuhamaki upesi na kutelekeza ndoa, maana kuna mengi ya wanaume kama ulevi na vimada au kutojali nyumba ambako kumefanya wengi wafikiri waume zao hawawapendi kama vile Masihi anavyolipenda kanisa.

Talaka ni aibu kwa watu wanaompenda Mungu. Dhamira inakuwa ina dosari na kumshtaki mtu "Ningefanya hivi pengine nisingepata talaka." Zamani mtu aliyeachwa au kuachika asingechaguliwa kwenye shughuli za jamii kama Raisi au Mchungaji n.k. Siku hizi tunazidi kurudi Misri. Italia, kwa muda mrefu ilikuwa na sheria ya kutokuwa na talaka. Watu milioni kumi na sita, walitoa talaka mara baada ya sheria kuvunjwa! Kwenye hali mbaya na ngumu sheria za talaka zaweza kumlinda mke na watoto. Hatuwashutumu waliopata talaka ila, katika kitabu hiki tunajadili mambo ya talaka, na ni vizuri jumuiya ione jinsi ya kusuluhisha watu waliotengana badala ya kuwaongezea magomvi.

Talaka husababisha shida nyingi kwa watoto pia, mbali na kuleta matatizo kwa jumuiya. Watoto wanajiona kana kwamba wamepungukiwa, wakijilinganisha na wenzao walio na wazazi wawili. Kaka yangu na mke wake walipoachana, watoto wao waliokuwa kwenye rika la kubalehe waliumia sana. Kijana wao mkubwa alisema, “Shangazi, ningekuwa na njia ya kufahamu kama nikioa nitaachana na mke wangu, nisingeoa. Ni afadhali mke wangu afe, kuliko tuachane!” Watoto wa wale waliochana wana hatari kubwa ya wao kuachana. Na watoto wanaolelewa na mzazi mmoja hukosa upendo wa mzazi mwingine. Watoto pia hujiona duni, hukosa kujithamini na kujikuta kwenye umasikini uliokithiri. Watoto wanaogopa kuolewa, au huingilia vitendo vya uasherati au uzinzi. Maendeleo ya darasani na hata ya kiafya huwa si mazuri. Talaka inaumiza moyo sana, ni kama msiba ambao hauna mazishi na hiyo hukuza chuki baina ya wawili. Huweza kufikia hatua ya kujibizana na kutupiana matusi na kukaribisha maisha yasiyo safi.

Niliona mume mmoja akileta mtoto kwa mama mmoja (nadhani yule mume baada ya kuachana, alikaa na mtoto mwisho wa juma na mama alikaa naye katikati ya jana.) Wakiwa kwenye kituo kimoja cha mafuta, yule mume alimsukumia yule mke mtoto na kumtemea mate usoni! Mume huyu kabla ya kuoana, aliwahi kusema hawezi kuishi bila huyu mama, ila sasa baada ya talaka mambo yamekuwa ya kuvunjiana heshima na kukosa utu. Wengine husema tumeshindwa kuelewana. Kila mtu alikuwa amegangamaa kufuata njia zake, akidai ana haki ya kuwa na furaha, na bado waliamini kuwa wangeendelea kuwa marafiki. Hakuna urafiki wa maana baada ya talaka, ni uongo tu. Wengine huendelea kulala pamoja, jambo ambalo laleta picha mbili. Kwa talaka omba Mungu msamaha; usitoe udhuru! Na jaribu kutatua tatizo lako la ndoa kabla hujarukia ndoa nyingine na kumpa huzuni mwingine. Wale wampendao Mungu wajaribu kusaidia.

Injili ya Mathayo 5:31-32 inasema; “Kila atakayempa mke wake talaka.....amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini.” Pia angalia Mathayo 19:3-12. Katika Malaki 2, Mungu ansasema anachukia talaka.

Kwangu mimi kuzungumzia msimamo wa talaka kwa wote wanaompenda Mungu itakuwa kitendawili kigumu; kwani kila mtu ametoka na maoni yake. Baada ya kusoma Neno la Mungu kwenye kulea tunataka jambo la kusaidia watoto na siyo kushutumu. Watu wengine husema talaka ni dhambi isiyosameheka; Hili si kweli ni dhambi inayosameheka. Najua wote tumefanya dhambi 1Yohana 1:8-9. Talaka ni dhambi inayohitaji wawili kujifunga. Kuna talaka nadra sana ambazo kuna mmoja hana kosa! Kutokuwa na hatia si silika ya binadamu (Innocence is not human virtue). Hatuko hapa kusonda vidole kwamba nani ndiyo mkosaji. Wale waliojiweka kwenye talaka waungame dhambi zao na kuanza upya. Watu waweza kutengana kwa muda tu, na kujaribu kupatanishwa. Katika muda wa kutengana mume au mke asiingie kwenye mahusiano mengine. Viongozi wa kiroho wasaidie kusuluhisha; ili watu wasiende kwa watu wa dunia kupata mawazo yasiyo sahihi. Marafiki na ndugu wasaidie maana huu ni wakati wa huzuni kama kwa yule aliyefiwa. Wenye wivu si wakati wa kusema sema maneno; “Angalia walijidai wanapendana, afadhali wawe kama sisi;” n.k.

Hebu usifanye watoto na ndugu zako wamkasirikie yule mwenzi wako wa zamani kwa kufunua mambo yake ya kweli na yasiyo ya kweli ili wakuonee huruma. Usifanye watoto wawe upande huu au ule. Wao wenyewe wataona ukweli. Hata hivyo tabia ya watoto inakuwa mbaya kama wataanza kumtukana na kumlaani mzazi wao hata

kama ni mbaya. Usiwape talaka watoto wako pia. Wazazi wengine baada ya kuachana wanatelekeza watoto kabisa. Baba mmoja Polisi pale Morogoro alitelekeza watoto wake watatu na mke na kukaa akitunza watoto saba wa mwanamke mwingine! Unapopata usaidizi wa wazazi au jamaa kutunza watoto hebu uwe na shukuruni na uondoe hasira wala usianze kugombana na watu wengine na huku watoto wakishuhudia.

Tatizo jingine ni jinsi ya kulea au kutunza watoto katika ndoa nyingine, hasa kwa wale wanaoamua kuoa au kuolewa tena.Utakuta mwanamke amekuja na watoto wake, mwanamume na wake na kisha wale wenzi wapya wakazaa watoto wengine pamoja. Jaribu kuwa na mawasiliano mazuri mkitatua matatizo pamoja kwani sasa hali ni ngumu kuliko awali. Mna seti tatu za watoto ambao watakuwa changamoto kubwa kuliko awali. Isitoshe kila mtu ana vifurushi vya hisia fulani toka alikotoka. Huu si wakati wa kumlinganisha huyu mwenzi na yule wa zamani.

Kuna mambo mengi yanayofanya nyumba zivunjike. Jambo kuu katika yote ni shetani mwenyewe ndiye mfalme anayeleta shida zote na maumivu. Mengine ni kiburi, pesa , wazazi au ndugu, kutoa siri za familia, kutokuwa mwaminifu, hasira, kutokuwa na mawasiliano mazuri, kazi na marafiki, kupigana, kujamiiana watu wa familia moja, na kutojaliana.

Kwa kuwa ndoa ni muungano wa maisha, pateni ushauri kutoka kwa mwenye hekima anayempenda Mungu. Jaribuni kutunza ndoa na kusameheana na kuanza upya kuposana, kuomba pamoja na kujaliana. La ikiwa haiwezekani, mwangalie mambo yenu yasiingie na kuharibu matunzo mema ya watoto. Mara nyingi dhamira zinapowashitaki na kuwa na mioyo mizito, izueni hali hiyo isipite ikaenda kwa watoto. Zungumzeni na watoto kabla ya talaka. Wajulisheni kuwa wao si sababu ya ninyi kuachana. Waambie upendo wenu kwao hautabadilika. Watoto wanahitaji usalama na uhakika wa maisha. Usifanye watoto wawe upande wako au wa mke/mume wako. Waache watoto waende kumwona baba/mama yao mara kwa mara. Zungumza na walimu kujua maendeleo ya shule.

Watoto huathiriwa kiuchumi, kihisia, kisaikolojia na kisheria. Watoto wanaweza wasionyeshe hisia zao, lakini ndani ya mioyo wamepondeka. Watoto sasa wanaona wakigawanywa huku au kule. Wanaweza kuwa na tabia tofauti kama kupinga mamlaka, kunyanyasa wanafunzi wengine (bullying), kukacha shule, kuingia ulevini, uvutaji wa sigara au ngono haramu. Usianze kufanya mahusiano ya watu wa jinsia nyingine na kuwaleta ovyo ovyo nyumbani. Hii napunguza tabia njema na kuleta msongo kwa watoto. Watoto wenu pia wanaweza wakaogopa kuoa au kuolewa kutokana na jinsi kidonda kinavyokuwa. Hii ni nukuu kutoka kwa Mchungaji Festus Njagi 2004, Joedor Enterprise, Nairobi

Jinsi ya kuzuia talaka ni kujikita kwa Mungu. Lazima kujitoa kikamilifu katika maisha ya ndoa, waombe, waabudu na kusali pamoja. Wajifunze kusameheana, wajifunze mawasiliano mema; wapate muda wa pamoja kuzungumza mara kwa mara; wafanye kazi kama timu moja na mwili mmoja. Wote wajue kwamba ni dhambi kutotafuta kuishi kwa amani na kutatua matatizo; wajue kwamba kuishi na watu ni kazi, hata wazazi! Muwe na washauri wazuri wenye hekima, wasome na kwenda semina za ndoa.

Nilipata semina ya 'couple prayer' au maombi ya mke na mume. Ni huduma nzuri. Walifanya utafiti wakaona kwamba ndoa moja kati ya mbili huvunjika. Ila wakienda ibadani mara moja kwa juma na kuomba pamoja siku hiyo, ndoa moja kati ya sita inavunjika. Wakaona tena endapo mtu na mke wake wanasali pamoja asubuhi na jioni kila siku, ndoa moja kati ya 1,050 huvunjika! Siko hapa kusema siri, nafikiri wengi wetu tuna mapambano ya aina fulani katika ndoa zetu. Wanasema kwamba ni asilimia ishirini tu ya ndoa ambazo watu huishi kwa furaha. Wengi wanaishi ishi tu. Hii ni kwa mahusiano yote, yawe ya mzazi na mtoto, dada na kaka. Mahusiano mengi yamepasuka! Twahitaji maombi mazito.

Sura ya 15
MABABU NA MABIBI AU WALEZI WENGINE

Ni manufaa kuwashirikisha bibi na babu kwenye maisha ya mtoto. Babu na bibi wengi wana upendo, ukarimu na ucheshi kwa watoto. Wana hekima na uzoefu unaosaidia mawasiliano na makuzi ya watoto zaidi ya sisi wazazi. Siku hizi, wengine wanaishi mbali na babu na bibi ila wakiwa karibu watembelee na wafanye watoto wawe na mahusiano ya karibu kwao. Babu na bibi wana hadithi na wosia ambazo zina mafundisho kwa watoto. Mara zingine waweza kukusaidia kukaa na watoto kwa muda mfupi. Hiyo inafanya hata wao wajisikie wana umuhimu katika maisha ya wajukuu wao. Kukitokea talaka wazazi waendelee kuhusiana na babu/bibi za watoto. Waache wakusaidie katika hekima na mashauri ya kulea. Waeleze yale ambayo unataka kuyafunza kwa watoto ambayo wewe wayaona ya thamani ili wakusaidie. Na kama wao wenyewe hawajui mengine katika hizo nyanja mwaweza kutafuta na wengine wa kuwasaidia.

Najua kuna wengine wana shida na wazazi ambao ndoa zao zimevunjika toka udogo. Kwa hilo nasema mwombe Mungu akupe hekima. Hali ya msongo imefanya mabibi na mababu waingie ugomvi wa pesa na watoto wao. Mawasiliano yanakuwa mabaya na hata watoto wanagundua. Hili nimelikuta sehemu nyingi, watoto wenye uwezo wasiojali wazazi wao wazee, na wazee wenye tamaa wasioridhika watoto wakiwasaidia. Alimradi wanataka kuwaendesha watoto ambao wamehamia miji yao na kuharibu mahusiano na mkwe/mkamwana . Yule ambaye anagundua kwamba hahitaji ugomvi au ana mwamko wa kiroho, ajaribu kusuluhisha kwa kufanya haki zinazotakiwa, na ikishindikana ajaribu kuepuka magomvi, hasa kwa kukaa mbali kidogo na vyanzo vya ugomvi.

Si vizuri kugombana na wazazi wako, mtoto wako hapati mfano bora, hata kama wazazi wako ni wagomvi jaribu kuwapa mwanya. Mwenye nguvu akiwa hana wa kugombana naye mwishowe atachoka. Kimbia, si waoga tu wakimbiao. Yusufu alikuwa

mtoto mnyonge, akakimbia alipovuliwa nguo, akawa mshindi. Samsoni alikuwa shujaa, mwenye nguo zake na awezaye kumchapa mwanamke anayemjia kumposa (seduce) ila alianguka kwa kishindo kikubwa.

Mababu na mabibi wengine wamekuwa na upendeleo wakichangamkia au kuzawadia wajukuu wao wa mtoto fulani (hasa wa msichana) na kutojali wengine kabisa. Hii si hekima, ila huwezi kulazimisha upendo wa mtu fulani, unaweza tu ukashauri, pengine kile wanachokifanya hawatambui kwamba wanakifanya, kama wanatambua usiongeze shida. Chukuliana na jinsi ilivyo.

Ni vyema mababu na mabibi waendeshane na yale wazazi wanayoyathamini. Mfano ukipeleka watoto ambao hawali nguruwe, keki au peremende, ukiwapeleka kwa bibi/babu; je, wataheshimu maadili yako haya? Au kama unapenda watoto wako wasome neno la Mungu kila siku na babu/bibi wanapinga ufanyeje ili msiwe na ugomvi ila usaidie watoto wako? Ila usisite kuwaambia kabla hujawapeleka, ili mkubaliane vizuri.

Allergy (mzio) na historia ya afya ya mtoto ielezwe, kwa mababu, bibi, yaya, ndugu au shule. Usifikiri kwa vile ni ndugu wanajua. Mfano, mtoto akila mayai au maziwa, anakuwa na shida. Kijana fulani alikula ufuta toka kwa rafiki yake shuleni na alikufa kwa mzio.

Mayaya: Kwa vile kina mama wangi waenda vibaruani mayaya wamekuwa sehemu ya walezi wa watoto. Mara nyingi wazazi hawaangalii ni yaya gani wanachukua, wengi wakiona anaweza kazi za nyumbani basi wanachukulia anaweza kulea mtoto. Ni vizuri kuwa na elimu fulani unayoitoa na kuiandika kwa yaya ili aweze kukusaidia vizuri katika jukumu hili. Yeye pia ni mwalimu wa mtoto wako. Atamfundisha mtoto wako unayopenda na usiyopenda na hivyo weka silabasi ya mtoto wako. Mfundishe kuhusu afya ya mtoto pia, mfano, akiwa na joto au akiugua afanyeje.

Watu wengi siku hizi wameanza kufundisha mayaya huduma ya kwanza, mfano akijikata au akizimia ufanyeje, nafikiri hili ni jambo zuri pia. Wahitaji yaya mwenye maadili na adabu njema maana akiwa na adabu mbaya itajiakisi kwa mtoto, maana yeye ana muda na mtoto zaidi yako. Usifikiri ukiwa na yaya sasa umejitoa kwenye shughuli ya uzazi. Mara nyingi wewe unajua mambo ya uzazi au ulezi kuliko yeye na hasa akiwa msichana mdogo. Hata hivyo ana uchungu gani na mtoto kuliko wewe? Kama unaweza, kaa nyumbani utunze mtoto mpaka afikishe miaka minane ndiyo uende kutafuta kibarua. Watoto wengi wanapata faida ya kufundishwa na mzazi nje ya darasa mpaka wafike miaka minane au hata kumi; hasa wa kiume.

Mitihani ya taifa na jinsi maksi zinavyotolewa mara nyingi haviwasaidii watoto wadogo, na hasa wa kiume mpaka wafikie miaka minane au kumi hivi. Hili wataalamu wengi wa saikolojia ya kujifunza wameligundua. Soma waandishi kama Drs Moore – kwenye kitabu chake cha 'Home Grown Kids'. Watoto wengi walionza shule baadaye kama miaka 8-10 walionekana kufanya vizuri darasani hasa kama walichukua muda kukaa nyumbani na kujifunza kazi.

Kazi inakuza ubongo hata zaidi ya taaluma, hata hivyo watoto wanasoma ili waje wapate vibarua. Watoto wadogo wanaokaa darasani siku nzima wapo katika hatari ya

kupata magonjwa ya wasiwasi, kukata tamaa (sonona) na kuwa na nidhamu yenye shida zaidi. Watoto wadogo walikuwa zamani wakikaa darasani masaa mawili au matatu; tu ila siku hizi kwa ajili ya kina mama wengi kujiunga na shule imefanya waongeze haya masaa.

Chagua yaya vizuri. Pengine peleleza tabia ya zaidi ya mtoto mmoja na kisha ufanye ulingano ni nani anayekufaa. Waambie watoto wako umemleta mtu wa kuja kukusaidia siyo inatokea tu wameamka asubuhi nawe ukiwa kazini wanaona mtu mgeni nyumbani. Kwa watoto wadogo hii inaleta hofu. Mwonyeshe nyumba na hatari zake, na pia mwambie milango ni vizuri ifungwe wakati wote. Mpe sheria za watoto na umwandikie taratibu zote mfano wakati wa kulala, wakati wa kula, hakuna kupiga makelele, kuruka kwenye viti, hakuna kufungua runinga mpaka wamalize kazi za shule au kwa kipindi maalum tu.

Kaa na yaya umweleze mambo ya kuwafundisha watoto, kama ni kazi waambie watoto cha kufanya na yaya afuatilie. Weka chati kwenye ukuta baada ya kuwafundisha watoto zile kazi ili wazifanye vizuri. Watoto na wasaidizi wa kazi wanajenga kujithamini wakifanya kazi vizuri kwa mwongozo fulani. Wanaona nao waweza kusaidia na hata kutoa huduma.
Usipende kufoka kwa yaya na kumgombeza mbele ya watoto. Mchukue kando na mweleze jinsi ya kufanya kwa ubora. Mpe heshima na mwonyeshe unamweshimu mbele ya watoto. Mweleze mategemeo yake katika kazi mfano unategemea apike namna gani, kwa muda gani, nguo zifuliwe siku gani, unga usagwe namna gani, na jinsi ya kununua bidhaa zinazotakiwa nyumbani mfano chakula cha kuku n.k.

Usionyeshe kutoridhika kila mara (perfectionist) hata kwa kitu kilichofanywa vizuri, mtie moyo kwa kujifunza. Watu wengi walipata mayaya wadogo kwa umri toka kijijini wamewafundisha mpaka wameweza kumudu nyumba kubwa na kuwa watu wa kusaidia jamii hizo. Inapowezekana mzawadie hata kama ni kitu kidogo kama nguo n.k. Kila mtu anapenda kupendwa na kutiwa moyo aendelee na mambo mazuri. Ikiwezekana msaidie kazi na majukumu mengine unapopata nafasi. Hii itasaidia kuwafundisha wasichana, kwamba hata mama anafanya kazi. Baadaye wakiwa wakubwa nao watafanya kazi kwenye nyumba zao.

Mwambie yaya kwamba watoto wanapaswa wamtii na wasipomtii akueleze. Mtoto ye yote asipomtii mtu mzima anayemlea, hata wewe mzazi utakuwa namba mbili kutoheshimiwa kama yaya! Na Mungu atakuwa Namba tatu katika orodha ya kutoheshimiwa. Ni vizuri yaya na watoto wawe na vitabu vya kusoma pia. Mwonyeshe chakula cha kupika na wakati wa kukipika na kula. Niliona watu wanakula ugali na viazi, bila mboga ya majani! Lishe ni somo pana, jifunze na watu wa ndani ya nyumba yako.

Watu wengine hawawapi wafanyakazi wa ndani chakula au wanawapa chakula duni tofauti na watoto wao; au kuwatendea pungufu. Watoto wako wataiga haya yote na kuwafanyia wengine mambo haya. Yaya mmoja kule Moshi alihesabiwa punje za maharage na mahindi kama watu wa Korea ya kaskazini walivyofanyiwa (vyombo vya habari vilisema)!

Mweleze yaya yeye ni wa muhimu na anachukua sehemu ya wazazi akiwa na watoto. Watoto ni watoto na si watu wazima; na watoto wengi wanapenda watu

wanaocheza nao, wanaozungumza nao, wanaowasikiliza, na wanaowaita kwa majina yao. Hata wakiweza kuwasomea au kuwasimulia hadithi na kuwapongeza au kuwatia moyo, wanafurahia sana.

Watoto hulilia wazazi wakitoka ila baada ya dakika chache hunyamaza. Mayaya wengi wamekuwa msaada. Kumbuka kuna mayaya wenye tabia nzuri wanaompenda Mungu kuliko hata wazazi! Ukipata hao una dhahabu, ila nawe ujifunze kuwa na mvuto mwema na kumpenda Mungu! Wazazi; kwa sababu watoto ni kitu cha thamani kwako, chagua vizuri yaya anayewalea na pia wafanyie mema kwa utukufu wa Mwenyezi Mungu na ili usiwakwaze wakufanyie mabaya kwa kulipiza kisasi.

Sura ya 16
KUWEKA VIWANGO KWENYE FAMILIA (Setting family values).

Kulea mtoto ni zaidi ya kumpa chakula mavazi na mahali pa kulala.
Ikiwa mtoto wa miaka mitatu amekuja na kalamu ya wizi, nyumbani utachukua hatua gani? Yapasa mtoto aulizwe; “Ni nani amekupa kalamu hii nzuri?” Mzazi anapouliza anaonyesha kwamba hakufurahia mtoto kuwa na kitu ambacho siyo chake. Mtoto akijibu kwamba alichukua kwa mwenzake na haikujulikana, mzazi anapaswa kuwa mpole, si kuvuta kalamu na kuanza kugomba. Hii itafanya fundisho lisiweze kuwa kamili au mtoto aogope kukwambia yale ambayo yatakusaidia wewe kama mzazi kumwongoza vyema.

Mzazi ajaribu kuepuka hili kosa ili mtoto wake ajenge kujiamini ili amweleze mzazi kitu bila ya kudanganya au kuficha mambo. Hii ni nafasi nzuri kwa mzazi kuelezea maadili ya thamani kwa mtoto. Mzazi anapaswa kueleza kwamba uaminifu (honesty) ni muhimu sana na ni mojawapo ya vitu vya thamani kwa familia. Achukue muda na kumwelewesha mtoto vizuri, maana nyumbani ni darasa kila siku. Mzazi aweza kusema japo yule mwenzake alikuwa na vingi, Je, angesikiaje kama mtu amechukua na vikapungua? Je, anaweza kuomba badala ya kuchukua bila ruhusa? Je yeye angefurahi kama mtu angemchukulia kitu chake mfano mwanasesere?

Familia zote zina maadili ya namna fulani kutokana na kumjua Mungu na sheria za nchi. Hizi zafanya mfumo wa maisha ya kila siku. Mzazi anayempenda Mungu na kufuata kanuni za maadili mema ni lazima amsaidie mtoto kuyajua maadili haya. Mtoto anapoapa na kutumia jina la Mungu “haki ya Mungu” au kuzungumza matusi, akanywe. Aambiwe “maneno kama haya si ya kutumia, singependa kukusikia ukiyasema tena. Ni maneno mabaya kutamka, nyumbani au familia yetu hapa hatutumii maneno haya.” Mtoto akipenda kusema uongo, kupigana au kuharibu vitu aambiwe. Kwa njia ya mambo ya kila siku (informal), mtoto atajifunza kanuni na tabia za thamani za adabu njema.

Itikadi (values) zinatokana na desturi, mila, imani, vyombo vya habari, au mahusiano na watu. Wazazi jaribuni kuyarithisha maadili kwa kufundisha kwa njia mbali mbali. Wazazi msichoke, hata mkiona matunda ya kazi yenu hayaonekani papo hapo. Mwenyezi Mungu ni Mwaminifu, Amesahidi: “Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee.”

Ni kweli mara nyingine watoto wanatoka nje ya mstari, ila mara nyingi wanakumbuka na kujirudi. Maadili au tabia za thamani, watoto hawapati nyumbani tu bali shuleni, kwa jamii, na kanisani pia. Wataalamu wameona kwamba asilimia 40 ya maisha ya mtoto yanaathiriwa kutoka kwa mama, asilimia 20 toka kwa baba, asilimia 10% shuleni, asilimia 10% kanisani, asilimia 10% toka kwa mazingira anayoishi na asilimia 10% toka kwa mtoto mwenyewe.

Miaka mitatu ya kwanza ndiyo tabia ya mtoto inapojengeka, na akifikia miaka sita, tabia inakuwa imekamilika. Ila Mungu ni mwenye rehema, pamoja na kwamba tunakosea kama wazazi, tunaomba msamaha na kujifunza kusonga mbele kuwalea watoto wetu vyema. Kulea watoto mijini ni changamoto kubwa. "Utayaarishaji wa tabia ya mtoto mashambani ni bora mara kumi kuliko mjini." Hebu kama unaweza kuhamia mashambani na watoto wawe na kazi za mikono, kama kilimo fanya hivyo. Maisha mijini si halisi yana kujifanya kwingi. Wazazi wetu wa kwanza hawakuwekwa mijini ila bustanini.

Fanya mazingira ya nyumbani yawe rahisi, si yenye vitu vyenye gharama ndani ya nyumba kiasi cha kusahau kujenga tabia ya mtoto. Mtoto akiharibu kitu kidogo tu roho yako inaumia sana. Wakati huo huo watoto waone thamani ya nyumba nadhifu, tulivu, japo si ya gharama. Wapende vitu vya afya hata kama ni viti, mavazi au viatu kuliko kujionyesha. Maua na mapambo mengine, wema na upendo ni vya thamani zaidi kuliko anasa.

Jambo lingine ni vyombo vya habari. Mara nyingine watoto wetu wanapenda kufuatilizia jinsi watu wazima kwenye runinga au katika jumuiya wanavyofanya. Mfano mavazi au kusema uongo. Mara nyingi ule uongo unaoonekana kama si mbaya. Mtu akipiga simu, unamwambia mtoto aseme haupo, na wakati upo. Hii inamjenga mtoto kusema uongo bila kuogopa. Inaaminika kwamba mzazi akisema uongo, baada ya muda mtoto wako atakuzidi na kuwa fundi hodari wa uongo.

Tukumbuke pia watoto hawana mstari wa yaliyo halisi na yasiyo halisi. Akisema yeye ni zima moto anaamini kwa kiasi kikubwa. Hivyo tabia zozote mbaya ulizo nazo mtoto ataiga zaidi, kwa vile hajajenga hisia za kitu kamili. Hili nimeliona kwa tabia nyingi; mfano, kunywa pombe, watoto wanakuwa mabingwa na kuzidiwa kabisa na pombe kiasi hawawezi kumudu maisha kwa kufanya kazi au kujifunza ustadi fulani. Mzazi anapaswa mara zote kuwa mfano katika tabia za thamani au maadili yale ya thamani. Hatuwezi kusema hivi kwa watoto na kufanya vile. Tunapunguza nguvu za malezi bora. Najua tu binadamu na tunakosea sana tu ila nia yetu kwa uwezo wa Mola ni kufanya vizuri tuwezavyo, tukimwomba Mungu atujazie mapungufu tuliyo nayo.

Maadili mara nyingi hayaingii kwa mtoto kwa nguvu, au kwa adhabu kali kali. Mtoto anapaswa kuongozwa toka akiwa mdogo, kwa upendo, kwa mkazo na kwa mfano. Hii itamsaidia mtoto popote atakapoenda asiingie kwa kile kitachomdhuru. Familia zinatofautiana itikadi, mfano familia zingine zinaweza kutumia pesa kumnunulia mtoto mavazi mengi, na kumpeleka disko la watoto wakati familia nyingine ikatumia pesa kumnunulia mtoto vitabu vingi, na video za elimu, kalamu na penseli.

Napenda kurudia tena kwamba hakuna aliyefuzu na kusema kwamba yeye ndiyo bingwa wa kulea. Tunakosea kwa mengi na ndiyo maana ni muhimu kupata ushauri wa watu wenye uzoefu wa kusaidia kwa kusoma vitabu pia. Mzazi anapaswa kuwa msikilizaji mzuri mwenye uvumilivu. Ni wakati mzuri wa mzazi kujiuliza maadili yenye thamani kwake ni yapi. Inahitaji muda mwingi na mrefu. Inahitaji mzazi awe mdadisi, na awe na mipangilio ya kufuatilia. Hiyo ndiyo kazi ya mzazi. Ni vizuri kuwe na kikao cha familia na watoto na kutoa mawazo yao angalau mara mbili kwa mwezi. Kama wahenga wasemavyo: “Kulea mimba si kazi, kazi kulea mwana;” ni kweli kabisa! Mzazi anayetumia muda wake na moyo wake katika malezi, yawezekana atachukua muda mrefu; ila matunda ya kazi yake yataonekana. Ndiyo maana ni muhimu mzazi ajikabidhi kwa Mungu kila siku, akisoma Neno lake na vitabu vya matunzo ya watoto, akiomba kwa kicho na kumlilia Mungu mchana na usiku.

Tabia za thamani ni katika nyanja zote: Kiakili, kimaumbile, kiuchumi, kihisia, kisaikolojia, kiroho, na kijamii. Hii ndiyo dira ya mzazi. Mtoto atakua akipenda watu na Mungu. Ataweza kuhudumia watu na kuwa mwenye nia ya kusaidia na kujenga wengine. Atapenda haki na si rushwa au ubaguzi. Tunafahamu kwamba tunaishi duniani. Ufanye kazi hii kwa uangalifu, na kwa kuzungumza na mtoto, au hata kucheza na mtoto. Toa mifano unapopita na mtoto sehemu mbali mbali, hata mjadili magazeti na mazungumzo ya vyombo vya habari. Mfano kwa mtoto wa miaka kumi waweza kumwuliza; Je, ukipata Sh. laki moja utaigawanyaje? Nilijaribu kuuliza watoto wangu na nilipata majibu tofauti. Mmoja alisema nitanunua baiskeli, kisha nitakupa wewe elfu kumi, na watu masikini nitawasaidia na elfu kumi n.k. Uliza maswali ya namna hii kuona values za mtoto ni zipi?

Kwa Mkristo, amri za Mungu ni muhimu sana, mweleze mtoto.
Mweleze mtoto kwamba imani kwa Mungu wa mbinguni ni muhimu sana, kwamba tuko duniani kwa sababu gani, na tunaenda wapi. Tupo hapa baada ya kuanguka kwa mwanadamu katika bustani ya Edeni, na tunajitayarisha kwa maisha ya Milele. Ni muhimu kumweleza mtoto upendo wa Mungu tumia visa vya biblia: “Waacheni watoto wadogo waje kwangu wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa Mungu ni wao.” Na kwamba uzima wa milele ni kumjua Mungu; Yohana 17:3. hebu neno la Mungu liwe ndiyo nguzo; mtoto alione likithaminiwa na kusomwa kila siku. Maombi ya asubuhi na jioni yawe muhimu sana. Hata mzazi mmoja akiwa kibaruani hebu na aliyebaki aendelee.

Mtoto apewe mifano ya mashujaa waliofanya makubwa duniani na kubariki wengi kwa ajili ya kufuata uongozi wa Mola. Mfano Isaac Newton, mother Teresa, Mahatma Ghandi, Sulemani, Musa, Ibrahim, Yusufu na wengineo. Aelewe kuishi maisha ya kuhudumia na si ya umimi, mimi kama waingereza wanavyosema (me, myself, and I). Asiwe kisultani kidogo anayepiga yowe; “Nataka hiki na kile.” Akumbuke kwamba hata siku za usoni akiwa na uwezo, kutakuwa na watu wengi wenye mahitaji ya kusaidia na hata katika kazi ya kuendeleza kazi ya Mungu. Kumcha Bwana ni chanzo cha maarifa. Mtoto ni sehemu ya familia, athamini familia na asiishi kama mgeni nyumbani kwao. Pale si nyumbani kwake bali ni nyumbani kwao. Akisaidia kazi nyumbani asifikiri anafanya favor na anatakiwa alipwe! Akilipwa, ni fadhili na motisha tu.

Kwetu sisi waandishi, nyumba inayompenda Mungu ina mfano zaidi ya maneno ya kusema. maadili yake yatakuwa siyo ya kiungwana tu bali ya kuhuisha roho na

kuboresha jamii. Malaika wa Mungu watapenda kuwa hapo. “One well ordered disciplined family tells more on behalf of Christianity than all sermons that can be preached.” Ukarimu, upole, utu wema, kujaliana na upendo vitaonekana. Tunahitaji watoto wema zaidi ya watoto wenye akili nyingi! Hebu tuwe na ucheshi watoto wetu watuzoee kwa njia nzuri kuliko kutuogopa na kutuficha yale ambayo tungewasaidia.

Sura ya 17
WATOTO AMBAO NI WATU WAZIMA

Mara nyingi watoto wetu wakiwa wadogo na wanaonyesha ustadi, au uzuri wa aina fulani tunapenda kusema kwamba ni urithi toka kwetu. Wanapokuwa wakubwa na kufanya mambo ambayo hayatupendezi kama kunywa pombe, japo nasi ni wanywaji tunaona wanatuharibia jina la familia yetu.

Imetokea hali ambayo watoto ambao ni watu wazima bado wanaishi nyumbani kwa sababu mbali mbali. Waandishi wamechukua muda kuzungumza kwa sababu jambo hili limekuwa sugu katika jamii kuliko tunavyofikiri. Mtoto mtu mzima anakaa na wazazi kwa sababu mbalimbali: Kijana anatafuta kazi kwa muda mrefu, au amekosa kodi ya kupanga nyumba yake mwenyewe. Pia wazazi wakiwa na nyumba kubwa na uwezo kuliko mtoto. Watoto wa kike wasioolewa kuishi na mzazi ni salama zaidi na wengine pengine wameachana na wake au waume zao na wanategemea msaada wa wazazi wajikwamue kimaisha; au waweza kuja na mke au mume wake na watoto wao kusaidiwa kimaisha. Mtoto aweza kuwa akitegemea mzazi kwa muda mrefu na wakati mwingine kuzorotesha majukumu kwa kuendelea kuishi kitoto. Ila mamlaka na majukumu ni pacha. Mtoto aliye mtu mzima hawezi kuwa anataka mamlaka na haki kwenye nyumba ya wazazi wake bila yeyé mwenyewe kuwajibika.

Tumeona watoto walio watu wazima wakikaa nyumbani wakitegemea wazazi wawalishe, wawalipie simu zao za mkononi, wawafulie nguo zao, na kuwafagilia vyumba vyao! La kama si wao watumishi wa wazazi wao. Mara nyingine kizazi hiki kimekiuka kanuni za afya kama kutumia madawa ya kulevya, kula vyakula vya papo kwa papo kama chipsi, hivyo wameathirika na kushindwa kujitegemea na inabidi wauguzwe kwa shida zinazohusika na kutokuwa na afya au kiasi.

Haya yote tumeona kwenye michezo ya kuigiza ya radio au runinga. Ni mambo halisi na ni vyema kuyajadili kwa wale wanaotaka kuboresha mahusiano yao na watoto wao walio watu wazima. Ni vyema wajifunze kutoka kwa mifano mibaya mno na mizuri mno. Kukaa na kuficha ficha au kuzika kichwa chako kwenye mchanga kama mbuni ili usione shida zinazoendelea haitoi ufumbuzi. Pia usikae na kumezea mate mahusiano ya familia nyingine na kulinganisha watoto wako walio watu wazima na wengine. Mfano “Mtoto wa fulani anasaidia wazazi wake amewanunulia gari, na anawapa pesa kila mwezi;” au “Mtoto wa fulani hadoei wazazi wake kama wewe uliye mzigo hapa kwetu, wengine wana bahati kweli!”

Sentensi za kutamani vya wengine au kujilinganisha zitakuletea mzazi misongo tu na wala siyo ufumbuzi. Hata hivyo usionee wivu watu wengine waliochukua muda kulea watoto wao katika misingi mizuri na kutumia muda mwingi na watoto wao kujenga madaraja na urafiki wakati wewe ukiwa umemwachia jukumu hilo yaya, bweni au mashangazi kujenga mahusiano na mtoto wako. Pengine wenzako wamegundua njia za kufumbua matatizo yaliyowapata na kuweka muda ila wewe una haraka bila uvumilivu. Jaribu kumchukulia mtoto alivyo kuliko alivyokuwa "utundu wako huu toka utotoni, ulikuwa unafanya hivi, na hivi na hivi na tena unaendelea."

Mara nyingine watoto wetu wanakimbilia wengine wa makamo kutatua matatizo yao, kwa kutukimbia au wanaona utazidi kuwamiliki na kuwakumbusha yaliyopita ambayo wameona wamesamehewa na kumbe bado tunaleta mifupa ya kale. Jitahidi maneno yako yasiwe ya ugomvi ugomvi. Familia nyingi zimeshindwa kujifunza msamiati wa maneno matamu. Kila mara ni kutwangana makonde ya maneno au kubanguana. Wanaishi kama bisi sufuriani.

Kwa kawaida mzazi anampenda mtoto au mjukuu kuliko mtoto au mjukuu anavyompenda mzazi, hilo ni muhimu mzazi kuelewa anapohusika na mtoto aliye mtu mzima! Kwa desturi ya Kiafrika, mtoto mtu mzima kukaa nyumbani ilifanyika kwa nadra sana. Pengine ni kwa vile maisha ya mjini hayakuweko au maisha ya usomi wa muda mrefu. Hata hivyo watu walitegemea kilimo na ardhi ilikuwepo; na kila mtu alijenga nyumba yake akifikia umri fulani wa kupevuka. Jamii zilikuwa na sherehe za kuagana na mtoto akaishi kwenye ardhi yake aliyopewa.

Mara nyingi watoto watu wazima wakija nyumbani, sheria zao za kukaa nao ni ngumu zaidi. Maana wana mawazo yao tofauti na matakwa fulani. Mfano wataomba msaada (favour), ila hawatafuata kanuni zake: Kijana ataomba baiskeli ya baba au gari na kutaka kuirudisha katika wakati anaoutaka na bila petroli. Atakaa sebuleni na kusikiliza radio au runinga ambayo wazazi wanaona ni kero. Atatumia bafu kwa muda mrefu na huku mzazi anangoja kutumia aende kibaruani. Kila kizazi kinathamini vitu tofauti. Kukaa nyumba moja watu wa vizazi tofauti kuna kazi yake. Siku hizi kwa ajili ya maisha ya mijini hata vijijini kumezuka tabia ya babu/bibi kuishi kwa watoto wao watu wazima mijini ambao wana watoto watu wazima!

Vijijini hata kama hawakai nyumba moja, ila kile kizazi cha katikati (nitakiita B) ndicho chenye majukumu ya kuwabeba kizazi cha mababu na mabibi (nitakiita A) na cha watoto watu wazima (nitakiita C). Na wakati mwingine hawa watoto C wana watoto wao! Kwa hiyo ni vizazi vinne (nitakiita D). Kukaa vizazi tofauti kwenye nyumba moja ina mibaraka yake mingi na shida zake nyingi. Uzuri wake ni kama vile, kusaidiana kiuchumi kwa chakula mavazi au nyumba. Kusaidiana kulea watoto na mashauri ya kimaisha. Wengi wanaoishi hivi wanaoelewana wanafurahia sana mpango huu. Tumeona wenzetu wahindi katika biashara zao. Ila kuna kutesa wakamwana, n.k.

Mifano mingine, wale wa kizazi C huwasaidia kizazi B na teknolojia na mambo mengine ya kileo ya maendeleo, kitaaluma, na kijamii, wakati ambapo wale wa A wanasaidia wengine kwa nasaha, kulea watoto, na maneno ya busara yenye kutia moyo na uvumilivu. Mara nyingi wale wa kizazi B wanasaidia mambo ya kiuchumi. Ila mara

nyingine mkao huu unaleta fujo kwenye nyumba kama kila mtu anataka kuwa mwenye nyumba au bosi. Wale wa A wanapenda kuwaeleza wa B jinsi wajukuu wanavyopaswa kulelewa japo wao hawakuwalea vile. Wanataka kudekeza wajukuu au mawazo yao ya malezi yamebadilika kutokana na mafunzo.

Tofauti ya vinavyothaminiwa kwa vizazi hivi inaleta magomvi mengi. Mfano wale wa A walilea watoto wao kwa maadili mema na makini (strict) na watoto wao wakawa wanayamudu maisha vizuri, ilhali wanataka wale wa B walegeze kamba na kuharibu watoto wao wasijali kazi na maadili ya muhimu kwa binadamu.
Ikiwa wale wa A wana uwezo kimaisha waweza kuharibu nyumba za watoto na wajukuu yaani B na C na hata D! Kwa kweli watoto ambao ni watu wazima waweza kuona maadili ya wazazi ni ya kishamba na ya kizamani japo kuwa ni mazuri na ya kumcha Mungu.

Waandishi hawako hapa kukutatulia tatizo hili, bali kukueleza au kukujulisha kwamba matatizo haya yapo na kwamba wale wanaotafuta kuwa wapatanishi watagundua kwamba matatizo mengine hayawezi kutatuliwa ila watu wafundishwe kuishi na wengine kwa amani japo wana tofauti kubwa. Najua wazazi wanaona watoto wao ni vifaranga bado japo kuwa ni watu wazima. Na watoto bado wanaona wazazi wao ndiyo wa kuwasaidia katika kila jambo; liwe la kiuchumi au kijamii.

Siku hizi kwa vile uchumi unaendelea kubadilika, wazazi wengine wanaonekana wana hali bora kiuchumi kuliko watoto wao. Hii ni kwa sababu wakati wao, mishahara iliweza kufanya mambo makubwa au biashara zilikuwa bora kuliko wakati huu ambao kuna ushindani; kwa vile wengi wamesoma na hivyo hata kupata kazi ya maana ni vigumu. Jambo hili ni gumu wazazi kulipokea. Nakumbuka hata mzazi wangu aliniambia kwamba watoto wako wanapaswa kukuzidi kimaisha, kimashauri na nyanja zote! Kwa hiyo wazazi wakiona kwamba wao bado ndiyo wanategemewa hawawezi “Mpaka kifo kitutenganishe!” Mzigo huu waweza kuwa mzito kwenye mawazo ya mzazi.

Kizazi hiki chaweza kuonekana kwamba hakijui kutunza pesa na kila mara kinataka maisha ya kujionyesha, kudoea na kuingia katika madeni. Wanasema wao ni watu wazima watapanga jinsi ya kutumia pesa, kuwa na marafiki na mengineyo ila wanafanya makosa mengi na kurudi kwa wazazi kuwasaidia. Jambo hili laweza kuleta mvutano, hasa wanapopewa msaada na B na kuonekana wauponda kwa kula chipsi hotelini badala ya kupika nyumbani au kufanyia kile ambacho wameombea msaada!

Watoto wengi watu wazima huona wazazi wao walikosea kuwalea nao wataleta tofauti sana kwa watoto wao! Wazimbabwe wanasema; “Anayejua kulea vizuri mtoto ni yule asiyekuwa na mtoto.” Lakini wakipitia pale watagundua kwamba hakuna mzazi mkamilifu. Kila mzazi anajutia makosa fulani aliyoyafanya katika kulea! Ila jambo kubwa ni neno la Mungu kukaa katika mioyo na maisha yetu na tujitahidi kulifanya ndilo pekee la msaada. Falsafa za dunia huja na kwenda ila Neno la Mungu litasimama milele.

Mara nyingi wazazi hawaoni kwamba watoto wao wamekua na wanaweza kuwaongoza kwa ushauri katika baadhi ya mambo. Mfano mtoto ambaye amekuwa mganga akishauri wazazi kwenye nyanja yake wazazi waweza kupuuzia na kufuata mashauri ya mganga mwingine ambaye yawezekana si bora.

Chochote kile kinachotokea katika familia yako sasa ndicho kinachojenga historia yenu. Familia zote zina fanaka na shida. Jinsi unavyoshugulika nao sasa, ndivyo ya mbeleni yatakavyojengeka. Usichukulie kirahisi (take them for granted) kama mahusiano yenu ni mazuri sasa. Jenga mahusiano mema. Usikate tamaa. Tia juhudi kuwapenda japo kuna matatizo. Jenga mawasiliano mazuri. Tuna mategemeo tofauti katika mahusiano yetu na watoto na wao pia wana mategemeo tofauti. Mzazi wa mitara aweza kutegemea watoto wa mke mwingine wasaidie watoto wa mama wa kambo kwa nguvu au watoto wa ndugu zake; “Utawasomesha hao upende usipende, la sivyo nitakulaani!”

Mategemeo yasiyofahamika na wote ni lazima yaondolewe au kuzungumziwa ili kuleta hali shwari kwenye mahusiano. Hakuna mahali ambapo sheria zimeandikwa kuhusu mahusiano, mengi ambayo watoto au wazazi wanategemea, hivyo ni vizuri kuwa mkweli na wazi. Ni muhimu hata kwenda kwa mshauri wa makamo mwenye hekima kutusaidia kuona tofauti zetu na jinsi ya kujengea madaraja. Inakuwa vyema zaidi kama mshauri huyu anampenda na kumtegemea Mungu kama matunda yake yameonyesha. Epukana na mshauri mgomvi, mchocheaji au msengenyaji. Na hata washauri wengine ni jamaa wa karibu wanaowafahamu sana na historia yenu itakuwa kwenye mawazo yao wasiweze kuwasaidia. ‘Mavi ya kale’ yanaingia katika mawazo yao na hawawezi kuanza kurasa mpya hata kama mmebadilika!

Napenda kusisitiza kwamba familia zote zina matatizo fulani kama tungeita karamu ya wote wenye matatizo na familia zao walikozaliwa, tungepata msururu mrefu. Hakuna ambaye angekuwa mtazamaji maana kila mtu angekuwa kwenye hilo gwaride!

Matatizo siyo kiungo mara nyingi, ila ni mito inayotutenganisha. Tukiwa na matatizo tunajifikiria zaidi wenyewe na kusahau wengine. Mara nyingi pia tunataka shida hizi ziwe siri na kuanza kuwashuku wengine au kuwakosoa au kuona yupi ana matatizo zaidi yetu. Kwa kujilinganisha tunaona tuna unafuu na kujiona bora. Niliona watu wanene Marekani wakipenda kukaa karibu na mnene zaidi yao, ili waonekane wembamba! Ni kweli wazazi tuna matatizo ila matatizo mengine yanakuja kwa ajili ya matatizo! Hebu tuorodheshe baadhi ya hayo matatizo: Kufilisika, kutoa mimba, madawa ya kulevya, madeni, kansa, hasira, ulevi, kutojitegemea, ukimwi, magonjwa ya muda mrefu, ubaguzi, imani tofauti, kisasi, kilema, kiburi, kuabudu kazi, tabia ya hasira na matusi mazito, ushirikina, kuvuta sigara, uhanithi, unyanyasaji wa ngono, kujamiina ndugu (incest), wizi, kamari, ushoga, kupoteza kazi, maradhi ya akili, majanga, unene, kupigana, jela, nafasi ya nyumba ndogo, upweke, kujiona duni (low self esteem), kuishi chumba kimoja watoto na watu wazima n.k.

Matatizo haya, na mengine waweza kuongeza yampata kila mtu. Waandishi hawatazungumzia kila tatizo hapa. Ila watatoa ushauri jinsi ya kushugulikia matatizo pindi yajapo ili usizae matatizo mengine. Andika orodha ya matatizo yako kutokana na unavyoona uzito wake. Jiulize; je, watoto wangu watu wazima wanayaona haya kama matatizo? Je, wao kwenye orodha yao wanayo yapi? Je watashangaa kuyaona yangu? Je, wanajua hitaji langu? au umeficha kwa sababu uliona hawatajali? Je, wewe na familia yako mnaepuka kuzungumzia mambo fulani hivyo hamjui kama ni shida japo yanakufanya wewe au wao msilale usiku?

“Nilipokuwa mtoto wa miaka minane hadi kumi na minne, nilikuwa na baba mdogo aliyekuwa akinishika shika mwili wangu na kuzungumzia ngono. Hakunikaba ila nilijua kwamba alikuwa hanitendei haki. Lilikuwa ni kosa nami sikusema kwa vile alipendwa nyumbani na baba yangu na mama pia. Wazazi wangu wasingeelewa. Sikuhudhuria mazishi yake, na wazazi wamekuwa wakiniuliza. Nikiomba ushauri wa watu wanasema niwaambie wazazi wangu ila mimi ni mtu mzima sioni haja ya kuwaeleza wazazi tena.” Kutokana na kisa cha msichana huyu: Je, unaona wako ukurasa mmoja na wazazi wake? Watu waweza kuishi nyumba moja na matatizo tofauti!

Mshauri mzuri atakwambia kwamba, “Yule ambaye anajiona ana nafuu ndiye awe wa kwanza kutafuta suluhu ya tatizo.” Kama unasoma hii sura inaonyesha una nafuu ya kuuliza msaada. Ili kusudi kuwe na uponyaji kati yako na watoto wako ujenge madaraja ya kutatua matatizo. Na kama ni wewe ndiye unayeleta matatizo kuhusu matatizo yaliyoorodheshwa maana yanakuja mara zingine kama mapacha, angalia mifano ya kutatua. Mfano una mtoto anayejihusisha na ushoga, Je, utalitatuaje tatizo hili endapo kijana wako atasema; “Mimi sina tatizo lolote, wewe ndo una matatizo, ndivyo nilivyoumbwa!”

Yaonekana kwamba kile wewe unachokiona ni kosa la sheria za serikali au dhambi, yeye anakiona kama kitu cha kawaida. Kama mnakaa nyumba moja mtafute suluhu badala ya kuwekeana mgomo baridi na kila mada ikija mnajumlisha na lile tatizo la awali; mmoja wenu anakimbiza sungura bila kutaka kujadili. Hali hii inajenga ufa zaidi. Hamwezi kuwa katika ukurasa mmoja. Makosa ya familia husababisha nini kwa makosa ya jinai ya watoto wao?

Mfano, “Kijana wetu alipofika miaka kumi na minane, alianza kuuza madawa ya kulevya na wizi. Alifanya hii kazi usiku na mchana alilala. Kuna wakati alipigwa vibaya akivunja nyumba za watu. Kila tulichomwambia hakikusaidia ila kilileta ugomvi mkubwa. Mwishowe tulimwambia tunakupa mwezi mmoja upange chumba chako utoke humu ndani. Mwezi ulipoisha alisema nifanyeje niendelee kuishi nanyi? Tukamwambia hakuna la kufanya ila kutoka unaruhusiwa kututembelea tu, na tutakupokea vizuri maana ukiwa karibu tunajenga uadui, chuki na magomvi. Aliondoka na baada ya muda mrefu alikuja kututembelea. Siku hizi huja kututembelea na akija kuna tofauti ya mahusiano yetu. Huja yeye, au na mke na watoto. Tunafurahi tukimwona. Kweli Mungu Ametuletea furaha katika majonzi yetu.”

Soma Kumbukumbu la Torati 21:18-20. Angalia katika orodha; je, yapi ni dhambi na yapi ni kosa la jinai (crime)? Napenda kusisitiza kesi kama hii ya kumbukumbu ilikuwa ni dhambi ambayo Mungu aliwaambia watu waziwazi.

Sisi sote ni wenye dhambi na hata kama wazazi, tunakosea. Biblia yasema “Heri kijana masikini mwenye hekima kuliko mzee mfalme mpumbavu.” Mara nyingine wazazi wengine wametumiwa na adui shetani kuliko watoto wao. Hebu wazazi na watoto wajifunze kujenga mahusiano yao na kusameheana. Na mnapotatua tatizo mfanye mpango wa kubadilika, msiwe watu ambao kila mara mnatafuta magomvi na msiotaka suluhu. Je, nini kinaleta ugomvi kwenu? Je, ni kutoheshimiana na kuvuka mipaka ya

kutaka kumtawala mwingine? Haya yote yasiogopwe kujadiliwa kama mnataka uhusiano mwema, kila mtu ni vyema aseme jinsi anavyoona uhusiano huu utakavyokuwa bora, na yeye atafanya nini ili uwe bora?

Badala ya kuzunguka zunguka na kupoteza muda hebu tafuteni. Si lazima muwe marafiki, ila urafiki ni kitu kizuri cha furaha moyoni. Je wewe unataka urafiki na familia yako? Unafanya nini kufanya hili liwezekane? Je unajijali binafsi na shida zako tu na kuwa mtu ambaye unajifikiria mwenyewe? Pambano kati ya nafsi zetu ni gumu ila inabidi tulishinde (battle against self). Utu wa kale inabidi ufe. Roho ya umimi (me, myself and I) ilikuwa ya watoto zamani, siku hizi hata wazazi wameonyesha kuwa nayo, wakibamiza watoto wao. Wanawaandikia barua za kuomba vitu. Mara baba anaomba pekee, kisha mama naye aomba. Wengine wana mahusiano mabaya kati ya mtu na mume wake. Watoto wanamtumia mama kila kitu. Baba analalamika, kisha wanamchukua mama kukaa naye mjini, moja kwa moja na baba akichochea masufuria kwa upweke kijijini.

Rafiki yangu wa Kisii alisema kwamba watoto walio Magharibi wanamtumia mama tiketi ya ndege, awatembelee na harudi tena. Wana wanakuwa upande mmoja na mama. Mama, hii ni tabia mbaya ya kumtendea mume na mzazi mwenzako!

Dhambi ni shida kati yetu na Mungu na kati yetu na watoto wetu. Tunaongeza tatizo kwa kushugulikia dhambi wenyewe. Dhambi zetu zinatufanya tuwe na picha tofauti kati yetu, na wengine. Hii yafanya vigumu kujitegemea sisi wenyewe au wenye dhambi na kuona, wengine kuwa tuko sawa kuzidi wengine. Endapo familia yako inahusika na matatizo ya dhambi yaliyotajwa au unayojua ila wanaona wako sawa; haupaswi kuona kwamba hawafanyi dhambi, la! Mungu Anajua dhambi zako na zao. Yeye anampenda mwenye dhambi ila anachukia dhambi. Ni rahisi kusema kuliko kutenda! Omba msamaha kwa dhambi zako, ujutie na kuziacha “usiseme kwa mtoto wako, “Najua nina dhambi ila zangu ukilinganisha na zako ni ndogo sana!”

Twajua umeumizwa na hali ya mtoto wako. Kama mtoto wako mtu mzima anakaa dhambini ni vyema umwambie kwa njia nzuri, na wala usitembee ukimsengenya na kumwambia kila mtu unayekutana naye kana kwamba watu hao hawana mizigo yao.

Mara zingine hata upo tayari kumwachia kijana au binti yako ila anakuganda. “Niligundua kwamba ninapenda kuburuza watoto wangu na ni dikteta. Nilikuza watoto wangu hivyo. Mume wangu na watoto na hata majirani waliniambia, ila sikusikia. Nikamwendea mtu wa nje anishauri akaniambia nikate kamba za kutawala watoto wangu watu wazima. Sasa nataka niache tabia hii. Nimewaambia wawe na maisha yao, mimi sitawatawala tena. Lakini unajua ni nini kimetokea? Kila mara wananiweka kwa mambo yao wakinisihi niwaamulie. Sitaki wanipe majukumu yao! Wanataka yakifeli wanilaumu! Wananiambia kwamba hawajui kubeba majukumu kwa vile walizoea mimi nilikuwa kiongozi wao saa yote na kuwaambia cha kufanya na wanataka niendelee kushikilia usukani huo. Sitaki hiyo kazi tena natoka!”

Wazazi wengine ambao wanakandamiza na kutawala watoto wao wakigundua, wanataka watupe jongoo na mti wake! Wanawapa watoto talaka! Uhusiano, ili uwe wa afya inabidi ubadilike, ila isiwe kwa ghafla namna hiyo. Pengine wazazi wapaswa kuepuka

mambo fulani kama ushauri au msaada. Ila usipite mpaka hata kumkana mtoto, kama kwenye mfano huu:

Kuna mjane ana mtoto ambaye alikuwa akimburuza kwa ukali mwingi akiwa mdogo. Hii ni tabia ya mama huyu mjane hata kanisani anataka kutawala na kuamuru kila kitu, na ameleta shida nyingi kanisani. Dada yake alipomtembelea tuligundua ana kijana mtu mzima waliyegombana naye mno akiwa miaka 22 na anasema kwamba hana mtoto. Kwenye kesi kama hii yule anayempenda Mungu ambaye alikuwa anamtawala mwingine ndiye anayepaswa kumfikia yule mwingine na kujenga daraja. Maana wale watoto watu wazima bado wana ile picha ya mzazi dikteta mpaka wapate picha nyingine. Yupi yuko sawa na yupi ana makosa isiwe sababu. Jambo kubwa ni mzazi kama anataka mahusiano na mtoto aweza kumfikia mtoto na kujenga urafiki.

Ni kweli mtoto akizaliwa wazazi wana jukumu la kila kitu mfano, kumpa mtoto jina, kuamua mtoto atazungumza lugha gani, ataishi wapi, atakuwa na imani gani, au atatibiwaje au hata atasomea wapi na masomo gani. Hii ni sawa kwa vile mtoto hana uwezo wa kuamua ila watoto wanapofikia miaka ya kumi, wanajiuliza inakuwaje wazazi wana mamlaka yote hayo? Wanaanza kuchagua mfano sipendi samaki, au napenda mihogo badala ya mkate. Mtoto akikua na kuanza kutaka mamlaka ya maamuzi yake anaanza kuona mamlaka yanakuja na majukumu. Hii, ni hali ya kukua na ni njema tu (healthy). Mtoto anagundua kwamba mzazi hawezi kutatua matatizo yote, na hata anafanya makosa mengi na kwamba siyo Mungu! Ila watoto wengi hawataki kujitegemea na watoke kwenye kiota. Mambo ni rahisi wakifanyiwa vitu na mzazi, kama: Pesa za matumizi, kubebwa kwenye gari, kununuliwa chakula na mengineyo.

Mzazi ajue kwamba japo alifanya makosa akiwalea watoto, sasa wamekuwa watu wazima wanaowajibika kwa maisha yao wenyewe. Mzazi aombe msamaha kwa Mungu na kuwabariki watoto. Ikiwa mzazi ataendelea kuwafuga na chuki iendelee atawaathiri hata wajukuu wake. Jinsi wanavyoendelea kukulaumu kama mzazi watapenda waishi kama watoto tu wasikue kimajukumu. Pale tu watakapochukua jukumu na kusema, “Japo tulilelewa vibaya sasa tu watu wazima Mola tusaidie tukabiliane na maisha;” watasonga mbele na kujisaidia maishani mwao.

Mara nyingine watoto wanakosea na kugundua siku zimekwenda mfano: “Tulimwambia kijana wetu tutamsaidia kusoma chuoni. Alitaka tumpe pesa akisema mambo ya usomi siyo yake, tulisema la! Ofa yetu ilikuwa ya shule. Sasa tumestaafu naye amekuja na kutuambia yupo tayari kwenda shule. Hatuwezi kulipia gharama ya shule kwa sasa na ni miaka mingi imepita, nasi tulishamsaidia kuchangia mahari na arusi yake.”

Mtoto akiwa mdogo vitu vya wazazi ni vyake pia. Ila mara nyingi watoto bado wana mawazo ya vitu vya mzazi pia ni urithi wao. Ni kweli watoto wengine wanajikwamua na kuwa na vitu vyao ila wengine wanabaki nyumbani. Mzazi ajadili jinsi ya kumsaidia binti au kijana kujitegemea kama vile kumpa ardhi, au kitu cha kumsaidia ajikwamue kimaisha kadiri inavyowezekana. Bado kiafrika na kwa agizo la Maandiko mtoto anasaidiwa kujitegemea na urithi wa aina fulani.

Wazazi tusiendelee kuishi na matatizo yale yale mwaka hata mwaka kama mtu mwenye jiwe kwenye kiatu ila halitoi. Ukiona matatizo yanayojirudia rudia jilinganishe na

wengine. Je, ni wewe unayeleta tatizo? Je, kuna jinsi ya kulitatua? Pengine ni wewe unayeweza kulitatua. Mfano binti yako anapenda kazi anayoifanya ila wewe wataka afanye kitu kingine; “Binti yangu anafanya kazi ya uhasibu, ila mimi nilitaka awe mwanasheria, najaribu kumwambia ila anaonekana ameridhika.” Pengine ndoto za mzazi zisizotimia kama kupiga kinanda au kusoma chuoni, anataka zitimie kwa watoto wake kwa nguvu.

Wakati mwingine tunafikiria watu wengine ndio wanatuletea matatizo, ila sisi tuko sawa. Hao wengine ni kama serikali, familia, kanisa, au jumuiya. Familia zingine zinafikiri matatizo yao yote yameletwa na mtu fulani, lakini si rahisi kujiambia ukweli kama wao wanafamilia wana makosa ya kujilaumu na kusahihisha.
“Nilijitoa maisha yangu kutunza watoto wangu, nikawa mtumwa wao. Vitu nilivyotaka kuwa navyo sikuvinunua, kila kitu nilikuwa nafanya kwa ajili ya watoto wangu. Sasa unaona nilichoambulia? Nina mahitaji sasa na hawanisaidii. Nina maradhi yaliyotokana na kuwatunza. Nimekuwa fukara kwa ajili yao, kwa sababu ya kuwapeleka vyuoni. Sasa nimebaki mpweke, kwa vile nilikuwa nashughulika nao badala ya kujijengea marafiki wengine. Hawanijali, hawana muda nami. Nimewapa kila kitu changu na sasa hawanipi chochote!”

Watu wengi huwa tunapenda kulaumu wengine. Kwamba; “Ni makosa yako ndiyo maana nimekuwa nilivyo.” Kulaumu wengine kunakufanya usifanye majukumu yako. Wapaswa kujua kwamba watoto wamekuumiza, nawe umewaumiza. Shida nyingine zinaweza kutokana na uleaji, pengine kuachana na mke au mume wako kuliwapa shida, au ulijali kazi yako tu, au pengine unyanyasaji wa kimwili au kijinsia ulitokea. Watoto wako wakubwa nao wana maneno ya kusema na haitasaidia kusuluhisha hata kama ni mahakamani. Kama ni kweli wajua kwenye moyo wako, uliwatelekeza nao wajua, angalia yale mazuri katika mahusiano yenu japo ni madogo. Na watoto nao wachague yale mazuri, mtafute mshauri mwenye hekima za Mbinguni na kumtumia kuwasaidia. Yabidi mkubali makovu ya hisia yaliyokuwepo kama vile mtu anavyoweza kukubali kilema fulani, angalia kile ambacho kinaweza kufanyika katika kujenga mahusiano na kusameheana.

“Mimi nilikuwa mvulana wa kwanza na nilimwona baba akimpiga mama na kuchukua wanawake wengine. Aliwapiga dada zangu pia. Alipompa mama talaka nilifurahi japo tuliishi kwa umasikini. Nimepata kazi nzuri, nimeoa na kupata watoto na naishi na familia yangu vizuri. Baba mkwe wangu amekuwa baba wa faraja mno kwangu. Nilipofanikiwa kimaisha nikagundua kwamba simchukii baba yangu mzazi tena. Tunaandikiana barua na nazungumza naye kwa simu. Ninapiga magoti kumwombea na nashukuru kwamba hakuharibu maisha yangu.”

Watoto wako wanaweza kuwa hawakufuata mifano mizuri uliyowapa. Walipuuza ushauri wako au imani yako au kukudharau wewe kama mzazi au kukuibia na kukuaibisha mbele ya jamaa na marafiki. Na wakazidi kuendelea kukulaumu kwa mabaya yao. Usikubali dhamiri yako ikushitaki kwa uovu wao. Ukiwa na maumivu ya watoto wako usibebe mzigo wote mwenyewe, haitawasaidia. Japo hakuwa mzazi mkamilifu ungama tu kwa makosa ambayo ni dhahiri yako, na usijisulubishe kwa yale ambayo yanatokana na tabia zao dhaifu. Endelea na maisha yako, ungama kwa mapungufu yako kwa Mungu, na kujua maisha ni zaidi ya uzazi. Chukulia yale yaliyobaki mazuri na familia yako na marafiki, na

tafuta vitu vya kufanya kukusaidia kupona vidonda hivyo. Usitembee ukipiga tarumbeta ya kulaumu watoto wako kila siku. Maana kuwasonda vidole na kuwalaumu itafanya wajihami nayo haitajenga ujamaa. Nawe wakikulaumu usijihami, bali kwa upendo kama ni tatizo la suluhu na siyo kukabana mashati na kutaka kujua nani mwenye kosa. Isaya 30:20-21.

Bwana atakuogoza kwa hekima ili usijikanyage, na pia usimlaumu mtu au kuzira mahusiano wakati

ambapo watoto wako walitaka msaidiane kutatua tatizo. Bwana atakupa hekima pale pa kuomba msaada wa wengine, na pale unapopaswa kufanya sehemu yako.

"Binti yangu ametumia watoto wake kama fimbo. Akiniomba pesa nisipompa, anawanyima watoto wake chakula kisha ananilaumu kwamba watoto hawajala kwa sababu yangu. Ametumia kitabu changu cha hundi na kugushi sahihi yangu. Nilikuwa namwachia anipige na bakora zake za malaumu. Ila sasa nimeona kwamba simsaidii. Alipoenda jela kwa ajili ya kugushi sahihi za watu wengine sikumtoa, nilimwacha akae mle na ndipo akajifunza thamani ya mahusiano yetu."

Jifunze kuwaambia watoto wako pale unapohitaji msaada au pale ambapo hupendezwi na jambo. Jua kwamba kuna mengi usiyoweza kutatua, kama unasaidia mtoto wako, angalia wewe mwenyewe usije ukatumbukia kwa vile huna nguvu za kutosha kukabiliana na tatizo hilo. Huwezi kutoa kile usichokuwa nacho. Wengi wetu tunataka kutatua tatizo kwa haraka. Ila mambo mengine hayana ufumbuzi ila jinsi ya kujua kuishi nayo bila kukuumiza (destroy you). Mungu hutupa nguvu na si kujibu maombi papo hapo. Yabidi tukubali mapungufu yetu, na ya watoto wetu ila tusizae matatizo juu ya matatizo. Kumbuka wewe ni mwenye dhambi na Yesu Amekuokoa na wote wa dunia hii, wakiwemo watoto wako, wote twahitaji msaada wa Mungu.

Mungu anataka tuwe na umoja ila asema kwamba mara nyingine watoto wako wanapingana na imani yako; Mathayo 10:34-37. Kama familia yako nayo inamwamini Mungu, basi una nafasi ya kutafuta suluhu na familia yako. Yeye ni msaada kwa familia iliyosambaratika.

"Baba ananisinya na mambo yake ya kanisa, kila mara ananikazania niende kanisani na kusema, tuombe. Wakati tulipokuwa wadogo hakutupeleka kanisani. Nasi tulikaa tu. Sasa amepata uongofu kwa ajili ya umasikini anataka anikandamize nao. Anakazana niolewe badala ya kuishi na rafiki yangu wa kiume wakati yeye hakuoa rasmi, ila aliishi na mama tu. Pia hataki ninywe pombe nami nilimwona akinywa kila siku. Sasa wamekuwa wazee na mama wanachungulia kaburi, wanaogopa wataenda jehanam na hawana cha kufanya wala kibarua kama mimi, ndiyo wananikazania. Shauri yao hawakunipeleka kanisani nikiwa mdogo."

Kama mzazi hukuwakuza watoto katika maisha ya imani, ulikuwa mtu wa dunia. Bwana ni mwingi wa rehema. Angalia katika mikutano ya familia kama wangekubali mwombe pamoja. Mkikutana kwenye sherehe, Je, wanataka ufanye yale yanayopingana na imani yako? Ukiweka hati ya mirathi (will), Je, waweza kuweka asilimia unayotaka kwa huduma za kazi ya Mungu? Maana ukifa, hawatafanya matakwa yako au hata mazishi.

Pengine watafanya yale ambayo wewe unafikiri hayamtukuzi Mungu. Wajulishe matakwa yanayohusu imani yako ili waelewe kwamba hili la imani ni kipaumbele kwako kwamba wanaweza kuamini wanavyotaka ila mheshimiane katika swala la imani zenu. Mathayo 5:44 inasema, "Adui wa mtu ni watu wa nyumbani mwake."

Neno kuu halisemi mimi nimwambie mtoto wangu au mwingine asamehe ila ni mimi nijifunze kusamehe na kuwa mpatanishi na kuwa muwazi ili watu waone mfano na kumtukuza Baba wa mbinguni.

KUKATA KITOVU CHA MTOTO

Matatizo kati ya wazazi na watoto walio watu wazima yahusisha hisia na namna tunavyozipokea hisia zetu. Je, umeshugulikia hisia zako za wasiwasi, kukatishwa tamaa (disappointment), hofu, kutoamini, dhamira kukushitaki, huzuni, kuchanganyikiwa, chuki (remorse), uchungu, kukosa tumaini? Watoto hapo zamani walijitegemea mapema, lakini siku hizi wanaishi nasi kwa muda mrefu. Na hata wakienda zao bado ni wetu! Wajerumani wanasema, "watoto wadogo, matatizo madogo na watoto wakubwa matatizo makubwa." Ni kweli wazazi wa watoto wadogo wanabadilisha nepi, wanaogesha watoto ila watoto wanazidi kuwa na mengi wakikua. Wengine wamekufa moyo kwamba watoto wao wamekuwa wabaya wakiwa watu wazima na wazazi wengine wamejilaumu. Ila wengine wamefurahi hawakutegemea watoto wao, sasa wamekuwa kama mnara wa taa! Kuna wazazi wengine hawaridhiki kwamba watoto wao wamekuwa walivyo, wanataka mambo makubwa zaidi au mategemeo makubwa. Mtoto mmoja aliambiwa na baba yake kwamba Abraham Lincoln alipokuwa umri wake wa miaka ishirini na mmoja alikuwa mwanasheria, baba huyu aliendelea kumbamiza mtoto wake na Abraham Lincoln, mwishowe siku moja alijibu, "Baba, Lincoln alipokuwa umri kama wako baba wa miaka hamsini, alikuwa rais wa Marekani!" Je, tuna mategemeo halisi kwa watoto wetu? Je, wana mategemeo halisi kwetu?

Mara nyingine ni kujisikia tunaweka siri tusionekane kwamba watoto wetu hawakuwa marubani, wanasheria au madaktari kama tulivyoota kwenye ndoto zetu! Uzazi ni uchungu na furaha. Hauwezi ukakoma kuwa mzazi siku moja, hata mtoto akienda. Kitovu kimekatwa ni sawa ila bado unakuwa mshauri wake, isipokuwa usiwe zimwi! Mara nyingi nimemwita mzazi wangu nikijua kwamba hakuna atakayenipa ushauri wa upendo na wenye uzoefu zaidi yangu kama yeye. Pale unapotafuta mabaya tu, jaribu kukumbuka na mema yapo pia! Hiyo ni kanuni kwa mtoto na hata kwa mzazi pia.

Wamarekani wana msemo, "Watoto wako wakiwa wadogo wanakukanyaga miguuni, wakiwa wakubwa wanakukanyaga moyoni!" Ila Usitie chumvi ule ubaya ukaukariri na kurudia rudia kwao! Na msemo wa zamani, "Mtoto anamzidi mzazi," ni kweli. Ukiona mtoto anajitegemea na kujikakamua kumudu maisha, mwache; usikae na kumsakama sakama na kumsimanga, bila kuridhika. Nimeona wazazi wengi wakiweka viwango ambavyo wao wenyewe walishindwa kufikia "nataka usome uwe mwanasheria, nataka uwe milionea!" yanasemwa kwa maneno au matendo kwenye familia nyingi!

Maswali ya utafiti (questioner) yalionyesha kwamba hizi ndizo tabia ya familia yenye afya (health family).

1. Wanawasiliana na kusikiliza (Communicates and listens).
2. Wanasupportiana na kupongezana (Supports and affirms)
3. Wanafundishana jinsi ya kuheshimiana (Teaches how to respect for others)

4. Wanajenga tabia ya kuaminiana (develop sense of trust)
5. Wanashugulika na kucheka pamoja (has a sense of play and humor)
6. Wanatekeleza majukumu yao (exhibits a sense of shared responsibility)
7. Wanaelekezana chema na kibaya (teaches a sense of right and wrong)
8. Wana mila na destruli za familia wanazofuata (has a strong sense of family in which rituals and traditionals abound)
9. Wana usawa na kuwiana kwenye familia (has a balance of interaction among members)
10. Wana imani inayofanana (has shared religious core)
11. Wanaheshimu mipaka ya mwingine, km. hawagombani mbele ya watoto (respects the privacy of one another)
12. Wanathamini huduma za wengine (values service of others)
13. Wanathamini kula na kuzungumza pamoja (fosters family table time and conversation)
14. Wanapanga masaa ya kuwa na burudani pamoja (shares leisure time)
15. Wanakiri kukiwa na shida na wanatafuta msaada (admits to and seek help owith problems).

Sura ya 18

WATOTO AMBAO NI WATU WAZIMA NA WANAISHI NYUMBANI

Mambo ambayo watoto wamekuwa nayo wakiwa wadogo wanahama nayo mpaka kwenye utu uzima pia. Mambo ya aina hii mengi yao inabidi yashugulikiwe ili yasijiinue kichwa chake watoto wakiwa wakubwa. Ilianza kwa yule aliyekuwa na shida ya ulevi,

kuondoka kwenye kukana kwamba anakunywa ili asaidiwe. Tabia ikaendelea kwa tabia zingine zinazoathiri familia. Ulevi wa kazi, ulevi wa chakula, ulevi wa sheria, ulevi wa ugomvi, ulevi wa ngono nk. Nchi nyingine wameanzisha chama cha AA (alcoholic synonymous) kushugulikia shida hizi. Napenda kusema japo kuwa kuna shida zinazojitokeza, kuwepo kwa watoto wengi nyumbani kuishi kwa watoto wengi karibu na wazazi kumekuwa mbaraka kwa pande zote

Mfano familia ambayo mama amekuwa akitoa udhuru kwamba baba yenu amechoka na amelala, kumbe amelewa! Na watoto wanajua na jirani pia wanajua ila ni siri ambayo watu hawajadili. Baadaye itakuja kuathiri watoto watu wazima na hata wale wanaooa au kuolewa nao. Watoto wanaona aibu kwa wenzao au mahali popote mpaka wanafikiri ile shida ilikuwa yao wakiwa wadogo, wakiwa wakubwa inajionyesha vingine. Familia zetu za kiafrika zinatunza siri mno, na hili limekuwa bomu kwenye familia nyingi kwa maisha ya leo kuficha siri vile! Mambo mengine yabidi yasemwe ili yapate usaidizi. Niliona watoto fulani waliokuwa watu wazima wakiona aibu mno kwa vile baba yao alikuwa akinywa sana na alikuwa na wake wawili. Aibu ilifika kwamba hawakusema kwamba baba yao yuko hai. Walikuwa wameshamtoa kwenye mawazo yao!

Tunapozungumza watoto wakubwa naomba tuweke hili maanani, kwamba kila familia ina mizoga yake, na mizoga mnayotaka kuendelea kuificha ukubwani hata kwa wakwe au wakamwana watoto wenu wataifanya pia. Ndoa inaweza kuleta mambo mengi yasiyo kuwa ya afya ya akili (mental health). Nimeona haya kwenye familia nyingi. Kama ulikuzwa kwenye familia yenye shida hizo angalia mambo ya Alcoholic Anonymous ili uweze kusaidiwa.

Siku hizi hakuna babu, shangazi, mjomba wa kukupa ushauri sana. Ila familia nyingi za kiafrika wanaoficha siri wameathirika kwa njia moja au nyingine. Siri hizi ni pamoja na ulevi, unyanyasaji, kijinsia au kingono (ukatili), kutotumia pesa vizuri na kila mara kutegemea wengine, kujiua kwa watu wa familia, tabia mbovu za kusataajabisha, kujiona kwamba wewe umeshindwa (perceived failure), magomvi yasiyoisha au magonjwa ya akili, kifafa, n.k.

Mwanasaikolojia Erickson anasema kwamba kazi ya mtoto kukua na kutoka nyumbani kwamba ajue yeye ni mtu kando ya mzazi si rahisi vile. Msaidie mtoto wako akitoka asiwe na dhamira ya kumshtaki, na asiondoke kwa kuwa wamegombana. Tafuta jinsi ya kuachana vizuri, mkisalimiana na kuendelea kusaidiana mnavyoweza. Mtoto ye yote anayetoka kwenda ulimwenguni kuishi peke yake anakuwa na hofu ya aina fulani. Hebu atoke vizuri akijua alipotoka alikuwa anapendwa, anathaminiwa na ni mahali pazuri hata akirudi tena atatendewa vyema (treated well). Watoto wasifikiri kwamba unawadai kitu, na kuwapelekea ujumbe walipo kwamba hamnisaidii hili au lile.

Ni jukumu la mzazi kumsaidia mtoto, lakini tamaa inaingia kwa wazazi wengi kupita mpaka wa mamlaka yale waliyopewa na Mungu, ya kumtawala mtoto. Wakati huo watoto wenye uwezo, hebu waone kwamba kuwasaidia wazazi wao ni kitu cha mbaraka na jukumu lao, hasa kwa lile ambalo liko kwenye uwezo wao. Watoto na wazazi wengi wamejitwika uovu katika sehemu hii aidha kwa ajili ya tamaa au kujibinafsisha bila kuangalia mambo kwa upendo. Ukitaka kupona katika mahusiano mabaya, kwanza UKIRI

YAPO! (uadmit) usiwe mtu wa kutaka kuishi ukificha, ukikanusha au kukimbiza sungura kila yanapotokea. Mficha maradhi, kilio humfichua. Hichi ndicho kitu Waafrika inabidi tujifunze.

Usifikiri utatatua hilo tatizo kwa kulikimbia lisisemwe kila mara linapokuja, lishike pembe yake kabisa ili lisijiiune. Kisha ukilikiri na kuliweka wazi kwenye moyo wako, zungumza na watu wa hekima wanaompenda Mungu kuhusu wewe na haya mambo, na uwe tayari kusikia, siyo tena uepe na kukimbiza sungura! Jaribu kutafuta habari au vitabu vya somo hili uangalie.au kama kuna semina za shida ya familia yako uende. Mfano unyanyasaji, ulevi nk. Vitabu vingi vimeandikiwa kuhusu watoto watu wazima au wazazi na ulevi na ukupe (co-dependency). Angalia haya kwenye internet. Fikiria maisha yako sasa na ya zamani ukiwa mtoto na shida hizo za ulevi. Waweza kufikiri dakika moja unazo na dakika ya pili hunazo! Kwenye ushauri wa wengi jambo linasimama, yaani halianguki. Angalia zile hatua "12 za alcoholic anonyomous" za kupona kwa wale walioandika wanaompenda Mungu. Hatua hizi zimesaidia wengi sana kupona katika mambo tofauti. Nawafahamu wanaofanya kituo kimoja cha hiki kitengo wanaitwa 'The Bridge'. Kwa vile kwenye kitabu hiki nafasi haitatosha kuongea haya mengi tafadhali rejea kwenye hiyo website, ya codependency or addiction and adult kids'

Imetokea hali ambayo watoto ambao ni watu wazima bado wanaishi nyumbani kwa sababu mbali mbali. Waandishi wamechukua muda kuzungumza kwa sababu jambo hili limekuwa la kawaida kwenye jamii kuliko tunavyofikiri. Mtoto mtu mzima anakaa na wazazi kwa sababu kama mtoto anatafuta kazi kwa muda mrefu, mtoto amekosa kodi ya kupanga mahali pake peke yake, wazazi wana nyumba kubwa na uwezo kuliko mtoto, au kwa watoto wa kike wasioolewa kuishi na mzazi ni usalama zaidi na wengine pengine wameachana na wake au waume zao na wanategemea msaada wa wazazi wajikwamue kimaisha na watoto wao au waweza kuja na mke au mume wake na watoto wao kusaidiwa kimaisha, Mtoto amekuwa akitegemea mzazi kwa muda mrefu na wakati mwingine kuzorota majukumu kwa kuendelea kuishi kitoto.

Ila mamlaka na majukumu ni pacha. Mtoto mtu mzima hawezi kuwa anataka mamlaka na haki kwenye nyumba ya wazazi wake bila kuchukua majukumu. Tumeona watoto watu wazima wakikaa nyumbani wakitegemea wazazi wawalishe, wawalipie simu zao za mkononi, wawafulie nguo zao, na kuwafagilia vyumba vyao. La kama si wao watumishi wa wazazi wao. Mara zingine kizazi hiki kimekuwa kikiuka kanuni za afya kama kutumia madawa ya kulevya, kula junk food za hoteli kama chips, hivyo wameathirika na kushindwa kujitegemea inabidi wauguzwe kwa shida zinazohusika na kutokuwa na afya na kiasi.

Mtoto anapokuwa nyumbani afundishwe jinsi ya kujitafuta mapato. Mzazi amrithishe mtoto kitu Fulani ili aweze kujitegemea kimaisha. Hili ni jukumu la mzazi la muhimu na liko kwenye Neno la Mungu. Mtoto alirithishwa ardhi ili aendelee kuitumia na kupata riziki. Hata ardhi ilitolewa kwa koo, ikimaanisha si ya mzazi tu bali na watoto wake. Kama mzazi hana ardhi amrithishe mtoto wake elimu au ustadi Fulani ili ajitegemee na atakapooa asikae na wazazi bali aishi na mke wake. Hili nalisisitiza, watu wengi tumejipeleka mibani na kulia machozi mengi kwa kuishi kwa mpango usiokuwa wa Mungu. Nafikiri ni muhimu mtoto kuwa na posho ya aina Fulani, akifika umri Fulani, mfano miaka 8 ili ajue jinsi ya kutumia pesa. Anavyoendelea. Hii shida nilipata japo kuwa mtu mzima kufika nchi ya mareknai yenye mikopo na creditcard nikajikuta kwamba pesa ya kukopa naitumia kwa haraka kuliko taslimu niliyonayo mkononi! Ila nikikua sikufundishwa jinsi ya kutushugulika na pesa kwa undani japo nilikuwa na wazazi wote waliofanya benki, elimu

hii waafrika hatujaelimishwa nayo. Jambo lingine niligundua ni kumwekea rehani mtu (bond). Mara sita kwenye kitabu cha Mithali chasema “Ni nani ambaye ni mpumbavu ni yule amwekeaye rehani mwingine!” Ni vizuri sana kusaidia, ila uweke rehani kile kitu ambacho hata mtu akishindwa kulipa utalipa! Niliwekea rehani watu 6 wengine magari, nikiweka sahihil bila kujua maana yake vizuri. Kati ya hao, watatu hawakutimiza ahadi zao; ikafanya historia yangu iwe mbaya benki. Fundisha watoto kwamba kuwekea kitu au mtu rehani ni kama wao wenyewe ndio wamekopa. Wafundishe watoto wasiishi kuzidi uwezo wao, wasiishi kwa kujionyesha, kutojikana nafsi na kuacha kununua vingine.

Haya yote tumeona kwenye michezo ya kuigiza ya radio au runinga. Ni mambo halisi na ni vyema kuyajadili kwa wale wanaotaka kuimprove mahusiano yao na watoto wao watu wazima ni vyema wajifunze kutoka kwa mifano mibaya mno na mizuri mno. Kukaa na kuficha ficha au kuzika kichwa chako kwenye mchanga kama mbuni ili usione shida zinazoendelea haitoi ufumbuzi. Pia usikae na kumezea mahusiano ya familia nyingine na kulinganisha watoto wako watu wazima na wengine. Mfano “mtoto wa Fulani anasaidia wazazi wake amewanunulia gari, na anawapa pesa kila mwezi” au “mtoto wa Fulani hadoei wazazi wake kama wewe, ni mzigo hapa kwetu, wengine wana bahati kweli”. Sentensi za kutamani vya wengine au kujilinganisha zitakuletea mzazi misongo tu na wala siyo ufumbuzi. Hata hivyo usionee watu wengine wivu waliochukua muda kulea watoto wao katika misingi mizuri na kutumia mida mingi na watoto wao kujenga madaraja na urafiki, wakati wewe ukiwa umeachia yaya, bweni au mashangazi kujenga mahusiano na mtoto wako. Au pengine wenzako wamegundua njia za kufumbua matatizo yaliyowapata na kuweka muda, ila wewe una haraka bila uvumilivu. Jaribu kumchukulia mtoto alivyo kuliko alivyokuwa “utundu wako huu toka utotoni, ulikuwa unafanya hivi, na hivi na hivi na tena unaendelea”. Mara zingine watoto wetu wanakimbilia wengine wa makamo kutatua matatizo yao kwa kutukimbia au wanaona utazidi kuwamiliki na kukumbusha yaliyopita ambayo wameona wamesamehewa na kumbe bado tunaleta mifupa ya kale.

Kwa kawaida mzazi anampenda mtoto au mjukuu kuliko mtoto au mjukuu anavyompenda mzazi, hilo ni muhimu mzazi kuelewa anapodeal na mtoto!
Kwa desturi ya kiafrika hichi cha mtoto mtu mzima kukaa nyumbani kilifanyika kwa nadra sana, pengine ni kwa vile maisha ya mjini hayakuweko au maisha ya usomi wa muda mrefu, hata hivyo watu walitegemea kilimo na ardhi ilikuwepo na kila mtu alijenga nyumba yake akifikia umri Fulani wa kupevuka, jamii zilikuwa na sherehe za kuagana na mtoto akaishi kwenye ardhi yake aliyopewa
Mara nyingi watoto watu wazima wakiija nyumbani, sheria zao za kukaa nao ni ngumu zaidi. Maana wana mawazo yao tofauti na matakwa Fulani mfano wataomba favor Fulani msaada, ila hawatafuta kanuni zake, mfano kijana ataomba baiskeli ya baba au gari na kutaka kurudisha wakati ambao anataka. Atakaa sebuleni na kusikiliza radio ambayo wazazi wanaona ni kero. Atatatumia bafu kwa muda na huku mzazi angoja kutumia aende kibarua. Kila kizazi kina thamini kwa tofauti, na kukaa nyumba moja watu wa vizazi tofauti kuna kazi yake. Siku hizi kwaajili ya maisha ya mijini hata vijijini kumezuka tabia ya babu au bibi kuishi kwa watoto wao watu wazima mijini ambao wanawatoto watu wazima! Kwa vijijini hata kama hawakai nyumba moja, ila kile kizazi cha katikati (nitakiita B) ndicho chenye majukumu ya kuwabeba kizazi cha mababu na mabibi (nitakiita A) na cha watoto watu wazima (nitakiita C). na wakati mwingine hawa watoto C wana watoto wao! Kwa hiyo ni vizazi vine (nitakiita D).

Kukaa vizazi tofauti kwenye nyumba moja ina mibaraka yake mingi na shida zake nyingi. Uzuri wake ni kama vile, kusaidiana kiuchumi kwa chakula mavazi au nyumba. Kusaidiana kulea watoto na mashauri ya kimaisha. Wengi wanaoishi hivi wanaoelewana wanafurahia sana mpango huu. Mfano wale wa kizazi C huwasaidia kizazi B na teknologia na mambo mengine ya kileo ya maendeleo, kitaaluma, na kijamii, wakati ambapo wale wa A wanasaidia wengine kwa nasaha, kulea watoto, na maneno ya busara yenye kutia moyo na uvumilivu. Mara nyingi wale wa kizazi B wanasaidia mambo ya kiuchumi.

Ila mara zingine mkao huu unaleta fujo kwenye nyumba kama kila mtu anataka kuwa mwenye nyumba au bosi. Wale wa A wanapenda kuwaeleza wa B jinsi wajukuu wanavyopaswa kulelewa japo wao hawakuwalea vile, wanataka kudekesha wajukuu au mawazo yao ya malezi yamebadilika kutokana na mafunzo. Tofauti ya values kwa vizazi hivi inaleta magomvi. Mengi mfano wale wa A walilea watoto wao kwa maadili mema na strict na watoto wao wakawa wanayamudu maisha vizuri, yet wanataka wale wa B walegeze kamba na kuharibu watoto wao wasijali kazi na maadili ya muhimu kwa binadamu.
Ikiwa wale wa A wana uwezo kimaisha waweza kuharibu nyumba za watoto na wajukuu yaani B na C na hata D! kwa kweli watoto ambao ni watu wazima waweza kuona maadili ya wazazi ni ya kishamba na ya kizamani japo kuwa ni mazuri na ya kumcha Mungu. Waandishi hawako hapa kukutatulia tatizo hili, bali kukueleza au kukujulisha kwamba matatizo haya yapo na kwamba wale wanaotafuta kuwa wapatanishi watagundua kwamba matatizo mengine hayawezi kutatuliwa ila watu wafundishwe kuishi na wengine kwa amani japo wana tofauti kubwa. Najua wazazi wanaona watoto wao ni vifaranga bado japo kuwa ni watu wazima. Na watoto bado wanaona wazazi wao ndiyo wa kuwasaidia katika kila jambo, liwe la kiuchumi au kijamii, na siku hizi kwa vile uchumi unaendelea kubadilika wazazi wengine wanaonekana wana hali bora kiuchumi kwa vile wakati wao mishahara iliweza kufanya vitu vikubwa au biashara zilikuwa bora kuliko wakati huu ambao una competition ushidani, kwa vile wengi wamesoma na hivyo hata kupata kazi ya maana ni vigumu. Hili ni gumu wazazi kulipokea kwani nakumbuka hata mzazi wangu aliniambia kwamba watoto wako wanapaswa kukuzidi kimaisha, kimashauri na nyanja zote! Kwa hiyo wazazi wakiona kwamba wao bado ndiyo wanategemewa hawawezi kukiyeusha hichi akilini mwao! Waonaona sasa kuzaa ni kama ndoa kwamba “mpaka kifo kitutenganishe” mzigo huu waweza kuwa mzito kwenye mawazo ya mzazi

Pia kizazi hiki chaweza kuonekana kwamba hakijui kutunza pesa na kila mara kinataka maisha ya kujionyesha, kudoea na kuingia katika madeni.
Wanasema wao ni watu wazima watapanga jinsi ya kutumia pesa, kuwa na marafiki na mengineyo ila wanafanya makosa mengi na kurudi kwa wazazi kuwasaidia. Jambo hili laweza kuleta mvutano, hasa wanapopewa msaada na B na kuonekana wauponda kwa kula chips hotelini badala ya kupika nyumbani au kufanyia kile ambacho wameombea msaada!

Watoto wengi watu wazima huona wazazi wao walikosea kulea nao wataleta tofauti sana kwa watoto wao! Wanasema wazimbabwe “anayejua kulea vizuri mtoto ni yule asiyekuwa na mtoto”. Lakini wakipitia pale watagundua kwamba hakuna mzazi mkamilifu. Kila mzazi anajutia makosa Fulani katika kulea! Ila jambo kubwa ni neno la Mungu kukaa katika mioyo na maisha yetu na tujitahidi kulifanya ndilo pekee ambalo ni msaada, falsafa za dunia huja na kwenda ila Neno la Mungu litasimama milele.

Mara zingine wazazi hawaoni watoto wao kama wamekua na wanaweza kuwaongoza kwa ushauri katika mambo Fulani. Mfano mtoto ambaye amekuwa mganga akishauri wazazi kwenye nyanja yake wazazi waweza kupuuzia na kufuata mashauri ya mganga mwingine ambaye yawezekana si bora.

Chochote kile kinachoitokea familia yako sasa ndiyo kinajenga historia yenu. Familia zote zina fanaka na shida, jinsi unavyoshugulika nao sasa ndiyo ya mbeleni yatakavyojengeka. Usichukulie kirahis (take for granted) Kama mahusiano yenu ni mazuri sasa. Jenga mahusiano mema. Usikate tamaa, tia bidii kuwapenda japo kuna matatizo.jenga mawasiliano mazuri. Tuna mategemeo tofauti katika mahusiano yetu na watoto na wao pia wana mategemeo tofauti. Mzazi wa mitara aweza kutegemea watoto wa mke mwingine wasaidie watoto wa mama wakambo kwa nguvu au watoto wa ndugu zake "utawasomesha hao upende usipende, la sivyo nitakulaani"

Mategemeo yasiyofahamika na wote ni lazima yaondolewa au kuzungumzwa ili kuleta shwari kwenye mahusiano. Hakuna mahali sheria zimeandikwa kwa mahusiano mengi ambayo watoto au wazazi wanategemea hivyo, ni vizuri kuwa mkweli na wazi.

Mara zingine ni muhimu hata kwenda kwa mshauri wa makamo mwenye hekima kutusaidia kuona tofauti zetu na jinsi ya kuzijengea madaraja. Usifanye siri kila kitu.mama mmoja alipenda kusema "wewe unatoa siri za familia yetu watu wengine watatucheka". Mama huyu hakupata msaada na familia yake iliendelea kulemewa akaficha kichwa chake kama mbuni kwenye mchanga, akifa na tai shingoni kwa kutaka kuonekana ni imara. Inakuwa vyema zaidi kama mshauri huyo anampenda na kumtegemea Mungu kama matunda yake yameonyesha. Epukana na mshauri mgomvi, mchocheaji au msengenyaji. Na hata washauri wengine ni jamaa wa karibu wanaowajua sana na historia yenu itakuwa kwenye mawazo yao wasiweze kuwasaidia, ya kale yanaingia katika mawazo yao na hawawezi kuanza kurasa mpya hata kama mmebadilika!

Napenda kusisitiza kwamba familia zote zina matatizo Fulani kama tungeita karamu ya wote wenye matatizo na familia zao walikozaliwa, tungepata msururu mrefu . Hakuna ambaye angekuwa mtazamaji maana kila mtu angekuwa kwenye hilo gwaride!

Matatizo siyo kiungo mara nyingi, ila ni mito inayotutenganisha, tukiwa na matatizo tunajifikiria zaidi wenyewe na kusahau wengine. Mara nyingi pia tunataka shida hizi ziwe siri na kuanza kuwashuku wengine au kuwakosoa au kuona yupi ana matatizo zaidi yetu. Kwa kujilinganisha tunaona tuna unafuu na kujiona bora. Mfano Marekani nilikutana na watu wanene, wapenda kukaa na wanene zaidi ili waonekane wembamba!.Ni kweli wazazi tuna matatizo ila matatizo mengine yanakuja kwaajili ya matatizo! Hebu tuorodheshe baadhi ya hayo matatizo

Kufilisika, kutoa mimba,sonona, madawa ya kulevya, madeni, kansa, hasira, ulevi wa kupindukia, kutojitegemea, kutoa mimba, ukimwi, magonjwa ya muda mrefu, ubaguzi, imani tofauti, kisasi, kilema, kiburi, kuabudu kazi, tabia ya hasira na matusi mazito, ushirikina, kuvuta sigara, uhanithi, unyanyasaji wa ngono, ngono na jamaa wa karibu (incest), wizi, kamari, ushoga, kupoteza kazi, maradhi ya akili, majanga, unene, kupigana, jela, nafasi ya nyumba ndogo, upweke, kutojithamini (low self esteem), udikteka n.k. mfano mzazi mmoja alimwambia mtoto wake mtu mzima "upende usipende utamlipia mtoto wa ndugu yako chuoni, lazima ufanye! uwe na hela au usiwe nazo". Alisema hivi akiishi nyumbani kwa mtoto wake!. Watu wana ujasiri wa kusema chochote nyumbani mwa mtu. Huu nao ni ugonjwa wa nyumba Fulani.

Matatizo haya juu na mengine waweza kuongeza yampata kila mtu. Waandishi hawatazungumzia kila tatizo hapa duniani ila watatoa ushauri jinsi ya kushugulikia

matatizo yakija ili usizae matatizo mengine. Andika orodha ya matatizo yako kutokana na unavyoona uzito wake. Jiulize je watoto wangu wangu wazima wanaona haya kama matatizo? Je wao kwenye list yao wanayo yapi? Je watashangaa kuyaona ?yangu. Je wanajua hitaji langu? Au umeficha kwa sababu uliona hawatajali. je wewe na familia yako mnaepuka kuzungumzia mambo Fulani hivyo hamjui kama nishida japo zinakufanya wewe au wao msilale usiku? Mfano

“Nilipokuwa mtoto wa miaka 8 mpaka 14 nilikuwa na baba mdogo aliyekuwa akinishika shika mwili wangu na kuzungumzia ngono. Hakunikaba ila nilijua kwamba alikuwa hanitendei haki. Lilikuwa ni kosa nami sikusema kwa vile alipendwa nyumbani na baba yangu na mama pia. Wazazi wangu wasingeelewa. Sikuhudhuria mazishi yake, na wazazi wamekuwa wakiniuliza. Nimeomba ushauri wa watu wanasema niwaambie wazazi wangu ila mimi ni mtu mzima sioni haja ya kuwaeleza wazazi tena”

Kutokana na kasa cha msichana huyu, je unaona wako ukurasa mmoja na wazazi wake? Watu waweza kuishi nyumba moja na matatizo tofauti!

Mshauri mzuri atakwambia kwamba “yule ambaye anajiona ana nafuu au akili bora (mature) ndiye awe wa kwanza kutafuta suluhu ya tatizo”. Kama unasoma hii sura inaonyesha una nafuu ya kuuliza msaada. Ili kusudi kuwe na uponyaji kati yako na watoto wako ujenge madaraja ya kutatua matatizo. Na kama ni wewe ndiye unayeleta matatizo kuhusu matatizo yaliyoorodheshwa maana yanakuja mara zingine kama mapacha angalia mifano ya kutatua. Mfano una mtoto anayejihusisha na ushoga, je utalitatuaje tatizo hili endapo kijana wako akisema “mimi sina tatizo ni wewe tu, ndivyo nilivyoumbwa”

Yaonekana kwamba, kile wewe unachokiona ni kosa la sheria za serikali au dhambi, yeye anakiona kama kitu cha kawaida, na kama mnakaa nyumba moja mtafute suluhu badala ya kuwekeana mgomo baridi na kila topic ikija mnajumlisha na lile tatizo la awali. Hali hii inajenga ufa zaidi. kwa makosa ya jinai kama wizi, madawa ya kulevya, uuaji etc. hatuwezi kuficha siri. Je familia inafanya nini kwa makosa ya jinai ya watoto wao

Mfano ‘Kijana wetu alipofika miaka 18 alianza kuuza madawa ya kulevya na wizi. Alifanya hii kazi usiku na mchana alilala. Kuna wakati alipigwa vibaya akivunja nyumba za watu. Kila tulichomwambia hakikusaidia ila kilileta ugomvi mkubwa. Mwishowe tulimwambia tunakupa mwezi mmoja upange chumba chako utoke humu ndani. Mwezi ulipoisha alisema nifanyeje niendelee kuishi nanyi? Tukamwambia hakuna la kufanya ila kutoka unaruhusiwa tu kututembelea na tutakupokea vizuri maana ukiwa karibu tunajenga uadui, chuki na magomvi. Aliondoka na baada ya muda mrefu alikuja kututembelea. Siku hizi huja kututembelea na akija kuna tofauti ya mahusiano yetu, akija yeye, au na mke na watoto. Tunafurahi tukimwona. Kweli Mungu Ametuletea furaha katika majonzi yetu”

Dhambi ni shida kati yetu na Mungu na kati yetu na watoto wetu. Tunaongeza tatizo kwa kushugulikia dhambi wenyewe, dhambi zetu zinatufanya tuwe na picha tofauti yetu, hata ya wengine. Hivyo ni vigumu kujitegemea sisi wenyewe au wenye dhambi wengine kuwa tuko sawa kuzidi wengine. Endapo familia yako inahusika na matatizo ya dhambi yaliyotajwa au unayojua ila wanaona wako sawa. Haupaswi kuona kwamba hawafanyi dhambi, la!

Mungu Anajua dhambi zako na zao. Yeye anampenda mwenye dhambi ila anachukia dhambi. Ni rahisi kusema kuliko kutenda! Omba msamaha kwa dhambi zako, ujutie na kuziacha. Usiseme kwa mtoto wako, “Najua nina dhambi, ila zangu ukilinganisha na zako ni ndogo sana!”. Wajua umefiwa na damu ya thamani na kwamba kama mtoto wako mtu mzima anakaa dhambini ni vyema umwambie kwa njia nzuri na wala usitembee

ukimsengenya na kumwambia kila mtu unayekutana naye kana kwamba watu hao hawana mizoga yao.

Mara zingine hata upo tayari kumwachia kijana au binti yako ila anakuganda. Niligundua kwamba ninapenda kuwaburuza watoto wangu na ninawaendesha kweli na kuwa kama bosi. Nilikuza watoto wangu hivyo. Mume wangu na watoto na hata majirani waliniambia, ila sikusikia. Nikamwendea mtu wa nje anishauri akaniambia nikate kamba za kutawala watoto wangu watu wazima. Sasa nataka niache tabia hii. Nimewaambia wawe na maisha yao mimi sitawafunga tena. Lakini unajua ni nini kimetokea? Kila mara wananiweka kwa mambo yao wakinisihi niwaamulie. Sitaki wanipe majukumu yao! Wanataka yakifeli wanilaumu! Wananiambia kwamba hawajui kubeba majukumu kwa vile walizoea mimi nilikuwa kiongozi wao saa yote na kuwaambia cha kufanya na wanataka niendelee kushikillia usukani huo. Sitaki hiyo kazi tena natoka!" Wazazi wengine ambao wanakandamiza na kutawala watoto wakigundua wanataka watupe jongoo na mti! Wanawapa watoto talaka! Uhusiano ili uwe wa afya wabidi ubadilike ila isiwe kwa ghafla namna hiyo.

Pengine wazazi wapaswa kuepuka mambo fulani kama ushauri au msaada. Ila usipite mpaka hata kumkana mtoto mfano kuna mjane ana mtoto ambaye alikuwa akimburuza kwa ukali mwingi akiwa mdogo. Hii ni tabia ya mama huyu mjane hata kanisani anataka kutawala au kuendesha kila kitu na ameleta shida nyingi kanisani. Dada yake alipomtembelea tuligundua ana kijana mtu mzima waliyegombana naye mno akiwa miaka 22 na anasema kwamba hana mtoto". Kwenye kesi kama hii yule anayempenda Mungu ambaye alikuwa anamtawala mwingine, ndiye anayepaswa kumfikia yule mwingine na kujenga daraja.

Maana wale watoto watu wazima bado wana ile picha ya mzazi dikteta mpaka wapate picha nyingine. Yupi yuko sawa na yupi ana makosa isiwe hoja. Jambo kubwa ni mzazi kama anataka mahusiano na mtoto aweza kumfikia mtoto na kujenga urafiki. Ni kweli mtoto akizaliwa wazazi wanajukumu la kila kitu mfano, kumpa mtoto jina, kuamua mtoto atazungumza lugha gani, ataishi wapi, atakuwa na imani gani, au atatibiwaje au hata atasoma masomo gani. Hii ni sawa kwa vile mtoto hana uwezo wa kuamua ila watoto wanapofikia miaka ya kumi na wanajiuliza inakuwaje wazazi wana mamlaka yote hayo. Wanaanza kujichagulia mfano sipendi karanga ila napenda nazi, au napenda mihogo badala ya mkate.

Mtoto akikua na kuanza kutaka mamlaka ya maamuzi yake anaanza kuona mamlaka yanakuja na majukumu. Na ni hali ya kukua na ni njema na afya- healthy. Mtoto anagundua kwamba mzazi hawezi kutatua matatizo yote, na hata wanafanya makosa mengi na kwamba siyo Mungu! Ila watoto wengi hawataki kujitegemea na watoke kwenye kiota. Mambo ni rahisi wakifanyiwa vitu na mzazi kama pesa za matumizi, msaada wa gari, kununuliwa chakula na mengineyo. Mzazi ajue kwamba japo alifanya makosa kuwalea watoto sasa wamekuwa watu wazima wanawajibika kwa maisha yao wenyewe. Mzazi aombe msamaha kwa Mungu na kuwabariki watoto. Ikiwa mzazi ataendelea kuwafuga na chuki iendelee atawaathiri hata wajukuu wake. Jinsi wanavyoendelea kukulaumu kama mzazi watapenda waishi kama watoto tu wasikue kimajukumu. Pale tu watakapochukua jukumu na kusema "japo tulilelewa vibaya sasa tu watu wazima Mola tusaidie tukabiliane na maisha" watasonga mbele na kujisaidia maishani mwao.

Mara zingine watoto wanakosea na kugundua siku zimekwenda mfano tulimwambia kijana wetu tutamsaidia kusoma chuoni. Alitaka tumpe pesa zote akisema mambo ya usomi siyo yake, tulisema la! Msaada wetu ulikuwa kwa ajili ya shule tu. Sasa tumestaafu naye amekuja na kutuambia yupo tayari kwenda shule. Hatuwezi kulipia gharama ya shule kwa sasa na ni miaka mingi imepita, nasi tulishamsaidia kuchangia mahari na arusi yake" Mtoto akiwa mdogo, huona vitu vya wazazi ni vyake pia. Ila mara nyingi watoto bado wana mawazo ya vitu vya mzazi pia ni urithi wao kwa nguvu. Ni kweli watoto wengine wanajikwamua na kuwa na vitu vyao ila wengine wanabaki nyumbani.

Mzazi ajadili jinsi ya kumsaidia binti au kijana kujitegemea kama vile kumpa ardhi, au kitu cha kumsaidia ajikwamue kimaisha kadiri inavyowezekana. Wazazi tusiendelee kuishi na matatizo yale yale mwaka hata mwaka kama mtu mwenye jiwe kwenye kiatu ila hatoi. Ukiona matatizo yanayojirudia jitazame na wengine. Je ni wewe unayeleta tatizo? Je kuna jinsi ya kulitatua? Pengine ni wewe unayeweza kulitatua. Mfano binti yako anapenda kazi anayoifanya ila wewe wataka afanye kitu kingine "binti yangu anafanya kazi ya uhasibu, ila mimi nilitaka awe mwanasheria, najaribu kumwambia ila anaonekana ameridhika". Pengine ndoto za mzazi zisizotimia kama kupiga kinanda au kusoma chuoni, anataka zitimie kwa watoto wake kwa nguvu. Epuka ndoto hizo za mchana.

Mara nyingi tunafikiri watu wengine ndiyo wanatuletea matatizo, sisi tuko sawa. Mfano serikali, familia, kanisa, au jumuiya. Familia zingine zinafikiri matatizo yao yote yameletwa na mtu Fulani lakini si rahisi kujiambia ukweli kama wao wanafamilia wana makosa ya kujilaumu na kusahihisha.
"nilijitoa maisha yangu kutunza watoto wangu, nikawa mtumwa wao. Vitu nilivyotaka kuwa navyo sikuvinunua, kila kitu nilikuwa nafanya kwaajili ya watoto wangu. Sasa unaona nilichoambulia? Nina mahitaji sasa na hawanisaidii. Nina maradhi yaliyotokana na kuwatunza. Nimekuwa fukara kwaajili yao, kuwapeleka vyuoni. Sasa nimebaki mpweke, kwa vile nilikuwa nashugulika nao badala ya kujijengea marafiki wengine. Hawanijali, hawana muda nami. Nimewapa kila kitu changu na sasa hawanipi chochote."

Watu wengi huwa tunapenda kulaumu wengine, kwamba ni makosa yako ndiyo maana nimekuwa nilivyo. Kulaumu wengine kunakufanya usifanye majukumu yako. Wapaswa kujua kwamba watoto wamekuumiza, nawe umewaumiza. Shida zingine zinaweza kutokana na uleaji, pengine kuachana na mke au mume wako kuliwapa shida, au ulijali kazi yako tu, au unyanyasaji wa mwili, ngono au hisia umelitokea. Watoto wako wakubwa nao wana maneno ya kusema na haitasaidia kusuluhisha hata kama ni kotini. Kama ni kweli wajua kwenye moyo wako uliwatelekeza nao wajua, angalia yale mazuri katika mahusiano yenu japo ni madogo. Na watoto nao wachague yale mazuri, mtafute mshauri mwenye hekima za Mbinguni na kumtumia kuwasaidia. Yabidi mkubali makovu ya hisia yaliyokuwepo kama vile mtu anavyoweza kukubali kilema Fulani, angalia kile chaweza kufanyika katika kujenga mahusiano na kusameheana.
"mimi nilikuwa mvulana wa kwanza na nilimwona baba akimpiga mama na kuchukua wanawake wengine. Aliwapiga dada zangu pia. Alipompa mama talaka nilifurahi japo tuliishi kwa umasikini. Nimepata kazi nzuri, nimeoa na kupata watoto na naishi na familia yangu vizuri. Baba mkwe wangu amekuwa baba kwangu wa faraja mno. Nilipofanikiwa

kimaisha nikagundua kwamba simchukii baba yangu mzazi tena. Tunaandikiana barua na nazungumza naye kwa simu. Ninapiga magoti kumwombea na nashukuru kwamba hakuharibu maisha yangu"

Watoto wako waweza kuwa hawakufuata mifano mizuri uliyowapa, wakapuuza ushauri wako au imani yako au kukudharau wewe kama mzazi au kukuibia na kukuaibisha mbele ya jamaa na marafiki. Wakazidi kukuendelea kukulaumu kwa mabaya yao. Usikubali dhamiri yako ikushitaki kwa uovu wao. Ukiwa na maumivu ya watoto wako usibebe mzigo wote mwenyewe, haitawasaidia. Japo haukuwa mzazi mkamilifu ungama tu kwa makosa ambayo ni dhahiri yako na usijisulubishe kwa yale ambayo yanatokana na tabia zao dhaifu. Endelea na maisha yako. Ungama kwa kwa mapungufu yako kwa Mungu na kujua maisha ni zaidi ya uzazi. Chukulia yale yaliyobaki mazuri na familia yako na marafiki na tafuta vitu vya kufanya kukusaidia kupona vidonda hivyo. Usitembee ukipiga tarumbeta ya kulaumu watoto wako kila siku. Maana kuwasonda vidole na kuwalaumu itafanya wajihami, nayo haitajenga mahusiano. Nawe wakikulaumu usijihami, bali kwa upendo kama ni tatizo la suluhu na siyo kukabana mashati na kutaka kujua nani mwenye kosa. Isaya 30:20-21

Bwana atakuogoza kwa hekima ili usijikanyage, na pia usimlaumu mtu au kuzira mahusiano wakati ambapo watoto wako walitaka msaidiane kutatua tatizo. Bwana atakupa hekima pale pa kuomba msaada wa wengine na pale unapopaswa kufanya sehemu yako. Na kama unampenda Mungu usichukulie kama kiboko, kila mara kuwakera "mimi naomba saa yote". Pengine hata wao wanaomba, jaribu kufanya vitu vingine bila kujisifia mambo ya kiroho sana uonekane wewe ndiye unaomba sana ila wao hawaombi.
'Binti yangu ametumia watoto wake kama fimbo. Akiniomba pesa nisipompa, anawanyima watoto wake chakula kisha ananilaumu kwamba watoto hawajakula Kwa sababu yangu. Ametumia kitabu changu cha hundi kuforge sahihi yangu. Nilikuwa namwachia anipige na bakora zake za malaumu. Ila sasa nimeona kwamba simsaidii. Alipoenda jela kwa ajili ya kuforge kwa watu wengine sikumtoa, nilimwacha akae mle na ndipo akaanza thamani ya mahusiano yetu"

Jifunze kuwaambia watoto wako pale unapohitaji msaada au pale ambapo hupendezwi na jambo bila matishio. Jua kwamba kuna mengi usiyoweza kutatua, kama unasaidia mtoto wako angalia wewe mwenyewe usije ukatumbukia kwa vile huna nguvu za kutosha kukabiliana na tatizo hilo. Huwezi kutoa kile usichonacho. Wengi wetu tunataka kutatua tatizo kwa haraka. Ila mambo mengine hayana ufumbuzi ila jinsi ya kujua kuishi nayo bila kukuumiza (destroy you). Mungu mara zingine hutupa nguvu na si kujibu maombi papo hapo. Yabidi tukubali mapungufu yetu, na ya watoto wetu ila tusizae matatizo juu ya matatizo. Kumbuka wewe ni mwenye dhambi na Yesu Amekuokoa na wote wa dunia hii, wakiwemo watoto wako. Wote twahitaji msaada wa Mungu. Mungu anataka tuwe na umoja ila asema kwamba mara zingine watoto wako wanapingana na imani yako

Mathayo 10:34-37. Kama familia yako nayo yamwamini Mungu basi una nafasi ya kutafuta suluhu na familia yako. Yeye ni msaada kwa familia iliyosambaratika.
"baba ananisinya na mambo yake ya kanisa, kila mara ananikazania niende kanisani na kusema tuombe. Wakati tulipokuwa wadogo hakutupeleka kanisani. Nasi tulikaa tu. Sasa amepata uongofu kwaajili ya umasikini anataka anikandamize nao. Anakazana niolewe badala ya kuishi na rafiki yangu wa kiume wakati yeye hakuoa aliishi na mama tu. Pia

hataki ninywe pombe nami nilimwona akinywa kila siku. Sasa wamekuwa wazee na mama wanachugulia kaburi wanaogopa wataenda jehanam na hawana cha kufanya wala kibarua kama mimi ndiyo wananikazania. Ni shauri yao hawakunipeleka nikiwa mdogo”

Wakati mwingine kama mzazi hukuwakuza watoto katika maisha ya imani, alikuwa mtu wa dunia, Bwana ni mwingi wa rehema angalia katika mikutano ya familia kama wangekubali mwombe pamoja. Je mkikutana kwa sherehe je wanataka ufanye vile vinavyopingana na imani yako? Ukiweka hati ya mirathi (will) je waweza kuweka asilimia unayotaka kwa huduma za kazi ya Mungu? Maana ukifa hawatafanya matakwa yako au hata mazishi pengine watafanya yale ambayo wewe unafikiri hawamtukuzi Mungu. Wajulishe matakwa yanayohusu imani yako ili waelewe kwamba hili la imani ni kipaumbele kwako, kwamba wanaweza kuamini wanavyotaka ila mheshimiane imani zenu. Mathayo 5:44 inasema “adui wa mtu ni watu wa nyumbani mwake”
Neno kuu halisemi mimi nimwambie mtoto wangu au mwingine asamehe ila ni mimi nijifunze kusamehe na kuwa mpatanishi na kuwa muwazi ili watu waone mfano na kumtukuza Baba wa mbinguni.

Sura ya 19

WAKILI WA MUNGU

Sisi sote ni mawakili wa Mungu kila tulichopewa ni dhamana na tutatoa hesabu kwa mambo matano au sita hivi! Muda, talanta, mali, mvuto, mahusiano yetu, afya, na hata haiba zetu. Hatuwezi kupenda bila kutoa. Angalia marafiki zako na jinsi urafiki wenu ulivyo; mara nyingi una furaha nao na unajisikia vizuri kutoa hata usipoombwa, unacheka mpaka jino la mwisho kwa sauti ya juu. Je, Yeye Baba wa upendo anayetupenda na kutukirimia yote mema, vipi? Tujifunze kuishi bila uchoyo na ubinafsi, ndiyo tutapata furaha na afya ya kweli. Roho iliyochangamka ni bora kuliko dawa Sulemani alisema. Hakuja duniani na kitu na tutaondoka bila kitu. Kwamba tunapenda vya bwerere, au tunapenda sana kupewa kuliko kutoa si jambo jema

Pengine uwakili mkubwa kupita wote ni kusisitiza kwamba uwakili ni zaidi ya yale tuliyoyaorodhesha kwenye paragrafu ya juu, uwakili wa muhimu sana ni siri za MUNGU za wokovu au injili, kuwaambia wengine upendo wa MUNGU, rehema, huruma, msamaha kwa kifupi kuwaelezea watu wajue tabia ya MUNGU na upendo wake na kwamba anataka aishi nao milele zote! Watu watajua tu mawakili wa kweli wa MUNGU endapo watatuona sisi na watoto wetu tunapenda watu na tunatenda haki na kuwa wanyenyevu na kupenda rehema.

Mjane wa senti mbili alipongezwa si kwa sababu ya vijisenti viwili alivyotoa, bali kwa vile alivyobakiza nyumbani! Mara nyingi tunatoa makombo yetu na vile vinavyotuzidi kwa masikini yatima, wajane au wahitaji. Ila watu tunawaowapenda tunawapa vitu ambavyo pengine hawavihitaji na huku 'tumekomba sufuria lote,'. Tujihadhari na hili limenihusu mara nyingi pia, naomba hekima kulikwepa.

Kutoa ni kwa ajili ya usalama kwetu na watoto wetu ili tusiwe na tamaa au wivu. Amri ya kumi ni ngumu kuliko zote kutekeleza, maana huioni! Ni rahisi kuona viwivu viwivu kwa wale walio na vitu kama wewe huna ukijaribu kuwapangia bajeti jinsi ambavyo wanapaswa kutumia pesa zao kusaidia watu, ikifika zamu yako kupewa na Mungu hizo, unababaisha babaisha kwa kuwapa chenji chenji watu wenye mahitaji, ila watoto wako unawapa vitu wasivyohitaji na wanaenda kujisifu. Watoto pia nao wataiga mifano yetu.

Rockferller tajiri wa Marekani mkubwa wa mafuta ya Petroli, alikuwa bahili na mchoyo wa mali yake, mwenye hasira na huzuni (miserable). Alipofika umri wa miaka hamsini, aliugua sana. Rafiki yake mmoja alimshauri awe anajitoa kihali na mali kwa wahitaji na atapona na kuishi vizuri. Alijaribu hili, na aliishi miaka tisini, akitoa ajabu! Kuna hata kitengo cha Rockfeller (foundation) kikisaidia mashule, scholarship, vilema n.k. Tusifikiri kwamba watoa kwa vile wanavyo! La hasha! hiyo ni nusu tu ya hadithi nzima. Mara nyingi nimekuwa mchoyo na kukumbuka hadithi niliyosoma nilipokuwa darasa la kwanza. Kwamba mama mmoja alikuwa mchoyo sana. Naye alikuwa na watoto wakambo waliomtembelea Alipoishi alikuwa na mtego wa paa ambao mume wake aliweka; aliposikia sauti, alijua paa amenaswa. Akaona kwamba wale watoto watafanya asifaidi ile nyama peke yake na mume wake na watoto wake. Aliwaaga wale watoto wakambo waende ghafla kama akiwafukuza waende kwao. Kuja akaangalie mtego kumbe ni chui, naye akamvamia na akauwawa kwa vile hakuwa na msaada wa watu wengine.

Mara nyingi nimetaka kupata mwenyewe ambapo ningealika wengine tupate pamoja nikakosa kabisa. Nimekutana na wale wanaokataa kugawa vitu vyao, hata iwe mirathi na kubania na mwishowe ikaliwa na tunutu, au kuleta huzuni nyingi. Mtu hapati furaha kwa vile alivyo navyo. Furaha yaja kwa kumjua Mungu, kumtumikia na kuhudumia watu. Furaha ya ajabu nafikiri ni Mungu mwenyewe anatoa, ukihudumu au kutoa kitu, unajisikia unavamiwa na tabasamu (smile attack) hata kama umevaa kiraka, una furaha kuliko wanaoishi majumba makubwa. Kuhusu majumba makubwa fasheni hii imeingia ya kujenga majumba makubwa ila hatukaribishi mtu. Tunajenga tupate sifa, na mtu anaweza kusaidiwa na mtu mwenye nyumba ya majani kuliko sisi wenye nyumba kubwa. Wengine tulianza mahali pagumu tukitembea bila viatu, tulipoona wale wenye viatu vingi tulifikiri wana roho za ukatili, kwamba wangetufikiria tu wangepata thawabu. Leo hii hatutoa vitu vya maana kwa mtu, tunanunua nguo Ghali mno, na zikituchosha ndiyo tunampa mtu ili aonekane alipewa na sisi.

Vitu vya dunia vinapungua thamani, leo ***nanunua kitu kipya na kesho huwa najiuliza***. “kwa nini nilipoteza pesa zangu na kitu ***hiki*** kibaya au kibovu, mbona hakivutii”. Wengine wadai wakitoa kusaidia kazi ya Mungu ‘zangu zitaliwa kanisani, hekaluni au msikitini.’ Hivi kama nimempa mtu pesa ya kumpa mzazi wangu, naye akatumia nitaacha sasa kumpa mzazi wangu pesa kwa sababu ya wizi wa niliyemtuma? Kama kuna watu

wanakula pesa za kanisani, washitaki wachukuliwe hatua. Usimpunje Mungu wako na kukosa baraka kwa watu wapitao kama moshi. Endapo unafikiri umempa Mungu sana, uwe na amani moyoni Yeye si dhalimu, atakurudishia ile ambayo unafikiri umezidisha! Ila kumbuka zaka yaani moja ya kumi ya mapato yako ni ya BWANA. Yaani Neno linasema ukichukua hiyo si wizi bali umepora kama jambazi mwenye silaha (rob). Jambazi ni yule anayechukua kitu cha mtu, mwenye kitu akiangalia, na kwa nguvu au silaha. Mrudishie Mungu 10% ya mapato yake, ili ubarikiwe au niseme ili usilaaniwe. Mwizi anaiba kwa kunyemelea wakati mwenye mali haoni, ni kama mdokozi hivi. Muumini asiyetoa zaka, anafanya ujambazi kwa kifupi.

Wanasema, “Nionyeshe ratiba yako ya siku na bajeti yako, nitakwambia usongo wako upo wapi.” ‘Show me how you use your time and your money, I will tell you what is your passion.’ Pia hundi Ni karatasi inayoonyesha upendo wako Kwa Mungu (Your cheque book is a theological document). Theology ni mafundisho yahusuyo kumpenda Mungu na kumjua. Usibanie banie vitu Na kuwanyima watu wasio na uwezo, ukiwapora vitu kwa namna mbali mbali. Tukifa hatutazikwa na vitu ila tunaweza kuvitanguliza leo mbinguni, vitungoje huko kwa kusaidia wenye mahitaji na kutoa sadaka kwa Mungu anayetupenda kupindukia.

Kila mtu ana talanta ya muda, hakuna asiyekuwa nayo! Ni kweli pengine hatuna mali, ila muda je? Tumia muda wako na karama zako za roho vizuri! Maana karama za Roho tumepewa kubariki wengine.
Soma vitabu vya uwakili Kama “The Blessed Life.” Tumia muda kuiombea kazi hiyo pia. Utashangaa utakavyopata upendo na furaha. Nilishangaa sana kwamba bilionea wa nchi masikini kama India ana nyumba ghali kupita yeyote duniani, dola bilioni mbili! Wakati ambapo Warren Buffet bilionea wa pili Marekani, alisema kwamba yeye anaishi nyumba ile ile aliyoishi miaka hamsini iliyopita ya vyumba vitatu vya kulala! Anatembea na gari la kawaida na anaishi maisha ya kawaida. Amehojiwa na wengi; historia ya maisha yake waweza kuipata kwenye web. Watu wengi wa nchi zinazoendelea wanaweza wakawa kama yule mtu ambaye hakutegemea atapata na wanafuja na kuonyesha visivyo kawaida. Watu wawili hawawezi kuwa matajiri kamwe nimefundisha somo hili kwenye uwakili nchi kadhaa kwenye mabara manne. Mwafrika na anayempenda Mungu. Mwafrika ana ndugu na jamaa na marafiki masikini weengi na jumuiya yake ina mahitaji mengi, hata leo ningepata dola bilioni mia moja ningekuwa na mengi ya kufanya kwani mtu anayempenda Mungu apaswa

kujua tunaishi kijiji kimoja cha dunia. Albert Sweitzer aliyefanya kazi Afrika ya magharibi kama tabibu alisema wewe umewekwa na Mungu duniani, na kumbuka una kaka zako wahitaji. Daktari huyu alisaidia afya za watu nchi hizo kwa miaka mingi, maisha yake yanapaswa kusomwa na kila mmoja wetu. Tajiri Rockfeller alipofariki, mhasibu wake aliulizwa na gazeti "Je, aliacha fedha ngapi?" Alijibu, "Aliacha zote!" he left it all.

Hata tukiwa na vitu vingi hatuwezi kuvitumia. Naweza kuvaa viatu jozi moja kwa wakati mmoja, au kulala kwenye nyumba moja kwa wakati mmoja au kuendesha gari moja kwa wakati mmoja. Na hata tukiwa na pesa sana hatuwezi kula Tanzanite au dhahabu. Tutakula wali, maharage, ugali au mboga tu. Tufundishe watoto wetu kuwa wakarimu na kusaidia wale wenye mahitaji kwa hali na mali.

Maisha yetu duniani tukizaliwa tunasema wacha ngoja niende shule nitakuwa na raha na kuridhika, kisha tunasema wacha nipate kibarua au nichume hela nitakuwa na raha, kisha wacha ngoja nioe na kuwa na watoto nitakuwa na raha, kisha wacha nistaafu nitakuwa na raha, kisha wacha nipate wajukuu nitakuwa na raha, kisha wacha watoto wajitegemee basi nitakuwa na raha, mwishowe uzee unaingia na tunasema mimi sina raha na siku hizi mara magonjwa na udhaifu, kisha kuwategemea watu kunaingia. Bibi yangu mzaa mama mwaka wa 1969 alikuja kututembelea tukiwa Arusha, alikuwa na miaka 48, nilimwona ni mzee sana, nikasema bibi wewe ni mzee hivi. Alinijibu 'Grace nilitazama tu upande huu nikigeuka nikajikuta ni mzee!, haikuchukua muda, hata wewe utazeeka na utashangaa miaka imeenda wapi!'. Ni kweli nilikuja Marekani nikisema nitakaa miaka sita mpaka leo nimekaa miaka mingi nje ya nyumbani Zaidi ya ndani, na sasa nina umri wa miaka kadhaa kumshinda bibi mwaka 1969, na nashangaa hivi muda umeenda wapi?

Hatukuja na vitu duniani na wala hatutaondoka na kitu. Isipokuwa tunaweza kutuma vitu vyetu mbinguni kabla ya wakati (advance) kwa kufanya matendo mema, ndipo nondo na kutu hawatakula mali zetu hapa duniani. Toa vitu vyako mpaka ikuume, si vile ambavyo ulikuwa unataka kuvitupa. "Nilikuwa na njaa ukanilisha, nilikuwa na kiu, ukanipa chakula, nilikuwa uchi ukanivika, nilikuwa gerezani ukaja kunitembelea," tunaambiwa kwenye Neno kwamba hiyo ni pasipoti ukifanya kwa moyo wako na siyo kulazimishwa. Hebu tuombe hili ili tuwe mawakili wema, na tusije ambiwa, "Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari ibilisi na malaika zake.". Mimi kwa neema ya Mungu sitaki kwenda motoni, wewe Je? MUNGU atatuhukumu kwa mabaya

tunayotenda, na pia yale mazuri ambayo hatutendi (commision and ommision).

Neno la Mungu lasema ufalme wa Mungu ni kama lulu kubwa ambayo mtu alipogundua katika aliuza kila kitu na kwenda kuinunua. Tukiwa wadogo tuliimba wimbo wa sauti ya Yankee Doodle, “Mkulima mwenye shamba alipanda viazi, akachimba chimba akaona almasi. Lo! Lo! Bahati ya mtu mwenye shamba, akatupa jembe upande akaenda zake mjini, kununua gari lake sasa ni tajiri. Lo! Lo! Bahati, Loo; Loo; bahati ya mtu mwenye shamba.” Ufalme wa Mungu ni kitu cha thamani, kwako wewe mpenda afya ni vyema uuze vyote na kununua huo. Usikazane kujiwekea hazina duniani sana na kujawa na tamaa ya pesa, maana kwa maumivu watu wengi wamejichoma sana. Watu wengi wamefanya mambo ya ajabu kwa ajili ya pesa, “Shina la maovu yote ni kupenda pesa.” Pesa itakubadilisha tabia, jihadhari, watu wengi wakiwa hawana pesa wanajua jinsi ya kuangalia wengine na kuwaona udhaifu wao wa tamaa ya kupenda pesa; ila wakiwa nayo wanajisahau kwamba na wao wana shida hiyo hiyo. Mara nyingi tuna tamaa ya vitu moyoni ila haionekani kwa vile tu maskini. Masikini ana tamaa pia ila hana nafasi watu waione (opportunity). Kamwe usiache kurudisha zaka (moja ya kumi). Hebu watoto wako wafundishe watoto wako kurudisha zaka na sadaka na kutoa sadaka. Buni miradi na kuwalipa hata kama ni pesa kidogo ili waweze kutoa sadaka kutoka katika akiba yao wenyewe, na si ya mzazi wakifika umri wa miaka nane hivi.

Kuna tabia ya wengi wetu kuwatendea mema wale tunaowapenda na si yeyote yule anayehitaji msaada wetu. Hata watu wabaya wanafanya hivyo kwa ndugu zao na marafiki zao. Utamaduni wa sisi waafrika kumpa mtu tusiyemjua ni mgeni. Kama ni watoto yatima tutatunza wa ndugu zetu, kama ni kumsaidia mtu tutasaidia ndugu zetu. Hiki nawasifu ndugu zetu wazungu sana kwani wanaweza kumpa mtu wasiyemjua hata shirika au taasisi fulani, kama vile watoto yatima, utafiti wa kansa n.k. Sisemi usahau ndugu zako; la, hasha! Kusahau ndugu zako ni kama kuwa kafiri. Ila katika ukarimu wako, ukisaidia watoto wa ndugu zako yatima sita, msaidie na mwingine mmoja usiyemjua mwenye mahitaji.

Nimekutana na mhubiri mmoja na mke wake, aliyeniambia yeye kipato chake ni kidogo na ndiyo maana hatoi zaka. Nilimwuliza anakula nini na kuvaa nini? Je, ana shamba? Basi atoe mazao yake. Wanawake wengi

au waume wengi wamewakataza wenzi wao kutoa zaka, **usiingie** dhambi hii. Watu wawili wanaona vitu kwa ubora kuliko wewe peke yako ukiwa ndiyo bosi wa kamati ya mtu mmoja kuamua pesa zitumiwaje nyumbani mwako. Zaka ni kwa ajili ya manufaa yetu na si ya Mola. Yeye ana kila kitu. Nikimpa senti mbili tatu zangu au nikiacha, yeye hawi masikini kamwe; ni kama mtoto wako mdogo unayemfundisha asiwe na uchoyo kwa kumwomba kiazi kidogo ulichompa akumegee. Hata hivyo kama unafikiri umempa Mungu zaidi ya unavyopaswa kumpa, Yeye si kama mfanya biashara anayengoja uende bila chenji kamili ili aichukue! Yeye ni mwaminifu, na kama ulimpa kupita inavyotakiwa, atakurudishia tu! Hakuna aliyetoa kwa Mungu akafilisika. Haleluya!

Wakati Musa akiandika Torati na kuongoza wa walikuwa na mafanikio ya kupita mpaka walikuwa wa ikitoa 33%; ambayo ni theluthi ya mapato yao! Kulikuwa hakuna aliyekuwa na njaa. Jumuiya ***ilibuni*** vitu vya kufanya ili kila mtu awe na kitu cha kumudu maisha au kupata riziki za kukidhi malazi, makazi na chakula. Mpangilio wa Mungu daima unakufanya uwe na heri na fanaka. Wape watoto wako na watu mitaji ya kujiendeleza na wasimamie ukiwa na ujuzi au umtafute mtu wa kuwaendeleza. Watu wengi wenye uwezo wanalia lia, au wanakuwa matapeli kuwaahidi watu mambo makubwa kisha hawaonekani wanayeyuka tu. Wengine walipokuwa hawana uwezo walifuata watu wenye uwezo daima, walipopata ahueni walisahau watu. Walikumbuka watu walipohitaji connection au kupata wateja wa kusikiliza ukubwa au maendeleo yao yalivyo. Wazungu husema huwezi kumpa Mungu zaidi ya anavyokupa, eti umuovertake, haiwezekani “You can not outgive God”. Anza kumtumikia Mungu na kumpenda Mungu kwa usongo na ushujaa mwingi. YEYE atakuwa njozi, utume, usongo na nyenzo (vision, Mission, Passion and provision)

Mvuto wako ni muhimu sana. Watu wanapokupenda na kukutetemekea, usitumie nafasi hiyo bila kuwa na hekima. Nilimjua Dwight Nelson mhubiri kule Michigan. Siku moja nikiwepo alitoa kisa cha safari yake, wiki hiyo. Alisema aliendesha kwenda Califonia akitoka Michigan, umbali wa kama kilomita 4000. Gari lake lilikuwa Honda ***kuukuu***. Alisema aliharibikiwa gari, mara saba hivi. Baada hotuba yake, wiki iliyofuata walijitolea kama watu kumi hivi kumnunulia gari jipya! Alikuwa na mvuto (influence). Angeweza kununua gari lake, ila aliwaambia watu wale walete hizo pesa waingize kwenye huduma yakusaidia wenye mahitaji. Je una yatima wangapi, wajane wangapi, masikini wangapi au wageni wangapi

unawaosaidia leo katika maisha yako. Naomba utafakari maaana ndiyo utu wa binadamu na dini ya kweli ilipo. Jipime na jichunguze leo. Je una magari yamezagaa zagaa nje ya uwanja wako, na utakapoaga dunia watagombania watu ambao hawakuyatolea jasho? Basi anza kuyagawa mahali penye mahitaji. Tajiri Colgate alimpenda Mungu sana, alitoa zaidi ya 10% kwa watu wenye mahitaji na kusaidia kazi ya Mungu ili watu wengi waende mbinguni, ila alipokufa alisahau kuandika mirathi. Watoto wake hawakujali watu wala Mungu na wakatumbua zile pesa wakisahau yale baba yao aliyoyasimamia. Leo hi weka mirathi, haimaanishi utakufa haraka ukiweka mirathi. La hasha. Watoto wako uwape vitu vichache tu vya kusaidia wawe na bidii ya kazi na kuendelea kuendesha maisha yao bila ufukara sana. Unapowakuza waonyeshe wewe unajali masikini, wajane, na yatima na kujilinda na mawaa.

Kutotoa zaka Ni kama ukimtembelea mtu ukiwa umempelekea kapu la vyakula (shopping), na vitu vingine kama zawadi, halafu ukishaondoka anakatalia hata lile kapu. Kiafrika, hata hapaswi hata kurudisha lile kapu likuwa tupu. Atajitahidi atafute hata kitu kidogo aweke ndani. Utamwonaje huyu mtu? Kwamba hana shukrani hata kidogo. Ndivyo tunavyomtendea Mungu wetu. Baada ya kutukirimia na mengi, tunakatalia hata kapu! Lakini tukitoa tunabarikiwa. Alisema tumjaribu, tuone kama Hatafungua madirisha ya mbinguni na kutumwagia mibaraka. Watu wengine wamebarikiwa kutoa zaidi ya 10%; walipobarikiwa kama mfamasia mmoja kule Uswiss, alitoa 90% kama zaka maana alibakiwa na mahitaji yake yote. Usijali vitu vidogo vidogo kwa ubahili unavihesabu.

Kama una nyingi, fanya kama ujumbe wa Yohana mbatizaji “Mwenye makoti mawili ampe moja mwingine”. Ukiwa hauongezeki saizi huna haja ya kununua nunua nguo na vitu. Msafiri wa mbinguni pesa zako zilete roho siyo vitu. Hata hivyo Roho Mtakatifu, si roho ‘Mtakavitu’ kama asemavyo rafiki yetu mwinjilisti. Rahisisha maisha yako, wanasema vichache ni vingi (more is less). Yaani una vichache kwa kutazama ila moyoni una furaha na mengi yanayoburudisha roho mpaka unajiona tajiri zaidi ya Bill Gates kwa vile Mungu amekupa roho ya kuridhika, na amekupamba, hata ukivaa kitu kisicho cha thamani watu wanauliza umepata hiki wapi jamani? Unanawiri ni ajabu. Nafikiri mbinguni patakuwa pazuri si sana kwasababu ya vitu bali kwaajili ya furaha moyoni, yaani pale kwenye mto maji yakitiririka, unaburudika, na kutabasamu, na wapendwa nao wanafurahi nawe, mnapiga masoga, kisha Malaika wanapita kuja kukaa nanyi, kisha Mungu anazungumza nanyi. Hata usipewe kitu yaani taabu zako zimeisha, hakuna

kifo, huzuni, vilio, maumivu, wala yote mabaya. Si mambo ya vitu la! Dhahabu kule itakuwa lami tu ya kila kinjia.

Ukiwa una talanta, una sura nzuri, haiba nzuri, mwandishi mzuri, n.k tumia haya yote kwa kuongoa roho. Siyo yakuletee kiburi, kwamba "Mimi ndiyo mwenyewe." Uwe mnyenyekevu. Unajua mnyenyekevu hajitambui? Mtu mmoja aliyekuwa mnyenyekevu sana hata alipewa medali na kijiji chake ya unyenyekevu. Siku iliyofuata alipoivaa, ilitwaliwa, kwa vile alikuwa anajitangaza unyenyekevu!

Panga bajeti yako vizuri ili usiwe na madeni madeni. Hali ya madeni na hasa ya nyumba imenipata; naomba usiku na mchana yanitoke. Ogopa madeni kama vile ukoma. Wiwa upendo tu. Ukiwa na madeni unampunja Mungu sana kwa kulipa madeni, maana waweza kwenda jela. Na hilo wengi twaogopa kuliko kumwibia Bwana; hata kama hutoi sadaka au zaka bora ulipe deni; ni hatari. Hata tunasema eti Mungu anaelewa kwamba nina madeni, nisipotoa zaka na sadaka.

Jifunze bajeti uishi kutokata na kipato chako. Usinunue usichohitaji au kuishi kwenye madeni. Wanaume wengi wanapokea pesa, na kupanga matumizi wenyewe. Mke ana mahitaji mengi, hasa kama hafanyi kazi. Ila fanya hivi: Jiweke kwenye viatu vyake, kwamba yeye ndiye mwenye mshahara nawe huna senti bali hakushirikishi kabisa, mradi anakupa taarifa kidogo hapa na pale inapobidi! Watoto wa nyumba hii wanagundua wakianza kufanya kazi wanamtumia mama tu na wala si baba. Kule Kisii watoto wengi walianza kuchukua mama zao kwenda Nairobi wakiacha mababa wabahili wenye roho mbaya wakijipulizia moto na kuchemsha ugali wenyewe. Baba hawa walikasirika maana walisaidia watoto kusoma kwa kiasi ila wakiamua tu (at their convenience). Wengine naoishi nao karibu wameleta mama zao ughaibuni, baba akawa anatoa dua lisilompata mwewe, yaani mke, ila linawapata watoto. Watoto wanapaswa wajali wazazi wao, hata kama wazazi hawakujali. Ni dhambi kumtelekeza baba hivyo au mama. Mama huyu apaswa amtetee mume wake na mzazi mwenzake. Mara zingine wakina mama wanaleta picha kwamba wameteswa sana na wanakuwa si wakweli kusema mema mengi ya mume wanavyopaswa. Tujihadhari sana tutachuma dhambi kwa Mungu. Nakumbuka nilipogombana na mume wangu na kukasirika mtoto wangu wa miaka saba aliniuliza na nikamweleza, akajibu 'mama usijali, akija baba toka kibarua mimi na mdogo wangu tutamchangia tumpige'. Mdogo wake

alikuwa na miaka mitatu. Hapo ndiyo nilingamua kwamba hata mimi nilikuwa na makosa makubwa tu kwenye huu ugomvi. Hata mume wangu ndiye alikuwa sawa. Na sasa nataka kuwaingiza watoto wadogo kwenye chuki na ugomvi wa muda mrefu na kisha walaaniwe kwa kumchukia baba yao na kutomsaidia kweli? Niliomba Mungu anihurumie na kunisamehe. Najua amenisamehe.

Zamani nilipokuwa sina madeni nikisikia mtu ana shida nilitoa. Siku hizi nalia lia madeni! Madeni! na wala sitoi. Tusaidiane kuombeana tabia hii tukome na Mungu atupe vipato. “Niende mbele za Bwana na mikono mitupu?” Ulisema wimbo wa watoto. Ni aibu, kama wewe ni maskini, na huna yaeleweka; ila ni aibu na si baraka kwako. Fundisha watoto wako kutoa sadaka na zaka. Wakuone unaitoa kila inapotolewa ibadani Sabato. Wafundishe jinsi ya kutumia pesa, najaribu hilo kwa watoto wasije wakakumbwa na yaliyonipata. Utasaidiaje watu wanaohitaji kusaidiwa kama unakopa kopa, na ambavyo si vya lazima. yatima au huduma fulani za kushuhudia watu na kuwaleta kwa Bwana.

Usisahau kutunza jamaa, “Mtu asiyetunza jamaa zake ni mbaya kuliko asiyeamini.” Wengine waambiwa wazazi wao ‘Korban’. Hii inamaanisha kwamba hawawezi kuwasaidia kwa vile vitu vyao vimewekwa wakfu. Mtu ambaye ana kitu na anashindwa kutunza wazazi wake au ndugu zake ni kama kafiri. Naelewa ndugu wengine hutawaweza, wana tamaa kibao, na wanaona wivu ukifanya kazi ya Mungu.

Ndugu zako na hata mke/mume wako, watakuendesha usisaidie watu wenye mahitaji. Watatazama kwa wivu unampa nani, nini na kusema wawafanya wawe masikini. Japo sijaona anayemsaidia masikini akawa masikini. Ahadi za Mungu ni za kweli kabisa. Na wengine wakiona unapatana na mume wako au mnaishi vizuri kwa amani na kumfanyia kazi Bwana; na miji yao wanapigana pigana atasema “mke wake kamkalia.” Tafsiri yake, mke asipendwe, akipigwa kofi ndiyo mambo sawa! Au, ‘wanajidai wazungu.’ Hivi wazungu ndiyo walikuwa Edeni kwanza au ndiyo wanaopendana kuliko waumini kweli? Hivi wao ndio wana upendo wa agape kweli? Mbona wanaachana kila kukicha na ***kesi za***kuuana ni zaidi ya kwetu? Au utasikia “wanajidai tu tutawaona, wataachana tu!” Hivi wewe unaombea maanguko ya wenzako tu?

Mtu mmoja alifurahi na kucheka wakati mtoto wa mwenzake anaharibikiwa akisema, “Amejiunga kwenye kundi letu. Amekuwa kama sisi, au watoto wake watakuwa wabaya kuliko wangu!” Na huyo mtu hakukuuliza kuhusu

ya watoto wako hata pengine alikuombea. Mtu mmoja alimwona bwana mmoja akimfungulia mke wake mlango wa gari akasema, “Mambo mageni haya; nafikiri ni mke mpya au gari jipya!”. Usiwe mtu wa kutaka wenzako washindwe, waombee. Mungu bado ana uwezo, mbona Sauli akawa Paulo bila hata yeye mwenye kuomba?

Tuliishi na rafiki yangu na mke wake Michigan. Walinionyesha barua waliyoandikiwa na kaka yao aliyewasomesha wakiwa sekondari, “Mpendwa tulikusomesha, na tumekuambia utununulie lori na trekta, mpaka leo hujatununulia, umeenda Marekani na sasa umebadilika, tutaomba Mungu akukatekate miguu ndiyo utatukumbuka nasi, na kutuona wa maana!” Rafiki hawa walilia machozi, kwani walikuja kusoma kwa kujitegemea, na walikuwa wakisaidiwa kodi na kufanya vibarua vidogo vidogo vya kubangaiza ili kuponea maisha (survive). Utakumbana na jamaa wa namna hii, ila hilo lisikupe homa ukaacha kuwasaidia wenye mahitaji ukiwa nacho. Kila siku ukiamka, mkabidhi Bwana mipango yako na umwombe akuongoze.

Tembea na vitabu na visome ukiwa unangoja mahali. Wape watu zawadi ya vitabu vizuri. Sio kutabasamu na kukenua nao meno tu, bila ya kuwapa kitu Chema kama unacho. Mvuto si wewe ukwezwe, bali Mungu aonekane katika maisha yako. Hata ukiwa umejaliwa nyumba nzuri, karibisha watu na uwaambie kwa upendo hukumu inayoijia dunia karibuni. Unajua Maandiko yanasema Mungu ana vitabu vitatu. Kimoja ni cha kurekodi mambo. Vitabu hivi vitaletwa hukumuni siku moja na kila tendo tulilotenda liwe jema au baya litaletwa. Filamu ya maisha yetu itapita pale na kila tulichofanya kitaletwa cha kila mmoja wetu. Unayakumbuka yale mambo unayoyafanya ya siri, ambayo hutaki hata mume, mke,mtoto, dada, kaka, bibi, babu, mjomba,mpwa, shanazi, au mtu yoyote ajue? Yote yataletwa. Ila zile dhambi tu ambazo zimeungamwa hazitaletwa. Mungu akitusamehe anafuta yote na mfuto wake mkubwa na kuzika dhambi zetu chini sana kama baharini Pacific kule Mariana Trench ambayo ni maili saba. Japo dhambi zetu ni nyingi na nyekundu kama damu zinakuwa kama theluji ya mlima Kilimanjaro tukiziungama. Je, leo mpendwa msomaji umeungama dhambi zako na toba ufungue ukurasa mpya wa maisha yako?

Mifano mingine ya kuonyesha watoto wako ni kwa kusaidia watu ili wajisaidie; siyo wakutegemee. Kwenye kitabu cha Ron Sead Rich, kwenye kitabu chake cha “waumini matajiri kwenye ulimwengu wa njaa, anaeleza

mambo ya ajabu mno! Anasema utafiti umeonyesha kwamba, Mwenyezi Mungu Amekuwa mwaminifu ni ajabu, (nitakufanya kichwa na wala si mkia)! Akasema 80% ya utajiri wote duniani umo mikononi mwa waumii wanaokiri Jina la Mungu. Akasema shida ni mabahili ajabu! Mungu ametubariki na matrilioni ila tukitoa msaada kwa maskini tunatoa chenji, chenji tu. Badala ya kupanga program za kuwakomboa watu wasitutegemee. Badala ya kutoa jozi ya ng'ombe, mbuzi au miradi itakayozalisha, tunatoa unga au kitu ambacho watakula kisizae ili kesho watuombe tena! Huu ni ukatili wa aina fulani. Ni vyema mno watu hawa uwape elimu, na mitaji midogo midogo ili wajikwamue. Wasiwe daima mbele yako wakikufagilia na kukusujudu tu.

Wachina wasema ukitaka kufanya tofauti kwa siku moja kula chakula kwenye hoteli nzuri. Ukitaka kufanya tofauti kwa mwezi mmoja oa/olewa (mfano mbaya). Ukitaka kufanya tofauti kwa mwaka mmoja panda bustani. Na ukitaka kufanya tofauti maishani 'panda mtu;' yaani saidia watu kupata elimu, au peleka watoto shule. Utakuwa umemkwamua mtu.

Mara nyingi tumejikuta tukisema kwamba masikini hawa ni waongo, hawahitaji msaada, na pengine ni wavivu. La! Ajabu tulipokuwa na hali mbaya au maskini, hatukufikiri haya, tulitaka tusaidiwe, na tukashukuru. Sasa tukiwa na hali nzuri tunapepeta mengi kuhusu jinsi ya kusaidia watu na kusema lazima nichunguze mno, kwani hawa watu ni waongo. Nimechunguza mara nyingi na nikagundua ni lazima niwe mwangalifu, kwani ni Mungu anayepima waongo na tochi yake. Hajanikabidhi kazi hiyo, au wewe amekukabidhi? Wengine tumesema, nikimpa msaada, aenda kunywea pombe, ni kweli, ila ni lini wewe, utamsaidia mjane, yatima au maskini ukifanya machambuzi haya mengi? Maneno ya "Nilikuwa na njaa, kiu, uchi, jela;" haikuzungumzia kwamba ufanye utafiti. Mungu atajaji. Hatusemi uwasaidie watu wasiohitaji, ila wengi wetu hatuko tayari kutoa, na tunapata sababu ya kuchelewesha utoaji au kutotoa, kwa kisingizio cha 'utafiti wa mwongo asiyehitaji msaada.'. Mara zingine nimependa kuangalia picha za maafa ya watu, watu kwenye mafuriko, tunaona kwenye runinga au kwa macho "yulee anaenda masikini". Ila hata senti hatutoi, na wala hatuwaombei kama hatuna senti. Hivi ni haki kweli, maafa ya watu yawe burudani yasiniume hata nitoe dola moja ya kusaidia mtu anayepatwa na huzuni vile?

Usiache mtu akuombe ombe na kukutegemea. Waumini wengine ni wachungu au bahili sana wakiwa na vitu, ila wanapokuwa hawana wanajua jinsi ya kuwapangia walio navyo kufanya kazi ya Bwana au huduma. Tunavaa nguo na vitu vya fahari, rafiki toka Tanzania alijisifu kwangu eti suti yake ni ya dola 5000! Ila tukisikia watu wenye shida tunatoa chenji chenji ndogo ndogo tu, na tunafikiri tunawabwaga watu, kumbe maskini tunajibwaga vibaya!

Nashindana na uchoyo, na kuomba Mungu kila siku niendelee kutoa; maana hatuwezi kumgusa Muumba bila kugusa viumbe vyake. Wengi tu 'shaba iliayo na upatu uvuma'. Hata ukiwa na vitu vingi sana; huwezi kuvaa viatu viwili kwa wakati mmoja, kuendesha magari matatu kwa wakati mmoja au kulala vitanda viwili kwa wakati mmoja. Hata nikikutembelea hauwezi kusema leo hapa ***tutakula*** dhahabu na almasi. La; hasha! Utakula ugali ule ule na mboga ***ile ile***, au vyakula vya kawaida tu, la sivyo matumbo yatadhurika! Toa vitu vyako mpaka vikuume, siyo kutoa chenji chenji hata zikidondoka mfukoni mwako ***huzitupii jicho.*** "Mjane wa senti mbili, alipongezwa kwa vile alivyobaki navyo na siyo alivyotoa"
Angalia kama nyumbani mwako kuna vitu vilivyozagaa zagaa, vitoe. Mama mmoja aligundua ana kaseti na DvD kama 200 hivi ambazo alikuwa ameangalia na wala hazitumii! Aliamua kuziuza na zile pesa atumie kwenye kazi ya Bwana. Usiwe mtu wa kulundika vitu vya bohari, ukifikiria kwamba kesho utapata shida na kuvihitaji, wape wengine na Bwana hatakutindikia kesho. Siyo mzungu tu eti anatoa kwa mtu asiyemjua, la Mwafrika pia, maana anajua uchungu wa umasikini.

Ndugu yangu toka Mara, niliona amejaza nguo tele kwenye makabati yake, hata vyumba vingine. Nguo nyingi za watoto za zamani. Anakaa nazo tu akikumbuka watoto wake walivyokuwa wadogo walivaa hichi au kile kiatu mguu wa mtoto ulikuwa mdogo! Shida hii nilikuwa nayo pia, mpaka rafiki yangu, Grace Zuzo wa Afrika kusini aliponiambia, "Ukiwa na nguo 20 au 30 zatosha kwenda kibaruani, na nguo yoyote ambayo huivai zaidi ya mwaka si yako wape watu wengine.". Mara zingine tumepata kuleta macontainer ya nguo, na vitu kwa wahitaji ila tumepata matapeli au ugumu wa kukomboa bandarini, lakini hii haina maana tuache kusaidia mtu kabisa au kutofanya utafiti wa kufanya mambo bora. Mara nyingi na rafiki yangu Zuzo tumeomba Mungu atusaidie kuishi karibu na mpaka wa Mexico au Sudan ili tuwe tunarusha vitu kule kwa watu maana tunapoishi watu

hutupa nguo kwenye takataka, na wengine hutupa chakula bure, hatujakata tamaa kuna siku Mungu atafungua milango, tunatamani maombi yenu.

"Nimegundua kwamba ninapotoa nguo zangu kuwapa watu, si sadaka ya dhati. Kwani mara nyingi fasheni ikiisha au zikinichosha nazitoa kwa watu maskini. Ni kweli watu masikini wanapata ila utoaji wangu unakuwa na walakini. Maana nguo ninazonunua ni ghali, ila siko tayari kutoa pesa kusaidia mahitaji ya kazi ya Mungu na nipo tayari kutoa mitumba ikinichosha kwa maskini."

Nimekuwa nikitafakari haya. Nawe pia nanyi waweza kuyacheua haya. Kwamba unanunua kitu ili uwe nacho kwanza uonekane uko kwenye fasheni kisha unagawa, yaweza kuwa sawa kama unampa binadamu, ila kama ni Mungu itabidi utathmini tena. Kama unasali nao kanisa moja, au unaishi nao kijijini, unawadhalilisha ikiwa kila mtu akiona wanavaa mtumba wako wanajua ni wewe ndiye umetoa.

Wengine wamekuwa na tabia ya kujenga nyumba kila mji zisizoleta kodi, bali gharama kuzitunza. Tukiweka watenda kazi tuje mara moja kwa mwaka watu wa kule masikini watushabikie, tajiri amekuja. Alinichekesha rafiki wa Korogwe aliyesema kwamba nyumba yake haikuwa na watu miaka mingi; hata kenge waliingia na kuishi mle. Mambo ya kununua vitu usivyopima vizuri ni shida, ila kama ni rasilimali ni sawa. Wengine wamejenga majumba makubwa kama mapango na kushindwa hata kufuta vumbi kwenye vyumba vingine. Watoto walishaenda makwao, Mtu anasumbuka kupiga deki na kutoa buibui, badala ya kufanya kazi ya kuhudumia watu. Mambo ya majumba makubwa Afrika yalikuwa hayapo, ila sasa yameingia, wakati wazungu wanataka kuyapunguza, sisi ndiyo tumeyakolezea moto. Wazungu wana majira ya wakati wa baridi, kwa hivyo waishi majumbani siku nzima. Sisi tuna hali nzuri ya jua, twaweza kuwa na nyumba ndogo, na kukaa nje na kupata hewa bora na jua!

Siku hizi kuna shida ya mali na muda wa kutunza hivyo tunashauri viongozi wa kiroho wasiwe na watoto zaidi ya sita. Huu si ulimwengu wa kuzaa watoto kumi kama zamani. Rafiki mmoja alisema, "Mpaka mayai yaishe. Mungu ametuumba tuwe na watoto, hivyo nitazaa wale atakaonipa." Mungu ameumba pia mizunguko ya mwili ya siku salama ambazo mtu hashiki mimba. Tumia hizo, maana hata kama una uwezo,

saa ngapi utajitayarisha na hukumu ya Mungu inayotujia karibuni ukiwa una watoto wadogo kwa muda miaka 30? Ila Ulizia njia za uzazi wa majira zisizoua mimba iliyotungwa. Siku hizi mapambano ya kulea watoto ni mazito, jihadhari usikwazike, maana watoto ni kitu cha maisha yote, hata wakipigana huko na mke au mume, watarudi kwako tena uanze upya.

Ni rahisi kuwa mwema kwa watu tusiowajua, ila maneno yetu yanakata kata watu wa karibu. Lazima tuwe na unyenyekevu mahali pote. Kwenye kitabu chetu cha malezi ya watoto, wazazi wengi, hasa sisi kina mama tuna maneno ya kufisha watoto moyo. Hatuyaamini, ila tunayasema: “Hutafaa kwa lolote maishani mwako!” Hilo ni kofi kubwa, afadhali umchape mtoto kiboko. Au “Mbwa wewe kama baba yako!” Kweli haya ni maneno ya binadamu aliyeumbwa na mfano wa Mungu kweli? Ukichanganua:- mbwa anazaa mbwa, na kama wewe umeolewa na mbwa ulifanyaje uchaguzi huu? Maneno yetu ni uwakili pia, je, wewe unapenda kutukana tukana maneno machafu yanakutoka saa yote kwa watu wa nje na ndani, na mahasira. Acha, haisaidii afya katu. Tafuta sabuni na Chlorite na mswaki uoshe kila unaponena maneno machafu. Tuepuke uhodari wa matusi. Doug Batchelor wa Amazing Facts, alinipa moyo. Alisema aliendelea kutoa lugha za matusi baada ya kumjua Mungu kwa miaka michache. Alikuwa mhubiri wa nguvu akihubiria watu kila mahali. Ila aliendelea kuzidiwa nguvu na matusi. Mwishowe alipiga magoti na kuomba; “Bwana midomo yangu ni michafu, najaribu kutotoa matusi, ila nikikasirika natupa makombora yo yote, nisaidie.” Alisema kutoka siku hiyo matusi yote yalimtoka. Ni ombi langu pia Mungu anisaidie matusi yanihame pia. Na ukipata ushindi kwa Neno lolote jema mshukuru Mungu na utoe ushuhuda. Wanasema kushuhudia wema wa Mungu kunamwangusha Ibilisi chini ‘wakamshinda Ibilisi kwa ushuhuda wa maneno ya mdomo wao na Kafara ya Masihi”.

, “Safari ya maili 1000 huanza na hatua moja.” Tulitoa nadhiri kwa Mungu kwamba akituwezesha kumaliza shule tutarudisha 25% kwake kama zaka na sadaka na kusaidia wenye mahitaji. Nipolimaliza shule na kupokea dola 2000 kwa mwezi, nilihama nilipokuwa naishi ili kupisha wengine wapya kusaidiwa na wamishonari wema; kisha nikaanza kutoa 25% mpaka 50% kwa zaka, sadaka, na wenye mahitaji. Mungu alibariki na tukashugulika na wachungaji na walei tofauti, kujenga vikanisa 80 hivi, (bush churches) na kupeleka watenda kazi (walei) 350 kwenye kozi mbali mbali. Wachungaji na walei pia walitufanya tuwe wabia (patner) wao kwa kufanya mikutano ya hadhara ya uinjilisti 65 hivi.

Imekuwa safari ya imani, na tuligundua kwamba mkristo hana mpaka, lolote lile muumini afanyalo jiunge tu, nawe utapata baraka, hatujawahi kukaa na ***kupanga*** vitu vya kufanya, kwa vile sisi si watu wa mipango vile, ila wengi wametubariki kwa kutujumuisha kwa mipango yao. Kweli hatuwezi kufanya mambo makubwa, ila yale madogo kwa upendo, na pia hata kama kazi yenyewe ni tone kwenye bahari, basi tukumbuke kwamba tone moja ndiyo linayofanya bahari iwe.

Zamani tulifikiri kwamba tukiwa na pesa au muda siku moja, tutafanya hili au lile katika shamba la Bwana. Tukajikuta kwamba hakuna siku tulikuwa na pesa kwenye akiba, ni kudunduliza na kukata kila tunapopata mshahara au kutoa muda wetu (kwa hali na mali). Kitu kikubwa ni kumtegemea Bwana na kuendelea siku kwa siku (consistent).

Shemeji yangu mmoja aliviona vile vikanisa vidogo tukivijenga, alicheka akasema, hivi msingi wake si imara vitaanguka; “Mimi nangoja nijenge kanisa kubwa la dola 50,000 lililo na kituo cha vijana kwenye ghorofa yake (youth center);” alisema. Baada ya miaka 10 alikuja kwangu na kusema, “Nimegundua kwamba hakutafika wakati kama huo, maana pesa inaingia mkononi na kutoweka, afadhali kujenga hivi vibanda vya makanisa kama vyenu!”

Mchungaji mmoja alituita siku moja ili tujenge kwa wahitaji kule Kigoma. Hatukuwa na uwezo. Akasema, “Je, hamna hata dola 100, tupate wanawake wachote maji na kukandika udongo na kuleta miti, ili niwajengee hawa watu nyumba ya udongo na majani?”. Kabla hatujafikiria nyota juu kwenye anga, wacha tufikirie madogo tu yale ambayo Mungu Anatuwezesha kufanya siku kwa siku. Ni nani ajuaye pengine siku moja akatukabidhi hayo makubwa tuyafanye? Hitaji letu kuu ni maombi tafadhali jiunge kuomba nasi ili Bwana atutumie katika shamba lake. Yeye aliyeaanza kazi njema moyoni mwenu Ataimaliza, ni jambo la kututia moyo katika uwakili wetu. Mwitiko wetu uwe, “Nipo hapa Bwana nitume!”. Kwa kifupi tukumbuke kwamba si tu 10% ya vyote tulivyo navyo ndiyo vya BWANA bali 100%.
Nimejiuiliza mara nyingi nitapata wapi. Na kwa vile nina watoto wadogo, maana nilizaa nikiwa na zaidi ya miaka 40, nimejiuliza sasa nikitoa kwa mtu watoto wangu watasomaje? Maana karibu nastaafu na nguvu zinanipungua ila watoto bado wadogo. Siku moja nikitembea mtaa nilioishi kule Jersey

City, New Jersey, maili tatu kufikia Manhattan yale majengo marefu yalipopigwa na magaidi. Nilimwona bwana fulani ana mbwa mkubwa sana mweupe, anapendeza kweli kweli. Nikamkimbilia na kumwuliza mbwa wake ana uzito gani? Akasema kilo 140! Nikashangaa sana, akaendelea kujigamba kwangu “Jibwa hili linakula si mchezo!”. Nikasema kwa mwezi anakula kiasi gani, akasema “natumia dola elfu moja kumlisha kila mwezi!!”. Nilishangaa maana tulikuwa sita ndani ya nyumba, na pengine tulitumia pungufu ya dola 500 kwa mwezi, na huyu mbwa tu anamendesha hivi. Ndipo jibu likaja moyoni, huyu anapenda mbwa na amemwomba Mungu wake amsaidie kufanikisha mapenzi yake hayo (hobby). Wewe kama unapenda watu mwambie Mungu akusaidie, daima hatakuacha, atakusaidia ili ufanye huduma ya kusaidia watu na kazi ya Mungu. Hebu tusaidiane kuombeana tuwe mawakili wema tushinde uchoyo kabisa.
Je leo ungeambiwa una masaa 24 tu kuishi, kesho ungekufa, ungefanya nini kwa haraka? Daudi asema ‘nimrudishie nini BWANA kwa wema wake alionitendea?’. Aligundua Mungu ana kila kitu, kinyangarika mimi nitampa nini Mungu. Akaona kilichobakia kwake ni kumshukuru BWANA, na kuwaambia watu wengine mema ya BWANA na yeyé mwenyewe kushika amri za BWANA, na shuhudua zake.

SURA YA 20

AFYA YA WATOTO NA WAZAZI

Napenda kusema kwamba kuna sheria kumi za afya ambazo zinafanya kazi kwa watu wazima na watoto pia. Yaani haya unayoyasoma umsaidie mtoto wako ayafanye nawe mwenyewe pia uyafanye. Nazo nitazielezea kwa undani. Kuwa na afya ni kitu cha furaha na pengine kisichukue muda wako mwingi. Nitayaita matibabu kumi, na chakula ni tabibu wa kwanza kwenye orodha hii.

Chakula siku hizi kinawekwa kwa kutamanisha vijana, kwenye vikasha vya rangi na picha za kuvutia kwa watoto au vijana. Angalia makasha hayo kwenye maduka makubwa. Hii inawalazimisha wazazi wanunue kutokana tu na matangazo. Gazeti la matatizo ya unene (Journal of obesity reviews), linasema lilifanya utafiti wa watoto 367na kukuta 89% wanakula chakula ambacho hakina lishe nzuri. Vyakula vingi vya watoto madukani vina upungufu wa lishe; aidha vina sukari nyingi, mafuta na chumvi. Watoto ambao chakula chao kinakuwa na shida hii, (Junk food); yaani vyakula ambavyo ni kama makapi, huwa na upungufu wa usikivu, kutofanya vizuri darasani na wanakuwa na shida ya kuchoka. Kutokula vizuri ni shida kwa maana watoto wengi wana shida ya kisukari kuliko ilivyo kawaida.

Asilimia 85% ya maswali yote yanayoulizwa na wahudumu wa afya, madaktari, manesi nk yanahusiana na chakula. Ni muhimu sana kuzungumzia mambo ambayo wazazi wanaweza kuyatumia kusaidia afya ya mtoto. Mambo hayo 10 ni: Lishe, mazoezi, maji, jua, kiasi, hewa, mapumziko, kumwamini na kumtegemea Mungu, roho ya shukurani, kuhudumia, na kujali wengine. Nitajaribu kuzungumzia haya kwa ufupi.

Baada ya uumbaji wa mwanadamu, kila kitu kilikuwa kikamilifu kiroho, kimwili, kijamii na nyanja zote. Baada ya kuanguka maradhi yaliingia na hata kifo.

Tujaribu sana kutoigiza mambo hasa yale ambayo hayatusaidii kiafya. Mfano tusiige vyakula, hasa vile vya watu wa Magharibi. Tunaamini vyakula vyote duniani vinafanana fanana ila vinatofautiana upande wa matayarisho. Ukimpa Mwafrika unga wa ngano atapika ugali, Mhindi atapika chapati, Mzungu atapika mkate! Jaribu kupika na kutayarisha vyakula vya asili kwa familia yako. Epuka Vyakula vilivyokobolewa kama sukari, mahindi yaliyotolewa maganda, mikate myeupe au ngano iliyokobolewa, mchele usio wa brown. Hivi vinatia sumu mwili.

Mafuta ya kupikia, jitahidi yawe kama ya nazi au alizeti yaani ya mimea. Epukana na Margarine. Mama jifunze kupika vizuri kwa afya. Mtoto wako ale kifungua kinywa vizuri ndiyo chakula muhimu kuliko vyote vya siku. Chai siyo chakula cha afya sana. Mtoto ale matunda, mboga mboga kama karoti, matango, nyanya, viazi, mihogo, uji na vinginevyo. Uji waweza kuwa wa ulezi, uwele, mtama na muhogo. Hizo ni nafaka nzuri na ukizichanganya unafanya lishe iwe bora (Rich). Wanasema nafaka zenye rangi na ndogo ndogo ndizo zenye lishe. Hizi ni nafaka zetu za asili. Mahindi ni mageni, na mbegu zake zimefanyiwa mengi na wataalamu wa kilimo kama GMO (genetical engineering) na kugoshiwa au kuchakachuliwa! Epuka kula mazao ambayo mbegu zake haziwezi kuota.

Ujifunze tiba rahisi za mtoto wako, maana wewe unamjua mtoto wako kuliko mtu mwingine. Siku moja mtoto wangu wa miezi sita alikuwa anagua maambukizo ya sikio, (ear infection), na joto lilipanda likafika nyuzi 42^0C na halikushuka! Nikaenda hospitali. Kufika kule walimchukua wakamweka kwenye maji ya uvuguvugu sana, kwa muda wa dakika 30 wakimwangalia asizame. Basi wakanipa mtoto, joto limepungua; wakanitoza dola 700 (kama sh milioni moja)! Nikawaza hili ningejifanyia kwangu; nina maji, nina beseni, ila nimetozwa pesa nyingi hivi?

Jifunze lishe na mpango wa mbingu wa ulaji wako. Mungu alimwumba binadamu akijua kitakachomfaa kula. Maelekezo ya chakula na mwili wake amekupatia, kama vile muundaji gari anavyotoa maelekezo ya kutumia gari. Hauwezi kuweka maji kwenye gari, ila petroli. Najua kabisa tunaishi dunia ya dhambi na pambano kati ya Mungu na Shetani linaendelea, na kwamba mara nyingine tunajaribu kufuata kanuni, ila magonjwa yanakuwa magumu, na juhudi zetu zinakwama. Ila usifanye shingo yako ngumu kwa kutosikiza. Jaribu unavyoweza kufuata mpango wa Mungu ili hata kama utaumwa utasema nimejaribu nilivyoweza. Ila ukila na kufanya kinyume hata dhamira yako haitakuwa huru, itakushtaki.

Tukumbuke kwamba bustani ya Edeni ilitoweka kwa ajili ya chakula na itarudishwa kwa kutawala tamaa ya chakula. Tunaelekezwa na Maandiko yale ambayo mama Samweli, Samsoni na wengine waliambiwa wale! Chakula ni muhimu kabla mama hajajifungua na baada ya mtoto kuzaliwa! Mfano Waliambiwa wasile nguruwe, pweza, kamba, pombe na wanyama najisi.

Maziwa mengi pia yanaonekana na madhara hasa siku hizi. Ngombe wa kisasa wanafugwa kwa madawa mengi ya antibiotics na vichocheo vya kuwakuza kwa haraka. Hata hivyo ni binadamu tu ambaye anakunywa maziwa ya mnyama mwingine na yameonekana na shida nyingi kwa wengi duniani, hasa wale wanaokula jibini, ambayo ni 'mrundikano wa maziwa mengi'. Nyama ambazo hatuna uhakika kama zimepitia ukaguzi vizuri na mengineyo. Chakula cha nafaka mfano ni uwele, mawese, mtama, na mahindi. Chakula cha jamii ya maharage ni kama dengu, choroko, njegere, kunde, na mbaazi. Chakula cha jamii ya karanga ni kama nazi, korosho n.k. Chakula cha jamii ya mboga mboga ni kama mboga za majani, viazi, mihogo, vitunguu saumu, vitunguu, biringanya, ngogwe, karoti, nyanya, vitunguu, matango, na hoho. Mwishowe aina zote za matunda ni kama maembe, mananasi, na machungwa.

Tukumbuke kwamba bustani ya Edeni haikuwa na masufuria. Fanya chakula chako kiwe dawa na dawa zako ziwe chakula. Watu wengi wanasema maziwa yanasaidia mifupa. Mtoto anapaswa kunyonya maziwa ya mama yake kwa ajili ya kuimarisha mifupa. Utafiti wa wale wenye nchi za utajiri wa maziwa kama Denmark na zingine za Magharibi huonyesha kuwa wana shida ya mifupa zaidi (Osteoporosis), hata kuliko sisi ambao tunalamba lamba maziwa kidogo. Wanasema ni wanawake ambao wana shida za kuvunjika vunjika mifupa. Ila wanawake wa kibantu yaani chini ya Jangwa la Sahara ndiyo wana mifupa migumu kupita ya wote duniani! Na ni wanawake wangapi hapa wanapata maziwa kama wale wa Magharibi wanaokunywa hata galoni kwa siku?

Kutumia mboga za majani, kupata jua la kutosha na kubeba mizigo mizito ndiyo huboresha mifupa. Mtoto ale mayai mawili tu kwa juma kama ni lazima sana, akila zaidi ya hapo siyo afya. Epuka kuweka chumvi nyingi kwenye chakula. Epuka viungo visivyofaa, kama ajino moto, pilipili kali, kungumanga(nutmeg) n.k. Viungo bora ni kitunguu saumu, kitunguu maji, manjano, tangawizi, giligilani au dania, basil, mint(mnanaa) , ndimu, na cumin(jira ya manjano).

Wafanye watoto wako waone jukumu la kutunza afya, ni lao. Kuwa mtoto mwenye afya bora hakumaanishi kwamba kutaondoa raha (fun!)
Utafiti umeonyesha kwamba watoto wanaokula vyakula vilivyokobolewa, vyenye mafuta, sukari na chumvi nyingi, uelewaji wao wa masomo ni mdogo. Jitahidi usiiigize lishe za nchi za Magharibi, umpapo mtoto wako chakula. Uji wa nafaka kama uwele ulezi na mtama au hata ufuta na soya uchanganywe, mtoto na watu wazima wanywe. Viazi, magimbi na ndizi zaweza kuliwa vyenyewe tu. Mwaweza pia kula ugali na mboga au wali usiokobolea na mboga asubuhi. Nafaka za kwenye makasha ni nafaka zenye sukari, ni kama kula peremende.
Watoto hurithi chakula na tabia za afya toka kwa wazazi wao. Watoto wengi wameanza kuwa na unene wa ajabu kama majabali ambayo yalionekana Magharibi. Siku hizi watoto wengi wamegundulika na ugonjwa wa moyo kabla hawajafikisha miaka kumi na sita!

Anza kumwanzishia mtoto vyakula vya afya. Azoee ladha yake na akirudie tena mara kadhaa. Mfundishe mambo yahusuyo lishe na mpango wa lishe kwa mtoto, kimwili, kiakili na kiroho. Tunaona kijana Samsoni alishindwa kutawala tamaa zake, hata asali iliyokuwa kwenye mzoga najisi wa simba anakula tu. Alishindwa kutawala tamaa zake, nayo yakawa maanguko yake. Mara nyingi twataka kuonekana wa kisasa kwa kuwapa watoto mapocho pocho.
Nilipokuwa nikilea watoto wangu nilibeba chupa ya chai iliyowekwa uji na kuwapatia nyanya, ndizi na matango. Marafiki na watu wengi walikuwa wakishangaa na kucheka! Kweli huyo mtoto atakula hayo? Cha ajabu wao walizaliwa kijijini na wakala vyakula hivi, na ndiyo maana wana nguvu! Watoto wangu walikula na kufurahi sana. Walipoanza shule marafiki na walimu waliwapa siasa za vyakula vingine kama chipi; tukayumbayumba ila baadaye kwa neema za Mungu wamegundua vyakula vya afya, na tunaendelea kufundishana. Ni safari ambayo Bwana anatupa nguvu. Rafiki zao walibeba maziwa ya kwenye kopo, chipsi, nafaka za kwenye makasha, nyama za kukaanga na vingine.

Japo hawa wazazi wengi wa kiafrika walikula vitu vizuri vya asili, bali kisomo walichokipata na kutembea nchi zingine kiliathiri mtazamo ule wa vyakula vya asili ambavyo Mungu alituumbia tuvile. Nimetembea kwenye mabasi, na makanisani na nimekuta watu wengi wakija na vyakula vya ajabu na kuwapa watoto; vyakula ambavyo vinaharibu miili na vitawafanya kuanza kuwa na magonjwa wakiwa na umri mdogo tu.

Wazazi wengi waliacha kunyonyesha watoto! Jambo hilo lilitokea kwenye nchi za Magharibi miaka michache iliyopita, wakati kina mama wakisema wanadai haki, na kutaka kuwa huru wasinyonyeshe watoto. Sasa, shida ya kisukari na nyingine zimengia na wanawake wa Magharibi wengi wameanza kunyonyesha tena. Mahali ninapoishi wanawake wa kizungu wamelitilia maanani sana hili; ila wale wa jamii zingine kama Waspanish na Waamerika weusi nao wanapitia yale Wazungu waliyopitia miaka 50 iliyopita na hawataki kunyonyesha! Mungu aliyeiumba miili yetu ajua lishe bora ya mtoto ni maziwa ya mama. Yana lishe ya mtoto anayetembea baada ya mwaka na si kwa siku ile ile anayozaliwa kama ndama.

Jitahidi watoto wako wasiwe wanakula ovyo ovyo siku nzima. Shida hii nimekuwa nayo, kwa watoto wangu na tunajaribu itutoke, na tuikemee! Watoto wapate muda wa

masaa matano wa tumbo kupumzika. Jaribu kuoka chakula badala ya kukaanga. Watoto wasile bila kuhisi njaa kwa sababu chakula kipo. Wakitaka kitu chenye sukari wape matunda. Usitumie sana chakula kama zawadi kwa mtoto utafanya mtoto awe mlafi. Wakati wa chakula uwe wakati wa utulivu si wa kugombeza mtoto na kukosoa, inafanya myeyusho wa chakula usiwe mzuri. Tafuta muda mzuri wa kuzungumza na mtoto na kumrudi.

Jaribu kutengeza chakula cha mtoto, badala ya kumpa pesa za kununua chakula shuleni; maana mara nyingi kitakuwa si kile chenye afya sana, mpaka uwe na uhakika. Ukiwa dukani pata nafasi ya kuwafundisha lishe watoto, gharama zake na pia wafundishe vizuri nembo za maneno zilizo kwenye vipakiti vya chakula. Si lazima uende shule kwa upishi ila jifunze tu kufanya upishi wako rahisi kwa kutumia marafiki, ndugu na vitabu. Watoto wajumuishwe kutengeneza chakula, mle pamoja na utoe mfano kwa mtoto wako. Mama mwingine alimwambia mwenzake una bahati mtoto wako anakula mboga, wangu hali.Yule mama akamwuliza yule mama kama yeye mwenyewe anakula mboga; akasema, “La, sipendi mboga na maharage ni ya watu masikini!” Sasa unategemea mtoto apendeje mboga na wewe mama huzipendi!

Ili kumfanya mtoto unayemwanzishia chakula apende mboga mzawadishe kwa mambo madogo madogo. Nunua vitabu vya kupendeza vya lishe kwa watoto wako ili wavisome. Mtoto ale matunda angalau matano kwa siku. Matunda yana rangi na ladha nzuri ambazo watoto huzifurahia. Yapande nyumbani kwako. Matunda yana vitamini na madini nyingi. Watoto waweza kuchagua chakula pale inapowezekana. Mtoto ale ashibe ila asijenge tabia ya ulafi. Asijipakulie vyakula vingi kwa wakati mmoja, maana vinaharibu tumbo, vinajenga uharibifu, na pia vitafanya asitawale tabia ya uroho. Watoto walio wanene sana wameshafika hapa Afrika jambo ambalo halikuwapo hapo zamani. Watoto hawa hawajiamini, wanachekwa na wenzao na wapo katika hatari ya kupata magonjwa. Wajulishe watoto kwamba vyakula vingi vya mahotelini (fast foods) si vizuri maana vina mafuta, chumvi na sukari nyingi.
Lishe hujenga maisha ya mtoto kitaaluma, na pia humpa kinga ya mwili. Magonjwa kama kukohoa na mafua yanaweza kupungua kirahisi kwa lishe nzuri.

Jaribu kuleta vyakula vya afya vyenye kupendeza kama matunda, kwa vile vibaya ulivyotoa. Mfano chapati za unga uliokobolewa anza na unga usiokobolewa na mboga iliyoungwa vizuri. Watakapotaka vitu vya sukari, tafuta tunda lenye sukari kama nanasi, au weka asali kwenye uji. Sukari si njema kwa mwili. Inapunguza kinga ya mwili kupigana na maradhi. Mara zingine watoto hawahitaji chakula ila wanahitaji mazoezi na vitu vya kufanya badala ya kukaa na kula kula saa yote. Badilisha rangi ya chakula cha mtoto, Mungu ana rangi kama za upinde kwa matunda na mboga tofauti, badilisha hizo kila mara na uwe na bustani!

Kama ulikuwa umefanya makosa katika lishe usikate tamaa. Mungu ni mwenye huruma nyingi pale pale ulipoanza, anakusaidia. Mazoea yanajengeka kwa kurudia rudia, hivyo ukileta chakula kigeni kwa mtoto kikikataliwa usiharakishe kukitoa. Endelea kukileta. Chakula cha kigeni kina harufu, hata watu wazima inawachukua muda kuzoea vyakula vigeni. Mfano tunda fulani, au nafaka ambayo mlikuwa hamuitumii. Mtoto anachukua muda kuzoea harufu na ladha mpya. Hasa kwa wale wakina mama wanaofikia hatua ya

kumwanzishia mtoto chakula baada ya miezi sita au wale wanaotaka kumwachisha mtoto kunyonya, kama miaka miwilii au mitatu. Hata sisi kama watu wazima kuna vitu tulianza kuvila ambavyo vilikuwa vigeni, na ilibidi tuvizoee na sasa tumevipenda, mfano parachichi (ovacado).

Badala ya kumpa mtoto kitu kisicho na afya kwa kuwa amekitamani tafuta mbadala atakaoupenda ambao una afya. Wakitaka vitu vyenye sukari, matunda kama mananasi, au asali kwenye uji watavifurahia. Mara nyingine watoto wanataka kula kula ovyo, kwa kukosa kitu cha kufanya; watafutie mchezo au kazi ya kufanya. Jitahidi usiwakaangie kaangie vitu na mafuta mengi, jaribu kuoka. Mara nyingi usipende kutoa zawadi ya chakula wataona kama ni faraja kwao na kuwafanya chakula kiwe rafiki wakati fulani na kufanya waongezeke uzito.

Wakati wa chakula usiwe wakati wa magombezo na mafarakano, na kumlazimisha mtoto kula kitu fulani. Lete utulivu wakati wa kula ili wakati wa kula uwe wakati wa furaha. Usimpe mtoto pesa kununulia chakula shuleni kama peremende, jaribu kutayarisha chakula na kumwekea kwenye chombo. Chukua muda utafute vitu vya afya. Mara nyingi watoto wanachekana kutokana na vitu walivyobeba. Wanapenda waonekane wa kisasa na wa kimagharibi kwa kula mapochopocho ya kwenye makasha; na kuona aibu mbele ya wenzao wakibeba magimbi, viazi vitamu au vitu vingine.

Chukua nafasi ya kwenda kununua chakula na watoto na kuwaelezea thamani ya lishe iliyomo kwenye vyakula mbali mbali. Waonyeshe kwamba kuwa na afya ni kitu cha furaha. Wafundishe mambo kumi muhimu ya afya bora, au tiba rahisi. Siku hizi wauzaji wengi wa vitu wamewalenga watoto kwa vyakula vya kwenye makasha na mapochocho yanayopendeza kwa macho ila ndani hayana lishe. Si kila walichokipamba kina lishe nzuri. Wapaswa ujielimishe kuhusu wauzaji wa vitu.

Watu wengi waliokuwa na tatizo la kufunga choo ni kwa ajili ya kutokula mboga na matunda. Mtoto asiende chooni akachukua muda kusukuma kinyesi kitoke. Watu wengine wameathiri moyo kwa kusukuma kinyesi kwa nguvu. Mavi yasiwe kama ya mbuzi kwa ajili ya kufunga choo ila yawe yanaelea kama unatumia choo ya maji, na umbo lake liwe kama S hivi, kuashiria kuwa utumbo mkubwa una afya. Rangi iwe ya kahawia (brown) au ya kijani kama anakula mchanganyiko unaotakiwa kwa uwiano wake.

Gazeti la unene (journal of obesity reviewe) lilitafiti vyakula vya watoto 387 na kukuta kati ya hivyo 89% vina lishe hafifu kwa watoto. Vingi vina sukari, chumvi na mafuta mengi kwa mtoto na hata kwa mtu mzima. Waingereza wanaita junk food, au vyakula ambavyo ni kama takataka kwenye miili yetu. Vyakula hivi vyenye sukari, chumvi na mafuta mengi vinafanya watoto wawe na usikivu mdogo, uchovu, na vinaongeza shida za kisukari na shinikizo la damu watoto wakiwa na umri mdogo. Shirika la kupunguza unene duniani; (The International Obesity Task Force), limeona kwamba

mtu mmoja kati ya watatu katika nchi nyingi duniani, ni mnene. Na mtoto mmoja kati ya watano pia ana shida hiyo. Jambo zuri ni kwamba hali hiyo inaweza kusahihishwa kwa kutumia vyakula vya asili vyenye lishe bora na ambavyo vinavutia.

Je, wazazi wawezaje kusaidia watoto wao wale vyakula vya afya.
Kwanza ni kujua kwamba ulaji unatokana na mazoea. Itachukua muda, usiharakishe. Watoto wanarithi chakula toka kwa wazazi kama vile ilivyo urithi wa maumbile! Na ndiyo maana kila taifa, kabila na jamaa, kwa miaka na mikaka, wanakula sawa na watoto wao. Mama ana nafasi kubwa ya kumfundisha mtoto chakula bora, kwani mama ndiye mpishi mara nyingi. Utafiti umeonyesha hata mwanamume aliyesomea shahada kubwa za lishe, haisaidii yeye kula chakula cha afya kama mke au mama anapika vyakula vinavyoharibu mwili. Wakina mama hapa tuna nafasi kubwa ya kusaidia jamii zetu na chakula. Lishe hujenga maisha ya mtoto kitaaluma, na pia hukinga mwili. Magonjwa kama kukohoa na mafua yanaweza kupungua kirahisi na lishe nzuri na hii si siri wala uhitaji kuwa injinia wa roketi kujua hili.

Mazoezi ni muhimu sana, kama mtoto anaweza kutembea kwenda shuleni, ni muhimu. Watoto hata wa miaka minne wanaweza kutembea kilomita tatu kwa siku. Mazoezi hujenga mifupa na kupunguza osteoporosis. Watoto wapate muda wa kucheza. Mtazamo wa kujiamini na kujithamini kunazidishwa sana na mazoezi.

Watoto wajifunze kunywa maji, maana asilimia 80% ya mwili ni maji. Mtoto wa miaka minne anywe glasi nne za maji. Kuanzia miaka tisa mtoto anaweza kunywa glasi sita na baada ya miaka kumi na miwili anywe maji kama mtu mzima. Asingoje mkojo uwe mwekundu au asikie kiu, maana wakati huo mwili utakuwa umeshapungukiwa na maji kwa kiasi kikubwa.

Watoto wengi duniani wana upungufu wa vitamin D na jua. Nilikuwa Naivasha kipindi fulani nikaambiwa kwamba vituo fulani vya kutunzia watoto vilikuwa vina nafasi ndogo. Watoto hawakuwa na pa kuchezea, hivyo hawakuota jua na wanafika kule asubuhi sana, na kutoka jioni bila kuota jua. Waligundulika na rickets, yaani mifupa kupinda. Hii shida ni zaidi ya mifupa maana ina athari nyingine mwilini. Wazazi, mtoto ahitaji angalau saa moja ya kuota jua la asubuhi.

Tufundishe watoto wetu kuwa na kiasi, kutotumia kabisa vile vibaya na vile vizuri kuvitumia kwa kiasi. Tufundishe watoto kuweka uwiano wa shule, mambo ya kiroho na ya kijamii. Watoto wasiwe na msukumo wa kufanana na watu fulani na kukimbilia mambo hayo ili afanane na jirani yake. Weka uwiano kati ya shule na mazoezi ya kufanyia nyumbani. Mtoto acheze na kufurahi. Hii humfanya aweze kuelezea hisia zake.

Watoto wengi siku hizi wamegundulika na magonjwa ya sonona (akili) au msongo (depression), kutokana na kwenda shule mapema sana. Wengine huamka saa kumi wakati mmoja na wazazi, ili kwenda kuwahi mabasi. Mambo ya watoto wadogo kwenda shule hayatokani na nia ya kutaka kujifunza, bali sana sana ni njia ya kuruhusu kina mama waende vibaruani. Ni vyema mtoto awe huru akiangalia uumbaji mpaka miaka saba. Hakuna masomo ambayo mama atashindwa kumfundisha mtoto nyumbani. Na hata asipojua kusoma kuna kazi nyingi za nyumbani na michezo mingi ambayo inakuza akili

mno hata kuzidi masomo! Natoa mfano wa Raisi Nyerere wa Tanzania aliyeanza shule akiwa na miaka kumi na mmoja na kumaliza shahada ya pili, masters akiwa na miaka ishirini na saba tu! Pengine kwa kurushwa madarasa? Watu wengi wanajivunia watoto wadogo kwa kusema amejua kusoma akiwa na miaka miwili tu. Si jambo zuri kiafya mtoto wako kuanza kusoma kwa miaka hiyo! Inapunguza umakini na kumfanya aruke mambo mengine mema katika maisha.

Mtoto asiwe kwenye mfumo rasmi akiwa mchanga vile. Watu kama Michael Jackson na wengine, wamewathibitishia wanasaikolojia wa watoto wengi kwamba mtoto akianza mifumo rasmi (formal education), kama vile kuigiza na drill zingine anaruka vingi ambavyo ukubwani vinakuwa si vya mbaraka kwake. Si vyema mtoto aende shule ya bweni (boarding) akiwa mdogo. Hutaweza kumfundisha mengi ya kufaa afya, ni vizuri aende akifika miaka kumi na miwili na kwa wengi hata huu umri bado ni mapema sana.

Muwe na ratiba ya kufanya mambo, mtoto wako akuone una kiasi. Asikuone unakunywa pombe, kahawa, sigara au madawa ya kulevya na na huku ukimkataza asifanye hayo. (Methali 20:1). Au asikuone una misongo mingi ukijikimbiza hapa na pale bila sababu. Matendo yako ndiyo mahubiri na mifano kwake. Mfundishe mtoto jinsi ya kugawa majukumu yake ili asiwe na msongo. Kazi ni mbaraka mkubwa kwa mtoto, wasema akili isiyo na la kufanya ni karakana ya shetani. Hebu mtoto asikae kivivu.

Mtoto alale kwenye chumba chenye hewa bora, madirisha yafunguliwe hata usiku. Uchafuzi wa hewa kwa viwanda na magari ni mgumu kwa mapafu. Wasema tuishi vijijini ila sasa asilimia 50% ya watu huishi mijini. Hata tabia ya watoto, wasema wataalamu, ni rahisi kujengeka mara kumi bora zaidi vijijini zaidi ya mijini. Watoto wajifunze kupumua vizuri kwa kuvuta pumzi kwa ndani (deep breathing). Watoto wa kwenye viwanda vingi vya mkaa, kama Uchina, wana mpaka asilimia 50 ya asthma.

Mtoto apate muda wa kulala. Mtoto akizaliwa aweza kulala masaa ishirini na mawili. Mtoto wa miaka 4-6, alale kwa muda wa masaa 12 mpaka 14. Na mtoto wa miaka 10 alale kwa masaa 10. Atapofikia umri wa miaka 16, alale masaa manane. Pia kupumzika siku moja ya juma ni muhimu. Mzunguko wa mwili wa binadamu uliumbwa apumzike siku moja kwa wiki “Akastarehe akapumzika akaitakasa Sabato...” Mtu asiyepumzika ana misongo inayotoa vichocheo vibaya kwenye mwili (cortisol) na kuchoka. Athari za kutolala ni kuwa na kisukari, presha, maambukizi, ajali, kutotulia (hyperactivity), kunenepa ovyo na mengineyo.

Watoto wasitazame televisheni au kunywa kahawa kabla ya kulala, na wawe na muda maalumu wa kulala; watangulie kulala kabla ya watu wazima. Wataalamu husema mtoto wa chini ya miaka miwili asitazame TV kabisa. Inaathiri hisia na macho.

Familia iwe na maombi ya asubuhi na jioni. Ni ya muhimu katika malezi na afya ya watoto; matumaini na imani inafanya mtoto akomae na kukua vyema. Wasomee hadithi za mafundisho ya dunia na ya Neno la Mungu. Fundisha watoto kutokuwa na harara. Wafundishe watoto kumtumaini Mungu na watu pia wasiwe watu wa kushuku shuku watu na wasiwasi. Ili linachukua muda na watoto wataona mtu wa kumtumaini na kwa namna gani.

Kuamini kunasaidia kijamii na kihisia, watambulishe watoto wako kwa watu wa kuaminika ili wajenge imani na watu. Watoto wanapenda mahali penye usalama (security). Watoto wakiwa wadogo tunawakumbatia, ila wakiwa wakubwa tunaweza kuwaonyesha uhakika kwa njia mbali mbali.
Pia wafundishe watoto wako kwa matendo, ili ukisema kitu waweze kukutegemea.

Watu wengine wameniuliza maswali kama ya kutumia majiko ya microwave, kuzibwa meno kwa zebaki, kutumia fluorine kwa watoto kuoshea meno kwa mganga wa meno na kuziba meno yaliyotoboka sana kwa kuua mzizi wa jino (root canal). Napenda kusema mimi si mtaalamu sana ila tabibu niliowaita kuzungumzia shida hizi kama Dr Agatha Thrash na Mercola Ucheepines.org na mercola.com walinifanya nifikie uamuzi huu:

Microwave ni mbaya kwa mwili wako. Ukinyweshea mmea maji ya microwave baada ya muda mmea huo utakufa. Fanya majaribio hayo na ukanyweshee mimea miwili; mmoja na maji ya microwave na mwingine maji ya kawaida. Plastiki nyingi zinayeyuka na zina sumu za dion. Usitumie chupa ya plastiki ya maji zaidi ya mara mbili! Watu wengine wamepata kansa kwa ajili ya plastiki nyingi kwenye mwili. Plastiki yenye namba kubwa kwenye kitako ndiyo nzito kidogo na nzuri, ila kama namba ni ndogo kama 1, 2 au 3 inayeyuka zaidi. Usiweke chupa ya plastiki maji moto au barafu kisha unywe utakunywa plastiki nyingi. Na usiitumie mara mbili tatu, tupa, inalika mno. Jaribu kutumia vyombo vya udongo au chuma ya stainless steel kuliko plastiki.

Zebaki (mercury) nyingi kwenye meno ni sumu kali. Nchi zingine zimepiga marufuku hizi. Fanya utafiti vizuri ujue na kuuliza watu huku ukimwomba MUNGU akusaidia kwani unafanya uamuzi kwaajili ya watoto wako ambao hawajui mengi na hilo ni jukumu zito. Kuna kuzibwa kwa vitu vingine japo havikai muda mrefu sana (compost). Kwa upande mwingine Zebaki inayeyeyuka ukinywa vitu vya moto na kuwa sumu kwenye damu. Mtu mwenye zebaki ya meno mawili au matatu si kubwa ila kama una mengi ni shida, na jinsi inavyozidi kuzeeka inayeyuka zaidi. Fluorine kwenye meno ni sumu kwenye mwili, jaribu kuangalia njia za kinga za kupunguza meno kuoza badala ya fluorine. Pia root canal imeonekana kufanya kinga ya mwili kupungua. Hebu soma utafiti hasa wa nchi za ulaya. Wao wana mambo ya afya kuliko Marekani.

Wengi wameniuliza kuhusu chanjo. Chanjo nyingi zimesaidia kuondoa magonjwa kama vile polio, duniani. Ila siku hizi makampuni ya madawa yanazidi kuja na chanjo nyingi ambazo zinazodhuru kwani zinatunzwa kwenye zebaki au alumium. Fanya upelelezi ni chanjo zipi zafaa mtoto. Chanjo nyingi siku hizi zinatolewa kwa mseto au mpigo sita kwa mtoto wa wiki sita! Hii imeonyesha athari kwenye nchi kama Amerika, kwa ubongo wa mtoto (autism). Ila kwa sababu inahusika na pesa kwa makampuni haya pengine, ukweli kamili usijulikane.

Zamani chanjo zilitolewa moja moja. Chanjo nyingine kama za mafua (flu), zimeonekana kudhuru watu, katika nchi za magharibi wengi wamejiuliza na kuuliza serikali maswali maana wana vyombo vya kutoa hoja au mawazo yao. Chanjo zingine zinatunzwa kwenye zebaki (mercury) ambayo ni sumu. Nafikiri kwa vile watoto wetu wanacheza na watoto wengi mzazi aangalie jinsi ya kumsaidia mtoto na chanjo zinazofaa kwenye jumuiya ili mtoto asidhurike. Zifanyie utafiti chanjo za mseto kwa makini. Zingine

ni za kuepuka; mfano chanjo ya mafua. Watu wengi tuliochanjwa zamani, haikutusaidia kitu; na pengine ilituletea mafua! Nasema machache ya uzoefu wangu, watu waliozama kwenye ulevi wana msemo (alcholic anonymous) wanasema kuwa wendawazimu, ni kuendelea kufanya jambo lile lile na kutegemea matokeo tofauti (insanity, is to continue to do same thing over and over, and expect different results)! Lazima uwe mteja unayetafuta maarifa (educated consumer).

Kama umepata chanjo za mafua kama sisi bila kuona tofauti, basi utajua mwili wako unahitaji jambo gani, kwa kiasi fulani. Jielimishe zaidi kwani hata zebaki kwenye meno wataalamu wengi walikazania ila leo hii zebaki (amalgalm/mercury) imepigwa marufuku nchi kadhaa kwani ni sumu mbaya sana. Sitamwambia mtu asichanjwe au achanjwe kwa vile chanjo nyingi zimesaidia sana nchi zinazoeendelea kama za Afrika. Chanjo za polio, tetanus na nyingine, zimeokoa maisha ya watu wengi. Hata hivyo wachache wale ambao hawajapata chanjo wajielimishe kidogo maana chanjo za mseto na zinazohifadhiwa kwenye zebaki au aluminium zina shida yake. Wale ambao hawafanyi tiba rahisi au yale mambo kumi ya tiba rahisi ili kulinda afya inabidi tupate chanjo zitusaidie kwa vile kinga zetu za mwili zimekuwa hafifu. Kila mtu apaswa kujielimisha jinsi mwili unavyofanya kazi (anatomy and physiology) hata kama hufanyi fani ya afya, ili kuweza kufanya maamuzi bora zaidi.

Ni muhimu sana wazazi kujifunza huduma ya kwanza mfano mtoto akipaliwa na kitu kwenye koo, akinywa sumu, akiacha kupumua ilhali moyo ukiwa bado unapiga, n.k. Hata wasaidizi wa watoto wafundishwe (choking, cardiac pulmonary resuciation etc). Nashauri uende kliniki ya karibu na waulize watu wa kituo cha afya wawe na semina hizi kusaidia watu. Waweza kusaidia kuokoa maisha ya watoto wako na jumuiya kwa ujuzi huu. Niliishi na anayenisaidia mtoto homa ilikuwa juu sana 41^0C na hakugundua kwa vile hakuwahi kuwa na mtoto au uzoefu. Mashirika kama Red Cross au Madaktari waweza kuwa msaada kwako zaidi kwa yale ya muhimu yahusuyo huduma ya kwanza.

Usijiunge na ushirikina kwenye tiba ya watoto wako kwa kuwawekea hirizi, na kutafuta mganga wa kienyeji kuagua, na wachawi. Kuna waumini wengi, hata viongozi wa kiroho, wanaoenda kwa waganga, eti kukingwa na hirizi au chanjo! Hili ni jambo la kusikitisha sana. Kinga yetu ni MUNGU, nguvu yetu mwamba wetu na wokovu wetu,

Mtoto akiwa anaharisha na kutapika, anapaswa kuongezewa maji na kumpeleka hospitalini mara moja; maana ana uwezekano mdogo sana wa kupona. Ukiona mtu 'Amemwangalia mtoto kwa jicho baya;' chukua muda kusali, maana huwezi kujikinga na uovu kwa nguvu zako. Mwombe Mungu akukinge na uovu. Soma Zaburi 91 au 23 Daudi alizovuviwa kuandika na MUNGU 91 na uzikariri pia. Waovu watakuwepo siku zote, ila jikite kwa Mungu, na kuwa magotini, ndiyo tu unaweza ukakabili uovu wa aina yoyote.

Mtoto mdogo anayetambaa, awe kwenye mazingira safi. Akiokota na kula vitu vidogo ana hatari ya kupaliwa. Uwe mwangalifu unaposhika mifugo au vinyesi vyao na huku ukimhudumia mtoto. Ni vyema viatu vitolewe nje na visiingie ndani maana ni hatari kwa mtoto na watu wazima kuleta uchafu wa mji wote kwenye nyumba yako. Chemsha maji ya kunywa mara zote. Uwe na mpango wa huduma ya kwanza kama mtoto amekula sumu au ameumia. Mkaa uliosagwa unafaa sana kukabiliana na sumu. Uliza kituo cha afya

kilicho karibu kuhusu namna ya kuendesha huduma ya kwanza. Mtoto asichezee mifuko yoyote ya plastiki na kujivisha anaweza akose pumzi. Vyakula vingine kama zabibu iwe ni mwiko kumpa mtoto mdogo bila kuponda; imeua watoto kadhaa.

Kitu kingine cha kuzungumzia kuhusu watoto ni usalama. Mtoto ana hatari nyingi na ni vizuri kukagua mazingira yake mfano, mafuta ya taa. Watoto wadogo wakiwa na kiu wanaweza kuyanywa. Kuchezea moto au viberiti ni hatari. Watoto wasivuke barabara wenyewe wala wasiruhusiwe michezo ya kupanda mitin a awe mbali wakati wa kupiga deki. Angalia michezo wanayocheza watoto wadogo, kama ina usalama. Angalia mtoto asichezee silaha zilizo nyumbani kama panga, kisu, shoka nk. Je, kuna mashimo makubwa kwenye uwanja wako ambayo ni hatari mtoto kutumbukia? Je, una kisima, na vitu vya namna hiyo? Je, una bwawa la kuogolea au unaishi karibu na mto? Je, unao mtungi wa gesi? Je, umefungiwa kwenye kabati na una kufuli? Je, dawa zako zote ziko mbali na umezifungia? Ni muhimu sana, ujue mtu wa kumwita kama mtoto amekunywa sumu. Je, unaangalia usalama wa mtoto unapopikia jiko la mkaa? Usiondoke tu na kumwacha mtoto, kama kuna jiko la mkaa lililowashwa.

Watoto wengi wanaumia kwa kuvunjika kwa sababu ya michezo au mazingira ambayo wazazi hawajayatilia makini. Mahali pengine watoto wanajilea wenyewe tu, mtoto wa miaka minane ndiye anaangalia wale wadogo akiwabeba mgongoni na kuwalisha! Wazazi huenda mbali kwa muda mrefu na jirani wa siku hizi hawashuguliki; na jamaa zako wa karibu wako mbali. Wazazi; watoto ni lazima waangaliwe!

Mara nyingi tulifikiria kwamba watu wa Magharibi hawawajali watoto ila nimeona watu wa Magharibi wanaangalia usalama wa watoto zaidi kuliko sisi. Wanafundisha watoto cha kufanya moto ukitokea; simama, jidondoshe na ubiringike (stop drop and roll). Huwaelekeza pia njia ya kukimbia, mtu mgeni akimwulizia kitu asemeje, akipotea asemeje, ajue anapoishi, jina na namba ya simuya mzazi. Haya yanafundishwa rasmi. Watoto wasitumwe usiku mbali penye hatari peke yao.

Siku moja usiku karibu na mtaa wetu mama mmoja aliwatuma watoto wake wa miaka kumi na mbili na miaka sita, saa sita ya usiku kununua chakula, katika hoteli ya kichina. Ilikuwa ni mjini, taa zinawaka, ila walipigwa na bunduki wakafa! Kwa usalama wa mtoto mfundishe mambo haya, kwa vile haya yote yanalinda afya ya mtoto. Mhimize aripoti akiona jambo geni. Mama mmoja alisema kijana wake wa miaka kumi na tano, alipata kansa ya kizazi (testicular) na hakusema; alikuwa anaogopa. Akaenda kwa mganga kwa bahati nzuri, mganga akagundua ila ilikuwa imefika hatua mbaya na alipata mionzi na ikarudi.

Napenda kuzungumzia afya ya watoto wakubwa (miaka 12-18) kwa sababu wana mahitaji na changamoto tofauti. Wao wana uwezo wa kuchagua ila wana msukumo wa rika ambao unafanya uchaguzi wao uendane na rika lake hata kama hautamfaa. Ni muhimu kwa afya ya vijana kuchagua marafiki wa kufaa, burudani za kufaa na chakula bora. Jinsi ya kutumia muda wao na sherehe zao za makulaji. Kuwa na afya ni nyanja zote kiroho, kimwili na kiakili. Vijana wachukue muda kufanya mazoezi na kutokula vyakula ambavyo si vyema. Wasome maadili ya afya na kujaribu kuyatekeleza.

Jipende mwenyewe na jithamini. “Hakuna mwingine kama wewe, umeumbwa kwa kusudi maalumu.” Uwe muwazi kwa wazazi kueleza mambo yanayokuhusu na kusaidia afya yako. Kujua jinsi ya kuchukuliana na misongo na presha za maisha. Chukua muda kujisomea Neno la Mungu, na kujenga madaraja na urafiki na wengine. Nuia kuishi na watu vizuri na kuomba msaada endapo unahitaji bila kuogopa. Kwa afya njema hakikisha unakula matunda, mboga na nafaka zisizokobolewa. Jamii ya maharage na karanga ni muhimu. Usiache kula kifungua kinywa; huu ni mlo muhimu sana kwa akili inayokua. Kula chakula wakati akili imetulia. Kunywa maji vizuri na epuka vyakula au vinywaji vyenye sukari. Tafuna chakula chako vyema.

Unapotembea hakikisha mwondoko wako (posture) unakuwa bora. Mwondoko bora husaidia mifupa na misuli kukua vizuri. Chagua vyema viatu vyako; visiwe vya kubana au vya juu sana. Viatu vya fasheni nyingine vina shida za afya kama kuleta vidonda, kuharibu mgongo na vivimbe kutokea kwenye miguu (bunion). Nguo ziwe za kuendana na hali ya hewa, miguu na mikono isiwe wazi wakati wa baridi. Mikanda isiwe ya kukaza na kuvaa nguo za kubana vinafanya mapafu yasitanuke inavyotakiwa na usitembee au kusogea unavyotaka. Ukisimama kwenye ukuta kichwa, mgongo, makalio na visigino viguse ukuta nyuzi 90.

Tembea na mzigo kichwani husaidia kuwa na mwondoko nzuri, fanya hili zoezi mara kwa mara. Fanya zoezi la kuvuta pumzi kwa muda na kuitoa kwa muda (deep breathing). Mazoezi ni muhimu, yanalinda magonjwa mengi na yanafanya ujithamini na kuwa mtu mwenye furaha. Fanya mazoezi unayofurahia na yenye faida. Wenye uwezo wa kusikiliza muziki waweza kufanya vile. Kula vyakula vyote vya afya, vinasaidia ubongo. Mfano wa vyakula hivyo ni matunda, mboga, karanga, nafaka na jamii ya maharage. Pia unywe maji kwa ajili ya ubongo wako kwani asilimia 90 ya ubongo ni maji! Hakikisha umefungua madirisha yako. Tembea nje pia ili upate hewa bora. Panga muda wa kusoma ili usisome usiku wote wakati wa mitihani. Punguza usumbufu wakati wa mitihani na jifunze njia bora za kusoma na kukumbuka. Usingizi wa masaa manane ni muhimu.

Kuna kitu kingine kimezuka cha madhara kwa watoto; nacho ni madawa ya kulevya. Tabia ambazo ni hatarishi. Katika nchi nyingine watoto wamekuwa wakijiweka kamba shingoni kwa kujaribu na kuitoa. Hii inafanya wajisikie kama wamelewa. Jambo hili limeua watoto, maana mara nyingine hawakuitoa ile kamba kwa wakati wake. Wengine wamekuwa wakinusa harufu ya petroli au gundi, ili iwaleweshe, na mambo mengine ya kushangaza kila kukicha, cha karibuni ni sigara za elektroniki ambazo zimeharibu mapafu ya vijana wengi na wakafa. Kweli dunia inafikia kilele, kwani imekuwa tambara bovu. Vijana wengine pia wamefikiri kujiua au kutishia kujiua inasaidia kwa mstakabali wao. Jambo hili si kweli, Wazazi, kitu tunachoweza kufanya ni kuwa karibu na watoto wetu na kuwapenda. Ila hata hilo halitoshi, inabidi tuwakabidhi kwa Mungu maana yeye ndiye anayejua mawazo yao zaidi ya sisi. (Soma mengine zaidi kuhusu muziki na tabia au usalama wa mtoto).

Miaka ya karibuni watoto wengi wamekuwa wakijiua kwa ajili ya watoto wengine kuwanyanyasa (bullying). Mtoto anaweza akateswa na mtoto mwingine mpaka akakata tamaa ya maisha. Bully anamtishia “Ukiwaambia wazazi wako au mwalimu utaona!” Nakumbuka nikiwa na miaka saba, nikiwa darasa la pili, kulikuwa na bully mtoto wa

darasa la tano mnene sana, karibu na njia niliyopitia nikitoka shuleni. Akiniona napita anakuja na kunipiga makofi. Nilikuwa na hofu sikuwambia mtu kabisa! Sasa ukubwani ndiyo naliwazia kwamba ni wangapi wanateseka hivyo kama mimi, bila kusema? Hebu uchunguze na kuwauliza watoto.

Mtoto wangu wa miaka saba alipanda basi, kwenye mji wa wazungu na walimfanyia vile vile pia. Siku moja mtoto mmoja wa darasa lake alikuwa na miaka tisa, ila alikuwa na shida ya kujifunza (learning disability) na hakujua kusoma. Alimpiga mara kumi na mbilli! Mtoto aliponiambia, baada ya kuficha kwa muda mrefu, nilienda kwa mwalimu mkuu. Mwalimu alimwita mtoto naye akaja na mzazi wake, ambaye alifikiri haki ni yake kwa sababu "Mwafrika hana thamani!" Mwalimu na wazazi waliomba msamaha. Mtoto ni jirani wa karibu na sasa nimeona ana heshima ya aina kidogo. Peleleza kama watoto wako wananyanyaswa. Angalia kwenye internet www.breakingthesilencenow.org kuhusu tabia hii. Angalia pia kwenye tovuti www.doorpost.com na www.restorationinternational.com ,

Mambo mengine ya kuzungumzia ni kujichora miili (tattoo), kutahiri watoto wa kike, kutoa meno, kuchonga meno, au kutoboa miili. Haya si mambo ya kuendekeza. Vifaa vinavyotumika vina maambukizi -ni budi viachwe kutumiwa. Kwa jumla vipigwe marufuku kwani ni madhara kwa mtoto na hata watu wazima. Kuna kazi nyingine ambazo mtoto akienda kutafuta anaweza asipate kwa ajili ya michoro hii. Hata akitaka kuifuta inakuwa vigumu (irreversible). Zamani tulicheka wamakonde na wengine kwa kujichora ila leo mataifa ya magharibi yanatumia mamia ya dola kujichora, Neno la Mungu limezungumzia hili kidogo. Soma Kumb. 14:1 na Mambo ya Walawi 19:28.

Kwa wasichana nitasema kwamba mambo ya kuvaa nguo fupi au za kuonyesha sehemu nyeti ni hatari kwa afya, maisha na usalama. Tunahitaji kuvaa kwa adabu kama tunataka afya yetu iwe kamili. Wanaume wanaangalia na tunatuma ujumbe wa namna fulani, kwamba tunataka waje kwetu. Msichana mmoja akawa amevaa nguo fupi sana tena ya kumbana ajabu, akawa anatembea barabarani. Kulikuwa na genge la wavulana wakaanza kumwita kwa kumpigia miluzi. Msichana akawa amekwazika, akaniambia, "Tafadhali waambie hao wavulana wawe na adabu." Nikamwambia; "Kati yako na hao wavulana, ni nani anapaswa kuwa na adabu?"

Hebu tuwaambie wasichana kwamba kuna sehemu nyeti (private parts). Hizi ni pamoja na mapaja, matiti na mabega. Tunapovaa na kuacha sehemu hizi wazi, tunajikosesha heshima sisi wenyewe. Na wavulana watafikiria kwamba sisi ni wa bei rahisi. Tunawaalika pale tunapoitangaza miili yetu. Hebu tusipitie kila mtindo ili mradi ni mtindo. Usijifariji kwa msemo wa Let 'everybody' do it, because you are not 'everybody.'

Msichana japo wasema kwamba wanawake na wanaume ni sawa, hiyo si kweli. Wewe msichana ukitoka usiku wa manane na kutembea mjini unahatarisha afya yako na maisha yako kwa namna zaidi ya moja. Jua kwamba wewe ni msichana, na kwamba

unapaswa kurudi nyumbani kabla ya giza. Jifunze kutogombana na watoto wa kiume na kujiunga na magenge yao maana unajiletea hatari.

Viatu vya wasichana vimekuwa vimebuniwa na wanaume, na vingi havina afya. Vimetengenezwa kufanya mwili uonekane na kutingishika kwa namna fulani. Nina imani wanaume waliotengeneza viatu hivi kwa ile suluba vinavyotoa, wao wasingeweza kuvivaa hata kwa masaa mawili, ila sisi tunashinda navyo siku nzima!

Mabadiliko ya kukua yanapotokea huwa ni changamoto kwa wazazi na vijana. Kwa mfano kuwa na hasira na kugombana. Hili limezungumziwa kwenye sura za **'Ujana'** na pia **'Afya ya vijana.'** Jamiii ina matazamio ya kielimu, kusaidia kazi nyumbani na misukumo ya rika.

Mchunguze mtoto wako kama ni mtu anakuwa na huzuni, hasira, woga, kutotilia makini vitu, kurudi nyumbani usiku, kutotaka marafiki, kukaa peke, kusikia sauti, nia ya kujidhuru au kudhuru wengine, anaharibu vitu kwa makusudi, anakunywa pombe au kuvuta sigara, anakataa kula au anakula na kutapika, analala siku nzima, anasema hawezi maisha, ndoto mbaya, kujifikiria kwamba ni mbaya, anasita kukata shauri, anarudia vitendo mara nyingi kama kuosha mikono (obsessive compulsive), dhamira kumshtaki na mengine kama hayo. Mara nyingine mabadiliko ya mwili na hisia katika kukua yanaleta haya, na pengine anahitaji msaada wa kuzungumziwa na kujua kwamba haya ni stage tu na kwamba yeye si tofauti sana. Anaweza kupata mshauri mwenye hekima na uzoefu.

Mara nyingi kwa kupendeza jamii (social life) watoto huanza kunywa hata kabla hawajafikisha miaka kumi na miwili! Hii ni hatari. Mithali 20:1, inasema; "Mvinyo ni hudhiha, kileo huleta ugomvi." Kama kuna vinywaji vingi tu ambavyo haviharibu afya yako, mfano zabibu, limao, tangawizi au tufaha (apple), mbona unywe pombe? Kunywa juice pamoja na matunda ni bora kuliko pombe inayoathiri ubongo na afya yako kwa jumla. Mambo mengine ni kama kunusa gundi au petroli, kujikata mwili ili kupunguza maumivu ya hisia, au kuvuta sigara za electroniki na kufanya mapafu yafe. Haya kila mzazi yapasa ayapeleleze kidogo na kuyajua yanayoendelea kwa vijana kwenye mtandao au kwenye maisha ya kila siku, kwani kila kukicha adui anavumbua vitu visivyo na wema ila vinachukua maisha ya vijana wetu kiroho au kimwili. Hebu tuombeane kwa haya yote maana hatuwezi kujua yote, ila tujikabidhi kwa MWENYEZI MUNGU kila siku na kumwomba HEKIMA.

Kitu kingine cha kuzungumza kwa vijna ni afya ya ngono. Media vyombo vya habari, magazeti, tv na radio vimefanya watu wanaoshugulikia ngono nje ya ndoa ni mashujua na wajuzi. Wanasema chochote kinachokupa furaha kukifanya. Mungu ana viwango vingine kwetu. Anataka tuweke mpaka na kuishi maisha ya usafi na furaha na bado tuwe katika mpango wake.

Wasichana wadogo wamekuwa na msukumo wa kuvaa kama wanawake na kuanza ngono mapema. Nikifanya kazi katika hospitali kubwa ya magonjwa ya akili Hagerstown (wagonjwa 2000) niligundua kwenye utafiti wangu kwamba zaidi ya asilimia sabini ya wagonjwa hawa walikuwa wamefikia hali hii kwa kutokana na mambo ya ngono au ulevi. Niliona msichana mmoja akila kila kitu alichokiona, alikuwa na miaka kumi na tisa. Alikuwa amepasuliwa mara nane kwa kula balbu, misumari, na vitu vingine. Alilindwa na mtu

mmoja; kila akienda hata chooni mlango uliachwa wazi huku akijisaidia. Chumbani kwake kulikuwa na vitu vichache mno. Alishiriki mambo ya ngono kuanzia utotoni na wazazi hawakulijua hilo.

Aliponzwa na msukumo wa kutaka aonekane kwamba anafaa kwa rika lake, na kwa vile vijana hawakuwa wakimfuata alihisi kuwa maumbile yake si mazuri sana japo yalikuwa mazuri. Aliona wazazi wake wana shuguli nyingi na kwamba hapendwi akaendelea kujaribu kutafuta upendo kwa wavulana ambao kwa kweli walitaka kumtumia tu. Hata wengine walimnyanyasa kingono kwa nguvu, (kumbaka) akiwa mtoto wa chini ya miaka kumi na sita! Alikuwa hajithamini kabisa.

Msukumo wa ngono unaharibu afya ya wasichana na hata wavulana wengi. Ushoga umeingia siku hizi na hata wavulana wadogo wanaanza kulawitiwa. Hata kama ni viongozi wa dini; kama magazeti yalivyotoa kwamba, maelfu ya watoto wanahudumu kwenye kibweta wakati wa misa walikuwa wamelawitiwa na viongozi wa dini! Hata mtindo kujamiiana wanawake (lesbian) umekita katika shule za mabweni, (boarding). Shetani ameingiza mawazo kwa watu kwamba waliumbwa hivyo!!! Wanasema 'Tupo tofauti' "we are different!" Mwombee mwanao na ujaribu kumlinda kadri uwezavyo, ili kibinadamu akuone rafiki na kukwambia mengi usiyoyaona au kuyawazia.

Magonjwa ya zinaa yanaongezeka kwa watoto. Shule moja waliuliza watoto wasichana wa umri wa miaka kumi na mitano, asilimia 45 walikuwa wamefaya ngono na 31% ya wavulana. Kuna haja ya kuzungumza na watoto mambo ya ngono safi na haramu. Hata kuhusu mambo ya mimba na kutoa mimba. Mwisho wa watoto wanaohusika na mambo haya ni kutokuwa na nyumba nzuri na/au talaka. Watoto wakizaa hawana baba au usimamizi, na watoto wanalea watoto.

Waelimishe watoto kuhusu kujitunza na usafi wa ngono. Wazazi wengi wanafikiri kwamba kutumia kondomu ndiyo ufumbuzi. Nimeona mama mmoja akimpatia msichana wake kondomu! Si kweli, hii inajenga mtoto kuwa mpotofu zaidi, na hata hivyo kondomu yaweza kuzuia mimba ila haiwezi kuzuia huzuni, kutojithamini na kutofaa. Kutumia kondomu kwaweza pia kuwadhuru mawazo yao. Usimweleze mtoto wako kuwa kondomu ndiyo mpango wa furaha, bali msisitizie kungoja mpaka wakati wa kuolewa au kuoa.

Washauri watoto wako kwamba usafi ndiyo ushujaa, kama Yusufu alivyoonesha ushujaa pale alipomwambia mke wa Potifa, "Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkosee Mungu?" Mwanzo 39:9. Vijana watawale mawazo yao na kutafuta mambo ya kuwashugulisha badala ya ngono. Waombee kwa bidii, waepuke kutongozwa na watu na kukaa kwenye sehemu za giza au kujishugulisha na marafiki wa namna hiyo. Kama ni msichana mkubwa na ameenda na mchumba wake mahali pawe mahali pa wazi, penye

watu wengine na mpange washauriwe kuwa na shuguli za kufanya ili mawazo yao yasitawaliwe na yale ya uovu.

Mungu ni mwenye Rehema. Wakati tunapopotoka (maana sisi tu binadamu) tukiungama tunaanza ukurasa mpya. Lazima tugundue hitaji letu ili Atusaidie. Kama umeanguka kwenye jaribu la ngono kijana jitoe katika hali hiyo haraka. Sali kila siku, watu wazima wenye hekima wakusaidie utoke kwenye shimo hilo. Jua kwamba ukiungama kwa dhati unaanza safari upya. Shetani asikukumbushe ya zamani. Akizidi kukukumbusha yaliyopita na wewe mkumbushe yatakayomjia yeye, yaani Jehanamu.

Wazazi, kuweni mfano bora nasi tufuate mpango wa Mungu wa usafi wa ngono. Kina mama wengine au kina baba wanaleta marafiki zao wa kiume/kike na kulala nao, huku watoto wakiona! Hii haisaiidii malezi ya watoto na tabia hii itakuletea aibu na laana. Watoto wataiiga, “Like father like son.” Nimeona rafiki wa kiume wa mama akianza kumwingilia mtoto wake wa kike! Usihatarishe afya ya mtoto.

Mambo ya madisko kama unawapeleka watoto wako kwa kweli ni kitu cha kuangusha maadili. Wangapi walipelekwa na wazazi wao disko? Je, ukimwona kijana amemshikilia binti yako kwa kubanana na taa zimezimwa au vimulimuli utaonaje? Ngoma za jadi za kiafrika zilikuwa zina adabu zaidi watu walicheza mbali mbali. Hata mashuleni watu waliocheza ngoma za jadi sikuona watu wakikumbatiana vile. Maumbile ya kike na kiume si ya kukumbatiana vile labda mtu na mume wake au mtoto na mzazi. Na hata mzazi, mtoto akiwa mtu mzima unampa nafasi yake (space). Ni heshima. Mambo ya shule za sekondari kuwa na madisko ya watoto yameleta uzinzi na uasherati mwingi. Nasema niliyoyaona. Japo sikutilia maanani kwamba ni jambo baya, na sikwenda, lakini niliona athari zake kwa waliokuja bwenini kuhadithia.

Msichana mmoja katika dansi walianza kufanya ngono na kijana mpaka walifukuzwa kwenye dansi, ila waliendelea na urafiki na siku moja tukisafiri kwa meli walifanya ngono kwenye meli na watu walishuhudia! Hamuwezi kukumbatina kwa dansi na kusema mko salama kimaadili. Awe mke wa mtu au siyo staili hiyo ni ya mtu na mke wake tu ndiyo wameruhusiwa. Hata hivyo umeona wanaume Waafrika wangapi wakipeleka wake zao kwenye dansi (disco)? Hebu jaza mwenyewe. Na sina mjadala zaidi na hilo. Kama wewe ni mtu mzima hasa mwanamume au mwanamke umenielewa vyema kabisa sina haja ya kusema zaidi.

Fundisha watoto wako kuwa na huruma na kuwa na marafiki ambao wana kilema au upungufu fulani. Watoto wana ukatili kwa watoto wenzao walio na ulemavu; mfano kigugumizi. Huwa wanawacheka na kuwasema kwa sauti kubwa na kuwatenga. Tabia hii si nzuri.

Habari ya mzio (allergy) ni ya kuangalia sana. Kuna watoto wasiopatana na vyakula, dawa au hali ya hewa fulani. Hii yawafanya wawe wagonjwa. Vyakula vingi mara nyingi vina mzio mdogo mdogo; vingine vina athari kubwa sana hata kuua. mzio ni namna

ya mwili ya kuitikia kwa jazba kubwa kitu haniwa ni hatari na kumbe si cha hatari au kwa kawaida ni rafiki.

Mtoto mmoja alikuwa ana uzio wa ufuta, na rafiki yake alimpa kipande cha kuku shuleni, na kilikuwa na ufuta. Kijana huyu akashindwa kupumua na mwili ulivimba kwa haraka sana akaanguka na kufariki papo hapo! Ila wengi wana shida ya vyakula hasa maziwa, nguruwe, nyama ya kondoo, mahindi, ngano au mayai. Waweza kupunyuka nywele, kuota upele, kutoka vidonda, kupata shida ya kupumua au kuwa na pumu nk. Mzazi agundue kile kinacholeta uzio na kukiondoa. Dawa ni kumwambia tabibu au wewe mwenyewe panga kutompa. Mfano watoto wengi wana uzio wa ibuprofen. Kwa hali ya hewa tofauti au kwa chavua za maua, omba ushauri wa tiba jinsi utakavyoweza kuepuka shida hii.

Tabia nyingine kama kuwa na hasira imegharimu afya za watoto na wakubwa. Zungumza na mtoto kuhusu hasira za waziwazi na zile za ndani. Jinsi ya kuondoa hasira n.k. Kuna watu wengi wanatembea na hasira toka utotoni wakiwa wamezifungia na siku ya kulipuka zinakuwa na madhara makubwa. Mama fulani wa kimarekani, akiendesha gari alikuwa anakuwa na hasira (road rage) ya kupiga honi, mtu akichelewa kidogo, na kunyoshea madereva wake mikono wanaochelewa au kumpita vibaya. Haya yanatokana na mambo yanayoendelea katika maisha yake na siyo sana sana wale wanaokuwa barabarani.

Siku moja mama huyu aliyekuwa anabeba bunduki, alimlenga dreva mwingine akapiga bunduki na kumwua eti kwa sababu aliendesha pole pole! Mtu asiyemjua kabisa! Halafu akimpiga bunduki akasema “pole sana.” Twaweza kushangaa ila tabia hii ya hasira ipo kila mahali na inajitokeza kwa watoto pia wakiwa wanacheza na hiyo huwa ni hatari. Ni muhimu kufundisha watoto wakiwa na hasira wafanyeje? Je, ni sawa kwa sababu ya hasira yake amwumize mwingine au ajiumize? La hasha! Katika dunia ya misongo kwa watoto na watu wazima ni muhimu kulitambua hili swala na kulishugulikia baada ya kulijadili.

Epuka kuabudu marafiki na tunza watoto wako. Nimeona mama wengine wana watoto wadogo ila mgeni akiingia wanasahau hata mtoto yuko wapi. Au akipigiwa simu anaacha anachomwambia mtoto hapo hapo “halo, halo;” tumeziabudu simu mpaka tukakosa adabu hata mbele ya watoto wetu! Wewe utajisikiaje ikiwa unazungumza na mtu na ghafla akaanza kusema “halo halo?” Jifunze nidhamu, “Sema samahani, naomba nipokee hii simu.” Watoto wako watakuiga, na mtakuwa nyumba ya halo, halo na siyo mahali pa mafunzo.

Epuka na kuabudu marafiki na tunza watoto wako. Nimeona mama wengine wana watoto wadogo ila mgeni akiingia wanasahau hata mtoto yuko wapi. Au akipigiwa simu anaacha anachomwambia mtoto hapo hapo “halo halo” tumeziabudu simu mpaka tukakosa adabu hata mbele ya watoto wetu, .wewe utasikiaje ikiwa unazungumza na mtu na ghafla akaanza kusema “halo halo”. Jifunze nidhamu, “sema samahani nipokee hii simu. Watoto wako watakuiga mtakuwa nyumba ya halo halo na siyo mahali pa mafunzo. Yawezekana si kitu kwa watoto wakubwa ila wadogo ni kitu.

Mtoto wangu akiwa na miaka miwili alikuwa anakuja kunitoa kwenye simu, alikuwa akisema kitu sisikii kabisa! Nampa usikivu wangu rafiki wa simu, Alipofika miaka mine alisema “mama wewe hunijali unapenda simu tu hata mtu akikuambia nyumba inaungua hutasogea” alijaribu kupindua shingo yangu ili nimsikilize akisema kitu au alipiga makelele ili nitoke kwenye simu. Mara nyingine jifunze kusema “nitakuita baadaye” kama unataka uwaweke watoto wako sawa na karibu. Mbona neno la Mungu hulikazanii kama simu, je umeshamwambia rafiki “ huu ni muda wangu wa kusoma au kuomba niite wakati mwingine?”. Mtu mwingine alisema endapo tungejali simu zetu kama NENO la MUNGU tusingeacha kutembea nalo wakati wote, na wala na wala lisingepata vumbi na kusahaulika mahali miaka mingi mpaka shida au dhiki itokee ndipo tunalishugulikia.

Sura ya 21
KUTII

Yasemekana kwamba mfalme Edward wa Uingereza alitembelea Marekani mwaka 1936 na akasema haya; “Uingereza watoto wanatiii wazazi, ila hapa Amerika wazazi wanatii watoto!”. Je mwaka huu wa 2019 tungeweza kusema nini kuhusu nukuu hii? Tabia ndicho kitu pekee tutakachokwenda nacho mbinguni. Tabia si kitu tu cha kuonekana mbele ya watu. Tabia ni kitu kinachojengeka katika maisha ya mtu (lifetime). Utii ndilo somo la kwanza ambalo mtoto anapaswa kujifunza. Katika kitabu cha Methali 22:6, tunaambiwa: “Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.” Je, Biblia inaongopa? Ni njia ipi hii impasayo mtoto? Siku hizi kuna kilio kikubwa kati ya wazazi wengi, kwamba watoto wa siku hizi wameshindikana! Je, shida iko wapi? Je, kosa ni la watoto, wazazi au nani? Kwa kuwa tunafahamu kwamba Neno la Mungu ni la kweli, basi hitimisho ni kwamba malezi (njia impasayo) ndiyo yana kasoro.

Wengi wetu tumechelewa kulea watoto wetu, Kwani inatakiwa tuanze mapema, wakiwa wachanga. Walipokuwa wanalilia vitu, hata ambavyo tulifahamu kabisa kwamba havikuwafaa kwa wakati huo, tuliwapatia tu, labda kwa kufikiria ni haki yao kupewa kila kitu wanapokitaka, au kwa kutaka kukatisha usumbufu na kelele za kuliliwa. Wakati huu ndio ulikuwa mzuri wa kuwafundisha somo la maana maishani: UTII. Tunamshukuru Mungu kwa maana kwake hakuna kisichowezekana. Kwa neema zake tunaweza kuanza hata sasa, Yeye anafahamu mapungufu yetu, na atatusaidia.

Hebu watoto wajue kuhusu mema na mabaya wakiwa wadogo. Hebu wajue ni wakati gani wa kusema ‘ndio’ na wakati gani wa kusema ‘hapana.’ Na tuwafundishe kwamba wanaposema ‘ndio’ wamaanishe hivyo, na wanaposema ‘hapana’ pia wamaanishe hivyo. Wafundishe kuheshimu watu na vitu, vitu vyao na pia vya watu wengine. Wafundishe kuhusu miili yao na sehemu zao za siri, yakiwemo mapaja, matiti na tumbo. Tusivae nguo na kuacha sehemu hizi wazi! Mungu anataka tuheshimu na kutunza miili yetu. Kila siku, angalao kwa dakika chache (25-30) barizi na kuzungumza na mtoto wako, kuhusu aliyoyafanya shuleni/kazini siku hiyo. Tusingojee wafanye makosa ndio tuwape ‘lecture’ (msomo), hiyo huwa haisaidii sana. Wasipofahamu wakiwa nyumbani, watapata waalimu, hasa rafiki zao,

watakaowafundisha. Tunamshukuru Mungu kwa maana kwake hakuna kisichowezekana. Kwa neema zake tunaweza tukajaribu, kwani anaelewa mapungufu yetu.

Wapangie watoto majukumu na kazi za kufanya. Wasipokuwa na kitu cha kufanya, mwovu atawapatia. Wasizurure tu hapa na pale, wakitembelea marafiki bila ruhusa yako kama mzazi. Muwe na sheria chache tu katika familia, ambazo kama mzazi utaweza kuzifuatilia, na kutoa adhabu kulingana na umri wa mtoto. Hakikisha kwamba baba na mama mnakubaliana na sheria mlizoziweka na pia adhabu mnazozitoa. Baba akisema hili, mama asipinge, wote muwe kitu kimoja katika kuadhibu. Kama hamkubaliani, hebu msipingane mbele ya watoto.

Mume wangu anapenda watoto wazungumziwe kwa sauti ya upole. Nilipokuwa ninawagombeza na kuwakemea kwa sauti ya juu, angenyamaza tu, kisha baadaye tukienda chumbani, ananiambia, “Jamani, kama kelele unazopigia watoto zingekuwa zinasaidia, kweli ungekuwa bado unazipiga? Si wangeshakuwa kama malaika? Tafadhali uwe unaongea na watoto kwa sauti ya upole.” Alisihi. Namshukuru Mungu kwa kunipatia mume mpole na mnyenyekevu, sifa ambayo wengi wanadhani kwamba ni udhaifu! Amenitoa mbali na kunifundisha kufikiria kwanza, kabla ya kuropoka maneno.

Pia hapa lazima niseme kwamba, usiadhibu wakati una hasira. Wafundishe watoto kuomba msamaha, na wakati mwingine uwasamehe. Waadhibu tu wanaporudia kosa hilo mara kwa mara, hata kama wameomba msamaha. Kumbuka Mungu wetu anavyotusamehe pia, ingawaje wakati mwingine tunalipa kwa makosa/dhambi zetu. Kama Musa alisamehewa alipopiga mwamba badala ya kuuzungumzia, lakini akaambiwa hataingia katika nchi ya ahadi. Msichana akipata mamba akiwa shuleni, Mungu atamsamehe lakini mimba haitatoka. Atafukuzwa shule, na akijifungua, mtoto hatakufa kwa sababu alisamehewa, itambidi amlee mtoto huyo. Kwa hiyo mfundishe mtoto kwamba kuna hathari (consenquences) za makosa au dhambi zetu, hata tukisamehewa.

Wafundishe kumheshimu na kumpenda Mungu na siyo kumuogopa. Heshima inatokana na upendo. Tunapowapenda wazazi na walimu wetu, tutawaheshimu. Waambie kwamba Mungu anataka wazazi pamoja na watoto wao wote waende mbinguni.

Mume wangu ambaye ni mchungaji, aliambiwa kipindi fulani alipokuwa ameenda kwenye makambi kwamba ‘Mchungaji, katika kipindi cha jioni cha Kaya na Familia, usitufundishe kuhusu uhusiano wa mume na mke, tafadhali tunaomba utufundishe juu ya kulea watoto, wametushinda!’ Basi tangu wakati huo, aliamua kufundisha kuhusu malezi ya watoto wakati wa makambi. Hili ndilo dhumuni la kitabu hiki. Kuona ni “njia ipi impasayo” mtoto, na ambayo “hataiacha hata atakapokuwa mzee.”

Katika kitabu cha Kutoka 2:9, binti Farao alimwambia Yokebedi: “Mchukue mtoto huyu ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako....” Binti wa Farao alimlipa mama ya

Musa mshahara, lakini alilipwa zaidi ya mshahara na Mungu, ambaye alimlipa mshahara mzuri zaidi ya pesa. Alikuwa na furaha ya kumlea mtoto wake “katika njia impasayo,” nje ya anasa za Misri na akawa mkombozi wa watu wa Mungu, na baadaye kwenda mbinguni. Hili ndilo JAMBO MUHIMU kuongoza watoto wetu kumfahamu Mungu na hatimaye waende mbinguni pamoja nasi.

Somo kubwa la kumpa mtoto ni kuikana nafsi na kuitawala nafsi. Mzazi pia awe mtu wa kuitawala nafsi na kuikana nafsi ili mtoto aone mfano. Mzazi na hasa mama asichoke, kila tendo ni tofali linalojenga tabia ya mtoto. Mtoto anahitaji upendo na nidhamu kwa kipimo kinacholingana! Mtoto anajenga familia, familia inajenga kijiji, kijiji kinajenga wilaya, wilaya inajenga mkoa, mkoa unajenga taifa, taifa linajenga bara na bara linajenga dunia. Inabidi mtoto ayashinde majaribu, ili tabia iweze kuwa ya kiwango cha juu.

Mzazi awe na malengo na magoli ya utii na nidhamu. Utii ndiyo somo la kwanza mtoto anabidi kujifunza. Usifikiri mtoto wako hapendi utii, la hasha. Ukimwacha afanye anavyopenda atafika mahali ataogopa, maana ataona hana usalama na watu hawampendi maana hawamshugulikii! Kama mzazi hajui amri za Mungu ajielimishe na Neno la Mungu na Amri zake! Mungu Amempa mzazi jukumu la thamani la kujenga tabia ya mtoto. Yule anayetaka kuvuna vizuri sharti atayarishe udongo vizuri. Kazi hii ni ya muhimu zaidi ya kutafuta pesa. Nyumba ndiyo maabara, chochote kilichopindika sharti kinyoshwe.

Wazazi msifanye kosa hapa kwa kujichosha kwa kazi nyingi. Uwe muwazi kwa watoto wako na kuwa mwaminifu na utaona matunda yake. Mama kupamba nyumba yako na usafi, umaridadi na nakshi ni jambo jema, ila ikiwa watoto wako watakuwa hawana adabu na tabia njema basi utakuwa umefeli somo. Tunaelewa haya hayawezekani ila kwa maombi mengi na kuongozwa na Roho wa Mungu. Hebu mweke Mungu kama nambari moja, Yeye Atakusaidia.

Ni muhimu wazazi wafundishe watoto toka wanapozaliwa kwamba ufunguo wa furaha uko katika kutii. Tunazaa ili tushugulikie watoto hawa, na siyo kukabidhi watu wengine kama mayaya, mashangazi au mabibi. Kutii liwe somo la kwanza. Hebu tufundishe watoto kutii na kuthamini wazazi. Watoto hawawezi kumtii na kumthamini Mungu endapo wanakosa adabu kwa wazazi, walimu na watu wengine wazima. Hebu wasikilize wazazi wanayosema na kuthamini mausia ya wazazi na kuheshimu mamlaka yao.

Watoto wanakuwa na furaha kamili wakiwa wanaadabishwa na kufundishwa nidhamu nzuri. Wataona baadaye kutii sheria za Mungu inaleta uhuru halisi hapa duniani na katika maisha ya baadaye. Kufanya mapenzi ya Mungu ambayo ndiyo sheria yake ni sheria ya mbingu pia. Hebu wazazi tuwafundishe watoto kwamba mtindo wa maisha ya mbinguni tunaanza kufanyia mazoezi hapa hapa duniani. Historia ya Adamu na Hawa yatuonyesha wazi jinsi utii ulivyo wa muhimu. Waliishi katika bustani nzuri, na wakimiliki dunia nzima. Lakini kwa kutotii, walianguka na kuanzisha dunia kuwa na mlolongo wa shida nyingi kama, maumivu, vilio, na kifo. Hebu na tusome Neno la Mungu na watoto wetu ili tuone jinsi mibaraka ya kutii inavyomwagwa. Watoto wajue kwamba Kristo alikuja duniani kutupa mfano hai kwa kutii. Watoto waweze kutofautisha wema na ubaya. “line upon line and precept upon precept.

Toka umri mdogo, mara nyingi tunawaachia watoto wa miaka mitatu hata minne bila ya kushugulikia utii na ubinafsi unakua na shetani anajiinua kichwa chake katika watoto hawa. Jinsi siku zinavyokwenda ndivyo inavyozidi kuwa vigumu kukunja samaki mbichi. Mara zingine tunaona kama analeta vichekesho kwa kutotii 'Huyu ni mtundu sana' "He is so cute." Biblia yasema, "Mtoto anajulikana kwa tabia yake toka udogo." Mtoto mwenye ukaidi au nia ngumu (strong will), asaidiwe ili awe na kiasi; ajitawale nafsi. Mtoto mdogo, asikie, aelewe na atii kile anachoambiwa.

Mzazi apaswa pia ajifunze Neno la Mungu ili yale matakwa yake kwa mtoto yawe ni mapenzi ya Mungu. Jambo hili litasaidia kujenga mawazo ya watoto ambayo yatajenga matendo, ambayo yatajenga mazoea na mazoea yatajenga tabia na tabia itajenga mustakabali (thought, action, habit, character, destiny). Mtoto asideke na kulilia akijigaragaza chini. Mfano kile ambacho unaona hakifai na ukampa kwa kumdekeza au kupunguza bughudha kitakuja kumgharimu siku moja. Mzazi na hasa mama, apunguze ghadhabu na asionyeshe wazi hisia zake (outburst of anger). Mzazi asimamie yale aliyomwambia mtoto kama yamefanywa. Kufuatilia ni muhimu, kusipokuwa na kufuatilia, mtoto hatawajibika. Tofali la tabia litakuwa limebomoka.

Wazazi watawale tamaa zao za mwili kama hasira, ulafi kabla ya kushugulikia hisia za mtoto. Mzazi asichoke kutenda wema, atoe mfano bora;
1 Wakorintho 15:58 . Alexandar wa Makedonia aliona ni rahisi kuteka nyara miji ya dunia kuliko kutawala tamaa zake (self control). Usiache watoto wakakosa adabu kwako na kuzungumza chochote. Mama asiwe anapendelea watoto katika kutiisha au kuadabisha, awe mtu wa haki. Mama asiwe na shuguli nyingi na kufuatilia maadili ya mtoto kukaachwa. Watoto wako waonyeshe kwamba kufuata sheria ni muhimu, hata sheria za nchi; kama hazipingani na za Mungu. Watoto wajifunze kutulia wasiwe na tabia ya kelele nyingi na kupiga mayowe siku nzima nyumbani. Wazazi wafundishe watoto kuthamini mali ya nyumbani na ya watu wengine pia, Wasiharibu haribu vitu. Wasipojifunza kuthamini mali za wengine, hata zao wakifika wakati wa kuzipata, watazitapanya ovyo.

watoto wafundishwe kumaliza kazi walizopewa, mara nyingi watoto huanza kazi kwa furaha na kuchoka katikati na kutaka kubadilisha, au kwenda kucheza. Watoto wajifunze kujikana nafsi, wasiwe wakijifikiria wenyewe tu, wajue maisha ya kuhudumia watu na kujali wengine. Watoto wajifunze kuwa waaminifu, na usafi wa moyo. Wawe na bidii ya kazi. Wajifunze kutatua matatizo, hii itawafanya waweze kuwajibika kwa majukumu yao, (problem solving).

Najua wengine tumeshakosea mengi ila napenda kusema kwamba tusikate tamaa, Mungu ni mwenye rehema na atatusaidia kuanza upya pale tulipo, hata kama watoto wamekuwa wakubwa. Twajua kwamba kuna watoto wengine hawatasikia mashauri japo wazazi wamefanya yote kwa uwezo wao kuwaadilisha. Lakini utakuwa umefanya sehemu yako ya malezi bora. Hebu wazhazi wawachagulie watoto mazingira mema katika malezi ya watoto. Niliona wazazi Dar, wakipeleka watoto wao katika madisko ya watoto, na michezo ambayo kwa msingi itazaa dhambi, shida au ubatili maishani. Mzazi apaswa kuepukana na vitu ambavyo ni dhahiri, hata wazazi wetu wa zamani hawakufanya.

Kutunza mtoto ni zaidi ya kumpa, chakula mavazi na malazi. Ni kushugulikia tabia yake. Hebu tupande mbegu ambazo ni sahihi. Tusiwachokoze watoto au kuwanyanyasa. Waefeso 6:4. Hiyo hufanya tabia iwe potofu. Nimeona wazazi wengi hasa wakina baba wanaopenda watoto wao wamtii Mungu, na kusoma Neno lake na kwenda kwenye mikutano ya dini, kama makanisa, ila wenyewe hawaonekani huko.

Watoto wengi wamependa matendo ya giza, kama kunywa pombe, kuishi maisha ya uasherati na mengineyo ila mzizi wake watokana na wazazi wao. Maelfu ya watoto wanapotea kwa ajili ya wazazi kutokuwa na mwongozo wowote wa kiroho na kufanya dhambi za wazi wazi mbele ya jamii. Hebu baba ambaye ndiye kiongozi na kuhani wa familia aonyeshe tabia ya Mungu kwa watoto. Mtoto kuweza masomo shuleni tu, si msingi wa kuishi maisha mema na ya mbaraka duniani. Watoto wengi wamesoma vizuri na kupata kazi nzuri ila maisha yao yamekuwa ya ubinafsi na anasa nyingi.

Wazazi wanajenga tabia bora ya mtoto kwa kutumia wakati wao kusaidia watoto. Hatuwezi kusema fanya anavyokwambia na siyo anavyofanya kwa mtoto. Mzazi ajifunze kanuni za Mungu na kwenda kwa kina katika kumsaidia mtoto. Mzazi achukue muda kumwombea mtoto. Mzazi ameleta mtoto duniani ambaye hakuwa na uchaguzi, hebu basi asizembee mtoto huyu akaenda jehanam! Mara nyingine mzazi anamtetea mtoto hata mbele za watu; “Mtoto wangu ni mwema sana hawezi kufanya hivi au vile.” Jua kwamba adui apenda kutumia watoto. Mtoto asaidiwe kukua Kiroho, kimwili na kimawazo. Hata afya inafanya mtu kuharibikiwa na maadili. Hebu chakula cha ubongo na mwili kiwe safi. Mtoto akiwa na uwezo wa akili darasani ila maadili maovu, atakuwa amefeli. Hebu wazazi tuombe hekima ya mbinguni, na kuwasaidia watoto wetu kuchagua uzima na siyo mauti.

Tabia mbovu ya mtoto mmoja huathiri wengine pia. Hata matendo yanayonekana madogo ambayo ni maovu yana mvuto mkubwa. Matendo mabaya yanatendeka na kuigwa kirahisi kuliko mazuri. Bongo za watoto ni kama udongo wa mfinyazi ulio mbichi kwani unachukua umbo unaloweka. Vitendo hivi vya udogoni ndivyo vinavyoleta maisha ya ushindi au maanguko.

Mzazi asomee haiba ya mtoto na kujua atamsaidia mtoto na maadili mema. Tabia za giza zisaidiwe kuondoka, zitolewe; na zile nzuri zipewe jukwaa. Kuna watoto wanaohitaji kuadabishwa kuliko wengine. Kuadabisha kwa watoto kunatofautiana na haiba. Kila mtoto ana nia (will) na hiyo lazima isalimishwe kwa Yesu, kwa kuelekezwa na siyo kuburuzwa. Afundishwe kutawala nafsi. Ovu lolote linapoonekana lishugulikiwe. Hakuna aliye mchanga sana asishugulikiwe na nidhamu. Ikiwa watoto wadogo wa miaka miwili, wanafanya maovu na kuongozwa na Shetani, basi hata kuongozwa na Mungu kunawezekana zaidi!

Sura ya 22
WAKWE NA WAZAZI WENZA

Watoto wetu wanapotafuta wachumba inabidi tuwe msaada kwao kwa kuwaelezea mambo ambayo yatawasaidia; kwani mapenzi yanaweza kuwa na upofu wa aina fulani. Jitahidi kuwa na sababu za msingi kwa mtoto wako kuhusu kuchagua mchumba. Usiangalie sana habari ya umasikini alio nao au kabila lake. Usiwe mtu mwenye kugandamiza kwa udikteta mtoto wako aoe au asiolewe na fulani bila sababu za kuridhisha. Wazazi wengine wanakuwa na picha ya wale ambao wanataka watoto wao waoe: kwa mfano; awe tajiri, au awe mtoto wa mtu mashuhu, kabila, rangi, sura, kisomo au umbo fulani!

Jifunze "kumwacha" mtoto wako ili aambatane na mke wake au mume wake. Waingereza wasema kata kamba bila kukata mahusiano! Sasa ni watoto wa kila mtu katika jumuiya. Waweza kuwapa upendo ila si mawazo yako . Jifunze jinsi utakavyoheshimu ndoa ya mtoto wako. Kina mama na baba wengi wameharibu ndoa za watoto wao wakifikiri kwa vile waliwazaa na kuwalea wana mamlaka ya kuendelea kufanya hivyo. Ni vyema kila mtu awe na mahali pake pa kuishi ili muachane, labda iwe dharura tu. Na wale ambao wameoa na wanakaa pamoja, kama makaka wawili, ni vizuri wapeane nafasi ya kukaa mbali mbali ili watu wasiingie katika magomvi bila sababu na kumruhusu ibilisi kuwatweza. Mama mwingine alisema ukiolewa na mwanamume yatima na asiye na dada una bahati! Nikamwuliza kwani? Akasema, "Huna mama mkwe au wifi wa kukutawala na kukuchukia na kukuburuza buruza. Na mume wako kwa vile alikuwa hana familia anakutendea mema kwamba angalau sasa ana familia!".Jamani, mtu alifikiria mazito hata kuona kwamba mtu akiwa yatima ni vizuri!

Wazazi ni zawadi toka kwa Mungu, watoto wasio na wazazi wana umasikini mwingi. Ila kuna wazazi ambao wanaharibu ndoa za watoto wao. Watoto wao pia wanaenda kuharibu ndoa ya kaka au dada yao. Kuna njia nyingi ambazo wazazi wanajiingiza katika ndoa za watoto wao kuleta vurugu au kuachanisha.

Napenda kusema kwamba moja wapo ya shida zinazotokea hasa siku hizi ni mzazi kuchukia sana au kusikitika sana yule ambaye mtoto wake anachumbia na hatimaye

kuoa/kuolewa. Mama aweza kutaka kijana wake aoe msichana mwenye bidii ya kazi, anayevaa nguo za heshima, anayemwacha kijana wake huru aje nyumbani saa yoyote n.k. Baba anaweza kupendelea msichana wake aposwe na pengine, kijana ambaye ana kazi nzuri, anayempenda Mungu, asiyeonekana kihuni katika mavazi n.k. Ninaelewa kabisa kwamba hatutapata mtu ambaye ni mkamilifu (perfect), tungekuwa tupo mbinguni! Hata sisi tulipoolewa au kuoa tulitolewa maksi ukweni tukakutwa tumepungua. Lazima tuwe wakweli kwamba, mambo mengine tunavyotaka wakwe au wakamwana wawe navyo, nasi hatuna. Mfano wataka mkwe asiyelewa nawe walewa, ni haki? Je, hauna mizoga yako inayojulikana?

Hata hivyo una wakati wa kumshauri mtoto wako asioe au amwoe fulani. Kwa vile yeye ni mtu mzima, anaweza kufanya kinyume cha matakwa yako. Basi ni vizuri uheshimu uchaguzi wake na umezee. Na kwa vile wataishi mbali nawe, tafadhali waheshimu, usitembee huko kila mara kutafuta magomvi. Na wakiwa na shida wasaidie usiwazire! Ndiyo, yawezekana ana mume mvivu, asiye na kibarua na ni binti yako ndiye aleta riziki kila siku, ila nyamaza na kaa kwako! Anaweza kuoa binti mchawi, mvivu na mwenye kuvaa mavazi yasiyo na adabu kabisa, mwache huyu mume wake amwambie na si wewe! Ukishindwa usiende na kiherehere au kuwa kiberenge huko na kuharibu nyumba ya watu. Je, kama wanaishi kwako ufanyeje? Fanya utaratibu kuwasaidia wajitegemee ili kila unapoamka asubuhi usichafuke roho! Tujitahidi kuishi na watu wote kwa amani na utakatifu bila hivyo hakuna kuona Paradiso.

Tunaona mifano tele kwenye neno la Mungu. Mfano Ibrahim na Lutu walikuwa na magomvi na wachunga wao. Nabii au Mzee Ibrahimu alisema kwa hekima chagua huku, ukienda kushoto mimi naenda kulia nawe ukienda kulia mimi naenda kushoto. Hekima hii ni nadra siku hizi tunaishi na watu wanaotaka kubwatika, kulumbana au kupigana siku nzima. Jamani; tujifunze msalabani, shetani anachukua nafasi hii kutufanya tuwe watoto wake!

Tatizo ambalo limezuka ambalo watu wengi wameniuliza ni nitafanyaje mtoto wangu akiwa shoga akaoa mwanamume? Naomba ufuate ushauri huo wa juu! Mshauri mtoto, chukua muda. Tafuta na mshauri wa hekima wa karibu afanye vile, ikishindikana, usiendelee kubwatika bwatika au kuimba imba hilo kwao. Kama wanakuheshimu wewe, itabidi na wewe uwaheshimu. Kwetu Afrika, polisi wanashugulikia hilo kama kosa la jinai wacha washugulikie, usijiingize kwa kazi ambayo Mungu hakukupa! Hata Mungu anatukubali na dhambi zetu. Anatupa uchaguzi wa kuomba toba na kuacha. Hatulazimishi kufuata sheria au staili bora ya maisha anayotaka tuwe nayo. Je, waweza nawe kujifunza kwa hili? Wakina baba na mama wengi hawachoki kugombana, utafikiri Mungu amewapa kibarua cha kuchunga watu wazima, na kuwatawala. Watoto wako wakubwa wakisema “Tafadhali tuheshimiane;” nyanyua virago vyako(back off) upotee!. Endelea kuwaombea, maana sala yafanya kazi kuliko mgomvi! Ila usiwaambie kwamba unawaombea! Kwa ufahamisho, maombi yafanya kazi bila hata wewe kusema unaomba!

Sura hii yazungumzia wakwe kwa namna mbili: Wakwe wa familia yenye watoto wadogo, na wakwe wa familia ya watoto wakubwa. Kwa familia ya watoto wadogo babu na bibi wengi ni mbaraka kwenye malezi ya watoto. Waweza kusaidia kulea watoto mkiishi karibu kwa masaa ila msiache wakae nao muda mrefu kama inawezekana maana

kudekeza watoto, bila kuwa na nia mbaya kwatokea. Walivyowalea ninyi ni tofauti na watavyolea wajukuu. Mtoto aweza kuachiliwa afanye ukorofi, akirudi kwako unashangaa mbona amebadilika! Mara nyingine babu ana pesa nyingi na kuendekeza wajukuu na watoto wanaacha kujikana nafsi. Mababu wana muda mwingi pia ambao wazazi wanakuwa hawana na hili ni zuri kwa watoto kuwafundisha stadi, kama kuvua samaki, kulima, kushona n.k

Wakwe wa mume na mke wenye mtoto. Ili kuadabisha watoto wenu wadogo vyema mwangalie wazazi wenu wasiwe wakiwaamrisha na kuwaendesha. Wazazi wengine wanatawala na fimbo hata wakiwa mbali wanapenda kuwa madikteta. Na hii inategemea tabia ya mtu, wengine wanafujo katika maisha yao na wanaleta kwa watoto wao, na hatimaye kwa wajukuu. Wengine wanaona wivu kwamba maisha yao yalikuwa ya huzuni na watu walioumizwa wapenda kuumiza (hurt people hurt). Endapo utaleta wazazi wako ndani ya nyumba angalia mazingira ya watoto. Mara nyingi watu wa namna hii huona udhaifu na kukosoa, pia huegemea upande mmoja, wakiharibu amani ya watoto na familia kwa ujumla. Wana ndoa muwe pamoja.

Mara nyingine tunakaa na jamaa wengine kama binamu, dada, kaka, shangazi, n.k. Hili pia linaleta msongo hasa kwa mke. Jamaa wengine wapenda kuwa ndiyo wenye nyumba, wanasengenya na kupeleka umbeya kuhusu nyumba yako kila mahali. Wanafundisha watoto mambo mabaya, na wanaweza kutumia vyombo vya habari kuangalia mambo machafu wakati watoto wapo, na wengine wanaiba vitu.

Huzuni ya kuishi na jamaa yaweza kuleta shida na hata watoto watake kuhama nyumba au kuuliza, “Ataondoka lini?” Jitahidini msifanye mambo bila kupatana, kama kutuma pesa kwa siri kwa jamaa, kupendelea upande mmoja wa wakwe au kusema siri zenu kwa jamaa. Kwa jumla mpende ndoa yenu na kulinda urafiki wenu kuliko urafiki wowote mwingine. Mume awaonye ndugu zake wakianza shida, na mke awaonye ndugu zake pia. Usimuumbue mke au mume wako kwa kusema yeye ndiye mbaya na hataki kusaidia. Kusaidia ni jambo jema ila usiahidi vitu ambavyo huwezi, na vya muda mrefu. Uwe muwazi usiwe mtu wa siri siri. Usionekane kama unaficha mahusiano yenu na jamaa wa upande wako au kwamba mko karibu na unamtenga mume/mke wako.

Washauri wengi wanasema mama wakwe na mawifi ndiyo chanzo ya matatizo mengi hasa kwa upande wa mume. Pengine kwa vile pesa na umakini ulipungua na kwenda kwa mke baada ya arusi. Mama mkwe aweza kunyanyasa, kupiga, kugombana au kutoa maneno ya kashifa. Aweza kumsema mkamwana kwa mume wake au ndugu wengine. Aweza kuchukua vitu vya nyumbani alimradi tu kutaka mke afukuzwe ili kijana wake aoe mwanamke mwingine. Pengine hampendi mkamwana kwa sababu hana mtoto wa kiume au wa kike, malaumu yote huwa yanaangukia kwa mkamwana.

Mama wa mke pia anaweza kuwa na shida ya kugombana gombana na kumwomba mkwe pesa. Anaweza akawa akimwambia jinsi ya kuishi na binti yake. Haya yote huleta

huzuni kwenye ndoa. Na wakwe wengine hawapendi ndoa ya wengine iwe nzuri, kwa sababu yao ilikuwa mbaya na hawakupendwa. Wanatamani ya wengine nayo iwe mbaya zaidi hivyo wanakita hapo na kufurahia maanguko ya wengine ili wafarijike kwa kuwa klabu moja! Kuna wengi duniani hasa jamaa wa karibu wanaofurahia misiba ya wengine. Si mpita njia atakayekuharibia mambo ni mtu wa karibu. “Kikulacho ki nguoni mwako.”

Wakati mwingine shida inatokea kwa wana ndoa wenyewe na si kwa wakwe. Mume anaweza kuwa alikuwa na matata na wazazi wake akikua na wanaendelea na uhusiano uliovunjika na kuathiri mke na watoto wake. Mume anaweza kuwasaidia wazazi wake na kuacha mke na watoto, au jamaa za mke wakiwa wanateseka bila msaada. Anaweza asitembelee wakwe hata wakiumwa ila anatembelea jamaa zake na kuwasaidia huku akisema mambo mabaya ya wakwe, au shemeji zake.

Mke pia japo ameolewa anaweza kuwa kila mara anaenda kwao na zawadi nyingi, ila hakanyagi kwa wakwe. Na wakati mwingine anawasema vibaya wakwe au ndugu za mume. Mwanamke aweza kufanya zawadi zake siri kwa jamaa. Ndugu zake wakitembea kuna vicheko na wanapewa chakula na makaribisho mazuri ila wakija wakwe wanapata makaribisho mabovu na magomvi.

Mch. Njagi Festus, wa Nairobi, mshauri wa kaya na familia anasema, “Makaka na madada wa wanandoa ni wa kuangalia sana. Kwa desturi nyingi za kiafrika kaka na dada wa mume ndiyo wenye fujo na magomvi mengi. Wengi wakija wanataka kushika usukani wa nyumba wakitoa amri. Hawa wanaweza kuwa wabaya zaidi ya wakwe (baba na mama). Wengine ambao hawana nyumba zao au wameachika wanafurahia wana ndoa wakigombana na kukonyezana. Wanaweza kuchukua nguo za mke na vitu vingine bila ruhusa ya mke. Dada wa mke waweza kuwa shida pia, ila si kama jamaa wa mume.”

Kila mwana ndoa aangalie jinsi ya kushugulika na shida au ukorofi unaotoka katika familia yake. Mwanamume ndiye anayepaswa kumlinda mke wake na jamaa hawa vinginevyo shida hii haiwezi kwisha. Mume asimame kidete na mke wake kuona yeye ndiye mtawala wa nyumba na si jamaa zake.

Mwanamke asiache mama yake amwambie jinsi ya kukaa kwake. Vinginevyo atakuwa anachimba kaburi la ndoa yake. Kila mwanandoa aeleze kwa maneno na vitendo kwamba wao ni watu huru na wanahitaji kuendesha serikali ya nyumba yao wenyewe katika mambo ya fedha, nidhamu ya watoto, mambo ya kiroho, na ya uendeshaji familia siku kwa siku. Upendeleo wa upande mmoja ukome. Ni kweli damu ni nzito kuliko maji, ila hutaweza kwenda mbele kama unataka kutunza watoto wako vyema na kuwa na ndoa bora. Hata watoto wako watajifunza huo mvunjiko na kuhamisha kwenye familia zao wakioa/kuolewa.

Makaka na madada wanaotaka kutawala nyumba yenu waonywe na ikishindikana wasaidiane wakiwa kwa wazazi wao maana hawa ndiyo wakiwa na tabia mbovu, ndio wanaleta na umbeya, ukorofi na ushambenga kupita jamaa mwingine maana wanaona ni haki yao kuwa pale.

Watoto wako wakiwa watu wazima, Jaribu kuheshimu mkwe au mkamwana. Usiwe mtu wa kuwachukia maana hawa ni watoto wako. Jitahidi kuwa mtu ambaye unafanya

unyumba wako udumu. Kama mtu mzima uwe mtu wa kusuluhisha. Usiwe mtu wa tamaa na kuwaitisha wakutumie vitu vikubwa vikubwa kila mara, ambavyo hawawezi kugharimia. Ni furaha kubwa mtoto wako kuoa au kuolewa. Asingempata mtu wa kuoa au kuolewa naye, hata wewe ungesikitika. Jitahidi kuchukua muda wa kutembeleana na kufanya mambo pamoja angalau mara chache kwa mwaka kama mnakaa karibu.

Jaribu kutoenda nyumbani kwao mara nyingi mpaka wakuchoke na kuwaamrisha vitu vya kufanya. Wakina mama wengi wanataka kuendelea kuwa namba moja kwenye maisha ya watoto wa kiume hata kama wameoa. Gundua kwamba yeye amekuwa mwili mmoja na mke wake sasa. Uache nyumba yao ukijua huyo ndiye kijana wako aliyemchagua, na ukienda kwao uwe na heshima kwani hawa ni watu wazima nawe ni mgeni pale. Maneno yako yasitiwe chumvi, ujue kuishi nao wewe si mtawala wa nyumba yao sasa. Hata wakiwa wamekosea jambo, waambie vizuri na kama kuna shida wao ndiyo wataishugulikia (keeo off grass)

"Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama na wataambatana na mke wake hao watakuwa mwili mmoja." Kuondoka, kutoka, kuachana, au kutelekeza! Hili linashangaza; ila ndiyo neno lenyewe lilivyo kwa kiebrania. Mama mmoja alimwambia binti yake siku ya ndoa, "Mimi ndiye nilikuwa muhimu kwako, ila sasa ni mimi na mume wako!" Wazo hili ni potofu sana. Mungu ndiye namba moja kisha wana ndoa; ni pembetatu na si nne! Ndoa haisemi usisaidie majukumu ya wazazi wako ila ujue wewe sasa ni karibu na mwenzi wako kuliko wazazi; u familia nyingine, mpange cha kufanya.

Ujaribu kujitegemea ili uwe huru na kamba za wazazi. Haupashwi kuamshrishwa kwa maisha yako ya kila siku. Wewe u mtu mzima. Sasa wapaswa kumsikiliza mwenzi wako na kumpenda kuliko wazazi, hata utii wako wapaswa kuwa zaidi kwa ndoa yako. Waweza kushauriwa bado hapa na pale lakini siyo uende kupata mwongozo wa kila kitu huko. Waweza kupata ushauri ila mwenzi wako wa ndoa ndiyo uamuzi wa mwisho; unafanya naye na kuafikiana kuhusu huo uamuzi. Msilaumu wazazi kama ushauri wao ulikuwa mbaya, wana ndoa ndiyo wanaamua wachukue ule uamuzi au waache.

Sura ya 23
BABA NA MALEZI YA WATOTO

Kuwa baba ni kazi takatifu yenye mfano wa Mungu wa mbinguni. Hata tukiomba twasema, "Baba yetu uliye juu mbinguni.". Mpango wa familia, Baba, mama na mtoto ni mpango wa kimbingu. Baba ana uhusiano wa kiagano na mtoto wake. Kufanya nyumba ya furaha si shughuli ya mama tu bali hata baba. Baba anayependa na kujali watoto wake ni mbaraka mkubwa. Watoto wengi wanamsikiliza baba kwa makini. Watoto wengi wanapenda kutamba kuhusu uwezo wa baba zao wakiwa na wenzao. Hebu mtoto awe na kujivunia kwako baba, asione aibu kukutambulisha mbele za watu. Mtoto awe na kielelezo kizuri cha baba yake. Akiulizwa kazi ya baba ni nini asiseme, "Ulevi, kupiga bao, na kumpiga mama." Baba awe na maelezo mazuri na sahihi ya kumfundisha mtoto. Mfahamu mtoto wako na kiwango chake cha kuelewa.

Baba ni sehemu muhimu ya mpango wa Mungu katika maisha ya mtoto. Yeye ndiyo kiongozi anayetoa mwongozo na maamuzi ya mwisho ya familia. Watoto wanamwangalia kwa uongozi. Asiwe mwepesi kufoka na kukaripia hata watoto wamwogope naye ashindwe kuwafikia. Mara nyingine mtoto akizungumza twasema, "Mawazo mabaya hayo umetoa wapi?" Badala ya kusikiliza na kumsaidia, ili siku nyingine akwambie mengine ambayo unajua yahitaji usaidizi! Baada ya muda mtoto anaficha uovu kwa kuogopa, anakuwa mwongo, na hakwambii ukweli, ila ndani ya moyo wake na matendo yana uovu ule ule bado, na sasa huwezi kumsaidia kwa kuwa hujui anachowaza. Umefunga mlango! Au aweza kukua kwa mapungufu. Mfano umemwona kijana wako wa miaka 15 akizungumza na msichana fulani na kumkemea hata bila kujua maongezi yenyewe. Anaweza kuanza kuzungumza na wasichana wadogo wa miaka 3 au 4 au na ajuza tu wa miaka 100!. Nayo pia haina mizani (balance). Mtoto wa kiume na wa kike ni muhimu waweze kuzungumza na watu wa umri wowote kwa jinsi inavyotakiwa.

Utafiti unaonyesha mapungufu kwa baba kwani, watoto zaidi ya asilimia hamsini wanalelewa bila baba; hata hapa kwetu. Kina mama wanashugulika kuona watoto wamepata chakula, wana nguo, wamefanya kazi za masomo au wamekwenda kusali.

Kuna baba kama Eli kwenye maandiko matakatifu ambaye, japo alikuwa kuhani mkuu hakuwaadabisha watoto wake kumcha Mungu. Ubaba wake ulishindwa na kufanya ukuhani pia uvunjike. Alikuwa hajui kinachoendelea wakati vijana wake wanaiba kafara na kubaka wanawake kwa nguvu. Hakuwa amemheshimu Mungu kwa ajili ya kuwaachilia watoto wake, alikuwa busy.

Mara nyingi Mtoto akiishi maisha ya ulevi, ukahaba, ujambazi, na kutomweshimu Mungu ni kwa sababu ya kina baba kupoteza mawasiliano na watoto na kutelekeza kazi yao.

Utafiti katika nchi ya Marekani ulisema kwamba, baba wa kawaida huzungumza au kuwasiliana na mtoto wake, yanayomhusu mtoto, kwa dakika tisa pekee kwa siku; na mama kwa dakika ishirini na sita! Hilo ni pengo kubwa sana. Na lina mchango mkubwa sana wa kufanya nidhamu ishuke kwa watoto na vijana. Mtoto anamhitaji baba kwa mengi na si kwa kuzaliwa tu. Anamhitaji kwa kukua katika uwiano sawa wa kiakili, kwa upendo, maadili, makuzi, elimu, kazi za wanaume, dira ya maisha, ulinzi, ubora wa maadili, na kumwonyesha taswira ya Baba wa mbinguni. Mtoto anahitaji baba anayempenda Mungu kwa dhati na si anayependa dini! Dini si Mungu na Mungu si dini! Dini ni mfumo wa mwanadamu katika jitihada zake kutafuta namna ya kukidhi kuhusiana na Mungu. Mwanadamu ana tundu moyoni mwake lisilozibika kwa kitu chochote isipokuwa Mungu.

Katika Mila nyingi za kiafrika kina baba walithamini watu. Katika kitabu cha kwanza cha Samuel kuna familia ya Eli ambaye alikuwa kuhani mkuu. Alikuwa na watoto wenye tabia mbovu. Hatuna historia ya kuzaliwa na makuzi, ila ni habari mbaya ya watoto walioharibika kitabia. Watu walitoa dhabihu-ng'ombe au kondoo katika utaratibu uliofaa. Watoto hawa walitaka kujichukulia nyama kwa nguvu na kula pasipo utaratibu. Walikufuru ibada hiyo ya muhimu. Walijihusisha na uzinzi na wanawake waliokuwa wakifanya kazi kwenye viwanja vya hema ya kukutania. Mwanzo Eli hakujua ila baadaye alisikia maisha ya uovu ya wanawe. Wakati huo amekuwa mzee aliwaonya 1 sam 2:25. Eli alikuwa amechelewa mno kwakuleta matokeo kwa wana wake. Mke wake hakuelezwa hata! Hatujui sababu. Pengine naye alihusika na kupata adhabu yake, au pengine yeye alijitahidi sehemu yake ila mchungaji ndiyo aliharibu sehemu yake.

Eli alikuwa amekosa mawasiliano muda mrefu hakujua kinachoendelea. Alishakuwa mzee nno na kukosa kueleweka na watoto ambao ni kizazi tofauti. Alikuwa amepoteza mamlaka yake juu ya wanawe. Watoto wake walikuwa wameharibika sana kitabia kusaidika.
Kamwe makuhani wasingetoka katika mlango ule, wangekufa wakiwa vijana pia mlango wa Eli ungekuwa masikini au omba omba. Eli alishindwa kuwainua na kuwakuza na kuwaelekeza watoto wake wamheshimu Mungu. Kisa hiki ni cha kusikitisha sana.

Ukuhani ni wito wa Kiungu. Makuhani wahitajika kuwa waadilifu. Watoto waone kirahisi kwamba unamwakilisha Mungu. Watoto wetu wanahitaji baba yao pia kuhusika na matunzo yao, hata awe busy kiasi gani! Semina na kazi za ofisi zitaendelea, ila watoto wako wana nafasi moja tu katika maisha yao ya matunzo yatakiwayo! Wewe kama mke, panga haya na kuzungumza na mume wako. Si kwa uchoyo wa kufikiria watoto wako tu ila kwa kusaidia watoto wawe na tabia njema. Tabia ndiyo pekee yake watakwenda nayo mbinguni, si mavazi, chakula, au vitu.

Mungu aliumba watoto wawe na wazazi wawili. Mungu ni wa upendo. Kina baba wengi wanajulikana kama wasiojali familia zao na kuwajibika. Hata wale ambao wanamtumikia Mungu! Wanasafiri mbali na kukaa muda mrefu, kwenye masemina na mambo mengine. Hawaonyeshi shauku (interest) ya maendeleo ya kila siku yawatoto wao. Hakuna mtu wakati anapokufa anajuta akisema, “Ningejua ningekaa muda mrefu zaidi ofisini!” Lakini nimesikia wengi wanajuta kwamba wangejua wangetumia muda na watoto wao, au wake zao, au mambo fulani.

Tunaona madhara ya ukuhani na ubaba ulioshindwa au ubaba usio wa Kiungu ni mzito kwa baba mwenyewe, mke na watoto. Inawezekana wachungaji wengi na wake zao wanatumikia hukumu ya Eli. Wanafanana naye kwa kupoteza amawasiliano ya siku nyingi na watoto, na wameshaharibika. Wanachukia kazi ya baba yao na hawamtii Mungu. Wanaishia katika maadili mabaya na hawaoni aibu. Yapasa mchungaji na mke wake ajiulize alikuwa wapi mtoto wake alipofikia hatua hiyo ya maisha. Hapa Afrika kuna watoto wengi waliofikia hatua hiyo.
Mara nyingi tumesikia, “Ah! Watoto wa viongozi wa dini wako hivyo hivyo, hawasikii!” Kwa kweli si lazima tuwe wa twakwimu hiyo! Ila pia tufahamu kwamba wachungaji ndio amiri jeshi wakuu wa jeshi la Bwana. Kama Daudi alivyomtuma jemedari wake mkuu Yoabu amweke Uria mbele ambapo vita ni vikali ili auawe, ndivyo pia shetani anashambulia watoto wa watumishi wa Bwana ambao ndio wako katika msitari wa mbele; ili kudunisha kazi ya mchungaji. Kwa neema ya Mungu tuwaombee watoto wa watumishi wa Mungu na kuwashugulikia ili nao wampende Mungu na kumtumikia.

Soma vitabu vya matunzo ya watoto na uliza ushauri wa wale wanaompenda Mungu wenye uzoefu. Usiogope vitabu. Soma! Wanasema ukitaka kuficha jambo kwa mtu mweusi, weka kwenye maandishi! Hatupendi kusoma. Ni utamaduni wa aina fulani. Hebu tuukanushe!
Ukipata maarifa ya kutunza watoto, utasaidia hata watoto wa jumuiya au wa ndugu na jamaa.

Napenda kusema kwamba hakuna mzazi aliyefuzu malezi! Ni Mwenyezi kutusaidia na kuwaombea watoto wetu. Kuhani aliyemfuata Eli aliitwa Samuel, yeye watoto wake walikuwa na shida hiyo hiyo pia. Ila yeye hakulaumiwa. Inaonyesha kwamba alifanya

alivyoweza ila wale watoto walichagua njia mbovu. Kwa hiyo fanya sehemu yako na mengine umwachie Mungu.

Mwandishi wa kitabu cha, Paul Rader, aliandika haya kuhusu baba yake; “Baba yangu alipokaribia kukata roho, aliangalia juu akatabasamu tabasamu la pekee sana. Rafiki yake akamuuliza ‘Daktari Rader, mbona unatabasamu hivyo ilhali hakuna hata mtoto wako mmoja anayempenda na kumtumikia Mungu?’ Baba yangu alimjibu, ‘Niliwalea katika njia Zake na jinsi alivyoniagiza. Atawarudisha wote.’ Na kweli, leo mimi pamoja na ndugu zangu wote, tuko kanisani na tunamtumikia Mungu wa baba yetu.”
Nyumba inayompenda Mungu yenye mipangilio, ni kielelezo na mahubiri makubwa kwa jumuiya, kuliko yale mchungaji au kiongozi anayohutubia jukwaani au kibwetani.

Hebu nyumba zetu ziwe kimbilio kwa watoto au vijana wanaopata matatizo na majaribu. Tukionyesha shauku kwa vijana na kuwazingira, itafanya tofauti kubwa. Kusomesha na kuhurumia watoto wenye mahitaji ni muhimu. Kama una kitu kidogo usistarehe kwamba watoto wako tu ndiyo unapasa kushugulikia. Saidia watoto wengine kwenye jumuiya, utashangaa, Utakuwa baba wa wengi, na ni nani ajuaye pengine wale wengine ndiyo watakukumbuka zaidi? Pia utakuwa umepunguza watu waovu kwenye jumuiya yako. Nimeona mchungaji na mke wake wamechukua watoto kumi wa kijiji cha kimasai wakiwasaidia kuwasomesha.

Mara nyingi kusaidia hakuhitaji makuu sana. Ni baraka sana kusaidia watoto wengine zaidi ya wako. Neno la Mungu linasema, kutunza watoto yatima kunakubariki wewe na watoto wako, na watu wanaojulikana watakatifu walikuwa na matendo mema kama haya Chukua muda kujua neno la Mungu vizuri. Shugulisha akili yako kwa kujiendeleza na kujua yanayoendelea. Mwombe Mungu akupe furaha ya kweli ya moyoni.

Watoto wetu wanajifunza kwa yale tunayofanya si yale tunayosema. Wao ndiyo shamba letu la kwanza la kumfanyia kazi Mungu, atatuuliza “Wako wapi watoto niliokupa?” Kama wazazi yapasa tutilie makini.
Tuwe makini sana kusema na kusengenya watu. Endapo tutasema watu vibaya, watoto wetu wakisikia ni laana kwetu. Najua kuna watu walioharibu watoto kwa kusengenya watu hata kama unayosema ni ya kweli, watoto waweza kuharibikiwa. Ikiwa kama kuna mambo ya kusema kuhusu mtu fulani, zungumzeni kati yetu watu wazima msije mkamkwaza mtu na kumtweza Roho wa Mungu. Napenda kusema hata kama ni ya kweli usieleze mbele ya watoto wako wao hawaoni Mungu wa mbinguni wanaona wale watumishi ‘waovu’ na kumdharau Mungu wa mbinguni. Hii inaleta uvundo. Mara zingine waweza kufanya sehemu yako kama watoto wa Nabii Samuel ila watoto wachague njia yao, hapo huna la kufanya.

Tunajua hakuna aliye mkamilifu ila Baba yetu wa mbinguni. Kwenye neno la Mungu tunaona watumishi walioanguka na kurudi kama Daudi. Ungama na kuwa na toba ya kweli; “Eeh Mungu unirehemu, sawasawa na fadhili zako kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu, unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu, maana nimejua mimi makosa yangu na dhambi yangu na mbele yangu daima.” soma zaburi 51 yote. Usiwe mbishi na kukataa kwamba umekosa, au kwamba sheria za Mungu si muhimu, la! Mshahara wa dhambi ni mauti bali, karama ya Mungu ni uzima wa milele. Mungu ametoa njia ya kuzifuta dhambi zetu, tuungame na atatupa nguvu. Wote tumetenda dhambi na kupungukiwa utukufu wa Mungu. Tuombe msamaha na kuanza safari tena katika shamba la Bwana maana YEYE ni mwenye Rehema nyingi.

Tegemea makubwa kutoka kwa Mungu, nuia na kufanya makubwa kwa Mungu. (Expect great things of God. Attempt great things for God.
Baba wa kiafrika walipenda watoto sana, mpaka kuvuka mpaka wa kuoa mke mwingine, mke wa kwanza asipokuwa na mtoto. Na pia mume na mke walipoachana watoto walibaki kwa baba wakitunzwa. Endapo mtoto alikuwa wa kunyonyesha angechukuliwa na mama na angerudishwa tu baada ya kuachishwa ziwa. Japokuwa baba ana shuguli nyingi na hasa kibaruani au nje ya nyumbani kwake, hebu achukue muda kufanya nyumba yake iwe ya utulivu, amani, furaha, adabu na uchaji wa Mungu. Baba ndiye mtunga sheria za nyumbani na mfano wa kuzitunza sheria. Yeye ndiyo nguzo inayobeba familia. Watoto wanajulikana kwa jina lake. Hebu awe mkakamavu, mwenye kutia moyo, mvumilivu, mwenye bidii na kichwa bora. Yeye ndiye kuhani wa familia yake anayeongoza shuguli zihusuzo mahusiano na Mungu ausubuhi na hata jioni kwa sala. Yeye anamwakilisha Mungu katika familia yake. Asiitelekeze kazi yake kuhimili na kuadabisha watoto wake. Hebu awe mtu wa kusoma neno ya Mungu na kuomba, maana kazi yake ni nzito sana. Asiwe mtu wa harara na kupima mambo kama mtoto na kuparamia mambo tu. “Nilipokuwa mtoto nilinena kama mtoto....” 1 Wak. 13:11.

Mwanamume asimamie nyumba yake si kama mtoto ambaye hana nidhamu akizungumza matusi na chochote bali ajifunze tabia yenye maadili mazuri. Hebu baba ajifunze maadili mazuri ajisomee vitabu na kuuliza watu wenye hekima. Ajinyenyekeze kwenye mkono hodari wa Mungu ili watoto wake waweze kuwamudu kimaadili pia. Usionyeshe mabavu yako kwenye nyumba bila kutuia upendo kwa watoto, utakwaza na kupoteza watoto. Fanya maisha ya watoto kuwa ya furaha. Uvumilivu, upendo, kujikana nafsi, ukarimu uonekane katika maisha yako, hata kama una kazi ngumu kiasi gani ya kuleta riziki nyumbani kwako. Mkimbie shetani naye atakukimbia. (Resist the devil and he will flee from you.)

Ukiwa karibu unatweza na hasira, kutokuwa na uvumilivu au upendo hebu sujudu na kuomba Nguvu toka kwa Mungu. Haiwezekani kuwa baba bora bila Mungu! Hasa katika ulimwengu wa leo. Umeshaona katika vyombo vya habari mambo yaliyotokea kwa mababa wengi. Mababa wamechukuliwa kama watu wa futuhi wasiotilia maanani kazi yao. Usiache watoto wako wakutafsiri vibaya na kuona kwamba nia yako si njema kwao. Kwamba unataka kujinufaisha mwenyewe tu na una ubinafsi mwingi. Watoto wajue

unamjali mama yao na kwamba uko tayari kujitoa mhanga kwao kwa mambo madogo na hata makubwa. Kazi ya kuwa baba si ndogo
omba Mungu akuwezeshe, hutaiweza mwenyewe, hasa katika siku hizi ambazo jukumu la kuwa baba linapigwa vita na shetani sana.

Nilimsikia mwanamume mwingine akisema kwamba kuwa mwanamume ni kazi kubwa kwani mke anakutegemea na watoto pia. Akasema "Afadhali ningekuwa mwanamke!" Jambo hili ni la kusikitisha na la kweli. Niliendelea kusoma magazeti mengi na kukutana na jambo hilo kwamba katika nchi zingine kama wanaume wengi walijibadilisha kuwa wanawake au kuwa mashoga li kukata ukali wa maisha. Na kweli kazi ya mwanamume si ndogo. Yeye ndiye mtendaji mkuu, mwanamke ni msaidizi tu.

Jitayarishe vizuri katika ibada na familia yako kama vile unavyofanya kibaruani, usibabaishe mpaka watoto waone hapa baba hajui kitu. Mama mmoja alisema, "Mume wangu ni profesa wa chuo kikuu, anafundisha hesabu, ila maombi ya nyumbani, anaboesha watoto, kila siku anakuja na fungu hilo hilo la Yoh 3:16, kwenye ibada ya nyumbani. Hajitayarishi, watoto wamechoka, nami naona aibu kumwambia maana nitamvunja moyo, na aache. Unajua wanaume siku hizi wengi wamepotea mitini kwenye mambo ya kiroho angalau yeye anakuwa nasi kila jioni." Kina baba japo mna wasaidizi, msiwaweke kina mama kuwa watendaji wakubwa' mkikwepa majukumu mengi kati yale mliyokabidhiwa na mwenyezi Mungu.

Mke aunge mkono katika kazi hii ili tabia zao ziwe kamilifu. Mwanamume asikwepe jukumu lake hili takatifu la kuwa mtawala wa nyumba yake. Aitawale nyumba yake kwa upendo na kufanya watoto wawe na utii. Awe mtu wa kiasi na kujitawala, asiwe mtu wa kunywa pombe na kula ovyo ovyo hata vyakula vinavyomdhuru. Auadilishe ulimi wake kuwa na ladha ya vyakula vya kumsaidia katika jukuu lake. Vyakula vingine vinaleta hasira na papara. Anapaswa kuelimika na kutia makini katika vipengele vyote vya kuadilisha mtoto kwa ubora wote. Hebu watoto wajue ni baba anayeongozwa na Mungu katika kuwahekimisha. Aweze kuwa mwenye huruma, rehema na mwepesi kusamehe watoto na kuanza upya.

Maneno ya baba ni mazito, aumbe maneno ya kuponya mtoto na si kujeruhi. Tunaumba mambo kwa ndimi zetu, twapaswa kuwa waangalifu. Haimpunguzii thamani yake akionekana amesujudu anamwomba Mungu. Aongoze nyumba yake katika ibada asubuhi na jioni. Ajitayarishe vizuri asiwe mbabaishaji tu. Atekeleze mamlaka yake kwa unyenyekevu. Majukumu ya baba hayawezi kuhamishiwa kwa mama!

Imebidi baba wengi watafute kazi yenye majukumu tofauti ili waweze kukaa na watoto wao kila siku. Usitoke kibaruani ukaenda kutembea urudi usiku kila siku. Jitahidi kutoingia nyumbani kwako kama mtalii bali kiongozi wa familia. Marafiki zako

hawakuhitaji sana katika kuwajenga kama watoto wako. Punde watatoka na kwenda kuwa na miji yao, Je, watakukumbuka wewe kwa nini?

Siku zinaenda mbio, nawe utakuwa umestaafu na mzee ila hujajenga mahusiano na watoto wako. Utaonekana kama mgeni katika maisha yao. Watoto wanaitwa kwa jina la baba na kwa waafrika wengi, watoto ni wa baba! Ila wakiona kwamba mama yao ndiye anawajali, wanashugulikia zaidi! Jambo hili ni la kusikitisha. Kina baba wengine wamechukua muda kuabudu kazi, biashara, kileo, marafiki au vitu vingine. Wakizeeka watahitaji watoto, kwa njia moja au nyingine. Kama hela ya matibabu, shughuli au riziki; watoto wanatuma msaada kwa mama ndiye amgawie baba! Na akipiga mayowe na kulalamika, “Ninyi watoto mimi ni mtu mzima, mbona mnafanya mama yenu ndiyo anigawie pesa kila mara?”

Niliona wakina baba waliofanya kazi kwenye mashamba ya wakoloni ya katani walijengewa nyumba wakae wakiwa wazee kwani walipoenda huko wengine walisahau familia wakatumbua maisha mwishowe walisahau watoto. Walipozeeka hawakuwa na pa kwenda na mjerumani aliyetawala aliwajengea nyumba wakaishi pale kwa huzuni na upweke.

Hawasemi mengi, ila wakiona baba na mama wana ugomvi na mama yao hana furaha au anafanyiwa vitendo vya hiana wanamchukua mama yao wanaenda kukaa naye mjini. Baba anakaa nyumbani na kujipikia, kuchunga na kuangalia mji kwa hasira au huzuni. Watoto wengi wamekuwa na chuki na baba zao maana baba wengi walijisahau na kuwatelekeza watoto wakawa watawala wasio na upendo. Pengine masikini baba hawa waliona hali hii kutoka kwa baba zao na wameigiza, bila kujua na inaendelea kizazi hadi kizazi. Kata hii laana ili isiingie kizazi kichofuata. Mwanamume jua una jukumu kubwa kabisa na unamwakilisha Mungu hapa duniani.

Zamani katika jadi ya kiafrika mwanamume ndiyo alisaidia dada zake, wadogo zake na wazazi. Umetokea mtindo wa wavulana wachache wa siku hizi kuwa wavivu na kutojibidiisha shuleni, kula karo wakipelekwa kusoma na kujiunga na magenge mabaya na hata wasimalize shule. Hii inafanya jukumu lao la ubaba lisitekelezwe vizuri. Dr Nedley wa Nedley solutions.org alisema zamani akili za wanaume zilikuwa 5% juu kuliko watoto wa kike Marekani. Ila utafiti wa sasa unaonyeha kwamba wanaume wameshuka kwa na hii imefanya wanawake wapande kwenye maksi za kuingia vyuoni na kwingine.

Mwanaume aliumbwa na uwezo mkubwa si siri, ila amejiweka katika mambo mengi ya kuharibu mwili. Wengine wameanza kutafuta kuolewa na wanawake matajiri, zamani wanawake walitafuta mume mwenye pesa, masomo makubwa au kazi nzuri. Siku hizi wanaume wengine wameanza kufanya hivi, na kufanya majukumu yao kama watawala kupungua thamani na kuchujika. Mwanamume asitembee katika maisha bila kujua jukumu lake zito kama baba na mume. Afanye mambo yake kwa bidii. Hata siku hizi yaonekana waumini katika madhehebu mengi kama 70% -80% ni wanawake. Hili nalo ni gumu kwani mwanamume ndiye alipewa uongozi wa madhabahu. Haya yaliyotokea kule zamani ambapo Farao na Herod waliua watoto wa kiume walielewa fika kwamba ukiua mtoto wa kiume, umeua taifa. Hii ndiyo shida pia ambayo walifanyiwa wanaume wale wa kiamerika weusi. Alisema rafiki yangu aliyetembelea nchi moja ya Afrika magharibi kwamba, “Wanaume wamebakia ni wa mbegu tu!” Jambo hili ni la huzuni sana. Kwani Mungu

alimpa mwanamume majukumu mazito zaidi ya kuzaa na kuongezeka tu. Hebu sote kwa pamoja wanaume na wanawake tuombeane, ili nyumba zetu ziwe taa kwa majirani na msaada. Isiwe sisi ndiyo ambao kwenye jumuiya tunachosha watu na kesi na kugombana kila mara au kutotenda wajibu wetu. Hebu wote tushuke magotini na kuombea changamoto za wanaume kama mababa,

Wanaume wengine wamefanya jumuiya kulea na kugharimika na watoto wao kwa ajili ya uovu waliojikita nao. Mfano kulewa sana na kutotunza familia, ukali na ukatili wa lupita kiasi, kujiingiza kwenye zinaa na kupotea au kupata magonjwa yanayofanya watoto wawe yatima na mengineyo. Mungu ametoa furaha itokanayo na tabia ya kuishi maisha ya usafi yenye utakatifu. Maneno na maisha yanayojali watoto wako na binadamu wengine yatakubariki sana.

Pata likizo na muda wa burudani na watoto wako na kuwapeleka mahali ambapo kwa furaha mtajifunza mambo mapya na kupumzika na kufurahi pamoja. Huitaji kutumia pesa nyingi kuwa na burudani. Panga vitu vya karibu au kwenda kwa watu ambao hamtatumia pesa nyingi. Cheza na watoto wako na kuzungumza nao. Michezo ambayo haileti ushindani ila inajenga mahusiano. Chagua burudani zako vizuri, siki hizi kuna burudani za anasa zinazoharibu tabia njema Hebu kwa kuona, kugusa, kuwaza, kusikia na kunusa yawe yale yatakayojenga tabia za watoto. Burudani zisiwe za kupoteza pesa nyingi na kufanya watoto wawe na ubinafsi badala ya kuangalia wenye mahitaji.

Baba funza watoto ukarimu. Waone unampa mama yao mahitaji na pesa, ili wajue ukarimu ni kitu cha maana. Na hata waone unawapa wazazi wako na wakwe wasiojiweza mahitaji. Watajifunza kufanya vile vile kwa wakwe, wazazi na wake zao. Uko katika shule kila dakika mpaka mtoto atoke kwako, usijiziuke. Baba anayejali watoto ana zawadi kubwa sana hapa duniani na mbinguni. Hebu baba aanze kufikiria jinsi atakavyowasaidia watoto. Kina baba, mkijaliwa na mali mtenge fungu ili watoto wenu wasiwe mzigo wa mtu mwingine. Na anapowasaidia anaona nyinyi mnatumia mali zenu kwa vitu visivyoeleweka. Haijalishi una uzoefu mdogo kiasi gani kama baba, au kama una nia. Haijalishi kwamba una mke mgumu kuelewa mambo au una watoto wakorofi, Mwenyezi anakutaka uweke mguu wako kwenye maji kwa imani kwa kazi hii aliyokupa.

Hofni na Fineasi walikuwa na watoto kwenye neno la Mungu wakifanya kazi hekaluni na baba yao kama kuhani mkuu. Walikuwa na tabia mbovu ya kuiba sadaka na uzinzi. Maandiko yanasema baba yao hakutilia maanani sana tabia hii. Pengine alikuwa na shughuli nyingi kama “Rais” wa nchi na kuhani mkuu wa nchi, ila tunaambiwa ana hatia. Alikuwa na ubaba uliopasuka na kuvunjika. Jina la Mungu lilitukanwa kwa ajili ya kutoadilisha au kusimamia watoto wake ambao yasemekana alishindwa kuwamiliki. Aliweza kutawala nchi nzima ila alishindwa watoto wake. Yawezekana asiwepo mbinguni kwa ajili ya watoto wake. Yeye mwenyewe alikuwa mtu mwenye tabia nzuri. Kumbe hata watoto wetu waeweza kutufanya tusiende mbinguni?

Hata sisi wote wazazi tuna hatia ya hili tunategemea shule, nyumba za ibada, au jumuiya itawasaidia watoto wetu tabia na sisi tunaendelea na shuguli zetu. Kibarua chako kama baba huwezi kumwachia yaya au mama yao au mtu mwingine. Sali uzungumze na Mungu kila siku akusaidie, uwafundishe uamkapo, usimamapo, ukaapo na ulalapo. Uandike kwenye viwimo vya mlango wako! Kum. 6:6-9. Mlee mfundishe, usimwambie tu! (train and not teach).

Mweleze mtoto kwamba Mungu yuko upande wake na anampenda sana, na kwamba ni Baba yake pia. Tafuta kubadilisha mawazo na mioyo yao na si matendo. Mioyo itakapobadilika hata matendo na mawazo pia yatabadilika. Haitakuwa kwa siku au wiki au mwaka mmoja lakini utaona matokeo mazuri karibuni! Watoto wajue Mungu anajua hata wakikuficha wewe au watu wengine. Jua watoto wako walipo mara zote. Pombe, sigara, uongo, uzinzi, pornography, madsko na mifano mibaya uikatae ili watoto wasiigize mambo maovu. Tafuta kwanza ufalme wa Mungu hata watoto watakuiga.

Baba asiwe mwenye mamlaka madogo au makubwa sana kwa mtoto! Baba asiwe mkatili kwa watoto. Jifunze kuwa na tabia ya Mungu ili watoto wako wakiigiza wawe na tabia ya Mungu. Ukisema uongo, inakuwa vigumu kwa watoto kuelewa ni wakati gani unasema ukweli! Matunda mazuri ya tabia ni upendo, furaha, amani, kujikana nafsi, kutii, uvumilivu, upole fadhili, upole, kiasi, utu wema na imani. Matunda mabaya ya tabia ni chuki, uchafu, ufisadi, uchawi, uasherati, uchoyo, ubinafsi, tamaa za kutotawala nafsi, kujisfu, kujionyesha, kutotiii, unyanyasaji, kuabudu sanamu, ugomvi, uadui, uzushi, faraka, wivu, hasira, ulevi, na fitina. Mtwike Mwenyezi tabia za watoto mbaya na zako awasaidie muachane nazo.
Ukijisikia kama unapwaya, kwamba huna nguvu ya kazi ya ubaba na kuweka mfano mzuri Mwombe Mwenyezi akusaidie. Utii wa nje hausaidii ni utii wa ndani ndiyo unaleta mabadiliko ya kweli! Mwenyezi aweza Kuwalinda na watoto wako msijikwae na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu.

Kitabu cha Waefeso 6:4, kinasema kina baba msichokoze watoto wenu. Hii inahusu pia kina mama. Kukejeli watoto kwa mzaha, au kuwazomea, inatokea mara nyingi kuliko tunavyofikiri. Sidhani kama kuna mtu hajafanya hivyo. Hatufanyi kwa nia mbaya ila hatufikirii madhara yake kwa mtoto. Kumchokoza mtoto ni kuwa na tabia isiyokuwa ya kiutu uzima (immaturity). Tabia hii inaleta makovu kwa mtoto. Hebu tufanye tunavyoweza kuitupilia mbali.

Baba panga uzazi. Usiwe na watoto wengi unaoshindwa kuwalisha na kuwatawala, na ukaachia wengine wakusaidie kazi yako. Jua marafiki wa watoto wako ni wapi, na watoto wako wapi jioni. Watoto wako wa kiume wasikae kijiweni kwenye magenge. Nenda kawatafute! Wasiwe na uhuru upitao kipimo, kuna mengi ya kuharibu watoto. Waweke watoto wako nyumbani mwako, watu wakisema eti watashindwa kuhusiana na watu, waambie hilo si kipaumbele kwako ila mahusiano ya tabia njema. Watoto wana mabaya

zaidi ya mema ya kujifunza kwenye magenge. Wafundishwe kuepuka majaribu, nakukimbia marafiki wabaya. Kuna mahali ambapo si kukosa haki kuwasindikiza watoto wako. Watoto wameachwa kwenda kwenye vituo vya basi peke yao, wanapoenda shuleni, au mahali ambapo wangefaa kusindikizwa, na mengi yakazaa balaa.

Usiache watoto wako walale nje bila kujua wako wapi. Karamu za kulala "sleep over" ziwe mwiko! Hata mtoto wako usije ukamwacha akaenda kwa majirani ovyo ovyo tu. Watoto wengi wamepigwa bunduki au kubakwa kwenye nyumba za watu. Wasichana wengi wamebakwa na majirani au hata ndugu wa karibu! Mama mmoja aitwa Ellen White alisema "Nikienda nyumbani kwa watu wengine sikubali watoto wangu walale kitanda kimoja na wengine, naomba walale chini tu kama hakuna kitanda kingine." Sasa ndugu msomaji, huyu mama alilea watoto vizuri sana, jaza jedwali kwa ini alisema hivi?

Siku hizi na enzi za ushoga, si watoto wako wa kike tu wataweza kuharibiwa, hata wa kiume pia. Nilipita kituo cha polisi Mara, nakuona mtoto mdogo mvulana amelawitiwa, na mama yake alikuja kuripoti kiutoni. Haditihi ilikuwa ya kutia huzuni. Watoto wana hatari na majaribu mazito siku hizi. Watoto wako wasizoee kulala na watu wengine, hata kama ni wa kiume wenzao. Wafundishe kukana nafsi na kuwa wazi kukwambia hatari zao. Usikazanie uonekane nadhifu na tai na nguo za ghali wakati familia yako inaharibikiwa. Ni vizuri ule na watoto wako! Baba wengi walikula peke yao na watoto wakapewa chakula kidogo, na vile vitamu kama kuku, walipewa mchuzi au miguu tu, na baba akabugia mwenyewe vile vitamu vitamu. Watoto wako watachukua maksi kwa tabia hii na hata baadaye utaona matunda yake. Watoto hawa baba yao akiwa mzee hawamjali, wanamjali mama, na hii inaleta ugomvi wa ndoa, na kasha watoto wanakaa na mama yao na baba anajipikia pikia kwa huzuni na hasira.

Bidii yako iwe katika kujenga tabia ya watoto. Hayo mengine yasikuyumbishe, yapange kama yako kwenye uwezo wako. Wewe ndiye unayeongoza hiyo serikali! Kila serikali ina sheria, wafundishe watoto wako kutii sheria. Wafundishe watoto wajiheshimu na kuheshimu serikali yako, ya taifa na Mungu, haki za watoto zijaliwe kama elimu na vingine. Usidekeze watoto wako wala usiwanyanyase. Ujiweke kwenye mkono hodari wa Mungu ili akutegemeze. Jifunze na soma zaidi kuhusu kuwa baba bora, siku hizi nimeona hata sekondari shule zingine duniani zinafundisha wavulana kuwa baba bora, wameona inaleta tofauti. Watoto wa kiume nakutana nao wamebeba mwanasesere mwenye uzito wa mtoto, kila akilia yabidi wamshugulikie kama mtoto wa kweli. Hili ni somo lenye maksi, yabidi walifanye kwa mwezi. Rekodi inachukuliwa kama wanaamka kila mtoto akilia na kusema wanapaswa kufanya nini. Kuzaa ni zaidi ya starehe, ni jukumu toka kwa Mungu mwenyewe. Utafiti umeonyesha kuwa wakina baba waliokuwa tayari kutunza watoto wao hata wale waliokuwa hawajaoa wanapunguza namba za wanawake wanaotoa mimba. Kwa vile Kutoa mimba ni kuua, hebu wakina baba wasaidie jumuiya na malezi ya watoto kwa Njia hiyo.

Napenda kusema kuna mamilioni ya watoto wanaosifu baba zao kwa mema, upendo na malezi mema. Mimi Nikiwa mmojawapo. Nilikuwa na baba aliyetujali sana si kwa Chakula, mavazi na malazi tu, bali hata kwa kucheza nasi, alitupeleka kuogelea, michezoni, hata katika safari za kazi tulitembea naye pale iliporuhusu. Kwa watoto ambao baba zao walikuwa na mapungufu, hebu wafundishwe kusamehe na kusonga mbele. Maana kutosamehe ni kumeza sumu, na kutegemea mwingine atakufa. Na Kipimo cha

kusamehewa na Mungu ni kusamehe wengine. Tusaidie watoto wetu wasibebe vinyongo, chuki, visasi kwa kutosamehe maisha yote. Watu wengi wamekutana na watoto wao ukubwani na kusawazisha na kisha wakaanza safari mpya. Ni ni nini Mungu asichokiweza? Hata kama mzazi ana makosa, anasamehewa kwani yoyote Yule aliyekuwa mzazi atagundua anafanya makosa mengi naye pia, bora tu asahau yale aliyofanyiwa na wazazi wake ili apate baraka za kulea watoto wake naye.

.

Watoto wako watachukua maksi kwa tabia hii na hata baadaye utaona matunda yake. Bidii yako iwe katika kujenga tabia ya watoto.hivyo vingine visikuyumbishe vipange kama viko kwenye uwezo wako. Wewe ndiye unaongoza hiyo serikali! Kila serikali ina sheria, wafundishe watoto wako kutii sheria. Wafundishe watoto wajiheshimu na kuheshimu serikali yako, ya taifa na ya Mungu.haki za watoto zijaliwe kama elimu na vingine.usidekeshe watoto wako wala usiwanyanyase.. Ujiwekwe kwenye mkono hodari wa Mungu ili akutegemeze. Saidia wenye mahitaji katika juuAnza toka watoto wakiwa muiya yako. Uwe ndiye mfano wa kutoa zaka na sadaka katika familia yako.. Upange matumizi ya pesa vizuri, hata watoto kuwapa kitu kidogo na kuwafundisha matumizi bora ya pesa. Usiwe mfujaji kwa matakwa yako ila bahili wa mambo ya mji wako. Rekodi matumizi vyema usiwe mfujaji. Usiwe mvivu! Uwe mkarimu hata kwa mke wako. Uwe na akiba kwa dharura za familia yako hilo ni jukumu lako kama Kiongozi wa nyumba. Jifunze toka mtoto akiwa tumboni kuwa mzazi bora. Watoe watoto wako wakfu kwa Mungu. Nyumba yako iwe na mipangiliio. Fanya maisha ya kumtegemea Mungu kuwa ya kuvutia kwa watoto, hapo ndipo utafanikiwa. Uwe mwaminifu kwa viapo vyako vya ndoa na huduma, uvifanye vipya (renew) mara kwa mara. Hebu usiwe kama mtu wa Laodikia, utakayetapikwa bali uwe mshindi. Ukifanya ya upande wako utaona tu kwamba utakuwa kichwa na si mkia kwa mambo yote yale yenye kuleta utukufu katika jumuiya na zaidi kwa BABA wa mbinguni.

Punde watatoka na kwenda kuwa na miji yao, je watakukumbuka wewe kwa nini? Siku zinaenda mbio, nawe utakuwa umestaafu na mzee ila hujajenga mahusiano na watoto wako. Utaonekana kama mgeni fulani katika maisha yao. Watoto wanaitwa kwa jina la baba na waafrika wengi ni wa baba! ila wakiona kwamba mama yao ndiyo wanajali, utaona wanashugulika naye zaidi!. Kule Kisii niliona watoto wengi watu wazima wenye vibarua vizuri walichukua mama zao mijini na kuishi nao wakimwacha baba mzee akijipikia mwenyewe. Wengine walimtumia mama yao tu pesa, ndiye alimgawia mzee, na mzee akinungunika walimchukua kwao, hata watoto wengine waliishi nje ya nchi walichukua mama zao Marekani au Ulaya na kuacha baba zao wakiishi maisha magumu.

Walifanya makosa ya kutosamehe baba zao walipokuwa wadogo. Wengine ilikuwa laana maana walirudia jambo hili kwa wake na watoto zao pia, japo walifanya kuonea huruma mama zao. Kama kuhani wa watoto wako, wafundishe watoto wako kusamehe watu, kujisamehe na kusamehewa na msamaha ambao MUNGU anatoa. Kabla ya kwenda kulala mwombe MUNGU msamaha kwa makosa yao na yako, na waambie wao wenyewe kwa yale makosa wanayoyakumbuka wamwombe MUNGU msamaha na yale wamewakosea wengine waombe msamaha.

Wajue kwamba tuna kuhani na wakili mkuu mbinguni anayetuombea na kwamba siku ya hukumu tutapokelewa bila mawaa, si kwasababu tulikuwa watakatifu, la! Bali kwasababu tulikubali na kutii neno lake kwamba Tukiungama dhambi zetu YEYE ni mwanamifu na wa kweli kutuosha dhambi zetu zote.
Wafundishe watoto wako kwamba siku moja kila binadamu atasimama hukumuni, na yule aliyemwamini MUNGU na kuungama dhambi zake atakuwa na uzima wa milele, naye aliyeficha dhambi zake atahukumiwa. Wasisitizie upendo wa MUNGU na kwamba anatuombea tufanye maamuzi bora ya kumpenda watu na kupenda watu.

Sura ya 24
MAMA NA MALEZI YA WATOTO

Kando ya uhusiano wa Mungu na mtoto, uhusiano wa mama na mtoto ndiyo unaofuata. Tunaambiwa, “Je mama anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya?” Jibu ni, “Ndiyo!”. Mwenyezi MUNGU tu ndiye anayependa watoto wetu au watu wote kuliko sisi. Kwa

kuwatupa chooni, mapipani au kuwaua tumeonyesha kwamba wakina mama si kilele cha upendo kwa mtoto. Mtu mwingine alisema katika nchi ya Marekani wakina mama milioni nne wanatoa mimba na hivyo kuua kila mwaka; na nchi zingine duniani watu milioni 50 kila mwaka hutoa mimba. Hili ni jambo la huzuni, na bora kuulizia vitengo vya serikali au vya huduma kuchukua watoto hawa kuliko kuwaua. Mama ana mchango mkubwa sana; watalaam wasema 40%, kwani mama hukaa na mtoto zaidi ya baba. Wakina mama wengi wamepata shida kwenye uzazi kwa ajili ya watoto wao. Usemi kwamba kulea mimba si kazi bali kulea mwana mara nyingine si kweli. Kina mama wakikueleza taabu za uzazi, "Nimechungulia kaburi, mguu mmoja ulikuwa duniani mwingine kaburini;" utashangaa!

Hebu mwanamke atambue kazi yake. Hebu afundishe watoto wake wawe wa kufaa kwa maisha yao, ya jumuiya na hata yale ya milele. Mama awe msaidizi mwema kwa mumewe. Asifanye kazi zote kama mtumishi wao na wao wanakaa tu, eti wanasoma! Watoto wanasoma ili wapate kazi, na kazi za kalamu zitasaidia nini kama hawajui kazi za mikono? Watoto wajue kufua nguo zao. Mtoto wa miaka kumi asiyejua kufua nguo zake umemchelewesha. Aanze hata akiwa na miaka mitano, kufua nguo ndogo ndogo; hata kama utazirudia. Mtoto ajue kwamba anapaswa kuoga kila siku. Watoto wengi wamejaribu kujificha wasioge! Hebu mweleze mtoto jinsi ya kutunza mwili wake, sehemu za siri na za wazi, jinsi ya kuzisafisha. Nimeona watoto wengi wanaoga ila hawaoshi nyuma ya masiko au mgongo!

Kufua nguo za ndani ni muhimu. Mtoto asiloweke nguo za ndani eti atafua kesho hasa msichana. Najua wengine wana mashine za kufulia au mfanyakazi, ila jua kufua bila mashine maana kuna siku itakubidi ufanye vile. Hata hivyo waweza kufua nguo moja ndogo na Mashine na kuharibu maji, sabuni na umeme kweli? Dunia inabadilika hata yawezekana siku itafika wote turudi kulima; Je, watoto wako wataweza kazi za mikono? Mfalme katika kiti chake cha enzi; kazi yake ni ya muhimu kama tu ya mama. Yeye anaumba tabia ya watoto wake ili ifae kwa ufalme wa milele. Hebu asitake kukazana na taaluma na kazi ya kuajiriwa kabla hajashugulikia tabia za watoto wake.

Mama ni malkia kwa watoto wake. Mara nyingi mama haridhiki na kazi hii ya kumlea mtoto; ikifika jioni hana cha kuonyesha alichokikamilisha: Amepika, ameangalia watoto na kufanya usafi wa nyumba, kufua n.k. Hakuwa kama mfanya biashara aliyepata pesa, au mkulima aliyelima mazao, au makenika aliyetengeneza gari hivyo amechoka kilichomchosha hakionekani. Kama macho yetu yangefumbuliwa na kuona kazi ya mama tungeshangaa sana. Mama ni zaidi ya malkia au raisi anayepita kwa vingora na kusindikizwa (motorcade). Makanika, au mpasuaji wa ubongo yaweza kazi yake isionekane mbinguni ila kazi ya mama yake ina mwangwi mpaka mbinguni.

Hebu ajitahidi sana amwakilishe vizuri baba ili watoto wawe na adabu na wapate baraka, hata kama baba yao ana mapungufu. Nasema hili japo ni gumu, kwani kuna siku zinatokea nachukia kwa jambo na hivyo nahitaji kujikana nafsi. Nakumbuka siku moja

nilipofikiria mume wangu amenionea kwa jambo na watoto walisikia tukizungumza, mtoto wangu mkubwa wa miaka 7 aliniambia “mama tumchangie baba tumpige, mimi tu mwenyewe nitampiga na mdogo wangu atanisaidia!”. Nilishtuka sana. Nikasema lazima nibadilike kabisa. Mama wengi walioficha mapungufu ya baba wamebariki watoto wao kwa Njia nyingi. Kwani watoto wanamsamehe mama kirahisi hata awe mbaya, maana kuna maelfu wa mama wabaya maana wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.Nina nani aliye kamili kweli? Nionyeshe kama umemwona maana hata Kitabu kikuu kimezungumza mama hao kama vile Jezebeli au Atalia.

Mama atambue zawadi kubwa kwa malezi yale atakayotoa kwa watoto wake. Kazi yake ni sawa au zaidi ya yule aliyeenda kazini. Wale walioachiwa watoto na wakafanya wanavyopaswa wanatambua hilo. Mtoto akifika miaka mitatu tabia imejengeka, na miaka sita tabia imekamilika. Mama ni wakala wa Mungu kufanya watoto wamjue Mungu. Maana kutoka Mungu upendo wa mama kwa mtoto ndiyo unaofuatia! Mvuto wa mama ni mkubwa. Mama ajue kupika na kushugulikia afya ya watoto. Chumba cha watoto kiwe na hewa bora na jua lipenyeze. Mapambo yawe yale rahisi; siyo ya kumshugulisha mama mpaka aache kushugulikia maslahi ya watoto. Upole na upendo kwa mtoto ni wa muhimu nao unaonyeshwa kwa kutoa muda wako. Mama lazima uwe na muda na watoto wako.

Mama aangalie afya yake, kwa kutozaa watoto wengi na kutokuwa nafasi nao. Mama Susan Wesley alizaa watoto kumi na tisa alihakikisha ameomba na kila mmoja kila siku. Watoto wake walikua na kuwa watu mashuhuri waliobariki dunia kwa huduma zao zenye mvuto mzito. Wakati huu si wa kuzaa watoto wengi vile maana watakuwa mzigo kwa kanisa na hata wewe kama utafanya umishonari kidogo sana endapo mara zote utakuwa unalea watoto wadogo. Hata wale ambao hawaamwamini Mungu wa mbinguni wanaamini historia ya dunia imeisha kwamba siku za karibuni watamwona Kristo (Isa Bin Mariamu) akishuka mawinguni. Jisomee zaidi hili katika Danieli 2, 7, 8 na 9. Nasisitiza kwa hili maana nisipolisema dhamira yangu inanishitaki kwamba siku moja isisemwe “Kama uliyajua haya mbona hukutuambia?”. Zawadi Kubra kwako mama na baba na watoto wako ni kupata uzima wa milele. Mengine yote ni “na kadhalika”. Hata tunapojifunza malezi, si tu uishi na mtoto wa adabu, bali hatimaye uwe naye mbinguni kwa neema zake Mwenyezi Mungu.

Mama wengi wanajali sana jinsi jirani na watu wengine wanavyomfikiria kwa mavazi yake na anavyolea. Mama asijali watu wanavyofikiri ila awalee watoto wake ili wawe wenye rehema, na kupenda haki na kuwa na unyenyekevu. Nimetembelea nyumba nyingine nikaona watoto wanalala mpaka saa nne au tano mchana wakati shule zimefungwa, eti wafanyakazi wanawafulia watoto na kutandika vitanda. Wengine wanafanya hivi kwa ajili yakuangalia televisheni mpaka saa nane ya usiku. Runinga si mbaraka kwako, inaweza kuwa na mambo matatu mazuri ila mia moja mabaya! Siku hzi mapicha yaliyopo tunazidi kuyazoea ila mengi ni machafu yanayoleta mawazo maovu. Jambo la kulala hivi ni la siku hizi, sisi hatukulikuta hilo, kama mzazi wako walifanya hivyo lilikuwa ni kosa. Mtoto alale mapema aamke asubuhi, ajisomee, asali na kufanya kazi. Masaa 8-10 yametosha, asijigaragaze kitandani na kuwa kwenye simu siku nzima.

Inajenga uzembe ambao ningekuwa na muda ningeeleza zaidi. Mama amheshimu mume wake; watoto wasione mtengamano.

Mama kazi yako ya kwanza ni kufunza watoto na si taaluma na mapambo. Mama vaa kwa heshima. Usioge na watoto. Weka mstari ili watoto wakuheshimu. Usijiachie.Mtoto anajifunza kuvaa kwa heshima toka kwa mama. Wanaume hawana vishwawishi vya kuvaa ovyo ovyo kama wakina mama Siku hizi hata mama wa makamo, hata wazee wanavaa nguo fupi sana, suruali za kubana au migongo wazi!! Je, mama ukivaa hivi, binti yako atavaaje? Huwa ninasema muda si mrefu, Yesu asiporudi mapema, wanawake watatembea uchi!. Hivyo, mama jifunze kuvaa vizuri kwa afya na kwa adabu. Binti zako wataiga. Nilimuuliza binti mmoja wa kisasa, amemaliza chuo kikuu kwamba kwa nini yeye alikuwa tofauti na rafiki zake, waliokuwa wanajipamba kupindukia na kujipaka rangi kila mahali? Akanijibu, “Mimi sijazoea, maana sikuwahi kumwona mama yangu akipaka rangi.”

Nguo za watoto, ukiweza kujifunza kushona na kuwavisha watoto ni vyema sana itakata makali ya gharama na pia itafanya kuwavisha watoto kwa jinsi va kufaa. Madukani ninapoishi nilijaribu kwenda nikakuta suti za kike, makoti yake ni mazuri ya heshima, ila sketi zake ni fupi mno au zina mpasuko mkubwa (slit). Kama Raisi Nyerere alivyosema wengi wetu tunafikiri nguo za kutungua ndizo nzuri (ready made); wakati nchi zingine wabunifu wa mavazi wanaoshona wanapewa pesa nyingi kushona kuliko nguo iliyotunguliwa. Mfano iliyotunguliwa ni dola thelathini, na iliyoshonwa dola mia nne! Mama jifunze kushona, unless kuna sababu inayokuzuia. Wazazi wengi wenye mabinti wana changamoto wakienda kununua nguo. Mabinti wanataka kununua fupi na za wazi kuendana na fasheni.

Mwaka 2012, katika kongamano la Dodoma wanawake tulialialikwa kutembelea bunge. Tulipewa masharti: Usiingie bungeni na nguo fupi, lazima iwe chini ya magoti, na isiwe wazi au ya mikono mifupi au malapa! Hata serikali inajua nguo isiyo na heshima eti! Somo la nguo ni muhimu sana ila kwa sababu ni refu sitazungumzia sana ila tuna email tumeandika kama unataka maelezo zaidi. Mabinti zako uwafundishe kazi za nyumbani kama kupika, mtoto akifika miaka kumi na miwili awe anajua kupika hata usipokuwepo. Akiwa mke nyumbani kwake ana thamani sana akijua kupika kuliko akijua compyuta. Mafundisho kwa watoto wetu ni ya kurudia rudia, kila mada au topiki tunarudia rudia tena na tena kwa njia tofauti tofauti.

Ujue watoto walipo wakati wote, hata wale wakubwa. Watoto wengi wakienda nje wana majaribu mengi ambayo kuyashinda ni vigumu. Kuna wenzao watakaosimama nao njiani kupiga guzmzo la uvivu tu, na kupanga kufanya yale ambayo yatakuwa hayajengi. Kurudi usiku usiku kusiwe mtindo. Usifukuze watoto kwa sababu uko busy eti wanakupigia kelele. Kile unachofanya wafunze nao, ndiyo watakavyopata maarifa. Mtoto wako ni kitu cha thamani, usimwachie mary, Asha au Amina ye yote unayemwona. Kina mama wengine wanaogopa watoto kuharibu vifaa vya kazi kama pasi, mashine ya kufulia au mifagio maalum. Mtoto asifanye kila kitu kuwa cha kuchezea kama mwanasesere. Mwonyeshe jinsi ya kutumia kifaa vizuri na simamia ili uharibifu usijengeke ila mtoto ajifunze ustadi. Usiwe mkali kupita kiasi ila uwe na mkazo ili watoto wajue kifaa hicho kutumia ipasavyo ni muhimu. Mtoto asiyejua kutunza vitu vya wengine hata vyake itakuwa vigumu.

Watoto wanafurahishwa kirahisi na kukasirishwa kirahisi. Wafundishe kufanya vitu vyema kwa upendo na mamlaka kama mama. Ukifundisha usizungumze na hasira bali mtoto aelewe hichi ni “hapana” na hichi ‘ndiyo” kufanya. Kumbuka hata wewe ukiwa mdogo ulijifunza na kulikuwa na ugumu. Jiwekwe kwenye viatu vyao. Ila jitahidi usiwe mtu mwenye kuamrisha, kukaripia na kukemea kila mara, njia hiyo ya kufundisha imeonekana kwamba ina mafanikio ya muda ila baadaye unapoteza mtoto.

Mpaka mawazo ya watoto yakite kwenye Mambo ya kiroho ndiyo tabia itakuwa nzuri. Hata wanafalsafa au wanasaikologia wasemeje, mtoto lazima akite pale ili hata akiwa peke yake afanye anavyopaswa bila ya kuogopa mzazi. Mara nyingi tunawaogopesha na kuwaadabisha watoto wetu kwa bidii tukifikiri watatusikiliza na kufanya tunayowaambia. Kumbe tukitoka tu hivi wanafanya maovu!

Niliona msichana mmoja akivaa nguo nzuri akitoka nyumbani ila alibeba nguo fupi na za wazi, akavaa akijionyesha mbele ya watu, mbali na kwao. Watu walimwambia mama ila hakuamini, na aligombana na watu na kuwapakia maneno, “Ninyi mnamsingizia mtoto wangu, na wenu ni wabaya zaidi ya wangu.” Usimtetee mtoto mno. Mtoto ni binadamu anaweza akupendeze machoni pako ila moyo wake haupo pale, hivyo la kwanza mfundishe mtoto Amwogope Mungu Kwanza na mengine yatajipanga.” Bali utafuteni kwanza ufalme Wake na haki Yake, na yote hayo mtazidishiwa;” Mathayo 6:33.

Maombi ya asubuhi na jioni ni muhimu sana kama baba alishaenda kazini au hayupo, wewe ndiye msaidizi wa kuhani. Mtoto hata wa miaka sita ataweza kusoma neno la Mungu kila siku. Ila atahitaji mwongozo kila siku. Wasaidie kuweka ngome kwa kujikita kwa neno la Mungu. Mama hugundua vipando vya shetani kwa watoto wake kuliko mtu mwingine. Wafundishe watoto kujikana nafsi ili kama wana tabia mbaya wanaweza wakaiacha kwa urahisi kwa neema za Mungu.

Mama mmoja aliniambia jirani yake alipeleka watoto wa kiume wadogo wa miaka mitano na kumi boarding. Mume hakutaka maana aliona wanahitaji mwongozo wa wazazi bado ila neno la mama likawa na nguvu wakaenda. Wakirudi likizo yaya aliona kwamba yule mkubwa alikuwa anafanya kitendo kibaya cha kumlawiti mdogo wake na akwambia mama, ila mama alikiambiwa alikuwa na shuguli hata maneno haya hakuyatilia maanani. Yaya aliendelea kusema hili, ila mama alienda kibaruani na kurudi jioni. Ndipo baba alipogundua kwamba yule mtoto wa miaka mitano anatembea kama ana kidonda. Baada ya upelelezi aligundua kwani yule mtoto wa alimweleza baba yake kilichofanyika.

Kuna shida nyingine pia ambayo watoto wengi wanaingia nayo inaitwa punyeto. Hii nikuchezea viungo vyao vya uzazi. Wataalam wamegundua hili linaathiri akili. Kina mama tusiwe na mashuguli mengi. Mungu hakutupa kazi ya kwenda vibaruani ila kutunza watoto wetu na waume wetu. Kina mama wengi wameingia mashule makubwa makubwa; sisemi hivi kwa ubaya ila lazima uone cha kipaumbele kwako ni nini. Pengine, wengine ni vyema kumaliza shule ndiyo tuanze kuzaa.

Kunyonyesha watoto ni muhimu sana, kusema kwamba hatuna muda wa kunyonyesha mtoto ni kumkatili mtoto, najua kwamba filosofia nyingi zinaingia za

kufanya maziwa yawe urembo na mengineyo, ila si kazi ya kwanza ya matiti. Watoto wengi siku hizi wamegunduliwa na magonjwa yanayotokana na wakina mama kutonyonyesha. Wazungu baada ya kututoa kwenye kunyonyesha wao sasa wamefanya utafiti na wakarudi kunyonyesha. Nikijifungua kulikuwa na mwalimu rasmi kila hospital wa kufundisha kina mama kunyonyesha! Na anapita kila masaa matatu akisaidia maana, ukianza kumpa mtoto maziwa ya chupa, baadaye unafikiri uache tu kunyonyesha, ni bughudha. Mama mmoja mzungu, aliniambia, "Unajua siku hizi hatuna shida na waamerika weupe, ila waamerika weusi hawataki kunyonyesha japo zamani walinyonyesha kwa vile walikuwa wanafuata mila na wahakuwa na pesa nyingi kama sisi." Naona mapinduzi haya yamekuja kwetu. (Soma sura ya maziwa).

Dada mmoja msomi wa shahada za juu mwafrika, alipojifungua mwenye pesa nyingi za maziwa ya chupa, maana ni ghali alinimbia, "Mume wangu ameniambia nisinyonyeshe kwani mtoto anapata gesi tumboni, ila maziwa ya chupa ndiyo mazuri!" Mama huyo alikuwa hana kibarua kwa miaka mingi tu alikuwa mama wa nyumbani. Alikuwa amezaliwa kijijini na mama yake alimnyonyesha, sijui alipata haya mawazo wapi masikini, niljaribu kumweleza ila haikusaidia. Mara nyingi jiulize haya ninayofanya ni mpango wa maumbile? Ni mpango wa Mungu? Nilipojifungua daktari wa watoto na manesi waliniambia nisilale na mtoto chumba kimoja alale peke yake! Hata nilishaangaa kwamba hata mimi na mume wangu ni watu wazima, na tunataka tuwe pamoja; itakuwaje mtoto mdogo? Nitajuaje kama anasikia joto au baridi? Jambo hili limefanya pia watoto wasiwe karibu na wazazi kwa mawazo yangu. Kama mama ana usingizi wa ajabu au anakunywa pombe, ndiyo vizuri akae mbali na mtoto. Nafikiri haya utayaona yanavyokufaa pia zungumza na mhudumu wako wa afya zaidi.

Mtoto afundishwe usafi, unadhifu na mpangilio wa vitu vyake nyumbani. Asitoke kitandani bila kutandika au kupanga chumba na kukunja nguo zake ni sehemu muhimu ya elimu. Itawachukua muda ukilinganisha na wewe ila utajenga tabia ili wawe msaada kwako siku za karibuni. Wajisikie chumba ni chao na wao wanawajibika kukifanya kiwe kisafi. Mama atoe maagizo na jinsi ya kupanga. Fanya nyumba yako iwe mfano. Wakumbushe watoto kwamba Mungu wetu ni wa mpangilio. Hiyo ni sheria ya kwanza ya mbinguni; mpangilio ulio na unadhifu. Waingereza wanasema, "Usafi ni next to God." Ikiwa wazazi wanataka watoto wao wapende usafi wa mazingira na moyo ni lazima wawe walinzi wa hilo. Nimeona wazazi wengi wakiachia dunia kufundisha watoto wao ngono (sex)! Hili ni kosa kubwa. Eti wanaona aibu, shetani amefanya zawadi iliyotolewa kwenye ndoa ionekane ni ya aibu, ila mambo ambayo si ya Mungu yaonekana kwamba ni ya kujisifia na fahari.

Mtoto wangu wa darasa la sita alikuja na kitabu cha sayansi kinaeleza yote kwa undani yahusuyo ngono, na picha! Sasa usifikiri ukianza kumwambia mtoto wa miaka mitano umewahi. Masomo ya uzazi yanaanza mapema shuleni. Na kuna rika rake wanaopata habari nyingi, na kuna msukumo wa rika. Asijifunze toka kwingine ila kwako na kwa hatua. Akikuuliza swali omba hekima ya kulijibu. Wanaume wengi wanajaribu kuepuka maswali ya watoto. Ngono si dhambi, ila nje ya ndoa ila shetani anataka tuifanye kitu cha aibu kuzungumza na watoto wetu. Usijitie unaona aibu na tendo hili, kama ni la aibu vile usingelifanya na Pili inajulisha kwamba hujui mpango wa Muumba kwako. Anza na

mambo rahisi anayoyajua kwenye mwili wake: “Je, tofauti ya wavulana na wasichana ni nini? Kwa nini mimi siwezi kulala na dada yangu kitanda kimoja ila wewe unalala na baba kitanda kimoja?” Watoto ni wadadisi kama mimi na wewe. Watoto wangu wameniuliza maswali mengi sana mfano, “Mimi nilitoka wapi? Niliiingiaje tumboni mwako?” (Soma sura ya pili). Majibu yazingatie umri wa mtoto na yale anayoyajua. Mwambie mtoto, akiwa mdogo, kwamba asimruhusu mtu ye yote kushika sehemu zake za siri. Katika elimu hii, kazia usafi ngono na wa maisha (sex and purity). Kama hujagundua tunaishi katika dunia ambayo kuna wagonjwa wengi wa akili wanaopita na kudhuru watoto. Sisi kama wazazi tunalala ila shetani halali ni simba angurumaye akitafuta wa kummeza, usije ukawa wewe au mimi!

Watoto wadogo wameingia kati mambo ya hatari ambayo walimu wanajua ila wazazi hawajui. Mwalimu mmoja Nairobi aliniambia kwamba siku moja aliposhuku kitu, aliingia chooni kwa wasichana akakuta kila choo kina watoto wanazungumza. Watoto hawa wasichana walikuwa wawili wawili kila choo. Walipoambiwa wafungue walikataa, mwishowe kwa kubembelezwa walifungua mlango. Ilibidi walimu wawape kinga, “Tuambieni mlikuwa mnafanya nini, mkituambia ukweli hamtapata adhabu.” Walisema kwamba walifundishwa nyumbani kwao mambo ya ushoga; na kwamba usipokuwa na mtu na kufanya yale walifanya utakuwa umepitwa na wakati!

Pengine kila mmoja wetu amesikia haya maana nimekaa karibu na walimu watoto wengiine wanaleta mikanda michafu nyumbani na kutazama wazazi wakilala usiku! Sitii chumvi kwa haya ninayosema, naomba usiweke kichwa chako michangani kama mbuni ukifiri shida hizi zitapotea zenyewe. Kina mama fundisheni watoto wenu kila kitu wasije wakapata mafundisho mabaya pengine. Kuanzia kazi mpaka uzazi. Msikate tamaa, kazi yenu kama wazazi yaweza isionekane papo hapo ila matunda yake yataonekana baadaye.

Mama aepuke maneno ya kumkashifu mtoto, hasira, matusi, kulinganisha watoto, kumgombeza gombea, kumfokea kwa sauti ya juu. Haya hayasaidii kumjenga mtoto badala yake mtoto atayaigiza na kuyatumia akienda kwenye mji wake! Mfundishe mtoto maneno mazuri kama: pole, asante, samahani au naomba! Usione aibu kuomba msamaha kwa mtoto wako! Mtoto ajifunze kutoa. Tabia ya kuingilia mazungumzo ukiwa unazungumza na mtu mwingine, ni mbaya. Mwambie asubiri (kama siyo dharura), hadi umpe nafasi ya kuongea. Nguvu au mvuto wa mguso wa mama ni muhimu, mpongeze mtoto kama amefanya jambo zuri, mpe mkono au mshike begani kwa jambo zuri alilofanya. Mtoto anapata moyo akiwa na maumivu mama akimshika na kusema “Usiwe na hofu;” anapata nguvu za kuendelea na maisha.

Matabibu wanaendelea kugundua mvuto wa mguso, ‘power of touch,’ kwa wagonjwa hospitalini na pengine. Kina mama wengi wa kiafrika tunaona aibu na kujisikia awkward, kukumbatia watoto watu wazima. Twawapa faraja watoto wadogo ila wakikua tunaogopa kuwashika hata kuwakumbatia kwa nyakati ambazo ni muhimu. Tunaweka

madaraja na watoto kwa ajili ya mila zetu japo mioyoni tunawapenda kweli kweli! Mama ajaribu kutafuta wanawake wenzake ambao ni wa msaada kupeana maarifa na kutiana moyo maana mara nyingi anabaki peke yake na watoto. Mume anakuwa mbali kwenye shughuli na anaona kazi yake hailipi au ni duni, jambo ambalo si kweli. Ujithamini, ujiheshimu na shughulika kujifunza vitu vipya hapo nyumbani kama vile kufinyanga vyungu, kushona nguo na masweta, kufuma, n.k. Mama jihadhari na kusengenya na kusema wengine; watoto wataiga hii tabia mbovu. Ni vizuri ucheze na watoto ili wajifunze maadili na kucheza bila magomvi.

Wanawake wako karibu na watoto kwa miezi tisa ya kwanza ya tumboni. Huduma ya mtoto ni pana nzito na ya kipekee. Wanawake wengi hawahitaji kushauriwa kuwa tayari kwa kushugulikia maslahi ya mtoto. Mwanamke ambaye ana elimu na amepewa msingi, ni rasilimali ya pekee kwa kufundisha mama na walezi wa waoto walio katika shida, wanawake wenzake na watoto wa kike kuendelea na kushugulikia malezi ya mtoto kitaifa. Kina wa mazingira magumu wahitaji kuombewa, kutiwa faraja, kushauriwa na kuwezeshwa kusaidia jamii. Mama wanahitaji kuelimishwa kuhusu lishe, afya, usafi na nafasi ya mama katika familia.

Wanawake wana uwezo wa kubadilisha mambo mengi kitaifa kama Malkia Esta. Alikuwa mmoja ila akawa mkombozi wa taifa lake. Esta ni sauti ya wanawake wanaomcha Mungu kuwachukulia watoto walio masikini kama watoto, na kuwasaidia kwa njia mbali mbali. Wanawake wanapaswa kueleweshwa na kutambua umuhimu wao kwa mpango wa malezi bora ya mtoto. Mwanamke apewe mbinu za kufaa ili asaidie watoto walionyanyaswa, watoe huduma ya maombi, elimu, afya, maelekezo, ushauri, kuwatia moyo.

Mama, wewe ndiye malkia wa nyumbani mwako, hebu shikilia usukani, ukiongozwa na Mungu, usimamie nyumba yako. We are the home makers, hilo ni jukumu tulilopewa na Mungu Mwenyewe. Tunapata matatizo kwa sababu tunataka kubadilisha majukumu aliyotupangia Mungu mwenyewe. Biblia inasema “Mwanamke aliye na hekima hujenga nyumba yake, bali aliye mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe.” Methali 14:1. Biblia inataja wajenzi wa unyumba wawili tu: Mungu (Zab 127:1), na mke. Mwanaume anatajwa kama kichwa cha mke, na kazi zake ni za uongozi katika familia.

Kazi za nyumbani kama kupika, kufanya usafi ndani na kupanga nyumba. Kupangia watu wa nyumbani mwako, (hata wafanyakazi) kazi, kuamka mapema, na kufanya mengi yaliyoandika katika Methali 31. Fungu la 28-29 linasema: “Wanawe huondoka na kumwita heri, Mumewe naye humsifu na kusema, binti za watu wengi wamefanya mema, lakini wewe umewapita wote.”Tumeharibikiwa kwa kutaka usawa katika nyumba, eti tugawanye majukumu, kwa sababu siku hizi wote tunaenda vibaruani, hivyo tuna ratiba ya kazi za nyumbani!! Baba ana siku yake ya kupika, kufua, kudeki, n.k. Kusaidiana kazi za nyumbani ni sawa kabisa, sipingi. Ila ni kazi zipi ambazo mwanaume anaziweza na zipi ambayo tungevumilia kuzifanya hata kama tumechoka? Kamwe mwanaume asimuogeshe binti wa kike, hata akiwa mdogo, na kumbadilisha nepi au pampers. Nilimsikia mama mdogo wa kileo, akisema, “Ngoja ambebe, sasa ni zamu yake, mimi nilimbeba kwa muda wa miezi

tisa tumboni!" Alimwachia mume kubeba mtoto mchanga kanisani, hata akilia, baba ndiye atahangaika kumtoa nje, na kumbembeleza!

Jambo jingine ambalo tunashauriwa katika Maandiko matakatifu ni "Kuwatii waume zetu kama kumtii Bwana wetu." Waefeso 5:22. Tuwatii katika Bwana. Tukate mabishano na magomvi madogo madogo, (nagging). Msichana wa kisasa alikuwa anagombana gombana ovyo na mume wake, akaja kuniambia, eti "Nikipika kuku, anakuja anasema anataka kula samaki, sasa mimi nachoka kupikapika!" Nikamwambia si ukamnunulie umpikie tu? Akasema, kwani ni wa kununua? Wamejaa kwenye jokofu, (friji)! Jamani! Kutoa samaki kwenye friji tu na kumyeyusha kuna shida gani kuliko kuanzisha ugomvi?

Sura ya 25
KUCHAGUA MWENZI WA MAISHA

Hatuna budi kuzungumzia kuhusu kuchagua mchumba, sisi kama wazazi tunashauri watoto wetu wanapotaka kuoa au kuolewa wako watakusaidia kazi ya kumshuhudia Mungu. Waweza kujitahidi kutunza mtoto wako, ila asipojua vitu vya kuangalia kwa yule atakayekaa naye maishani, nyote mwaweza kuwa na huzuni. Kwa kawaida, binadamu anakaa na mwenzi wake muda mrefu zaidi kuliko nyumbani kwao. Kuchagua mwenzi wa maisha kikamilifu ni jambo la muhimu sana.

Hatuna budi kuzungumzia kuhusu kuchagua mchumba, maana mke au mume wako watakusaidia kazi ya kumshuhudia Mungu. Ili kazi ya Mungu, na malezi ya watoto yawe bora lazima uwe na mke au mume wa kufaa. Kwa kuzingatia Biblia, uhusiano wa

hawa watu wawili ya kupendana, kujaliana na mwanamke kumtii mumewe ndiyo nguzo ya kufanya kazi ya ulei; la sivyo, ukae msela kama Paulo, ila 'usiwake tamaa.' Ni vyema vijana, (wa Kike au kiume), wajitunze vizuri bila kuhusika na ngono nje ya ndoa, uzinzi au uasherati. Maadili haya ni muhimu, hata tunaowaongoza wakiyaona inatusaidia kuwaadabisha ipasavyo. Yote tunayotenda na kusema ni mawasiliano.

Mungu ndiye alianzisha mpango wa ndoa, kazi na mapumziko baada tu ya uumbaji; ni vyema kuandaa unyumba bora utakaokabili maisha na malezi ya mtoto. Tusidanganyike kwamba tunaweza tu kufanya tunavyotaka: Kuzaa na mtu yoyote wakati wowote, bila kuathiri kazi yetu ya ulei!. Furaha ya ulei nyumbani, na watoto inaongezeka mkijaliana. Mungu ni mwenye rehema, kama tumekosea bado tuna nafasi ya kujitahidi na kuwa waume au wake bora. Ndoa ni kamba ya nyuzi tatu, yaani mwanamume, mwanamke, na Mungu. Hatuwezi kuwa na ndoa bora tusipomshirikisha Muumba. Ndoa inakuwa na nderemo na vifijo, ikimaanisha, ni kweli kabisa si vyema mtu akae peke yake.

Kila mwaka ndoa zinafungwa kwa wingi, ila asilimia nyingi ya ndoa zinavunjika kabla ya miaka mitano. Nafikiri zaidi ya asilimia 50 ya ndoa zinavunjika au zinabaki zikiegeshwa. Miaka ya sabini, nikiwa sekondari pale Dar, kulikuwa kuna visa vingi vya wachumba, vilizotukatisha tamaa wengi wetu kuolewa au kuoa. Nitasimulia kisa kimoja kicholifanyika katika kanisa moja, pale mjini Dar. Msichana aliyekuwa anataka kuolewa alidanganywa na rafiki yake kwamba yule bwana ana msichana mwingine. Siku ya arusi, alipoulizwa kama anamkubali yule bwana, alisema la! Yule bwana alishangaa! Wlitoka nje akajaribu kuzungumza naye akimshauri/shawishi. Alipokataa kabisa, yule bwana alisema mbele ya wote pale kwenye mimbari, kwamba alikuwa nje ya nchi na alikuja kuoa ili arudi masomoni, na kama kuna msichana yeyote aliye tayari kuolewa naye aje wafunge ndoa. Yule rafiki wa bibi arusi aliyetoa habari za uongo kwa bibi arusi alijitokeza na ndoa ikafungwa. Yule bibi arusi alisikitika. Hata wazazi wake walishangaa, kwamba amewaleta mbali hivi na kuwaabisha; si angemwambia tu yule bwana wakiwa wenyewe kwamba hataki kuolewa naye?

Ndoa nyingi zimeleta athari kimwili, kiakili na kijamii. Kazi ya Mungu imepata pigo kwa ndoa zilizo na shida kwa ajili ya uchaguzi mbaya wa mwenzi, kutokuwa na sababu halisi ya kuoa na kutokomaa kiakili au kuolewa kwa tamaa ya kimwili tu au hata tamaa ya mali. Ukomavu wa kimwili, kiroho na kijamii ni muhimu sana. Mara nyingi tunakuta watoto wanalea watoto. Ni muhimu mtu kupevuka. Kukomaa kiroho ni pamoja na: Kumpenda Mungu, kuvumilia maudhi, kukubali kukosolewa, kutawala hasira, kufadhili wengine, kutokuwa na wivu, majivuno, kuheshimu watu wa rika zote, kutojipenda binafsi, kuishi sawa sawa na imani yako, kuchukia uovu na dhuluma, kutokuwa na chuki, kuwa na imani na mtu mwingine, kuheshimu mazuri wasemayo/watendayo wengine, kufurahia mambo yaliyo kweli, na kutotia chumvi au kutofanya majaribio ya tendo la ndoa kabla ya kufunga harusi.

Matayarisho ya kupata mchumba ni kama vile uwe na sababu ya kuoa au kuolewa na kuandaa sifa njema. Baadhi ya sababu nzuri za kutaka kuolewa ukifika muda wake ni kama: kupata mtu wa kusaidiana katika shamba la Bwana, kupata msaidizi na mwenzi

katika maisha, kuendeleza kizazi, kupata hadhi ya mtu mzima, kuhalalisha tendo la ndoa na kuzuia uasherati, na kujipata mlinzi (security) kwa wanawake.

Hebu yule anayetaka kufanya ndoa awe mtu wa tabia nzuri, “Mtu asiudharau ujana wako bali uwe kielelezo kizuri.” 1Tim 4:12. Usiwe na tabia mbili, nzuri mahali fulani, na mbaya pengine. Hebu waheshimu wazazi na pia wakwe zao. Mwanamke usipomheshimu mume au wakwe zako, italeta shida kwa watoto pia. Watajua unamchukia bibi au babu yao, na wao pia watafuata maadili hayo. Wazazi wajulishwe, kuhusu mambo ya posa, na kuwe na mawasiliano mazuri, heshima, kuchapa kazi kutafuta riziki, na usafi, uaminifu kazini, uhusiano mwema na watu wengine, sifa nzuri kanisani, utii kwa wazazi, usafi wa maisha ya kiroho, mtu asiye na ubaguzi, mtu wa maombi, mtu wa kusoma Neno la Mungu, kupenda watu na Mungu, anayeungana na wengine kuongoa roho, uaminifu popote, na mawasiliano mazuri, n.k.
“Apataye mke apata kitu chema, naye ajipatia kibali kwa Bwana.” “Uangalifu, mkubwa ungechukuliwa na vijana wakristo katika kufanya urafiki na katika kuchagua mwenzi, jihadhari usije ukakuta kile unachodhani ni dhahabu safi kinageuka madini ya chuma.” Kuna vitu vinavyojitokeza na kuleta udanganyifu, na kuzuia kutambua au kutofautisha dhahabu safi na madini yaliyo na thamani. Kuchagua mchumba ni swala muhimu na nyeti. Ni suala litakalokufanya aidha ufurahie maisha au uwe na maisha machungu na familia yako. Litakufanya uweze kuendelea kumtumikia Mungu au kuacha kabisa. Kita kwenye uchumba si urafiki wa mihadi (courtship Vs Dating).

Jiulize, Je, unataka ndoa ya aina gani? Yenye furaha na umoja au iliyopasuka? Je unataka mume au mke ye yote alimuradi umeolewa?
Je, muungano huu utakuelekeza mbinguni? Je, maisha yako yatakuwa na thamani zaidi, au nyanga nyanga? Kama majibu ya maswali haya ni hapana, nakushauri sitisha mipango ya kutafuta mchumba. Usifikiri tu kwamba upendo mlio nao eti unatosha! Ni kweli Biblia inasema kwamba “Upendo hufunika mabaya yote;” lakini mbona ndoa zinasambaratika baada ya muda mfupi tu? Nilishuhudia ndoa iliyosambaratika baada ya wiki tatu tu! Wengine walikosana wakiwa honeymoon, na waliporudi kila mtu akashika njia yake? Ina maana huwa siyo upendo wa kweli ila tamaa ya ngono. Wakati wa uchumba ni vizuri muulizane au kuona yale ambayo ni ya thamani kwa mwingine. Niliona mlei fulani akimwuliza mchumba wake, kama anarudisha zaka au kutoa sadaka, alijibu; “Mara zingine narudisha, kutokana na mambo yanayonikaba.”

Ni vyema kujua kwamba watoto wenu mtawakuzaje, au hata kama mkijaliwa mngependa watoto wangapi? Mlei mmoja alitaka mtoto mmoja tu ili aende dunia nzima kuhubiri, ila mke wake alitaka watoto hata kumi! Mlei huyu aliendelea kujadili hili, ili aone kama lingeleta ufa au angeendelea na uchumba huu. Je, mchumba wako anapenda kusoma neno la Mungu kila siku na kuomba au hufanya haya kwa nadra au akijisikia? Je, anaheshimu siku ya ibada na anawahi kuja kanisani, na hata kuja vipindi vya mchana? Je, anaenda maombi ya kati ya wiki na mikutano mingine ya dini kama makambi, semina n.k.? Vitu hivi pengine, si sababu ya kufuta uchumba ila viletwe ili muone kwamba vina thamani gani kwenu nyote, hasa kama mnataka kumfanyia Bwana kazi. Wengine wako tayari kuacha yale hafifu na kufanya mema, ila wahitaji waambiwe tu na kuona lile ambalo mchumba wake anapenda.

Mlei mmoja alimwambia mchumba wake kwamba anarudisha zaka ya asilimia thelathini, mchumba wake alishtuka na kuona kwamba hii itafawanya wawe masikini. Kijana mmoja aliniyetaka kunichumbia, hata kabla hatujaendelea sana, aliniambia kwamba yeye ni vegetarian (mlaji wa mboga), na kwake hakutawahi kupikwa nyama. Pia aliniambia kwamba, kwake sabato lazima itunzwe kwa masaa ishirini na manne kikamilifu, na kama nitaolewa naye, niamue mapema, kwani lazima nizingatie hayo kwake. Je, mtakuwa na akaunti moja, na kupanga pesa zenu pamoja ikiwa ni zaka na sadaka? Je, kusaidia jamaa kunapangwaje? Ni jamaa wa pande moja tu wanasaidiwa, au wale wenye shida? Je. Mnapokaa na jamaa na wakaleta ugomvi, ni nani anawaambia masuluhisho, ni yule mwenye jamaa au ni mkwe?

Angalia ubora wa mwenzi, furaha, nidhamu, ubora wa kijaamii, mwombe Mungu wakati wa kuchagua, wengi wanasema, “Ningelijua hili nisingeoa au kuolewa.” Wanajuta hawakufikiria hilo, hawakufikiria ukubwa wa jambo hilo, pengine ilikuwa kwa misukumo ya jamii au ya kimwili.
Kitabu kikuu chasema, “Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa.” Kila aombaye atapata, kila atafutaye hupata, na kila abishaye hufunguliwa.

Mipango ya uchumba isiwe ya siri, uongozi wa wazazi, na viongozi wacha Mungu ni muhimu. Tambulisha, uwe mkweli usiye na wachumba wengi na ambaye anajali utu, na si pesa. Usiwe na haraka, uwe na nafasi ya kufikiri kikamilifu na muda tosha. Mapenzi yasiwe ya ghafla kama kimbunga. Hata kwa yule ambaye ulimfahamu siku za nyuma, ni vizuri muwe na angalau miezi sita ya uchumba. Ila uchumba wa muda mrefu pia ni shida kubwa. Kuna maelfu waliounganishwa katika ndoa ila hawapatani. Vitabu vya mbinguni vimelemewa na misiba mibaya, uthabiti mwingi na dhuluma zisizoelezeka, ambazo zimesitirika chini ya joho la ndoa. Hii ndiyo sababu kubwa ya kuwaonya vijana walio na umri wa kuoana ili wasiharakishe kitendo hiki cha kuchagua mwenzi wa maisha.” Pia epuka vitendo vya kutafsiriwa vibaya waweza kukosa mtu anayekufaa (apperence of evil). Binti, usijirahisishe, na kukaa hadi usiku wa manane na mchumba wako mahali po pote. Epukeni kuwa peke yenu, hata watu wakiwaona kwamba mu watu wa enzi za mawe. Wengi wameingia shida nyingi. Napenda kusema kupata mwenzi bora wa maisha ndiyo sehemu kubwa ya siri ya ndoa bora, na ulei bora! Ndoa ni kati ya mwanamume na mke, na siyo mambo yalikuja siku hizi. Usiwe na wachumba wengi na kila mtu unamwahidi utamwoa au utaolewa naye.

Niliishi katika kanisa fulani ambalo mwanamume mmoja mlei na kiongozi wa kundi, alikuwa anabadilisha wachumba, kila mara kwa miaka ishirini. Hii ni aina ya uzinzi. Unamwahidi mtu utamwoa unambwaga, kisha unachukua mwingine! Hii haina maana kwamba uoe hata asiyefaa, ila uwe na marafiki wa kawaida, na kati ya hao chagua mmoja, unaposema uchumba umefika mbali, japo kama mambo yameharibika, usisite kufuta uchumba. Bora kukatisha uchumba kuliko kukatisha ndoa. Endapo umetoa ahadi kinyume cha maandiko matakafitu, kwa hali iwayo yote itangue bila kuchelewa, tubu kwa kupumbazika kwako, ambapo kulikufanya uharakishe kutoa kiapo ili usimdharau Muumba wako.

Ndoa isifanye haraka, maombi yawe mazito, usitoroshe mke, huo ni wizi. Mwenzi mtarajiwa awe mtu wa kiroho, na usiwe na mazoea ya kukutana na mchumba kisirisiri, shetani ni stadi wa kutengeneza mitego. Kama umefanya uchumba na mtu ambaye huelewi tabia yake vyema usidhani uchumba unalazimika kutoa kiapo cha ndoa. Usiunganishwe na mtu ambaye haumpendi au kumheshimu, ni dhambi.

Napenda kusema walei epukeni uongo katika kutambulisha watu. Mlei mmoja aliniiambia kwamba mhubiri mwenzake alimtafutia mchumba, akasema kwamba ni mtu mwema. Ila mchumba huyu alikuwa ameshaolewa pengine, alikuwa hajaachika na pia alikuwa na mtoto. Watenda kazi wengine wa Mungu wanapenda kusema uongo wa tabia za ndugu zao ili waolewe au kuoa, eti wakipata mtu mwema watabadilika tabia yao mbaya. Katika usichana wangu, nilikutana na wazee wa makanisa au wahubiri wakija kuposa kwa wazazi wangu kwamba niolewe na watoto wao. Wengine watoto wao walikuwa walevi, na waliacha imani, ila hawa hawakuona kwamba wanamfanyia vibaya mwingine, waliona ni sawa kabisa kwamba ndugu yao atapata mkristo. Mtu akikuuliza tabia ya mtu ambaye unapeleleza kuoa, kama hutaki kusema mabaya mwambie apeleleze, usiseme uongo.

Rafiki yangu mhubiri toka Kenya alisema, “Mimi nikijua hata kama mtu ni mwizi, mwasherati na mtu mbaya sana siwezi kumwambia mtu, maana watu watanichukia. Nilimwuliza na kama mtu huyu anaenda kuoa binti yako pia uungependa ufichwe? Alisema hilo ni tofauti. Saidieni wale wanaotaka mashauri ili wawe na ndoa bora, ila kuna wale wanaokataa. Mlei mmoja rafiki yangu aliambiwa kwamba mke anayetaka kuona ni bomu, yeye alimjibu hata mchungaji wake, “Mimi ni mtu mzima na ni mimi nitakaa naye, pilipili usiyoila yakuwashiani?” Walipooana, mke alimpiga na hata kumfukuza nyumbani alale nje, hata wakati ambapo jamaa zake walikuwepo, ilikuwa jambo la huzuni sana.

Ni jambo linalojulikana kwamba kutambulisha watu ni riski, ila kama binadamu sijui tunawezaje kuliepuka. Baba yangu nakumbuka, alifanya kazi na binti mwema sana na akamtambulisha kwa jamaa ya upande wa mama aliyekunywa pombe. Baadaye yule binti alipata ukimwi na akaambukiza nyumbani! Niilimsikia baba akisikitika, kwamba yule msichana alikuwa mtu mwema na alijuta, kwa nini alifanya kitendo cha kuwatambulisha. Sisi si malaika, mara nyingi hatujui tabia ya mtu ila tukijua, tusione mtu anaingia kwenye huzuni na sisi tunanyamaza kimya. Ni vizuri kama unashauri watu mambo ya ndoa uongee nao uso kwa uso. Kwani mawasiliano ya 58% yako usoni, na sauti na mengineyo. Yale maneno yana uzito kidogo, pengine pungufu ya 10%. Nashauri kila mtu anayefunga ndoa aende kuona mshauri wa ndoa. Na kusoma vitabu vya ndoa, hasa siku hizi ambapo jamii hazina msaada sana kwa ajili ya umbali au kupasuka. Ile amri ya kumpenda jirani yako kama nafsi ni jambo zito kuliko tunavyofikiri.

Kuna mambo kadhaa yanayoathiri ndoa. Mambo haya ni kama: Jinsia yake , imani yake, umri wale, kabila au taifa, elimu aliyonanyo, dini, kazi yake na cheo chake, masaa anayofanya, kipato chake kwa mwaka, ni mtoto wa ngapi kwenye familia kati ya watoto wangapi, anataka muwe na watoto wangapi? Je, anataka mpate watoto baada ya muda gani baada ya kufunga ndoa? Anaishi mjini au mashambani? Anaishi mwenyewe au na wengine; mmefahamiana kwa muda gani na uchumba utachukua muda gani, kabla ya kufunga ndoa? Je, marafiki zake wanafikiriaje kuhusu nyinyi kufunga ndoa? Je, ana

mtoto? Je, ni mjamzito? Je, ana rafiki mwingine wa kiumekike? Kama ni mvulana, Je, ameshawahi kuolewa au kuoa kabla? Je, wazazi wake bado wameaoana au wameachika? Je, amekuzwa na nani, kma hana wazazi?

Nitajadili machache kati ya haya, mfano: Umri, ni muhimu kwa sababu watu wengi siku hizi hawakai na jamii na hivyo kusaidiwa mawazo ya kuishi katika ndoa, ni vizuri wawe na zaidi ya miaka ya ishirini kwa mke na zaidi ya ishirini na mitatu kwa mume. Kuwa mtoto wa ngapi kuzaliwa yasemekana inaathiri tabia za watu, mfano, mtoto wa kwanza apenda kushika sheria na kuwa kiongozi na anakuwa kama mtu mzima mapema.

Walipokuwa wanaangalia maraisi wa Marekani walikuta kwamba wote ni watoto wa kwanza kuzaliwa isipokuwa Nixon, naye ni kama alikuwa mtoto wa kwanza, kwani kaka yake mkubwa alizaliwa na utindio wa ubongo na hivyo alikuwa hakuweza kutembea, kujilisha au kufanya shughuli za kawaida. Mtoto wa pili apenda kuwa na mahusiano mazuri ya jamii na watu ila si mtunzaji mzuri wa pesa, na wa tatu apenda biashara, diplomasia, futuhi na kutegemea mwengine kama ndiyo wa mwisho. Napenda kusema haya mambo si 100%, ila yanapita asilimia 75% na huo ni ushahidi tosha. Kuna wakati ambapo watoto wamepishana sana na kufanya hata watoto wa mwisho wawe kama watoto wa kwanza n.k

Jinsia; mfano wanawake, wanatumia maneno elfu arobaini kwa siku wakati wanaume wanatumia maneno elfu ishirini. Yaani mume akija nyumbani amemaliza maneno yake na mama ndiyo anaanza. Mawasiliano ni muhimu, kabla ya kuoa wapenda kumsikiliza mchumba akikueleza hisia zake, na jinsi anavyofikiria mambo. Je, utaendelea hivyo kwenye ndoa? Mfano, ukienda kumtembelea mama ambaye amejifungua na mchungaji wako, ukirudi, mke aweza kukuuliza, Je, mtoto alikuwa ana uzito gani? Ni msichana au mvulana, ana urefu gani, alizaliwa saa ngapi? Uchungu ulikuwa wa masaa mangapi? Utajikuta wewe kama mwanamume hukuuliza hata kama ni mtoto wa jinsia gani; na kuona hayo yote si ya muhimu. Kwa wanawake haya ni muhimu, hivyo kila mmoja wenu ajifunze kumfurahisha mwingine kwa yale anayoona ya thamani kwake kwa jinsi inavyowezekana.

Kuaminiana ni muhimu tukitaka ndoa zetu ziwe bora, Mshauri Migombo alitusimulia kisa cha mke aliyekuwa kila mara anamshuku mumewe. Siku moja alipokuwa anarudi nyumbani mama aliyefanya naye kazi alimwomba ‘lift’. Kesho yake alipokuwa kwenye gari na mke wake, mke wake alikiona kiatu kimoja tu, naye akafikiria ni cha Yule mwanamke aliyempa lift jana yake. Akaogopa hili litazusha ugomvi na mke wake ambaye hakumwamini. Basi alipoona mke wake hatazami alikitupa kile kiatu gari likiendelea. Walipofika kule walipokuwa wakienda, mke alitoka kwenye gari na kuanza kutafuta tafuta kitu. Mume wake alipomwuliza anatafuta nini, alisema “kiatu changu, nimekipata kiatu changu kimoja tu, sijui kingine kimeenda wapi”. Mume huyu alishindwa kusema

kilichotokea, kwa kujua kwamba atawasha moto mkubwa. Hebu wanaume na wake tuwe watu wa kuaminiana na upendo ambao Mungu anatasa tuwe nao.

Napenda kusema kwamba si kila mtu anayeoa au kuolewa. Wengine wana karama ya useja. Na hilo lieleweke, kama hawajihusishi na mambo ya uzinzi, na wamejiweka wakfu kuhudumia Watu na Mungu, au wamezaliwa vile. Hawa wasifikiri kwamba ni lazima wafunge ndoa, watawapa wenzi wao shida bure maana hata wengine wana woga wa kujitegemea au kutokomaa. Hebu wasifanye kosa la kuingia katika ndoa takatifu. Jaribu kuangalia wale wote kwenye Neno la Mungu waliokuwa waseja kama Daniel, Paulo n.k.

Mzazi ana nafasi kubwa ya kushauri wachumba au wale wanaopanga kuoana, hebu na aombee hili na kuwa mwangalifu sana. Ni dhambi kutosema kweli unaposhauri. Tafuta muda w kushaauri, na usome vitabu ili kutafuta maarifa kusaidia watu kuwa na ndoa bora. Naambatanisha kwa lugha ya kingereza mambo kujadili kwa wachumba, wale wenye ndoa changa. Wazazi au jamaa kupata mashauri, na wewe kama mzazi unawajua kuliko wale wasiowaona uso kwa uso. Mara zingine jamaa wa karibu wanatoa ushauri pia, lakini kama hawamjali Mungu, wewe kama mzazi mcha Mungu, ndiye utakayewasaidia kuliko mwingine. Ni muhimu ukizungumza nao uso kwa uso, maana kwenye simu humwoni mtu uso wake na ni vigumu kujua mengi kama huoni uso wa mtu! Mawasiliano karibu yote yanapatikana kwenye uso wa mtu, sauti na majibu ya uso kwa uso. Hebu mtakie mema mwenzako (goodwill, best intentions)).

SURA ya 26

BURUDANI, MICHEZO NA MARAFIKI (SOCIAL LIFE).

Ratiba ni muhimu katika mambo, ya kazi na hata yale ya burudani tuyaweke ratiba na tuifuate. Hakuna mtu ambaye ni kisiwa. Tunaishi katika jamii. Je, watoto wetu washiriki burudani gani? Burudani ni mambo ya nje ya moyo. Moyo ndiyo ufanyiwe kazi kwanza, ili mambo ya nje kama vile burudani au kuvaa yabadilike. Usifanye kazi na mtoto wako ukianzia nje, anza ndani, ndiyo shina. Tunaishi wakati wa masherehe kila mahali. Hata watu wengi wanachelewesha arusi kwa sababu wanahitaji pesa nyingi za maonyesho ya arusi kwa vile kuna sherehe hata tatu kwenye ndoa moja!

Mara nyingi marafiki zetu ndiyo wanaweka rula ya maisha yetu ya jamii. Hata sisi watu wazima tunaathirika kwa wema au ubaya na mahusiano na watu sembuse watoto? Mahusiano yetu yaweza kuwa mbaraka au laana. Watu husema, “Niambie marafiki zako nami nitakuambia wewe ni u mtu gani.” Vilevile, “Ndege wanaofanana huruka pamoja.” Usifikiri wewe ni jiwe hautabadilishwa kabisa na marafiki zako. Moyo wa binadamu una tabia ya kuvutwa na sumaku ya tabia potofu kuliko njema, “Ole wangu ni nani atakayeniokoa na mwili huu, lile jema nalotaka kutenda...”.

Jitahidi kutojihusisha na wale wapendao anasa kama, mavazi, televisheni na picha potofu, pombe, dansi. Wale wapendao anasa mara nyingi ni vigumu kupenda yale mema ya kuboresha maisha au ya kumwabudu Mungu. Wakati huo huo haupaswi kuwa peke yako ukijitenga! Ila gundua kwamba kila uhusiano hata mdogo una mvuto fulani, ukitegemeana mwelekeo au upendo wako, na muda unaotumia. Tusijiweke kwenye majaribu ambayo tunashindwa kutoka. Vijana wanashawishika kuliko watoto kwa maisha haya na yale ya milele. Ulimwengu usituwekee viwango, bali sisi tuwekee ulimwengu viwango. Tunaona Samson kijana mwenye nguvu alilelewa vizuri nyumbani, akawa na maadili, akili ila alishindwa kustahimili majaribu aliweza kuua simba ila akashindwa na msichana asiye na nguvu. Hii ni kwa sababu ya mivuto ya mazoea ya marafiki na jumuiya aliyokuwa anaishi. Waweza usione hatari na kufikiri ukipata kishawishi utashinda kwa maksi nyingi ukajishangaa umepigwa daflau.

Ikiwa mazungumzo ya watoto yatakuwa kwa mambo yanayoendelea kama vile picha mpya za mikanda, vyakula vya kuhafifisha mwili, mizaha na futuhi yatafanya yale mambo ya wakfu yaonekane ya kawaida. Kama tukiwa watu ambao tunashirikiana na Mungu ili kutunza watoto wetu, atatusaidia hata katika mazingira magumu. Watoto wengi wanaingia kwenye tabia potofu kwa ajii ya kuchekwa na wenzao, “Wewe si mwanamume, onja kidogo, glasi moja ya pombe inakubabaisha!” Au, “Hata huna girlfriend umepitwa na wakati.” Epuka TBS ndogo (viwango) na maadili machafu.

Jina jema ni bora kuliko dhahabu, baadaye utapata furaha kwa kushinda tabia potofu. Epuka kujihusisha na jamaa wenye maadili potofu. mara zingine tunakimbia watu wa mbali wenye maadili potofu ila tunakaribisha jamaa na wanaharibu watoto wetu. Hebu tuchukue muda kuchuja burudani na michezo yetu, si mambo yatukute tu na tuendane nayo kwa vile kila mtu anafanya. Tujiepushe michezo ya ushindani na roho za kuona wengine wanashindwa nasi tunawaona kwamba ni mabwege au watu wasio na thamani.

Nilipokiwa mdogo wa umri wa miaka sita, bwana mmoja wa miaka kama ishirini na miwili alitembelea nyumbani mara nyingi, akapewa bia kunywa. Mama alisema “Huyu ni wa kwetu, ni mjomba wako.” Kitu cha kustaajabisha ni kwamba, siku moja mama akiwa kazini na msaidizi wa kazi yupo jikoni, Huyu kijana alikuja karibu yangu akiwa ametoa nguo zake na uume wake unaonekana akajaribu kunishika mkono. Nilikuwa gizani kabisa kuhusu tendo hili, lakini ile tu mtu mzima kutokuwa na nguo ilifanya nipige kelele, “Nitamwambia mama!” Akakimbia akatoka ndani ya nyumba.

Msisitize mtoto akueleze tabia na mambo yanayoendelea akiwa kwa marafiki, hasa unaowashuku. Wazazi wawe na nafasi ya kuchagua marafiki wa watoto usiache mtoto akaendelea tu mwenyewe katika urafiki bila kujua mwenzake ni wa aina gani. Ujue mtoto wako ameenda wapi na kwa muda gani? Anapaswa awe nyumbani. Katika nchi nyingine mtoto hatoki kwao labda akiwa shuleni na shughuli nyingine maalum. Usifikiri mtoto akianza kutembea amekuwa huru kufanya chochote, huo ndiyo wakati mbaya. Mtoto atembea akiwa na mwaka, ila kujenga maadili ni maisha yote! Kutii iwe mazoea ya mtoto, hakuna ambaye hataharibikiwa kwa kuenda katika company mbaya.

Mzazi asiache mtoto ajichagulie burudani anayotaka. Wafundishe watoto wako kuthamini ushauri unaowapa katika hili. Watoto wafundishwe jinsi vishawishi vinavyokuja na jinsi ya kuviepa. Mtoto asiangalie runinga siku nzima, mwili unanyong'onyea na kupozesha mawazo. Mtoto afundishwe kuona matokeo mabaya kwenye vitu vingine na akubali adhabu za machaguzi mapotofu. We have heaven to win and hell to shun.

Masherehe na starehe ndiyo shida nyingine ambayo ni ya kuangalia ili watoto wetu wasiingie katika mambo mapotofu. Watoto wameingia kwenye pombe, kuvuta sigara, maneno machafu kwenye masherehe. Sherehe ni siku nzuri ya kutoa shukurani kwa muumba mfano, siku ya kuzaliwa, si siku ya mtoto kuwa kama mheshiwa, akijifikiria siku nzima kana kwamba ana haki ya kufika umri huo au alifanyia kazi fulani, akafuzu kutunukiwa sherehe hiyo. Uwe wakati wa kushukuru kufikia mwaka mwingine na kuweza kupata nguo, mavazi , malazi na baraka ya wazazi. Uwe wakati wa mtoto kutoa sadaka ya shukurani kwa yale ambayo amewezeshwa kuyafanya. Ni wakati wa mjadala wa mwaka uliopita kama umekuwa mbaraka na jinsi ya kutembea katika njia bora mwaka mwingine.

Wakati mwingine hata sikukuu za dini tumefanya mambo mapotofu hata utashangaa kama kweli ni siku kuu ya dini! Kama sherehe ya krismasi, watu wamefanya upotofu wa kushangaza kama ulevi kwa wakati huu, ambao eti ulimwengu ungemkumbuka Muumba wao, aliyezaliwa kama mtoto ili atukomboe.

Mtoto mmoja alimuuliza baba yake wakati wa krismas, "Baba, mbona watu wanaandika Chirstmas kwa kifupi kama Xmass?" Baba alipokosa jibu, mtoto akaendelea, "Labda ni kwa sababu wamemkata Yesu kutoka katika Chirstmas, baba, si kweli baba?" Baba kwa kutojua la kusema, alijibu, "Labda mwanangu, labda." Hebu wakati wa sherehe za dini, usiwe wa kunywa, na kujionyesha kwa mavazi na vitu. Kama kuna wakati wa kuutafakari ukuu wa MUNGU na kusaidia wenye mahitaji ni wakati huu.

Siku ya mwaka mpya wengi wamepoteza maisha na kuugua, au kupata ajali kwa kuendesha magari wakiwa walevi. Je, ni jambo jema wewe kukaa ukingoja mwaka mpya na kutawanya mali kwa ulevi au kuchuja yaliyopita? Hebu kula kuwe kwa kiasi. Nimeona watu wakila mpaka wakitupa chakula kwa sababu ni sherehe! Vyakula vinapikwa vingi na vinywaji mpaka matumbo yataka kupasuka! Hapa kwetu Afrika na umasikini wetu twapaswa kuona kwamba kumwaga chakula si mbaraka. Kama una kingi, gawia maskini, wapo wengi sana. Itakuwa umewabariki pia. Hata wengine waenda kutapika na kurudi kula tena! Je, hii ni sherehe itakayojenga watoto wetu au kubomoa wakifikia uamuzi au umri wa kufanya sherehe? Sikatii, furaha ni muhimu ila isipite mpaka ikawa si baraka tena.

Burudani ni muhimu na kuchukua likizo kufurahia michezo au utalii. Tafuta burudani zitakazojenga tabia za watoto, yabidi uzipange vizuri kabla ya kuchuka likizo. Burudani zile zitakazokuchosha sana epukana nazo, maana yabidi urudi ukiwa freshi na siyo kuwa na uchovu mwingi kiasi kwamba kazi yako ya kulea na vitu vingine vikawa mzigo badala ya furaha.

Sura ya 27
MAGONJWA YALETWAYO NA FASHENI
(urembo kwa watoto wa kike).

Yaonekana watu wengi na hasa watoto wa kike tuna shida ya mambo ya fasheni. Shida hizi ni za toka zamani sana. Viatu, mavazi, mapambo ya mwili. Nitajaribu kuweka mifano kwenye neno la Mungu inayozungumza kuhusu mapambo. Kwa vile kitabu hiki kinazungumzia afya ya kimwili, kiroho, na kijamii, nitaanza na maandiko ya zamani sana ya kiroho, kuonyesha hivi vitu si vigeni. Fasheni ni pamoja na kutumia vitu visivyofaa vikiwemo vileo, Hebu chochote kilicho kileo kisiingie kwenye vinywa vya watoto wetu na wasione mifano mibaya kutoka kwetu.
“Bwana Akasema tena, kwa sababu binti za Sayuni wana kiburi, na kuenenda kwa shingo zilizonyoshwa, na macho ya kutamani, wakienenda kwa hatua za madaha, na kuliza njuga kwa miguu yao.” Sura hii imeonyesha vitu vingi vya mapambo tuliyonayo ni ya miaka zaidi ya miaka 2500 iliyopita! Mapambo kama vile, “Pete za masikio, vikuku, taji, dusumali, mafurungu, vitambi, vibweta vya marashi, matalasimu, pete, azama, mavazi ya sikukuu, vilemba, kitani nzuri, vioo vidogo, debwani, shali, vifuko, utaji, mishipi, nywele zilizosukwa, kisibau;” vilivumbuliwa zamani sana.

Viatu
Viatu vivaliwe kutokana na shughuli, usafiri na afya ya mtu. Viatu vinaweza kuwa vya michezo au shughuli maalum. Viatu vya wazi vina uzuri wa kupunguza fangas ila kuna kazi za hatari ambazo miguu inabidi ifunikwe ili isidondokewe na vitu. Wenye shida ya fangas au kunuka miguu, pengine kuloweka miguu kwenye magadi au siki yaweza kusaidia kiasi fulani. Kausha miguu isiwe na maji.

Kwa kawaida madisaina wa viatu ni wanaume. Wangeambiwa wavae viatu ambavyo wanawake wanavaa wasingeweza hata kwa saa moja! Ila wanawake tunatembea na viatu vyenye visigino virefu siku nzima! Na hata kama vinatuumiza tunajikaza. Wengine siku

hizi naona wanatembea na mfuko wa malapa, wakifika mahali wanabadilisha na kuendelea na shughuli zao. Viatu vingine vina visigino vya zaidi ya sentimeta kumi na mbili na chini ya vidole sentimeta mbili. Nafikiri katika muundo huu disaina anataka mwili wa mwanamke uweze kutoa picha (pozi) hii.

Kwanza, mguu uonekane mfupi. Mahali pengine uzuri wa mwanamke ni kuwa na miguu midogo. Kuna mtu aliandika kwamba, watoto wa kike katika nchi ya China, wamekatwa miguu au kuvalishwa viatu vidogo ili ili mguu usiendelee kukua, la sivyo hataolewa!
Pili, matako yaweze kutingishika na kutokezea. Tatu, kisigino (ankle) kitingishike ili mtu abaunsi, na kifua kitokezee mbele. Daktari wa miguu Alan Kalker wa Marekani alisema "Kama unachagua viatu vyako kufurahisha macho badala ya miguu, jitayarishe kupokea madhara ya kiafya."

Viatu visivyochaguliwa kwa kujali afya vinaleta shida ya kubadili umbile la vidole vikubwa (deformity),
Vinaleta vidonda na infection, vifanya misuli kuathirika na kuwa mifupi na kuonekana kama kiazi nyuma ya mguu (contracture of calf muscle), vinaleta baridi yabisi kwenye magoti, shida ya mgongo na miguu kupata maumivu, ajali za kuanguka au kuvunjika na kucha za vidole kuingia kwenye nyama.

Utafiti Marekani ulionyeshakwamba asilimia tisini ya wanawake huvaa viatu vya saizi ndogo kuliko wanayopaswa. Pima miguu yako vizuri kabla ya kununua kiatu. Nunua viatu wakati wa jioni wakati miguu yako inakuwa mikubwa kuliko asubuhi, na kama unavaa stocking au soksi, basi ziendane na viatu ili zisikuumize. Tumia pesa kununua viatu vizuri na imanai, stable, comfortale na vyepesi ambavyo vitafanya miguu ipumue vizuri.

Tunza miguu isipasuke pasuke, weka mafuta, miguu iliyopasuka inaingiza bakteria na yaweza kuchana matandiko. Kula vyakula vya asili vya mboga na matunda kupunguza mipasuko. Vaa viatu, na safisha vizuri maana udongo mwingine ni rahisi kupasua miguu. Usisimame muda mrefu, na punguza uzito kuisaidia miguu yako. Ni bora kutembea muda mrefu kuliko kusimama muda mrefu! Tunza miguu yako vizuri inalinda afya yako na kama una kisukari, angalia kama una mkwaruzo hata mdogo maana vidonda vingi haviponi haraka, ukiwa na ugonjwa wa kisukari.

Nguo
Nguo ina uhusiano mkubwa na afya, iwe kujilinda na hali ya hewa, mazingira, sare, kazi au uchafu. Nguo zimekuwa tatizo la miaka mingi toka pale Adam alipojitengenezea mwenyewe kutoka kwenye majani ya mkuyu nguo ambazo hazikufaa wala kumstiri na mke wake mpaka Mungu akawatengenezea kutoka kwenye ngozi ya kondoo.

Lengo la mavazi ya kwanza ilikuwa ni kuficha uchi, ili tusipate aibu. Kila mtu ana utupu au uchi, na uchi si wa kuonyesha kwa watu upitapo barabarani. Kila mtu anao

utupu. Ni aibu kwako kuonyesha uchi kisaikologia na sababu nyingine. Lazima tujiulize tunapovaa, Je, mavazi yetu yanatusaidia kiafya? Yanatusitiri, yanatusaidia kijamii, kiroho, kiuchumi au kimawazo. Waweza kufikiri ni jambo dogo ila mambo ya fasheni yameumiza wengi.

"Tazama naja kama mwivi, heri yule akeshaye na kuyatunza mavasi yake, asiende uchi hata watu wakaiona aibu yake;" Ufunuo 16:15. hata wanaume wanapaswa kuvaa mavazi ya heshima, wasiache suruali zinadondoka. "Kisha utafanya kanzu kwa ajili ya wana wa Haruni...nawe wafanyie suruali za nguo ya kitani, ili kufunika tupu ya miili yao; suruali hizo zitafika tangu kiunoni hata mapajani.. nao watazivaa watakapoingia hema ya kukutania ... wasije wakachukua uovu, wakafa; hii itakuwa amri ya milele kwake yeye na wazao wake. Kutoka 28: 42,43.

Nchi za magharibi wana sehemu za juimiya, ambako watu wanaenda bila nguo kuogoelea au kwenye hoteli maalum, zingine wanaenda na watoto wao. Nilitembea nchi fulani za ulaya, na kukuta watu hawavai nguo wakiwa ndani ya nyumba zao na ukipiga hodi, wakikuona kwamba wewe si wa pale, wanakimbia kuvaa nguo zao! Nikiwa na rafiki yangu tulimwona mama fulani anafagia mbele ya nyumba yake bila nguo hata moja ila alikuwa na viatu. Tukamwona Bwana mwingine anatengeneza bustani bila nguo. Alipotuona alipiga mbio, na rafiki yangu akamwambia, "Baba kama ulitaka watu wakuone, mbona unakimbia?" Alienda kuvaa akatoka nje tena. Hawa wote walikuwa watu wazima wa miaka arobaini.

Je, umeona ndugu msomaji, hakuna asiyejua kwamba kukaa uchi ni shida? Nafikiri wewe hutapenda kujitembeza uchi au nusu uchi bila sababu, hasa ukiwa mwanamke utajiingiza kwenye matatizo ya kubakwa, kutokubaliwa na mengine. Utashangaa japo unakula chakula cha afya ila hujali mambo mengine ya binadamu utaharibikiwa.

Ni vizuri nguo za wanawake ziwe tofauti na wanaume. Wataalamu wa maandiko ya zamani wanasema kwamba wote walivaa kanzu za heshima na kaptura ndani, ila rangi zilitofautiana. Watu wengi wanasema wavae tu kama jinsia yoyote kwani wanawake na wanaume ni sawa isipokuwa viungo vya uzazi. Ni kweli wanawake na wanaume ni sawa mbele za Mungu ila kuna tofauti ya maumbile na shuguli kutokana na uumbaji. Sasa wewe kama unataka kuleta hili kwenye ndoa yako utaiharibu. Mwanamume ana sehemu yake na mwanamke pia. Ndoa nyingi zimeharibika kwa mashindano. Mheshimu mume wako, naye anatakiwa akupende. Ndoa isiyo na huzuni inaleta furaha na afya. Kama hujagundua jaribu kuangalia watu unaowajua. Mavazi yaonekana kuwa na sehemu kubwa katika maisha ya binadamu na hata katika ibada ya kweli.

Tunaona wanawake wawili wamewekwa kama mifano ya ibada ya kweli ya Mungu na ya adui. Ufunuo 12 na 17 yaelezea kidogo. Si heshima kuvaa nguo yenye maandiko ya kukashifu watu au kukaribisha ugeni usiofaa; kama "I am available." Watu wanakusoma akili yako kirahisi kwa mavazi yako na kukuweka kundi fulani. Najua twanunua mitumba au kuvaa kanga mara zingine bila kusoma. Nimeona mabinti wana T-sheti zilizoandikwa

“Unakaribishwa uende nami nyumbani!” Je, wewe unatafsirije haya maneno? Na mwanaume yeyote akimfuata, msichana atakataaje, ilhali nguo yake yazungumza?

Nguo zisizo na afya ni zile fupi, zinaoonyesha sehemu za mwili kama kifua, mapaja, mgongo, zenye mikato mikubwa au zimebana mno. Nguo hizi zingine ni nzito upande mmoja, zinafagia barabara, zinaacha miguu isikie baridi. Kuna magonjwa mengi yaletwayo na fasheni za nguo zisizoendana na afya. Watu wengi wanauwawa kwa fasheni kuliko unavyofikiri. Mifano ya magonjwa ni kama vile: mapafu kubanwa, mishipa ya fahamu na ya damu kubanwa, vichwa kuuma (damu pungufu ubongoni), myeyusho wa chakula kuathiriwa, damu kutoka puani n.k. Na kwa waumini wanaotaka kuwa na afya ya kiroho, “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha zini naye moyoni.” Kila mtu ana jukumu la kutunza afya yake ya kiroho ila unapovaa nguo na kuwakwaza wengine pia kuna shida. Wanaume wanavutiwa na vitu vya kutazama kwa jinsia nyingine na wanawake wanavutiwa na kujali au upendo wa jinsia ya wanaume. Usivae nguo bila kujali watu, na hata kama ni wanawake wenzako kwa nini ujiabishe? Nguo inakuletea sifa fulani; nzuri au mbaya.

Kwa kifupi kwanini sisi na watoto wetu tuvae nguo za kufunika utupu? Kwasababu Mungu amesema. Tulipoingia dhambini na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Hatukupendeza kutembea na utupu. Mungu akamchinja mwanakondoo ili amvike mtu aliyejivika vijani vichache vya mikuyu.

Kuvaa vizuri (modest) hakuanzi na nguo, bali moyo. “Mwanangu nipe moyo wako”. Mtu anayepata maarifa na kumpenda Mungu hawezi kuvaa ovyo ovyo. Hapa wazazi yabidi tuwe makini mtoto akiwa mdogo avishwe kwa adabu na si kubadilisha jinsi ya kuvaa akipevuka. Hii itamzoesha mtoto. Mtoto aliyelazimishwa na mama yake, kukaa chini kwa mara kadhaa alisema “nakaa ila moyoni nimesimama”. Tuombe Mungu awasaidie watoto wetu na sisi wenyewe tumpe mioyo yetu na mengine yatafuatia.

Zamani polisi walipasua nguo za watu wajionyeshe vitu vyote, au wengine walipima nguo kwa rula zifike hapa au pale, haya hayakusaidia bali kwa muda tu. Mungua tupe hekima maana tukienda kununua nguo na watoto wetu ni changamoto, hawataki hii au ile, na mara zingine wanatembea na nguo na wanapoenda wanabadilisha kisha watu njiani wanashangaa. Wengine hufikiri suruali kwa msichana si nguo ya adabu bali gauni, ila wasichana wengine huvaa suruali na blauzi inayofunika vizuri tu. Hii inakuwa na adabu kuliko magauni ya namna fulani, Dini zingine zinafaa kuigwa mfano kwa kuvaa nguo za adabu. Kwa kila kitu hata kwa nguo za adabu tuwe na kiasi, ili tusipitilize tukawa watu wa sheria (legalistic) na kukwaza wengine. Twende taratibu na kwa hekima tusipoteze roho za thamani (precious souls)

Vijana wengi wanavaa tu kwa kufuata mkumbo,(fasheni) afanane na rafiki zake au watu anaowaona kwenye televisheni. Wengine wanawaiga hata wazazi wao. Unaona kina mama walio na watoto wa kike wanavaa nguo za ajabu! Unatarajia binti huyo atavaaje? Make lazima aongezee au apunguze kidogo, ili asivae kama mama yake. Hebu tusivae kwa mkumbo, jamani. Huwa ninawaambia wanafunzi wangu kwamba, “Let everybody do it, you are not everybody.”

Kitu kingine ambacho nimekiona ni kwamba fasheni yanapunguza unyenyekevu. Nimeoa watu kwenye nyumba za ibada hasa makanisani maana misikitini wanawake wanavaa kwa heshima sana. Wanawake wakiingia na vinguo vya ajabu kuabudu na viatu vya michuchumio vya makelele ili watu waone fasheni zao na kujitembeza hapa na pale bila sababu. Kama una jaribu la kujionyesha anza kuchagua mavazi machache tu ya adabu utumie kwenye nyumba ya ibada. Ibada si mahali pa mashindano, kujionyesha na kujifikiria wewe; ni mahali pa mawazo yetu kuelekea kwa Mungu na si kwako au kwangu. Tutakuwa tumepoteza lengo la kuabudu au kwenda ibadani.

Nywele

Zamani hatukuwa na shida sana ya nywele ila siku hizi watu wa nchi zingine wametuletea fasheni nyingi za nywele. Masaluni mengi yana mivuke ya kemikali za nywele na yana madirisha madogo ya kutoa uchafuzi huu wa hewa. Madawa kama ammonia, sodiumu hydroxide, PPD na formaldehyde yanayotumika ni sumu zinazojulikana. Chunguza zaidi kwenye website madhara ya madawa haya. Kwa mawazo yangu usafi na unadhifu ni muhimu, ila kujionyesha ni jaribu letu binadamu wote.

Kila kitu kifanyike kwa kiasi. Tunaona Yezebel “Akapata habari, katika wanja wake machoni mwake, akapamba kichwa chake akichugulia dirishani.” Huyu mama namtaja kwa vile japo “Alijishugulisha kupamba mwili hakushugulisha kupamba roho.” Sitasema mafungu mengi maana haya ni mambo ambayo huwezi kumwambia mtu sana, na hayana mstari kamili, ila mtu anapoendelea na safari ya kumcha Mungu na kuishi maisha ya kiasi na utauwa anagundua vya kuacha na vya kuendelea navyo. Kila mtu yuko steji tofauti.

Mtu wa Mungu anashauri: “Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kwa kusuka nywele na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi, bali uwe utu wa moyoni usioonekana katika mapambo yasiyoharibika; yaani roho ya upole na utulivu, iliyo na thamani kuu mbele za Mungu.” Nafikiri fungu hili la Petro tatu liliandikwa baada ya kuonekana kwamba tunajaribiwa mara nyingi na kujionyesha na vitu vya nje. Kuna kujipamba ambako kunapita kipimo. Dada mmoja alimwambia, “Hivi Bwana Atakapokuja kutoa thawabu siku ya mwisho atakuwekea taji wapi? Umeshajipamba kiasi cha kutosha! Una shanga, na vitu vingi tayari kichwani!” Nafikiri hii ilikuwa ni futuhi, ila ilinifanya nifikiri, kweli tunapoteza muda mwingi kwenye kujipamba badala ya kujali maisha yetu ya kiroho. Je, masaa yale tunayoshugulikia vioo na nywele ndiyo tunayoshugulika kumtafuta Mungu kwa kusoma neno lake, ibadani na sala?

Wigi nyingi zimetengenezwa na mikia ya farasi, plastik, na nywele za watu wengine. Na hizi zinaleta joto miilini mwetu na uzito kichwani mwetu. Pia zinafanya usafi wa nywele kupungua. Vyanuo au kofia za moto zina madhara kwenye kichwa, na hasa wakiweka kemikali kwenye utosi. Watu wengi wamepoteza nywele. Spray za nywele pia zinaathiri mapafu. Mambo ya kujipamba nywele yamekuwa maelfu ya miaka, na kweli nywele ni utukufu wa mwanamke na kuleta uzuri, mwanamke usijiachie ukatisha ila tuwe na kiasi. Yale ya muhimu tushugulikie kwanza. Nywele zisafishwe mara kwa mara ni jambo jema. Watu wengi wanakaa mwezi au zaidi, bila kusafisha nywele na zimefunikwa na wigi; hiki ni kitu cha madhara.

Tumia chanuo chako mwenyewe na kama yabidi uazime hakikisha kimeosha na sabuni kujilinda na magonjwa ya ngozi au chawa. Nywele zisizotakiwa mwilini kama vile kwenye videvu vya wanawake, tumboni au pengine zikatwe na mkasi na sio kukwaruzwa na wembe. Nywele zahitaji protein ya Keratin hivyo lishe ni muhimu. Upungufu wa madini kama zinc au vichocheo vya mwili vyaweza kuathiri nywele.

Nywele ni pamoja na vinyweleo, nyusi, kope na mavuzi. Vinyweleo husaidia ngozi kutoa takataka za mwili na kusaidia mwili usiathiriwe na vumbi au jasho. Mavuzi yanasaidia usafi, kupunguza unyevunyevu, muwasho, kunuka n.k na hili linapunguza baktiria. Inashauriwa mtu asinyoe nywele hizi zote abaki upara kwa ajili ya shuguli inayofanywa nazo. Michubuko ya makali ya wembe au kemikali za kuondoa nywele inatoa mwanya kwa bacteria na virusi kupenya. Ngozi iliyoachwa wazi bila nywele hupata athari inapogusana na jasho lenye taka toka mwilini. Punguza nywele kwa mkasi ziwe fupi kadiri inavyowezekana. Uzioshe kila siku na kuzikausha ili usilete unyevunyevu na kisha fangas au baktiria.

Kope na nyusi huondoa vumbi na uchafu unatokana na kuganda kwa mafuta na vipodozi tunavyopakaa. Kukata nyusi si jambo jema ila zipangilie vizuri. Hata kwa wale wenye nyusi nyingi ukinyoa zinaota nyingi zaidi. ila ukiziacha zinaendelea vizuri. Zamani watu hawakukata nyusi na kila kitu kilikuwa sawa! Labda uwe na shida maalumu kubwa, ziache. Krimu za kuondoa nyusi nyingi ni mbaya kwa vile zina kemikali na kuleta mwasho au shida za macho.

Mvi mara nyingi huja baada ya miaka thelathini na mitano; ila urithi, vichocheo, kemikali, vileo, sigara, na vyakula vyenye asidi nyingi vyaweza kuleta mvi mapema. Wanawake wengi wakiwa watu wazima (menopause) na kuacha hedhi, wanaanza kuota ndevu. Hii ina changamoto ya kisaikologia. Akipata mvi akingali msichana mdogo, hali ni ngumu zaidi. Pengine ni vizuri apimwe vichocheo na kushauriwa. Mwanamke anapenda aonekane kama mwanamke bila ndevu, hivyo kama unataka kuzitoa tunashauri ukate kwa mkasi badala ya kunyoa.

Wasichana wadogo itabidi watafute ushauri zaidi wa matabibu kuhusu vichocheo hivi. Baadhi ya ndevu zinatokana na: Vichocheo kuzalishwa kwa vingi kwenye mfuko wa uzazi, uvimbe kwenye mfuko wa mayai, matumizi ya dawa za majira, matumizi ya vipodozi vyenye dawa za vichocheo vya wanaume (testosterone au steroid), uvimbe wa tezi la karibu na figo (adrenal), unene wa kupindukia unaleta vichocheo vya wanaume (androgen), matumizi ya dawa zenye kemikali kama vile Danazol au cyclosporin.

Chunusi nyingi zaweza kujitokeza, hata kwa watu wazima. Baadhi ya sababu ni: Kubadilika kwa mzunguko wa hedhi, ndevu nyingi, ugumba, kusinyaa kwa matiti au mfuko wa mimba, kuwa na sauti nzito au kunenepa kwa kisanduku cha sauti, kuvimba sehemu za uke (clitoris) kuota nywele mapajani, tumboni, kiufani, miguuni, mikononi, mgongoni na kwenye makalio.

Kucha

Rangi na kucha bandia zinaleta maambukizi ya kucha na kupoteza kucha, kupungukiwa na kucha vidoleni kuwa na vipele karibu na ngozi ya kucha. Mungu ametuumba kwa njia ya

ajabu, alijua kwa nini aliweka kila kiungo cha miili yetu, hata kiwe kidogo namna gani, kina kazi yake. Kwa nini tunamrekebisha Mungu? Hebu soma Zaburi 139:14. Kama Mungu angetaka kucha zetu ziwe nyekundu, bluu, kijani au rangi yo yote ile, si angetuumba nayo? Kama angetaka tuwe na mashimo mwilini, pia angeyatoboa Mwenyewe.

Rangi za midomo
Jiulize; Je, nahitaji marembo haya yote? Mara nyingi rangi hizi si nzuri kutumia kila siku, kwa afya, na zaondoa rangi ya asili kwenye ngozi (pigmentation)

Rangi za macho
Hizi huleta maambukizi (infection) ya jicho, ngozi, upofu, vinyweleo, kuwashwa, kansa ya ngozi, allergy, vipele, na kope kukatika.

Vipodozi (crème), losheni na shampoo
Zaleta macho kuwasha, ngozi kudhurika, muunguzo wa ngozi, rangi kubadilika, vidonda, damu kutoka, ngozi kuwa pana, kansa ya ngozi, kubugudhiwa na jua (sun sensitivity). Mara nyingi watengenezaji waandika ni vitu vya asili (natural). Haina maana kwamba vitu vya asili ni vizuri. Kuna mimea mingi ina sumu ya kuua, inadhuru au inalevya! Hata kama ina vitu vya asili inaweka kuwa na kemikali, baktiria, mbolea za viwandani, au dawa za kuua wadudu. Wakiandika hivyo, haina maana kwamba kitu cha asili ni 100% pure, salama na safi.

Watu wakitumia rangi za macho au mascara ya macho wanalowanisha brashi ya kope na mate na kuleta infection, wanalala na rangi na kuathiri macho, wanaziweka kwenye joto la zaidi ya nyuzi thelathini na mbili, wanafikisha machoni, na hizo rangi zinaingia kwenye macho. Wanaathiri kioo cha jicho (cornea), wanafanya kope zidondoke, wanaathiri kutoona vizuri na hata upofu.
“Ujapojivika mavazi mekundu, unapojipamba mapambo ya dhahabu, ujapojitia wanja machoni, unajifanya kuwa mzuri bure tu, wapenzi wako wanakudharau na kukutafuta roho yako.”

Mara nyingi vito na urembo vinahusishwa na uasi, uasherati, uzinzi, na kutongoza wanaume. Hivi naona kama havisaidii katika afya ya kiroho; basi tuwe na kiasi. Hii tabia pia inawahusisha wanaume pia maana kujipamba kwenye nia ya kupotosha wengine kumeingia jinsia zote.

Mapambo ya vito mara nyingi yalikuwa yanawatoa watu kwenye ibada ya kweli walipoanza kuabudu vile vito kama sanamu, au kujionyesha. “Bwana akamwambia Musa waambie wana wa Israel, ninyi ni watu wenye shingo ngumu; kama mimi nikiingia kati yenu kwa dakika moja nitawaangamiza; basi sasa vueni vyombo vyenu vya uzuri ili nipate kujua nitakalowatenda. Basi wana wa Israel wakavua vyombo vyao vyote vya uzuri tangu mlima wa Horebu (Sinai?) na mbele.” Yaonekana vito mwilini ilikuwa aina ya ibada, kwa mila nyingi. Twaona Yakobo akiambia familia yake, “Ondoeni miungu migeni iliyoko kwenu, mjisafishe mkabadili nguo zenu”.

Na mara nyingi katika historia ya wana wa Israeli, walipijitakasa kwa ibada maalum, au kwa kutubu, walitoa mapambo yote ya dhahabu na mengineyo, kwa nini ilibidi wafanye hivi? Mapambo ya mwili ya vito yanaleta madhara ya ngozi kama kuvimba kwa masikio (keloids).

Vipodozi

Matumizi ya vipodozi yana uhusiano na afya ya ngozi ya mtu. Ngozi hulinda mwili kwa mashambulizi ya baktiria na fangas, jua kali, kurekebisha joto, kutoa uchafu mwilini, kusaidia mawasiliano yasiyohitaji maneno, kutoa mafuta ya kusaidia mwili, kuzalisha vitamini D kwa kinga. Vipodozi vingi vya leo vinaathiri ngozi kama vina viambato vya sumu na dawa. Hivi vyaweza kuchubua ngozi, kucha hata nywele. Vipodozi vingi vina sumu ya hydroquinone na nyingine.

Ngozi huweza kupata mabaka, kukunjika na kutovutia. Vipodozi vingine vyafanya ngozi iwe nyembamba na kuchanika kirahisi au kupata shida kushoneka mtu anapopata kidonda kikubwa. Vipodozi vingine vinaleta allergy, pumu au kikohozi kwa harufu yake au chunusi kwenye mwili. Vipodozi vyenye vichocheo (hormones) vya wanawake vinaathiri vichocheo vya mtu na kusababisha mzunguko wa hedhi kwa wasichana uwe tofauti, au uwe na mabadiliko mengine mwilini.

Vipodozi vingine vinavyotumika kwenye kucha vyaweza kuwa na “Formaldehyde au toulene” na kuleta madhara. Afya ya ngozi na kucha hutegemea sana chakula bora, zaidi ya vipodozi. Madini kama ya chokaa, protini, vitamini A na B pia ni muhimu kwa uboreshaji wa ngozi na kucha.

Usafi wa kucha ni muhimu sana ili kusiwe na baktiria za kukuletea magonjwa. Nawa vizuri kwa sabuni, aloe vera au kitunguu saumu. Usikate kucha na meno, ukiwa na nail cutter waweza utumie. Tupa ya kucha ni msaada pia wa kufanya zisivunjike vunjike ovyo ovyo. Usikwangue vocha za simu na kucha, siyo afya. Kucha za miguuni zikiwa ngumu kukata, ziloweke kwanza, au zikate baada ya kuoga.

Je, umeridhika na jinsi Mungu alivyokuumba? Kuridhika ni jambo muhimu sana. Usijidhanie kama huna thamani mpaka ujiongezee mambo fulani. Nina imani kabisa kwamba kuna wengi ambao hawavai vito ila mavazi yao ni ya kujionyesha na ya ghali zaidi ya wale ambao wanavaa vito! Ila kitu kikubwa hapa ni kuwa na kiasi.

Vipodozi vya kuweka kwapani ili jasho lisinuke vyabidi kutiliwa makini kwa vile vinaathiri mitoki. Jaribu kupata vipodozi vya kuweka makwapani ambavyo havina sumu. Vingi vina alminiumu ambayo ni sumu, hivyo usipake. Kuna wengi wametengeneza vipodozi vyao wenyewe, kwa kutumia vitu vya asili. Bado ninapeleleza juu ya kipodozi cha kwapani kisicho na sumu.

Mama mmoja aliniambia kuwa shampoo ya kuoshea nywele zake, anachukua siki vijiko viwili na baking poda vijiko viwili na maji. Anasema inamsadia sana. Soma kwenye kopo, kama cream au mafuta ya nywele yana placenta, au vichocheo (hormones) za wanawake na uepuke.

Wanawake wa kmarekani weusi wametumia vitu hivi zaidi yetu, hivyo majaribio yao tuyasome. Yaliyoandikwa kuwa mfano ni: wengi walipoteza nywele wakifikia utu

uzima kwa permanent perm, kansa ya matiti iko karibu mara mbili kwao kuliko wanawake wa kizungu; kwa sababu ya kutumia mafuta ya kukuza nywele ambayo yana vichocheo vya kike (oestrogen).

Waweza kutengeneza mafuta yako mwenyewe, ukiwa na nia! Waweza hata kutengeneza sabuni zako mwenyewe. Sabuni nyingi za nje siku hizi zina allergy. Sabuni ya mkaa, iliyoitwa 'mbuni' zamani, ndiyo yenye afya kuliko sabuni nyingi! Nimepewa na watu sabuni za uso za kutoka uchina wanasema zinarembesha! Mara nyingi vitu vya nchi nyingine havina viwango sana na wanatuletea Afrika vitu ambavyo havijapitia viwango vya kuthibitishwa. Ila wanaogopa kuharibu soko na nchi za magharibi; hivyo wanapeleka huko vitu vizuri tu.

Sura ya 28
KUADABISHA (discpline)

Kuadabisha ni kitu cha wakati wote katika maisha yetu. Sababu ya kuadabisha ni kurudisha, tendo la upendo, kusahihisha na siyo kuharibu au kukomoa. Kuna vitu vichache vya adabu na vya mila, ila vingi vinahusu watoto wa dunia yote, mfano sheria za Mungu. Kama Tanzania mtoto kusalimia watu ni adabu, hasa kama wewe ndiye umewakuta mahali. Kusaidia mtu mzima, na kupanga maneno tunapozungumza na watu. Maana mtoto akiwa mdogo kuadabisha kunatoka nje ila akiwa mkubwa yeye mwenyewe anakuwa na nidhamu kutoka katika moyo wake. "Mwanangu nipe moyo wako" , tunahitaji kuwa na moyo wa mtoto! Katika kumfundisha (training) mtoto ni muhimu sana moyo wake au nia (akili) yake ibadilike na si matendo ya nje tu! Kama ni matendo ya nje tu, somo litakuwa halikufanikiwa. Kubadilisha nia au moyo wa mtoto ni kazi Kubwa, ila ikifanikiwa, hata usipokuwepo atafanya mema, ila kama ni matendo ya nje tu usipokuwepo atafanya Yale unayomwambia asifanye.

Watu wengi hufikiri nidhamu ni kuadabisha, kusahihisha, au kukaripia. Sababu ya kuadabisha ni kuleta utii na nidhamu. Kuadabisha ni elimu, ya kufanya mtoto awe na tabia inayotakiwa. Pengine kumkinga na hatari mfano: "usichezee barabarani;" au kumsahahihisha; "usichukue kitabu cha mwenzako bila ruhusa." Tunaadabisha watoto ili waweze kuwa na tabia njema. Hii inafanya mtoto ajue ni nani mwenye mamlaka na pia inamlinda mtoto kwa kumwekea mipaka.

Kila apendwaye huadabishwa: "Mwanangu, usiyadharau marudio ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa naye. Maana yeye ambaye Bwana ampenda humrudi, naye humpiga kila mwana amkubaliye... ni mwana yupi asiyerudiwa na baba yake?..mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, mmekuwa wana haramu ninyi na wala si wana halali." Ukiwa unaadabisha mtoto epuka kuwa mkali kupita kiasi, kukosoa, kulaumu,

kuchukia, kumshuku, kumlinda mtoto sana au kumpa uhuru mno na pia uweke mkazo ila uwe na upendo.

Mara nyingine wazazi tunachoka kuwa kama polisi. Mama anaweza kuonekana kama “mtu mbaya” au pia baba, akianglia makosa, haki, tabia njema na kutia moyo. Mara nyingi nimelia nikisema, watoto hawa siwezi kuwaadabisha wangekaa kwa “fulani” angewezea hii kazi zaidi yangu. Usichoke; watoto wako, kama umefuata mpango wa Mungu katika kulea watakuja kukushukuru. Narudia, Anza kufanya kazi kwa moyo, na mabadiliko ya nje yataonekana. Usianzie nje, anzia ndani. Moyo/akili ikibadilika hata matendo yatakuwa rahisi. Wengi tunaangalia anayofanya mtoto nje, yale ni matokeo tu!

Mtie mtoto wako moyo kufanya vitu vyema au kuwa na nidhamu njema, ukiona maendeleo mpe hongera na endelea kufanya kazi naye. Kuna watoto wengine wanaona aibu kusifiwa kwa wazi, tafuta njia inayompendeza mtoto ya kumsifu. Ila narudia kazania mabadiliko ya moyo. Siyo sheria au mambo ya kufanya nje. Hii itakuwa rahisi kwa mtoto kubadilika nje.

Hii shida inatokea kwa watu wa Mungu wengi wanaofikiria wanaokolewa kwa matendo ya sheria. Mioyo yao inakuwa haijabadilika, ila matendo ni mazuri. Ndani wanaona kongwa kutenda mema, maana hawajui kwamba tunaokolewa kwa imani na si sheria. Matendo ya sheria yanaonekana kirahisi ila kubadilisha moyo ni kazi. Mtoto anayeambiwa, “nguo hii usiivae, haina heshima,” kama moyo haujabadilika ndani, basi akiwa mbali na wewe atavaa nguo za kutisha! Mzazi mtoto asione kwamba anakufanyia wewe yale mambo kukupendeza ila kwa ajili yake na Mungu wake, na hatimaye jumuiya.

Angalia jinsi unavyoweza kusaidia nia ya mtoto. Si kila mtoto anayekuwa na nia ngumu (strong willed); kwamba kila kitu atachokifanya ni kibaya. Kuna tabia mbaya kama kuvuta sigara au kunywa pombe. Mtoto akiwa na nia ngumu ya kutofanya ni jambo jema, ila mtoto akiwa na nia ngumu ya kufanya mambo mabaya yabidi ulifanyie kazi hilo. Itachukua muda, ila ni muhimu umsaidie mtoto afanye uchaguzi wa tabia njema yeye mwenyewe, anapozidi kuwa mtu mzima, bila kusimamiwa; yaani kujitawala (free will choice). Mtoto mwenye nia ngumu (Strong willed) kwa mazuri itakuwa vigumu kuwa na msukumo wa rika kwa matendo maovu kama kuvuta sigara au kunywa pombe. Hivyo usimtweze mtoto na kumkatisha tamaa kama ana nia ngumu (Strong) na kumwambia kila kitu “la au hapana” bali uchukue nafasi hii kama kwa henzirani ya Farasi kuielekeza upande wa tabia Njema.

Mama mmoja alichoka. Akiamka asubuhi anauliza: Umepiga mswaki? Umetandika kitanda? Umekunywa maji? Umesali? Umefagia chumba chako? Watoto wa miaka kama saba, unaweza kuwaandikia ratiba ya kufuata, wakiamka. Baada ya muda watakuwa wanajitawala kwa shuguli hizi za awali. Hiyo ni nidhamu. Mtoto wa miaka minane aoshe vyombo, wa miaka kumi afue nguo zake na wa miaka kumi na miwili atayarishe chakula chenye lishe bora. Angalia kukomaa au kupevuka kwa mtoto kiakili.

Kujitawala kunakuwa rahisi kwenye kumfundisha mtoto kazi. Mtoto akusaidie kazi na usiwe mtumishi wake saa zote. Mzazi asema hizi ni nguo zetu, hiki ni chakula chetu. Mtoto asiseme nawapikia chakula chao! Kazi, na michezo inasaidia kujenga tabia na nidhamu. Nidhamu si bahati nasibu; inafundishwa kwa shuguli za nyumbani, sala, unadhifu, mpangilio, utulivu, kutunza muda na mengineyo.

Mzazi, uwe na usawa usiwe lege lege au mkali kupita kiasi (too harsh). Usimkandamize mtoto sana au umwachie huru sana! Ili mtoto atembee kwa usalama inabidi awe na wigo fulani. Mzazi anapasa afanye tathmini ya jambo linalofaa. Balansi imekuwa changamoto kwetu; wazazi wengi tuna mtindo wa kuelemea upande mmoja! Maana tunasaidia majirani kazi, nyumba za ibada, mashuleni na kuacha shughuli nyingine muhimu, kama kuwapeleka watoto wetu burudani au kuwasaidia shughuli fulani.

Mama mmoja alisema alikuwa na baba ambaye “alisaidia watu wengi ila hakutusaidia sisi watoto”. Mara nyingi alikuwa hatupi muda wake. “Mnanipotezea muda;” alisema. Alikuwa mtu wa kusaidia jumuiya kama tabibu na mwalimu (community service).Kuwa na adabu ni pamoja na kufikiria wengine. Kusalimu watu katika mila zetu ni mojawapo ya mambo muhimu katika adabu. Mtoto asalimie watu wazima. Asaidie watu wenye mahitaji, kama mzee anayehitaji kusaidiwa shughuli au kumpisha kiti.

Mjue mtoto wako vizuri, na usiwe na upendeleo wa watoto, itakuwa ngumu kuadabisha. Utapoteza mamlaka. Uwe na furaha kwa tofauti zao; na uwapende kwa usawa. Katu; usiwalinganishe. Wote tumefanya hivi pia. , wewe ungependa mtoto wako akulinganishe na mtu mwingine? “Ningekuwa na mama Rehema kama mzazi wangu au baba Bahati,” ungefurahia?

Walimu shuleni watakusaidia kidogo kuelimisha watoto wako ila mfano wako ndiyo utakaofanikisha mambo kuliko kitu kingine chochote. Mzazi mmoja alirudia kwa mtoto “wakati Abraham Lincoln alipokuwa umri wako, alijua kusoma, wakati Abraham Lincoln alipokuwa umri wako alijua kujenga nyumba”. Mtoto siku moja alijibu “Baba wakati Abraham Lincoln alipokuwa umri wako alikuwa rais wa Marekani”. Wazazi wengi tunapenda mtoto awe namba moja au apate A ingawa hata sisi hatukupata hiyo A! Kama ni urithi, mtoto huyu atapatia wapi hayo tunayosisitiza awe nayo?

Unavyozungumza, unavyofanya shughuli zako, upole wako, majibu yako, kujikana nafsi, kujitawala nafsi kwako, ndiyo masomo makubwa, mtoto anayopata kila siku! Jitahidi usiwe na jeuri ya majibu kwa watoto wako, zungumza na watoto wako kwa adabu maana maneno yako ndiyo kitabu. Hebu zungumza kwa ukunjufu wa moyo, watoto wanaathirika kwa maneno machache tu, na yakiwa rafu na ya kugombeza gombeza hayatakuwa na msaada kamwe. Mzazi anapaswa awe na nidhamu ya kuzungumza. Azungumze kwa upole, na bila kuharakisha au harara. Hili litakuwa somo kwake na kwa mtoto. Nimeona watoto wangu mara nyingi wameiga hasira zangu, nao wanakuwa na harara. Tukifundisha watoto kujikana nafsi lazima naye tujikane nafsi. Tukishinda, nao nafasi yao ya kushinda ni kubwa! Tunda halianguki mbali na mti. Mama mmoja alisema “nilikuwa naona mzazi wangu akifanya mambo Fulani, nami nimejitazama kwenye ‘kioo’ nikasikitika kwamba nimekuwa kama mzazi wangu kabisa copy right! Hata navyocheka, mitazamo navyotembea, kumbe ni copy ya mzazi wangu kabisa”.

Kila wakati unaposhindwa kutawala nafsi na kutokuwa mvumilivu unafanya kosa kubwa sana kwa watoto wako. Usiwe mtu wa kulaumu laumu watoto wako, hawezi kuchukua mzigo huu. Kama wewe huwezi kustahimili, kulaumiwa laumiwa asubuhi, wao ndiyo kabisaa hawataweza kwani wana uzoefu mdogo. Usiwe unatafuta makosa yao kila mara. Kuwakosoa zaidi ya kuwajenga, utawafundisha watoto kuzungumza hivyo hivyo. Maneno yako yaweze kuwa kama jua kwao. Goli kubwa la nidhamu ni kufanya watoto waweze kujitawala, na kujitegemea. Hebu mtoto afundishwe kuona kwamba vitu viko chini ya sheria na kutotii sheria inaleta maumivu, na disasters (ajali). Wajifunze kuheshimu mamlaka ya wazazi na Mungu.

Wafundishe wasiwe watu wa kushawishika kirahisi. Waweze kutawala nafsi zao. Waweze kufikiri wenyewe. Watoto wengi ambao walikuwa wametawalia kwa fimbo na mamlaka magumu wakitoka nyumbani kwao wanashawishika kirahisi kuwa na mwenendo mbaya. Hawana uti wa mgongo wa tabia. Hawajazoeshwa kufikiria wenyewe na hivyo mawazo yao hayajajengwa wala kuimarishwa. Wamekuwa wakiburuzwa na wazazi na kuwategemea kuwafanyia maamuzi yote na hivyo wanashindwa kujiongoza. Je umeona viongozi wanaolewa, wabaradhifu au wahujumu wa mali, waasherati n.k? walianza vizuri tu, walikuwa watoto wachapa kazi, wanafunzi wazuri na mengineyo. Tabia ya ndani ya mtu, inajitokeza zaidi wakati wa dhiki au wakati wa mafanikio!

Ni kweli watoto wahitaji kuheshimu, na kuongozwa nia zao ziweze kuungana na wazazi wao ili waone uzito wa kusikiliza mausia ya wazazi ili wakiondoka nyumbani waweze kujitawala wenyewe na kuwa mawakili wazuri. Mzazi asitumie hofu sana na kutawala mtoto katika kumtiisha, maana mtoto atakapotoka kwako atafanya makosa na kufeli mitihani ya maisha. Mungu hakuumba binadamu mmoja atawale kabisa mawazo ya mwingine au kuwa kopi wa mwingine. Hofu waweza kutumia wakati mchache sana, la sivyo haitazaa matunda mema. Wazazi wasicheze na tabia za watoto, maana tabia haitabadilishwa mbinguni! Ni hapa hapa duniani. Nidhamu ya mtoto inaanza kushugulikiwa anapozaliwa kwanza kwa masaa ya kula na vitu vingine vidogo vidogo. Usitoe nidhamu kwa hasira! Jitahidi na umwombe Mungu Akuwezeshe; la sivyo, utapoteza watoto badala ya kuwajenga.

Maneno mazito ya magombezo hayasaidii, yanakutoka mara nyingi kwasabu ya kutojitawala nafsi, na hii ukiwa nayo waweza kumwambukiza mtoto pia asitawale nafsi na kububujika maneno bila kujitawala. Wale wanataka kutawala na kutiisha wengine ni lazima wajitawale na kujitiisha kwanza. Usimpige mtoto kwa hasira kwa harara, labda kama nawe unataka awe na tabia hiyo! Waweza kumpiga, maana mara nyingine ni muhimu ila ujiulize kwamba, Je, umejitawala nafsi yako kabla ya kufanya hivi? Jiulize pia kama unafanya hili kwa upendo!

Mara nyingi wazazi wengi wanakula vyakula vibaya vinavyofanya hasira na nidhamu zao kuwa mbaya na hii pia inaenda kwa watoto. Jaribu kutumia reason na maombi pia kuadabisha watoto wako. Kila kiunga cha nidhamu mnachopitia na kushinda

ni daraja la kushinda mengine makubwa mbeleni. Neno la Mungu ni mwongozo mzuri kwa nidhamu ya watoto. Wazazi ambao wameligundua hili wamepata njia ya kuelimisha na kufundisha watoto wao. Mungu Hawezi kuchukua watoto waasi wanaovunja amri zake, wazazi wafundishe watoto wao vile Mwenyezi anavyosema. Ombea watoto wako, Mwenyezi Apenda kujibu maombi ya namna hiyo. Wazazi wasikilize ushauri wa walimu, marafiki wenye hekima na wengine. Usisieme: "Naamini watoto wangu;" bali uwe mvumilivu na kusikiliza ya wengine. Wafundishe watoto matokeo ya kukiuka amri au kanuni za afya. Kama vile kulala kwa wakati wake, kukaa kwa afya ya mgongo, kula vyakula bora, kutii unapotumwa n.k.

Chakula kina mvuto mkubwa kwenye nidhamu, mtoto ajue anakula ili aishi na siyo kwamba anaishi ili ale. Kuwa na kiasi ni muhimu katika nidhamu. Kina mama waepuke viungo vinavyoathiri kiasi kwa watoto kama vile achari, pilipili, ajino moto (monosodium glutamate) n.k. Mama ndiye kiongozi wa matengenezo ya afya, kiasi na nidhamu! Vyakula vya nyama vimeonekana vinaleta udhaifu kwa nidhamu ya kutawala hasira na mengineyo. Jaribu kufanya utafiti katika kesi mbali mbali katika nchi; Je, ni nani wanaohusika au ni wapi wana hasira au ukatili mwingi? Utaona zinaegemea mkoa fulani au Jimbo fulani.

Zamani vyakula hivi vililiwa mara moja moja, ila siku hizi kwa vile kuna maduka na babucha. Huli vyako tu ulivyofuga mara moja moja, ila ukiwa na pesa waweza kula nyama kila siku, wengine wanakula kila mlo! Huu haukuwa mpango wa asili, nyama au samaki ilikuwa kitu cha mara moja au mbili kwa Wiki.

Nidhamu inahusisha mtoto akiwa mdogo, kutawala tamaa zake. Kina mama wakiona watoto wanajishika sehemu za siri wanafikiri ni sawa tu ni wadogo, ila mara zingine tabia hii inaendelea kukua na kuwa punyeto (masturbation) na kuleta hata magonjwa ya akili na uovu wa kuingia Ponografia 9maudhui ya ngono) ukubwani. Hii inaharibu mipango ya ndoa iliyowekwa na muumba. Watoto ni vito, watunze na ili wasipate mambo ya kuharibu tabia na nidhamu yao.

Wazazi wasiache watoto wao wadogo watembelee watoto wengine bila uangalizi. Mambo ya Pajama party au pati za kulala kwa watoto wengine, yawe mwiko. Watoto wa kike wasikimbilie kuolewa mapema mpaka wapate kuelimishwa na kupata ustadi. Vivyo hivyo wavulana wawe na nidhamu na mahusiano ya jinsia nyingine. Wafundishe watoto wako wa kike wa miaka ya kumi na (teen) jinsi ya kujibu majibu ya hekima wakifikiwa na watoto wa kiume kuhusu urafiki wa kimapenzi. Hakuna haja ya kujibu kwa ujeuri ila busara. Mahali pengine wanasema wavulana na wasichana wachanganyike; hii imeleta shida kubwa. Nidhamu hii ni muhimu iwekwe, maana mahusiano yamekuwa mabaya hata kwenye shuguli za kanisa, kama kwaya n.k. Nimeona hata vyuo vikuu, vijana wa kike na kiume wakikaa mabweni pamoja na kutumia vyoo vimoja. Hili limeleta madhara mengi ya uasherati na huzuni.

Nidhamu kwenye jengo la ibada pia ni muhimu sana. Kutokuwa na heshima kwenye nyumba ya ibada na kuzungumza zungumza ni kosa kubwa, waswahili wanasema ni kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Wazazi wakisaidiana na kanisa, wahimize vijana kwamba si vizuri kuingia kwenye internet na kufacebook kanisani! Jinsi tunavyoheshimu viongozi na wakubwa wa nchi, hebu tumpe Muumba wetu heshima maradufu. Kama

macho yetu yangeonyeshwa jinsi ambavyo malaika wanavyoliona hili, sijui tungelionyeshwa nini masikini! Hebu mahali patakatifu pawe na heshima yake!

Kwa wale wasio na pa ibada wakisali chini ya miti na pengine, iwapo nafasi itokee ya kujenga nyumba ya ibada ili kusisitiza heshima kwa Mwenyezi Mungu fanyeni vile. Kitabu cha Hagai chasema tunakaa nyumba nzuri ila Mola hana nyumba. Mtoto mdogo apigaye kelele na kufanya fujo atolewe nje ili watu wengine waweze kusikiliza. Nyumba ya ibada si mahali pa kucheka cheka, kuzungumza, na kunong'onezana. Tabia hii yaweza hata kuaambukiza wengine, hasa watoto.

Wazazi msichezee au kutojali (careless) na mambo ya nidhamu. Siku ya kiyama tutaulizwa maswali kuhusu watoto wetu na malezi tuliyotoa kwa watoto tuliokabidhiwa. Mamilioni ya wazazi wataona kudekeza watoto na upendo wenye upofu, utakaofanya tabia za watoto kuharibika na kukosa uzima wa milele. Wazazi wasiokuwa na mfano mzuri ambao umeingiza watoto kwenye ulevi na kutojikana nafsi, watajiliaumu siku hiyo. Yasemekana wazazi wa Stalin, Napoleon au mafashsti wengine walikuwa wakatili na kutojali watoto na kufanya watoto kukosa upendo.

Kuna rekodi kwenye vitabu vya mbinguni naamini picha zinachukuliwa za matendo yote mabaya na mazuri; hebu fikiria picha zitakazokuja za watoto wako na wewe mzazi. Huu ndiyo wakati wa kusahihisha picha hizo. Mtu akifa hawezi kusahihisha, too late, muda umepita. Maneno, mawazo na matendo yetu pia yataletwa siku ya hukumu. Je, tumekuwa watu wasio jari? Je, tumepuuza jukumu letu kama wazazi la kuwasaidia watoto kwa nidhamu wawe watiifu? Je, tunaongeza raia wa mbinguni au wa jehanam?

Wazazi waaminifu watapokea tuzo. Mbinguni si pa kukosa, "Mbingu is worth everything!" Tusilale wazazi, katika kushugulikia nidhamu za watoto wetu.
Wafundishe watoto wako kwamba ni watoto wa Mungu. Na kwamba furaha yao inakuwa kamili kwake tu. Waambie Mungu ni Baba yao, na kwamba ni muhimu kumpa heshima. Wazazi wamekabidhiwa watoto kwa muda kuwafundisha na kuwaadabisha, hebu wafanye hii kazi kwa uaminifu. Mbinguni watoto wetu watakuwa kaka zetu na dada zetu, nasi sote tutakuwa watoto wa Mungu.

Nidhamu pia inajengeka na unadhifu, usafi na nguo za heshima. Hebu kina mama wavae nguo za heshima na kuwanunulia watoto wao nguo za heshima. Nguo pia ziwe nadhifu, makucha yakatwe, nywele ziwe nadhifu, viatu vipigwe rangi, yote haya ni muhimu kwa nidhamu. Siku hizi nguo zimekuwa bei nzuri kwa sababu ya mitumba, ila tuwe makini, kwani mitumba mingi ina nguo zisizo na nidhamu za kuigiza utamaduni wa fasheni fulani, ambao unaathiri nidhamu ya watoto. Angalia maneno ya Tshirt ukinunua. Mengine ni matusi au matangazo mabaya, mfano "Nipo kwaajili yako".

Maisha ya usafi hata wa moyo yaonekana kama yamepitwa na wakati au enzi za mawe, hii si kweli. Tunahitaji nidhamu nyakati zote. Watoto wasipende vitu vya kujionyesha, yawe ni mavazi au chochote. Ni vizuri mavazi ya wanaume yawe na tofauti na ya wanawake, hili nalo linasaidia nidhamu.
Hebu picha mbaya, vitabu vya nadharia visivyofaa, michezo ya computa isipate nafasi nyumbani. Jambo moja baya tu laweza kuharibu nidhamu ya mtoto na kuleta mbegu za uovu. Vitabu kama vya Harry Potter vya uchawi, au michezo ya kuua iwe ni mwiko.

Mtoto mdogo akijiangusha na kujigaragaza ili umpe kitu fulani ufanyeje? Zungumza naye na mguse, yeye si sultani kila anacholilia apewe. Usifikiri sana kwamba unaabishwa mbele ya watu, wewe ndiye mwenye mamlaka.

Mtoto adekaye ni yule anayeendekezwa kwa kupewa kila atakacho. Anatupatupa vitu na kuvunja vunja au kuharibu vitu, anazomea au kufyonza wengine, anatolewa udhuru wa tabia yake kila mara, anasoma au kuangalia vipindi vyo vyote anavyotaka kwenye TV; hafundishwi mambo ya kiroho ili yamwongoze na anapigana na marafiki zake kama yuko vitani.

Mara nyingi tunasema watoto wa siku hizi hawana nidhamu, hiyo ni kweli, lakini Je, ni watoto wa siku hizi kweli, au wazazi wa siku hizi? Tunapowalaumu watoto, hatuwezi kuwaacha wazazi nje. Je nini kinasitisha nidhamu? Baadhi ni:

1. Maendeleo ya haraka ya jamii na uharamia (violence).
2. Kutengana talaka na kutokuwa na mpango wa kusaidia.
3. Mifano mibaya ya marafiki, wazazi na watu wazima
4. Hatua zinazochukuliwa kwa nidhamu hazima ufuatiliaji mzuri.
5. Vyombo vya habari vinasifia adabu mbovu, na
6. Mambo ya vitu badala ya watu.
   (Materialism)
7. Mifano ya viongozi wa nchi.

Kuadabisha ni elimu, kuna riski za kuadabisha vibaya hasa kama huna elimu ya nidhamu njema. Wazazi ambao wana magomvi na kutengana inakuwa ngumu watoto kuadabisha. Watoto wanajikuza na wengine wanaishi barabarani au kuelimishwa na vyombo vya habari.

Mzazi ana sehemu kubwa kumfanya mtoto awe na nidhamu. Mahusiano mema na mtoto yanafanya mzazi aweze kumsaidia mtoto kinidhamu kwa urahisi. Mwenendo wa mzazi pia unafanya mtoto aweze kufuata nyayo. Wazazi wanaochukua muda kusikiliza na kumpa mtoto uhuru wa kuelezea mafikara yake wanasaidia mtoto kuwa na nidhamu itakayodumu. Uwazi na uvumilivu vinajenga kwa wazazi pia kunajenga nidhamu bora.

Kumkaripia mtoto kuwe kwa kujenga dhamiri yake kwa maadili. Usikaripie kwa hasira au vitisho. Zungumza na mtoto kwa upole na maneno chanya. Utoapo adhabu toa kwa upendo, malengo na haki. usitie chumvi, na kama umehahidi kitu tekeleza. Zawadi na adhabu zibalance kwenye mizani! Fanya kwa hekima ili usilete chuki. Zawadi au adabu si kiini cha nidhamu! Usitukane kama adhabu, cheki sauti yako unapoadabisha. Ni vyema usimwadabishe mtoto kwa mahitaji muhimu kama vile chakula au malazi. Ila utapima mtoto huyu anabadilishwa na athari zipi (consequences).

Kuna vichocheo vingi vinavyoweza kutumiwa kuleta nidhamu mfano, kumpeleka mtoto mahali, au kumnunulia saa au zawadi nyingine. Ufanyapo kazi ya kuleta nidhamu angalia zinaendana na maadili ya familia, uwe muwazi na watoto waelewe. Watoto wasaidie katika kujadili mara zingine. Mbinu ziwe chache na rahisi kutekeleza, na zipitiwe

kurekebishwa. Usipotumia discipline vizuri waweza kwenda kinyume cha unachotaka yaani ujenge maadili mabaya badala ya mazuri.

Katika kusifu waingereza wanasema usimsifu sana mtoto akaja kujivuna (appreciate but do not praise); umpunguzie majaribu ya kujenga kiburi na ubatili (vanity). Watoto pia wasisifiwe sana kwa mavazi, akili, maneno au sura zao! Wafundishe watoto kwamba urembo na uzuri wa kweli ni wa moyoni. Tabia! Hebu maisha ya watoto yawe rahisi (simple). Wasiwe watu wa kujionyesha onyesha, hilo litasaidia nidhamu sana. Tabia inajengwa kwa kazi ngumu na kutokata tamaa. Lenga shabaha yako juu!

Miaka mitatu ya kwanza ndiyo utakunja tabia kirahisi kina mama. Kama umekosea hapa anza kumwomba Mungu akusaidie kwenye utii na kukana nafsi, hayo ndiyo masomo makubwa. Napenda kusema kuadabisha na kuleta nidhamu siyo jambo rahisi. Mara nyingi wazazi wametumia viboko na adhabu za kujeruhi ambazo zimefanya wazazi wajisikie vizuri ila hazikusaidia watoto. Adhabu lazima itolewe kwa haki na si kwa sababu mzazi amekuja na hasira toka kibaruani.

Watoto wengi wanajifunza kwa kuona. Mara nyingine mwambie mtoto, “Tusafishe chumba chako sasa;” badala ya kufoka: “Safisha chumba hiki haraka sana, au utajuta.” Endelea kumsifia mtoto akifanya vyema, hii ni sehemu ya kuadabisha pia. Wanasema watoto wanasifiwa mara moja nakufokewa mara mia moja! Wazazi wawe watu wa kiasi si wa kubwatika na kugombeza gombeza saa zote. Angalia watu waliogombeza watoto wao sana, bila kujadiliana nao; wanakuwa na pengo kati yao na watoto wakikua.

Je unaona kwamba watoto wamefanikiwa sana? Au walipokuwa huru kutoka kwa mzazi walishusha pumzi na kuingia kwenye upuuzi mwingi? Ni muhimu kuweka mipaka kama mzazi na kuifuatilia ila uwe mwangallifu kwa kauli zako, asipofanya toa nafasi moja tena kisha toa adabu. Fanya kwa step; siyo kulipuka tu, na kumrushia mtoto vitu! Nimeona wazazi wakilifanya hili. Watoto wengi wamejifunza hasira na ukatili kutokana na mawasiliano ya wazazi. Elewa, wakati wote, kwamba kuonyesha upendo wakati wa kuadabisha ni muhimu.

Jitahidi usimdhuru mtoto, watu wazima wametingisha watoto wadogo kwa hasira wakafa au kuwa na utindio wa ubongo. Mama Fulani alikasirishwa na mtoto, akachemsha maji na akamwambia mtoto mkubwa amshike mtoto mdogo msichana na kumwagia maji kwenye uke! Walikuwa watu waliosoma vizuri wakifundisha chuoni. Mtoto alienda shuleni keshoye akashindwa kutembea walimu walichunguza na kuelezwa na mtoto. Polisi walimfuata baba kazini na kumweleza. Masikini yule baba bila kujua akasema, “Kwetu mtoto akikosa lazima aadhibiwe.” Hakujua kama kile kilichotendeka si adhabu bali ukatili! Mama yule alipelekwa jela kwa miaka kadhaa. Watoto walichukuliwa na serikali, kwani serikali ilisema hata baba mwenyewe hajui linaloendelea. Sasa watoto walikosa kila kitu; mama na baba. Methali 20:11 inasema, “Hata mtoto hujijulisha kwa matendo yake, kwamba kazi yake ni safi, kwamba ni adili.” Katika kuadabisha na kuadhibu yote tufanye tukimwogopa Mungu.

Sura ya 29
UMASIKINI NA MAZINGIRA MAGUMU YA MTOTO

Zamani umasikini ulikuwa ni upungufu wa vitu muhimu kama chakula, maji, malazi, elimu, ardhi, ukame, afya, mbinu na ujuzi wa kuondoa umasikini. Umasikini umeathiri watoto sana. Ni kweli kwenye jumuiya umeongezeka wizi, ulevi, ukahaba, ujambazi. Umasikini ni kukosa utashi na upeo wa kubadilisha au kutumia mazingira na kufanya maisha yawe bora. Watu wa zamani walikuwa maskini ila walikuwa na ardhi na bidii ya kazi na maisha yaliendelea.

Mazingira magumu ya mtoto yaletwa na vita, ugomvi wa familia, majanga, mila na desturi, ujinga, na taratibu fulani za dini. Walio masikini hawana chakula, mavazi au malazi, maji safi, ardhi, rasilimali. elimu na n.k.

Umasikini umekuwa mnyonyoro kwa kwenda kutoka familia hadi familia. Hata itikadi zingine zinazopinga mtoto kufanya kazi zimekuwa changamoto kwa watoto wetu kufanya kazi. Rafiki wangu mmoja mama yake alimwambia “wewe ni msomi huna haja ya kwenda shambani kulima, au kufanya kazi za nyumbani, mimi na ndugu zako tutazifanya?. Mtoto anajifunza kujitoa kwenye umasikini kwa kufanya kazi, mdogo na mkubwa, aliye shule na asile shule. Kazi inaongeza akili kwenye ubongo, hivyo tuwe waangalifu na kuwapa kazi watoto kwa kiasi ili wajikomboe toka kwenye umasikini siku moja,

Kwa kuendelea, Umasikini umenyanyasa watoto wadogo ambao wamekuwa na ajira mapema kuanzia miaka mitano hadi kumi na mine; na kukosa kuhudhuria shule. Kazi kwa mpaka ni sawa ila kukosa shule ni huzuni. Ajira hizo ni kama kilimo, migodi na biashara. Watoto wakambo, jamaa na yatima wamenyanyaswa zaidi pale ambapo kuna umasikini. Watoto walemavu wamepewa chakula kidogo wakisema hawazalishi. Kutibiwa na kupona kwao huachiwa Mungu kwani wanasema hawana faida. Elimu yao haishugullikiwi. Watoto wengi wanapofuka au wanakuwa viziwi kutokana na ukosefu wa chakula. Wazazi hulazimika kujamiiana hata kama watoto wapo chumbani, maana wana chumba kimoja tu. Mama kahaba huwaambia watoto watoke nje mteja akija. Umasikini wafanya watu wakose vyoo, maji salama au hewa ya kutosha, na kuishi chumba kimoja na watoto. Watoto wadogo wanaishi kwa ukahaba.

Maumivu ya umasikini kwa mtoto ni makubwa. Masikini ni watu kamili, hebu tutafute njia ya kusaidia masikini. “Nilikuwa uchi ukanivika, nilikuwa na njaa...” ndiyo tutaulizwa na si kwamba; “Ulikuwa hekaluni au msikitini siku nzima?” Japo kwenda ibadani ni muhimu, ila matendo ya kusaidia masikini ni ya muhimu mno, hata wasio jamaa zetu,

jirani yako ni ye yote mwenye mahitaji. Mpende Mungu wako kwa moyo, nguvu, akili na roho yako yote na jirani kama nafsi yako. Dunia nzima ina watoto wa mitaani. Afrika kuna wasiopungua milioni ishirini na tano mitaani. Wengine wanazaliwa mitaani, na kukua mitaani na kuoa mitaani. Wengi wamewachukulia kama taizo au balaa kwa jamii. Watoto hawa hawana jinsi, maana ndiyo njia pekee ya kujipatia maisha. Hawana uelewa, upendo, wema haki au usalama. Pengine anaishi mtaani kwa sababu ni yatima, amekosa upendo au ametelekezwa na kunyimwa nafasi ya kufanikiwa kimaisha. Huwa anajiona ametupwa nje na kubaguliwa. Anajaribu kutafuta maisha, mahali pa kujisitiri na nguo.

Wengine ni kwa sababu ya umasikini uliokithiri kwa akina mama, mtoto akawa mzigo wasioutaka au wasio tayari kuubeba. Wazazi wengine waliopata watoto nje ya ndoa au bila kutarajia wakionyesha hisia hizi kwa mtoto kwamba yeye ni 'ajali' na chanzo cha gharama wasizoziweza! Basi, mtoto huchagua kwenda mtaani. Mara nyingi tunafikiria watoto hawa watakuwa majambazi na makahaba. Tufanyeje na watoto kama hawa?

Watoto hawa ni vyema, tufanye tunavyoweza kuwasaidia. Je, vyanzo vya umasikini ni nini? Ni uchumi mdogo, hakuna uzalishaji. Akina mama wana kazi nyingi: kazi za kilimo, kuwa shambani, kupika, kutafuta kuni, na kuchota maji kwa mtu mmoja ni ngumu. Asilimia kubwa ya watu, zaidi ya hamsini, wako chini ya miaka minane. Hebu kina baba wapange kilimo vizuri na jinsi ya kusaidia familia zao. Kilimo si kitu duni. Nimeona Tanzania, wengi wana ardhi ila hakuna anayeshugulika sana kulima au kuwa na bidii. Ardhi ni rasilimali Kubwa. Kisha ustadi (skills) za kukabili maisha inafuatia. Wazee wetu zamani hawakwenda shule ila walikuwa na ardhi, nyumba, ustadi wa kilimo, ufundi n.k na wakakabili maisha vizuri tu. Hawakuwa masikini kwani walikuwa na Chakula, mavazi, na malazi. Shule watoto wanasoma ili wapate ajira, wazee wetu walijiajiri.

Matumizi mabaya ya mazao ya chakula yachangia umasikini. Makabila mengine baada ya kuvuna wana sherehe kibao kama ya kutoa mwali nje, au kuongeza mke. Ni muhimu jamii ipange itakavyotumia mazao yake kwa busara. Watu wasiwe na matazamio ya msimu bali wajifunze kuweka akiba ya chakula. Siku hizi hatukaushi mboga za majani kama jamii za zamani, hili ni la kujifunza, kwani nchi za magharibi zimesaidika mno kwa utunzaji wa mazao kwa miaka mingi. Hii inasaidia miaka ya ukame ikitokea. Serikali nyingi pia zabidi zijifunze kusaidia raia wao kwa kuondoa ubinafsi, vita, kutoa elimu, na kuchunguza suala la haki za watoto magerezani hasa wale wa mitaani umasikini ni pingu, zinazomweka mtu kwenye mabano ya makandamizo makubwa. Serikali zishugulikie ustawi wa jamii. Watu wahamasishwe kuhusu magonjwa kama ya ukimwi, VVU na mengine. Watu wafanye kazi na serikali zao.

Mungu amewajalia wengine kazi za serikali ambao waliishi katika shida hizi hivyo wanazijua fika. Tafadhali tusijisahau. Dada mmoja rafiki wa Uganda alinunua jozi mia mbili za viatu na suti za dola $200; alipopata uwezo na kazi nzuri. Alisema aliishi katika umasikini na sasa analipizia. Nilipomwambia kama anaweza kuwekwa kwenye list ya kusaidia wenye mahitaji, hakuona umuhimu. Serikali nyingine kama ya Zaire, ilikutwa haisaidii watoto kiafya, 'wakati wa Mobutu ila pesa nyingi zikiwa benki ya Uswisi na watoto wengi wana utapiamlo, magonjwa yanayojirudia na mengineyo' vyombo vya habari vilitueleza.

Ulikuwa si mpango wa Mungu kuwa na masikini bali watu washirikiane kwa walivyo navyo. Endapo dunia nzima watu wasingekuwa na uchoyo na kufikiria miradi ya kuwasaidia wengine mahitaji mazito ya umasikini yangepungua. Nchi nyingine zinatumia dola milioni themanini, kwenda mwezini mara moja, na mabilioni ya dola kupigana vita. Kila mtu ni mtunzaji wa ndugu yake "brothers keeper" usidanganyike! Katika kitabu: "Matajiri wanaomwamini Mungu, Kwenye Dunia Yenye Njaa;" au "Rich Believers in the world of Hunger" Ron Seed anasema kwamba, "Asilimia themanini ya utajiri wote duniani umo mikononi mwa watu wanaosema wanampenda Mungu, ila wakitaka kusaidia watu wanatoa chenji chenji tu au visenti vidogo, badala ya kubuni miradi ya kusaidia ili kuwakwamua watu hao toka kwenye umasikini.". Miradi midogo midogo kama ya kufuga, mfano kutoa ngombe au mbuzi watatu kwa familia moja, ni rahisi kuifanya kwa watu wenye pesa. Hebu tuige yale mema ya kusaidia watu. Isitoshe mali tulizo nazo siku moja hazitakuwa na thamani kabisa, ila wale watoto tuliowasaidia watakuwa wa thamani mno. Wachina wana msemo unaofanana hivi, "ukitaka kuwa na furaha ya siku moja, nenda ukale chakula kitamu kwenye hoteli, ukitaka kuwa na furaha ya wiki moja, tembelea sehemu mpya, ukitaka kuwa na furaha ya mwezi mmoja oa (mfano mbovu), ukitaka kuwa na furaha kwa mwaka mmoja panda miti, bali ukitaka kuwa na furaha ya milele leta tofauti kwa maisha ya mtoto". Tofauti ni pamoja na kutia moyo watoto, kuwasomesha na kubadilisha maisha yao kuwa bora.

Ni kweli Mungu ni mwaminifu amejalia watu wengi uwezo ila tunafuja fuja mali tu. Ukienda kwa mtu ana magari mengi yasioenda kokote, majumba mengi yenye vyumba vingi, na hana watoto, wote wameenda makwao anabaki kufagia na kufuta vumbi bila sababu. Nimeona mipango hii hata kwa wale watu ambao wanasema wanamcha Mungu. Katika mipango yako ya bajeti wekea watu masikini pia. Hata wale ambao hawana vingi, utaona tukimwaga mabaki ya chakula kuliko nchi zile tajiri.

Tajiri Rockfeller alipokufa mhasibu wake aliulizwa aliacha kiasi gani cha pesa alisema; "Ameacha kila kitu-He left it all;" nafikiri ilikuwa mabilioni ya madola. Hauwezi kuendesha magari mawili au kulalia vitanda viwili au kuvaa jozi mbili za viatu kwa wakati mmoja. Pia Hautaenda mbinguni mwenyewe, utaenda na hawa watu masikini. Una utajiri wa watoto wako, hebu wajifunze kazi, huduma na kuhangaikia kipato. Usiwarithishe vitu vingi, kwani wakirithi watakuwa wabaradhifu na wabinafsi kuliko aliyechuma mwenyewe. Watatapanya mali kwa fujo au anasa. Wengine wanasema 'wanajifanya tu masikini, wana pesa nyingi! Au Wavivu mimi mbona nimechumia juani, na sasa nalia kivulini'. Nani amekupa uwezo wa kuwahukumu? Je, utapata thawabu endapo wana mahitaji ya kweli? Na kama si nabii utajuaje? Buni mipango; mfano wa kumpa mtu ng'ombe au mtaji na kumpa elimu ya kupata kipato ili ukate mnyonyororo wa umasikini wa kizazi hicho. Kuna wengi ambao wangeweza kusaidia hata mtoto mmoja elimu, ili aikwamue familia yake kutoka katika umasikini.

Watoto wengi hufa kabla ya kufikia miaka mitano. Maskini wengi wana madeni, ya kufanya hata wauze watoto wao au viungo vya mwili, hasa kule India. Wengine wana utegemezi, kutengwa, kutelekezwa, udhaifu wa mwili au ulemavu, kubaguliwa na kutokuwa na mahitaji muhimu. Umasikini wa mtoto mara nyingine ni mgumu kuupima.

Umaskini unaweza ukatokana na mahali mtoto amezaliwa, desturi na mila, mtaji wa kifedha/ rasilimali, nchi aliyozaliwa mtoto n.k. Karo ya shule, sare, vita, na zana za kazi zafanya wengi wasiende shule. Nusu ya watoto hawaandikishwi shuleni, na nusu ya watoto walioandikishwa hawamalizi shule ya msingi. Mambo haya ya huzuni yanawatokea binadamu wenzetu, hebu tujiweke kwenye viatu vyao. Sheria yote, Manabí na mitume imeegemea kwenye " Mpende Mungu, kisha mpende jirani yako, kama nafsi yako". Watakuwepo Paradiso wengi ambao hawakuwahi kuingia nyumba ya ibada, bali wameishi kutokana na nuru waliyokuwa nayo ya kuwa na matendo mema mengi ya huduma. Hatuwezi kugusa mbingu, bila kugusa watu! (we can't Couch divinity, without touching humanity).

Kusoma, kuhesabu na kuandika ni muhimu sana. Kwani mtoto atawezaje kusoma neno la Mungu na kumjua Mungu bila kujua kusoma? "Na uzima wa milele ndiyo huu, wakujue wewe Mungu wa pekee na Yesu Kristo uliyemtuma." Yoh 17:3. "Mwamini Bwana Mungu wenu ndiyo mtakavyotibithika, waaminini manabii wake, ndiyo mtakavyofanikiwa". 1 Mambo ya nyakati 20:20. Hizi ndizo siri za mafanikio, kufanya ya mwenyezi Mungu na kuwa pale anapotaka tuchukue nafasi. Imani inakuja kwa kusikia, na kusikia neno la Mungu. Je watoto wetu, watasikiaje Sauti ya Mungu wasipojua kusoma?

Kuna umasikini wa kiroho, kimwili, kiuchumi na kijamii. Shugulikia haya katika jamii yako. Umasikini wa kiroho ni kukosa uhusiano sahihi na Mungu; na njia ya uhakika ya kuushinda, ni kushinda dhambi. Umasikini wa kiuchumi ni kukosa mahitaji muhimu, na kuishi katika uchafu, magonjwa, ujinga, msongamano, bila choo au maji n.k. Umasikini wa kijaamii ni kukubali mazingira manyonge na kuamini kwamba huwezi kuyaboresha. Umasikini wa kimwili ni kuwa na dhiki ya mwili, kuugua, au kufariki. Umasikini hunyang'anya mtu hali ya kujithamini; na humfanya mtu ajione ameachwa bila msaada au kujaliwa. Kwa maana hiyo umasikini ni kanusho la upendo na rehema za Mwenyezi Mungu kwa watu hao.

Basi ndugu msomaji, vita dhidhi ya umasikini unaogusa watoto ni jukumu langu na lako. Hebu Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kusaidia kwa hili. Mafanikio si namba ya watoto waliosaidiwa, bali utayari wa kusaidia watoto (willingness).

Sura ya 30
KUSAIDIA KAZI, KUHUDUMIA NA KUFUNDISHA WATOTO USTADI NA UJASILIAMALI

Kazi na huduma ni mbaraka mkubwa. Kujifikiria mwenyewe kunamwangamiza mtoto ila kuhudumia wengine ni muhimu sana. Katika jamii zote, wale waliotunza mbegu ili wapande mwaka ujao ndiyo wamefanikiwa. Ila yule aliyekula mbegu hakuweza kuongeza nyingine. Vivyo hivyo kujifikiria nafsi kwafanya tusifanikiwe. Mtoto ajue nyinyi ni timu moja, katika kazi na mchezo pia!

Vijana wana nguvu nyingi ila wengi wanakaa kivivu. Vijana wengi wanataka kushugulika na mambo ya faida yao wenyewe bila kuangalia wengine. Anzeni hata

biashara ya familia ili muweze kufanya kazi pamoja na kufundisha watoto kazi. Itasaidia watoto wajithamini na kuwa na maisha ya furaha. Mtoto wa miaka kumi na mitatu, anapaswa kufanya shuguli karibu zote nyumbani. Na ndiyo maana Wayahudi wana sherehe ya barmitvah ya kumkaribisha kwenye utu uzima.

Kaa na watoto wako uwafundishe kazi mkiwa pamoja. Mtoto anapata somo lake ya kwanza la kuwa seremala, tabibu, mwanasheria, mwandisi, mhasibu nyumbani. Uhalifu mwingine wa watoto unatokana na wazazi kutocheza na kuwa karibu na watoto wao. Zungumza nao na usikilize wanachosema, usionyeshe kwamba wanachosema huna faida nacho. Hii itasaidia nao wakusikie baadaye! Ilinichukua muda kupata motisha wa kucheza na watoto, nilijiona mimi ni mzima, kujirusha rusha na watoto, kulinitia uvivu! Hasa kwa wanawake, tunaacha michezo tukifika umri fulani. Wanaume wao wanaendelea na mipira hata uzeeni. Nilipoanza kujirusha nao, niliona tunakuwa karibu, wakitaka kunipendeza au kutii nikiwaambia maagizo. Wanasema tunazeeka kwa vile hatuchezi, na si kwamba tunacheza na ndiyo tunazeeka!

Panga nao kazi na huduma. Ukifeli kupanga utapanga kufeli. Waache watumie bongo zao kufikiri, uwe karibu nao ukiwasaidia wasiwe watu wa kukopia mawazo ya watu au kufuatisha kirahisi bila kujua sababu. Waulize maswali ya, “kwa nini?” Wape mamlaka kiasi fulani, watakushangaza. Unavyowakarimia muda wako, ucheshi na kutojifikiria ni shule ya kuwafundisha jinsi ya kufanyia wengine.

Ukiwa mvumilivu, unayejali, na mwenye upole kwao ukiwasahihisha watakuheshimu na pia kukupenda kirahisi. Ukiwaambia usile chakula fulani, au usifoke nawe ukafanya kinyume, unapunguza mvuto wako. Usiachie vituo (instituitions) kufundisha watoto wako na kukaa nao wakati wote! Mwachie mtoto, majukumu, kazi na polepole mamlaka. Taasisi zimeachiwa mambo ya huduma, au kufundisha watoto mambo mema, hili ni kosa. Watoto ni kama inzi, wanaona na kugundua miozo yetu ilipo kwa haraka. Mwonyeshe kwamba una mategemeo mazuri naye, kwamba atafanya vizuri “expectations.”

Mungu alitoa kazi kwa Adam na Hawa kwenye bustani kabla ya maanguko yao katika dhambi. Kazi ilikuwa kwa furaha yao. Watoto wafunzwe kazi za mikono na ustadi. Mtoto apewe msukumo wa kuwa na uwezo endelevu wa kujipatia mahitaji ya msingi ya maisha. Aweze kujua kuzalisha na kujitosheleza, ikiwezekana hata aweze kujenga nyumba yake mwenyewe, hata kama ni kibanda kidogo. Hebu mtoto ‘asibukue’ kitabu tu bila kazi za mikono, dunia hubadilika aweza kupata shida ya kujisaidia, ikawa kama aliyekatwa mikono. Mzazi kumfanyia mtoto kazi eti ni msomi, ni kosa kubwa na hata mara zingine ni dhambi. Elimu ya kufaa ni muhimu kwa vile hupanua upeo, huleta ubunifu, hujenga moyo wa kujiamini, hufanya mtoto afikiri, na kujenga maarifa ya taaluma. Shahada za Ulaya zilileta nchi zetu kujali kukariri masomo bila kazi, Sada za Marekani ni tofauti, mtu hupewa Shahada na masomo yaliyomo ni pamoja na kazi za mikono. Mtoto wangu akienda shule anapewa na walimu kazi za jumuia (community service). Hizi nazipenda maana hapa hatuna mfanyakazi sasa asipojua kazi mimi nitakuwa “boi” wake muda wote kweli? Na akioa hawatazozana na mkewe? Maana hata sasa nikitoa kazi hutoroka akiona siangalii, hivyo yabidi niweke bidii, kabla mambo hayajawa mabaya! Mtoto wangu mwingine anapenda tecnología akae kwenye Kompyuta eti anabuni vitu. Kwa kweli hata

mtu akibuni vitu yabidi ale Chakula na Chakula chatokana na jasho na si kubuni vitu saa yote.

Mtoto pia aweze kupata ujuzi wa uzalishaji, na ustadi wa kufaa kujipatia kipato. Kukariri mafungu ni vizuri kufanya ubongo ukue, ila wasikariri bila kujua maana yake. Kuna haja ya kumwezesha kila mtoto kutambua na kukuza ustadi katika fani anayoipendelea hadi kufikia kiwango cha ujuzi katika fani hiyo ili kumwezesha kuishi maisha bora na kuweza kusaidia wengine. Tunaona maisha ya manabii na watu wa Mungu hayakuwa ya uvivu na ufujaji. Hakuna yaya, mwalimu au yoyote atakayewasililiza watoto, kuwapenda au kuwajibu kama mzazi. Hii ni muhimu kujenga ustadi na huduma.

Mama wa Thomas Edison, aliyevumbua taa, alikuwa hana shahada ila aliweza kumsaidia mtoto kufikiri, kuwa na ustadi na kuvumbua vitu. Usimharakishe mtoto mdogo ajue kusoma na mambo ya taaluma; mfundishe kufanya kazi, ndiyo muhimu zaidi. Itajenga ustadi mwingi na tabia. Watoto wanaoingia shule mapema wanakuwa si wavumbuzi na wenye ustadi mwingi kwa vile wanafikiria ndani ya boksi la pale walipo (shule) na yale mwalimu anayofundisha. Kila mtoto anajifunza kirahisi penye joto la upendo, kujaliwa na kutiwa moyo. Kama hujui kuwaonyesha watoto wako upendo, tembelea familia nyingine, iliyofaulu kwa hilo, ukaone. Bila kukusudia wazazi wengi tunaacha makovu ya kutojiamini kwa ustadi wa watoto.watoto wanatofautiana, na wanatiwa moyo kwa njia tofauti.

Leo hali ya uchumi yazidi kuwa ngumu, muda unayoyoma na wazazi wote wanaona wanahitaji usaidizi wa kazi za nyumbani. Ila hawajatafuta ufanisi wa kufanya hili zoezi. Wanasema kwamba inachukua muda kufundisha watoto zaidi ya kutunza muda. Watoto wako wakifikia umri wa miaka kumi na minane, watakuwa na wewe nyumbani masaaa 32, 234. Ili kupata shahada ya kwanza inachukua masaaa 2001 ya kufundishwa na kujisomea! Nyumba yako ina muda wa mara 16 zaidi!

Watalaamu wanasema ukiwa unasoma vitabu kwa saa moja kwa siku katika fani fulani kwa siku sita za juma, utakuwa mtaalamu (expert) katika nyanja hiyo baada ya miaka mitatu . Hebu tuchague nyanja fulani na kusoma na watoto wetu na kufanyia vitendo kila siku, tutajenga stadi, na mwelekeo wa mawazo.

Watoto wako wakitoka mlangoni mwako na kuwa huru na kuwajibika, Je, watakuwa tayari kukabili changamoto watakazozikabili? Je, wanajua shughuli za nyumbani, kukarabati vitu, kupika kwa afya, kupanga vitu vyao, na kupanga bajeti? Je, tuache mafundisho haya wajifunze kwa pata potea katika maisha yao? “Nipe samaki nitakula leo, nifundishe kuvua nitakula maisha yangu yote.” Haujachelewa. Tafuta vitabu usome. Kitabu cha Bonnie Runyan Mc Cullough na Susan Walker: “Ways to get your kids

to work at home;" ni moja wapo wa vitabu vizuri sana. Angalia website ya Mc Cullough. Website zingine nzuri ni kama Doorpost.org, reviveour hearts, breakingsilencenow n.k. Kujenga Ustadi wa watoto mpaka wafikiapo miaka kumi na minane; kuwapa kazi, kufundisha kazi, kuwapa moyo watendapo kazi, jinsi ya kuwasaidia kupanga vitu nyumbani, kuwafundisha jinsi ya kutumia pesa, usafi, upishi, kununua vitu na kuchagua kazi au taaluma maishani. (angalia chati ya kazi za nyumbani)

Katika utafiti wa watoto mia mbili na hamsini, ilionekana 97% ya watoto walipenda kusaidia wazazi wao. Walitoa sababu kwamba, walifanya hivyo ili 'kumpunguzia mzazi wangu shughuli, ili kuwafanya wazazi wao wawe na muda nao, kuwa msaada kwa kuchukua majukumu katika familia, kujisaidia nikiwa na nyumba yangu, kupata uzoefu, kupunguza uchafu nyumbani', na mengineyo. Tuwafundishe na kuwapa nafasi ya kufanya hizi kazi. Inaongeza kujithamini, na kuweza kujitegemea, wanathamini vitu na kuthamini huduma zao wakijua juhudi unazofanya kufanya kazi hizi. Watoto wanaofanya kazi wanafurahia maisha na hawaboeki kirahisi.

Wape hamasa watoto wako wafanye kazi itakayokuwa ya faida kwao na kwa watu wengine. Shughuli yo yote itakayofanywa, ishughulishe mikono na mawazo yao. Vijana Wajue kwamba maisha ni kazi, majukumu na kusaidia watu wengine. Watu wanahitajika watakaokuwa tayari kukabiliana na dharura yo yote, wakisaidia watu na si kujifikiria wao tu. Tumeokolewa tuokoe (saved to serve). Ni kweli watoto wanahitaji kuthaminiwa ili waweze kufanya mazuri. Ila wasitafute thamani yao kwa kujikusanyia vitu. Mafanikio, kwa kupitia maoni mazuri ambayo wengine wanasema kuwahusu ni ya muda mfupi tu; ila kuthaminiwa na Mungu hakuna ulimwengu au chochote kinachoweza kutikisa.

Kufanya kazi ya mikono ni muhimu kuepuka majaribu na katika nyanja zote za maisha. Ni makosa kufikiria kazi za mikono ni za daraja la chini. Kila mtu ajue kazi ya mikono, na si kuwa mwalimu, karani, au mwanasheria tu. Watoto wa kike wasifikiri kazi ya nyumbani ni ya kudharauliwa na za hadhi ya chini. Watoto wa kiume, wathamini kazi (dignity of labor). Watoto wawe na zamu za kusafisha vyombo, kupika, kufua, hata mzazi akiwa tajiri kiasi gani. Hii ni muhimu katika makuzi yao kuwa kamili. Wazazi mabilionea wa chi za magharibi wamegundua hili, na wanajitoa mhanga kufundisha haya kwa watoto wao, mke anakaa nyumbani akipangilia ratiba ya siku nzima na kuisimamia kila siku. Mama wengi wanaona wanakaa kishamba wakiwa nyumbani hata kama mume ana kazi ya kutosha mahitaji. Nafikiri Mithali thelathini na moja 'mwanamke bora' si lazima aajiriwe, na si mvivu bali ana ujasiliamali wa aina Fulani ili asimamie watoto na mji wake upate mafanikio.

Wasichana wajue kushona, na shuguli zote za nyumbani. Watu wachache wenye uwezo Afrika wameweka wafanyakazi ambao wanafanya kazi masaa kumi na manne kwa siku bila kupumzika; wakifikiri kwamba wanasaidia watoto wao kwa kuwadekeza na kuwafanya wavivu! Hebu mama kumbuka hata huyu mfanyakazi anahitaji kupumzika, jiweke kwenye viatu vyake. Mara nyingi hawa wasichana wa kazi huwa ni watoto tu hata hawajafikisha umri wa miaka kumi na minane, lakini ana kazi nyingi na masimango mengi kupita umri wake' bibi majivu'. Watoto wako wapaswa kufanya kazi kila siku, ijapokuwa si kama mfanyakazi, la sivyo, utawalemaza watoto.

Wazazi tuepuke kupendelea watoto wetu kiwaziwazi kwa kuwapa wafanyakazi, watoto wa kambo, na jamaa kazi nyingi huku watoto wetu wakistarehe; tukifikiri tunawabariki watoto wetu na kumbe tunawalaani. Tukisema tunawalipa vipesa vidogo na hata wengine hatuwalipi tunasema wanakula vya bure! “Lieni matajiri kwa kunyanyasa watenda kazi “Yakobo tano ilisema. Watoto watajifunza kunyanyasa watu wengine. Mungu amejihusisha na watu wanaonyanyaswa kama yatima, masikini, wajane, na wageni. Utaona baadaye wale watoto walionyanyaswa wanakuwa na maisha ya uwezo na wale uliojaribu kuwakinga wanakuwa ombaomba! Toa laana hii ya kunyanyasa watoto unaoishi nao kwenye nyumba yako, ambao hukuwazaa. Ni vyema usikae nao, au kusema unawasaidia kuliko kulaani watoto wako. Napenda kusema kwamba hata wao wahitaji mapumziko.

Neno la Mungu linasema, siku ya saba ya juma wasifanye kazi, “Wasifanye kazi wageni wa malango yako na mfanya kazi.” tunawatumikisha na sisi tunasema tumepumzika siku hiyo ila wao bado tunawatumikisha tukifikiri tunatii neno la Mungu. Ninajua kabisa kuna wafanyakazi wengi wabaya, wezi na mengineyo. Wafanya kazi wengine ni wavivu, wakizoea mahali wanaweza kuleta magomvi, au uovu Fulani. ila kwa madhumuni ya kulea watoto sitazungumza ya upande huo.

Kina mama wengi walizaliwa vijijini, na wanajua kazi. Walifundishwa kabla ya kuwa na matabaka mengi, sijui kwa nini wanaona watoto wao wawe mayai. Tabia hii pia inajenga tabaka kwa watoto wako nao watatesa wafanyakazi vile vile kama watajaliwa kuwa na uwezo kidogo. Wakijaliwa kuoa au kuolewa wataleta kesi nyingi za uvivu. Nafikiri ni vyema kila binadamu ajue kulima bustani. Zaidi ya asilimia hamsini tuko mjini na hatulimi. Wenye ardhi ni vibibi vizee ndivyo vinalima mashambani. Vijana wako barabarani kwenye mastendi ya basi na biashara ndogo ndogo ambazo haziwezi hata kuwalisha. Ndiyo, biashara ni nzuri, ila lima pia. Niligundua magharibi kwamba wengi walihamia vijijini, wakapata bustani, majani ya kukata na wanyama wa kufuga ili watoto wapate kazi za kutosha!

FAO (shirika la kilimo) linasema asilimia tisini ya mashamba hapa Afrika hulimwa na wanawake, wanaume hushughulika na kufyeka mashamba mapya na kutoa visiki. Kina baba fundisheni watoto wenu wa kiume wasiwe wavivu na kuchagua kazi. Wapike, wafue wadeki nyumba hasa wa mijini kwani hakuna shuguli za nguvu za wanaume mijini. Watoto wa kiume wakikua na kuoa wakiwa kwenye miji yao ndiyo watapikiwa na kufanyiwa hayo yote, ingawaje siku hizi pia wanasaidiana na wake zao, kwa sababu wote wanaenda vibaruani. Mama yao hawezi kuwa mtumwa kwao, la hasha!

Si kila mtoto wa kiume ni mume! Anayepigiwa magoti na kuletewa chakula. Hilo ni kosa! Dada zake wanamfulia eti yeye hana shuguli yoyote, anakaa tu. Kazi inaleta furaha. Mtu mvivu anamwalika shetani kuchezea akili yake kufanya vitu viovu. Na Neno kuu lasema, “Asiyefanya kazi na asile;” hili ni neno zito. Mtoto wa kiume atakuwa ndiyo mwenye kazi, mke ni msaidizi. Mume ndiye aliyepewa kufanya kazi kwa jasho!

Tunapaswa kufanya kazi masaa manane kila siku! Mama afundishe watoto kwamba yeye si mtumwa. Eti watoto wanakaa au kuzurura siku nzima, huku yeye anasumbuka toka asubuhi mpaka usiku! Usiwe mtumwa wa muda ila muda utumiwe vizuri.

Kazi za mikono zinaleta unyenyekevu na zinatayarisha watu kwa vitu vikubwa. Nimeona mfano wa watu mashuhuri duniani; katika matunzo yao wamekuwa watu wa shughuli nyingi kama kukamua ngombe, kulima, kuchunga, kufua, kutunza wagonjwa, kupika, na mengineyo.

Fundisha watoto kufanya kazi vyema na kwa muda mfupi, ili wote mfurahi na kucheza pamoja. Mama anayefanya kazi muda wote hana muda wa kucheza na kufurahia watoto wake. Mama usiwe mchovu kupita kiasi, acha upumzike kwenye kiti, na watoto wafanye kazi. Watoto wameitwa interview ya kazi, hata ya kufagia wameshindwa! Hata mbinguni tutafanya kazi, hakuna uvivu pale. Hatutatoka jasho ila furaha ni tele kwa mtu ambaye anashughulisha mikono na mawazo yake. Shughuli ya mikono ni muhimu zaidi ya sayansi. Mbinguni hakutakuwa na wanasheria, matabibu. Kazi nyingi zitafutwa, ila kulima itakuwa huko kwa vifijo.

Kutojali kwa wazazi, kuwafundisha kazi watoto ambao wamewaleta duniani kumeleta uovu na mengi yasiyosemeka. Ni makosa kuacha watoto kukua bila kuwa na ustadi fulani kujisaidia kimaisha. Si kila mtu atakuwa na shahada, ila kila mtu anapaswa kuwa na ustadi wa kujitafutia maisha. Watoto wajue jinsi ya kutumia zana mbali mbali kama za ujenzi, useremala, kilimo n.k.

Hakuna nyanja ya kazi za mikono yenye umuhimu duniani, kama kama kilimo. Tunakula mara mbili au tatu kwa siku, ila tunaweza tukaishi bila kukalia meza na viti. Yeye anayejipatia kipato kwa kulima ana faida nyingi sana kama kujiajiri, kuwa na chakula, uvumilivu na kuepuka vishawishi vingi vya shetani. Fundisha watoto majira mbali mbali ya kilimo, jinsi ya kutumia pembejeo kama plau na ukiweza trekta, ili kuleta ufanisi zaidi kwa kilimo. Mazao fresh uliyolima ni tofauti na ya sokoni! Hasa siku hizi wanapotumia mbolea na mbegu mbaya ambazo zikitoa mbegu huwezi kupanda zikazaa! “Genetically engineered,” au GMO, “Genetically Modified Organisms.” Soma zaidi kuhusu haya kwenye website kama mercola.com au mosanto.

Mazao ya namna hii ni ya kuepuka, hata nchi za ulaya zinaanza kupiga marufuku. Wanatuletea mbegu hizo na wakulima wetu wananunua na kuacha kutunza mbegu zao mwishowe wanakuwa hawana mbegu. Mbegu zote zabidi ziagizwe nje ya nchi kwa pesa! Ni kama mtu aliyekatwa mikono. Pia zina athari kubwa za afya kwenye mwili. Jua unachokula kwa kuepuka uvivu wa kulima.

Japo wazazi wangu walikuwa wafanyakazi walihakikisha wana shamba la mboga nje ya mji wa Dar. Watu wengi walikuja na kupewa chakula, na hiyo ilitufundisha kazi ya kulima na ukarimu wa kutoa vitu kwa watu! Hata leo ninapoishi Marekani nahakikisha nina bustani na bado tunagawa chakula kingi kwa watu. Kazi yo yote, hata ya kilimo, ni lazima uiwekee malengo na ifanywe vizuri. Mwanzo 1:29 ukilima zao na lile zao mbegu yake isiote kuna walakini. Kila mtoto amalizapo shule hata kama ni darasa la saba au nane, hakikisha kwamba ana ustadi fulani.

Tufunze watoto uchumi. Nimeona watu wengi wakipika na kutupa chakula, kilichohangaikiwa muda mrefu! Watoto wanahitaji kujua kwamba chakula ni mbaraka na

kukitupa ni laana. Chakula kinakuja kwa shughuli nyingi. Hata kwenye sherehe ukipata chakula cha bure usipakue kama unajua hutakimaliza! Rudia hata mara kumi, ukimaliza ndiyo uende kupakua tena. Ila usiwe mlafi! Wagiriki walijulikana kwa Kula na kutapika ili wamalize chote mezani, mfano huu ni mbaya kwa malezi. Tuwe na kiasi. Kiasi, ni bora na ustaarabu kuliko kupakua kingi kasha ukitupe! Si sifa kutupa chakula, ni vibaya sana, hasa kwa nchi masikini kama zetu za Afrika. Mamilioni wafa na njaa kila mwaka, wengi tunajisifu, 'tulikula na kusaza' unachosaza wape wenye mahitaji!

Tufunze watoto kutokuwa watu wa kufuja vitu na kuharibu haribu vitu ovyo. Nimeona hata watu wanapewa kinywaji mfano juisi, wanakunywa na nyingine wanamwaga chini. Niliuliza wanasema eti "Tulifundishwa kwetu kwamba, hunywi yote, nyingine unawamwagia mende na viumbe wingine.", Je Hii tabia ni ya tambiko? Wafundishe watoto wako jinsi ya kutumia pesa. Pesa ina kazi tatu tu. Mahitaji yetu, mahitaji ya wengine (jamaa, marafiki, jirani na masikini), na mahitaji ya kuongeza ufalme wa Mungu. Watoto wajue pesa inatokana na kazi si bure. Wape (posho) pocket money kidogo kila mwezi ili wajue jinsi ya kutumia pesa. Kuanzia miaka kumi. Watoto wafundishwe kutoa zaka na sadaka kwa Mungu. Mungu ndiye mpaji, hili ni la muhimu sana watoto kuelewa. Muwe mnapanga bajeti pamoja ili wasizidi vipato vyao. Watoto wengi hawakufundishwa kabisa jinsi ya kutumia pesa, walipokuwa wadogo, na wakianza kuwa na vipato wanashindwa kupanga bajeti; kulingana na vipato vyao. Wanaingilia njia mbaya za kupata vipato haramu kama vile wizi na umalaya ili kukidhi maisha.

Nakumbuka kuingia katika madeni mengi ambayo nafikiri ningekuwa na elimu ndogo ya uhasibu ingenisaidia sana. Hasa siku hizi zenye mikopo ya 'Credit card' Epuka hizo. Mtoto akifanya kazi kidogo apewe motisha ya pesa kidogo. Waeleze kwamba ni motisha na siyo mshahara. Ili wasipende pesa sana maana, "Kupenda pesa ni shina ya maovu yote ila utauwa na kuridhika ni tunu kubwa." Watoto wasidai kwamba kila kazi lazima wapewe motisha, wewe ndio uamue. Ni haki (right) ya mtoto kumrithisha ardhi, elimu na ustadi. Katika neno la Mungu tunaona kwamba ardhi ilikuwa ya jamii yote. Wazazi wengine wamekuwa na tamaa ya kukaa na kila kitu bila kugawia kwa watoto kitu cha kuwasaidia wajitegemee. Kweli, watoto ni waharibifu wakati mwingine, usiwakabidhi vitu vikubwa wasivyovifanyia kazi, na hivyo watavifuja tu, na hawatakuwa na uchungu navyo. Hata hivyo tufundishe watoto toka wakiwa wadogo jinsi ya kutumia mali, kupata riziki, na kusaidia wenye mahitaji.

Mambo haya tunaasiwa yawe kwenye mioyo yetu, tuwafundishe watoto wetu waamkapo, wasimamapo, wakaapo na walalapo. Tuwafundishe watoto wetu kuwa mifano

yetu ya ukarimu, na ya bidii ya kazi. Tungependa kuwafundisha watoto wajitegemee katika jumuiya. Vyombo vya habari vyaonyesha watoto wavivu, wazembe wasiopenda kazi ila tu kustarehe. Shida ni kwetu wazazi; kuleta watoto duniani, na kuwaachia watu wengine wawafundishie!

Ni kweli watoto wetu wanaishi wakati ambapo maisha ni magumu. Zamani kazi zilikuwa nyingi na pia mshahara ulitosha kukidhi malazi, mavazi na chakula. Siku hizi watoto wetu wanaanza maisha na shahada ila kazi ni adimu na wakipata hazisaidii kukidhi mahitaji ya muhimu. Hata hivyo tuwasaidie kuwafundisha kuhusu bajeti, hundi, mikopo, madeni ya shule, au credit cards maana hivi hawatafundishwa shuleni. Pia kutumia pesa kwa hekima, ni jukumu letu wazazi kufundisha maana shule haitafundisha hayo. Kama tulivyoona mtoto akipewa posho afundishwe kutumia kwa hekima, kuweka akiba na kusaidia wengine.

Kazi zingine za nyumbani waweza kuwalipa kidogo, ila zile za kawaida kama vile kutandika vitanda, kupika, kulisha wanyama, kusafisha nyumba, kutupa takataka, kuosha vyombo n.k; si za kulipwa! Wakifanya kazi zile ambazo unaona ni ngumu na waweza kuwalipa kidogo, wanaweza kununua nguo, vitabu, kuweka akiba au matumizi yao ya binafsi. Ni vizuri kuweka kumbukumbu unapowapa pesa, ili mtu asisahau na kuacha kutimiza yale ambayo mmeafikiana.

Wakimaliza shule ya msingi waweza kutafuta vibarua kwingine na kuanza kujisaidia kwa matumizi madogo madogo; au hata kwa msaada wenu waanze biashara nyumbani. Watoto wasifanye kazi tu ya kutumia akili kwa mahesabu, ila pia wafundishwe kubalansi pesa na kutumia pesa vizuri, wajue zinazoingia na kutoka. Watoto wanaojinunuliwa vitu wenyewe wanapunguza ufujaji, pesa inauma ikiwa yao wenyewe! Wataangalia nguo nzuri ila bei nafuu. Nguo walizonunua wenyewe watazitunza vizuri zaidi.

Mtoto anayeweza kuhesabu aanze kufundishwa mambo ya pesa. Katika neno la Mungu fedha au pesa imetajwa mara 3500; na mifano ya pesa kwenye visa (parables) ni thuluthi mbili ya mafundisho yote. Mahali pesa ipo ndiyo mioyo ya watu wengi ilipo. Fundisha watoto kwamba, kupenda pesa ni shina la maovu yote. Usiwape watoto wako pesa ovyo au nyingi, inaharibu tabia na nidhamu! Watoto waonyeshwe maisha ya watu maskini sana ili waweze kuwa na roho ya kuona kwamba wao wametunukiwa sana.

Hapa kwetu Afrika wale wenye uwezo wachukue watoto wao kuhudumia watu hawa na kukaa katika mazingira haya kwa miezi, au hata mwaka. Watoto wengine wanatoka nyumbani mapema wakifikiri kwamba maisha yatakuwa rahisi kwa vile hawakupata maarifa ya kutumia pesa. Wazazi waangalie talanta za watoto wao ili wasipate maarifa au kisomo kwa vitu ambavyo hawatavitumia. Vijana wakitaka kuoa au kuolewa ni vyema wapewe semina za kutumia pesa na wenzi wao. Utafiti unasema kwamba asilimia sabini na tano ya ndoa zote huvunjika kwa ajili ya pesa. Hebu wapange bajeti ya mwaka mmoja ionekane kama ni kitu kinachowezekana. Wafundishe watoto kutunza muda, muda ni mali. Wasipoteze muda bila sababu. Waweze kuwahi mahali pa

kazi. Mahali pengine wanafunzi wapata mikopo ya kusoma chuo kikuu, wafunze watoto kurudisha kile walichokopa.

Wafundishe watoto wabajeti sehemu ya kusaidia watu hata bila ya kurudishiwa, ni ya muhimu. Wazee, wagonjwa, na wenye mahitaji mengine, kama wanahitaji kuchotewa maji, kuchanjiwa kuni, kusafishiwa nyumba hata kukarabatiwa nyumba zao, na mengine. Nimeona watu wengine ukitaka kuwasaidia kujenga nyumba ya huduma zao wenyewe (maktaba) wanaanza kukutoza pesa ya labor. Wanafikiri wao hawana huduma yao ya kujitolea japo kuwa wamepewa msaada. Kijana mmoja mwenye kazi mjini, alitoa bati na vifaa vya ujenzi kujengea wazazi wake nyumba. Ndugu zake waliojua kujenga, hakuwakutoa kitu na walitaka kumchaji kwa ujenzi na kutunza wazazi, japo wote walikuwa watoto wa mtu mmoja. Watu wengi wanataka kusaidiwa kila kitu hawafikirii mchango wao ni muhimu. Hiyo ni roho ya kimasikini. Watoto wafundishwe kujitolea bila malipo.

Watu wa nchi za magharibi wamefanya kujitolea kuwa somo katika fani nyingi. Waenda nchi mbali mbali wakijitolea (volunteer) hata watoto wa mamilionea wameanza program ya kuwapeleka nchi nyingine watoe huduma zao bure kupunguza ubinafsi. Watoto wanazaliwa na uchoyo mwingi, na uchoyo huu unaongezeka wakizidi kukua. Wajifunze kujitolea kwenye vituo vya walemavu, watoto yatima, wagonjwa na kadhalika. Nikiishi Marekani niliona kwamba watu weusi (black Americans na sisi waafrika) tunafanana kwa kutotoa vitu vyetu bure kwa watu tusiowafahamu. Tunatabia ya kusaidia ndugu na jamaa zetu wa damu tu. Hatuwezi kutoa kwa watu baki au mashirika! Tunabidii ya kukaa na ndugu au jamaa kwenye nyumba zetu na kutunza yatima wa ndugu zetu tu! Ila wenzetu wazungu waweza kusaidia mtu wasiyemfahamu. Sisi tunasema kwamba eti ni matajiri. Mungu Amekuwa mwaminifu sana siku hizi nikitembelea marafiki tuliosoma nao nimeona wana utajiri mwingi. Majumba makubwa mengi, magari pia. Ila wanasaidia jamaa zao tu. Hata watu waovu wanasaidia jamaa zao tu! Ukiwa unampenda Mungu utavuka maili ya pili. Wanasema ukarimu unaanzia nyumbani ila hauishii hapo (charity begins at home, but does not end there).

Dini ya kweli ni kusaidia yatima na wajane na kujilinda na mawaa. Jifunze kutoa au kujitolea kwa wenye mahitaji usiowafahamu. Utapokea baraka tele na kufundisha watoto wako kwamba mtu wa kumfanyia wema au kutoa zawadi si jamaa tu peke yake! Tupa mkate wako kwenye maji na utaupata baada ya siku si nyingi, “Give and it will be given back.” Kutoa kwa kupata ni motisha namba mbili ila motisha namba moja ni ile ya kujifunza kukana nafsi na kuondokana na uchoyo. Hii ni tabia ya mbinguni. Nasema hivi, nikijua wale wa karibu kwako pia hutawasau, kwani ‘yeye asiyesaidia wa nyumbani kwake na ana uwezo ni kama kafiri’. Mwafrika na anayempenda Mungu hawawezi kuwa matajiri kwani tuna wengi tunaojua wenye mahitaji, ndugu, jamaa, marafiki na hata jumuiya.

Wazungu, pengine walituharibu na tip, bakshishi. Siku hizi mwanamke anaweza kukwama na gari, mwanamume mtu mzima, anakuja, na hata kabla hata ya kusaidia, anauliza, “Utanilipa ngapi kusukuma pembeni?” Na watoto wanasikia! Watajifunza kwamba hakuna cha bure!

Watu wanaojitolea kusaidia wenye mahitaji wamepata faida nyingi sana kama kuishi maisha marefu, kuwa na furaha ipitayo maelezo, kusaidiwa, kubarikiwa watoto wao kuwa na maendeleo makubwa n.k. Ukiwa na ustadi fulani, kama mganga, mhandisi, mjenzi tenga muda wako mwingine kusaidia watu bure. Isiwe kila kitu kidogo lazima ulipwe. Ni umasikini wa namna, kuweka pesa mbele kuliko mbaraka kwa watu. Kusitokee ubaridi kati ya watoto na wazazi tafuteni muda wa kujua talanta, ladha , tabia na hisia ili mjue jinsi ya kuwasaidia na kujikana nafsi. Wafundishe watoto wako kwamba unawapenda na ndiyo maana unataka wajifunze kazi.

Wafundishe watoto jinsi ya kuandikisha mirathi sawa maana ukisahau, utakapokufa, jamaa zako watachukua mali yako pengine bila kujali watoto wako! Nenda kwa mwanasheria na kwa gharama ya chini, usaidie watoto wako na wengine maskini au kubariki kazi ya Mungu.

Tajiri milionea Colgate, wa dawa ya mswaki, hakuandika kazi ya Mungu kwenye mirathi yake. Pesa ile ilishikwa na watoto ambao hawakujali hilo, na upendo wake haukufuatwa. Kuandikisha mirathi ni muhimu ili matakwa yako kama mzazi yatimie na pia watu wasidhulumu watoto wako.

Watoto wajifunze kupenda kusoma! Hata kama hawako shuleni. Vitabu vina thamani kubwa. Unajifunza mengi na hasa yale ya kiroho. Nimeona watu wazima ambao wana shahada na wanamaliza mwaka mzima bila kusoma hata kitabu kimoja! Huu ni umasikini. Mpe mtoto kitabu wakati wote, ili ajenge tabia ya kupenda kusoma. Maisha ni mafupi kujifunza uzoefu mwingi, ila vitabu vitakusaidia kupata uzoefu huu; “Long life learning books, self improvement books.” Nilifundishwa kupenda vitabu na mama nikiwa mdogo. Natembea na vitabu mara zote hata nikingoja basi. Wengi hata napoishi wanashangaa “Unapenda kusoma sana;”

Niliona mtu moja ameandika kwenye t-shirt; “So much books and no time to read!” “Vitabu vingi na hakuna muda wa kusoma!” Ila chagua vitabu vyako viwe vya kukusaidia uwe mtu bora kiakili, kijamii, kiroho na kimwili. Usisome vitabu vya nadharia na mapotofu. Usikae mahali hata kwenye kituo cha basi, ukiangalia watu, magari na majengo, bila kitu cha kufanya mwishowe unaanza kuseng’enya; wakati ambapo ungesoma kitabu na kujengeka. Wanasema katika ukimbiaji kushindwa kunatokeza wakati wa kupokezana vijiti! Hebu tuwapasie watoto wetu vijiti kwa ufanisi ili wajue jinsi ya kukimbia kwa uhodari.

Sura ya 31
UNYANYASAJI WA WATOTO

Mamilioni ya watoto wananyanyaswa kwa njia mbali mbali duniani. Wakifanyakazi za viwandani na mashambani wnafanyishwa kazi hadi mikono inaota sugu na migongo kupinda. Wengine wanajiuza miili yao katika miji mikubwa na kupata ukimwi na baadaye hata hufa. Wengi wanakufa kila siku kwa magonjwa yanayotibika. Watu wanaopenda na kutetea watoto wanajiuliza kwa nini jamii na hata serikali nyingi zinatelekeza watoto. Mchungaji Mbenah ametusaidia kwa utafiti kuhusu unyanyasaji wa watoto. Mazingira ya mtoto yanakuwa yasiyo salama, unyanyasaji na kukatili dhidi ya mtoto. Watoto wanapaswa walindwe dhidi ya mazingira ambayo wanaweza kuumia, kuumizwa, kukandamizwa, kufanyiwa ukatili na kunyimwa haki zao.

Kuna umuhimu wa kuzungumzia unyanyasaji wa watoto kwa vile utafiti na macho yetu yameona hili ni tatizo kubwa duniani. Asilimia, kati ya 20-65 ya wanafunzi shuleni wanatendewa vibaya na wenzao bila msaada. Adhabu kali za viboko na hasira mashuleni. Watoto milioni mia moja ishirini na sita duniani, wanafanyishwa kazi ngumu, na za hatari zikiambatana na kupigwa, kubakwa, kutengwa, kuteswa na hata wale walio katika taasisi kama vituo vya watoto yatima.

Kila mwaka watoto wasichana milioni mia moja hamsini, na wavulana milioni sabini na tatu duniani wanabakwa au kufanyiwa ukatili wa kijinsia na watu ambao mara nyingi wanawafahamu kama ndugu wa damu au jirani! Kila mwaka watoto elfu hamsini hujiua kutokana na unyanyasaji na milioni mbili hutibiwa hospitalini kwa majeraha ya unyanyasaji wa kimwili. Watoto milioni 5.7 hutumikishwa kama vibarua kwa ukahaba, na kuuza madawa wa kulevya. Takwimu hizi si rahisi kuzipata kwa vile unyanyasaji mwingi hufanyika kwa siri.

Unyanyasaji wa familia una uwiano na unyanyasaji wa watoto. Unyanyasaji ni tendo lolote analofanyiwa mtoto kwa kudharimia hata kusababisha majeraha, na kuathiri ukuaji au maendeleo ya mtoto.Wazazi, walezi, walimu , waajiri, wanafunzi na watu wa karibu ndiyo wanaofanya unyanyasaji. Unyanyasaji unasababisha matatizo ya muda mrefu ya kiafya kama vile mfadhaiko, tabia ya ukatili, ujambazi, ukahaba, kutumia madawa ya kulevya, magonjwa ya moyo na maini, kutofanikiwa masomo na mahusiano mabaya na watu kama magomvi, kutoheshimu watu, n.k.

Unyanyasaji ni matumizi ya makusudi ya nguvu ya kimwili au madaraka kwa uhalisi au kutishia mtu na kuleta madhara ya kifo, saikolojia, haki za mtu, kudumaa makuzi. Unyanyasaji ni aina zote za mateso ya kimwili, kisaikologia, utesaji kingono, kutojali, kutelekeza, au kumnyonya kibiashara au aina nyingi ya kusababisha madhara halisi au ya baadaye. Unyanyasaji unatishia juhudi za kusaidia maendeleo ya mtoto ili afikie urithi wake au aende sambamba na mazingira yake.
Aina nne za unyanyasaji ni
Uyanyasaji wa hisia ni maneno na vitendo vya mfululizo anavyofanyiwa mtoto na kusababisha jeraha kwenye hisia zake. Mama wa kambo mmoja alimsimanga mtoto, akamtukana na kumdhalilisha, akimlaumu kwa makosa madogo madogo; “Maiti wewe!” Mtoto akajiona hana kauli wala msaada. Mtoto huyu atakuwa mharibifu, asiyependa

kucheza, mwenye hasira , mwenye misemo ya kujidharau, asiyejithamini, mwenye aibu, mwoga, mkali, na mkorofi.

Kutelekezwa ni tendo la mzazi au mlezi kumnyima mtoto mahitaji ya msingi kimaisha kwa kukukusudia au kutokusudia au kutoweza. Mtoto aliyekosa chakula atakuwa na shida ya afya na kudhoofika. Mavazi huleta heshima na hadhi au utu wa mtu, mtoto akikosa mavazi atashindwa kufunika aibu yake, kukosa heshima au kujikinga na baridi au joto. Mahitaji mengine ni afya bora. Mtoto asiposhugulikiwa aweza kupata maumivu, ulemavu, au hata kifo. Mahitaji mengine ni upendo, matunzo ya mtoto na elimu. Mtoto aandikishwe na kuhudhuria shule.

Mtoto pia anapaswa aangaliwe ili asiwe hatarini. Hii itasababisha mtoto aumie au kuumizwa. Jambo jingine la kutelekeza watoto ni kutowapa watoto fursa ya kuzaliwa au kuishi. Mamilioni ya mimba yanatoleewa kila mwaka. Katika nchi ya Amerika pekee, milioni nne! Mama mjamzito na mumewe wana wajibu wakutengeneza mazingira mazuri ili mtoto azaliwe salama. Hiyo ni pamoja na lishe bora, kupumzika, amani, kutotumia sumu kama sigara na vileo, kutotupa watoto chooni au majalalani.

Unyanyasaji wa kimwili ni tendo lolote analotendewa mtoto katika mwili wake hata kusababisha majeraha katika mwili wake au kuathiri maendeleo yake. Hii ni pamoja na kumwadhibu mtoto kwa kumpiga, kazi nzito, kumhusisha katika taratibu za dini au jumuiya za kupita kiasi zinazomchosha na kumnyima haki yake ya kupumzika au kucheza. Michezo yasaidia kumkuza mtoto, na kumwezesha kukabili maisha yake ukubwani. Michezo ya kujipikilisha, kuwinda , mke na mume n.k ni majaribio au mazoezi ya maisha kamili kwa watoto (rehersal).

Viboko vimejengwa kwa msingi kwamba mzazi au mlezi anataka kumwonyesha mtoto mamlaka yake. Mara nyingi ni mila na tamaduni. Viboko vinapaswa kutumika kwa nadra sana, bila hasira. Pia kwa upendo mwingi. Wazazi wengi wana ghadhabu wakiwa wanachapa watoto na wamekata tamaa na maisha yao. Serikali nyingi zimeanza kupiga marufuku kuchapa viboko mashuleni; maana watoto wamekufa. Mara nyingi mtu hutoa hasira yake na hii haimsaidii mtoto. Adhabu kwa mtoto ilingane na upendo Wako kwa mtoto.

Nimeona watoto wengine darasani wanapigwa kila siku kwa kuwa na maksi pungufu hata wale ambao wenye urithi mdogo wa akili au mazingira magumu. Wazazi pia wanataka walimu wafanye miujiza; watoto wao wawe namba moja, wakati wao wenyewe hawakuwa namba moja; na wao ndiyo waliwapa urithi watoto mdogo kiakili. Hakuna mzazi anayekubali kwamba mtoto wake ni wa wastani, kwa hiyo ategemee na aridhike na maksi za wastani toka kwake. Hata hivyo adhabu hizi nzito nzito hazijengi mazingira ya kujifunza. Urithi hafifu na mazingira ni magumu yanazamisha boti kabisa.

Licha ya viboko wengine huadhibu watoto kwa kuwachoma moto, kuwapiga ovyo, kumchoma na ncha kali, kumpiga makofi, teke au vikumbo, kukunja viungo vya mwili wake, makwenzi, mijeredi, kumfinya, kumfunga kamba, kumkata au kumnyima chakula. Mara chache kumchapa mtoto kuna faida ila ni vigumu kujua viwango gani vya uchapaji vinakuwa unyanyasaji kimwili. Si kila mtoto anahitaji kiboko. Matumizi ya kiboko yakivuka kiwango fulani yanafanya mtoto awe sugu, mkatili na asiyejali. Kumpa mtoto kazi nzito kushinda mwili wake, kama kunbebesha ndoo nzito ya maji ni unyanyasaji. Watoto hupigwa na kudhalilishwa, kuchubuka, kuchanwa- chanwa nguo na ngozi, kwa sababu ya kukosa sare rasmi, kuwa duni kimasomo, kuchelewa shuleni, kutolipa karo, na mengine ambayo hayako kwenye uwezo wao!

Mambo mengine ni kuweka watoto wadogo katika sherehe za muda mrefu, kama harusi na kufanya wapate huzuni au njaa kwa vile hawafurahii (enjoy) tukio hilo. Jambo jingine ni kama kutahiri watoto wa kike. Hii inaathiri magonjwa, kujifungua , furaha ya ndoa na mengineyo.

Jinsi ya kujua mtoto aliyenyanyaswa kimwili ni michubuko na alama za mapingo, alama za damu zilizovia, maelezo ya mtoto yasiyotosheleza, michubuko migongoni, matakoni, paji la uso, mapaja na pengine. Dalili nyingine ni kama: Vidonda vilivyo katika hatua mbali mbali za kupona, makovu katika sehemu mbalimbali za mwili, misokoto ya tumbako, alama za kuungua kwa maji ya moto, au alama ya pasi au umeme, kuvunjika kwa viungo mbali mbali au mikwaruzo kwenye mwili ambayo haieleweiki au haina maelezo yakutosha.

Mtoto huyu huwa anaogopa kukutana na watu wazima, ana hasira, anajitenga, hapendi kuguswa, huogopa wazazi au walezi, huwa na hofu, anachelewa shuleni au anawahi sana, hutembea kwa shida, hulalamika maumivu, anapenda nguo zifunike mwili wote hata wakati wa michezo ili kuficha majeraha au makovu na sngu. Kwa mfano atavaa sweta la mikono mirefu, hata kama jua linawaka. Anaweza kutoroka nyumbani ili kuepuka mateso.

Unyanyasaji wa kijinsia ni tendo la kumwingilia mtoto kijinsia bila kujali kama aliridhia au hakuridhia. Inajumuisha kumwamsha tamaa ya kimapenzi, kumwonyesha picha za ponografia (umalaya wa picha), ubakaji, kujamiiana na mtoto, kufanya mchezo wa kimapenzi na mtoto, kuahidiana kufanya mapenzi na mtoto, kumpa mtoto elimu ya ngono isiyolingana na umri wake, kumfunua au kumvua mtoto nguo katika mazingira yasiyomsaidia, kumpapasa mtoto sehemu za siri au zingine ambazo kwa kawaida hufunikwa na kumwozesha mtoto kabla ya kufikia umri wa miaka kumi na minane.

Kila mwaka watoto milioni moja duniani wanaingizwa kwenye ukahaba au ponografia (umalaya wa picha) kwa kulazimishwa, kushawishiwa, kudanganywa au kupewa vizawadi. Dalili za mtoto anayenyanyaswa kijinsia ni kutembea au kukaa kwa shida, madoa ya damu kutoka kwenye nguo zake, kuwashwa au kutoa damu sehemu za siri, au za haja kubwa. Magonjwa ya zinaa kabla ya kuvunja ungo au mimba za ujanani, kutopenda kubadili nguo, kutoshiriki michezo, kujitenga, huzuni nzito, tabia ya ujuzi usio wa kawaida kwa mambo ya ngono, vitendo vya kuchekesha visivyo vya kawaida, kutotaka kuguswa, majaribio ya kujinyonga, kutokuwa na mahusiano mazuri na wazazi,

wenzake au walimu, kuwa na zawadi au fedha nyingi zisizoelezeka, tabia ya ubembelezaji wa ajabu, pia mtoto anakuwa msiri sana. Madhara ya unyanyasaji huu ni kama: Ujauzito, kuchanika kwa sehemu za siri, magonjwa ya zinaa, ukimwi, kifo, na madhara ya kisaikologia ambayo yanakaa kwa muda mrefu hata utu uzima.

Kuna baadhi ya mambo ambayo huchangia kwa unyanyasaji wa watoto, kama:

Mila na desturi potofu huchangia unyanyasaji wa mtoto mfano kuwaoza watoto wadogo. Katika jamii fulani, inachukuliwa kama heshima kwa mzazi kwa sababu atainusuru familia na aibu ya kupata mimba kabla ya kuolewa.

Ujuzi finyu wa malezi na kujenga urafiki na watoto, hawajui kuwakuza katika upendo ila kuwakaripia , kuwakemea, kuwaadhibu na kuwakatili.

Ulevi: Vileo hufanya wakose utashi wa kuwajali na kuhudumia watoto na kuwa na magomvi na migogoro ya wakati wote. Pia ugumu wa maisha, watoto wanalipia madeni ya familia au wanalisha familia zao.

Historia ya kunyanyasa watoto katika familia: Tunda halianguki mbali na mti. Japo watoto hawa walinyanyaswa na kuwa na wazazi wenye tabia mbovu kama ulevi, wamejifunza hayo mabaya na watayaendeleza katika maisha yao. Ingawaje kwa neema za Mungu wengine wanaweza kubadilika.

Kwa kawaida mtoto ana maswali mengi ya msingi na wazazi wasio na ufahamu wa jinsi ya kujibu maswali hayo ,huwafukuza kila mara kwamba, “Sitaki maswali,” wanawavunja moyo watoto wasiulize tena. Udadisi wao hauishii hapo, bali mtoto ataendelea kutafuta majibu kwa maswali yake na pengine kwa kificho au kwenye mazingira yenye uwezekano wa kunyanyaswa.

Mazingira holela ya mijini, na makazi yasiyofaa kunakofanya wazazi waishi na mtoto chumba kimoja, yafanya mambo ya kubaka na kulawiti watoto yaongezeke. Wazazi kutopata muda wa kutosha na mtoto ili wamlinde na kumshauri mtoto. mtoto atoe taarifa, waonapo dalili za kutendewa maovu au mtazamo usio sawa.

Ni muhimu kuweka viwango vya kukubalika na kueleweka ili kuona watoto wanakua salama. Sera na miongozo inabidi iwekwe ili kudumisha mazingira ya upendo kwa watoto. Kuwe na mafunzo kwa watoto na wazazi kuhusu kanuni, dalili na miongozo ya usalama watoto. Umoja wa mataifa umejaribu kuweka viwango hivi. Ila upendo wa ndani kabisa ni kuwa na ‘nia mpya’ toka kwa Mwenyezi Mungu!

Wazazi, jamii, taasisi, dini, wapewe uelewa wa kutosha kuhusu wajibu kwa mahitaji na usalama wa mtoto. Swala la utetezi wa mtoto ni jukumu la kila mtu mzima na taifa zima kwa ujumla. Watu wote wanaofanya kazi na watoto wachukuliwe historia zao na jamii ieleweshwe kwa mapana na mwongozo uwekwe na kujulikana. Watoto na wazazi waelimishwe yote yahusuyo unyanyasaji kwa kina na jinsi ya kuzuia.

Sifa za mtetezi wa mtoto ni mtu anayempenda Mungu, mwenye tabia njema, mtu mwenye upendo, anayechukia umasikini na kuamini kwamba kuna uwezekano wa mabadiliko, mwenye msimamo mkali dhidi ya wanaonyanyasa watoto, anayejitolea. Hebu awe mtu wa maombi na kufunga na kusoma Neno Mungu na kuwaombea watoto. Ataje majina na mahitaji yao mbele za Mungu. Aseme shida za watoto kwa niaba yao,

aishi maisha ya utulivu, awe mlinzi wao dhidi ya hatari zote. Awe na mikakati ya kuzidi kuelewa masuala yanayogusa watoto kwa vitabu , magazeti, ajue malezi ya watoto wa vipaji maalum na watoto wenye mahitaji maalumu, kma vilema vya mwili, mawazo au utashi. Lazima athamini watoto na kuwaona wameumbwa kwa mfano wa Mungu na hivyo wasiwe katika mazingira hatarishi.

Kiini cha utetezi wa mtoto ni kumtendea haki, kumtoa katika hali duni mateso, hatari au vita. Kumpa tumaini, mahitaji muhimu, na upendo. “Fumbua kinywa chako kwa ajili yake aliye bubu; uwatetee watu wote walioachwa peke yao. Fumbua kinywa chako uhukumu kwa haki; uwapatie maskini na wahitaji haki yao. Mithali 31:8,9. Viongozi wa jumuiya, serikali, wazazi , makundi maalum, wanalo jukumu la kuwa msemaji wa watoto. Mtoto ashirikishwe katika maamuzi yatakayoleta ufanisi kwake. Mtetezi wa mtoto anatambua kwamba kila mtoto ana thamani na hili ni jukumu toka kwa Mwenyezi Mungu mwenyewe.

Sura ya 32
MUZIKI, UCHAWI NA MENGINEYO

Hatutaweza kunyamaza kuhusu muziki katika mazingira tunayoishi. Utamaduni wa kigeni umeingia mwingi na kuigwa. Muziki una nguvu sana za kubadilisha mwenendo, hisia na tabia. Waweza kufanya maamuzi ya ubongo kutindikiwa na kutenda kitu ambacho hakikudhamiriwa. Muziki wasemekana kutopita kwenye ubongo na kuingia kwenye hisia (bypass frontal lobe-thinking site). Biashara zimetumia muziki kutuuzia vitu ambavyo hatukupanga na visivyo na maana kabisa!

Muziki ni kama lugha fulani ambayo mtu yoyote aweza kujua kwamba sauti hiyo ni ya furaha, chuki, n.k. Hatuwezi kuachia watoto wetu kusikiliza chochote na wakawa na maadili. Tukumbuke kwamba Shetani alikuwa kiongozi wa kwaya na mwimbaji maarufu. Na kwa vile hapendi kumsifu Mungu anataka kufanya tuingie katika nyimbo zake. Kama tunataka usafi wa mawazo na moyo lazima tuepuke nyimbo za aina ulani, ambazo zinafanya maaumzi yetu na kufikiria kuondoke kabisa! Ili kushinda lazima umjue adui yako,wengi wanasema ‘hatuamini kama shetani yupo, ni hekaya tu za mabaradhuli’. Napenda kusema Neno la Mungu latueleza wazi katika kitabu cha Ayubu, Mwanzo na Ufunuo 12 kwamba Ibilisi aliumbwa na Mungu na alikuwa kerubi. Aliasi, na atafuta wafuasi wa kwenda Jehanamu naye. Ibilisi anatumia muziki, michezo, vyombo vya habari, vitabu, kwa mvuto mkubwa siku hizi. Tuchunge sana mambo haya na kusali usiku na mchana, tusije ingia mitegoni mwake. Nchi kama marekani, inafanya futuhi kwa kuweka siku ya kusherekea wachawi, Oktoba 31 (haloween), masikini hawajui kwamba ibilisi ni kuumbe ambacho ni moto wa kuotea mbali.

Nyimbo nyingine za kumsifu Mungu zafanya Mungu aonekane kama rafiki wa kiume (boyfriend)! Hizi zinapunguza utukufu wa Mungu. Nyimbo kama za Rap zimekuwa za kawaida miongoni mwetu na hasa kwa vijana. Tunapenda sana kuigiza vitu vya magharibi hata kama vinatuumiza. Tunavipambia. Nimeona soda ya coca cola ambayo si

nzuri kwa afya, hata ukiweka jino ndani, litayeyuka matangazo ya biashara yalisema : “Sababu bilioni moja za Afrika kunywa coca cola;” na tuna matunda mengi hapa Afrika!

Magari ya abiria kama matatu au dala dala yamekuwa yakiweka sauti kubwa, na kupasua ngoma zetu za masikio. Katika kumwomba kondakta siku moja apunguze sauti alisema, “Wewe mama mzee, ndiyo maana hupendi nyimbo zetu.” Kondakta mwingine alimwambia rafiki yangu: “Kama unaona huu muziki ni makelele kwako, basi shuka utafute usafiri wako, maana wengine wanaufurahia.”

Utafiti wadhihirisha vijana wengi wanakuwa viziwi mapema na maadili kupasuka kutokana na nyimbo za ajabu wanazozisikiliza. Nyimbo si maneno tu yanaokuwa yana maadili pungufu ila midundo pia. Mtu asikudanganye kwamba muziki ni maneno tu! Midundo inaleta fikra, hisia na misisimuko ya aina fulani kwa ubaya au wema. Wasichana mia tano ishirini na mbili wa mijini walifanyiwa utafiti, wakakuta wanapiga walimu wao madarasani mara tatu kuliko wengine, kwa vile wanasikiliza miziki ya rap. Jaribu kuangalia kwenye internet website hizi kuhusu muziki Ivory Myers, the destruction by Christian Berdahl au Battlefield Holywood.

Muziki waweza kubadilisha fikara sana. Mwanamke mwenye mimba anayesikiliza muziki wa sauti iliyotulia na nzuri, ana nafasi kubwa ya kuzaa “mtoto mwenye akili nyingi na mahusiano chanya;” mfano, muziki wa Mozart. Na anayesikiliza rap aweza kuzaa mtoto ambaye ni mkatili na asiyependa watu. Jamani miziki tunayosikiliza nyumbani kwetu na kuwawekea watoto ni lazima ichujwe sana. Staili za ajabu zinaingizwa pole pole. Mnajua wanamuziki wale wa ‘metal’ jinsi maisha yao yalivyokuwa. Kelele nyingi na fujo pia.

Wanamuziki wengi wanaojulikana kwenye nchi nyingi wameingilia madawa ya kulevya na kujiua. Mfano Elvis Priestley, Whitney Houston, Bob Marley, Michael Jakkson na wengineo ambao mnawafahamu. Siyo siri, miziki mingi imewaingiza vijana wetu kwenye uasherati, ukatili, ujambazi, wizi, ulevi, ugomvi, na tabia zingine mbaya kwenye jamii. Chuo kikuu cha North Carolina, katika utafiti wake wa mwanamuziki; Andre Adams, album ya “Hell’s kitchen;” maneno yake yako wazi kufanya vijana waingie uhalifu, na kutumia madawa ya kulevya.

Wameona pia wanawake wanalengwa sana, hasa wale wasiojiheshimu na wanafanywa kama vyombo vya wanaume kuwaridhisha tamaa zao za mwili. Miziki hii mibaya imeonekana inaleta maradhi ya akili kama sonona. (depression). Hebu miziki ya namna hii iachwe kuwekwa kwenye radio zetu za jumuiya mara moja.

Chuo cha Josephson Institute kimeona kwamba, kwenye miji mikubwa yenye magenge ya uuaji na kutumia silaha ilihusiana na nyimbo za rap na hip hop zenye maneno yanayolenga ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa wanawake, ukatili, na ubakaji zimeleta huu upasukaji wa mambo. Magazeti kama Essense yamekuwa na kampeni ya “Take back the music;” yaani, urudishe muziki mbaya. Kwa kweli kila mahali vijana wameweka role models (mifano) kwenye wana muziki, ijapokuwa tabia zao ni mbaya. Rap ina tabia ya kujikita kwenye utajiri ambao unatokana na magenge, madawa ya kulevya na vile vinavyokiuka sheria. Ujumbe ni kwamba; “Uhalifu ushabikiwe, na uhalifu una manufaa;” na unalipa kwa

njia kubwa kuliko ajira za halali! Maisha yaonyesha ya jkutamanika na kuvutia kwa vijana, na kwamba watakuwa matajiri haraka. Yanamfanya mtu asijikane nafsi au kutawala nafsi na kuwa na "umimi" mwingi. Mambo haya ya utajiri na anasa yashawishi vijana wengi wasisome au waache shule ili waimbe tu. Wasichana waonekana wakidansi kando ya magari ya kifahari kama benzi. Hii ni kama kivutio, kwamba watakuwa na maisha hayo. Picha za sigara, pombe na nguo zisizo na adabu au uasherati vinaambatana na miziki hiyo.

Asili ya muziki kwa wataalamu wa historia zamani ilikuwa kumtukuza Muumba na kumsifu. Nyimbo nyingine, kama zile za taifa za patriotic (Uzalendo) n.k hazina ubaya. Bali wengi siku hizi waimba kusifu watu na kuwafanya vimiungu vidogo. Yule mtu wa kale (kiburi) inabidi awekwe kwenye kikapu na si kushabikiwa, maana ni udhaifu wetu binadamu. Ukisikiliza mapigo na maneno yake utatambua tofauti. Nyimbo nyingine za zinahusiana na mambo ya uchawi, juju, au nguvu za giza ambazo ni jadi na desturi nyingi Afrika na duniani wamekuwa wakishugulika nazo. Miziki rap na hip hop ina uovu mwingi. Ni muhimu watoto waiepuke kabisa.

Watu wengi hawajajua kwamba shetani ni kiumbe halisi! Ana ufalme na kudanganya watu wawe upande wake. Twasisitiza, Kumjua adui yako ni Mwanzo wa zaidi ya asilimia tisini, ya kushinda vita. Kuna falme mbili tu za kutumikia nazo ni Mungu wa mbinguni na shetani. Kila mmoja wetu anatumikia moja wa falme hizo, jiulize unapolea unatumikia falme gani? Je kulea watoto wako kimaadili utasaidiwa na Mungu au shetani?

Tunapopeleka watoto wetu kwenye matibabu, Je, tunawapeleka kwa waganga wa kienyeji wapewe hirizi na matibabu ya nguvu za giza au tunatafuta yale mambo ya kufaa kwetu. Mchungaji mmoja alipeleka watoto wake kwa mganga wachanjwe. Watoto walikosa shule muda wa wiki nzima, waliporudi, walionyesha wenzao chanjo kichwani. Walikuwa wamechanjwa katikati ya nywele ili chanjo zisionekane!

Kuna mstari mwembamba kati ya uganga wa nguvu za giza na ule wa matibabu yatokayo kwa Mola. Jaribu kutumia muda wako kupeleleza unapoona vibao vya waganga. Najua watu wengine wa tiba rasmi za afya, wana uzembe wa kazi zao na migomo mingi. Mara nyingine tunakata tamaa kuwafikia; ila wao wana vipimo vya kujua kama tuna malaria, typhoid au kansa. Je waganga wa kienyeji wanaoandika, "Daktari toka Zanzibar anatibu shida za boma, kurudisha vitu vilivyopotea, mapenzi, kupendwa, nguvu za kiume, utasa; watakusaidia kweli kuliko wale wenye vipimo? Hata wakikusaidia je, unajua nguvu wanazotumia?

Mambo ya uchawi hasa kwa watoto yameingia mno duniani. Na hata nchi za magharibi kitabu cha Harry Potter na jiwe la uchawi cha watoto kinatumika hata mashuleni kama text book. Kitabu hiki kiliandikwa na dada mmoja wa Uingereza, akisimulia uchawi kama ni kitu kizuri cha kusaidia watu. Watu wamekichukulia kitu cha uchawi kama fantasy na kuchekesha na kwamba si cha kweli. Anaeleza kwamba Harry Potter ni mtoto yatima ambaye wazazi wake waliuwawa na mchawi. Anatumia uchawi kusisimua mawazo ya watoto (imagination) na kutoa masomo ya maadili.

Masomo ya kizimwi namna hii yameharibu watoto na kuwaingiza wengi kwenye uchawi. Wanaonyesha kwamba uchawi si kitu kibaya hata unaweza kuwa na huruma na

kufanyia jamii huduma. Kitabu hiki na filamu nyingi za watoto zimejaa madragon yanayotoa mioto mdomoni, mazimwi na wachawi wanaoruka na mifagio. Zinazungumzia mengi ya sorcerer divination (uganga wa kichawi), witches, palmistry (utabiri wa kusoma viganja), astrology (unajimu), majini, numerology (utabiri kwa kutumia namba) na mengine yanayofanana na hayo.

Shuleni ninakofundisha, tuliwakataza wanafunzi wetu kusoma vitabu vya Harry Potter. Baada ya muda, kukawa na makambi. Alikuja mhubiri maarufu sana (Randy Skeete) toka Marekani. Akawa anawapa watoto nafasi ya kumuuliza maswali, lakini kwa kuwa walikuwa wengi sana, aliwaambia waandike maswali yao. Na kila siku kabla ya kuhubiri angechukua muda mfupi kujibu maswali hayo. Siku moja alisoma swali hili, "Shuleni kwetu, walimu wetu wanatukataza kusoma vitabu vya Harry Potter, Je, vina ubaya gani?"

Sitasahau jinsi alivyojibu mtu huyu wa Mungu; alisema: "Shukuru Mungu saana kwamba una waalimu wa aina hiyo. Kama una vitabu vya Harry Potter, tafadhali sana kavichome leo. Na ninawaomba wazazi wote mliopo hapa, tafadhali sana, kawasaidieni kutafuta vitabu vyote vya Harry Potter, na mvichome leo!" Kisha aliendelea kueleza ubaya wake, kama tunavyoeleza hapa.

Kumb. 18: 10-14, inasema; uchawi mweupe au mweusi (black or white magic) wote watoka kwa shetani. Si kitu cha kucheza nacho katika malezi ya watoto. Watoto wengi wamechukuliwa kwenye uchawi na wazazi au jirani na kufanyiwa ukatili mwingi kama wa misukule, hebu wazazi tuepuke kujiunga na vitu ambavyo vinachochea mambo haya.

Angalia nchi za magharibi na uchawi wa wicca. Afrika watu wanafikiri ni viini macho na mazingaombwe (fantasy na harmless)! Kumbe wanachezea moto kwenye malezi ya watoto. Wicca ni dini ya uchawi, hutoa laana, na kuzungumza na wafu na imechukua watoto wengi! Watoto wanaotoka kwenye nyumba zilizovunjika wamekuwa wakipata uongozi (guidance) kwa wachawi hawa na kupoozwa maumivu yao kwa muda.

Wapenzi wa vitabu hivi kama vya Harry Potter na wicca, wengi wameanza kuamini wachawi, wengine bila hata kujua, maskini! Wanafundisha maadili fulani mazuri na kuingiza uchawi ndani, ndivyo shetani anavyopenda kuchanganya (deception). Wana wachawi wazuri na wachawi wabaya, kitu ambacho si kweli, wachawi wote ni wabaya, yaani nguvu za Ibilisi.

Watoto wengi waliojiwa wamesema wamejisikia kama wachawi wenye nguvu nyingi za uchawi. Katuni nyingi za watoto zimeingiza uchawi pia kinyemela! Picha tu ndizo zinaonekana za watoto, ila maneno yana uovu na ni ya watu wazima! Wazazi wengi wanapenda watoto wakisoma na kwamba kuna mafundisho fulani mazuri! Je, mafundisho machache mazuri na mengi mabaya ya ibilisi ni tosha kuridhika tuwape watoto wetu.

Miziki wanayosikiliza vijana wetu ipimwe, wengi hufikiria kama muziki unataja jina la MUNGU basi ni mzuri japo kuwa mapigo yake ni ya dunia. Kuna vitu vitatu vinavyopaswa kupimwa kwenye muziki, hivi ni muhimu sana kuviangalia, baada ya kuangalia maneno ya muziki. Miziki ambayo mabasi yetu inaonyesha si utamaduni wa mwafrika kabisa! Ni mambo ya ajabu sana. Utamaduni wetu ni wa heshima sana, na tunaheshimu watu wakubwa ila kwenye mabasi watu wasio na nguo za heshima na mambo ya ngono yamejaa kwenye muziki na watoto wa rika zote wanayasikiliza na kuyaona kwa macho. Hebu viongozi washugulike na haya mambo kusaidia vijana wetu. Nilijaribu kuzungumza na makondakta wa mabasi kama 28 hivi wasiweke hizi kanda ila hawakusikia. Hata yale mabasi ya wacha MUNGU nilipoyapanda, nikifikiria kwamba yameandikwa mafungu ya Biblia basi hawatakuwa na dansi za ngono walikuwa na dansi hizo za ngono. Mambo ya ngono yasipoenda kwa utaratibu MUNGU alioweka huleta magonjwa, mauaji na kushindwa kwa maisha kwa namna ya ajabu. Ni moto ambao mtu hawezi kuushika kwenye mikono yake na kuacha kuungua yeye na watoto wake. Viongozi wengi wana magari yao na hivyo hawajui kinachoendelea kwenye mabasi, Nilipozunguzumza na viongozi wa makanisa walikuwa hawana habari na kinachoendelea kabisa! Hawajui taifa lipo kwenye mapambano makubwa na ibilisi, na hata mataifa yenye mali kama Marekani uovu kama huu unaruhusiwa uungalie mwenyewe kwa siri nyumbani mwako na si kumwonyesha kila mtu kwenye kadamnasi. MUNGU aweze kusaidia mikanda hii ipigwe marufuku kabisa.

Tunaambiwa katika neno la Mungu, Ufunuo 12, kwamba kulikuwa na vita mbinguni, na ibilisi alitupwa duniani na thuluthi ya malaika. Ndiye anaitaabisha dunia miaka yote hii. Je. wewe unataka kumtukuza huyu nyumbani mwako? Kila mtu yupo vitani na ibilisi kila siku, tujue au tusijue, adui yetu ana usongo mkubwa wa kumteka kila mmoja. Soma Kutoka 22:18; na Ufunuo 19:31. Hebu usiingize miziki au mambo yajayotukuza uchawi au kupoteza maadili ya watoto. Mambo ya chanjo yaepukwe Walawi 19:28, watu walichanjwa na kuharibu sura zamani, siku hizi watu wengi wa magharibi wameingia dini hii na ukikutana nao wanatisha. Kwaajili ya media wengine wameingia mambo ya kujikata kata (cutting, na kujifungia kamba shingoni na kuitoa wanaposikia wamepata burudiko kama la kileo). Watoto wengi wamefariki masikini kwa mitineo ya kuigiza kama hii.

Sura 33

WATOTO NA VYOMBO VYA HABARI NA TEKNOLOJIA
MEDIA – (RADIO, TV, SIMU, COMPUTER)

Zamani hatukuwa na vitu hivi. Tulikuwa na muda mwingi sana wa kuzungumza na kushauri watoto wetu. Ingawaje vitu hivi ni muhimu sana, lakini vina madhara kadhaa. Ni muhimu tufahamu kwamba tunachokila ndicho kinajenga miili yetu. Ukila vyakula vya afya, utajenga mwili wa afya. Vile vile, mambo tunayoingiza katika mawazo yetu, ndiyo yanajenga akili zetu. Ukiingiza mawazo mazuri (positive), utapata matokeo mazuri. Ukiweka akilini mawazo mabaya (negative) pia utapata matokeo mabaya.

Hebu tuanze na muziki. Siku hizi kuna vifaa ambavyo vinatuwezesha kusikiliza muziki kila mahali, hata tukitembea. Muziki uko kwenye simu na kila mahali. Miziki au nyimbo nyingi hazijengi tabia hata kidogo. Midundo na maneno yake ni ya kuhimiza uhalifu, kama kutoa mimba, (ushoga) homosexuality, lesbianism, uzinifu, mauaji, ujangili, wizi, n.k. Kijana akisikia maneno haya kwa muda mrefu anayakariri na kuyaamini na yanaathiri fikra zake. Atapenda kujaribu kufanya kama wimbo unavyosema. Andrew Fletcher aliandika zamani, mwaka wa 1703; kwamba “Wewe andika sheria, na mimi niandike nyimbo, na nitaitawala nchi yako.”

Mtunzi mmoja wa nyimbo alisifia jinsi kuzimu kulivyo mahali pazuri, ambako watu wanafurahi na kusheherekea, na kwamba unahitaji uende huko, manake rafiki zako wote watakuwa huko. Walishauri kwamba huko hamna kuboeka kama mbinguni. Mtoto akisiliza maneno ya wimbo huu kwa muda mrefu, atatamani aende kufurahia huo uzuri wa kuzimu. Nyimbo nyingine zinamdharau Bwana na kumkufuru Mungu.

Mwimbaji mmoja alitunga wimbo wa kuwaambia vijana wasiwatii wazazi au wakubwa wao, unasema “fanya unavyotaka mwenyewe,” bila kujali ye yote. Wimbo mwingine unasema, “umejaribu pombe, haikusaidia, umejaribu madawa ya kulevya, hayakusaidia. Umejaribu ngono, haikusaidia, kwa nini usijaribu kujiua?” Looh! Ndiyo maana vijana wengi wanajinyonga siku hizi???

Lakini siyo kwamba nyimbo zote ni mbaya. Kuna nyimbo nzuri. Wazazi tunatakiwa tuwanunulie watoto kanda (cd/dvd) za nyimbo nzuri, tangia wakiwa wadogo. Nyimbo nzuri zinahuhisha na kumwinua mtu kiroho na kiakili.

Televisheni ni shetani mkubwa aliyekuja kutuibia familia na watoto wetu. Nyumba nyingi zimevunjika kwa sababu ya runinga au televisheni. Baba anataka kuangalia mpira au malumbano ya wanasiasa, hali mama ana kipindi chake, na watoto wanataka vipindi vya watoto; nayo televisheni ni moja!!! Uwezo wa kununua mbili au tatu hamna. Sasa unafikiri itakuwaje, kama siyo ugomvi wa kila siku humo ndani? Walio na uwezo wameweka tv kwenye kila chumba, hata jikoni, lakini wamepoteza watoto. Utafiti umeonyesha kwamba tabia za watoto zinaathiriwa sana na matukio wanayoyaona kwenye runinga. Wazazi wengi wanalia. Mashirika mengi yakiwemo ya kidini yanahimiza wazazi kufuatilia na kudhibiti vipindi ambavyo watoto wao wanaangalia kwenye runinga. Mzazi mmoja akasema, “serikali itusaidie jamani!” Serikali itasaidiaje? Je, ndiyo inanunulia watu televisheni au itakuja kucontrol jinsi ya kuiangalia nyumbani kwetu? Vipindi na mavazi mengi ya wanaokuweko ni kinyume cha maadili mema.

Televisheni ina baadhi ya habari na mambo mazuri, lakini mengi ni mabovu ambayo, kweli tusingependa watoto wetu washuhudie. Kwa mfano, ujambazi, lugha chafu, ngono potofu, mavazi mabaya au mauaji. Utafiti mmoja ulisema kwamba mtoto ambaye anaangalia runinga kwa muda **wa saa nne kila siku, atakuwa ameshuhudia mauaji elfu kumi kwa mwaka!** Utafiti ulisema kwamba “Hisia za mtoto huyu zitakufa, kiasi kwamba atamimina chai anywe wakati anashuhudia mama yake akikata roho!”

Mtoto anayeangalia uhalifu sana, licha ya kukubaliana na hali hiyo, hata yeye atakuwa mhalifu, pia ataiga lugha hiyo hiyo. Kama tulivyosema, watoto wanapenda kuiga sana lugha na matendo ya watu wakubwa. Mtoto au hata mtu mzima si jiwe kwamba asibadilike! Wakati fulani shuleni mtoto mmoja mdogo, wa chekechea, alikuja kumshtaki mwenzake kwamba anataka kumbusu. Nikamuuliza uliona wapi watu wakibusu, akasema kwenye runinga. Nikamuuliza mama alikuwa wapi? Akasema mama huwa anakuja usiku, na mimi ninaangalia hicho kipindi na ‘auntie.’

Kupitia TV watu wengi wameamini kwamba ngono kabla ya ndoa, au hata ndani uasherati hauna shida. Asilimia sabini na tano (75%), ya ngono inayoonyeshwa kwenye TV ni kati ya watu ambao hawajaoana, hata kama si vijana. Hii inaonyesha kwamba ngono nje ya ndoa ni nzuri na ya kupendeza. Huu ndio ujumbe ambao watoto wetu wanajifunza kila siku!

Pombe pia inatangazwa sana kwenye runinga. Waigizaji wote, wabaya kwa wazuri wanaonyeshwa wakinywa pombe. Kwa mfano, wanaonyesha kwamba ukitaka kuwa na furaha, lazima unywe pombe, ukiwa na uamuzi mgumu, ukinywa pombe ndio akili itafunguka, ukitaka akili itulie au usahau matatizo yako, pombe ndiyo itakutuliza. Mtoto wangu aliona tangazo Kubra la wanaume wamekaa wakinywa pombe ya Tusker, na maandishi “karibu kwenye meza

ya wanaume! Ndiyo maana vijana wengi wameingilia unywaji wa pombe! , eti ndiyo ishara ya kuwa mwanamume. Picha za mauaji huimarisha tabia ya kuua, na ukatili. Uhai wa mtu unakuwa hauna thamani. Mtazamaji aweza kujifunza na kuambukizwa na tabia hizo. picha za ponografia (umalaya) zinaamsha mwelekeo wa tabia za kikatili, ikiwa pamoja na ukatili wa ngono. Huwezi ukaangalia picha hizi mara kwa mara na usibadilike.

TV pia inapoteza muda sana. Watu wengi wamekuwa ulevi (addicted) kwa runinga. Ukiangalia Tv sana unakuwa mvivu au unakosa hamu ya kufanya mambo ya maana, kama kusoma, na hasa Biblia. Vitabu vinakosa ladha. Akili pia inapumbaa, haifikirii jambo na kulichambua kwa kina. Akili inataka suluhisho la haraka haraka, kama lile la kwenye TV. Unajikuta umebweteka siku nzima na kupoteza muda wa kukaa na watoto wako au wa kufanya vya maana ukitazama vipicha. Nenda kalime upate mazao . wanaocheza picha wapo kazini na wanalipwa,kwanini nawe usilipwe badala ya kuwashabikia?

Mtoto mmoja akasema, afadhali aangalie TV siku nzima, kuliko kucheza nje, eti nje kunamboa. Baiskeli ni zile zile, michezo ya kudandia (swings and slides) ni ile ile! Mtoto mwingine wa miaka 11, aliacha kufanya kazi ya shuleni/nyumbani kwa sababu ya TV. Anasema, 'nisingenyanyuka kutoka kwa TV, hata niliwasahau marafiki zangu.' Mama mmoja akasema, watoto wanaoangalia TV sana, hawana ubunifu; "Wanapoambiwa kuandika insha shuleni, wanaandika mambo au hadithi walizoziona kwenye TV." Nilimuuliza mzazi mmoja wa mtoto niliyekuwa ninafundisha shuleni, kwa nini mtoto wake alikuwa hafanyi kazi ya shule na za nyumbani (homework), mama huyu akasema, "Mwalimu, itabidi unisaidie, mtoto hawezi kunyanyuka toka kwenye Tv, hadi umlazimishe kwenda kulala!" Nikashangaa nitamsaidiaje, kama yeye mwenyewe mzazi aliyenunua hiyo Tv ameshindwa kumzatiti mtoto.

Janet Page ni mke wa Mchungaji anayeshauri wachungaji wengine. Walitutembelea Nairobi kwenye mkutano mkubwa wa wachungaji na wake zao. Wanasimamia pia idara ya maombi katika katika kanisa na wanaishi Washington DC, Marekani. Walitufundisha kuhusu maombi na jinsi ya kulea watoto. Wakati wa kipindi cha maswali, mama mmoja aliuliza; "Inaonekana kwamba sisi wazazi tutaenda mbinguni bila watoto wetu. Tunaomba utuelezee jinsi ya kuwalea watoto, ili twende nao mbinguni."

Mama Page alijibu kwa ufupi tu kwamba "WAOMBEE." Lakini pia akaongezea kwamba; "Unapoomba, ufanye pia sehemu yako. Je, una TV nyumbani mwako?" Akatusomea lile fungu letu la Methali 22:6, kwamba, "Mlee mtoto kwa njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee." Akaongezea kwamba, lakini hata wewe utembee katika 'njia' hiyo. Kwa mfano, kama unataka watoto wasome Biblia, hebu wakuone na wewe ukiisoma. Kama unataka wawe watu wa maombi, hebu wakubahatishe na wewe ukiomba. Kama unataka waende kanisani, hebu uende nao, na kwa wakati unaofaa. Usiwapeleke shuleni, kisha wewe uende kanisani! Au uwahi kibarua kanisani uingie wakati watu wanatoka. Kama unataka wasiangalie runinga basi usiwafukuze waende kulala na wewe ubaki ukiimiliki runinga.

Mama huyu alitushangaza alipotuambia kwamba yeye aliamua akiwa msichana kwamba hatakuwa na TV nyumbani mwake. Alipokuwa anachumbiwa alikuwa anawapa wavulana sharti hili. Mwishowe alimpata mchungaji Page, ambaye ni mume wake hadi sasa. Wakasema wamelea watoto wao bila TV nyumbani mwao! Tulishangaa sana, manake wazungu ndio walituletea TV, na tunafikiria kwamba wanaithamini sana.

Labda haiwezekani kutupa TV kabisa katika karne hii! Nakumbuka watoto wetu walipokuwa wadogo tuliamua kwamba hatutanunua TV. Watoto wakawa wanajificha na kwenda kuangalia kwa majirani. Ilibidi tuwatafute toka kwa jirani mmoja hadi mwingine! Baadaye tuliamua kununua, ili tuwe tunacontrol wenyewe nyumbani, kwa maana huwezi kumuwekea jirani masharti.

Watoto wanaogopa kuchekwa na kuonekana 'tofauti' kama hawana TV kwao. Ni kweli baada ya majuma machache ya kutoona Tv wataonekana tofauti, kwa sababu watakuwa na furaha, watakuwa wachangamfu/wacheshi, watakuwa watulivu, wabunifu, watawajibika kimwili na kiroho na watapendeka. Hii inategemea na mzazi, lakini ushauri unaotolewa ni huu:

Kwanza, watoto wadogo ambao hawajafikia umri wa miaka 6 (mwaka 1- 6), wasione TV kabisa. Pili, watoto wa darasa la pili (miaka 7) na kuendelea wasione TV siku za shule, Jumatatu hadi Ijumaa, ila wanaweza kuona siku za wikendi, lakini siyo zaidi ya vipindi viwili kwa siku. Ukifanya hivyo utaona mabadiliko mara moja kwa mtoto wako. Tofauti kubwa itaonekana katika tabia zao, kati ya siku wanazoangalia Tv na siku wasizoangalia. Ila jihadharini vipindi vya TV usiku na mchana vinazidi kuwa visivyofaa, labda wale wenye madish ya channel Fulani zenye malengo maalumu kama vile Kids TV, son Light, 3ABN, nazo pia saa moja kwa siku inatosha kwani watafanya mengi saa ngapi?. Uwe karibu ukiangalia maana channel zabadilishwa ukiwa mbali.

Tatu, wazazi wanatakiwa wakae chini pamoja na watoto wao, waangalie ratiba ya vipindi vinavyotolewa kwenye TV, kulingana na umri wa mtoto wao. Wakubaliane ni vipindi vingapi na vipi ambavyo mtoto ataviona kwa siku au kwa wiki. Waviandike chini, na mtoto apewe jukumu la kusahihisha kila anapoviona. Hii ni njia nzuri ya kumfundisha mtoto kuwajibika na kujizuia (self control). Pia inamsaidia mtoto kujifunza kufanya maamzi ya maana.

Nne, nunua mashine ya kurekodi, na uwe unarekodi vipindi vizuri ambavyo wataviona wakati ujao. Pia kuna kanda nzuri za DvD ambazo unaweza kuwanunulia watoto na familia kwa ujumla. DVd kama the Visual Bible, Kids time, kujifunza lugha zingine, vipindi vya sayansi n.k

Kama wazazi, tuna jukumu kubwa la kuamua vitu ambavyo watoto wataviingiza akilini mwao. Kumbuka tukiingiza mazuri katika akili zetu, tutavuna mazuri, lakini tukiingiza mabaya, hakuna jingine ila kuvuna mabaya. Jambo ambalo siku hizi pia limeingia ni watoto wetu kuwa na simu zao za mikononi na humo wanasikiliza vitu vyote na hatuna uwezo wa kufanya lolote na jambo hilo. Kijana wa miaka 17 aliyekuwa na simu alisikiliza kuhusu mamboya filosofia na dini za mashariki za 'New age' ambazo hawaamini MUNGU wa mbinguni na wala hawamjui. Alianza kuzungumza kuhusu dini hizo na akaanza kupoteza upendo wake kwa MUNGU wa mbinguni.

Uwepo wa vyombo vya habari unafanya mazingira ya kujenga tabia nzuri za wototo kuwa ngumu zaidi. Utandawazi umeletwa na kufanya jambo linalotokea mahali pamoja linasambaa haraka kote. Wakati wa arusi ya mjukuu wa malkia wa Uingereza inafanywa "ulimwengu wote" ulikuwa unashuhudia. Walionyesha walikuwa wanaishi pamoja kabla

hata ya kuwa mume na mke! Matukio ya vita, ukame, vifo , sensa, na mengine duniani yanashuhudia wakati ule ule au katika masaa machache. Dunia inakuwa kama kijiji kimoja.

Vyombo vya habari ni vizuri kwa watoto kwa kiwango kidogo na hatarishi kwa kiasi kikubwa. Vyombo vya habari husambaza utamaduni mpya na kubadilisha vitu ambavyo jamii inavithamini. Kuangalia televisheni muda mrefu kunapoteza uwezo wa mtu kutambua kati ya ukweli na masimulizi ya kubuni au uongo. Televisheni inasambaza fikara za anasa na kununua nunua visivyohijika (ubaradhifu).

Tunatawaliwa na vyombo vya habari mno kwa makusudi mabaya na mazuri. Maadili yao mengi wanayotaka kutuletea yanahusiana na pesa, ngono chafu na mamlaka; (money, sex and power). Vyombo vya habari ni kama televisheni, radio, sinema , mtandao internet, magazeti , vitabu, majarida. Vyombo hivi vinachangia hisia, mitindo, maoni na mwelekeo wa kumpenda Mungu. Watoto wangu walikataa kula ugali wakiwa wadogo; “Baba chakula chako cha kiafrika utakula mwenyewe, sisi tunataka vile vya kwenye Tv.”

Ni kweli kwamba kuna habari muhimu za kuhitaji kuelimishwa na kuhamasishwa kama sayansi na matukio mengine muhimu. Ila vyombo hivi pia huvuka mipaka ya kuhamasisha na kutoa ushauri, kutia moyo na kuimarisha nia ya watu kwa mambo ambayo si mema. Kwa mfano, magomvi, vita, au mitindo fulani ambayo haiendani kabisa na maadili yanayosaidia adabu kwenye jumuiya au kumcha Mungu. Faida za TV ni chache sana ukilinganisha na hasara, na huja katika furushi moja; sasa utachagua mwenyewe! Siku hizi TV ana dada yake aitwa compyuta. Mabaya yanayosemwa humo mtoto Wako akiyatamka utainamisha kichwa.

Kutokana na umri wao watoto hawatofautishi kuhusu uhalisi wa picha hizo. Kwa watoto wa chini ya miaka mitatu, “wanafikiria kwamba mtu wa Tv akimtazama angeweza kujua anachofanya.” Utafiti unaonyesha kwamba ugomvi na ukatili na maadili mengine mabovu ya ngono vimepunguza maadili mema na hisia za huruma. Mtoto wa nchi za magharibi akiwa mtu mzima anaweza kushuhudia mauaji zaidi ya laki kwa kuangalia Tv kwa muda wa masaa mawili tu kwa siku.

Wakiona matangazo ya biashara baada ya muda wanafikiria wanahitaji bidhaa hiyo. Tusisahau kwamba hii pia ni kwa watu wazima, piga Tv marufuku hata kwa mtu mzima. Matendo yako ndiyo mfano bora. Usingoje waende kulala nawe ukaanza kuangalia picha za ajabu. Watakugundua tu! Chini ya miaka miwili, uangalifu na usikivu wao una mtawanyiko. Baada ya hapo huifanya tv kama sehemu ya mchezo, mwishowe inajenga ulevi na mtoto anafikiri kwamba hiyo ni sehemu muhimu ya maisha ambayo hawezi kuishi bila hiyo.

Tunarudia! Madhara ya vyombo vya habari ni mengi mno kuliko faida kwa kujenga tabia. Watoto wamepoteza masaa ya kujifunza kazi, maana kila siku wanaona Tv. Wanategemea wazazi wawapikie na kuwaletea chakula na kuwafanyia shughuli zote. Kazi inajenga tabia na si TV. Habari nyingine za vyombo si sahihi, zinasifu binadamu mno na

zina upendeleo na ubaguzi kwa yale shetani anayopenda tufanye. Hadithi za mapenzi holela, pesa, ushoga, usagaji, ukimwi, ujambazi, ngono haramu, utajiri wa haraka, mahusiano yaliyovunjika, mitindo ovyo ya mavazi, uchawi, kulewa, umizimu, na uvutaji wa sigara vinatukuzwa. Mtu anaonekana shujaa akifanya maovu kama haya. Na anakuwa kama "ameachwa na basi," asipofanya haya. Hata mtoto akiwa na tabia njema unamfundisha mambo mabaya tena na tena ambayo hakuyajua na kuchafua moyo wake. Hata hivyo kurudia rudia uovu, una nafasi gani ya uovu?

Kati ya filamu saba zilizouzika zaidi ya dola bilioni moja duniani kwa miaka mitano iliyopita, zilihusina na uchawi na mambo ya mizimu. Uchawi na kuutukuza unapamba moto dunia nzima. Wengi wanafikiria kwamba waafrika tu ndio wachawi! Wamegundua kwamba, katika sinema nyingi watu wanafurahia wakizungumzia mambo ya mizimu. Kutukuza uovu kunatokeza bila mtu kujijua! Mtu anajikuta anaimba nyimbo mbovu za matangazo ya biashara bila kufikiri kwa vile ina tune nzuri; mfano, "Tumia chibuku, ni pombe nzuri" x2!

Vipindi vingi vya Tv havina elimu ya watoto hasa hapa Afrika. Kama vipo, vinaonyeshwa muda ambao watoto wapo shuleni au nje ya nyumba. TBC ya Tanzania inaonyesha burudani na michezo ya kuigiza katika muda muhimu. Mchezo wa 'Ua Jekundu,' wa kimapenzi, usaliti, wivu na maisha bandia ulionyeshwa watoto wakiwa nyumbani.

Watoto vijana hupata mtazamo wenye kasoro kutokana na upevu wao. Ugomvi na ukatili huchukua sehemu kubwa hasa kwa wale ambao tayari wana mwelekeo huo. Sinema, video na computer huongeza hali hiyo kihisia na mazoea ya vurugu. Watu wanakuwa si wapenda suluhu au amani, bali wanapenda kulipiza kisasi kama wanavyoona kwa watu wa TV.

Wanapoona kitendo cha kujamiiana , wanajenga ndani yao hali ya kufanya kitendo hiki kiholela na kuwa makahaba au wabakaji. Kwa jumla televisheni si rafiki ya mtu anayempenda Mungu kwa sababu vipindi vyake vimekita kwenye mambo ya ngono isiyo safi, ugomvi, ulevi, ukatili, ponografia, anasa za kidunia, lugha chafu, na tabia chafu. Watoto huwa duni sana kimasomo. Mwelekeo wa kusoma vitabu unakuwa mdogo. Ni watazamaji tu na si watendaji. Udadisi, umakinifu, uchanganuzi unakuwa mdogo sana. Watu wa familia wakiangalia Tv au computer games wanakosa mawasiliano ya msingi baina yao, maongezi yanakoma, na kiu yetu la kuangalia tv inaongezeka. Tv inakuwa kama yaya wa kutunzia watoto. Baada ya muda watoto wanapenda kuangalia tv kuliko kuongea na baba au mama. Familia haichezi pamoja, haijadiliani. Inabomoa madaraja ya familia ya kuwa karibu.

Matangazo ya biashara yana bidhaa, wasanii, anasa, mashindano, tamasha, na urembo wenye utamaduni "unaopendwa" na mtu anatuzwa au kusifiwa kwa kufanya maovu. Wanampa mteja hisia kwamba haijalishi unanunua nini, furaha inapatikana kwa kununua bidhaa hiyo wanayoipigia debe, Madhara ya vyombo vya habari ni kuwa na mambo mengi ambayo hayasaidii kutoa mvuto wa kumcha Mungu. Baada ya kuangalia Tv, au kusoma vitabu au magazeti mengi mtu haoni ladha kabisa ya kusoma neno la Mungu

au kusali! Wewe jaribu tu utajionnea! Katu Watoto hawawezi kujengwa kusoma neno la Mungu na vyombo vya habari!

Kujihami na vyombo vya habari ni kupiga marufuku tv nyumbani mwako unless utaisimamia kikamilifu! Nimeona watoto wakiamka usiku wa manane au wazazi wakitoka wanaangalia Tv au internet (Kompyuta). Nchi nyingine wana channel 900!

Huwezi kuwa kama askari wa magereza kulinda watoto na tv ukafaulu na mashuguli yako yote, mpaka utie nia. Hata hivyo siku hizi hapa Afrika, picha za wasichana wakiwa nusu uchi na za ukatili zinaonyeshwa kila siku, wazi wazi, kwenye matangazo ya biashara kwenye tv ya umma. Vyombo vya habari vina nguvu kama mfuriko wa maji. Watoto na watu wazima walio na hekima ya vitu vya kuangalia, ni nadra sana, hivyo ni bora kuvipigia marufuku.

Kama mzazi unataka kuacha computer yako sebuleni au tv hakikisha una ufahamu mzuri wa kinachotakiwa ili uimiliki kwa uwezo mzuri. Mzazi ajue falsafa, athari, faida, vipindi, saa ngapi na pia mikanda yote inayoingia nyumbani mwake aijue. Ila matangazo ya biashara sijui utayaepaje?

Waone wahusika wa vyombo vya habari pia kwa maoni kwa mambo ambayo hayana maadili, maana wewe ni mteja kwa kusikiliza au kusoma, na wao wanapata faida. Ni muhimu mzazi ajue nguvu za vyombo vya habari kwa watoto wake na utamaduni wake au maisha yake ya kiroho. Siku hizi hata mabasi yana radio zenye maneno na nyimbo chafu mno. Yabidi tuombe!

Yote haya nilipima nikaona sitayaweza, kwangu tunafunga Tv, maana nina watoto wadogo. Tunaweka tu mikanda ya elimu, mahubiri au nyimbo nikiwepo. Tumetoa channel za kawaida. Je, ukiwa na wageni nyumbani kwako na wanataka kuangalia vitu vibaya utawakataza au utawaheshimu, na kuwaacha waendelee tu kuangalia kwako? Yabidi mjadili kabla hawajaja kuwatembelea! Mayaya wanaangalia picha chafu hali watoto wapo! Hii ni shida kubwa. Niliona siku moja kwenye tv Tanzania, tukiwa sebuleni; mimi na mtu na mkwe wake na watoto wadogo, mambo ya aibu kwenye Tv. Kila mmoja alikodolea macho tv, ila hakuna aliyetaka kuzima! Walijionea aibu kimoyoni.

Televisheni na simu vimekuwa vimungu vidogo. Mtoto wako akitukana matusi ya televisheni unachukia, lakini tv yaweza kusema utumbo wowote. Ole wetu na Tv!

Wengi wameulizia usalama wa simu za mkononi kwa watoto, kwa vile ni kitu kipya bado kujua madhara yake, hatutasema mengi. Wakati sigara ilipoingia ilichukua miaka mingi bila kujua kwamba ingeleta shida ya kansa ya mapafu au mdomo, kwa vile haichukui miezi kupata kansa ya mapafu. Matabibu wengi waliofanyia utafiki hili, kama Mercola.com wa Chicago, wanashauri kwamba watoto wadogo wasitumie simu za mikononi, labda iwe ni dharura, kwani mafuvu yao ni membamba na bongo zao zinakua kwa kasi na hivyo kuathiriwa na mionzi kuliko watu wazima. Hata hivyo simu za mikononi zanapoteza mida

yetu mingi ya kuwasaidia watoto maadili, kila saa tuko kwenye “halo halo” na SMS. Watoto wa nchi kama Japani wamepoteza uwezo wa kuwasiliana na kujipatia marafiki maishani kwa vile wapo kwenye vifaa hivi vya teknolojia saa zote, watu kama hawa watakuwa vilema kwenye jumuiya ya watu.

Marafiki zangu wanaofanya kazi kwenye minara ya simu Marekani wamepewa masharti kutokana na mionzi yake, Mmoja aliniambia kwamba mwajiri wake alimpa form na kumwambia kama hana mtoto bado asifanye pale. Ni vizuri kuweka simu hizi kwenye speaker, na kutoweka mifukoni au karibu na mwili. Ni vyema kutotumia wakati ‘charge’ ni ndogo au mahali ambapo mawasiliano yanakuwa na shida (poor reception) kwa vile mionzi inakuwa mikubwa zaidi nyakati hizo.

Sura ya 34
WAZAZI SOLEMBA (SINGLE PARENTING)

Mzazi solemba ni yule ambaye mwenzi wake amekufa, wametengana au wameachana. Yule mzazi aliyebaki ndiye anachukua majukumu yote ya familia ya kimwili, kiroho, kihali na kimali. Hii ni changamoto kubwa hasa katika dunia ya leo, ambayo watu wanaishi mijini bila jamaa au mtu wa karibu. Maisha ya leo katika kulea hata mkiwa wazazi wawili na misongo, uchumi na shuguli ni nyingi na ngumu, sembuse mmoja! Jua kwamba Mungu atakuwa tegemezi au fungu lako (provision) katika matatizo ya maisha.

Mara nyingi mzazi solemba anakuwa mwanamke, ila mara chache anakuwa mwanamume. Wengi wanahangaika wakijaribu kubangaiza maisha wapate riziki kwa watoto wao. Wengi wanapambana na magomvi na mzazi mwenzake, mtoto anaathirika na hapati upendo wa kweli kutoka kwa wazazi ‘wapiganaji.’ Jumuiya iweze kuwasaidia kwa namna moja au nyingine, ili wasione kama wamechukiwa.

Dhamira yako isikushitaki kwamba hujamfanyia mtoto vya kutosha ikiwa umejitahidi kwa uwezo wako. Ni vizuri uwe na marafiki wenzako wanaokuwa wazazi solemba pia. Kuna haja ya kuita watu wa jinsia ile mtoto anayokosa (kina baba au mama) kwenye jumuiya kama nyumba za ibada na kupata maarifa ya kukabiliana na hili. Angalia afya yako na watoto pia. Jenga mawazo chanya, ondoa hasira. Usiyoweza kufanya

yaache, mfano kumlazimisha mzazi mwenzako awe anakupigia simu au ashugulikie mtoto kama hataki. Kuwa na mzazi mwingine mama au baba ni muhimu ila si kila kitu.

Mwache mtoto azungumze na mzazi wake, usifunge mlango. Ugomvi ulikuwa kati yenu wawili, watoto hawahusiki kabisa. Hivyo siyo vizuri kuwadhulumu mawasiliano na baba au mama yao. Huwezi kuwapatia baba au mama mwingine, hata kama utaoa au kuolewa tena. Sema mazuri mbele ya mtoto, kuhusu mwenzako.

Wale kina baba wanaolea watoto, wengine wanasaidiwa na mama, mayaya au dada zao. Jitahidini kuchukua muda na mtoto. Msiache mtoto awe anakuzwa tu na watu wengine bila nyinyi kushugulika. Mpate muda wa kupata masomo kutoka kwa baba wengine, ya kupunguza makali kwa sababu ni jambo jipya kwa wengi.

Tunaona kwenye Biblia mjane wa Sarepta, na Naomi Ruthu 1:20 na I Wafalme 17 na Hanna Luka 2:36 . Utaona kwenye Biblia wazazi solemba walikuwa wanawake. Pengine ni kwa sababu wanaume walioa tena. Mwanamume aweza kuoa akiwa na miaka 70 wakati ambapo mwanamke wa miaka 30 anaweza asiwe na mume wa ndoa. Je, wanawake hawa waishije?

Wamtegemee Mungu kama vile Yer 49:11 inasema, au kama Hanna, wakiomba kwenye hekalu, wawe na matendo mema na kukuza watoto wao katika kumcha Mungu. Waombee familia zao usiku na mchana na familia za kanisani. Wajiepushe na mambo maovu kama usengenyaji, uvivu, na uzinzi. Wafanye kazi ili wawe na vipato vya kulisha familia zao. Watu wanaompenda Mungu wawasaidie na wawaheshimu, hasa wale ambao ni wajane. Wasiwe na ubaguzi kwa wazazi hawa; 1 Tim 5:3, maana hata kama watoto wamezaliwa nje ya ndoa, watoto hawana hatia na pengine mama ameacha maisha ya zamani. Watembelewe, wasaidiwe na kutiwa moyo katika matatizo au huzuni walizo nazo. Washugulishwe kwa shughuli za kufikia na kusaidia wengine ili wasikae kufikiria taabu zao tu.

Kuna wazazi wale ambao walizaa watoto nje au kabla ya ndoa; hebu waishi maisha ya usafi wakiacha tabia zao za zamani. Wasaidiwe na kutowakashifu kwamba wanaishi kama Malaya; kwani hata wanaume waliowapa watoto hawana sifa mbaya kama wale wanawake! Si kwamba watu wengine ni watakatifu kuliko wao, pengine wanafanya mengine kwa siri au hawajashikwa au wana uovu wa aina nyingine. Hebu jamii isifanye matendo ya kumwaibisha na kumsonda kwamba ni janga limempata.

Maisha yako yawe ya kuomba, naye Mungu atakuwa mzazi wa pili. Mzazi solemba ajihesabu kwamba uvumilivu wake utalipa, na watoto wake wanaweza kufanikiwa kama mzazi yoyote yule maana hawa pia ni watoto wa Mungu. Hebu shetani asikufanye uone kwamba hakuna njia ya kutokea kwenye shida yako. Wale wanaovumilia mateso wana taji. Mwenyezi hatakuacha au kukutelekeza.

Wasaidie watoto usiwe na na hasira au chuki, itawaambukiza watoto. Kama ni kitu cha kusamehe jaribu hata mpate msaada ili mweze kuachana na ya kale na kusonga

mbele. Yale unayofanya kama mzazi solemba yanajenga msingi kwa watoto au kuleta makovu. Mruhusu Mungu aponye vidonda vya moyo. Wahitaji kufanya vitu vitakavyokufanya uwe na furaha , kuridhika (fulfillment) na uponyaji.

Epuka kuleta marafiki wa jinsia nyingine boyfriend au girlfriend mara tu baada ya kuwa pweke. Unahitaji wakati wa kufikiri na kupona vidonda, na hata mtoto pia. Mara nyingi si vizuri kumleta kila rafiki mpaka uwe na uhakika mnaenda kuoana. Utafanya mtoto amzoee na kuchanganyikiwa zaidi au mtoto hatapenda kuona unambadili baba au mama yake haraka vile.

Omba peke yako, na pia na watoto wako kila siku. Jikabidhi kwa Mungu. Pengine kipato kimebaki kimoja na hali ni ngumu. Hebu shetani asikupe jaribu la kulalamika kila mara. Mtoto ameshakuwa na upungufu tayari, jaribu usiweke mategemeo makubwa kwa watoto wadogo na wakikosea kitu ukafadhaika mno. Usiweke siri kwamba una mtoto ukioa/kuolewa tena. Siri ya mtoto itafichuka, mtu asiyependa mtoto Wako, hata baadaye wewe hatakupenda.

Mtoto aweza kujisikia upweke akiwa na wenzake kwa ajili ya hali ya familia. Pengine apenda baba yake amsaidie kazi za shule, ampe ushauri au kumsifu kwa kazi nzuri. Mzazi mmoja hawezi yote haya, nawe ukae ukijua kwamba hutaweza kuwa baba na mama wakati huo huo. Ila Ni Mungu tu Atakusaidia. Usiwe na shughuli nyingi ukaacha kujua kinachoendelea kwa mtoto. Mtembelee shuleni, zungumza na walimu na marafiki zake ili ujue hata yale yaliyojificha. Msukumo wa rika upo, uangalie usiwe wa kumkwaza mtoto, maana mtoto aweza kujiunga na makundi mabaya kutafuta kupendwa. Akirudi toka shule kama ana funguo (latch key child) za nyumba jaribu kufuatilia mambo yanavyoendelea.

Ni kweli mzazi solemba anakuwa karibu na mtoto zaidi. ila jaribu mzazi usifanye urafiki na mtoto kama vile mwenzi wako. Utashindwa kumwadilisha ipasavyo. Nimeona wazazi wengine wanalala na mtoto na kutafuta ushauri kwa mtoto mdogo na hii ina athari zake. Wazazi wengine wanawaambia siri zao zote. Mzazi mmoja wa kike, alimwambia binti yake mdogo, wa primary, siri zake zote, hata za maboyfriend wake. Mtoto alikuwa anatuambia shuleni kwamba, “mama ana boyfriend mzungu, na anataka kumuoa!” Hata wakawa wanaenda matembezi yote pamoja na mtoto!!

Wengine wanawadekeza saana kwa kuwapa vitu vingi wanavyotaka na wasivyovitaka, wakifikiria kwamba wasipowapa, watajuta na kutamani kwamba wangekuwa na yule mzazi mwingine. Hii itakuja kuwaharibu baadaye, maana hawatawajibika, na watakuwa waaribifu.

Usigombane na mzazi mwenzio kwenye simu, au uso kwa uso mbele ya mtoto. Usiseme ubaya wake mbele ya mtoto na kuharibu jina lake, na kujipendekeza kwa mtoto. Pia usimtukuze ilhali unajua ameharibu au kumwumiza mtoto.

Wazazi solemba wasaidiane kwanza wamjue Mungu kama mtu yoyote, na kushauriwa mpango wa Mungu wa mtoto kuletwa duniani. Wapendwe na kuzingirwa na watu wa jumuiya, wawe na seminar za kuwasaidia kupunguza makali na machungu ya maisha. Na mwisho wasaidiwe kama kuna uwezekano kutafutiwa waume au wake ili kusudi nao wasiwe pweke.

Ni kazi ya Mungu tu, itakayopunguza makali ya mzazi solemba, mtegemee sana. Kama mzazi mwingine wa mtoto anaishi na anapenda kutekeleza majukumu yake mruhusu, na kama anaepa tafuta ushauri kwa wenye hekima jinsi ya kuchukua hatua za kutafuta mtu wa kuongea naye au kisheria. Pia usipende kuwatwika watoto mzigo wako mzazi, kama una mtoto wa kiume kwamba sasa awe baba au wa kike sasa awe mama. Tathmini jukumu ili wakati mwingine litafanya mtoto alemewe.

Gawa majukumu kwa watoto wakusaidie ili upate muda wa kucheza nao na kuzungumza ila uwe mwangalifu.
Watu wengine wamesema kwamba kukusudia kuwa na mtoto bila mzazi wa pili ni aina ya kunyanyasa watoto! Niliona kwenye gazeti Amerika, dada fulani alifanya mpango wa kuzaa watoto saba kwa madawa teknologia, na alikuwa hana mume! Ni kweli alizaa watoto saba kwa mbegu za kiume za uzazi toka kwa benki za shahawa hizi, hospitalini; ila ilikuwa vigumu kuwalea watoto hao saba, maana alikuwa hana kazi; japo serikali ilikuwa inamsaidia au ustawi wa jamii, jambo hili ni kinyume na maadili mema ya kutunza watoto.

Siku moja tuliita mshauri (counselor) shuleni kwetu, kuongea na wazazi kuhusu malezi na ideal home. Akasema kwamba nyumba yenye mazingira bora kwa ukuaji wa mtoto ni ile yenye baba na mama, akasema ndiyo ideal, ingawaje alisema hatutaepuka kifo, ila talaka tunaweza kuepuka kwa uwezo wa Mungu. Mzazi mmoja akakasirika sana, akainua mkono kumpinga: “Kuna wengine wetu ambao tumeamua kuwa single wazazi solemba, na hatutaki kuolewa, ila kuzaa tu na kutunza watoto wetu wenyewe. Kwa nini unasema hiyo siyo ideal home?”

Nilimpenda sana huyo mama counselor. Alimjibu tu kwa upole kwamba, huo haukuwa mpango wa Mungu. Akamuuliza, Je, unataka kutuambia kwamba, tuwafundishe mabinti zetu kwamba hiyo ni sawa? kutafuta tu mbegu ya mwanaume ikuzalishe, na utunze mtoto peke yako? Shetani ameleta mchanganyiko wa mawazo na mitindo, ambayo inakuwa vigumu kuchanganua mbivu na mbichi au takataka na kisafi. Hebu Mungu wetu aturehemu kwa maamzi magumu kama haya.

Sura ya 35
KUFUNDISHA WATOTO NYUMBANI. (Home schooling.).

Zamani kabla ya mashule watu walifundisha watoto nyumbani. Baadaye watu waliona ni gharama ya muda na pesa, zikabaki familia zilizo matajiri zikiajiri walimu na watoto wakafundishwa nyumbani. Shule nyingi zilikuwa ndogo, zenye darasa moja mpaka la nane katika chumba kimoja, na watoto walifundishwa kama kifamilia.

Nchi nyingi zinaruhusu kufundisha watoto nyumbani hasa wadogo kama mzazi ana uwezo. Jambo hili ni zuri kwani mzazi anapata nafasi ya kuwa na mtoto na kusaidia tabia yake. Niliona shule nyingine, Tanzania na Kenya zina watoto zaidi ya mia moja kwenye darasa! Siku moja niliambiwa kule Mvomero shule ya wanafunzi 700 ilikuwa na mwalimu mmoja. Mzazi anakuwa na mtoto mmoja hadi sita hivi, ni tofauti na yule wa watoto mia moja. Watoto wengi wanafika darasa la tatu bila kujua kusoma, kama mzazi hajashugulika nao. Hebu angalia zaidi haya kwenye tovuti, maana yanawezekana kabisa, yana changamoto kwa vile mtoto anakuona wewe ni mzazi kisha ni mwalimu, ila mtoto anasaidika sana. Wakina mama wengine wanaazimana vitabu. Jaribu kuweka mipangilio vizuri, ili kuwe na utaratibu. Zamani watoto kwenye maandiko matakatifu walifundishwa nyumbani na pale iliposhindikana zilifunguliwa shule maalumu na Manabíi kama Samweli ili jumuiya inayomcha Mungu isaidie wale wasiokuwa na uwezo wa kuelimisha watoto wao, maana silabasi zingine za kileo zina mengi magumu kwa mtoto. Napoishi watoto wote wa shule ya sekondari Wiki muhula uliopita waliambiwa wavae nguo zenye rangi ya upinde kama nembo ya mashoga ili kuadhimisha (awareness) ushoga. Hilo lilikuwa tamko toka kwa mwalimu mkuu na serikali. Tunamwomba Mungu serikali zetu ziweze kutupa uhuru kumpa utukufu Mungu. Tunapoelekea ni pagumu, maana watu waliokuwa na utamaduni huu waliendelea na mambo yao bila kumlazimisha mtu ajiunge nayo, ila sasa wameingia ukali.

Shule ya kwanza ya mtoto ni nyumbani. Mtoto anajifunza kazi zaidi akiwa nyumbani na misukumo ya rika na kuiga tabia na maneno ya wengine inakuwa pungufu. Mtoto anajifunza mengi ambayo yanahusiana na imani na vitu unavyovitahamini. Mfano shule nyingi zinaanza kufundisha watoto wadogo utumiaji wa kondom au ngono isiyo safi inayotoa promotion ya uzinzi au uasherati na uibukaji, epuka uovu huu.

Familia inakuwa na muda wa kuelekezana maadili na tabia njema, hii ni kama familia inafanya sehemu yake. Wazazi wengi wanaona aibu kufundisha watoto mambo yahusuyo jinsia au ngono. Hili ni kosa kubwa, kwani watoto wako wanapaswa kujua kutoka kwa mzazi, kutokana na kimo chao, mambo haya ili wasiingie shidani na waweze kukua inavyopaswa.

Tabia ya uongozi ni rahisi kufundishika nyumbani. Mzazi anajua tabia ya mtoto na jinsi anavyojifunza, hivyo mtoto anajifunza kwa urahisi. Na kama ameelewa somo, hakuna haja ya kungoja watoto wa darasa zima ila mnaendelea mbele. Mtoto ambaye anayejifunza taratibu, (slow learner), mzazi pia anakuwa na nafuu ya kumshugulikia kulinganisha na kusomea shuleni. Kawaida miezi mitatu hadi sita inamtosha mtoto kujifunza kusoma kiswahili. Watoto pia wanajifunza uvumilivu na ualimu kwa kuwafundisha wadogo zao. Watoto wanapenda kujisomea vitabu na kujiongoza wenyewe kwenye madarasa. Unyanyasaji wa watoto kutoka kwa wenzao au uongozi wa shule unakuwa mdogo sana (Bullies)-angalia breakingsilencenow. Shule nyingi inatoa mitihani ya kila mara inayoleta hofu shuleni. Hofu hii inapungua mtoto anapofundishwa nyumbani.

Ila mzazi inapaswa ajifunze na aone mifano ya wale wanaofanya hiyo kazi ili aweze kuwa na ufanisi zaidi, nchi nyingine, kama hapa Marekani, wazazi wanaofundisha watoto wao nyumbani wana klabu yao.

Watoto hujifunza mengi, ya ustadi, kama kupika, useremala, kubajeti pesa, kununua chakula chenye afya, kuomba darasani na kuzungumzia neno la Mungu au mambo ya Kiroho.
Muda unatumika vizuri, hata masaa mawili kwa watoto wadogo yanatosha kwa vile muda haupotei, watoto wakifanya gwaride, kupanga mistari, kungoja mwalimu, ukaguzi, kungoja wapishi, au mapumziko. Wanaweza wakaenda kushugulikia mambo mengi nje ya nyumba kama kulima na kurudi kuendelea na shule.

Watoto wengi wanaosomea nyumbani wamepata maksi juu ya wastani wa watoto wengine. Wazazi ambao wanajishugulisha na taaluma za watoto wao, wana mafanikio makubwa. Watoto pia wako karibu na wazazi na wao wenyewe. Wanathamini wazazi au ndugu zao, hii inapunguza msukumo wa rika (peer pressure). Ni rahisi kushika kazi ya uongozi na kuongoza vizuri.

Mzazi aweza kutunza (save) pesa kwa kutoshughulikia usafiri wa watoto shule, au kufunga chakula cha kwenda nacho shuleni. Pia mtaala (curriculum) ambayo waipenda mwenyewe inayoweza kubadilika na kuchukua mambo mengine ambayo yanatokana na haiba ya mtoto na uwezo wake.

Hasara za wale wanaosoma nyumbani ni chache; kama, kutokuwa na michezo yenye timu Kubra, bendi ya nyimbo au (timu Rasmi). Mzazi ambaye si nadhifu au mvivu, katika ufundishaji wa mazingira ya nyumbani, anamfanya mtoto kuwa mvivu au kuwa nyuma kitaaluma. Pia gharama zake za kununua vitabu mwenyewe na kulipia field trip, na vifaa vya shule.

Wakati mwingine shule hii inaweza kufanya mtoto asipate elimu na mawazo tofauti kuliko ya wazazi. Hili ni gumu hasa kama wazazi hawajali mambo ya kiroho. Wazazi pia wanakuwa busy kwa vile wanafundisha siku nzima na kujitayarisha somo, pia inachukua muda. Na hata kusoma mwishoni mwa wiki. Pia kuna wazazi ambao ni wavivu na hawaweki ratiba vizuri. Kila mara wako kwenye simu, wakiongea na wapitaji wa hapa na pale bila nidhamu. Hili linaweza kuleta makovu kwenye elimu ya watoto. Mara nyingine pia wazazi hawako wazi kwa watoto wakiuliza maswali, ila walimu wengine shuleni

wangekuwa tayari kuelezea lile walilopaswa kujua kama elimu ya mahusiano na jinsia tofauti.

Ni kweli kabisa watoto wengine wanakuwa na usikivu mwingi kwa mtu baki na watakuwa na kazi kuwafundisha nyumbani. Hili nalo ulipime na kuliombea, ila naona kwa mtoto mdogo mpaka darasa la tatu hivi kama unaweza, mfundishie nyumbani. Uzoefu wangu unaonyesha asilimia tisini na tisa ya watoto wanapata faida kubwa wakifundishwa na mzazi aliye mdadisi na kupata maarifa kidogo kuliko mwalimu shuleni hasa katika umri mdogo.

Mafundisho kama nguo za kuvaa na kutumia fedha yaweza kuwa kama “Kutafutia mtoto nguo za mtumba”. Si kwamba ni masikini tu wanaovaa nguo za mtumba. Siku hizi kila mtu anazivaa. Chukua muda kuchagua nguo za watoto ili wawe na mavazi mazuri ya hadhi. Watoto wako wasivae nguo mbaya mbaya na wewe na mume wako mkitembea nao waonekane watoto wa mitaani. Hata wewe mama vaa nguo nzuri nyumbani si lazima utoke nje, watoto wako na mume ndiyo inabidi wakuone ni mzuri si watu wa nje. Watajifunza nao kuvaa vizuri. Usiwe kama vile vifimbo vilivyovalishwa kufukuza ndege shambani! Fua nguo za mtumba vizuri na kuanika kwenye jua kali na kupiga pasi. Usivae nguo ambayo haijafuliwa, waweza kupata magonjwa. Hebu nguo zako na za watoto ziwe za adabu. Zisiwe .

Nguo mara nyingine zinaonyesha tabia ya mtu –kama ni unyenyekevu, usafi, kiburi, tabia mbovu n.k. achana na mambo mengi ya kutoboa watoto masikio na kuwavisha heleni, lipstick au nguo za jinsia nyingine! Acha mtoto akitaka atoboe mwenyewe baadaye, lakini asije kukulaumu kwamba ulimtoboa masikio, pua, n.k. na hapendi.

Sura ya 36
MIFANO YA KAZI AMBAZO UNAWEZA KUWAPA WATOTO KUTOKANA NA UMRI

Kazi ambazo watoto wanaweza kupewa na umri wa wastani (zihusuzo vitu vyao au miili). Umri wao umewekwa kwenye mabano.
Kurudisha nguo za kulalia, kumenya maharage (2-4). Kuweka michezo yao vizuri (2-6) kuvua nguo (2-4). Kuchana nywele (2-5). Kuosha uso na mikono (2-5)
kupiga mswaki (2-5). Kupanga chumba chao (2-8). Kuvaa nguo (3-5) kutandika kitanda (3-7). Kukata kucha, kudeki (5-10). Kuacha choo safi baada ya kutumia (6-10). Kuosha nywele na kuoga vizuri sehemu zote (7-10), kwenda kusuka au kukata nywele (10-16). Kununua sabuni/vifaa vya usafi (8-18)

Shuguli zihusuzo nguo:
kutoa nguo chafu na kwenda kupeleka kufua (4-8). Kuanua nguo (5-9) kusafisha makabati na droo (6-14). Kuosha na Kukunja nguo (6-16) kuanika nguo (8-16) kupiga pasi (11-16). Kubrashi viatu (8-18). Kuosha nguo kwa mashine(9-16) kwenda kununua nguo (11-18). Kuondoa madoa kwenye nguo (12-18)
kufua nguo (9-12). Kukarabati nguo, mashimo na vifungo (12-17)
kushona (12- 18). Kuchambua na kufua nguo kutokana na rangi/uchafu (8-18)

Kazi za ndani ya nyumba:

Kufuta meza (2-5). Kufuta maji yaliyomwagika (3-10). Kupangusa vumbi (3-12)
Kuandaa meza (3-7). Kuondoa vyombo mezani (3-13). Kuokota takataka(4-10)
Kukung'uta zulia dogo (4-8). Kusafisha ukuta (4-12).
Kusafisha milango(4-12). Kufuta Tv, vioo, computa (4-8).
Kulisha wanyama (5-10). Kusafisha choo (5-8). Kusafisha sink na bafu(5-12)
Kutoa takataka (4-10). Kufagia uvunguni (4-10). Kufuta viti (6-11)
Kuchagua sabuni za kuoshea (6-14). Kusafisha vyombo (6-12).
Kuosha vyombo (6-12). Kusafisha vyanuo na brashi (6-8)
Kusugua sakafu na kudeki (6-13). Kusafisha bafu (6-12).
Kusafisha zizi la wanyama (7-13). Kutumia ufagio wa umeme (7-12)
Kusafisha vyombo vya wanyama vya chakula (7-13)
Kuandika ujumbe wa simu au mgeni (7-12). Kufagia na kuzoa (8-12)
Kumwagilia mimea maji (8-14). Kuosha gari, baiskeli (8-16).
Kupalilia (9-13). Kubadilisha mashuka (10-13).
Kubadilisha taa kutokana na nguvu (10-15). Kusafisha mafiga/moto (10-15)
Kubadilisha fyuzi ya umeme (11-18). Kukata majani na michongoma (12-18)
Kuweka mafuta kwenye milango au baiskeli

Kuosha madirisha (13-18). Kuita simu ya mbali (9-13). Kuzibua sink (13-18)
Kupolish sakafu (14-18), kubadilisha bomba (15-18)
Kununua vitu vya kukarabati nyumba (16-18).

Upishi:
Kujua makundi ya vyakula na lishe (5-14). Kuweka chakula kabatini (6-16)
Kutengeneza juisi(6-9). Kutayarisha mikate-sandwich (6-12).
Kutayarisha chakula cha kula shuleni (7-12). Kupima chakula cha kupikwa (7-14)
Kuoka (10-14). Kuchemsha mayai (7-13). Kusoma mapishi (7-12)
Kujua chakula kilichooza(10-18). Kupika chapati maji (pancake) au chapati (10-17)
Kusoma lebo za vyakula vyenye lishe bora (10-15). Kusafisha jiko (12-18)
Kutengeneza kachumbari (11-15). Kukaanga maandazi (10-16)
Kupika ugali (10-16). Kutengeneza mseto wa matunda (13-15)
Kusafisha friji (12-18). Kuchuma mboga (8-12). Kusafisha oven (15-18)
Kwenda kununua chakula cha wiki (13-18).
Kukaanga samaki, kuku au nyama (14-18).

Kutumia pesa:
Uhuru wa kutumia posho ndogo (5-12). Kuhesabu chenji (8-12)
Kujua ubora wa kinachonunuliwa, kama nyanya isiyooza (8-12)
Kulinganisha bei na ubora (10-18). Kufanya bajeti rahisi (12-18)
Kurudisha kitu dukani kama kina hitilafu (10-18).
Kuandika cheki (14-18). Kutunza akiba (10-18).
Kuweka akaunti benki (10-18). Kujua chenji ya pesa (14-18)
Kujua bili za kulipa nyumbani-kodi, maji, simu, umeme (15-18)
Jinsi ya kutumia hundi na kadi za ATM (16-18)

Usafiri na ramani:
Kujua anuani ya nyumba (4-6). Kujua simu ya nyumbani (4-6)
Kusafisha gari/baiskeli (8-14). Kupanda basi/taxi 8-16)
Kukarabati baiskeli (10-15). Kusoma ramani, kupanda basi la mjini (7-14)
Kuweka petroli kwenye gari/pikipiki na kucheki oili (15-18).
Kuweka maji kwenye radieta(16-18). Kubadilisha tairi (16-18)
Kuongeza upepo kwenye tairi (16-18). Kuendesha gari (18)

Ustadi mwingine muhimu:
Kuita simu za dharura –polisi, moto, ugonjwa (5-12)
Kujifunza kuogelea (5-14). Kuazima kitabu maktaba (6-10)
Kujua huduma ya kwanza (10-18). Kupanga sherehe ndogo (12-18)
Kuelewa jinsi ya kutumia dawa na ovadozi (10-18)
Kupaka chumba rangi (12-18). Kupiga chapa (14-18)
Kumwita mwenye nyumba kama nyumba ina shida (14-18)
Kupanga na kusafisha nyumba yote (15-18)

Kusafisha hita ya maji (16-18). Kukata miti (?)
Kukarabati ukuta uliopasuka (16-18). Kusafisha makapeti na sabuni(16-18). Kuua mende, mchwa, panya (?)
Kulima shamba (8-14)

Chati hii itakusaidia ujue mtoto wako alipofikia na jinsi unavyoweza kumsaidia kwa yale yanayopungua au mengine unayotaka ajue. Weka magoli. Angalia upevukaji wa mtoto. Angalia kama mtoto ana masomo mengi darasani na wewe una shughuli nyingi za kusimamia. Fanya yale ya kila siku kama kupika, kufua. Wakati wa likizo waweza kufanya zaidi.
Magoli ni muhimu, mfano:
Tendo:Sulemani ataweza kupangusa vumbi;
Vyombo: akitumia tambara kwa saa moja, kila Jumapili baada ya kifungua kinywa.
Ifanywaje: Mama akute hakuna vumbi kwenye viti, meza na kabati la meko.

Sura 37
NENO LA MUNGU
BONASI- kwa vile ni muhimu mzazi aombe na kusoma neno la Mungu ili aweze kumsaidia mtoto, tumeongezea sura mbili za kusoma neno la Mungu na maombi.

NENO LA MUNGU

Asilimia sitini na tano ya wazazi wengi hawasomi neno la Mungu. Kwenye takwimu za ninapoishi, dai lao ni kwamba hawana muda. Japo karibu kila nyumba ina biblia zaidi ya moja. Hii ni huzuni kwani kule Uchina, India, na mashariki wengi hawajawahi kuona Biblia (forgottenchristmas.org).

Ubora wa Mzazi hautokani na kisomo chake, ila kujilisha kiroho ndiyo kipaumbele. Kila siku akiamka aseme “Bwana nipo hapa, unataka kuniambia nini leo?”. Usiwe mnafiki na kuishi maisha feki na mashughuli mengi, ukajisahau. Unasema kitu ila hukifuati, utajidanganya mwenyewe, na wala si watu! Watagundua mapema, na mara nyingi hawatakwambia. Haya yaliwapata mafarisayo, walijua mengi mpaka kwa nukta. Ila hawakuyafanya.

Mtoto wangu wa miaka saba, aliona nachelewa kutoka ndani ya nyumba kwenda kanisani, akasema mama wewe ni mfarisayo! Nikasema una maana gani? Akasema, “unasema mambo, ila wanaishi maisha tofauti, ila wanategemea wengine wafanye

wanavyosema. Jiulize mwenyewe maswali haya ukisoma zaburi 139 ya unichunguze: Je, mimi ni mkweli? Muwazi? Safi? Au mbinafsi.

Mashughuli mengi yanafanya upunguze ufanisi, na njozi ya wito wako wa kuendeleza karama yako ya uinjilisti. Kristo alikuwa tayari kujibu maswali ya mafarisayo na kukabiliana na yote, kwa vile alitumia muda na Baba yake. Wengi wanaamini kwamba Neno limevuviwa na lina nguvu ila hawalisomi! Inashangaza kwa kiasi fulani, ila kwa sababu shida hiyo iliwahi kunipata, naielewa vizuri.

Wengi walipoulizwa unaisikiaje sauti ya Mungu walijibu kwa maombi na matukio!. Jifunze kupenda Neno la Mungu. Kutokuwa na muda si ukweli, ni kipaumbele, tuna masaa ishirini na manne kwa siku, na mia moja na nane kwa wiki.

Kusoma biblia mwanzo mpaka mwisho, kwa mwendo wa kawaida, huchukua masaa themanini tu. Je, una muda wa kuoga, kupika, kwenda shule au kazi? Basi una muda wa kulisoma Neno. Tusisome kama anayezima moto, wakati wa dharura tu na wakati mambo yameharibika, bali wakati wote. Najua watu ambao wamemaliza kulisoma kwa wiki mbili. Simaanishi tulisome kwa wiki mbili, ila tuna muda wa kulisoma.

Japo nimekuwa mkristo kwa miaka zaidi ya thelathini na mitano. Nimelitilia makini kulisoma miaka michache tu iliyopita.

Shetani ameniibia muda wangu wa mahusiano na Bwana, naomba Mungu anisaidie pale tunutu alipokula. Ni Kama miaka kumi hivi nimetia umakini wa kulisoma kila siku. Zamani nililisoma ila siku nyingine nikiwa na shuguli niliiacha. Kimbilio na kinga yetu ni Neno la Mungu. Endapo unapata barua ya Raisi wa nchi au mtu unayempenda huwezi kusema kwamba huna nafasi ya kusoma. Nilisikia msichana fulani kwenye taarifa ya habari ametuma SMS elfu sita kwa mwezi! Shetani ana mambo ya kutushugulisha, japo mambo hayo ni mazuri tu, na si dhambi, yeye hajali, alimradi yanatupoteza kulenga kwenye shabaha yetu ya NENO.

Zamani watu waliniambia Neno ni tamu kusoma, “Je wanaona nini kitamu?’ Kama mwalimu wangu toka Uingereza, wa miaka 80 alisema; “Siwezi kukaa bila kusoma Neno, lanipa faraja. Ni kitu ambacho nakingoja kwa hamu, nikiamka nikifanye!”. Sasa ndiyo nimeanza kuelewa masikini! Neno linalinda moyo na unyenyekevu. Tuishi kujenga mahusiano na Yesu na si kuwaonyesha watu kwamba unachunguza neno na siku ya hukumu tukataliwe!

Wengi tunaishi kwa mapokeo na kujipurukusha hapa na pale ila hatusomi, mpaka tuwe wazee. kisha tunawalaumu watoto kwamba hawasomi, na wanatujibu “Ninyi mko karibu kufariki hivyo mwahitaji kuwa karibu na Mungu.” Ni nani ajuaye siku yake? Siku hizi haijalishi umri, mtu alala usingizi wa mauti wakati wote. Nashauri wazazi msifanye kosa hili. Watu wengi wanafikiri wale watumishi walioajiriwa saa 11 jioni wakapata mshahara ni sawa kabisa, na wale wa saa 12 asubuhi kwa manufaa! La, hasha! Wale waliokuja asubuhi walijenga mahusiano makubwa na Bwana. Fikiria mtu unayetaka kutumia muda wako wote naye, na ukapata kufanya vile, hautafurahi?

Jifunze kukariri mafungu ya Neno la Mungu na mtoto wako . hili Halina maswali mzazi. wakati wa shida utazidai ahadi, kama unazijua na hiyo ni sababu tosha. Kuna

website ya kusaidia watu kukariri mafungu inaitwa 'FAST memorization of scripture.' Kuna wengine kanisani kwetu wamekariri, mawazo toka kwenye mlima wa Baraka yaani mathayo 5,6 na 7. na kitabu cha Waefeso ambacho ni kitabu kizuri mno kwa mahusiano na ufupi. Kinakusaidia mambo karibu yote kwa muhtasari, jaribu kukariri waefeso, Zaburi 91, Isaya 53, I wakorintho 13 n.k.

Kitabu hichi kikuu, kimeandikwa kwa miaka 1700, kina vitabu 66, sura 1089 na waandishi 40. miaka 400 ilipita kutoka agano la kale kuja agano jipya. Watu hawa hawakuonana ila waliandika kwa mtiririko mmoja. Mambo yaliyotabiriwa kama Danieli 2, Daniel 7, Daniel 8 na mengi yametokea. Anza kusoma hizi sura za Daniel. Baba yangu hakutilia makini kuhusu maandiko, ila alikuwa mwanahistoria, nilipomfunullia Daniel 2 na 7 na kuzungumza mambo ya Alexander mkuu wa Makedonia na falme zile zote, alishangaa akasema, " Kweli ni ajabu, haya tuliyasoma yote kwenye historia." Neno la Mungu lisome, liamini, lithamini, litafakari, likariri, litii na liishi (live it).

Unaona hata Mathayo ananukuu zaidi ya mara 27 agano la kale. Tusisome tu na kushangaa maajabu ya hadithi, kujua majina ya watu na jiografia, bali itubadilishe mioyo na nia zetu. Mungu anazungumza nami katika Neno lake, ananipa hekima, uwazi na mibaraka ninayohitaji. Anahitaji nikae miguuni pake na kumsikiliza. Katika maombi, ni mimi nazungumza naye. Nikisoma Biblia, ni yeye anazungumza nami. Utakuwa kama mti uliopandwa mtoni.

Siku hizi tuna watu wengi wenye shida ya kutojiamini. Wanasaikolojia na wanamapokezi wanatuuzia bidhaa zao ili kutusaidia tutojiamini. Je, mzazi umekata tamaa, na una woga? Je, unahitaji kuwa na tabia yenye kina cha kiroho? Je, una ndoto mbaya za kutisha (nightmare) basi soma kitabu hiki na umkiri Yeye ni Mwenyezi na muumba. Tunaambiwa kwamba mtu anayemwamini Mungu anakuwa kama mti uliopandwa mtoni. Angalia maisha ya wale waliomthamini kama Ayubu, Paulo, Yusufu au Daniel. Mungu alikuwa kiini cha maisha yao. Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya upendo, nguvu na mawazo bora.

Soma biblia na kuiweka kiini cha maisha yako. Mtu ambaye kitabu chake cha Neno la Mungu kimechakaa na kupasuka, kwa kawaida yeye mwenyewe anakuwa hajapasuka au kuvunjika, bali yu imara. Vitabu vinginevyo kwa tabia ni makapi, viko tupu, havina kina. Kita kwenye Neno. Usikae bila ya kusoma kila siku. Kaa ndani ya Muumba, mwombe Roho wa Mungu kabla ya kufungua neno ili uelewe. Hili ni muhimu. Lisome, sikiliza kile Mungu anataka kukwambia, liamini, litii, nawe utafanikiwa.

Katika zaburi 119 tunaona Daudi Akichukua na kulitafakari neno. Amelitaja Neno kama 'amri, shuhuda, kanuni, n.k,' Isome Zaburi 119 mara kwa mara! Watu wengi siku hizi hupoteza muda kuangalia mikanda ya 'kwetu kuzuri', futuhi, na michezo ya kuigiza makanisani badala ya kusoma neno. Yote haya si mabaya, ila yanapoteza shabaha ya kulenga pale tunapohitajika, na adui apenda.

Mikanda ya mahubiri na neno ni muhimu sana, wachache wamerekodi mahubiri au biblia kusikiliza. Nyimbo za kumsifu Mungu, tutafakari maneno na si 'kutumbuizwa tu.' Usigandishe macho yako kwenye kuangalia kanda za 'Kwetu Kuzuri' saa yote, haiwezi

kuchukua nafasi ya NENO, kamwe! Watoto Wako wafundishwe Neno la Mungu na jinsi ya kushare na wengine. Watoto na vijana wengi wanaimba imba tu, ambapo wangeweza kufanya mengine zaidi ikiwemo na kuimba. Watoto waweza kuhudumia watu, kusoma neno, kufundisha wengine n.k

Mara nyingi pia tuna mijadala (debate) kuhusu hoja mbalimbali. Nilisikia Tanzania, balozi wa nchi fulani alikuwa akisema atakuja na shoga wake, nafikiri akimaanisha mwanamume ambaye ameoa mwanamume mwingine! Niliona watu wakiingia mijadala kwamba ni vibaya au vizuri!. Kwa kweli tunayafahamu yale Aliyotuonyesha Mungu; yaani jinsi ya kuoa. Ushoga ni dhambi, na hilo halina mjadala, nukta! Funga majadiliano na usijihusishe nayo tena. Hata kuishi na mwanamke au mwanamume bila ndoa ni dhambi.

Neno la Mungu liko wazi kuhusu mwanamume kuoa mwanamume au mwanamke kuoa mwanamke, usipoteze muda wako kwa debate, full stop. Wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu, ila tuombe msamaha na si kusema si dhambi. Wapaswa kusema, 'Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako,' Zab 119:18.

Biblia ina ukweli mtupu na kweli tu (absolute truth) Neno la Mungu limeidhinishwa mbinguni milele.

Ametuambia kwa kukazia, kwamba ni rahisi mbingu na dunia kupita, bali Neno lake litaishi milele! Hili ni jambo zito sana. Kama huelewi kitu, mwambie Mungu akueleweshe. Maana Yeye awaonyesha watu wadhaifu, ila wenye viburi waweza wapitwe na maana halisi ya fungu hilo. Waweza wabishane usiku na mchana ila wasielewe kitu.

Nilisoma kwenye Seminari moja, na kule watu walikaa kwenye debate(mdahalo) usiku mzima, mfano wakijadili: Je Kristo ni 100% Mungu na 100% binadamu? Wakifika usiku wa manane, wamechoka, wanazungumza kwa kutofikiri sana, na kugombana, gombana. Niliona akili zangu si nyingi na haya sikuyaelewa. Wataalam wanasema ukiwa umechoka na usingizi utendaji wako ni kama mtu aliyekunywa chupa nne za pombe. Nilijiondokea maana yalinipita hewani.

Nashauri hata kama wewe ni mtu wa teknolojia ya CD au vinginevyo, pata kopi halisi ya Biblia. "Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao na kuwaongoza na kwa kuwaadabisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda katika kila tendo jema," anatukumbusha Paulo kwenye 1 Tim 3:16,17.

Neno la Mungu, ni Mamlaka, mamlaka ya Mungu mwenyewe. Mungu akizungumza, tunanyamaza na kufuata, majadiliano ya hilo suala yaishe hapo hapo. Waingereza wanasema; "The Lord says it, and I believe , and that settles it.' Yaani Mungu amesema, naamini, na hilo ndilo hitimisho.

Neno limebadilisha maisha ya watu waliokuwa wenye dhambi na uovu mwingi. Hakuna ambaye alishawahi kusema nilisoma uhasibu ukanibadilisha moyo wangu kuacha wizi. Au hisabati ilibadilisha moyo wangu na kuacha uzinzi. La hasha! ni Biblia tu, yaani Neno la Mungu linalotubadilisha, nafikiri mlei utachunguza katika maisha yako kwamba

unaendelea katika safari na kuzidi kubadilishwa na neno, “Hivyo Bwana Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi.” Neno lake, ndiyo mamlaka pekee na mamlaka ya mwisho.

Wewe unafikiri una mawazo ya hekima, nami pia nafikiri ninayo mengi ya hekima! Hiyo haijalishi, mawazo yangu ya hekima, au yako ya hekima ni upuuzi (irrelevant). Akizungumza Bwana, hatuna haja ya mjadala. Uzoefu wetu si Mamlaka ya Neno la Mungu, waweza kuwa na uzoefu mzuri, lakini unapopingana na Neno la Mungu basi uzoefu huo hauna maana, ni wa kutupilia mbali. uzoefu wako, wakati wote, uupime na Neno, usijiweke wewe kuwa kiini na uzoefu wako, bali Neno la Mungu. Uzoefu wetu si kweli yote (absolute truth). Waumini wengine wanapata mambo ya kutoka kwenye ndoto au mapokeo yanayopingana na Neno la Mungu na kuyahubiri na kukwaza watu. Epuka haya.

Wakristo wengi hapa Marekani wamezungumzia mambo ya Near death Experience kwamba walikufa wakarudi tena kusimulia. Hii inapingana na Neno la Mungu. Ila wengi wameliamini na kupata ndoto nyingi zaidi kuhusu ili. Huu si ufunuo wa Mungu. Wengi wasema ni manabii na Bwana amewafunulia mambo fulani nje ya biblia (extra biblical). Epukana na hawa! Waweza kuonekana wana hari (excited) ila jihadhari. Neno ndiyo mamlaka pekee ya sauti ya Mungu(sole authority). Neno ni sauti ya Mungu, na ufunuo wa Mungu, na siyo kitabu cha saikologia cha kukusaidia maisha (self help book).

Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu zaburi 119:105. Tunza shuhuda za Mungu kwa moyo wako wote, si nusu nusu. Tuombe ombi la Daudi “ Ningependa njia zangu ziwe thabiti, nizitii amri zako, ndipo sitaabika, nikiyaangalia maagizo yako yote, Zab. 119:5.6.

Tuombe toba ya kweli, tukae ndani ya Kristo, Yeye ni mzabibu wa kweli. Kuna waumini waliojichomeka kwa waumini wenzao na wala si ndani ya Bwana. Hii ni hatari kubwa. Ushauri wa Laodikia kwenye ufunuo tatu yabidi tusome mara kwa mara. Nayajua matendo yako (works). Matendo tunayo mengi ya kazi za Mungu ila asema atatutapika. Tunamtia kichefu chefu! Yaani mara nyingine kazi zetu kama walei zamtia kichefu chefu. Tunafikiri tunamfanyia Yeye, kumbe zinamtapisha!

Nimekuwa nikitafakari hili kwa miezi mitano sasa. Nimeomba msamaha kwa Mola kwamba kazi zangu au matendo yasimtapishe. Nisije nikajichosha kwa matendo mengi, ‘works,’ nikijisumbua kumbe ni kichefuchefu tu. Matendo hata ya huduma yaongozwe na Roho wa Mungu.

Ni rahisi kufanya matendo ya Muumini, kuliko kuwa muumini (to do, instead of to be!). Nimegundua hili na naomba Mungu Anisamehe nisijifanyie kazi zangu na kumtapisha, ila niwe ndani yake na kufanya analotaka nifanye na siyo lile nataka.
Soma neno kwa undani. Tulianza kunywa maziwa ila sasa inabidi tule vyakula vigumu. Maombi mazito yabidi yatumwe mbinguni, ombea na wengine unaowafikia. Usiombe na hasira, usione dhambi za wengine tu, ona na zako na kuuungama. Lazima tujikabidhi kwa Mungu na kumpinga shetani. Ni Muumba tu anayeweza kutusaidia kufanya haya.

Tumepewa nguvu za kuishinda dhambi. tunapoanza kuona hatutaona vizuri kama yule kipofu aliyesema; “Naona watu wanatembea kama miti,” ila baadaye aliweza kuona vizuri.

Tunatupa makombora na kusonga mbele (It is a battle and a march). Ni pambano na kusonga mbele. Hatukai pale pale. Kuhesabiwa haki ni kazi ambayo Mungu anafanya kwetu. Ila binadamu yabidi amruhusu Mungu.

Neno la Mungu si kwaajili ya kutujulisha habari, ila kwa ajili ya kutubadilisha (it is not for information, but for transformation). Wanasema watu wanakita kwenye tabia mbali mbali za Mungu. Mungu kama mhukumu, Mungu kama mtawala mwenye nguvu, Mungu kama upendo na mwenye rehema. Yabidi tuyaweke haya yote pamoja, si kuchukua tabia moja tu.

Yasemekana majani hamsini ya tunda la tofaa (apple) yanatoa apple moja, kusoma kwetu Neno kutaonyesha matunda yetu. La sivyo, itakuwa majani tu kama ule mtini na hakuna matunda! Asema “Ndipo sasa kwa matunda yao mtawajua” Tunda hili ni lile tunda la Roho la wagalatia 5. yaani utu wema, upendo, furaha, upole, uvumilivu, imani, n ayote mema.

Neno ni kama nyundo, linagonga na kuweka wazi dhambi, ubaguzi na kila uovu. Zaburi 119:14 yasema, “Nimefurahia njia ya shuhuda zako kama kwamba ni mali nyingi. Ni tamu kuliko asali. Vitu vya ladha nzuri, huli haraka haraka ukamaliza. Unamungunya polepole, ili ufaidi uhondo huo. Basi Neno ni vile vile, usipite ukiwa na haraka, na kuparaza paraza.

Martin Luther mwana matengenezo wa Ujerumani alichukua masaa matatu, hata akiwa busy sana, kusoma na kuomba. Uzazi ni kazi nzito, akili zetu zisikae juu juu tu, “Watu wameniita inabidi niende;” bila kusoma. Kumbuka Kristo mwenyewe aliyeandika Neno alichukua muda kulisoma! Akasema ‘imeandikwa’. Hushangai kwamba hakusema, nalijua ni mimi mwenyewe nimeliandika, sitalisoma?

Neno ni upanga ukatao, ukiangalia hata mawazo. mawazo ya watu yaweza kuwa ya kweli ila, si ukweli kamili. Neno la Mungu ni kioo cha uhalisi. Si kama vile vioo vinavyoonyesha kichwa kikubwa kuliko mwili au miguu mikubwa na kichwa kidogo kwenye maonyesho. Nitajuaje mimi ni nani? Wenzetu wengine wameshasema tumetoka kwa sokwe.

Siku moja nikiwa duka la nguo mtoto wa miaka kumi na sita alinijia akasema, “Mama, si kwa ubaya ila nataka kukuuliza, unatoka Afrika?” nikamwambia “Ndiyo.” Akasema, Je, wanavaa nguo huko?” Nilimweleza kwa uzuri hali halisi. Alishangaa. Wengi wanaamini mambo ya ajabu! Jamaa yangu aliniambia kwamba mmishonari mmoja kule Musoma, miaka ya hamsini, alikuja na nguo za watoto zimeshonwa pa kuingiza mikia! Kwamba huku watu hawajakatika mikia. Wengi wana ukweli pungufu wa mambo halisi.

Neno la Mungu ndilo litakueleza ukweli kamili kwamba wewe ni nani. Halitakudanganya kamwe. Je, unaishi kutokana na Kitabu cha Mungu? Kwa vijana, "Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Zaburi 119:8,9. Siyo kutokana na maisha chuoni, au kijijini mwake.

Tulitembelea chuo kikuu Nairobi, tukitoka Chuo cha Baraton, Eldoret, tukakuta mambo ya ajabu! Katika vyuo vingi Afrika, wavulana na wasichana wanachanganyikana mabwenini, na si siri. Hata mabafu wanatumia pamoja; eti mambo ya kisasa! Wanasema wanafuata wazungu, jinsia zote ni sawa; (Co-education?O Tukaona pazia limeweka kwenye chumba tulichoingia kwenye kitanda kinachofuata. Basi tukilala tukasikia sauti ya mwanamume anakohoa. Nikauliza, "Kuna nini hapa? Wanaishi pamoja?" Bafu zote na choo ni pamoja na kadhalika?

Mambo haya ya kisasa yanayopingana na neno la Mungu yameletea machozi mengi kwa mabinti na vijana wetu. Binti akija likizo unaona unafikiria ni Yule binti yako kumbe tayari ni mke wa mtu! Njia isiyo ya Mungu ina huzuni nyingi. Wakasema hapa si shida eti wanatumia kondom. Nikashangaa, hivi kondom inasaidia kufuta huzuni, na hatia? Je, watu hawajapata shida ya kupata ukimwi au mimba wakiwa na Kondom? Na hata usipopata ukimwi au mimba, bado ni uhalifu mbele za Mungu.

Kweli kuna njia njema machoni pa mtu ila mwisho wake ni majuto. Ni Neno tu litatusaidia. Maana wote tumepotea, ila tutaonaje njia bila Neno? Lo lote, nje ya neno linaleta huzuni nyingi.

Nchi zingine kama Marekani, watu wanaheshimu Neno, kila nyumba inazo, wastani wa nne, ila hawazisomi. Dhambi itakufanya uwe mbali na kitabu hiki, na kitabu hiki kitakufanya uwe mbali na dhambi. Nashauri mzazi, kisome na kukimaliza kila mwaka angalau mara moja. Kisome, kikariri, kitafakari, kinakili, na kitende. Ni sabuni ya dhambi, tafakari kila siku, omba. Neno ni takatifu, linatusafisha kwa miujiza ya Mungu. Linatufanya tuwe watakatifu kwa neema Yake.

Jaribu linapokuja, Roho Mtakatifu analeta kwenye mawazo yale tuliyosoma ili tushinde majaribu. Usisome kutimiza wajibu, tulitafakari, na kuwa watendaji wa neno na si wasemaji au wasomaji tu. Usilalamikie kioo, ambalo ndilo neno. Tusiwe na kichwa kilichojaa maandiko ila moyo uliojaa dhambi. Neno halijatolewa kwetu kutufanya watenda dhambi werevu (smarter sinners) limetolewa litubadilishe. Ni kama ujumbe wa afya si kwa ajili ya tuishi maisha marefu tukitenda dhambi (healthy sinner) bali tubadilike na kufanana na Yeye.

Wahubiri wengine wanaohubiri kwenye Televisheni wamesikika, badala ya kuinua Neno wanasema, "Tuma pesa kwetu, na utapata baraka mingi." Wengine wameonekana kama wana program ya kuomba omba pesa badala ya kulisha watu neno. Ukipata muda wa kuhubiri hadharani, redioni, na popote, epuka hii tabia ya Gehazi. Huyu Alikuwa mtumishi mwema, ila alijali mali kuliko Neno la Mungu.

Bingwa wa upasuaji alikaa kumngoja mgonjwa wake, mgonjwa alipowasili alimkuta mpasuaji anasoma Biblia. Alimwuliza huyu tabibu, "Je, usomaji wa Neno la Mungu unakusaidia kabla ya upasuaji au baada?" Yule mpasuaji alijibu, "Wakati wa upasuaji!"

Ndiyo hivyo kwetu pia, linatusaidia tunapopitia kwenye shuguli zetu za kila siku. Kila siku uwe kwenye Neno. Tunarudia kusema, Lisome! Likariri! Litii!. Kama hauna muda fanya mbinu hii, imenisaidia mimi sana. Sema hivi; "Leo nina shughuli nyingi, sina muda wa kusoma Biblia, hivyo hata muda wa kula sina." Na usile; mpaka umelisoma! Ukikosa milo miwili au mitatu, utatoka spidi na kwenda kulisoma. Ndiyo mbinu (trick) nimetumia na imefanya kazi.

Wimbo wa zamani ulisema

"Milima yote na mabonde, itayeyuka, Neno lake
Bwana imara, litasimama.
Chorus: Simama imara jilinde, neno lake Bwana imara, kesha kila siku uombe ukasimame."

Neno la Mungu si mashauri au maoni! Ni amri, na maneno ya mwisho yenye mamlaka duniani na mbinguni.

Mamilioni ya watu wamelifia Neno hili. Hebu tumwombe Mungu, "Fungua macho yangu nione maajabu ya Neno lako." Utashangaa; kweli ni kipi ambacho neno hili halijachanganua? Lina majibu kwa kila hali unayokutana nayo. Ni kweli, latoka kwa Mungu Mwenyewe. (Open my eyes that I may behold wondrous things in your life).

Mzazi ana shuguli nyingi zinazohusiana na mtoto, atafute riziki, aangalie tabia ya mtoto, amlishe mtoto, amvishe mtoto, aangalie ya taaluma ya mtoto, achanganue marafiki wabaya wa mtoto, ampikie mtoto, ampeleke mtoto ibadani, amfute machozi mtoto, asaidie kulea wajukuu, apange arusi ya mtoto, aende kumtoa mtoto jela, amwuguze mtoto, amwadabishe mtoto, amsomee mtoto maandiko na mengine mengi, je anaweza kufanya yote haya bila msaada au maelekezo toka kwa Mwenyezi Mungu?

Kuna njia mbali mbali za kusoma Neno la Mungu. Pengine hata maelfu! Ila mimi nitasema chache nazozijua:
Kamwe Neno lisisomwe bila kuomba Roho wa Mungu Atuonyeshe kama kioo makosa yetu na kutuvuvia. Tusome ili litusaidie katika kumwongoa mtoto. Si wewe unayeongoa roho (nitamwongoa) bali Mungu. Hata kama unaijua sana, utashangaa mwangaza mwingine utakaoonyeshwa kwenye fungu hilo hilo.; Je, tusipojali Neno? sisi tutaponaje?

Hata watoto watafaidika, Paulo anampa nguvu mtoto wake Timotheo kwamba ameyajua maandiko toka utoto 2 Tim 3:15.. Waweza kusoma kurasa moja kwa siku na kumaliza miaka 3, au tatu kwa siku na kumaliza mwaka. Jaribu, kwa neema za Mungu.

Aina za kusoma:
1. Kusoma kwa sura na baadaye uichambue hiyo sura:
   a. Wazo kuu ni nini? Mfano, wazo kuu la Mwanzo moja ni uumbaji.
   b. Somo linaloongoza ni lipi? (leading subject)
   c. Fungu maalumu ni lipi katika sura hiyo?
   d. Fungu unalolipenda kupita yote ni lipi?
   e. Watu gani wanahusika sura hii?
   f. Sura hii yaonyesha nini kuhusu Bwana?
   g. Ni mfano gani wa muhimu kufuata katika maisha

yako leo? (personalize)

h. Je, kuna ahadi gani kwangu katika sura hii?
i. Kuna jukumu, linalobidi nilitelekeleze kwa mtu fulani baada ya kusoma sura hii?
j. Mambo ya kuombea katika sura hii ni yapi?

2. Kusoma kwa paragrafu.
3. Kusoma kutokana somo au kichwa cha habari (subject). Kama. mifano ya Yesu, maombi ya watu mbali mbali, miujiza, visa, na mazungumzo ya watu waliotajwa.
4. Soma kwa mafungu; mfano, Warumi 8:28
5. Kusoma kutokana na maneno, agano la kale kwenye Kiebrania lina maneno 8,674 na agano jipya maneno 6,000 hivi.
6. Kusoma kutokana na maombi ya watu. Agano la kale lina sala themanini na tatu na na jipya sala arobaini na tisa.
7. Kusoma kutokana na historia ya maisha ya watu. Mfano, Mfalme Daudi au Yusufu, Mume wa Mariam twaona biblia ina Zacharia thelathini kwenye agano la kale, na kumi na watano katika agano jipya. Yona wako saba na Yakobo watano.
8. Kusoma kutokana na unabii uliotimia; mfano, unabii wa Daniel 2 au 7.
9. Kusoma mafungu yote yenye Kristo katika Biblia yote. Luka 24:27, yasema maandiko na manabii yamweleza Yeye.
10. Kusoma kitabu kimoja; mfano, Mathayo yote, kwa siku moja na kuitafakari.
11. kusoma kwa maswali na majibu au kunakili kitabu kizima ukiendelea kutafakari

Sura ya 38
MAOMBI

Maombi kwa mzazi ni kama pumzi, Kuna maombi ya aina mbili. Yale ambayo tunayapanga mfano asubuhi, na jioni. Kisha yale ambayo hatuyapangi, mfano wazo linakuja moyoni na kisha unaendelea kuliombea, na unaendelea kuomba kimoyo moyo siku nzima (Structured and unstructured prayer).
Ni maombi yafanywe kila mara, katika siku nzima bila kukoma! Ombea ushirika wako pia, hata katikati ya wiki nenda ukaombe na ushirika wako. Hii itasaidia watoto wako hata wakikua kuona maombi ya binafsi na ya ushirika ni muhimu. Mungu ametueleza wazi wazi kabisa kwamba, "Nyumba yangu, itaitwa nyumba ya sala." Si ya kuhubiri, kuimba, kusifu au ibada, japo haya ni ya muhimu yatanguliwe na maombi. Usiwe na mlolongo wa programu kanisani bila maombi. Spurgeon wa Uingereza aliyeanza kuhubiri akiwa na miaka 16, alisema ni bora amfundishe mtu mmoja kuomba, kuliko kumi kuhubiri. Maombi yana nguvu na ni funguo za mbingu za kufungua mengi tusiyoweza kama wazazi.

Imenichukua miaka 30 toka nimwamini Bwana kujua hili, kwamba kuwa magotini katika sala ndiyo jambo muhimu. Nilipokuwa mdogo, chini ya miaka sita, nilikuwa namsikia bibi akiomba kwenye nyumba isiyo na dari, saa kumi asubuhi, kwa sauti: "Mungu wa Isaka, Ibrahim na Yakobo...." Nikaona kama anapoteza muda, akiomba kila asubuhi, wala nilikuwa naona hainogi! Sasa ndiyo nagundua, na kuona ladha, aliyokuwa nayo ajuza wa watu! Dunia ina mengi hasa ya kukabili hasa kwetu wazazi.

Mzazi bora ni yule anayepata uongozi wake kutoka kwa Mungu akiomba, na siyo kwenye masemina. Daniel aliomba mara tatu kwa siku au pengine zaidi, tuombe bila kukoma. Kama uko busy kuomba, huwezi kufanya kuwa mzazi bora. Ni lazima kuwalisha, kuwakuza na kuwadumia watu, na haya yote hayawezekani bila maombi; Yer 10:21. Anza siku kwa kusikiliza sauti ya Mungu kwanza. Watoto wanagundua, baada ya muda, kama tu watu wa magotini au wa porojo tu. Tunaona wengine wakiomba hata vituoni mwa mabasi na tunashangaa, angalau wanatimiza wajibu wao. Maombi ndiyo suluhu yetu ya kwanza na si ya mwisho.

Tumwombe Mungu atufanye watu wa maombi ya dhati. Usikae kutatua shida za mtoto bila kutafuta uso wa Mungu. Tujifunze kuitambua sauti ya Mungu. Tafuta watu katika ushirika ambao wako tayari kufanya timu ya maombi ya kuombea watoto kama Momsintouch.org wanaombea watoto wao. Waambie watoto Wako wakuombe pia. Mungu asikia maombi ya watoto. Uwe na list ya watu unaowaombea, kila wiki au kila siku. Waombee uongozi wa Mungu, ulinzi, na mibaraka. Waombee watoto Wako kwa majina na shida walizo nazo. Kusali yaonyesha u tupu, na uko tayari Mungu akuvike. Bila maombi ni kuwa kama meli bila usukani.

Adui mkubwa wa maombi ni nidhamu ya kuomba. Warumi saba isomwe na kila mtu. Yale mema yote lazima uyapangie, huamki asubuhi na kujisikia "nina raha sana kuomba!". Lazima ujikaze na kuomba, ujisikie, usijisikie wewe omba! Kuwa busy, na

kujikimbiza hapa na pale hatukusaidii shuguli ya malezi. Fanya maombi, na kisha kujitoa kikamilifu kuwa kipaumbele. Tafuta patna wa kuomba naye, ikiwa hauwezi kupata omba naye kwenye simu. Yapange vizuri yale unayotaka kuyaombea kisha uyaandike. Kama vile Mungu asivyotutelekeza, nasi hatumtelekezi kwa kuacha maombi. Maombi ndiyo yanayotuwezesha kuwa wazazi bora, wanaofanya mapenzi yake.

Usiwe na maombi kama ya kuzima moto, tukiwa na shida tunapiga mayowe, zikiisha tunapotea kabisa. Mungu ni mwenye huruma, wote tumefanya hivyo. Tukiwa na shida tunaenda kwa Mungu, zikiisha hatuonekani, tunapotea mpaka shida nyingine inapokuja. Mzazi mmoja alipotembelewa na Askofu wake alisema, “Nimemwomba Mungu wee katika maisha yangu ili nipate utajiri, sasa amenipa, nikirudi kuomba tena atasema mbona wewe unaendelea kuniomba nami nimekupa?” Nafikiri ni vyema tutumie neno kusali.

Jambo muhimu ni mahusiano yako na Mungu. Katika Neno la Mungu , Mungu anazungumza na wewe. Biblia ni neno Lake, anazungumza nawe. Mara nyingi twapenda kumwambia Mungu mambo yetu, ila hatuna haja ya kusikia sauti yake. Tuwe na wakati mtulivu pia, wa kusikiliza sauti yake. Mengi yamezungumzwa kuhusu sala katika Neno lake. Kristo aliamka asubuhi akaenda kuomba, alipiga magoti. Kama Yeye alipiga magoti sisi je? Ni vyema kusujudu, labda mazingira yasiwe bora.

Nafurahia sana wapigao magoti bila kuona aibu na kuwa na kanuni za sala. Ni baraka kwetu kwa kadiri tunavyoweza kupiga magoti kwa maombi ya faragha na hadhara; hata mitume walipiga magoti pia. Tunaona kicho cha malaika mbinguni kwa utukufu wake wanafunika nyuso zao, na kusujudu, sisi je tutaponaje, tusipojali haya?

Tuombee tabia zetu, Roho mtakatifu atushukie, ili kufanikisha kazi yetu ya uzazi kila siku. Je, kazi yako yakufanya uwe mtu mwenye maneno ya mkato mkato, mashindano au ubinafsi. Mwombe Mungu akupe nyingine, maana katika hukumu utashindwa kusimama. Kumbuka wayahudi siku ya upatanisho waliacha kazi zao ili wawe na upatanisho na Mungu (at one tent). Ombea mambo kama haya, usiache yakufanye ukose uzima wa milele.

Ombea dhambi, si kitu kidogo. Dhambi yatutenganisha na Mungu wetu. .Tukazanie ombi la Zaburi 139; “Unichunguze njia zangu uone zile zinazoleta majuto.” Dhambi ni hali ya uasi inayofanya Mungu asisikie dua zetu. Tuweke kila kitu kando na kuingia katika Hekalu kama wana Israel siku ya upatanisho. Waliacha kupika na kazi zote, kuutafuta uso wa Mungu.

Mambo mengine hayawezekani mpaka kwa kufunga na kuomba. Shughulikia jambo muhimu kwanza. Somo la kufunga ni refu kidogo. Kwa kifupi nakushauri kama hauna shida yoyote ya afya, kufunga mara moja au mara mbili kwa wiki kunasaidia kiroho na hata kimwili.. Kuna kufunga kwa aina nyingi. Katika kitabu hiki hatutaweza kwenda kwa undani sana. Mifano: Kwa kula vyakula rahisi vya mimea (ondoa nyama, maziwa, samaki, mayai, sukari, vilivyokaangwa, vilivyoungwa sana, vya kukoleza mno, vya kukobolewa na kadhalika); hiyo ni aina ya kufunga. Kufunga kwa kutokula kwa masaa 24, ukinywa maji tu, na kisha kula mlo mmoja tu; kwa siku, kwa siku kumi. Kufunga kwa masaa 72 ukinywa maji tu, na kisha matunda na mboga mboga tu kwa siku saba.

Kunywa maji tu kwa siku saba mpaka arobaini au juisi za matunda na mboga (hii wahitaji tabibu wako aidhinishe). Kufunga kwa siku 21, mfungo wa Daniel 10 (unaacha vinywaji, nyama na mkate). Kwa kweli kuna mifungo mingi. Ila kuacha Kula na kunywa maji tu ndiyo wengi hufanya , labda afya isiruhusu.

Kufunga kwasaidia mwili, roho na jamii. Angalia sura zote za mifungo kwenye biblia kama ile ya Isaya 58 yatueleza saumu ambayo Bwana ataka tufanye. Tunaambiwa tukifunga tusiwe kama mataifa kwa kujionyesha. Twaona kama Yona akihubiri hata watu wote na wanyama wakafunga. Mabadiliko yakatokea na Mungu Akaghairi mabaya bali Yona alikuwa mgumu kuwasamehe. Tunafunga ili kujinyeyekeza kwa Bwana atubadilishe mioyo yetu na kusikia dua zetu. Tunaweza kuwaambia wengine wajiunge nasi, kwani maombi mengi, yana nguvu nyingi.

Mzazi ye yote yule asiye na shida ya afya asipende chakula sana kufikia hatua ya kutofunga. Mzazi asile kila mara bila kuweka nafasi ya kufunga. Hili ni muhimu kama vile maombi yako unavyoyapa nafasi. Kuwa na siku za kuombea familia yako, ushirika wako au hata jumuiya yako, ni muhimu sana.

Maombi ya kufunga siyo tu kuacha chakula, bali kusoma neno na kuomba. Nimefunga mara nyingi nikajikuta niliacha kula ila sijasoma neno wala sijaomba kwa vile niko busy kibaruani, nikitumika kwenye nyumba ya wazee. Kufunga ni kuacha kula kwa kujijenga kiroho. Ukifunga weka muda maalum wa maombi, wengine nimeona wameweka kila baada ya masaa matatu, mpaka walale. Kama saa tisa usiku, saa kumi na mbili asubuhi, saa tatu asubuhi, saa sita mchana, saa tisa alasiri, saa kumi na mbili jioni, saa tatu usiku, na kuendelea. Nafikiri ingekuwa vizuri uombe zaidi ya mara tatu kwa siku ukifunga au zaidi ya unavyoomba siku za kawaida. Modern Manna Ministry by Dan Vierra wana habari kidogo za maombi ya kufunga na maombi.

Kutokana na Neno la Mungu kila mtu anapaswa kufunga, hata mlo mmoja kama ana shida ya afya. Twaona siku ya upatanisho na siku zingine. Narudia!. Susan Wesley wa uingereza alikuwa na watoto 19, nafikiri 16 waliishi mpaka utu uzima. Alihakikisha ameomba na kila mmoja wao na kuwa na mambo ya kufunga. Tayarisha mawazo yako, kupokea baraka toka kwa Bwana na kuwa na ari (attitude) ya kufunga. Hatuhitaji uvuvio zaidi kwamba kufunga ni agizo la Bwana.

Siku hizi nimeona waumini wengi wameng'amua kwamba kufunga huwapa nguvu za kushinda majaribu na kuepuka tamaa za ulafi. Kama unapata majaribu ya kula vyakula vya junkfood, vya kukaanga sana, au vya makolezo mengi na kukobolewa, funga kwa siku tatu kwa kunywa maji tu, kisha matunda na mboga mbichi, uchu wa vyakula vya vikolezo utatoka. Utaona hata machicha ya karoti baada ya kutoa juisi, yana ladha nzuri!

Maombi yako yawe ya imani, bila imani ni vigumu kumpendeza Yeye. Yabidi tuamini yupo, na yuko tayari kutupa thawabu. Thawabu yaweza usiione, ila Mungu atakuonyesha vito vilivyofichika, vya thamani kuu. Usingoje ufunuo maalum ili ufunge. Mtu anayefunga hupata mwangaza maalumu, husaidiwa kiafya, inamsaidia kuipokea haki ya Yesu, kuelewa utukufu wa Mungu. Maombi mengi ya kufunga yajibiwa, ambayo yasingejibiwa. Unapata uongozi wa Mungu na kuridhika. Unaburudishwa na mwili kuuhusishwa (restoration). Kufunga kunaongeza nguvu za mtu.

Kufunga ni msaada wa mambo mengi, yajue ili uyadai. Ukilenga sufuri, utapata sifuri. Daudi amesema kwamba kufunga kunamsaidia awe na unyenyekevu, Zaburi 35:8. Tujinyenyekeze kwa Bwana naye Atatukweza. Yakobo anatuambia tunafunga ili kukaribia karibu na Bwana. Twafunga pia ili kuelewa neno vyema, mawazo yetu yanakuwa shwari bila takataka nyingi, twaelewa neno kwa kina. Tukiwa na shida kama ya Yehoshafati, 2Mambo ya Nyakati 20, twapata suluhisho.

Maombi ya kufunga pia ni huduma kwa ajili ya kuombea wengine wasaidiwe katika shida au mahitaji yao . Je umeshawahi kufunga na kumwombea mwalimu wa mtoto wako? Weka list ya vitu vya kuombea, na ukiirudia baada ya miaka michache utashangaa!

Kama hujawahi kufunga, anza mfungo mfupi kwa kutoa chakula cha usiku, utakuwa umefunga masaa kumi na manane. Ukiwezea hilo, toa milo miwili yaani, kifungua kinywa na chakula cha mchana. Utakuta umefunga kwa masaa ishirini na manne hivi. Kama huna shida ya afya funga masaa sabini na mbili, ukinywa maji. Waebrania 11:6, Mungu anatoa thawabu katika huduma yako, utashangaa Mungu anaibariki ukiomba na kufunga ili ufikie watu.

Ukinuia kufunga, usibadilike badilike ukiona chakula au ukikaribishwa, labda iwe dharura; Daniel 9:3. Ukisikia maumivu ya njaa, chukua muda kusali na kukaa pahali patulivu. Tumbo lako limezoea chakula, utasikia njaa! Usiwe mwoga wa njaa. Kunywa maji, tumbo litatulia kuunguruma unguruma. Kufunga kunafichua matatizo yetu ya kiroho na kimwili, usilaumu kufunga ndiyo kumeleta, ila mshukuru Mungu na mwombe akusaidie suluhisho. Ukizoea mfungo, hutasikia njaa.

Ukifunga kwa muda mrefu kama wiki na ukitaka kufunga kwa matokeo mema, chukua muda kupumzika na kusoma neno, hata uchukue off kazini mwako, fanya mazoezi na kupata hewa bora, itakuongezea nguvu. Kunywa maji mengi hata lita nne au tano kusafisha mwili vizuri na kutumia maji ya vuguvugu ya chumvi asubuhi (salt flush). Waweza kukamua ndimu kwenye maji yako. Usinywe chai wala kahawa. Kama unakunywa chai iwe ya mitishamba (herbs).

Chunga kufunga choo, Kama una shida hiyo, kunywa maji ya chumvi kila asubuhi kwa siku zile za mfungo, kama tumbo halina kitu (salt flush). Chukua vijiko vikubwa vya chumvi viwili, isiyo na madini ya iodine na kuweka kwenye lita ya maji ya mto ya vugu vugu. Kunywa kwa mkupuo. Itafanya uende chooni, ni njia nzuri ya kusafisha mwili. Kwani ukifunga mwili wajisafisha na ukifunga choo uchafu unaosafishwa

unanyonywa tena na mwili, hivyo jitahidi kuuotoa na maji ya chumvi (salt flush) wengine hutumia enema za kahawa, ila maji ya chumvi ni rahisi. Ukishayanywa, uwe karibu na choo. Maana utaenda kama mara mbili tatu na kuacha utumbo wazi na msafi.

Angalia wakati huu mjaribu aja kwako na kukuvamia au kukukatisha tamaa. Jambo muhimu si kuacha chakula, ila kutumia muda wako kujikaribisha na Mungu. Waweza kuona furaha, amani na ucheshi unakutoka. Waweza kuwa na hofu, upweke, wasiwasi na kushuku (doubt) . Usikaribishe hisia hizi zikuandame.

Mathayo 6:16 yatutahadharisha tusijisifie kufunga kwetu kama wanafiki, maana wanameshapata thawabu yao. Najua tukifunga mara nyingine inabidi watu wengine wajue, kama wa nyumbani mwako, ila epuka kujisifu. Hii pia inahusika na kukariri mafungu. Nia ya kufunga au kukariri neno si watu watuone! Endelea na shuguli zako kwa unyenyekevu kama kawaida!

Wachache hupata shida ya vichwa kuuma, kizunguzungu na kichefuchefu. Wataalamu wengi wasema hili lahusika na mwili kusafishwa, na damu ina uchafu unaotolewa (cleansing) mwili ukimaliza kazi, mawazo na mwili huwa shwari. Kama ni dharura ya afya mwone tabibu. Kuyeyusha chakula ni kazi kubwa, na unaacha mwili wako huru kudekiwa siku hizo.

Unapoanza kula tena baada ya mfungo, jihadhari usile kwa pupa. Tumbo litakupa shida, anza na matunda na mboga na vitu rahisi. Tumbo linakuwa kama la mtoto! Pupa ya kula inaharibu mwili baada ya deki nzuri na inabomoa miamko ya kiroho. Tumbo limepungua ukubwa, na ukila unashiba haraka. Ila sasa utaanza kusikia njaa! Baada ya kufunga kwa muda njaa inapotea. Pengine unafikiria vyakula vyote ambavyo ungekula, vile vitamu vitamu usifikirie sana wakati wa mfungo.

Shida hii imetutokea wengi wetu, tukifungua tunakula kwa pupa ili tule vyote ambavyo tuliviacha, hata usiku ukiwa umeshafika! Hii si sawa, huku si kufunga, kwamba uliacha kula mchana sasa usiku ule mpaka usiku wa manane. Ulafi ndiyo dhambi ya kwanza duniani, iliambatana na kutosikia mausia ya Mungu kwa Hawa na Adamu. Kwa vile mboga na matunda twapishanisha. Ukifungua jipe masaa mawili tu hivi ya kula. Saa moja mboga na chakula, pumzika, kisha ule matunda. Baada ya hapo ngoja kesho.

Huu ni wakati mzuri wa kuanza tabia nzuri za afya, na kutupa zile mbovu za zamani kirahisi. Mambo ya kula kama kiwavi au mchwa yapitwe na wakati! Kufunga hakusaidii sana kupunguza unene endapo ukianza kula ufanye pupa, utarudi pale pale.
Kuna aina mbali mbali ya mifungo kwenye Neno, mfano ya siku arobaini bila chakula au maji. Hii kwa binadamu haiwezekani ni Mungu tu. Kristo, Eliya, Musa na Paulo walifanya hivi. Esta na wana wa Israeli walifunga siku tatu bila maji. Kwa hali ya leo hatukushauri kuacha kunywa maji!

Mfungo wa Daniel 10:2-3 alikula vyakula rahisi. Daniel alikuwa ana machozi na huzuni; Mathayo 5:4. Endelea kukutana na kuomba na wengi na ushirika wako kwenye mifungo mingine, maombi mengine yajibiwa mkiwa pamoja na siyo ukiwa peke yako.

Maombi ni kuzungumza na Mungu kama rafiki. Wanasema hatuwezi tukadilisha mawazo ya Mungu. Ila Mungu hughairi jambo kutokana na mabadiliko ya mioyo yetu. Mfano kule Ninawi Najua kabisa Mungu anafurahishwa tukimwomba mambo makubwa. Siwezi kwenda kwa Raisi wa nchi yangu, akasema omba lolote nitakupa, nikaomba chungwa moja au sindano. Tunamtukuza Mungu tukimwomba makuu katika mapenzi yake. Tukiwa tumeungama dhambi zetu ili aweze kusikia dua zetu, Tuwe na imani na ahadi zake, tuombe kutokana na Neno na kudai ahadi zake. Nina imani kwamba mambo mengine Mungu hawezi kutufanyia mpaka tuwe tumeomba! Tudai ahadi zake, “Ombeni mtapewa, tafuteni, mtapata, bisheni mtafungulia. “Hamna kwa sababu hamkuuliza.” Na mimi sitakaa bila kitu kwa sababu ya kutouliza, bali nitauliza! Tuna maneno mengi ya kuzungumza na marafiki, bali wakati wa kuomba tunakaukiwa maneno ya kuzungumza na Mungu, kwanini?

Mzazi anaweza hali mbaya ya uchumi. Usiogope Omba Mungu atajibu nana kukusaidia riziki na watoto wako. Watembelee na watoto watoto na kuhudumia wenye shida. Waonyeshe unajali mahitaji ya familia zao. Usiwe na woga na kujiona duni. Chukua muda kuombea wale kwenye mamlaka pia, maana wakitunga sheria za nchi watakuwa maajenti wa kukuza watoto wetu vyema. Usitegemee nguvu zako kulea, ila omba. Omba! la sivyo, utaishiwa nguvu. Waombee majirani ombea mji Wako, maana watoto Wako wanaathiriwa wanapoishi kama Lutu alipoishi Sodoma. Chukua muda kuomba asubuhi, mchana na jioni na utembeapo wakati wote, omba bila kukoma. Wewe ni balozi wa Mungu pale ulipo

.

Malaika wa mbinguni wanashangaa kwamba Mungu yupo tayari kutoa vingi kwetu, ila hatumwombi! Jambo la ajabu hilo. Lazima tuombe kwa imani. Twaweza kuhamisha milima kwenda au matatizo kuyeyuka kwa maombi?

Soma mafungu yahusuyo maombi katika NENO. Yatakufundisha kanuni za kuomba. Panga siku ya maombi maalumu ya binafsi na hata na wengine

Jiweke wakfu mara uamkapo, piga magoti na kushukuru kwa kuamka, omba msamaha na uongozi wa Mungu. Weka programu zako zote na watoto wako kwake, mwombe uishi ndani Yake Naye ndani yako. Jitoe kikamilifu. Endelea kuwa na mawasiliano na Mungu kwa siku nzima, kama rafiki wa karibu. Zungumza naye, mwachie

masumbufu yako yote. Bwana Anataka kutufanyia makubwa sana, ni bahati yetu namna gani kunywa kwenye chemchem yake ya upendo usio na kifani?

. Tusisite kumtegemea hata kama majibu mengine yatachukua wakati. Maombi ni ufunguo wa imani, kufungua hazina za mbinguni. Bila maombi ni rahisi kuingia majaribuni; Tukiwa na kiu ya haki yake, Yeye atatujaza. Tumeambiwa ombeni, nanyi mtapewa, Tuombe kwa imani, kwamba Yeye yupo na anatoa thawabu. Mara nyingi kwa ajili ya dhambi zetu hatujui chema kwetu, na tusipopokea, tujue kwamba Yeye anajua chema kwetu. Tukija kwake tuwe na roho za rehema na kusamehe wenzetu. Tuwe wepesi, kushukuru kwa kila yale ambayo Bwana anatufanyia. Wanasema Mungu hana la katika kujibu maombi bali ndiyo, ngoja au nina jema zaidi ya lile ulilloomba.

Hatuna haja ya kuwa watauwa na kutumia muda wote kwa maombi, Maisha yetu ya maombi, yajae kumsifu na kumtukuza Mungu, na si kuuliza vitu tu. Mungu wetu ni mwenye huruma na rehema na tusione kama kazi yake ni ya kuleta huzuni kila mara. Tuwe na furaha tukimwabudu . Mungu hafurahi tukimwona Yeye kama bosi asiye na huruma. Hebu daima tumsifu na kumtukuza kwa nyimbo, tunapoomba.

OMBI LA MZAZI na AHADI (PLEDGE)

Mtakatifu Mwenyezi Mungu nimezidiwa na majukumu ya uzazi wewe usipokuwa karibu nami juhudi zangu zitakuwa bure. Nakusifu kwa vile wewe ndiye chemchemi ya furaha, ushindi, shukurani, na yote mema katika maisha yangu. Asante kunipa watoto, ni mbaraka mkubwa.

Nisaidie Baba kulea watoto wangu katika mpango japo sifai na ni mwenye madhaifu mengi. Nisaidie nisiwatukane na kuwakatisha tamaa kwa kuwaita majina ya ovyo na kuwaaibisha. Nisaidie niwatie moyo kwa yale mazuri wanayofanya na kuwakumbatia nikiwazingira kwa maneno ya kuhuisha nafsi. Ninaelewa kabisa kwamba utokana na tabia yangu haya si rahisi!

Nisaidie nishike hatamu ya ulimi wangu wakati ambapo napaswa kusikiliza badala ya kubwatika. Naomba niweze kuwasikiliza pale wanaponihitaji. Unisaidie nisiwasakame sakame. Nirekebishie sauti yangu wakati ambapo nawaadabisha. Niweze kuwa mvumilivu, kuwasaidia wawe na tabia njema na kuweza kuwa watu wa kukabiliana na majukumu yao. Naomba hekima ili nisidai wafanye vile ambavyo haviwezekani.

Naomba niwe na tabasamu kwenye uso wangu. Hebu nyumba yetu ijae furaha na vicheko. Nisaidie nijue wakati wa kuacha kazi kando na kufurahia maisha na watoto. Naamini utanisaidia kujenga nyumba ya furaha na kumbukukumbu njema kwa watoto wangu ambayo itaendelea hata kwa wajukuu wangu.

Nisamehe kwa mapungufu na dhambi ambazo nimezifanya siku za nyuma kuhusu malezi yao. Nisaidie niwasamehe watoto pia. Nisaidie niachane na hasira, manunguniko,

wivu, dhamira ya kunishitaki, na chuki ambayo itafanya nisiwasaidie watoto. Naomba unisaidie niwaonyeshe upendo toka udogo mpaka utu uzima. Hebu wajue upendo kwa sababu wameupata hapa nyumbani.

Watoto wangu ni watoto wako baba. Nawakabidhi kwa mkono hodari. Hebu mfano wangu wa kukupenda na kukutumikia ukawe wao, ili wapende kukutumikia wewe milele na watu ambao wana mahitaji. Nisaidie kujenga tabia yako ndani yao, ambayo ndiyo pekee watayokwenda nayo mbinguni na wala si magari, nguo au mashamba.

Naomba kuliko yote unisaidie uvumilivu wa kujitawala nafsi. Baba sikufundishi kuomba, bali wewe wajua mimi na watoto tunachohitaji kuliko yote kwa malezi bora. Asante kwa vile unaenda kutenda zaidi ya yale niliyokuomba au kufikiri. Nakupenda Mungu wangu, na asante kwa kuwa unajibu maombi kwa maisha ya mbeleni ya hawa watoto. Naamini utatusaidia mahitaji yetu yote katika wakati uliopanga.
Amina
Tarehe----------
Jina----------

Sura ya 39
AFYA ya MZAZI

Napenda kusema kwamba kuna sheria kumi za afya ambazo zinafanya kazi kwa watu wazima na watoto pia. Nazo nitazielezea kwa undani.. kuwa na afya ni kitu cha furaha na pengine kisichukue muda wako mwingi . napenda kuesema hizi sheria kumi ni

Chakula siku hizi kinawekwa kwa kutamanisha vijana, kwenye vikasha vya rangi na picha za kuvutia kwa watoto au vijana. Angalia mabox hayo kwenye maduka makubwa. Hii inawalazimisha wazazi wanunue kwaajili ya matangazo. Gazeti la matatizo ya unene Journal of obesity reviews, linasema lilifanya utafiti wa watoto 367 na kukuta 89% wanakula chakula ambacho hakina lishe nzuri. Vyakula vingi vya watoto madukani vina upungufu wa lishe aidha vina sukari nyingi, mafuta au chumvi. Watoto ambao chukula chao kina kuwa na shida hii wanapata magonjwa mengi wazungu wanaita Junk food. Na kuimba shairi junk food, no good! Wanakuwa na kupungufu wa usikivu , kutofanya vizuri darasani na wanakuwa na shida ya kuchoka. Takwimu ya chama ya kushulikia unene duniani yasema "Kutokula vizuri ni shida kwa maana watoto wengi wana shida ya kisukari imezidi kuliko ilivyo kawaida".

Asilimia 85% ya maswali yote yanaulizwa kwa wahudumu wa afya- madaktari, manesi nk yanahusiana na chakula . ni muhimu sana kuzungumzia mambo ambayo wazazi wanaweza kusaidia afya ya mtoto.

Nayo ni 10.

1. Lishe
2. Mazoezi
3. maji
4. Jua
5. Kiasi
6. Hewa
7. mapumziko
8. kumwamini na kumtegemea Mungu
9. roho ya shukurani(attitude of gratitude)
10. kuhudumia na kujali wengine (community service)

Nitajaribu kuzungumzia haya kwa ufupi. Baada ya uumbaji wa mwanadamu, kila kitu kilikuwa kikamilifu kiroho , kimwili,kijamii na nyanja zote. Baada ya kuanguka maradhi yaliingia na hata kifo. Tujaribu sana kutoigiza mambo hasa yale ambayo hayatusaidii kiafya. Mfano vyakula, hasa vile watu wa magharibi walitufundisha, tunaamini vyakula vyote duniani vinafanana fanana ila matayarisho. Jaribu kupika na kutayarisha vyakula vya asili kwa familia yako. Epuka Vyakula vilivyokobolewa kama sukari, mahindi yaliyotolewa maganda, mikate meupe au ngano iliyokobolewa na mchele usio wa brown. Hivi vinasumisha mwili. Mafuta jitahidi yawe kama ya alzeti, ufuta, mzeitunu au mimea. Mama jifunze kupika vizuri kwa afya. Mtoto wako ale kifungua kinywa vizuri ndiyo chakula muhimu kuliko vyote. chai si kitu cha afya isipokuwa ya miti tofauti na ile chai ya kawaida ya uchina tunayoijua. Mtoto ale matunda, mboga mboga kama karoti, matango, nyanya, viazi, mihogo,uji na vinginevyo. Uji waweza kuwa wa ulezi, uwele, mtama na muhogo. Hizo ni nafaka nzuri na ukichanganya unafanya lishe iwe bora. Rich. Wanasema nafaka zenye rangi na ndogo ndogo ndizo zenye lishe, na hizi ni nafaka zetu za asili, mahindi ni mageni, na mbegu zake zimefanyiwa mengi na wataalamu wa kilimo kama GMO-genetical engineering na kugosishwa? Epuka kula mazao ambazo mbegu zake haziwezi kuota. Ujifunze tiba rahisi za mtoto wako, maana wewe unamjua mtoto wako kuliko mtu mwingine. Siku moja mtoto wangu wa miezi sita alikuwa anagua sikio ear infection, joto lilipanda lilifika 42C na halishuki,nikaenda hospitali. Kufika kule

walimchukua wakamweka kwenye maji yaliyozidi vuguvugu kwenda moto kwa muda dakika 30 wakimwangalia asizame. Basi wakanipa mtoto ,joto limepungua, wakanitoza dola 700 (kama sh milioni moja). Nikawaza hili ningefanya kwangu, nina maji, nina beseni, ila nimetozwa pesa nyingi hivi. Jifunze lishe na mpango wa mbingu wa ulaji wako. Mungu alimwumba binadamu. Yeye anajua ale nini, maelekezo ya chakula na mwili wake amekupa, kama vile mwundaji gari anavyotoa maagizo yakutumia ya gari, hauwezi kuweka maji , ila petroli. Mwanzo 1:29. Najua kabisa tunaishi dunia ya dhambi na pambano kati ya Mungu linaendelea, na kwamba magonjwa mara zingine tunajaribu kufuata kanuni ila yanakuwa magumu. Ila usifanye shingo yako ngumu kwa kutosikiza. Jaribu unavyoweza kufuata mpango wa Mungu hata ukiumwa utasema nimejaribu navyoweza. Ila ukila na kufanya kinyume hata dhamira yako haitakuwa huru.

Tukumbuke kwamba bustani ya Edeni ilitoweka kwaajili ya chakula na itarudishwa kwa kutawala tamaa ya chakula, tunaelezwa kabisa kwa mama Samuel , Samson na wengine yale ambayo waliambiwa wale! Chakula ni muhimu kabla mama hajazaa na baada ya mtoto kuzaliwa! Mfano Waliambiwa wasile nguruwe, pweza,kamba , pombe na wanyama najisi. Maziwa mengi pia yanaonekana na madhara hasa siku hizi, ngombe za kisasa zinafugwa na madawa mengi ya antibiotics na hormones za kuikuza haraka. Nyama ambazo hatuna uhakika kama zimepita ukaguzi vizuri na mengineyo. Chakula cha nafaka mfano uwele, mawese, mtama, mahindi, na jamii ya maharage kama dengu, choroko, njegere, kunde, mbaazi, jamii ya karanga kama nazi, korosho, jamii ya mboga mboga kama mboga za majani, viazi, mihogo, vitunguu saumu, vitunguu, biringanya, ngogwe, karoti, nyanya, vitunguu, matango , hoho, na ina zote za matunda kama maembe, mananasi, machungwa. Tukumbuke kwamba bustani ya Edeni haikuwa na masufuria, fanya chakula chako kiwe dawa na dawa zako ziwe chakula. Watu wengi wanasema maziwa yanasaidia mifupa. Mtoto anapaswa kunyonya maziwa ya mama yake kwa mifupa, ila kwa utafiti wale wenye nchi za utajiri wa maziwa kama Denmark na zingine za magharibi wana shida ya mifupa tu Osteoporosis, hata kuliko sisi ambao tunalamba lamba maziwa kidogo. Maana wasema kwamba wanawake ambao ndiyo wenye shida za kuvunjika vunjika mifupa wale wa kibantu yaani chini ya sahara ndiyo wana mifupa migumu kupita ya wote duniani

Na ni kwaajili ya kutumia mboga za majani, kupata jua la kutosha na kubeba mizigo mizito. Mayai mawili kwa wiki ndiyo afya labda iwe na dhiki fulani ya chakula imetokea. Epuka kuweka chumvi nyingi. Epuka viungo visivyofaa.

Fanya jukumu lako liwe kutunza afya ya kiroho, kimwili, kimawazo, kijamii na kiuchumi. waone jukumu la kutunza afya ni lao. Kuwa na afya bora haimaanishi kwamba itaondoa furaha (au fun!). Mzazi awe mfano kwa kufuata kanuni za afya njema na kujielimisha.

Utafiti umeonyesha watoto wanaokula vyakula vilivyokobolewa vyenye mafuta, sukari na chumvi nyingi uelewaji wao wa masomo ni mdogo, jitahidi usiiigize lishe za magharibi umpapo mtoto wako chakula, uji wa nafaka kama uwele ulezi na mtama au hata ufuta na soya uchanganywe mtoto au watu wazima wanywe. Na kisha viazi, magimbi na ndizi zaweza kuliwa, mwaweza kula ugali pia na mboga au wali usiokobolea asubuhi.

Watoto hurithi chakula na tabia za afya toka kwa wazazi wao. Usiwe mwigizaji wa vyakula vibovu, eti mwaona kwenye Tv mwaishi kuiulaya. Waulaya wameshtuka sasa wamo mbioni kufanya matengenezo. Watoto wengi wameanza kuwa na unene wa ajabu kama majabali ambayo yalioonekana magharibi. Siku hizi watoto wengi wamegundulika na ugonjwa wa moyo kabla hawajafikisha miaka 16. Anza kumtambulisha mtoto vyakula vya afya aozee ladha, unakirudia tena mara kadhaa. Mfundishe mambo yahusuyo lishe na

mpango wa lishe kwa mtoto kimwili, kiakili na kiroho, tunaona kijana Samsoni alishindwa kutawala tamaa zake, hata asali iliyo kwenye mzoga najisi wa simba anakula tu. Alishindwa kutawala tamaa zake, nayo yakawa maanguko yake. Kula vyakula rahisi (simple foods). Hii ni muhimu zaidi ya kufunga! Inabadilisha ladha yako kuleta uchu wa kula vyakula vya kuamsha tamaa ya ulafi. Mara nyingi twataka kuonekana wa kisasa kwa kuwapa watoto mapocho pocho. Nikilea watoto wangu nilibeba thermos la uji na kuwapa nyanya, ndizi na matango . marafiki na watu wengi walikuwa wakishangaa na kucheka kwa kuzomea "uko marekani unakula vya kijijini Afrika". Waliona ni ushamba mwingi na au kutokuwa na maendeleo. " Kweli huyo mtoto atakula hayo?" Watoto walikula na kufurahi sana ila walipoanza shule marafiki na walimu waliwapa siasa zingine za chips tukayumbayumba ila baadaye kwa neema za Mungu wanaendelea kugundua vipi vya afya, na tunaendelea kufundishana ni safari ambayo Bwana anatupa nguvu na si safari rahisi, kwani tuna mapambano mengi bado.. Waafrika waliokuja kutembelea watoto wao watu wazima magharibi, walitumia, juice, maziwa , chips, nyama na vingine. Japo hawa wazazi wengi wa kiafrika walikula vitu vizuri vya asili, bali kisomo walichokipata na kutembea nchi zingine kiliwaathiri mtazamo ule wa asili kwa Mungu alivyotuumba tule. Walianza kupata magonjwa ya kisukari na mengineyo wakarudi kwenye vitu vya asili walivyokua navyo. Ama kweli mpango wa MUNGU wa chakula ndiyo tunapaswa kuufuata.
Nimetembea kwenye mabasi, na makanisani na nimekuta watu wengi wakija na vitu vya ajabu nakuwapa watoto vitu ambavyo wakifika umri mdogo tu wataanza kuwa na magonjwa yale yanayoharibu miili. Wazazi wengi waliacha kunyonyesha watoto. Jambo hilo lilitokea magharibi miaka michache iliyopita , wakina mama walisema wanadai haki, nakutaka kuwa huru wasinyonyeshe watoto, ila sasa shida ya kisukari na nyingine zimengia na wanawake wa magharibi wengi wameanza kunyonyesha tena. Mungu aliyeiumba miili yetu ajua lishe bora ya mtoto ni maziwa ya mama. haya yana lishe ya mtoto anayetembea baada ya mwaka na si kwa siku ile ile anayozaliwa kama ndama.
Jitahidi watoto wako wasiwe wanakula ovyo ovyo siku nzima. Wapate muda wa saa 5 wa tumbo kupumzika. Jaribu kuoka chakula badala ya kukaanga, watoto wasile bila njaa kwa sababu chakula kipo. Wakitaka kitu chenye sukari wape matunda. Usitumie sana chakula kama zawadi kwa mtoto utafanya mtoto awe mlafi. Wakati wa chakula uwe wakati wa utulivu si wa kugombeza mtoto na kukosoa, inafanya myeyusho wa chakula usiwe mzuri. Tafuta muda mzuri wa kuzungumza na mtoto na kumrudi. Jaribu kutengeza chakula cha mtoto, badala ya kumpa pesa za kununua chakula shule maana mara nyingi kitakuwa si kile cha afya sana, mpaka uwe na uhakika. Ukiwa dukani pata nafasi ya kufundisha watoto lishe, gharama zake na pia wasome vizuri lebo za maneno kwenye vipakiti vya chakula.si lazima uende shule kwa upishi ila jifunze tu kufanya upishi wako rahisi kwa kutumia marafiki, ndugu na vitabu. Tunaajiri watu wa taaluma kutengeneza nyumba zetu, kushona nguo zetu hata bustani zetu. Ila wapishi wetu hawana elimu yoyote ya kupika vyakula vya lishe. Hili ni kosa. Afadhali uwe na mshoni asiyeelimika kuliko mpishi asiyeelimika. Watoto wajumuishwe kutengeneza chakula, mle pamoja na utoe mfano kwa mtoto wako. Mama mwingine alimwambia mwenzake "una bahati mtoto wako anakula mboga, wangu hali" . yule mama akamwuliza yule mama " je wewe mwenyewe unakula mboga?" " akasema la sipendi mboga na maharage ni za watu masikini" . Mtoto unayeanza naye kumfanya apende mboga mzawadishe kwa mambo madogo madogo. Nunua vitabu vya kupendeza vya lishe kwa watoto wako wasome. Mtoto ale matunda angalau 5 kwa siku, matunda yana rangi nzuri na ladha watoto hufurahia, panda nyumbani pako pia. Matunda ya vitamin na madini mengi. Usiweke miti

ya kupendeza macho tu bali ya kula. Watoto waweza kuchagua chakula kama yawezekana ila uwe uchaguzi unaowezekana. Mtoto ale ashibe ila asijenge tabia ya ulafi, usiweke vyakula vingi kwa wakati mmoja,yaharibu tumbo, yajenga uharibifu, na pia itafanya asitawale tabia ya uroho. Watoto walio wanene sana wamefika hapa afrika jambo ambalo halikuwepo. Watoto hawa hawajiamini, wanachekwa na wenzao na wana riski ya magonjwa. Wajulishe watoto kwamba vyakula vingi vya mahotel si vyema (fast foods) vina mafuta, chumvi na sukari nyingi.

Watu wengi waliokuwa na kufunga choo ni kwaajili ya kutokula mboga na matunda. Mtoto asiende chooni akachukua muda kusukuma kinyesi kitoke. Watu wengine wameathiri moyo kwa kusukuma kinyesi kwa nguvu. Mavi yasiwe kama ya mbuzi kwajili ya kufunga choo ila yawe yanaelea, na shep yake iwe kama s hivi . kuonyesha utumbo mkubwa una afya. Rangi iwe ya brown ya kijani kama anakula mchanganyiko unaotakiwa kwa ratio yake.

Lishe yajenga maisha ya mtoto ya taaluma, na pia kinga ya mwili. Magonjwa kama kukohoa na mafua yanaweza kupungua kirahisi na lishe nzuri na hii si siri wala uhitaji kuwa inginia wa roketi kujua hili.

Mazoezi ni muhimu sana, kama mtoto aweza kutembea shule ni muhimu watoto hata wa miaka 4 waweze kutembea km 3 kwa siku. Mazoezi yajenga mifupa na kupunguza osteoporosis, watoto wapate muda wa kucheza. Mtazamo wa kijamii na kujithamini unaongezwa sana na mazoezi.

Watoto wajifunze kunywa maji, maana asilimia 80% ya mwili ni maji, mtoto kama wa miaka 4 anywe glass 4 za maji kuanzia miaka 9 mtoto aweza kunywa glass sita na baada ya miaka 12 anywe maji kama mtu mzima. Asingoje mkojo uwe mwekundu au asikie kiu, maana mwili utakuwa umeshapungukiwa na maji.

Mtoto ajifundishwe mwili unavyofanya kazi , sayansi hii ni ya muhimu kwa afya. Mtoto afundishwe unadhifu na usafi. Ni muhimu kwa afya. Watoto wawe na jukumu kufanya mahali wanapolala nadhifu, wakaguliwe . hebu chumba chao kiwe cha kuvutia hata kama hauna pesa waweza kukipamba chumba kwa pesa ndogo au bila pesa. Vitu vilivyotapakaa ndani ya chumba vinaleta msongo wa mawazo nakufanya kutotilia makini vitu. Weka mipaka ya kulala. Watoto wako wasilale na kila mtu! Hii imeleta shida. Hata ukisafiri nao afadhali walale kwenye sakafu kuliko kulala na watu hapa na pale. Walinde watoto wako kutokana na hatari za msukumo wa rika. Hizi zaweza kufanya watoto wasipende shule, wasiwe watii, waingie kwenye ulevi au tabia zisizo na afya. Sisitiza maisha ya usafi wa moyo na mwili kwa afya njema.

Hakuna jambo la muhimu kwa afya njema kama mama anayekaa na watoto wake nyumbani na kuwafundisha kwa upendo na upole mambo ya maisha, kupika chakula bora na kanuni za afya. Wafundishe kwa njia zote hatari za afya zao. Darasa laweza kuwa nje, au ndani ya nyumba. Jaribu mambo yawe ya kufurahisha na kupendeza, si marefu ya kuchosha. Wafundishe na siyo kuwaambia tu! Waambiwe uvivu unaua. Wajue chakula kinacholiwa kwa jasho kina ladha nzuri! Wafanye kazi kabla ya kucheza!

Kumbuka watoto ni watu, na kama vile tunavyokuwa na huzuni kama watu wazima, watoto pia wanahisia hizo hizo. Shetani pia anawateza kwa njia mbali mbali, mara zingine wanakasirika kwaajili ya maneno yetu. Tusikwaze watoto na kuwaambia maneno ya kukasirisha bila sababu kwa vile tuna jazba Fulani. Watoto wakikasirika sisi wazazi hatujui jinsi ya kushugulika na hili na hii inafanya watoto wasikie vibaya moyoni na kuhuzunika. Hebu ujue hawa nao ni binadamu na siyo mahali pa kumalizia hasira zako! Tusiishi kwa harara, wivu, chuki ambazo zitaendelea kwa watoto pia kisha tunashangaa kumbe ni sisi

tumezileta. Wakati mwingine tunaposhindwa kuwa wa faraja kwa watoto hata watoto nao hawawezi kuwa wa faraja kwetu. Jifunze hisia ya kila mtoto, na kuona jinsi wanavyohusiana na wengine. Kulazimisha kukunja nia ya mtoto sana kwa kila jambo ni kosa. Akili ni tofauti na wakati mwingine usipotumia hekima waweza kuleta uasi ndani ya moyo wakati wewe unafikiri unajenga. Mtoto mmoja aliambiwa kukaa, na akasema angependa kusimama (palikuwa mahali ambapo angempa uhuru mtoto) mwishowe mzazi aliposisitiza mtoto alisema " mama nimekaa tu kwa vile umeniambia ila moyoni nimesimama!". Jua tabia ya mtoto ili ulete badiliko la moyoni. Mara nyingi watoto wenye nia ngumu wakiongozwa na Mungu na mzazi vizuri wanakuwa majitu makubwa katika kufanya vitu vingi vizuri , maana wana msimamo mkali. Angalia jinsi tabia ya mtoto ilivyo na yawezaje kumfanya awe mtu bora. Uwaongoze ila usiwaburuze.

Wajifunze kwamba wana uwezo mkubwa mikononi mwao kufanya maisha yawe ya kupendeza au kuhuzunisha. Neno la mungu liwe la muhimu sana katika mafundisho kwani lina mengi ya kulinda afya.

Watoto wengi duniani wana upungufu wa vit D na jua. Nilikuwa naivasha mwaka huu na kuambiwa na kuambiwa vituo Fulani vya kutunzia watoto vilikuwa vina nafasi ndogo. Watoto hawakuwa na pakucheza, hivyo hawakuota jua na wanafika kule asubuhi sana, na kutoka jioni bila kuota jua. Waligundulika na rickets, yaani mifupa kupinda. Hii shida ni zaidi ya mifupa maana ina athari zingine kwenye mwili. Wazazi, mtoto ahitaji angalau saa moja ya jua la asubuhi. Mtoto anahitaji nafasi ya kukunjua viungo vyake kwa kucheza na kuruka. Asikae siku nzima kwenye desk. Kwa kweli mtoto ni vizuri aende shule baada ya miaka saba. Kabla ya hapo afurahie maua, milima, vipepeo, majani na uumbaji. Huyo atakuwa mtoto mwenye afya kamili katika nyanja zote nazo ni kiroho, kimwili, kijamii na kiakii. Tufunze watoto wetu kuwa na kiasi, kutotumia kabisa vile vibaya na vile vizuri kuvitumia kwa kiasi. Tufundishe watoto kubalance shule, mambo ya kiroho na ya kijamii, watoto wasiwe na msukumo wa kufanana na watu Fulani na kukimbilia mambo Fulani ya kufanaana na jirani au rafiki Fulani. Balance shule na homework. Mtoto acheze na kufurahi, yamfanya aweze kueleeza hisa zake. Watoto wengi siku hizi wamegunduliwa na magonjwa ya sonona (akili) au depression, kwaajili ya kwenda shule mapema sana. Wengine waamka saa 10 usiku na wazazi na kwenda kuwahi mabasi. Watakuwa wafanyakazi maisha yao yote. Mambo ya watoto wadogo kwenda shule si kujifunza, ila kuruhusu vibarua kwa wakina mama. Narudia mtoto ni vyema awe huru akiangalia uumbaji mpaka miaka 7. hakuna masomo ambayo mama atashindwa kumfundisha mtoto nyumbani. Na hata asijue kusoma kuna kazi nyingi za nyumbani na michezo mingi ambayo inakuza akili mno , hata kuzidi masomo! Natoa mfano wa Rais Nyerere wa Tanzania aliyeanza shule kwa miaka 11 na kumaliza shahada ya pili masters akiwa na miaka 27 kwa kuruka madarasa pengine! Watu wengi wajivunia watoto wadogo kwa kusema amejua kusoma na miaka 2. si jambo zuri kiafya mtoto wako umkalize asome kwa miaka hiyo! Labda apende kujifunza menyewe kwa njia isiyo rasmi.

Walimu wa magharibi wamegundua michezo na kazi ndiyo nzuri ila kusoma mapema huathiri akili. Mtoto anapungua umakini na kumfanya aruke vitu vingine vyema kwa maisha. Mtoto asiwe kwenye mfumo rasmi akiwa mchanga vile. Watu kama Michael Jackson na wengine wameonyesha wanasaikologia wa watoto wengi kwamba mtoto akianza mifumo rasmi (formal education) au kuigiza na drill zingine anaruka vingi ambavyo ukubwani inaleta magonjwa ya hisia na akili kama sonona. Si vyema mtoto aende shule ya Bweni akiwa mdogo, mengi hutaweza kumfundisha ya kufaa afya , ni vizuri aende baada ya miaka 12 na kwa wengi hata hii 12 ni mapema sana. Mtoto mdogo

anayetambaa mazingira yawe safi, akiokota na kula vitu vidogo ana hatari ya kupaliwa. Mifugo na kinyesi chao mtoto kushika inabidi umakini. Ni vyema viatu vitolewe nje na visiingie ndani maana ni hatari kwa mtoto na watu wazima kuleta uchafu wa mji wote kwenye nyumba yako. Chemsha maji ya kunywa mara zote. Uwe na mpango wa huduma ya kwanza kama mtoto amekula sumu au ameumia. Unga wa mkaa unafaa sana kwa sumu, uliza kituo cha afya kuhusu huduma ya kwanza unapoishi. Mtoto asichezee mifuko yoyote ya plastic na kujivisha anaweza akose pumzi. Vyakula vingine kama zabibu mwiko kumpa mtoto mdogo bila kuponda imeua watoto kadhaa.

Muwe na ratiba ya kufanya mambo, mtoto wako asikuone huna kiasi, asikuone unakunywa pombe, kahawa, sigara au madawa ya kulevya na unamkataza pro 20:1. Asikuone una misongo mingi ukijikimbiza hapa na pale bila sababu, Matendo yako ndiyo mahubiri na mifano kwake. Mfunze mtoto jinsi ya kugawa majukumu yake ili asiwe na msongo. Kazi ni mbaraka kubwa kwa mtoto, wasema akili isiyo na la kufanya ni karakana au gereji ya shetani. Hebu mtoto asikae kivivu. Mtoto alale kwenye chumba chenye hewa bora, madirisha yafunguliwe hata usiku. Uchafuzi wa hewa kwa viwanda na magari ni mgumu kwa mapafu. Wasema tuishi vijijini ila sasa asilimia 50% Ya watu huishi mijini, hata tabia wasema wataalamu ya watoto ni rahisi kujengeka mara 10 bora zaidi vijijini zaidi ya mijini. Watoto watajifunza kulima na kujitegemea, hawatakuwa na njaa. Pia kuishi mjini bila kazi na magenge kutatoweka. Watoto wajifunze kupumua vizuri kwa kuvuta pumzi kwa ndani(deep breathing). Watoto wa kwenye viwanda vingi vya mkaa kama uchina wanampaka asilimia 50 ya asthma.

Mtoto apate muda wa kulala. Mtoto awe na mazingira matulivu, si kelele na kuharakisha mambo mara kukimbia huku na kule. Mtoto akizaliwa aweza kulala masaa 22.mtoto wa miaka 4-6 muda wa masaa 12 mpaka 14 na mtoto wa miaka 10 mpaka masaa 10 ni sawa atakofikia 16 masaa 9 ni sawa. Pia kupumzika siku moja ya juma ni muhimu. Mzunguko wa mwili wa binadamu uliumbwa apumzike siku moja kwa wiki circadian rhythm. " akastarehe akapumzika akaitakasa Sabato... ". Mtu asiyepumzika ana misongo inayotoa vichocheo vibaya kwenye mwili (cortisol) na kuchoka. Athari za kutolala ni kuwa na kisukari , presha,infection, ajali, kutotulia hyperactivity, kunenepa ovyo na mengineyo.watoto wasitazame televisheni au kunywa kahawa kabla ya kulala, na wawe na muda maalumu wa kulala watangulie kulala kabla ya watu wazima. Wataalam wasema mtoto wa chini ya miaka miwili asitazame Tv kabisa. Inaathiri hisia na macho. Familia iwe na maombi ya asubuhi na jioni. Haya ni ya muhimu katika malezi na afya ya watoto. Matumaini na imani inafanya mtoto akomae na kukua vyema. Wasomee hadithi za mafundisho ya Dunia na ya Neno la Mungu. fundisha watoto kutokuwa na harara, wafundishe watoto kumtumaini Mungu na watu pia wasiwe watu wa kushuku shuku watu, na wasiwasi. Ili linachukua muda na watoto wataona mtu wa kumwamini, na kwa namna gani. Wanasema watoto wanaosomewa wanajifunza vizuri kuandika kuliko wanaoangalia Tv. Wa TV wanakuwa hawana mawazo ya ubunifu (imagination) na kuandika imla inakuwa shida.

Kuwa na imani kunasaidia kijamii na kihisia, waexpose watoto wako kwa watu wa kuaminika ili wajenge kuamini watu kiafya. Watoto wanapenda mahali penye
usalama security . watoto wakiwa wadogo tunawakumbatia ila wakiwa wakubwa tunaweza kuwaonyesha assurance kwa njia mbali mbali.

Wafundishe pia watoto wako kwa matendo ukisema kitu waweza kukutegemea .

Watu wengine wameniuliza maswali kama ya kutumia microwave, kuzibwa meno kwa zebaki, kutumia fluorine kwa watoto kuoshea meno kwa mganga wa meno na kuziba

meno yaliyotoboka sana kwa kuua mzizi wa jino(root canal). Napenda kusema mimi si mtaalamu sana ila tabibu niliowaita kuzungumzia shida hizi kama Dr Agatha Thrash na Mercola
Ucheepines.org na mercola.com walinifanya nifikie uamuzi huu
Microwave ni mbaya kwa mwili wako, ukinyweeshea maji ya microwave mmea baada ya muda utakufa, fanya majaribio hayo na ukanyweshea mimea miwili mmoja na maji ya microwave na mwingine maji ya kawaida. Plastic nyingi zinayeyuka na zina sumu za dion, usitumie chupa ya plastic ya maji zaidi ya mara mbili! Watu wengine wamepata kansa kwaajili ya plastic nyingi kwenye mwili. Plastic yenye namba kubwa kwenye kitako ndiyo nzito kidogo na nzuri, ila kama namba ni ndogo kama 1, 2 au 3 inayeyuka zaidi. Usiweke chupa ya plastik maji moto au barafu kisha unywe utakunywa plastic nyingi. Na usiitumie mara mbili tatu, tupa, inalika mno. Jaribu kutumia vyombo vya udongo au chuma ya stainless steel kuliko plastic. Zebaki nyingi kwenye meno ni sumu kali. Kuna kuzibwa kwa vitu vingine japo havikai muda mrefu sana, zebaki ina yeyeyuka ukinywa vitu vya moto na kuwa sumu kwenye damu. Mtu mwenye zebaki ya majino mawili au matatu si kubwa ila kama una mengi ni shida, na jinsi inavyozidi kuzeeka inayeyuka zaidi. fluorine kwenye meno ni sumu kwa mwili jaribu kuangalia njia za kinga za kupunguza meno kuoza zaidi ya fluorine. Pia root canal imeonekana kufanya kinga mwili kupungua , jaribu kusoma utafiti hasa wa nchi za ulaya. Wao wana mambo ya afya kuliko marekani. Wengi wameniuliza kuhusu chanjo. Chanjo nyingi zimesaidia kuondoa magonjwa kama vile polio, duniani. Ila siku hizi makampuni ya madawa yanazidi kuja na chanjo nyingi ambazo zinazodhuru. Fanya upelelezi ni chanjo zipi zafaa mtoto. Chanjo nyingi siku hizi zinatolewa kwa mseto au mpigo sita kwa mtoto wa wiki 6. hii imeonyesha athari kwenye nchi zingine kama America kwa ubongo wa mtoto (autism). Ila kwasababu inahusika na pesam kwa makampuni haya pengine, ukweli kamili usijulikane. Zamani chanjo zilitolewa moja moja. Chanjo zingine kama za Flu (mafua) katika nchi za magharibi zimeonekana kudhuru watu, na zingine zinatunzwa kwenye zebaki (mercury) ambayo ni sumu. Nafikiri kwa vile watoto wetu wanacheza na watoto wengi mzazi aangalie jinsi ya kumsaidia mtoto na chanjo zinazofaa kwenye jumuiya ili mtoto asidhurike. Ila zingine za kuepuka aweza kuona jinsi ya kufanya . lazima uwe mteja unayetafuta maarifa (educated consumer). Angalia website ya mercola.com na zingine. Sitamwambia mtu asichanjwe au achanjwe kwa vile chanjo nyingi zimesaidia sana nchi zinazoeendelea kama za afrika. Na pia wengi wetu kwa vile hatufanyi vitu vile 10 vya tiba rahisi ili kulinda afya zetu inabidi tupate chanjo zitusaidie kwa vile kinga zetu za mwili zimekuwa hafifu
Ni muhimu sana wazazi kujifunza huduma ya kwanza mfano mtoto akipaliwa na kitu kwenye koo, akinywa sumu, akiacha kupumua ila ana mapigo ya moyo, na hata wale wasaidizi wa watoto wafundishwe. Niliishi na anayenisaidia mtoto homa ilikuwa juu sana 41c na hakugundua kwa vile hakuwahi kuwa na mtoto au uzoefu.
Kama ulikuwa umefanya makosa katika lishe usikate, tamaa Mungu ni mwenye huruma nyingi pale pale ulipoanza kusahihisha anakusaidia. Mazoea yanajengeka kwa kurudia, hivyo ukileta chakula kigeni kwa mtoto kikikataliwa usiharakishe kukitoa. Endelea kukileta. Mfano tunda Fulani, au nafaka ambayo mlikuwa hamtumii. Mtoto anachukua muda kuzoea harufu na ladha mpya. Hasa kwa wale wakina mama wanaofikia hatua ya kumtambulisha mtoto kwa chakula kama miezi 6 au wale wanaotaka kumwachisha mtoto kunyonya, kama miaka miwilii au mitatu. Hata sisi kama watu wazima kuna vitu tulianza kuvila ambavyo vilikuwa vigeni, na ilibidi tuvizoee na sasa tumevipenda, mfano ovacado, beet root nk. Badala ya kumpa mtoto kitu kisicho na afya kwaajili anakazania tafuta

mbadala atakaoupenda ambao una afya. Wakitaka vitu vyenye sukari, matunda kama mananasi, au asali kwenye uji watafurahia. Mara zingine watoto wanataka kula kula kwa kukosa kitu cha kufanya watafutie mchezo au kazi ya kufanya. Jitahidi usiwakaangie kaangie vitu na mafuta mengi, jaribu kuoka. Mara nyingi usipende kutoa zawadi ya chakula wataona kama ni faraja kwao na kufanya chakula kiwe rafiki wakati Fulani. Hii yaleta ulafi na kufanya waongezeke uzito. Wakati wa chakula usiwe wakati wa magombezo na mafarakano, na kumlazimisha mtoto kula kitu Fulani. Leta utulivu wakati wa kula ili wakati wa kula uwe wakati wa furaha. Usimpe mtoto pesa kununua chakkula shuleni kama peremende, jaribu kutayarisha chakula na kumwekea kwenye chombo. Chukua muda utafute vitu vya afya. Mara nyingi watoto wanachekana kwa vile vitu walivyobeba. Wanapenda waonekane wa kisasa na magharibi kwa kula mapochopocho ya makasha! Na kuona aibu mbele ya wenzao wakibeba magimbi, viazi vitamu au vitu vingine. Chukua nafasi ya kwenda kununua chakula na watoto na kuwaelezea thamani ya lishe kwenye vyakula mbali mbali. Waonyeshe kwamba kuwa na afya ni kitu cha furaha. Wafundishe mambo 10 muhimu ya afya bora, au tiba rahisi. Watu wengi siku hizi wauzaji wa vitu wamewalenga watoto na makasha kasha na mapochocho yanayopendeza kwa macho ila ndani hayana lishe. Sikila walichokipamba kina lishe ya nzuri. Wapaswa ujielimishe kuhusu wauzaji wa vitu. Gazeti la unene journal of obesity reviewe lilitafiti vyakula vya watoto 387 na kukuta kati ya hivyo 89% vina lishe hafifu kwa watoto. Vingi vina sukari, chumvi na mafuta mengi kwa mtoto na hata mtu mzima, waingereza wanaita junk food, au vyakula ambavyo ni kama takataka kwenye miili yetu. Vyakula hivi vyenye sukari, chumvi na mafuta mengi vinafanya watoto wawe na usikivu mdogo, uchovu, na vinaongeza shida za kisukari na shinikizo la damu watoto wakiwa na umri mdogo. Shirika la kupunguza unene duniani the international obesity task force limeona kwamba mtu mmoja kati ya watatu nchi nyingi duniani ni mnene wa na mtoto mmoja kati ya watano pia ana shida hiyo.

Jambo nzuri ni kwamba hali hiyo inaweza kusahihishwa kwa kutumia vyakula vya asili vyenye lishe bora na ambavyo vinavutia.

Je wazazi wawezaje kusaidia watoto wao wale vyakula vya afya.

Kwanza ni kujua kwamba ulaji unatokana na mazoea. Itachukua muda usifanye haraka. Watoto wanarithi chakula toka kwa wazazi kama vile ilivyo urithi wa maumbile! Na ndiyo maana kila taifa, kabila na jamaa miaka na miaka wanakula sawa na watoto wao. Mama ana nafasi kubwa ya kumfundisha mtoto chakula bora, kwani mama ndiye mpishi mara nyingi.utafiti umeonyesha hata mwanamume aliyesomea shahada kubwa za Mama ana nafasi kubwa ya kumfundisha mtoto chakula bora, kwani mama ndiye mpishi mara nyingi.utafiti umeonyesha hata mwanamume aliyesomea shahada kubwa za lishe, haisaidii yeye kula chakkula cha afya kama mke au mama anapika vyakula vinavyoharibu mwili. Wakina mama hapa tuna nafasi kubwa ya kusaidia jamii zetu na chakula.

Chakula kipya kina harufu, ladha na kuonekana tofauti. Mpe muda mtoto kukizoea, mfano watoto wengi ukiwaletea ovacado kwa mara ya kwanza wanaikataa. Au mtoto aneyeletewa vyakula kwa mara ya kwanza, wa miezi 6 itabidi ujaribu mara kadhaa. Hata wale ambao wanaachishwa kunyonya, inabidi wazoee chakula polepole.nafikiri hata sisi watu wazima kikiletwa chakula kigeni itakuwa vile.. jaribu kuleta vyakula vya afya vyenye kupendeza kama matunda, kwa vile vibaya ulivyotoa. Mfano chapatti za unga uliokoboleewa anza na unga usiokobolewa na mboga iliyoungwa vizuri.watakapotaka vitu vya sukari, tafuta tunda lenye sukari kama nanasi, au weka asali kwenye uji. Sukari si njema kwa mwili. Inapunguza kinga ya mwili kupigana na maradhi. Mara zingine watoto

hawaitaji chakula ila wanahitaji mazoezi na vitu vya kufanya badala ya kukaa na kula kula saa yote. Jaribu kuoka vyakula badala ya kukaanga na mafuta mara kwa mara.
Kutoa zawadi ya chakula kwa mtoto inafanya mtoto afanye chakula kama faraja, hili laweza kumfanya awe mtoto wa kula kula saa yote. Tafuta zawadi nyingine. Usifanye wakati
Kitu kingine cha kuzungumzia kuhusu watoto ni usalama. mtoto ana hatari nyingi ni vizuri kukagua mazingira yake mfano, mafuta ya taa watoto wadogo wakiwa na kiu waweza kunywa. Kuchezea moto au viberiti. Kuvuka barabara. kuanguka kwenye michezo kama kupanda miti au wakati wa deki mtoto awe mbali kidogo. Mtoto mdogo, angalia michezo wanayocheza kama ina usalama. Angalia mtoto asichezee silaha zilizo nyumbani kama panga, kisu,shoka nk. Je kuna mashimo makubwa kwenye uwanja wako ambayo ni hatari mtoto kutumbukia? Je una kisima, na vitu vya namna hiyo. Je una bwawa la kuogolea au unaishi karibu na mto. Je mtungi wa gas umefungiwa kwenye kabati na una kufuli.je dawa zako zote ziko mbali na unafungia, ni muhimu sana, na mtoto akinywa sumu unajua mtu wa kumwita. Je jiko la mkaa mtoto akiwa karibu unaangalia usalama wake? watoto wengi wanaumia kwa kuvunjika kwa sababu ya michezo au mazingira ambayo wazazi hawajayatilia makini. Mahali pengine watoto wanajikuza wenyewe tu, wa miaka 8 ndiyo anaangalia wale wadogo akiwabeba mgongoni na kumlisha. Wazazi waenda mbali muda mrefu na jirani wa siku hizi hawashuguliki, na jamaa wa karibu wako mbali. Wazazi watoto wanaangaliwa, mara nyingi tulifikiri watu wa magharibi hawajali watoto ila nimeona watu wa magharibi wanaangalia usalama wa watoto na kufundisha watoto cha kufanya moto ukitokea (simama, anguka , biringika)stop drop and roll. na njia ya kukimbia, mtu mgeni akimwuliza kitu asemeje,akipotea asemeje, ajue anapoishi,jina la mzazi na namba ya simu hivi vinafundishwa rasmi. Mtoto asitumwe usiku mbali penye hatari. Siku moja usiku karibu na mtaa wetu mama alimtuma mtoto wake wa miaka 12 na 6 saa sita ya usiku kununua chakula hoteli ya kichina. Ni mjini taa zinawaka, ila walipigwa na bunduki. kwa usalama wa mtoto mfundishe vitu hivi na mengine ya vile haya yote yanalinda afya ya mtoto kama kuripoti akiona jambo Fulani geni, mama mmoja alisema kijana wake wa miaka 15 alipata kansa ya kizazi (testicular)na hakusema alikuwa anaogopa, akaenda kwa mganga kwa bahati na mganga akagundua ila ilikuwa imefika stage mbaya na alipata mionzi na ikarudi.
====Napenda kuzungumzika afya ya watoto wakubwa miaka 12-18 kwasababu wana mahitaji na changamoto tofauti. Wao wana uwezo wa kuchagua ila wana msukumo wa rika ambao unafanya uchaguzi wao uendane na rika lake hata kama hautamfaa. Ni muhimu kwa afya ya vijana kuchagua marafiki wa kufaa, burudani za kufaa na chakula bora,jinsi ya kutumia muda wako na sherehe za kuhudhuria au kua. Kuwa na afya ni nyanja zote kiroho, kimwili na kiakili. Vijana wachukue muda kufanya mazoezi na kutokula vyakula ambavyo si vyema. Wasome maadili ya afya na kujaribu kuyatekeleza. Jipende mwenyewe na jithamini, hakuna kama wewe, umeumbwa kwa kusudi maalumu. Uwe mwazi kwa wazazi kueleza mambo yanayokuhusu na kusaidia afya yako. Kujua jinsi ya kuchukuliana na misongo na presha za maisha. Chukua muda kujisomea neno ya Mungu, na kujenga madaraja na urafiki na wengine. Nuia kuishi na watu vizuri na kuomba msaada endapo unahitaji bila kuogopa. Kwa afya njema hakikisha unakula matunda, mboga na nafaka zisizokobolewa. Jamii ya maharage na karanga ni muhimu. Usiache kula kifungua kinywa huu ni mlo muhimu sana. Kwa akili inayokua. Kula chakula wakati akili imetullia kunywa maji vizuri na epuka vyakula au vinywaji vyenye sukari. Tafuna mlo wako vyema

Kwa mtembeo wako hakikisha mwondoko wako posture inakuwa bora. Posture bora inasaidia mifupa na misuli kukua vizuri, viatu vyako uchague vizuri sii vya kubana au vya juu sana. Viatu vya fasheni nyingine vina shida za afya kama kuleta vidonda, kuharibu mgongo na vivimbe kutokea kwenye miguu (bunion). Nguo ziwe za kuendana na hali ya hewa, miguu na mikono isiwe wazi wakati wa baridi. Mikanda isiwe ya kukaza na kuvaa nguo za kubana vinafanya mapafu yasitanuke inavyotakiwa na usitembe au kusogea unavyotaka. Ukisimama kwenye ukuta kichwa, mgongo, matako na visigino viguse ukuta nyuzi 90. tembea na mzigo kichwani unasaidia kuwa na posture nzuri, fanya hili zoezi mara kwa mara. Na la kuvuta pumzi kwa muda na kuitoa kwa muda (deep breathing). Mazoezi ni muhimu, yanalinda magonjwa mengi na yanafanya ujithamini na kuwa mtu mwenye furaha.fanya mazoezi unayofurahia na yenye faida. Wenye uwezo wa kusikiliza muziki waweza kufanya vile. Kwa ubongo wako vyakula vyote vya afya vinasaidia matunda, mboga, karanga , nafaka na jamii ya maharage. Pia unywe ubongo. Asilimia 90? Ya ubongo ni maji! Hakikisha umefungua madirisha yako na tembea nje pia kwa hewa bora. Panga muda wa kusoma ili usisome usiku wote wakati wa mitihani.usingizi masaa 8 ni muhimu. punguza usumbufu wakati wa mitihani na jifunze njia bora za kusoma na kukumbuka.

Kuna kitu kingine kimezuka cha madhara ya watoto nacho ni madawa ya kulevya, na tabia ambazo ni hatarishi nchi zingine watoto wamekuwa wakijiweka kamba shingoni kwa kujaribu na kuitoa, jambo hili limeua watoto maana mara zingine hawakuitoa ile kamba kwa wakati wake. Wazazi kitu tunachoweza kufanya tu ni kuwa karibu na watoto wetu na kuwapenda, ila hata hilo halitoshi ila kuwakabidhi kwa Mungu maana yeye ndiyo anayejua mawazo yao zaidi ya sisi.(soma mengine zaidi kuhusu muziki na tabia au usalama wa mtoto)

Miaka ya karibuni watoto wengi wamekuwa wakijiua kwaajili ya watoto wengine kuwanyanyasa (bullying). Mtoto anaweza tu akateswa na mtoto mmoja mpaka akakata tamaa ya maisha, na anatishiwa ukiwaambia wazazi wako au mwalimu utaona. Nakumbuka nikiwa na miaka 7 darasa la pili njia ya kurudi nyumbani kulikuwa na bully mtoto wa darasa la tano mnene sana, akiniona napita anakuja na kunipiga makofi. Nilikuwa na hofu sikuwambia mtu kabisa, sasa ukubwani ndiyo naliwazia. Uchunguze na kuwauliza watoto. Mtoto wangu wa miaka 7 alipanda basi kwenye mji wa wazungu na walimfanyia vile siku moja mtoto mmoja wa darasa lake alikuwa na miak 9 ila alikuwa na shida ya kujifunza (learning disability) na hhakujua kusoma darasa la pili alimpiga mara 12. nikaenda kwa mwalimu mkubwa aliponiambia baada ya kuficha muda mrefu, mwalimu alimwita na pia mzazi wa kijana ambaye alifikiri basi ni lake kwasababu “mwafrika hana kitu” mwalimu aliomba msamaha na wazazi wake. Mtoto ni jirani wa karibu na sasa nimeona ana heshima ya aina Fulani. Peleleza watoto wako kama wana bully. Angalia kwenye internet www.breakingthesilencenow.org kuhusu hii tabia

Vitu vingine vya kuzungumzia ni kujichora miili, tattoo au kutoboa miili. Hili si jambo la kuendekeza. Na vyombo vinavyotumika na infection ni budi kuangalia kwa manufaa ya vijana wetu.

Kwa wasichana nitasema kwamba mambo ya kuvaa nguo fupi au za kuonyesha sehemu nyeti ni hatari kwa afya na maisha. Tunahitaji kuvaa kwa adabu kama tunataka afya yetu iwe kamili, wavulana wanaangalia na tunatuma ujumbe wa namna Fulani. Kwamba tunataka waje kwetu. Wasichana japo wasema kwamba wanawake na wanaume ni sawa, hiyo si kweli. Wewe msichana ukitoka usiku wa manaane na kutembea mjini una risk ya

afya yako. Jua kwamba wewe ni msichana urudi nyumbani kabla ya giza. Jifunze kutogombana na watoto wa kiume na kujiunga na magenge yao maana unajiletea hatari
Viatu vya wasichana vimekuwa designed na wanaume, vingi havina afya. Vimetengenezwa kufanya mwili uonekana kwa namna Fulani na kutingishika kwa namna Fulani. Nina imani wanaume waliotengeneza viatu hivi kwa ile suluba vinavyotoa wasengewea kuvivaa hata masaa 2 ila sisi tunashinda navyo siku nzima.
Mabadiliko ya kukua yanapotokea huwachangamoto kwa wazazi na vijana, vitu kama hasira na kugombana hii inaweza kuzungumziwa kwenye ujana na pia afya ya vijana. Maana jamiii ina matazamio Fulani ya kielimu, kusaidia kazi nyumbani na misukumo ya rika. Mchunguze mtoto wako kama ni mtu anakuwa na huzuni, hasira, woga, kutotilia makini vitu, kurudi nyumba shuleni, kutotaka marafiki,kukaa peke yake,kusikia sauti, nia ya kujidhuru au kudhuru wengine, anaharibu vitu kwa kusudi, anakunywa pombe au kuvuta sigara, anakataa kula au anakula na kutapika, analala siku nzima, anasema hawezi maisha, ndoto mbaya, kujifikiria kwamba ni wabaya, anasita kukata shauri, anarudia vitendo mara nyingi kama kuosha mikono (obsessive compulsive), dhamira kumshtaki na mengine kama hayo. Mara zingine mabadiliko ya mwili na hisia katika kukua yanaleta haya na pengine anahitaji msaada wa kuzungumza na kujua kwamba haya ni stage tu na si kwamba yeye ni tofauti sana.pengine waweza kupata mshauri mwenye hekima na uzoefu.
Mara nyingi kwa kupendeza jamii (social life) watoto waanza kunywa hata kabla hawajafikisha miaka 12. hii ni hatari. “20:1 wine is a mocker. Kama ni kuna vinywaji vingi tu ambavyo haviharibu afya yako, mfano zabibu, limao, tangawizi au apple tofaa ukiwa nalo. Vijuice pamoja ni bora kuliko vile vikavyoathiri ubongo na afya kwa jumla na kufanya usifae.
Kitu kingine cha kuzungumza kwa vijna ni afya ya ngono. Media vyombo vya habari, magazeti, tv na radio vimefanya watu wanaoshuguliikia ngono nje ya ndoa ni mashujua na wajuzi. Wanasema chochote kikikupa furaha kifanye. Mungu ana standard nyingine kwetu, anataka tuweke mpaka na kuishi maisha ya usafi na furaha na bado kuwa katika mpango wake. Wasichana wadogo wamekuwa na msukumo kuvaa kama wanawake na kuanza ngono mapema. Nikifanya kazi katika hospital kubwa ya magonjwa ya akili Hagerdon Usa (wagonjwa 2000Nj nilikuta utafiti kwamba zaidi ya 70% ya hawa walikuwa wamefikia hali hii kwaajili ya mambo ya ngono au ulevi. Niliona msichana mmoja akila kila kitu alichokiona, alikuwa na miaka 19. alikuwa amepasulilwa mara 8 kwa kuka bulb, misumari, na vitu vingine. Alilindwa na mtu mmoja kila alienda hata chooni mlango unakuwa wazi akijisaidia. Chumbani kwake kulikuwa na vitu vichache mno. Alishiriki mambo ya ngono toka utoto wazazi hawakujua. Msukumo wa kuonekana anafaa kwa rika lake, vijana kumfuata na kujiona maumbile yake si mazuri sana japo yalikuwa mazuri. Aliona wazazi wake wana mashuguli na kwamba hapendwi akaendelea kujaribu kutafuta upendo kwa wavulana ambao kwa kweli walitaka kumtumia tu. Hata wengine walimnyanyasa kingono kwa nguvu akiwa mtoto wa chini ya miaka 16. alikuwa hajioni ana thamani kabisa. Msukumo wa ngono unaharibu afya ya wasichana na hata wavulana wengi. Na kuna kitu cha ushoga kimeingia siku hizi na hata wavulana wadogo wanaanza kulawitiwa. Hata kama ni viongozi wa dini kama magazeti yalivyotoa meaelfu ya watoto wanahudumu kwenye kibweta wakati wa misa walikuwa wamelawitiwa na viongozi wa dini.. mwombee mtoto wako na ujaribu kumlinda unavyoweza kibinadamu akuone rafiki na kukwambia mengi usiyoyaona au kuyawazia. Magonjwa ya zinaa yanaongezeka kwa watoto,. Shule moja waliuliza watoto wasichana wa umri wa miaka 15 . 45% walikuwa wamefaya ngono na 31% wavulana. Kuna haja ya kuzungumza na watoto mambo ya

ngono safi na haramu. Hata kuhusu mambo ya mimba na kutoa mimba. Mwisho wa watoto wanahousika na haya ni kutokuwa na nyumba nzuri, talaka, watoto wakizaa hawana baba au usimamizi, na watoto wanalea watoto.. elimisha watoto kuhusu kujitunza na usafi wa ngono. Wazazi wengi wanafikiri kwamba kutumia kondom ndiyo ufumbuzi. Si kweli, hii inajenga mtoto kuwa mpotofu zaidi, na hata hivyo kondom yaweza kuzuia mimba ila huzuni, kutojithamini na kutofaa itakuwa imeshawadhuruu mawazo yao. Useja mweleze mtoto ndiyo mpango wa furaha mpaka wakati wa kuolewa au kuoa. Washauri watoto kwamba usaifi ndiyo ushujaa, watawale mawazo yao na kutafuta vitu vya kuwashugulisha badala ya ngono,waombe kwa bidii, waepuke kutongozwa na watu na kukaa kweney sehemu za giza au kujishugulisha na marafiki wa namna hiyo, kama ni msichana mkubwa na ameenda na mchumba wake mahali pawe mahali pa wazi, penye watu wengine na muwe na pangeni mashuguli ya kufanya ili mawazo yenu yasikae kwa yale ya uovu.

Mungu ni mwenye Rehema, tunapopotoka maana tu binadamu tukiungama tunaanza kurasa mpya . lazima tugundue hitaji letu ili Atusaidie. Kama umeanguka kwenye jaribu la ngono kijana jitoe katika hali hiyo haraka,Sali kila siku, watu wazima wenye hekima wakusaidie utoke kwenye shimo, jua kwamba ukiungama kwa dhati unaanza safari mpya. Shetani asikukumbushe ya zamani, akizidi kukumbusha yaliyoppita mwambie yatakayomjia yeye, yaani Jehanam. Wazazi kwa mfano bora nasi tufuate mpango wa Mungu wa usafi wa ngono. Wakina mama wengine au wakina baba wanaleta marafiki a kiume na kike na kulala nao pamoja watoto wakiona, hii haisaiidii malezi ya watoto. Nimeona rafiki wa kiume wa mama akianza kumwingilia mtoto wa kike , usihatarishe afya ya mtoto.

Mambo ya madisco kama unawapeleka watoto wako kwa kweli ni kitu cha kuangusha maadili. Wangapi walipelekwa na wazazi wao disco ? je ukimwona kijana amemshikilia binti yako kwa kubanana na taa zimezimwa au vimulimuli utaonaje? Ngoma za jadi za kiafrika zilikuwa zina adabu zaidi watu walicheza mbali mbali. Hata mashuleni watu waliocheza ngoma za jadi sikuona watu wakikumbatiana vile. Maumbile ya kike na kiume si ya kukumbatiana vile labda mtu na mume wake au mtoto na mzazi. Na hata mzazi mtoto akiwa mtu mzima unampa nafasi Fulani. Ni heshima. Mambo ya shule za sekondari kuwa na madisco ya watoto yameleta uzinzi na uasherati mwingi. Nasema niliyoyaona. Japo sikutilia maanani kwamba ni jambo baya, na sikwenda niliona athari zake kwa waliokuja bwenini kuhadithia. Msichana mmoja katika dansi walianza kufanya ngono na kijana mpaka walifukuzwa kwenye dansi, ila waliendelea na urafiki na siku moja tukisafiri kwa meli walifanya ngono kwenye meli na watu walishuhudia. Hakuna kitu kama kukumbatina kwa dansi na kusema mko salama kimaadili. Awe mke wa mtu au siyo staili hiyo ni ya mtu na mke wake tu ndiyo wameruhusiwa. Na sina mjadala zaidi na hilo. Kama wewe ni mtu mzima hasa mwanamume au mwanamke umenielewa vyema kabisa sina haja ya kusema zaidi.

Fundisha watoto wako kuwa na huruma na kuwa na marafiki ambao wana kilema au upungufu Fulani. Watoto wana ukatili kwa mtoto mwenzao ambaye ana kilema Fulani mfano kigugumizi, huwa wanamcheka na kusema kwa sauti kubwa na kumtenga. Tabia hii si nzuri

Habari ya allergy ni ya kuangalia, kuna watoto wasiopatana na vyakula Fulani, dawa Fulani au hali ya hewa Fulani. Hii yawafanya wawe wagonjwa. Vyakula vingi mara nyingi vina allergy ndogo ndogo ., bali vingine hatari kubwa sana hata kuua. Allergy ni mwili kureact kwajazba kubwa kwa kitu ambacho si cha hatari au kwa kawaida ni rafiki. Mfano mtoto

Fulani alikuwa ana allergy ya ufuta, na rafiki yake alimpa kipande cha kuku shuleni , na kilikuwa na ufuta. Kijana huyu akashindwa kupumua na mwili ulivimba kwa haraka sana akaanguka na kufariki papo hapo. Kesi extreme. Ila wengi wana shida ya vyakula hasa maziwa, nguruwe, nyama ya kondoo, mahindi, ngano au mayai. Waweza kupunyuka nywele, kuota upele, kutoka vidonda, kupata shida ya kupumua au kuwa na pumu nk. Mzazi aone kile kinacholeta allergy na kuondoa. Dawa mwambie tabibu au wewe mwenyewe usimpe. Mfano watoto wengi wana allergy ya ibuprofen. Kwa hali ya hewa tofauti au kwa chavua za maua, omba ushauri wa tiba jinsi utakavyoweza kuepuka

Shida hii. Wengi walipoachana na hamira ya aina yoyote ile wameonekana kupunguza mizio yao, maana utafiti mwingi waonyesha hamira si kitu kizuri kwa afya maana hamira ni kuvu (fungasi). Hili ulipeleleze vizuri mwenyewe.

Tabia zingine kama hasira zimegharimu afya za watoto na wakubwa. Zungumza na mtoto kuhusu hasira za waziwazi na zile za ndani. Jinsi ya kuondoa hasira n.k . kuna watu wengi wanatembea na hasira toka utotoni wakiwa wamezifungia na siku ya kulipuka zinakuwa madhara makubwa. mama Fulani akiendesha gari alikuwa anakuwa na hasira (road rage) ya kupiga honi, mtu akichelewa kidogo, na kunyoshea madereva wake mikono wanaochelewa au kumpita vibaya. Haya yanatokana na mambo yanayoendelea katika maisha yake na siyo sana sana wale wanaokuwa barabarani. Siku moja mama huyu aliyekuwa anabeba bunduki, alimlenga dreva mwingine akapiga bunduki na kumwua eti kwasababu anaendesha pole pole. Mtu asiyemjua kabisa! Halafu akimpiga bunduki akasema " pole sana" , twaweza kushangaa ila tabia hii ya hasira ipo kila mahali na inajitokeza kwa watoto pia wakicheza na kuwa hatari. Ni muhimu kufundisha watoto akiwa na hasira afanyeje? Je ni sawa kwasababu ya hasira yake amwumize mwingine au ajiumize? La hasha. Katika dunia ya misongo kwa watoto na watu wazima ni muhimu kulitambua hili swala na kulishugulikia baada ya kulijadili

Epuka na kuabudu marafiki na tunza watoto wako. Nimeona mama wengine wana watoto wadogo ila mgeni akiingia wanasahau hata mtoto yuko wapi. Au akipigiwa simu anaacha anachomwambia mtoto hapo hapo "halo halo" tumeziabudu simu mpaka tukakosa adabu hata mbele ya watoto wetu,.wewe utasikiaje ikiwa unazungumza na mtu na ghafla akaanza kusema "halo halo". Jifunze nidhamu, "sema samahani nipokee hii simu. Watoto wako watakuiga mtakuwa nyumba ya halo halo na siyo mahali pa mafunzo. Yawezekana si kitu kwa watoto wakubwa ila wadogo ni kitu. Mtoto wangu akiwa na miaka miwili alikuwa anakuja kunitoa kwenye simu, alikuwa akisema kitu sisikii kabisa! Nampa usikivu wangu rafiki wa simu , Alipofika miaka mine alisema " mama wewe hunijali unapenda simu tu hata mtu akikuambia nyumba inaungua hutasogea" alijaribu kupindua shingo yangu ili nimsikilize akisema kitu au alipiga makelele ili nitoke kwenye simu. Mara nyingine jifunze kusema "nitakuita baadaye" kama unataka uwaweke watoto wako sawa na karibu. Mbona neno la Mungu hulikazanii kama simu, je umeshamwambia rafiki " huu ni muda wangu wa kusoma au kuomba niite wakati mwingine?" . Mtu mwingine alisema endapo tungejali simu zetu kama NENO la MUNGU tusingeacha kutembea nalo wakati wote, na wala na wala lisingepata vumbi na kusahaulika mahali miaka mingi mpaka shida au dhiki itokee ndipo tunalishugulikia.

MAMBO zaidi ya 101 + TUNASHAURI UFANYE NA WATOTO

A. Mambo 101 ambayo tunashauri ufanye na watoto wako kama yawezekana karibu na mazingira yako. Watoto wanakua haraka na watatoka. Wengi wanakumbuka yale mambo waliyofanya na wazazi wao! Japo, kwa wengine, mambo haya yanaweza kuonekana ya kipuuzi, ila kwa watoto ni ya muhimu sana; kujenga nao mahusiano maana tunatumia muda wetu na kuonyesha upendo wetu.

Twaita, Orodha ya mambo ya kufanya kabla hawajaenda makwao!

- Ingia jikoni na pika nao, mapishi ya kawaida na mapya
- Waweke watoto wako kwa aina mbali mbali za sanaa kama ni vyombo vya muziki, uchoraji, na ustadi mwingine.
- Wafundishe watoto kujali wanyama wa nyumbani kama paka na mbwa na hata wale wa porini (wild life conservation).
- Waonjeshe watoto wako vyakula vya makabila na hata mataifa mengine.
- Wapeleke watoto kwenye ibada kila wiki.
- Wafundishe watoto kusoma neno la Mungu na kila mtoto apate kitabu chake mwenyewe.
- Wapeleke watoto kwenye jumba la makumbusho la taifa (museum).
- Wapeleke watoto wako kuhudumia jamii, hata kama ni kuokota takataka sokoni.
- Wape watoto visa vya watu mashuhuri duniani ambao japo hawakusoma saana wamepindua ulimwengu kwa ujasiri na tabia zao za kuhudumia watu kama Yesu, Mahatma Gandhi, Janet Goodal, na mashujaa wengine wa nchi.
- Wafundishe watoto wako mila na desturi nzuri za jamii yako na jamii nyingine pia
- Chukua muda upande basi au treni na kuwaonyesha watoto jinsi ya kulipa nauli, uwaonyeshe njia na jinsi ya kufanya wakipotea.
- Wapeleke watoto dukani na waonyeshe jinsi ya kutumia pesa vizuri.
- Wapeleke watoto kuangalia wanyama wa pori au fanya mpango waende na shule.
- Muwe na kikao cha kujadili mambo ya familia kila mwezi, watoto hata wa miaka kumi washirikishwe.
- Mfundishe mtoto wako kuwapa masikini nguo, viatu n.k.
- Kila mtoto akatiwe bustani yake na alime kila msimu.
- Piga magoti na mtoto WaKo mwombee mahusiano yenu pamoja
- Wapeleke watoto wakaone babu na bibi.
- Nenda kuvua samaki na watoto.
- Fanya mashindano ya kukimbia na watoto.
- Safisheni nyumba pamoja na watoto wako, wote baba na mama.
- Pigeni kambi nje ya nyumba na mjenge kibanda.
- Pandeni mlima wa karibu na kula huko, muimbe na kuomba pamoja.
- Rusha tiara pamoja na watoto
- Jengeni nyumba ya asili pamoja.
- Tembeeni baharini pamoja na kuchimba michanga na kufukiana.
- Kimbieni kwenye mvua.
- Nendeni mkachume matunda mwitu pamoja.
- Nendeni na mtumbwi pamoja kama siyo kina kirefu.
- Pandeni miti pamoja.
- Tengenezeni zeze, au tarumbeta au chombo cha muziki pamoja.

- Nendeni mkachukue picha za pamoja
- Tembelea mji mkuu pamoja.
- Kaa nao na kufanya mahesabu pamoja.
- Nenda nao sokoni na kuuza nao mboga au bidhaa za kutoka shambani.
- Waambie hadithi za ukoo wenu na mashujaa wenu.
- Wafundishe chombo cha muziki.
- Wafundishe kuogolea, au mjifunze pamoja.
- Wapeleke nje ya nchi, kama una uwezo.
- Tengeneza nao mwanasesere, vyungu na vyombo vya udongo.
- Choreni picha pamoja.
- Uwepo pale wanapopata maumivu.
- Wapeleke bungeni au mahakamani.
- Wanunulie vitabu vizuri vya kusoma.
- Waandikie barua ya kuwatia moyo.
- Wape kumbukumbu nzuri ya utoto wao.
- Wakumbatie watoto wako.
- Wafundishe kujitegemea na kuheshimu watu.
- Wafundishe kuwa watu wenye uvumilivu wapendao amani.
- Wafundishe ujasiliamali.
- Wafundishe watoto kumtegemea Mungu kwa uhakika.
- Wafundishe kutengeneza upinde, mkuki, manati na rungu.
- Tembea nao na uwaonyeshe mimea isiyo na sumu ya tiba rahisi na ambayo unaweza kula.
- Zima simu, tv au computer na ukae na watoto wako na kufurahiana nao, pia kusoma nao.
- Waachie uhuru watoto wako uone watautumiaje.
- Nenda na mtoto mmoja mmoja kwenye matembezi na kuongea naye akiwa peke yake. Waambie huo ni muda maalum kwao na kwako.
- Mpeleke mtoto maktaba.
- Tokeni nje ya nyumba na kula pamoja.
- Sikilizeni mziki au muimbe pamoja.
- Mhadithie mtoto wako hadithi za alipokuwa mdogo.
- Mtembelee mtoto wako shuleni kwake.
- Kaeni na kusema vitendawili na methali pamoja
- Safirini pamoja.
- Pandeni mbegu za miti au mboga pamoja.
- Jifunzeni tamaduni za makabila au nchi zingine.
- Wenye magari, pikipiki au baiskeli osheni pamoja.
- Nendeni benki na mtoto aone jinsi ya kufungua akaunti.
- Tembeleeni rafiki yenu wa karibu mlale huko.
- Fanyeni mchezo wa kuigiza pamoja.
- Chezeni ngoma ya jadi pamoja, (mfano ya wasukuma wakilima).
- Kaeni na kusikiliza kila mtu akitoa futuhi.
- Tengeneza list ya vitu mnavyotaka kufanya pamoja.
- Wachukue watoto kwenye kiwanja cha ndege.
- Ficheni vitu kisha mtafute pamoja.
- Angalia jinsi mnavyoweza kuandika kitabu pamoja (rough draft).

- Nendeni kwenye mgahawa na mnunue chakula cha bei rahisi, hata matunda.
- Chukueni muda kumshukuru Mungu kwa kufikia mwaka mwingine wa siku ya kuzaliwa au mwaka mpya.
- Tembea mjini na ukiona mtu masikini mpe kitu kidogo.
- Nunua kitabu kidogo (album) na bandikeni picha za familia yenu.
- Fanyeni mazoezi pamoja.
- Buni mchezo wa kucheza wote na kanuni zake.
- Tafuteni ndani ya nyumba na kuangalia kama kuna kitu cha kumpa mhitaji, bebeni muwapelekee.
- Fua nguo na watoto wako.
- Osha vyombo nao.
- Nendeni mkachune mboga kwenye bustani pamoja.
- Angalia list ya vitabu ambavyo mwaweza kusoma na watoto.
- Nenda na watoto ibadani kila wiki.
- Tengenezeni gari, manati au kinu pamoja.
- Tembeza watoto kwenye kituo cha polisi na kuulizia shughuli zao.
- Hudhuria arusi na watoto wako na waeleze umuhimu wa kufunga harusi na kutoishi bila ndoa
- Tembeleeni mtoto mgonjwa hospitalini.
- Tengenezeni juice, ya ukwaju, au mbuyu au rosera au juice ya matunda na mnywe pamoja.
- Pekecheni moto na kutengeneza silaha za mtu wa kale kwa mawe.
- Tengezeni bisi pamoja.
- Tembeleeni bibi au babu mzee na msikilize maisha yake ya zamani.
- Nendeni kwenye maonyesho, kama ya wakulima.
- Tembeleeni shamba kubwa lenye pembejeo kufujifunza.
- Nendeni kuwinda kwa ruhusa ya mamlaka.
- Pandeni maua nje ya nyumba.
- Laleni nje pamoja kama hakuna tayari.
- Fanya majaribio rahisi ya sayansi; mfano, weka jiwe kwenye chombo kilicho na maji na mgundue kwamba yale yanayomwagika ndiyo uzito wa lile jiwe.
- Nendeni kucheza kandanda au netboli pamoja, au mpira wa kawaida.
- Chezeni mchezo kama bao pamoja.
- Nendeni kwenye mnada pamoja.
- Tengenezeni mafuta kama ya karanga, ufuta au mawese pamoja.
- Mfundishe jinsi ya kufanya fomentesheni.
- Mfundishe mtoto jinsi ya kufanya massage.
- Mfundishe mtoto huduma ya kwanza.
- Msaidie aende scout au girl guide kama ipo kwenu. Pia chama cha watafuta njia.
- Mpeleke mtoto kwa chama cha watafuta Noia (pathfinders au adventurers)
- Tembeleeni shamba kubwa kama la mkonge.
- Tembea na watoto kwenye chombo cha utangazaji wa habari au TV stesheni.
- Anzisheni shuguli ya huduma na kuendelea kuifanya kama familia; kama kutembelea watoto yatima, vilema n.k.
- Kavueni samaki pamoja

B. Mambo 20 yanayosaidia tabia njema kwa watoto:

1. Mambo ya kiroho ya kumpenda na Mungu, kumtukuza kusali na kusoma neno lake yanakuwa kipaumbele.
2. Kazi ithaminiwe. Mtoto asiwe mvivu afanye kazi. Na apate muda wa kupumzika jioni na siku ya saba ya juma.
3. Mtoto amtegemee Mungu asiwe mtu wa kujitegemea yeye na akili zake.
4. Ajue maovu ni mabaya na yanapaswa kujutiwa. Aishi maisha ya usafi.
5. Ajifunze na awe na unyenyekevu.
6. Awe na ari na shauku ya kutenda mema.
7. Awe anatenda mambo kwa dhamira njema.
8. Atii mamlaka.
9. Aheshimu haki za watu wengine.
10. Aweze kuonyesha huruma, ukarimu na huduma.
11. . Aweze kuwa mpatanishi na kujua jinsi ya kutatua magomvi.
12. Aweze kuthamini kwa hali ya juu, uhai wa binadamu.
13. Alinde maisha, na mali za wengine. Aepuke vishawishi vya kuiba au kudhulumu.
14. Awe mtu mwaminifu mwenye viwango bora, (honesty and integrity)
15. Aweze kukubali matokeo au adhabu ya tabia mbaya, japo adhabu hiyo ni ngumu (accept the consequence of bad behaviour whatsoever).
16. Ajifunze kuwa mtu wa shukurani na ampongeze mtu anayepaswa kupongezwa. Akumbuke maneno matano ya dhahabu: Tafadhali, asante, pole, samahani, naomba.
17. Ajue kumaliza shughuli au majukumu (mzazi ufuatilie), na afanye akiwa na dhamira nzuri.
18. Ajue jinsi ya kuwa wakili mwema kwenye mambo ya fedha, asiwe mfujaji.
19. Atunze mwili na vitu vyake vyema, na kwa usafi, chakula, mazoezi yale kumi.
20. Ajue jinsi ya kujieleza mawazo yake na kusikiliza wengine wakieleza.

Sura ya 40
AFYA YA MZAZI
AFYA YA KUSAFISHA MWILI NA KUJITATHMINI AFYA YAKO

Kuna njia nyingi, pengine zaidi ya mia moja, za kusafisha mwili. Tunashauriwa kufanya hivi kila baada ya miezi mitatu mpaka sita. Kuna uchafuzi na misongo mingi katika maisha yetu ya kila siku, na hivyo kufanya usafishaji wa miili yetu kuwa jambo muhimu. Kabla hujazifanya ni vyema uzungumze na tabibu wako kama una magonjwa fulani, kama kisukari, itabidi uwe chini ya uangalizi. Mwili unajisafisha wenyewe ukifunga kula kwa muda; yaani ufungaji ambao unaambatana na kanuni za afya.

Wataalamu wa wanyama wamechunguza kwamba wanyama, hata mbwa, wakivunjika au wakiumwa, wanaacha kula kwa siku kadhaa, na hii inawaletea uponyaji. Watu wengine chini ya usimimazi wa tabibu wamefunga siku arobaini, kwa kunywa maji, pengine kwa kusaidia afya zao za kimwili au kiroho. Hili sitazungumzia hapa, bali nitazungumza kama njia nane za kusafisha mwili.

Wakati wa kusafisha mwili, epuka mafuta, nafaka za kukobolewa; kama mahindi, mchele, unga wa ngano au sukari. Kunywa angalau lita tatu za maji. usile jamii ya nyama, maziwa au mayai. Jitahidi kula mboga mbichi na matunda mengi. Fanya mazoezi, na upate muda wa kupumzika. Punguza chumvi na vikolezo vingine. Hakikisha unatumia vitunguu saumu kwenye saladi zako. Salad mbichi zenye vitu vifuatavyo:- vitunguu, nyanya, kabichi, matango, radish, beet root, karoti, pili pili hoho, celery, giligilani, maparachichi, korosho, nazi n.k.

Zamani Waafrika wengi walikuwa na njia za kusafisha mwili mara moja kwa mwaka. Walikunywa majani/miti fulani na kuharisha. Mengine yalikuwa hayajafanyiwa utafiti vizuri. Ila kwa sasa aloe vera, vitunguu saumu, ndimu na mchunga vimefanyiwa utafiti; na kuonyesha kwamba vinasaidia kusafisha mwili kuliko mboga nyingine. Pia hufanya tindikali (acid) ya mwili kuwa sawa,
(7.35-7.45). Hii inasaidia magonjwa kama kansa, flu, presha, na sukari kupungua sana. Mwili haufai kuwa kwenye tindikali (acid) bali jivu kidogo (base). Twapasa kula vyakula vya tindikali kwa 20% tu na jivu 80%.

Niliona madaktari wanaojaribu kutibu kansa na utafiti wa maji ya ndimu tatu na baking soda isiyo na alminium (sodium bicarbonate) kijiko kidogo, mara mbili kwa siku, ili kupunguza tindikali ya mwili na kufanya kansa itokomee. Angalia kwenye website majina ya matabibu hawa; Dr Mark Sircus n.k. Yaonekana miili yetu ikiwa na tindikali zaidi na kupungukiwa na Vit D inapungua kinga na kuwa na riski kubwa ya kansa.

Kusafisha mwili, kunarudisha tindikali na vinginevyo kwenye mwili kuwa katika hali njema kwa jinsi inavyowezekana (as closely as it can get). Vitu hivi vyenye bei rahisi mara nyingine havipendwi na kampuni kubwa zinazopata pesa nyingi kwa kutibu watu. Na hivyo utafiti wake hautolewi pesa sana maana utafanya mifuko ya wengi kusinyaa (shrink).

Unapofungua baada ya kufunga siku kadhaa, au unapokuwa unasafisha mwili, epuka kula vyakula vya kupikwa unapoanza kufungua, vinafanya tumbo lipate shida. Anza na matunda na mboga chache, au juisi halisi- zisizopikwa za matunda na mboga, kwa siku chache kabla ya kuanza kutumia chakula kilichopikwa.

SAMPLE za KUSAFISHA mwili:

1. Kunywa maji ya safi (distillled) lita nne hadi lita sita kwa siku kwa masaa sabini na mawili, au siku tatu (usipokuwa na ya distilled, jaribu yoyote yasiyo na dawa kama chlorine, ila maji safi au ya kisima). Kisha kula vyakula vibichi tu, visivyopikwa, yaani mboga na matunda kwa siku saba. Kwa kawaida siku ya pili , njaa yako yote inatoka. Usichanganye matunda au mboga- yaani kifungua kinywa kikiwa mboga, chakula cha mchana kinakuwa matunda n.k.

Dr Calvin Dence wa Savannah Tennessee, ametusaidia wengi kwa mpango wake huu wa kufunga. Wakati unaendelea kufunga zile siku tatu, tumia enema ya kahawa au maji kusafisha tumbo ili ule uchafu kwenye utumbo utoke, na usinyonywe kurudi mwilini tena. Maana usipoenda choo, utumbo unanyonya vingine ambavyo vilikuwa viwe takataka za kutupwa. Kama haiwezekanai kutumia enema, tumia chumvi na maji ya vugu la moto (salt flush). Asubuhi ukiamka chukua vijiko viwili vya chumvi isiyo na iodine, ile ya baharini (seasalt) vijiko viwili vikubwa, kwenye lita moja ya maji ya uvuguvugu, na unywe. Fanya hivi siku ya pili ya kufunga. Uyanywe mkupuo umesimama ili usiyatapike. Kaa karibu na chooni katika muda wa masaa 3 utaenda chooni. Kwa siku tatu kila ukiamka, tumia haya maji ya chumvi (salt flush). Katika siku hizi tatu pia chemsha maji mengi, zaidi ya lita nne, na uyafunike na kifuniko kwa ajili ya kujifukizia. Yakichemka chukua kiti na ukae, jifunike mwili wote na blanket, na

hata chini yasionekane mashimo pale ulipokaa (jokofu). Kisha ulete sufuria lile mbele ya miguu yako, ila lisikuguse maana ni moto sana (ndani ya blanket). Fungua sufuria lile na inamisha uso wako kidogo kulitazama, ukikoroga pole pole maji yake ili mvuke ukaribie na uso wako kwa mbali kidogo. Jasho jingi litakutoka. Ufanye hivi kila siku, kwa siku tatu au saba ukiweza (hii ni kama huna vifaa vya sauna bath!)

2. Kunywa kijiko kikubwa cha mkaa kwenye glass ukiamka asubuhi, baada ya saa moja, tengeneza aloe vera na kunywa glass moja (jani au unga), na baadaye Cayenne pepper punje chache kwenye maji. Endelea kunywa glasskumi na mbili hadi kumi na sita za maji. Fanya hivi kwa wiki mbili hadi mwezi. Kula salad sahani kubwa, yenye vitunguu saumu vingi! Wakati wa kusafisha mwili kumbuka kutokula vyakula vya kukobolewa, kutokula nyama, au mafuta. Kula mboga na matunda mengi. Ukiwa na dawa za chai (herbal tea) waweza utumie. Zinginezo ni kama mchunga, vitunguu saumu, ndimu n.k.

3. Kusafisha mwili kwa kutumia maji ya miwa, punje za pilipili ya cayenne na ndimu. Usipokuwa na maji ya miwa, tumia maple syrup na ndimu (au pengine sukari guru pure yaweza kufaa). Kila siku, kwa siku saba hadi kumi, chukua galoni la maji yaliyochanganywa na maji ya miwa, ukipenda galoni na nusu. Changanya ipendeze, kinywaji kizuri cha maji ya miwa, ndimu na pilipili ya cayenne ya unga kwa mbali sana (ichote na kidole gumba na shahada-pinch). Ladha yake inavutia, ila kama ni mnene sana punguza miwa kidogo! Utapungua kilo tano hivi kwa siku hizo!

4. Kwa siku kumi, toa mafuta, jamii za nyama zote (animal products), na vyakula vilivyokobolewa. Tumia zaidi mboga za majani na nafaka, maharage au jamii ya karanga kwa uchache sana, ukinywa glass 12-16 za maji au zaidi ukiweza. Kula kachumbari (salad) nyingi, mbichi mbichi.

5. Kunywa maji kwa siku saba, ila kila siku kwa ajili ya kufanya makamasi ya ukuta wa utumbo wako yasikwanguliwe (mucus lining), tengeneza glass nne za asali na ndimu unywe. Fanya hivi kwa siku saba, kama una ugonjwa wa kisukari au ugonjwa mwingine (mwulize tabibu wako).
6. Kuna aina nyingi za dawa za asili (herbs) ambazo zinasaidia kusafisha mwili, mfano:- gaia herbs (supreme cleanser), inasaidia wengi kupunguza mzio baada ya kusafisha mwili. Uchafuzi wa anga, wafanya wengi kwenye nchi za magharibi wawe na mizio mingi hasa wakati mimea na chavua za maua (pollen) zinaanza kutokezea. Hizi zipo kwenye maduka ya dawa ya asili (herbal stores) kwenye baadhi ya nchi.

7. Kusafisha mwili kwa kutumia Psyllium husks (kijiko kimoja kidogo) na mollases (kijiko kimoja kidogo), changanya kwenye maji glass moja na kunywa kabla ya kila mlo. Kama unakula mara tatu kwa siku fanya mara tatu! Fanya hivi kwa mwezi mpaka miezi mitatu. (Rejea juu vyakula vya kula wakati wa kusafisha mwili).

8. Jinsi ya kusafisha nyongo (gall bladder). Hii inashauriwa kila baada ya miezi sita. Endapo una shida ya mawe ya ghafla (acute) wapaswa umwone tabibu.

Vinginevyo, chukua juisi ya matofaa (apple juice kama nusu galoni mpaka galoni kwa siku). Kunywa juisi ya apple na maji tu! Ikiwezekana upate ile imeandikwa organic apple juice. Kunywa hii juisi na maji tu kwa siku nne. Ikifika siku ya tatu kabla ya kwenda kulala usiku (labda saa mbili usiku), chukua ¾ kikombe cha mafuta ya mizeituni (extra virgin, cold pressed oil), na ¾ kikombe cha maji ya ndimu au limao uliyokamua kisha yachanganye. Simama unywe, jaribu yawe na baridi kidogo ili uyameze kirahisi! Kisha lala upande wa kulia, na miguu yako uikunje, kama aliyepiga magoti kitandani. Kichwa chako kiwe juu ya mito miwili hivi. Lala mpaka kesho yake asubuhi. Ikifika asubuhi tengeneza lita ya maji ya chumvi na vijiko viwili vya chumvi isiyo na iodine (salt flush). Kisha unywe, kama una vimawe kwenye figo au nyongo kwa kawaida utayaona yanaelea ukienda chooni, yanakuwa ya kijani cha bluu hivi. Siku ya nne ya kuendelea kunywa hiyo apply juisi na maji, asubuhi yake kunywa tena yale maji ya chumvi (salt flush). Usiku wa nne waweza kuanza kula matunda na mboga au juisi za maji ya mboga na matunda.

9. chukua mkaa kijiko kimoja kikubwa, aloe vera na ndimu, na kunywa asubuhi na jioni kwa Wiki mbili hivi.

10. Kula mboga na matunda tu yasiyopikwa kwa miezi miwili au mitatu.

Kwenye website nyingi wameandika kutumia chumvi ya magnesium (Epsom salt or magnesium salt) wakati unasafisha nyongo- gallbladder cleansing, sishauri maana kuna wengine wana mzio mbaya wa hii chumvi (allergy), hata hivyo watu wengi wamefanikiwa na juisi ya apple, ila yahitaji nidhamu ya kutokula! Ambayo ni ngumu, ila kwa afya kama hauna magonjwa, ndiyo rahisi kwa pesa na afya kupita zote. Wale wa magnesium salt nafikiri wana siku mbili, za kushugulikia hilo na pia waweza kula. Fanya hii ya juisi ya apple, ambayo haina madhara mengi yanayojulikana (side effects).

Title: Uponyaji wa asili kwa kufuata sheria za afya
Sura ya 1
KUJIPIMA AFYA YAKO KWA MTINDO WA MAISHA YAKO (LIFESTYLE ASSESSMENT)

Angalia zaidi kwenye Natural Healing through the Laws of Health website
N.B. Mafundisho ya afya unayopata ni kwa elimu yako kwa ujumla na siyo kwa ajili ya ugonjwa ulilo nalo (not specific medical advice). Sisi si madaktari wa kukwambia unaumwa nini , mwone tabibu wako kabla hujabadilisha yale tuliyoandika. Kujipima na hiki kipimo kutakusaidia kuangalia unayofanya vibaya na hivyo ni muhimu uzungumze na tabibu akusaidie jinsi ya kufanya afya yako iwe nzuri. Shika hatamu ya afya yako.

Jina----------
Anuani yako---------- kabila----------
Andika listi ya shida za afya au magonjwa uliyo nayo:

Mara ya mwisho ulimwona tabibu lini?----------Je, uko kwenye matibabu wakati huu?----------
Kama ni ndio, unapata matibabu gani?----------
Andika upasuaji ambao umeshahi kufanyiwa na tarehe zake ----------
---

Umeshawahi kuugua magonjwa gani?----------
----------Weka duara kwa ugonjwa uliowahi kuugua kati ya haya: Kizunguzungu, kuzimia, kichefuchefu, maumivu, moyo kwenda mbio, uchovu mwingi, kusahau sahau, kutopata usingizi, kuvuta pumzi kwa shida, kufa ganzi, ngozi kuwa na baridi na kutoka jasho (clammy skin), miguu/mikono baridi, kufunga choo, kuharisha, kiungulia, mafua, kikohozi, macho kutoona vizuri, minyoo, kuvimba sehemu ya mwili, sehemu ya mwili kunuka, kutoweza kufanya tendo la ndoa (kwa wanandoa),kupoteza nywele, joto mwilini, infection, kutokwa damu, kupungua uzito, unene, kupungukiwa damu, matatizo ya hisia au maradhi ya akili
sonona, kutegemea mtu kupita kiasi, woga wa kupita kiasi (phobia), wasiwasi wa muda wote (chronic anxiety), manias, kurudia rudia vitu (obsessive compulsive disorder), bipolar, sizofrenia, neurosis.

Umri wako ----------Jinsia----------
Umeoa?----------umeolewa?----------umeachika?----------mjane/mgane?----------
Umekaa kwenye ndoa au kuachika kwa muda gani?--------
Uzito wako---------- urefu wako----------
Presha yako----------mapigo ya moyo---------- sukari------(chukua kipimo cha sukari yako masaa mawili baada ya kula).

Kolestroli-------- Mafuta kwenye mwili (triglycerides)------
Andika list ya madawa yote ya hospital unayokunywa----------

Je, unapenda kufanya matengenezo kwa mambo yanayoharibu afya yako?----------
---

Kwa jinsi gani?----------

Andika (list) miti shamba au vitamini zote unazokunywa.

LISHE: (chora duara au andika jibu pembeni)

1. Je, unakula nyama ya nguruwe, pweza, kamba,sungura- ndiyo hapana
2. Je, unakula nyama, maziwa, jibini, chocolate, mayai na samaki zaidi ya mara mbili kwa wiki? -Ndiyo hapana

Andika unavyokula----------
---

3. Je, unakula vyakula vilivyokobolewa kama vile sukari nyeupe, mikate myeupe, wali mweupe, mahindi au ngano iliyokobolewa? -Ndiyo ---------hapana
4. Je, unakula matunda mangapi kwa siku?---------

5. Je, unakula mboga kiasi gani kwa siku?----------
6. Je, unatumia viungo kama haradali, mdalasini, siki, pilipili manga, mayonnaise, tomato sauce, achari, nutmeg au ajino moto (monosodium glutamate)?-------
7. Je, unakula vyakula vilivyokaangwa?---------- Mara ngapi kwa wiki----------
---
8. Je, unatumia margarine? Au siagi? Mara ngapi kwa wiki?----------
---
9. Je, unatumia baking soda au baking powder?
   Ndiyo au hapana
10. Je unakula mkate uliookwa masaa 48 ya kwanza
    baada ya kuokwa?
11. Je, unakunywa milo, cocoa au kahawa?

    Ndiyo au hapana
12. Je, unapikia mafuta gani?----------
13. Je, unasoma lebo za vyakula kabla hujanunua?
    Ndiyo au Hapana.
14. Je, unatumia nini kwenye kinywaji ili kiwe kitamu?
    sukari, asali, sweet & low, equal, artificial sweeteners?
15. Je, unakula jamii ya karanga? Kiasi gani na mara
    ngapi kwa wiki?----------

16. Je, uko katika diet maalumu? Ni diet gani?--------
17. Je, unapenda kula nje ya nyumbani kwako? Mara ngapi kwa wiki?----------
18. Je, unatumia chumvi? Je, ina iodine?----------
19. Je, unafunga angalau mara moja kwa wiki, angalau milo miwili?----------

---

Mazoezi:

1. Je, unafanya mazoezi?- Ndiyo au hapana
2. Mara ngapi kwa wiki?----------
3. Mazoezi yako ni ya aina gani? Ya kawaida Ya nguvu
4. Je, unapenda mazoezi ya aina gani?----------
5. Je, unasikiaje baada ya mazoezi?----------
6. Je, unapata maumivu baada ya mazoezi?----------

Maji:

1. Unakunywa glasi ngapi za maji kwa siku?----------
2. Je,kwa kawaida unakunywa maji ya aina gani?---------
3. Je, maji yako yamechujwa na kuchemshwa?----------
4. Je, maji yako yanakaa kwenye plastiki kwa muda mrefu?----------
5. Unakunywa maji yako yakiwa na joto gani? (baridi, moto, uvuguvugu)----------
6. Je, unapenda kula barafu?----------
7. Je, unakunywa glasi ngapi za juisi kila siku?----------
8. Je, unakunywa chai, mvinyo, vileo, maziwa, soda, na maji ya vitamin?----------
9. Je, unakunywa maji na chakula chako pamoja?---------
10. Mkojo wako una rangi gani? - Manjano, kahawia, kama maji?

Jua:

1. Je, unaota jua angalau kwa saa moja kila siku, hasa la asubuhi na jioni?----------
2. Je, unakaa kwenye jua siku nzima? (swali kwa zeru zeru) Masaa mangapi?----------
3. Je, unadhurika na jua kirahisi? Au dawa unazokunywa zinakufanya udhurike na jua kirahisi?----------
4. Je, unachukua vidonge vya vitamini D?----------
5. Je, familia yako ina historia ya kansa ya ngozi?---------

Kiasi:

1. Unafanya kazi gani?
2. Andika listi ya kazi tano ambazo umeshawahi kuzifanya na miaka uliyozifanya.----------

3. Je, unatumia tumbaku?----------
4. Je, ulitumia tumbaku siku za nyuma? Kwa muda gani?----------
5. Je, unatumia kileo cha aina yoyote? Kileo kipi na umetumia muda gani?----------
6. Je, unatumia vinywaji vya kafeini, kama kahawa, cola, , red bull (vinywaji vya kuleta nguvu)? Andika listi:----------
7. Je, unakula kupita kiasi?- (Ndiyo, hapana, mara nyingine)
8. Je, unakula kwa haraka mno?- (Ndiyo, hapana, mara nyingine).
9. Je, unatafuta chakula chako vizuri? -Ndiyo, hapana
10. Je, unakula kula, au kunywa kati ya milo?- Ndiyo, Hapana
11. Je, unakula keki, peremende na vitu vyenye sukari? -Ndiyo au hapana.
12. Je, unakula kwa wakati maalumu kila siku? -Ndiyo hapana
13. Wakati gani unakula kifungua kinywa, chakula cha mchana na chakula cha usiku?----------
14. Je, waweza kusema unavaa kwa afya na kiasi?- Ndiyo au hapana
15. Andika list ya burudani unazopenda kushugulikia kama runinga, michezo, kudansi, au bao.
16. Je, unachukua muda gani kwa wiki kwa mambo ya burudani?----------
17. Je, unafanya kazi kupita kiasi, kwa masaa mengi kwa siku na za kuchosha mno?- Ndiyo, hapana
18. Orodhesha ulevi ulio nao, mfano pombe, sigara, kahawa au madawa ya kulevya----------
19. Je, umejihusisha na madawa ya kulevya?----------
20. Orodhesha vitabu unavyosoma kama ni vya fiction,fasheni, michezo ya computa, (ponografia), science ----------
21. Je, unahudhuria sinema, klab za dansi, masherehe (pati), Orodhesha ni ipi----------

---

22 Je, unacheza michezo ya hatari? Ipi?----------

---

23. Je, unasikiliza miziki ya aina gani? Orodhesha mfano: rap, disko, rock, ya kwaya za ibada, ya uzalendo (patriotic), n.k.

Hewa:

1. Unaishi wapi? Mjini? Nje ya mji kidogo? Kijijini?----
2. Je, unalala madirisha yakiwa wazi? -Ndiyo au hapana
3. Je, unafungua madirisha kila siku kupata hewa bora - Ndiyo au hapana
4. Je, unaishi kwenye moshi mwingi au karibu na viwanda? - Ndiyo au hapana
5. Je, unaishi na watu wanaovuta sigara? -Ndiyo au hapana.
6. Je, una mimea mingi uliyootesha ndani ya nyumba yako? -Ndiyo au hapana
7. Je, una machafuzi ya hewa yapi kwenye mazingira yako?

8. Je, unavaa nguo zinazokubana?

Mapumziko:

1. Kawaida unalala saa ngapi usiku?
2. Je, unaamka amka usiku? -Ndiyo au hapana
3. Unakula chakula mara tu kabla hujalala?- Ndiyo, hapana au mara nyingine
4. Je, unalala na taa zikiwa zinawaka?- Ndiyo, hapana au mara zingine
5. Je, unafanya kazi ya shift, yaani mara asubuhi au usiku? -Ndiyo au hapana.
6. Je, unaamka kabla ya kuchwa na unashindwa kulala tena? -Ndiyo au hapana
7. Je, unakunywa dawa za usingizi?- Ndiyo au hapana?
8. Je, una muda maalum wa kulala kila siku? -Ndiyo au hapana.
9. Je, unakomesha shughuli zako na kupumzika angalau mara moja kwa wiki? - Ndiyo au hapana
10. Je, unafunga angalau mara moja kwa wiki milo miwili?

Kumtegemea Mungu:

1. Je, unaomba kila siku?- Ndiyo au hapana
2. Kama la, Je, ungependa ufanye vile? -Ndiyo au hapana
3. Je, unasoma neno la Mungu kila siku?
4. Je, unarudisha zaka na sadaka ya uaminifu kwa Mungu?- Ndiyo au la?
5. Je, unapata shida kumtegemea Mungu kwa shida zako?- Ndiyo au hapana
6. Je, unajutia mambo fulani, dhamiri inakushitaki, unakuwa na woga au mashaka kwa sasa?- ndiyo au hapana
7. Je, unaamini kwamba ukiomba msamaha Mungu anakusamehe kabisa? -Ndiyo au hapana
8. Je, unapata shida kuelewa mapenzi ya Mungu katika maisha yako? -Ndiyo au hapana
9. Je, unafikiri familia yako ina mahusiano mazuri? -Ndiyo au hapana
10. Je, familia yako inapenda mambo ya kiroho? -Ndiyo au hapana
11. Je, unajisikia una amani na Mungu na watu pia?- Ndiyo au hapana
12. Je, umevunja nadhiri zako ulizomwahidi Mungu, ambazo ziko kwenye uwezo wako kutimiza?- Ndiyo au hapana
13. Je, unaona Mungu anakutendeaje ? how has the Lord been treating you?
14. Umekuwa ukimtendeaje Mungu?
15. Endapo leo ingekuwa siku ya mwisho au siku ya hukumu ili kwenda mbinguni au jehanamu; ukijua maisha yako unayoishi, Je, ungeokolewa?

(Majibu ya maswali haya yapo kwenye hiki kitabu. Form Ukijaza foamu hii na kuifikiria, itakusaidia).

Kuishi kwa afya kunasaidia kupunguza maumivu na pesa nyingi kupotea. Pia utasaidia wengine utakapogundua mambo haya. Kila utakapopita kama ndugu, jamaa, rafiki na familia. Utakuwa mtu mwenye nguvu zako za kufanya shughuli zako. Watoto Wako utawasaidia kwa ubora ukiwa na afya kwa kutafuta riziki, kucheza nao, n.k. hata watoto utawasaidia wawe na afya kwani tunarithi mitineo ya maisha toka kwa wazazi wetu.

Mtu mmoja alisema kwamba, “Kama ni kufa niache nife kwa raha, kama ni kula au kunywa vitu vibaya, si mwili wangu?” Miili yetu ina thamani kubwa. Mungu alituumba ili tumtukuze. Tukiumwa Muumbaji wetu anasikitika na hivyo kama tunaumwa kwa ajili ya mitindo yetu ya maisha ni lazima tutathmini na kufanya mapinduzi. Jamii yetu yatupasa itushugulikie. Mfano mtu anayeumwa kisukari na baadaye akakatwa miguu kwa ajili ya athari za kisukari, jamii yake itabidi imwuuguze, imtafutie chakula, imsukume kwenye toroli au kumsafirisha sehemu mbali mbali kwa kutumia.

Binadamu si kisiwa. Hata sasa tumekuwa kama kijiji cha dunia (global village). uzalishaji wa mgonjwa unakuwa mdogo. Familia yake, watoto na mume au mke wake watakuwa na huzuni kumwona katika hali hiyo. Hivyo si kweli kwamba afya yako ni yako haimhusu mwingine. Hata serikali inatumia pesa nyingi kushugulikia afya za watu katika nchi mbali mbali duniani. Tabibu wa kwanza ni wewe.

Kwa kawaida, Daktari hana nafasi, na mtu mmoja sana; ana watu wengi wamesimama kwenye mstari wakimngoja. Anachukua dakika mbili au tatu hivi, ameshakuandikia dawa! Hakujui, hajui unavyojisikia wala hana uchungu kama wewe ulivyo na uchungu juu yako. Wewe unajua unasikia nini mwilini na mambo yamekuwa yakiendaje kwenye mwili wako. Ni vyema uende hospitalini au klinik kwa check up na watoto pia; pengine kila mwaka, kama si magonjwa ya au dharura (acute); kama kuvunjika mguu, kupooza, au jambo la ghafla limetokea kwenye mwili wako. Vinginevyo palilia afya yako kwa kufanya mambo rahisi kila siku. Hata kwa majirani zetu tunawanyima, yale mema ambayo wangepata kwa ajili ya mifano yetu. Huwezi kuwasaidia kimwili, kijamii, kiroho au kiuchumi kama unaumwa. hata kuwasaidia kubeba mizigo wakihama. Ujirani mwema unakuwa ngumu maana wewe mwenyewe umefilisika na ni mhitaji wa nyanja zote. Hauwezi kuwasaidia, hata kama una nia hiyo.

Nchi za magharibi imeonekana watu wameishi muda mrefu, ila wanaishi wakiwa na magonjwa mengi ya muda mrefu (chronic) na maumivu mengi. Na maisha yanashikiliwa kwa “nyuzi ya buibui” kwa mashine au vitu fulani.

Lazima tuelewe kwamba elimu ya sayansi ya binadamu ya utabibu (medicine history) imetoka mbali! Mungu ndiye mponyaji mkuu na mwanzilishi wa sayansi. Wanasayansi wengi wa magharibi wasema tumetokana na sokwe, au chura! Naamini wewe huamini vile. Japokuwa waganga wa kienyeji wanatumia nguvu za shetani, ukiwaambia waliumbwa na

nani wanasema ni Mungu. Bali wanasayansi wenye vipimo vizuri vya tiba kama xray, malaria, damu na kadhalika, wanaamini walitoka kwa sokwe!

Baada ya kufanya katika vituo vya afya kama mahospitali, kwa muda wa miaka ishirini na miwili, nimegundua kwamba ni miaka kama sabini tu ambapo tiba imeweza kuwa na vipimo na mashauri mengi ya kufaa. Kabla ya hapo imekuwa pata potea na bahati nasibu. Kwenye kitabu, "Doctors killed George Washington," na vingine, wanaeleza historia ya tiba ya kisasa. Rais wa Marekani wa kwanza aliuawa na madaktari, mtu akiwa na homa enzi hizo walimchanja na kumtoa damu ili homa ipungue; "blood letting!" Hii ilimfanya aishiwe na damu! Hata watu waliougua kikohozi waliambiwa wapate mivuto mitatu ya sigara asubuhi na jioni kama tiba! Sasa imegundulika kwamba sigara ni sababisho la kwanza la magonjwa ya mapafu.

Hata kule kunawa mikono tu, wakati wa kushugulikia mgonjwa hadi mgonjwa, wakifanya upasuaji kumekuja karibuni! Asilimia themanini ya magonjwa yote hujiponya yenyewe bila ya kushugulikiwa! Ndivyo Mungu alivyotuumba. Jukumu letu ni kuleta mazingira yanayostahili ili miili yetu itumie hii asili ili kujiponya yenyewe kwa mafanikio.

Kuna kitu cha ajabu kwenye nchi nyingi kama Israel na hata Marekani kilichochunguzwa. Kwamba, wakati wa mgomo wa madaktari vifo vinapungua! Je, ni kwa sababu matabibu hawapo kuandika vyeti vya kifo? Au kuna sababu nyingine, kama kuambukizwa magonjwa mengine ambayo haukuwa nayo ukienda kulazwa, huduma hafifu n.k? Jitahidi kufanya upelelezi wako mwenyewe pia! Kila binadamu ana haki ya kufanya upelelezi huo, maana kila mmoja wetu ana jukumu la kutunza afya yake, si wafanyakazi wa afya tu wenye jukumu hilo.

Utafiti wa Marekani ulisema kwamba, watu mpaka laki nne hufa kila mwaka kwa ajili ya madawa ya hospitali. Matabibu wengi wangepaswa kukita kwenye kinga zaidi ya uponyaji. Wengine wana tamaa ya pesa mpaka kufanya upasuaji usihohitajika. Sehemu nyingine mpaka asilimia 50% ya wanawake hujifungua kwa kupasuliwa, (ingawaje wanawake wengine, wa kisasa huchagua kupasuliwa)! Niliuliza, katika hospitali nilipopasuliwa Marekani, wakaniambia kujifungua kawaida, ukikaa hospitalini siku tatu, ni dola elfu thelathini, ila ukipasuliwa ni dola elfu sabini na mbili; na nikapata bill kama kithibitisho! Najua nyingine zahusu kukaa hospital, mtoto kutunzwa na madaktari walioingia kwenye chumba cha upasuaji kama vile anayetoa ganzi, tabibu wa watoto, na tabibu wa uzalishaji. Yapasa uwe mteja unayejielimisha na mambo haya, maana yanatupata sote. Pesa ni shina la maovu mengi. Ingekuwa vizuri kama shina hili lisingegusa miili au afya zetu!

Ni kweli tiba ya kisasa imepitia hatua nyingi na kupata kuvumbua vingi vya kusaidia watu. Siku hizi tuna waganga ambao wanapata vyeti na kusaidia watu. Zamani kulikuwa na wachache wenye vyeti waliotibu watu. Nchi ya Marekani ikigombea uhuru miaka ya 1700, ilikuwa na watu elfu nne na mia tano waliofanya kazi ya utabibu, ila ni mia tatu tu waliokuwa na shahada za udaktari. Ni vyema watu wanaotibu wawe wa tiba rasmi au tiba mbadala; wajifunze na kupata leseni kama matatibu wa watu kwenye jumuiya.

Ikiwa utatibu watu kwenye nyumba yako na kujichukulia tu kama msamaria mwema anayewasaidia, basi nafikiri serikali haitakuambia uwe na cheti na leseni. Ila hata wewe unayetibu nyumbani ujue mipaka yako pale mgonjwa wako anapohitaji rufaa. Ni vyema ujifunze vizuri ili uwe na ufanisi mkubwa wa kusaidia watu. usikidiriki kusema kwamba wewe ni bingwa sana, unatibu magonjwa yote.

Napenda kusisitiza Mungu ndiye mponyaji mkubwa kwani aliumba mwili wa binadamu. Wengi tunajaribu, mengine tunaweza ila mengi tunashindwa. Hii ni vizuri kwa upande mwingine, maana inashusha kiburi chetu kama binadamu na kutufanya tuwe wanyenyekevu. Je, tungeweza kutibu kila kitu ingekuwaje? Nafikiri adui shetani angeinua mapembe yake.

Kwa kusisitiza, japo tuna magonjwa mengi duniani leo sababu zake ni chache mno. Magonjwa mengi yanakuja kwenye akili, hisia na misongo ya mwili ambayo inaletwa na kuinyanyasa miili yetu kwa maisha tunaoishi. Kula ovyo vyakula vilivyokobolewa, na kutofanya mazoezi, uchafuzi wa mazingira, kutokuwa na kiasi kwenye anasa, kazi na maisha ya ngono ni sababu nyingine. Si kila ugonjwa unaletwa na virusi au bakteria. Mara zingine tuna vitabia au mitindo ya maisha inayoharibu miilli yetu. Kuna bakteria wazuri kwenye matumbo yetu na tukila isivyotakiwa wanakufa na tunapata shida nyingi.

Je, unajua kile ambacho tunaita ugonjwa mara nyingi ni rafiki na si adui? Ugonjwa ni dalili au ishara ya kukwambia kuna kitu fulani kimeharibika jaribu kusahihisha! Mfano kama usingepata maumivu na umeweka mkono wako kwenye moto ingekuwaje? Mkono wote ungeungua hasa kama ulikuwa unatazama pengine. Vivyo hivyo hata joto mwilini ni njia ya mwili kusema kwamba kuna kitu kimeenda mrama na unahitaji kusahihisha. Joto linapoongezeka askari wa damu yaani chembe hai nyeupe zinaongeza kasi kwenda kushambulia vijidudu na mishipa ya damu wanayopitia inapanuka ili wapite kwa urahisi na kwa wingi. Sisi tukiona tunaumwa tunaharakisha kumeza panadol wakati ambapo tungeachia mwili nafasi kurekebisha mambo fulani. Unywe panadol kama homa ni kali ila kama si kali ngoja mwili ufanye mpango wa kuondoa shida.

Mara nyingine tukiumwa kichwa kidogo tunameza dawa haraka bila kujiuliza sababu: Je, tumelala vizuri? Je, tumekunywa kinywaji cha kusababisha kuuma kwa kichwa kama kahawa? Masikini binadamu hatujui kwamba ugonjwa ni njia ya mwili kutuweka kwenye hali ya kutoa sumu au kurekebisha mambo. Mara zingine tunatumia antibiotic kwa virusi wakati ambapo hazifanyi kazi kwa virusi.

Je, wajua maelfu wafa mahospitalini kwa madawa na madaktari (iatrogenic causes)? Hata dawa za kawaida kama Asprini ina madhara mengi tu. Jaribu kuangalia hili zaidi; aspirini yaweza kuleta moyo kudhoofika, kuvuja kwa damu, kuharibu vitamin C mwilini. usitumie dawa bila kufikiria.

Nilifanya kazi na Daktari aitwaye Michael Wagner New Jersey. Yeye alikuwa bingwa wa moyo, na alifanya kazi na Jeshi la Marekani Japan wakati Marekani ilipopeleka jeshi lake kule miaka ya zamani. Alisema wale wote aliosoma nao walifariki kabla hawajafikisha miaka hamsini! Nilimwuliza sababu; akasema ni kwa ajili ya mitindo ya maisha yao, kama vile vyakula vibaya (junk food), kutofanya mazoezi, pombe, sigara,

kutopata jua kwa vile wanafanya wastani wa masaa kumi na manane wakiwa ndani ya majengo. Hata kwenye utafiti walisema kwamba katika taaluma zote madaktari wanaongoza kwa ajali za barabarani kwa kuchoka mno, na wengi kutumia madawa ya kulevya, mara kumi, kuliko raia wa kawaida! Na manesi mara nne kuliko raia wa kawaida (impaired).

Tunasisitiza, Kuna madaktari wengi tu wenye tabia njema za afya wanaofanya mambo tunayozungumzia rahisi. Ila nachotaka uelewe, kusomea mambo ya afya na kuyafanya ni vitu viwili tofauti! Na vitu rahisi ndivyo vinasaidia afya mara nyingi kuliko vile vya teknolojia nyingi. Mungu Alifanya hivi ili kila mtu afaidike. Yeye Hana ubaguzi, anatupenda sote, na jua lake lamulikia watu wote; wale wanaomjali na wasiomjali. Tufuate masharti yake rahisi.

Jaribu kuchukua dawa yoyote na kuangalia madhara yake! Kutapika na kichefuchefu itakuwa kwenye karibu zote. Sisemi usitumie dawa, la hasha! ila usiwe na uzoefu wa kuziingiza mdomoni bila kujua unaumwa nini au kuchukua muda kufikiri. Wenye viwanda vya madawa wanataka utumie wakati wote, kwa sababu ni faida kwao. Ila wewe kama binadamu wapaswa kutumia jukumu lako la haki ya kufikiri na kuchagua kile kitachokusaidia kwa wakati huo.

Dawa yaweza kuwa sawa leo ila kwa siku nyingine pengine tiba nyingine ndiyo bora. Chuja mambo ya vyombo vya habari, jua mwili wako na familia yako, wapi utumie nini. Uwe mteja mwenye kujielimisha (educated consumer). Asilimia hamsini hadi sabini ya chakula chako kiwe vitu visivyopikwa yaani mboga na matunda. Na kama una ugonjwa mkubwa, asilimia 90-100%. Acha sukari kabisa ni mojawapo ya sumu za mwili. Kufunga choo ni kitu kibaya kwa mwili kwa vile sumu haziondolewi, na damu inazidi kuchafuka na kusumisha mwili.

Hatuna budi kusema kwamba usafi ni kitu muhimu sana ambacho kitabu hiki hakiwezi kujadili kwa undani sana. Usafi wa mwili, mavazi na mazingira yetu. Kila aina ya uchafu una mwelekeo wa kuleta magonjwa. Vijidudu vinavyoleta mauti vimejaa katika pembe za nyumba zenye giza na uchafu. Katika uchafu unaooza, unyevu na uvundo kuna madhara. Usiruhusu hata mboga za majani au malundo ya majani yaliyoanguka kubaki yakiwa yanaoza karibu na nyumba yako maana husumisha hewa. Kitu chochote kichafu na kilichooza kisipate nafasi ndani ya nyumba yako.

Miji mingi inayodhaniwa safi imeonekana na magonjwa mengi ya homa na kuambukiza watu wengi yamegundulika kutokana na takataka zilizooza. Kuna siku mvua ilinyesha magazeti yakaandika kwamba New York ina panya milioni kumi na mbili! Uchafu huizunguka nyumba kwa ajili ya uzembe. Oga vizuri na watoto wako uwafundishe kuoga na kufua nguo vizuri. Nawa mikono, na usiingie na viatu vyako nyumbani mwako baada ya kutembea mji mzima! Unaleta ugonjwa nyumbani. Nyumba isafishwe vizuri.

Usafi wa moyo ni muhimu sana. unaboresha afya yako. Chuki, masengenyo, wivu, tamaa, manung'uniko, kiburi, malumbano, malalamiko, kukosoa kosoa, kujivuna, dharau, kiburi, jeuri, ukorofi, ubinafsi, uchawi, ulevi, kutosamehe, ukatili, magomvi, ulafi, lawama, uasherati na mengineyo yanabomoa afya.

Mambo muhimu ya afya ni yafuatayo-tiba rahis . tunayaita matabibu 10:

1. lishe
2. mazoezi
3. maji
4. jua
5. kiasi
6. hewa
7. mapumziko
8. kumtumaini Mungu
9. roho ya shukurani

10 kuhudumia watu na ukarimu

Baada ya uumbaji afya ya mtu kimwili, kiroho, kihisia, kiakili, ilikuwa makamilifu. Pumzi ya uhai mtu aliyopuliziwa na Mungu ilimpa uhai kamili (whole or total health). Lakini baada ya kuanguka kwa mwanadamu maisha yalibadilika. Inabidi tujifunze maisha ya bustani ya Edeni na ya mbinguni. Ndiyo kamili kuyafuata maana ndiyo aliyoumbwa binadamu awe nayo. Yeye ndiyo ana masharti au maagizo ya matunzo ya miili yetu (body manual). Sisi ni wasafiri baada ya kuanguka kwa mwanadamu bustani ya Eden, ukarabati ulitakiwa. Pambano la wema na uovu limekuwa likiendelea toka dhambi ya kwanza ilipotokea mbinguni, na kuletwa duniani na Ibilisi, yeye alitupwa na theluthi moja ya malaika.

KUKUZA MTOTO WA KIUME AWE KUHANI KUSIMAMIA NYUMBA YAKE au (kukuza mwana awe mlei- wameandikiwa watoto wa kiume na wazazi)

Wengi wameandika vitabu vya kukuza watoto wa kiume kwa waumini. Kukuza mtoto wa kike hakuna tofauti kubwa na kukuza mtoto wa kiume isipokuwa pale majukumu ya jinsia yanapotofautiana, kama vile ambavyo Mungu alituagiza. Mungu ndiye mzazi mkubwa, Maandiko ndiyo kitabu cha malezi kikubwa, vingine ni kujazia hicho. Jambo kubwa la kuwasaidia watoto wetu, ni kuwafanya waweze kuishi bila sisi. Waweze kukabiliana maisha kwa mahusiano na Mungu, jumuiya yaani shuleni au kazini, ushirika, na familia zao.

1. ***Mbingu na dunia ndiyo vitabu vya mtoto wa kiume, kabla hajaanza kujua kusoma au kuandika, kama Zaburi 19 inavyosema. Zaburi 144: 12-15 yasema, 'Wana wetu na wawe kama miche waliokua ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni zilizonakishiwa kwa kupamba hekalu. Ghala zetu na zijae akiba za jinsi zote. Kondoo zetu na wazae elfu na makumi elfu, mashambani mwetu ngombe zetu na wachukue mizigo, kusiwe kushambuliwa. Wala kusiwe kuhamishwa. Wala malalamiko katika njia zetu. Heri watu wenye hali hiyo. Heri watu wenye Bwana kuwa Mungu wao."***

Tafsiri ya Mungu ya mwanamume ni zaidi ya kuonekana kwa nje; maana Ezekieli 22:30 yatuambia, ni mtu atakayekuwa tayari kutengeneza pale palipobomoka. Kuwa mwanamume katika Neno la Mungu ina maana kiroho, kiakili, kihisia na kimwili. Mtoto anasaidiwa nyumbani, kwenye jumuiya, shuleni na kanisani

Baada ya kupata watoto lazima tuwe na mipango maana Mungu ametupa wana kama mawakili, ni bustani yetu kupalilia, mpaka wakue na kukomaa. Hatuwezi kukaa tu na kufikiri mambo yatajipa yenyewe. Chakula na nguo havitoshi kukamilisha malezi ya watoto.

Watoto wetu wa kiume watakuwa viongozi katika jumuiya zao, watakuwa makuhani kwenye nyumba zao na watakuwa kaka zetu kule mbinguni siku moja. Tunamtayarisha mtoto wetu wa kiume kuwa mume, baba na muumini katika nyumba ya Mungu. Hii ni safari inayohitaji muda mwingi, na imekita kwenye mhimili wa Neno la Mungu.

Neno la Mungu ndiyo mwanzo na mwisho katika malezi (alfa na omega). Neno la Mungu ndiyo usalama wetu pekee wazazi na watoto wetu. Hebu uweze kuvuna matunda ya kazi yako, ya uaminifu kwa Mungu; na uweze kuwasaidia watoto wako kuwa mashujaa, wanaochukua majukumu na kuzaa matunda mengi ya haki. Luka 2:52 yasema, Yesu alikua kwa kimo na hekima akimpendeza Mungu na wanadamu. Miaka ya kumi na, (teenage), si lazima iwe na shida za ujana na uasi, bali ya uzalishaji (productivity) kwa mwana, wazazi na jumuia. Tusichoke kutenda mema. Maana siku moja 'baba yako na mama yako watafurahi , na yeye aliyekuzaa atashangilia'. 'Sisi kama wazazi tuwachukue watoto wetu kwenye semina za injili au walei, tusiwaache. Tuwachuku katika shughuli tunazomfanyia BWANA ili wajifunze kwa matendo na kuipenda kazi yake BWANA.

Kukuza mtoto wa kiume ampendaye Mungu yahitaji kuwajibika (commitment), maana watoto wetu wa kiume siku hizi wana changamoto ya kujishughulisha kwa bidii, kwenye taaluma na hata kazi za mikono. Asilimia 90% ya mashamba Afrika hulimwa na wakina mama watu wazima. Pia Asilimia 80 ya waumini wengi kwenye nyumba za ibada ni wana wa kike, na ndiyo waonekana na hari ya kwenda shule na kusoma vitabu kwenye nchi nyingi. Zamani kuna masomo ya hisabati au fizikia yaliaminika kuwa masomo ya kiume; na ndio walichukua namba za juu. Utafiti wa Dr Nedley Marekani unasema kwamba namba hizi zataka kufanana na za watoto wa kike siku hizi. Akaongeza kwamba watoto wa kiume wanaona hakuna haja ya kujishughulisha siku hizi kwani kupata mke wa kuoa ni rahisi, wala uhitaji mahari kama zamani.

Wasichana siku hizi ndio wanafuata wavulana. Hii inawafanya wasiwajibike au wasione changamoto au ari ya kufuatilia kitu. Anasema pia watoto wengi wa kiume wanaweza kumudu maisha yao wakitegemea wazazi au mke mpaka uzeeni, endapo mke atashtuka na kumwacha, mke huyu atachukua watoto aende nao, na mume atarudi kwa wazazi na kuwategemea.

Mtoto wa kiume ameumbwa kwa mfano wa Mungu naye aliumbwa kabla ya mwanamke. Kusudi lake halikuwa kuongeza na kujaza nchi kwanza, bali kumiliki na kutiisha nchi. Wana wetu ni lazima wajue hili kwanza. Mtoto wa kiume alipewa kazi ya bustani hata kabla ya maanguko ya binadamu. Utii kwa Mungu na mzazi, ndiyo somo la kwanza kwa wana wetu. kisha mipangilio,Ustadi, taaluma, kutawala nafsi, na kazi za mikono. Hivi vinamsaidia kukana nafsi na kutawala nafsi na kuitafutia riziki familia. Zamani mtoto wa kiume Afrika ndiye aliyetunza wazazi, na kutegemewa na dada zake au wadogo zake kama ndiye mtafutaji, mshauri na kiongozi. Jambo hili limeanza kupungua kwa kiasi fulani.

Japo hiyo ni takwimu ya Marekani, ila unapoona mwenzako ananyolewa, wewe anza kutia maji kichwani. Nchi hii ya Marekani inaweka viwango mara nyingi, japo ni vibaya kama vile vya ushoga, na watu wengine wanafuatilia kirahisi. Mengi siku hizi watoto wanayoona kwenye vyombo vya habari, hasa runinga, yanaigizwa na vyombo hivi

vyawa kama mzazi. Hii ni hatari maana vyombo vingi vya habari, vina machache mazuri, hata kwenye matangazo, watu wanavyozungumza na kuvaa kunakuwa na walakini.

Nilipokuwa mtoto, ilikuwa matusi kumwita mvulana 'msichana;' ila siku hizi hata wavulana wenye nguvu na akili wameingia desturi za maovu kama ushoga, jambo ambalo lilikuwa mwiko, hata kwa wale wasiomcha Mungu. Watu wa nchi kama Ufilipino wanasemekana wanaongoza katika takwimu ya kufanya upasuaji wa wanaume kujibadilisha kuwa wanawake ili maisha yao 'yawe rahisi'. Hii ni kutojua kwamba katika uumbaji, mwanamume ndiye alitangulia naye ni kichwa, na anapaswa kuheshimiwa na mwanamke. Na hata hivyo mwanamke ni mfanya dhambi wa kwanza na sidhani kama hilo linavutia mtu ye yote.

Herodi aliua watoto wa kiume. Farao pia, alijua akimaliza watoto wa kiume, taifa limekwisha. Hata Balaam aliangusha wanaume 24,000 wa Israeli, akijua akimaliza hao amemaliza taifa. Mungu amempa mtoto wa kiume na wanaume karama na jukumu ambalo wana wa kike hawakupewa, hivyo tunapokuza watoto wa kiume tuangalie hili. Wakina baba wakae na watoto wa kiume na kuwafundisha kwa matendo. Wanasema wakina baba wengi hukaa pungufu ya dakika nne kwa siku kuzungumza na watoto wao.

Yapasa kuwa na uchaguzi wa mambo mengi kama vile marafiki, miziki tunayosikiliza, vitabu tunavyosoma, elimu tunayopata, kanisa tunalohudhuria, nguo tunazovaa, na mengine mengi. Wazazi tusome neno la Mungu ili tupate majibu, na viwango vinavyofaa, pia tujifunze kuwa waumini waliokomaa, na kuhudumu pamoja. Hata wale wazazi solemba wanaweza kukuza watoto wanaompenda Mungu. Tunaona Timotheo, na bibi yake Loisi na mama yake Yunia, wakimsaidia Timotheo kuwa shujaa aliyehudumu wengi kama mlei na kisha mchungaji.

Lazima uwe na malengo na mipango ya mwaka mmoja. Huwezi ukafanya yote kwa pamoja, weka ramani kidogo, kile unachotaka ukipate, watoto wahitimu toka nyumbani. Watoto wakiwa wadogo wanakuwa kama sponge; inayonyonya maji mengi. Wanashika mengi ya sayansi na kukariri sana. Tumia muda huu kuwafundisha kutoka kitabu cha viasili na dunia. Mafundisho ya 1 Wakorintho 13 ya upendo, ni muhimu kwa watoto na sisi.

Daima watoto wetu wafundishwe uumbaji wa Mungu na si uibukaji, (evolution). Hili tulipatie kipaumblele; 1 Kor 3:19. Tutumie msaada wa mababu na mabibi kuwasaidia watoto.

Watoto wafundishwe kujenga nyumba, kushona, kupika, kulima na ustadi mwingine. Wafundishe watoto kuzungumza hadharani, kupanga muda wao, na kutathmini wanavyoendelea. Furahi nao kwa walichokiwezea. Wafundishe mashujaa wa mifano ya Neno la Mungu kama Daudi, Nuhu au Ibrahimu. Mwulize kijana wako mashujaa wake ni wapi? Ni watu wa filamu au michezo ya compyuta? Je, awezaje kuwa mshumaa au mwanga wa nyumba yake?

Soma vitabu kama '10 Boys Who Changed the World,' kilichoandikwa na Irene Howard. Je, anawahusudu (admire) watu ambao hawampendi Mungu kama Samsoni? Je, anasoma vitabu vya namna gani?

Maisha ya mwanamume yamejaa maamuzi mbali mbali, na kutenda kutokana na maamuzi, tuwatayarishe vijana wetu kuchukua majukumu kwa kuamua mambo inavyotakiwa. Watayarishe vyema kisha waachiwe nafasi wafanye maamuzi, na wanapokosea wajue kusahihisha. Jifunzeni hata toka kwa wadudu kama siafu, na mifano ya watu kama ya kijana Yusufu, Yethro, Abigaili, Msamaria mwema, Boazi na wengineo.

Usipokuwapo anafanya vitu vyema? Je, anasalimu watu?, anafanya kazi za nyumbani? Angalia kama anatumia muda wake vizuri, na kuacha vitu vyake katika

mpangilio na usafi. Je, anajua kutatua matatizo, au anasahau majukumu yake? Je, anajua muda ni mali na hasemi nitafanya kesho?

Mpeleke polisi, au kotini kutokana na umri na kisha mjadili kesi za kawaida. Soma visa kama vya Akani na Samsoni mjadili. Je, apenda kutoa udhuru au kutia chumvi, na kuweka ahadi asizotimiza? Je, anachukua vitu vya watu bila ruhusa? Je, anapenda umbeya na kushuhudia watu uongo? Tusiwakinge sana watoto wetu na maumivu au kushindwa. Mara nyingine ni lazima washindwe ili wajifunze, ila wasiwe na woga wa kujaribu tena. Soma habari za mashujaa 30 wa Daudi (1 Mambo ya Nyakati 11). Pia soma kuhusu mashujaa wa matengenezo kama Luther, Zwingli, Tyndale, Knox, na Huss. Je, aweza kukubali kukosolewa na ajifunze? Je, ana ujasiri wa kujua amefanya dhambi akatubu na kuiacha? Je, anaweza kusema amekosa na kuungama? Je, anaogopa watu zaidi ya Mungu?

Mwanamume ni kichwa cha familia, kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa, angalia tabia za wanaume kama Nuhu, Ayubu, Ibrahimu, Musa, Daudi. Ibrahimu shujaa alisifiwa, 'Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA wafanye haki na hukumu.' Mtoto wa kiume yapaswa ajue mafundisho makuu ya imani kwa uhakika na kutofautisha mafundisho ya uongo-doctrines. Maana atakuwa kuhani wa mji wake, na hata nyumba ya ibada. Awahoji wachungaji na viongozi wa kiroho vile wanavyoamini. Je, injili ni nini? Inawaathirije maisha yao? Kumbukumbu 6:7,8 wafundishwe watoto na wakariri. Wazazi wasaidie watoto wa kiume kuwa walimu.

Kujifunza uongozi ni muhimu. 1 wafalme 3:9; 'Nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako, na kuwapambanua mema na mabaya, maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi?' Hapa Sulemani aliomba hekima na uongozi. Twatoa mifano kwa wana wetu kuwa mahakimu wa haki. Tunapowaadabisha, tunainua sheria ya Mungu, na kuwasaidia katika mausia ya Bwana. Twafundisha kuzungumza na marafiki zao wanapowakosea, ili kuweza kurudisha uhusiano mwema, kusudi waweze kuwasaidia watoto wao wanapofanya makosa ya sheria ya Mungu. Hakikisha adhabu zako kwa mtoto zinalingana na upendo wako, endapo adhabu zako zinazidi upendo kuna walakini. Twasema vile tukijua wote ni binadamu tunakosea, na kila mtu ana mizoga fulani katika shuguli ya kulea, ila adhabu iwe ya upendo, kumrudi mtoto, na si hasira. Usimpe mtoto adhabu ukiwa na hasira, ngoja ipoe, kisha uzungumze naye, na kisha umpe adhabu.

Je, mtoto aweza kuwaongoza wengine kwa unyenyekevu na kugawa kazi, hata kuzisahahisha na kutathmini? Angalia “Brother Offender Checklist” na “21 Rules of This House” kwenye website ya maneno hayo. Muwe na koti nyumbani, ili muamue lipi lahitaji adhabu na lipi lahitaji maonyo. Angalia kwenye maandiko adhabu za manabii, za watu na za mitume. Orodhesha dhambi ambayo mtoto anapambana nayo, panga adhabu, na matokeo ya kukataa maonyo. Je! mamlaka yana majukumu gani, tunapaswa tutendeeje mamlaka. Je! mwana wako anakubali kufundisha wengine, kama darasa la watoto au vijana wenzake kanisani?

Mtoto wa kiume afundishwe kutokuwa na tamaa ya vitu vya mtu, na kushukuru kwa alivyo navyo, maana tamaa. Utauwa na kuridhika ni baraka kubwa, kwani tulikuja duniani bila kitu na tutaondoka bila kitu. Pale anapokosea afundishwe kuomba msamaha. Kwa vile atakuwa kiongozi afundishwe kutumia mamlaka na majukumu kwa hekima. Mfano wa waliotumia madaraka vibaya ni mafarisayo, na waliotumia madaraka vizuri ni

Nuhu, Ayubu Eliya, n.k. Ajue kwamba madaraka ni kuwa mhudumu au mtumishi wa watu na wala si dikteta wa kunyanyasa watu. Ajue kufanya kazi kwa mikono yake ili aweze kukidhi mahitaji yake na ya wengine. Apaswa kuanza kufunga na kuomba akifika miaka kumi na miwili hivi, maana mengi hayawezekani pasipo maombi na kufunga. Ajue kwamba mke na watoto wake watahitaji nguo, chakula na makazi na hivi ni sababu tosha ya yeye kujifunza kusali na kufunga.

Ukengeufu au upotofu waanza pole pole, kama vile kipima joto kinavyoongezeka; hivyo agundue kwamba baada ya muda atajikuta mbali. Ajifunze kutoka kwa wanaume wenye hekima na wenye tabia njema, maana wanaume hawa wamepitia maisha ya ushindi na maanguko, ili asikanyage pabaya, na kudidimia. Majaribu yanaonekana mazuri, ila hayasemi ukweli wote, asijaribu kupambana na majaribu bali amwuulize Mungu kutii na kuepuka mialiko ya kufanya uovu, kwani pambano ni la Mungu unapochagua, kutii sheria yake.

Kwa nini ni vizuri kijana asijihusishe na nyimbo nyingi kama za Rock muziki na za dansi? Kwa sababu zina uovu, watu wengi wanaoimba wanapendelea uasi wa sheria za Mungu, na kujiingiza kwenye dini za kuabudu miungu mingine zaidi ya Mungu wa Ibrahimu, wanajishughulisha na vileo au madawa ya kulewa, wanafundisha mambo ya giza bila kujua na pia wanafanya mambo ya kiroho yapungue, wakiongeza wasiwasi na kutotulia kwa moyo.

Elimu ni nzuri ila, anza kusoma vitabu mapema, kabla mambo hayajaribika. Mweleze kijana pia. Yaani asisome kitabu cha kuwa na ndoa nzuri baada ya kuachana na mke, ila kabla. Kuelimika na kusoma ni vitu viwili tofauti, unaweza kusomea shahada kubwa ila usielimike. Na pia kupata pesa na kufanya kazi ni vitu tofauti. Neno la Mungu limehakikishwa kwa kila hali ili lisaidie kwa mafundisho, kuonya makosa, kuongoza, kuadabisha kwa haki, ili mtu awe kamili na apate kutenda kila tendo jema.

Mtoto ajifunze kutii utawala, maana hata yeye siku moja aweza kuwa kwenye shuguli ya uongozi. Huwezi kuongoza watu kama wewe hujui kuwa mfuasi. Tunaambiwa katika Maandiko matakatifu kwamba tuwaheshimu na kuwatii wanaotuongoza, ili kazi yao isiwe ngumu au ya huzuni, maana watatoa hesabu kwa yale wanayofanya. Angalia tu shuguli ambazo serikali ya kawaida inasaidia raia. Tunaelewa kwamba tuna viongozi waovu, ila kwa kawaida viongozi ni msaada mkubwa na hatuwezi kamwe kuishi bila viongozi. Endapo wazazi tunafanya kazi ya viongozi kuwa ngumu au tunawadharau, watoto wataiga.

Kusamehe ni muhimu kwa mtoto wa kiume, na kutosamehe ni kama kunywa sumu na kutegemea mwingine afe. Na pia tukumbuke hata sisi tumewakosea wengine na wanatusamehe. Wapaswa kuwa huru kwa aliyekukosea na si mtumwa wake. Hata hivyo tunasamehewa tunavyosamehe.

Mwana ajifunze kusamehe, na kumwambia Mungu uchungu alio nao, na kumwomba aondoe uchungu huu, asiseme uongo bali kweli ya moyoni kwa Mungu, kwani BWANA anao uwezo wa kutoa uchungu na chuki yote, na atashangaa moyo wake utakuwa mwepesi. Mke, watoto na hata wazazi wanaweza kumkosea. Ila twapasa kujua jinsi ya kutatua haya matatizo, kwani tumeambiwa kwamba ni vyombo dhaifu, hivyo twahitaji hekima ya kuenenda nao. Ajifunze kumwachia Mwenyezi Mungu shida yake hiyo, na ikirudi mawazoni amwachie tena, mpaka itoke kabisa.

Kuweka visasi na chuki ni kitu cha kuangamiza kabisa, Je, tunawezaje kutoa mawazo machafu? Mawazo machafu yanakuja kwa kila binadamu Je, tunayaondoaje?

Wengi wanakosa kujikana nafsi na kuzungumza lolote, kuwaza au kutenda chochote. Je, ana hasira anayoshindwa kuikabili? Au mawazo mabaya? Zaburi 119:110 yasema, tuweke neno lake mioyoni mwetu ili tuondoe mawazo machafu, kisha kama Yoshua, tuchague nani tutamtumikia kila siku. Tuchague kumtumikia Mwenyezi naye atatuondolea mawazo machafu. Mawazo yetu lazima 'Tuyaangushe na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mwenyezi Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii BWANA;' 2Kor 10:5. na hatimaye, mwishowe tufikirie yote mazuri, ya ripoti njema na ya staha.

Udadisi wa mtoto uweze kukuzwa ili aweze kubuni na kuvumbua mambo. Mpe mtoto vifaa na muda, usiwe unajali sana kwamba ataharibu vitu, au anapoteza muda. Watu waliovumbua duniani walihitaji muda, watu kuwaamini na kutokuwa na presha au misukumo mingi. Ili mtoto aweze kuvumbua anahitaji maarifa katika masomo tofauti. Mungu ndiye mvumbuzi mkubwa, usipoteze muda wako kuvumbua uovu utakaongamiza watu kama wale waliovumbua mabomu ya nuklia!

Kitu kikubwa katika uvumbuzi ni kutokata tamaa. Thomas Edison alifanya majaribio 1,000 yaliyoshindwa ila alivumbua taa na mengineyo. Aligundua njia 1,000 za kutofanya majaribio kwa njia hizo (1,000 ways not to go). Usikate tamaa ushindwapo, jifunze kutokana na makosa na usonge mbele, utapata majibu.

Mtoto wa kiume ameumbwa avumbue nyimbo, program, vitu, mbinu, sanaa, vitabu, zana, na mengineyo. Hebu uwe mvumbuzi kama Mungu alivyokupangia, kuhudumia dunia, na kuishi maisha yenye maana. Ila usisahau afya ya mwili wako kwa kufanya mazoezi ili usiwe lege lege ukikaa kwenye maabara siku nzima bila kuona jua, na kupata hewa bora!

Mtoto wa kiume, ajifunze kuvumilia, na ajifunze kutunza urafiki. Asiwe mtu wa kukasirika ovyo ovyo na kushindwa kukarabati urafiki. Mara nyingi kama binadamu tunashindwa mengi, ila ujasiri na kujaribu tena na tena ni muhimu. Tunaona hata Mungu hatuachi tunaposhindwa na bado anakarabati maanguko yetu yaliyotokea kwenye bustani ya Edeni, Mwanzo 3.

Je, napaswa niwe wapi (belong)? Mara nyingine unaweza kuona kwamba haufai kuwa mahali fulani. Kwa kweli mbinguni ndiko kwetu sisi wote, huko ndiko tutapoona ni maskani yetu kamili. Usipoteze muda mwingi kuona kama unafit hapa, maana Mwenyezi ameenda kututayarishia makao, na hivyo mara nyingi tutajisikia tu wageni hapa, ila tuweke nia na shabaha yetu kwenye ile nchi ya Paradiso. Afadhali kuishi kama mgeni hapa ukijitayarisha kwenda mbinguni, kuliko ujisikie mwenyeji na mwishowe ulie na kusaga meno. Tutakapolenga mbingu, hata ya dunia itakuwa rahisi kuyakabili, ila tukilenga dunia tu, tutakosa mengi.

Kutenda haki ni muhimu la sivyo mvulana anakuwa mtumwa wa tamaa zake na kutojikana nafsi. Kutendea watu wote haki ni muhimu, na pia kuwiwa na upendo na watu. Twaona mfalme Sulemani alihukumu kwa haki, ila alipoanza kutojikana nafsi, kwa kuchukua wake wengi, alipoteza haki za watu, na kuharibu mahusiano na Mungu. Mara zingine vijana wa kiume wanafikiri haya hayawezi kuwapata wao. Wanasema tukifikiria kwamba haya hayawezi kutupata, basi tu wenye hekima kuzidi Sulemani, wenye nguvu kupita Samsoni, na tunampenda Mungu kuliko Daudi.

Maisha ni kufanya kazi, kusoma, kujenga, kuwekeza, usiwe mvivu na kukaa tu. Usikae kivivu kijiweni (jobless corner) mpaka nguo kuchanika kwenye makalio, huo si mpango wa Mungu kwa mvulana. Msichana aweza kuolewa na mtu mwenye uwezo, wewe mvulana ndiyo mtafutaji. Ni aibu kunyemelea msichana tajiri eti maisha yako yawe rahisi. Kama ni mipango ya Mungu itokee vile, basi nawe ujishughulishe na kuwa mtafutaji

ili usidharauliwe na mke au wakwe zako. Kama unataka kuwa injinia, lazima usomee hesabu na sayansi kuanzia leo. Kama unataka kuwa kuhani, anza kupanga mikakati. Mungu ametuumba kuwa watendaji na si watazamaji.

Jifunze kusoma Neno la Mungu, ukiamka tu, goli si kwamba umesoma kurasa ngapi, bali mahusiano yako na Mungu. Mungu anataka kuzungumza yale ya muhimu kwako (concerns), anataka ajue ndoto zako. Mungu ana nguvu tosha za kumwamsha mwanamume au mvulana mnyonge atoke kwenye kitanda na kusoma Neno lake, mwombe akusaidie uamke na kusoma. Mwumbaji ataka awe karibu nawe, hebu mruhusu.

Mara nyingi katika maisha watu watashindwa kutuelewa. Kutoeleweka kwingine (misunderstood), kama umesingiziwa, jifunze kukaba ulimi wako na kusema kweli tu mpaka yale uliyosingiziwa yapite. Ila kusingiziwa ni nafasi ya Mungu kutufundisha uvumilivu, unyenyekevu na kusamehe watu. Hata Bwana alisingiziwa na kusemewa uongo. Badala ya kukasirika na kushangaa, poa na umwombe BWANA nguvu. Uwe na amani moyoni, kwamba Mungu anaelewa, na kujua nia yako ya ndani. Kutenda mema ni silaha. Mwenyezi anatumia kupiga yale ambayo watu wanayotusingizia au kukupachika.

Mara nyingine hutaelewa na utachoka kusingiziwa na kueleweka visivyo, ila kumbuka tuko katika pambano kuu kati ya wema na ubaya. Shetani amemsingizia Mungu kwamba si wa haki, na wengine wameamini; ila siku moja karibuni, tabia ya Mungu itafutwa madoa machafu.

Jitahidi usiwe na nia (attitude) ya kufanya kazi ili ucheze. Wanaume wengi wanaona kwamba kazi ni njia ya kupata pesa ya kununua vitu vya kujifurahisha wachezee siku wasizo kazini. Wanaume wana michezo (adult toys) ghali kama vile magari ghali, pikipiki ghali, boti na vingineyo. Kumbuka kwamba kufanya kazi ili kutafuta riziki ni muhimu; ila kuna kazi nyingine pia za kusaidia watu kama wajane, maskini, yatima. Hii pia ni muhimu, kuleta kupona kwa wengine. Tumia karama na ustadi wako kufanya dunia iwe mahali bora.

Ili upate mahitaji kwa hali bora, wazazi wako wanafanya kazi. Mwana mwema hatataka kuchukua kazi au mali ya wazazi wake na kutumia kwa anasa zake. Unaporithi mali, uwe mwangalifu ili usaidie wengine wa kizazi kinachofuata. Tumeokolewa kwa neema na si kwa matendo yetu, hivyo tufikirie wengine/kizazi kingine.

Je, mwana anaogopa giza, mbwa, milima mirefu, au buibui? Kuondoa woga ni sehemu ya kukua na kuwa mwanamume. Inawezekana usiondoe woga wote, bali utanawiri na kushinda mazingira yako, japokuwa una woga fulani.

Musa alikuwa na woga huo, Kutoka 3-4. Yoshua aliambiwa, 'Uwe hodari na moyo wa ushujaa, usiogope wala usifadhaike, kwa kuwa BWANA, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendapo.' Mtu anashinda woga wake kwa kujua kwamba Mwenyezi yupo, na kwamba ana uwezo. Mwenyezi anajua unachohitaji, na atakupa ujasiri na kujiamini bali si kiburi. Ushindi unakuwa na utamu endapo umeushughulikia, 'Nawaandikia nyinyi vijana kwa vile mna nguvu na mmeshinda mwovu.'

Kila mwanamume anapata woga wakati fulani, hauwezi kushinda endapo hauna maadui wa kupigana nao. Kila mwanamume ana changamoto. Cha muhimu ni kushinda mapambano madogo unayokuwa nayo ya kila siku, mapambano yaliyo ndani ya moyo wako. Kuna siku hutataka kufanya kazi, bali itabidi ufanye. Ushindi unapatikana, hasa unapochukulia hasira, ulafi, tamaa za moyo wako kama maadui zako.

Asilimia 90% ya woga tulio nao ni vitu ambavyo havitatokea. Iliyobaki 10%, utapambana nayo, na unaweza ukashindwa machache, ila ukiendelea kupambana kwa nguvu, utashinda.

Uchoyo uwe mwiko, na kama una shida hiyo, si lazima uwe hivyo maisha yako yote. Mvulana atakuwa kiongozi wa nyumba yake na hata taifa, na kupanga mipango ya kusaidia watu, endapo ni mchoyo au anayejifikiria mwenyewe, ataumiza wengi. Wengi wanaosaidia mahitaji ya watu ya taifa kwenye ustawi wa jamii ni wanaume, hivyo mvulana ajifunze kuukana uchoyo au ubinafsi.

Kina mama wanatoa kwa ukarimu chakula au vitu vichache vya nyumbani, ila wanaume wanashughulikia mipango mikubwa ya kusaidia jamii na hata nchi nzima, na wakati mwingine kukiwa na matukio ya majanga au maafa wanaokoa wengi. Twapaswa kufundisha vijana wetu kutokuwa na 'umimi.'

Kijana aombe na kuwa mwazi 'Mwenyezi Mungu, mimi nina uchoyo, najifikiria kuliko mtu mwingine. Najua hupendi niwe hivi, naomba unifungue macho yangu, nione mahitaji ya wengine ili niweze kuwa msaada. Naomba niwe na tabia kama yako.'

Piga picha baba yako anavyosikia akija nyumbani, je waweza kumsaidia kufanya jambo fulani, na mama yako waweza kumpunguzia uchovu wake? Ukimtembelea mtu angalia yale unayoweza kusaidia, badala ya kukaa kwenye kona utazamwe. Tumia muda wako kwa huduma ni msaada kwako kuondoa woga na uchoyo wa kujifikiria mwenyewe. Usiwe na haya au aibu, maumivu, au huzuni zako; anza kusaidia wengine.

Kila kiongozi mwenye njozi lazima afikirie kuhudumia watu. Watu wachoyo wanakosa ujasiri. Watu jasiri hawangoji nafasi kubwa za kuwa mashujaa au kuokoa watu, bali nafasi ndogo ndogo zinazojitokeza kila siku. Hizo zakupa nafasi ya kuwa jasiri au mwoga.

Jifunze kupenda vitu vya aina fulani. Wavulana wengi wanalalamika; 'Sipendi mvua, sipendi kazi niliyopewa, sipendi jua kali, sipendi kuishi mji huu, sipendi hichi kijiji, sipendi, sipendi sipendi!'. Kama unataka kufurahia ukuu na mema wa Mungu, jifunze kuyapenda yale aliyokuwekea wazi kuyapenda. Una uchaguzi, wa kulalamika na kunung'unika kwa kunyatisha sura, au kuvipenda vile ulivyopewa. Ila huna haja ya kuweka sura mbaya siku nzima.

Mwanamume mmoja alisema utotoni alikuwa hapendi nyanya, ila alipooa, mke wake alimpikia na nyanya. Naye akasema 'Nyanya hizi zinafanya nini kwenye chakula changu?' Lakini mke wake hakubadilisha kitu; akaanza kuzipenda na hata leo anapenda nyanya na anazimiss zisipokuwepo. Lakini twasema usipende uovu au vitu visivyo na afya, ila kuna vitu vingi waweza kujifunza kuchukuliana navyo na ukakuta unavipenda.

Wengi wamependa uyoga, au parachichi (ovacado), japo walishindwa kula vyakula hivi, walipokuwa wadogo kwa kubadilisha nia zao (attitudes). Kukomaa, na kukua ni kupenda mambo mengi yale machungu na matamu pia. Usijikaze tu 'kula nyanya' ila jifunze kuzipenda. Mungu ana mema mengi katika milki yake, tusiishi tukiepusha pua zetu kwamba 'sipendi ladha yake.' kwa vile Mungu alituruhusu tule.

Ili kuwa mwanamume kila mvulana ajifunze kuchukuliana na maumivu. Ni sehemu ya maisha ya kupata hekima, nguvu na ustadi. Mtoto asiyejikana nafsi, anapiga mayowe kwa maumivu madogo; anafikiri furaha yake zaidi ya majukumu yake. Badala ya kufanya kazi shambani anafikiria jinsi jua lilivyo kali, au kuchoka kwake. Badala ya kumpisha kiti mama mzee, anafikiria raha au burudani yake. Akijikwaruza mkono kidogo, anakataa kuosha vyombo. Maisha yana maumivu mengi zaidi ya mikwaruzo midogo. Uumbaji wote unalalamika na maumivu ya aina fulani yawe ya kiroho, kimwili au kiakili. Hata wengi wana maumivu kwa mtu kusema maneno yasiyo ya upole, siyo tu kwamba wewe ndiye unayelengwa! Hivyo usijionee huruma ukiumia, kwa sababu kila kiumbe kinapata maumivu.

Mwanamume apaswa kujua jinsi ya kuchukuliana na maumivu, hawezi kujificha. Bila maumivu mara nyingine hakuna matunda au maendeleo.

Maumivu ni ya wote, na mara nyingi ni ya muda mfupi. Ila mbinguni hakuna maumivu, yale yanayotuumiza leo, yaweza kuisha kesho, hivyo usikite kwenye maumivu yako. Maumivu pia yana mwisho wake, ingawa kuna wakati tunaona tunashindwa kustahimili. Maumivu hayako huru kutufanyia yatakavyo kwani Mwenyezi anamiliki na kujua mwisho wa uvumilivu wetu, hivyo anatupa tu yale tunayoweza kuyastahimili. Mungu anajua kila urefu na uzito wa kila umivu, na ametoa ruhusa lije kwetu; 1Wak 10:13. Kama kisa cha Ayubu kinavyosema, hakuruhusu Ayubu kufikia anaposhindwa kustahimili. Maumivu yana uzuri fulani, Mungu hawezi kutupa bila sababu.

Mtu wa karibu nasi, anapotuumiza mioyo yetu kwa kutotuelewa au kwa mategemeo yetu kutotimizwa inatuumiza zaidi ya kawaida. Daudi alisema 'Kwa maana aliyetukana si wa mbali; kama ndivyo, ningevumilia. Aliyejitukuza juu yangu siye anichukiaye; kama ndivyo, angejificha asinione. Bali ni wewe, mtu mwenzangu, rafiki yangu niliyejuana nawe sana. Tulipeana shauri tamu; na kutembea nyumbani mwa Mungu pamoja na mkutano.'

Jinsi unavyojibu watu wanaokuudhi na kukwambia maneno ya kukuumiza, inaonyesha kama unakomaa kuwa mtu wa Mungu au unajifikiria wewe na maumivu yako tu. Mlilie Mungu ili akuliwaze, na usipige mayowe kwa muda mrefu kwa maumivu madogo, au kukasirika kama mambo hayakuendei unavyotaka.

Watu wengi wanapenda kuepuka maumivu ila wachache kati ya hawa wanafaa kwa ufalme wa Mungu. Ukiwa na maumivu au vidonda vya mwili, nenda hospitali ukashonwe, au kurudishwa mfupa sawa, ila usionyeshe kidonda chako kwa kila mtu.

Mwanamume lazima awe shujaa, asiyetaka huruma (pity) toka kwa kila mtu. Badala ya kuangalia kidonda chako kila wakati, angalia watu wa kuhudumia, ila utoe mawazo yako kutoka kwako na maumivu yako. Kwa maumivu ya moyo, usiwe kama mbwa anayelamba vidonda vyake siku nzima, ila 'ushinde wema kwa ubaya.' Hata Bwana 'Kwa ajili ya furaha iliyowekewa mbele yake, aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.'

Kuna wakati wa kutoa machozi, na kucheka. Siamini msemo kwamba 'mwanamume halii,' kwani hata Bwana Alilia; ila hakulia kwa huzuni zake ila za watu wengine. Kulia kunapunguza maumivu ya moyo. Hivyo kuna wakati wa kujikaza, na kuna wakati wa kulia, na hiyo Bwana atawawezesha wana kutofautisha, ili wasiwe watu wa kulia lia ovyo, au kutolia na kupata shida za hisia.

Unawezaje kujitayarisha kuishi na mke vizuri sasa? Waweza kufikiri u mdogo bado, kufikiri hili na ukacheka, na ni kweli si wakati wa kuoa, ila waweza kujitayarisha wakati huu. Waweza kujitayarisha kimawazo sasa, ili baadaye uwe mwanamume wa furaha na kuwa na ndoa ya furaha. Siyo kwamba unaharakisha kuoa, ila ni bora uwe tayari hata kama hautaoa au ukipata wito wa kuwa towashi. Jifunze kazi ambazo wanaume wanasaidia dada zao, au mama zao; kama vile kubadilisha tairi, kukarabati nyumba, kuzibua choo, kuweka mbolea, kufuga nyuki, kuchunga mifugo, kutoa visiki, kutumia nyundo na bisi bisi, kutengeneza zizi, kuchagua mbegu za kupanda, kuua panya au kupunguza matawi ya miti ya matunda.

Jinsi unavyowahudumia dada zako na mama yako sasa ndiyo darasa kubwa la ndoa. Wadogo zako wafurahi wana kaka mkubwa, wakupende, nawe uwapende pia. Jinsi ya kujenga mahusiano bora na dada au mama yako ndiyo jinsi ya kujenga mahusiano bora na mke wako pia. Usiwe jeuri, hata dada zako wakakuogopa na kutokwambia yaliyo

moyoni mwao. Uwe na upole, ili wakuamini, na wakikuambia shida zao, chukua hiyo changamoto ya kuwatatulia bila kutangaza tangaza au kujisifu.

Je, wanapenda nini, au hawapendi nini? Je, unajua njozi zao na woga au mashaka waliyonayo? Je wana mategemeo au matumaini gani ya leo au kesho? Ukiwa jeuri na mkatili, watakuficha. Kama dada yako alitaka kupata chombo cha muziki ajifunze, chukua changamoto hii na kumsaidia akipate.

Dada yako ndiyo darasa la kukufundisha jinsi ya kutafuta riziki ya familia yako siku za mbele.

Ujasiri wa Daudi kumshinda Goliathi, haukuja siku hiyo hiyo; bali alianza kumpiga simba na dubu kwanza, ndipo akatoa woga na kuliendea jitu la kifilisti. Wahudumie madada na mama zako. Usiwe unawakejeli, kuwadhililisha, au kushindana nao kwamba wewe ndiye kijana au mwenye nguvu. Uwe timu moja nao, ikiwa chakula acha wao wapate sehemu kubwa nawe uchukue ndogo. Wape nafasi nzuri ya kukaa.

Je, umefikiria kuwaambia dada zako au nduguzo wadogo msome pamoja nao neno la Mungu? Je, unaomba nao? Wasifu wakifanya mema, na wakifanya mabaya wasamehe, wasaidie wafanye vyema na kufunika makosa yao. Una nafasi ya kuwafanya wawe warembo nje na ndani ya moyo pia. Siku moja watasema, 'Kaka yangu alinipa nafasi ya kufikia njozi zangu, nampenda na kumheshimu.'

Mdogo, dada au mama yako akiwa wa kujifikiria na mchoyo msaidie. Mwombe Mungu akusaidie, na kazi yako itakuwa ni kurudisha mahusiano mema. Nawe pia uwe mfano kwa wadogo zako, dada na mama. Bwana amefanya mamilioni wasiompenda wampende, nawe fanya vile. Mvulana aliyekomaa haangalii nani anampenda na nani hampendi, bali anaangalia kufanya vyema bila kujali watu wanavyomtendea. Usifikirie wadogo zako, dada au mama hawataki uwasaidie na kuwapenda. Mara nyingi watabadilika. Wasichana wana kigeugeu wakati mwingine; ila wewe tafuta njia za kuwapendeza dada zako, mwulize hata mama yako, atakusaidia. Ni kazi ya mvulana na mwanamume kuwapendeza dada zake na hatimaye, mke wake.

Unapochagua mke, mpe Mungu nafasi ya kukuchagulia, omba na ungoje wakati atakaokuchagulia. Mtu anachagua anayoona nje, ila BWANA anajua moyo. Angalia kama anapenda mambo ya kiroho. Epuka michezo rafu unayocheza na wanaume. Iwe mwiko kudansi na wasichana, maana inaamsha tamaa mbovu. Mashule mengi ya bweni yanaweka dansi na yamewaingiza vijana kwenye tamaa na dhambi. Kila siku tuna mapambano vichwani mwetu, na falme ya shetani. Vaa mavazi ya vita ya waefeso 6, usijianike kwenye majaribu.

Dansi ni chombo cha shetani mwenyewe. Mwulize mwanamume yoyote kama atakubali mtu acheze dansi na mke wake wakikumbatiana, atakwambia la! Zama zile za ukoloni, watu walikatazwa kucheza ngoma za kienyeji eti ni za kishenzi, cha ajabu ni kwamba ngoma hizi watu walicheza mbali na mwingine, mwanaume na msichana hawakuwa karibu. Siku hizi dhambi zafanyika kwa wazi, za kukumbatia msichana asiye mke kwa karibu.

Wengi wanafundishwa mambo ya kuvaa kondomu, ila kwa mtu anayemweheshimu Mungu. Ngono ni ya ndani ya ndoa tu, nje ya hapo ni dhambi au uasi wa sheria za Mungu . Hata hivyo kondomu haifuti dhambi, haindoi dhamira kushitaki, haizuii mimba au ukimwi kikamilifu au kutoa huzuni.

Mtoto wa kiume daima ajue kwamba ni Mungu pekee ndiye msaada wa kuepuka dhambi za ngono. Wanaume wengi hasa katika ulimwengu wa leo wa ponografia (umalaya wa picha) wameangushwa au kuingia dhambini kwa mambo matatu yaani wanawake, pesa

na kiburi cha mamlaka (power). Kama mvulana au mwanamume anajiona yeye hawezi kuanguka mtego huo, basi lazima atakuwa na nguvu kumpita Samsoni, Hekima za kumpita Sulemani na kumpenda Mungu hata kumpita Daudi.

'Apataye mke apata kitu chema na kupata ijara toka kwa BWANA.' Mvulana atofautishe kati ya mwanamke mgeni wa Mithali 7; yaani malaya na mwanamke bora wa Mithali 31. Je, ana tabia kamili za msichana bora? Je, anajua tendo la ndoa katika Neno la Mungu lina sehemu gani? Mfundishe mabadiliko ya mwili kama vile kubalehe, na endelea kuzungumza naye katika kila hatua.

Wazazi wengi wazungumza na watoto wakiwa na miaka kumi na mitatu na kuachia pale; kisha wanashtuka mambo yakiharibika wakiwa na miaka kumi na saba! Kumbe walitoa somo moja tu la ngono na kuacha! Majaribu ya ngono yanafikia wengi na punyeto; mtoto afundishwe kuepuka haya kila mara. Watenge watoto wako wasilale na watu wengine, na mambo ya sherehe za usiku (pajama party au sleep over) yawe mwiko.

Mvulana kujiweka safi kwa maneno, mawazo na mwili mpaka aoe. Je, ana mpango wa kumwendea baba wa msichana kabla ya kufungua ndoa na si kukaa pamoja bila mipango ya ndoa? (come we stay). Je, yupo tayari kukwambia anapotaka kuoa? Je, yupo tayari kukaa msela endapo Mungu amemwita kuwa towashi, na kutoishi maisha ya ndumila kuwili?

Biblia si kitabu cha ushauri bora au maoni bora tu, bali mawazo ya Mungu mwenyewe, yenye mamlaka ya mwisho mbinguni na duniani. Neno la Bwana latueleza jinsi ya kuchukuliana na kumpendeza kila mtu unayekutana naye, awe rafiki, dada, kaka, wazazi, mwajiri, wasichana, wazee , maadui au watoto. Inawapa watu tahadhari na mitego, inakueleza jinsi ya kufanya kazi, kuwekeza pesa, jinsi ya kula, cha kula, na hata wakati wa kulala. Ina kanuni za kila nyanja ya maisha yako. Inatupa kina cha kujua Mungu anavyofanya kazi na kusikia sauti yake. Inafanya tujue maisha, mambo ya asili na hata ya sayari nyingine. Inatueleza kuanzia Mwanzo mpaka ufunuo jinsi ya kumpokea BWANA aliyejitoa kwa ajili yetu kwa kutupa uzima wa milele.

Wewe siyo mnyama kama elimu ya uibukaji inavyopoteza, umeumbwa kwa makusudi maalumu. Kila mvulana ajiulize yupo hapa kwa ajili gani, ametoka wapi, na nini kitatokea akifa. Neno la Mungu laeleza kwa nini kuna maumivu haya yote. Hakuna kitabu chochote kitakueleza yote haya. Saa moja kwenye kitabu kingine kamwe haitalingana na saa moja kwenye Neno lake.

Hakuna kitabu cha kusisimua kama hiki, na kinachobadilisha maisha ya mtu. Hesabu au kemia haiwezi kubadilisha maisha yako kama kitabu hiki. Ila Biblia si kitabu cha kupata habari bali kubadilisha maisha (not for information but transformation). Ukifuata ushauri wako, mambo yatakuwa halisi na utabadilishwa. Usipoteze muda kusoma hadithi za nadharia (novel) au fictions ambazo zinafanya usipende kusoma Neno la Mungu. Hadithi za kufikirika zafanya Biblia isiwe na ladha.

Akili zako zitapanuka, ukisoma Neno hili na hata utakuwa na uwezo mkubwa darasani. Soma na elezea marafiki, ulichopata kwenye sura hiyo. Wakati mwingine unyamaze kwa utulivu na kuangalia Utukufu wake. Kariri mafungu yake mengi, imba nyimbo. Marko 1:35 inasema, 'Alitoka kwa faragha aende kusali;' nawe, amka na ukasali.

Sikiliza mausia ya wazee, hautakuwa kama rika lako bali utakuwa na hekima ya kupita umri wako. Mashauri haya ya wazee yanaweza kuonekana yamepitwa na wakati, ila utakuwa unatafuna mambo na kucheua kwa hekima ambayo watoto wa umri wako hawana. Twaona Sulemani alipokufa kijana wake Rehoboamu aliomba ushauri kwa vijana wakampotosha, naye akapoteza ufalme wake.

Wazee wenye hekima hawazungumzi mawazo yao kwa haraka, wanapima mambo kwanza. Wanajua maisha ya mvulana au mtoto yatakuwaje, hata kama hawakwenda shule; kwani miaka ya uzoefu waliyonayo inawasaidia. Wengi wamepinga ushauri wao, na hii imewafanya wanyamaze, wakiogopa kujichumia uadui na vijana. Hivyo ni jukumu la wavulana na vijana kukaa na wazee na kuwauliza maswali ya taaluma nzuri ya kusomea au ustadi gani ni wa muhimu kupata, au uwekezaji gani bora, n.k.

Mpepeleze mzee kwa maswali kama haya: Je, mtu afanye yapi kuwa na mahusiano mazuri? Je, mambo gani yanaharibu mahusiano? Je, jamii imebadilika kwa namna gani leo? Je, imebadilika kwa mazuri au mabaya gani? Ni makosa yapi uliyoyafanya mambo yakaharibika? Ni sehemu gani ya maisha yako mambo yalikuendea vizuri sana? Nini waweza kunielemisha kuhusu ndoa na kuwa na watoto? Ukiwa mwajiri, ni mtu gani utamchukua kwenye kampuni yako? Ukiwa mdogo wakumbuka ushauri aliokupa baba yako? Je, uliufuata? Je, ni nini kilicho muhimu sasa kwenye maisha yako? Je, upo tayari kufa wakati wowote? Kama ndiyo! kwanini? Kama la! Kwanini?

Kuna wakati wa kuua na wakati wa kuponya (Mhubiri 3), na hiyo ni changamoto ya kukua au kuwa mwanamume. Watu wengi wanachanganyikiwa na kuua wakati wasipopaswa na kutoua wanapopaswa. Je, mvulana atajuaje? Mwanamume au mvulana si mnyama mwingine kwenye himaya ya Mungu. Alipewa mamlaka na milki. Anapaswa kuheshimu viumbe na kuwa wakili bora, si kuua viumbe au kukata miti bila sababu, eti alimradi iko kwenye milki yake. Anapaswa kuvitumia hivi vitu kwa mahitaji yake, ila si kwa ufujaji, akikata miti apande miti. Asiwe mkatili, ajue kuhifadhi, pia ni kitu gani atakachokihifadhi. Mfano, panya wako katika nyumba wanakula mahindi yako, Je, uwaue? Siafu walio porini uwaue? Je, paka anayekatisha barabara umuue? Ukiwa unaishi karibu na mbuga ya wanyama na una njaa, je, uue swala bila kibali? Usipuuzie kazi ambayo Mungu alikupatia, ya kuhifadhi na kujali viumbe. Hata wanyama wanajua ni nani anamcha Mwenyezi Mungu kutokana na huruma na utunzaji wanyama anaofanya huyo mtu. Je, mifugo yako inapewa malisho au chakula na kushiba? Au unafuga mbwa bila kumpa chakula mpaka mbavu zake zinaonekana? Kumbuka Nuhu aliambiwa aweke wanyama kwenye safina, Mungu aliweza kuwaumba wengine, ila aliwapenda wale wanyama. Biblia yasema Mungu akamkumbuka Nuhu na wanyama.

Ili mtu akidhi mahitaji ya familia yake kiriziki anahitaji kuua mara nyingine, ila asiue viumbe vya Mungu kwa ajili ya hasira au futuhi bali kwa riziki au ulinzi. Wakati vita vimetokea, tunajua wazi kwamba watu wengi wanaompenda Mwenyezi Mungu wamepigana vita vya kuleta uhuru na kulinda nchi zetu au jumuiya. Wengine kutokana na dhamira na sehemu Mungu amewapa kufanya, wamekataa kuua kwenye vita na kushughulikia majeruhi wa vita na hiyo ni sawa kutokana na mtu na kuelewa mambo fulani. Ila wanaume wote lazima wajue jinsi ya kulinda familia zao na kujua kuleta riziki.

Mwanadamu ana jukumu la kutunza hifadhi za karibu na kwake na kutokuwa mharibifu. Wavulana wengine wamepiga ndege kwa manati na kucheka tu bila sababu yoyote ya maana. Mwanamume anahitaji kutunza vile Mungu amemkabidhi, yakiwemo mazingira. Tunaishi wakati ambao watu wanaua hata watoto wao wenyewe kwa kutoa mimba au njia zingine. Watu wako tayari kuua watoto wao ila wanaogopa kuua mende kwenye makabati yao. Lazima tujue thamani ya binadamu, na wakati huo huo kuwa na ujasiri wa kuua vitu kama mende au panya.

Ibada ya nyumban ni muhimu. Usikunje ndita wakati wa maombi au ibada. Waisraeli walichukua muda mwingi wa ibada, na kutoa kafara, ila walikuwa na kujifikiria na

uchoyo. Kila siku ni siku ya ibada, pia kwa jinsi tunavyoishi tunaabudu. Maana twaweza kuwa waimbaji wazuri ila maisha yetu yana harufu mbaya. Twahitaji mioyo yetu kubadilika, ili tusiwe na vichwa vilivyojaa neno la Mungu bali mioyo iliyojaa dhambi.

Kama unataka kuwa mwanamume kweli ambaye Mungu atamtumia, jifunze kumwabudu Mungu jinsi anavyotaka kuabudiwa. Mwabudu kila siku katika uzuri na Utakatifu wake. Mahusiano na mawasiliano ni muhimu. Jifunze kuandika barua za kutia watu moyo. Jifunze kuandika barua rahisi, na unapoendelea kuandika utakuwa na ustadi huo, na utakuwa na barua nzuri. Wengi wanapata barua za kulalamikiwa, na watakapoona barua ya kushukuriwa, watashangaa na kupata ujasiri na watatunza barua yako milele.

Ninapoishi, watu wengi wanaogopa kupokea zawadi kwa ajili ya kujisikia wana deni, kiburi au hawataki kuwa kwenye 'mgawo wa ustawi wa jamii.' Wengine wanaogopa kuandika barua za kushukuru. Kutoa na kupokea zawadi kunajenga mahusiano mazuri. Ukiacha kupokea zawadi watu watafikiri kwamba wewe unaona vitu vyako ndiyo vya maana, au hutaki kutoa vyako na hivyo, unawafungia mlango. Kutoa ni mbaraka kuliko kupokea hivyo usifanye watu wengine wapoteze bara zao kwa kutopokea vyao, wakikupa kitu kwa nia nzuri.

Kwa watoto wetu, tunawapa mazoezi ya kutoa tukipokea pia. Ila andika barua ya kuwashukuru na ukilenga kile unachoshukuru; mfano: 'Asante kwa hela, zimenisaidia sana msimu huu kwa kilimo cha matango.' Wengi waandika barua kuomba vitu wakiwa wanafunzi shuleni (boarding), bali wakiwa watu wazima na hawahitaji kitu, hawaandiki ng'o; hili ni kosa. Mawasilianosi kwa kupata vitu bali huduma ya upendo.

Twajitayarishaje kuwa baba bora tukiwa vijana wadogo? Jibu: Kwa kufanya vile ambavyo tungetaka watoto wetu wawe! Usifikiri jinsi utakavyowalea watoto wako, bali fikiri vile Mungu anataka uwe kama Yeye. Watoto wako wakiwa rika lako, Je, wataka wawe wa tabia gani? Maana watoto wako watataka kuwa kama wewe. Je, wewe ni mwaminifu? Je, ni mtenda kazi mwema? Je, wapenda kunung'unika kila mara? Fahamu kwamba watafuata mfano wako.

Mungu ana huruma, japokuwa umeharibu mambo. Maana hatupi tunayostahili (exceptions). Si tabia zako zote mbovu zitaelekea kwa watoto wako bali 'tunda halianguki mbali na mti.' Watoto utakaozaa watafanana na wewe. Mvulana wako akiwa na miaka kumi na miwili atakuwa kama wewe ulivyokuwa miaka na miaka kumi na miwili. Kama u mvulana mwenye shukrani, na mwenye bidii naye atakuwa vile vile, ila kama u mvivu atarithi tabia hiyo mbovu. Ukiwa na bidii ya mazoezi ya chombo cha muziki, naye atakua vile. Somo lolote utakalofanyia bidii naye pia atalifanyia, unachofurahia nao watafurahia. Mfano wako utawafundisha mno.

Tabia ya leo itakufanya uwe mwanamume wa kesho, na hiyo itaathiri watoto wako. Waweza kufikiri mimi ni mtoto tu, nitashughulikia hili au lile nikiwa mtu mzima. Utashangaa siku zimefika, na u mtu mzima na kufanya tu yale uliyoyafanya ukiwa mtoto! Hivyo anza leo kubadilisha mwenendo, una nafasi ndogo ya kubadilisha mwenendo kesho. Uwe na njozi ya kufanya vitu kama mwanamume, na njozi hizi za hekima na maarifa zitakusaidia uwe na mahusiano mazuri na utajiri wa kikweli (true wealth). Kila siku ujenga matofali ya tabia ambayo inakuwa ngumu kama simenti, ikiwa mbaya ni kazi kuiondoa kizazi kinachokuja.

Tabia njema ni kama kuweka akiba kwenye akaunti ya watoto wako. Ukielewa somo, utaepuka mashimo mengi, wavulana waweza kubadilisha mambo kirahisi kuliko wanaume wazee. Angalia maisha yako kwa uaminifu na uyakague vizuri, waulize marafiki

au wazazi wako udhaifu wako na uzuri wako. Mwombe Mwenyezi akufanye wewe uwe mwanamume ambaye unafaa, kisha uanze kubadilisha mwenendo leo.

Je, mwana aweza kuongoza maombi na kusoma Neno la Mungu na kuneemeka? Je, aweza kugawa mamlaka hata kwa ndugu zake wafanye? Lazima kuwe na ratiba ya kufanya kazi kwa watoto wote nyumbani.

Kusaidia vilema na kutowacheka au kuwakejeli ni muhimu. Ninapoishi, mtu mmoja wa Afrika mashariki pamoja na mkewe, walikuwa wakicheka vilema wenye vichwa vikubwa na utindio wa ubongo, walipofanyia kazi. Walipofunga ndoa na kupata mtoto wa kwanza alikuwa na kilema kigumu cha kukosa njia yote ya mkojo, Ilibidi waishi hospitalini. Watu walisema, 'sasa hawana haja ya kucheka mbali, wana cha kucheka karibu, nyumbani mwao!' Walinyenyekea na kuwa watu wanaoelewa shida za watu. Ni kweli mara zingine tunapata shida ya ulema hata kama hatukucheka, maana mapenzi na utukufu wa Mungu hatujui, lakini tunapocheka shida za watu dhamira hutushitaki. www.truthforyourfamily.org by Joel Beeke.

Ukitaka kuwa mtu mcheshi mwenye bidii, watoto wako watakuwa vile pia. Watapenda kazi kama baba na kuwa wacheshi. Utasema, inakuwaje nami ni mvulana hivyo hawanioni sasa? Mpango wa Mungu wa kuishi, kwamba mti mzuri unatoa matunda mema, si kwa kubahatisha tu, bali ni sheria ya mbinguni.

Je, mtoto anajua maana ya uovu ni nini? Anajua amri kumi kwamba ndiyo kipimo cha haki? Je, anajua rehema za Mungu na kutendea watu kwa haki au ana ubaguzi? Maana Mungu anataka tuenende kwa haki, rehema na unyenyekevu. Je, aweza kuwakanya ndugu zake? Je, anapata hasira na kuwakasirikia ndugu zake? Je, hapendi kusahihishwa? Apaswa kujua kusimamia nyumba yake vizuri? Watoto wapewe kazi kutokana na umri, mfano kusafisha gari, kukata majani, kulima shamba, n.k.

Kukana nafsi ni muhimu kwani bustani ya Edeni ilipotea kwa kutotawala tamaa ya chakula, na ulafi. Mtoto afundishwe kuepuka hali hii. Kulinda moyo wake na mafikira kwa kutoangalia vya kuangusha kama Televisheni na compyuta zenye programu mbovu.

Aepuke kuingia kwenye madeni. Zungumzieni mambo ya madeni na jinsi ya kuepuka. Hasa siku hizi za credit cards. Alipe ikiwezekana na ajifunze kutoa sadaka na zaka. Asiwe mtu mwenye hasira, 'Asiyetawala roho yake ni mfano wa mji uliobomolewa, usio na kuta;' Mithali 25:28. Hata mtoto mdogo afundishwe kungoja bila kuwa na hasira, anapocheza na wengine.

Hasira zisizoweza kumilikiwa zinaweza kuumiza mke au watoto au mtoto wa kiume mwenyewe. Akiwa anashindwa kutawala nafsi, na kuwa na harara mfundishe 'kutojisumbua kwa neno lolote, bali katika kusali na kuomba akishukuru aweke haja zake kwa Mungu, na amani ipitayo akili itamhifadhi kwa moyo na nia.' Akiendelea kufikiri yote ya kweli, ya haki, safi, yenye kupendeza, yaliyo na staha, mema, na sifa nzuri, na kutafakari hayo.

Ajifunze jinsi ya kuhudumia familia, na kuwa na adabu njema (manners), maana hizi haziji zenyewe bila kuzifanyia mazoezi. Ajifunze kusema samahani, pole , asante, tafadhali, nisamehe, naomba. Ajifunze kutonyanyasa watu walio chini yake, maana watoto wengi walionyanyaswa na wazazi wao huendeleza tabia hiyo, ila aende mbele za Mungu, kuzikanusha nguvu hizo, au laana hiyo ikatike katika kizazi chake, ili isiendelee kizazi cha tatu na cha nne.

Je, ana muda mwingi wa kupoteza na kukaa kwenye TV. Je, anajifunza tabia za kuwa mtu wa bidii? Je, waweza kumtegemea akufanyie kazi fulani bila kupeleka mawazo

yake kwenye vyombo vya teknolojia? Je, marafiki zake wa karibu wanampenda Mungu au apenda kujiegesha na watu waovu kama Delila? Je, anajua jinsi ya kuwa na urafiki wa kawaida na wasichana bila kujiingiza kwenye urafiki mbaya? Je, ni tabia gani za kuepuka kwa marafiki?

Je, anatoa udhuru wa kuhudhuria ibada? Je, kila saa anatoka kunywa maji au kwenda chooni wakati wa ibada? Je, anamtegemea Mungu au ananung'unika mambo yasipoenda vizuri? Je, anaweza kumaliza kazi uliyompa kama vile Nuhu au Nehemia? Je anaweza kutimiza ahadi zake kama vile Elkana na mke wake? Au mawazo yake yanatawanyika huku na kule? Je, vitu vyake aviacha kila mahali? Hata akivua nguo suruali yake inasimama kwenye sakafu pale pale alivulia?

Mara zingine wazazi wanahusika na kuhudumia watu, na mtoto anapata attention ambayo wazazi hawajui. Hili nilijifunza kwa mhubiri Billy Graham, alipokuwa mashuhuri sana, watoto wake walikaa karibu na lango (gate) la nyumba na kabla wale watu kumtembelea mhubiri, wale watoto waliwaomba washiriki pesa au vitu. Wageni waliona aibu kwaajili ya baba yao wakawapa hawa watoto vile vitu, bila ya kuripoti kwake. Tabia hii alikuwa nayo Gehazi mtumishi wa Elisha! Aliomba nguo mbili na visenti na kupaka matope kazi kubwa ya nabii. Mhubiri huyu alikuja kugundua baadaye, kama wewe mzazi u mashuhuri au wahusika na mambo fulani ambayo watu wengi wakujia, angalia watoto jinsi wanavyohusika na watu, ili uwaepushe na uovu wa namna fulani.

Je, anaweza kuwa mkarimu kama Ibrahimu kukaribisha watu asiowajua na kupata mibaraka? Soma kuhusu ukarimu na kukaribisha wageni. Je, anajua ukarimu kwa familia yake pia? Je anaogopa kupokea simu, kujibu barua au kufungulia wageni milango? 'tazama nabisha mlangoni. Yawezekana Yesu akabisha mlango. Siku hizi pengine hatupati wageni nyumbani ila hata simu zetu mara zingine ni watu wanaohitaji ushauri au huduma kutoka kwetu. Nimejifunza mara nyingi pia ni watu ambao wananibariki mimi, na si mimi nawabariki, kama vile Abrahamu, mgeni yule alimbariki, na si Abrahamu alimbariki yule mgeni! Mwana ajifunze kuwa mhudumu, si kuepuka wageni

Basi mtoto wa kiume asiyejua kutafuta riziki, ni mwovu zaidi ya yule asiye muumini. Japokuwa wanawake wanajitafutia riziki wenyewe siku hizi, hili ni jukumu la kwanza la mwanamume. Hii inataka mwanamume asiwe mbinafsi, na wazazi tuwasaidie watoto wetu wa kiume waweze kuwa watafutaji kwa njia halali. Wasaidie wadogo zao, babu na bibi na pia miradi ya familia. Zungumzeni bajeti ya familia, na jinsi wanavyoweza kutafuta vibarua vidogo vidogo.

Je, aweza kujitafutia mahari yake mwenyewe? Je, anajua jukumu la kutunza wazazi waliozeeka? Je, anasaidia kazi za nyumbani kwa uaminifu? Je, ana ukarimu wa kusaidia wenye mahitaji na kumwonyesha jinsi ya kufanya? Ajifunze kuwa msikilizaji mzuri, na kutoingilia mazungumzo ya watu wengine

Je, anakumbuka kuwaombea wengine au huwa anajifikiria na kuleta shida zake tu mbele za Mungu? (intercessory)? Je, anajua kuungama dhambi akikosa? Je, anajua kusimulia kisa cha wokovu kwa dakika chache, akielezea mafungu yake?

Je, anataka kuoa binti wa namna gani? Je, anawaheshimu wasichana kama ni wake za watu wa siku za usoni na hivyo anawakinga na uovu, na uchafu ili wawe mabikira kwa waume zao baadaye?

Mara nyingi tumejaribu tunavyoweza, hapo tunamwachia Mungu ndiye MWEZA. Hatuwezi kujua kwa nini jambo fulani limetendeka kwetu, ila matukio mengi tunaweza kujua mwishowe yana mshahara gani.

Mvulana atakayeishi kutokana na hukumu na sheria za Mungu atavuna matunda ya watoto wanaompenda Mungu siku za usoni. Mithali 22:6. Hivyo unapojaribiwa kufanya uovu au upumbavu fulani, kama kuvunja sheria, fikiria maamuzi yako, na kwamba yatajirudia kizazi kijacho, hata cha tatu na cha nne. Hivyo ghairi ukanuie kuishi kwa msingi bora wa vizazi vijavyo. Utaishi bila majuto, na itakuwa ngome kwa watoto na wajukuu wako, Mungu atakapokujalia. Tukumbuke Mungu ni mvumilivu, mwingi wa rehema, na anasamehe uovu.

Je, mwana anapasa kuwa na uhusiano gani na kileo?jibu ni 'Asijaribu kuweka mdomoni, hata tone la pombe;, asivae hata tshirts zenye matangazo ya pombe au kileo au kusikiliza matangazo ya biashara ya namna hiyo. Asiende mahali ambapo kileo kinapouzwa au kumcheka mtu aliyelewa maana dhambi ni kitu cha huzuni. Kataa kutoa sababu kwamba ni lazima unywe, hata kama huna mpango wa kunywa, jua ni jaribu linaloweza kukujia, kwani wengi hawakufikiri wataingia katika ulevi. Waambie marafiki zako kwa upendo kwamba hutakunywa na sababu unamheshimu Mwenyezi Mungu. Mithali 23:32 yasema, 'Ukae mbali nayo kama unavyoweza kukaa mbali na nyoka.'. 40% ya wanywaji hawawezi kuacha (alcoholic). Je Ukiwa na mbwa anayeuma watu 2 kati ya tano wanaokuja kwako utaendelea kumfuga?

Mwana ajue kwa nini anapata adhabu au masahihisho ya tabia yake ili aongozwe katika njia njema ya hekima. Mwana anayependa wazazi wake atawashukuru pale wanapomsaidia. Ajiepushe kuharibiwa na misukumo ya rika ndiyo ilimponza Samsoni. Kumpenda Mungu na kutembea katika njia zake na kumtumikia kwa mioyo, akili, nguvu na roho zetu ndiyo hekima. Maneno yake yawe yametiwa munyu ili ajue kujibu watu maana maneno yanaonyesha tabia na kile kimeujaza moyo wake. Usafi wa mawazo, maneno, na matendo (purity) ni muhimu.

SURA YA 43

Kukuza mtoto wa kike awe mwanamke wa mithali 31-Mafunzo kwa mama na binti.

Daudi, mwandishi wa Zaburi, azungumza maneno ya baraka kwenye Zaburi 144:11-15. "Wana wetu wawe kama miche waliokua ujanani, na binti zetu kama nguzo pembeni zilizonakshiwa na kupamba hekalu...".

Bila shaka kukuza mabinti zetu mpaka utu uzima wakiwa wanampendeza Mungu ni baraka kubwa. Wazazi wengi kwa kuwa na shughuli nyingi, wanajaribiwa kuacha watoto wajikuze wenyewe. Mungu hakutupa watoto tuwatelekeze (neglect). Uzazi ni jukumu zito, kuliko wengi tunavyofikiri. Kina mama hatuwezi kuacha watoto wetu, hata wa sekondari, wakiwa ndani ya nyumba peke yao, na sisi tuko busy, au tunasafiri kila wakati.

Wengine twafanya kazi kwa shift, wengine twajitembeza hapa na pale, na tunaacha watoto peke yao; hili ni kosa. Mawazo ya mtoto yanatembea huku na kule wakati mwingi. Aweza kwenda kwa majirani, au kuangalia mambo yasiyofaa n.k. Wanaweza kuanza kufanya maovu, ila usiwe wewe ndiye uliyetoa nyufa. Wengine wamepeleka watoto wadogo magharibi wakawaacha huko wenyewe, bila wao kuwepo. Wengi walishindwa kumaliza shule, bali la kuhuzunisha zaidi, ni kwamba wengi waliacha imani. Waliingia kwenye ndoa za ajabu ili kupata vibali vya kazi, na kupigana na wenyeji wa nchi hizo, na wengine wakawa hoi, kwa michoko. Sulemani asema mtoto ana ujinga wa namna fulani.

Masomo ya chuoni au kwenda Magharibi yamekuwa kama miungu fulani siku hizi za mwisho. Maisha ya kumcha Mungu ni mpando. Usiache mtoto wako kwa mtu

akuangalilie kama siyo dharura, kwani utamlaumu huyo mtu. Watoto wana mambo mengi; hata kama ni mtu mwema umempa hiyo shughuli. Hata hivyo ana uchungu gani na mtoto wako zaidi ya wewe?

Tulikutana na msichana mkubwa wa sekondari, aliyelelewa mbali na wazazi wake, ambaye hakusalimia watu, hakushukuru watu walipomtendea mema, wala hakufungua mdomo wake aliposalimiwa au kuulizwa maswali ya kawaida. Tulidhani ni bubu au kiziwi, bali tuligundua ni tabia alivyokuzwa bila kufundishwa adabu, au kutofahamu, (ignorance). Wengine wakasema ni 'mtu wa haya'. Haya na kukosa adabu ni vitu tofauti.

Mabinti wetu wanahitaji mafunzo (training), kwani siku za usoni watakuwa walimu wa watoto wao na watahitaji mawasiliano bora na waume zao na hata wakwe. Je, unaweza kumkanyaga mtu kwa bahati mbaya na kutotoa hata samahani?. Hata hivyo ye yote anayetaka kuwa raia wa ufalme, lazima ajue kuwaambia watu habari njema! Je atanyamaza kimya, eti anaona aibu?

Mithali 31 ina mengi ya kusema kuhusu mwanamke anavyopaswa kuwa. Nafikiri jambo hili linaanzia katika matunzo udogoni, na si ukubwani. Wengi wamesema mwanamke wa mithali 31 ni muunganiko wa wanawake wengi! Tunaona ana watu wa kumsaidia kazi zake, ila ni yeye anabidi kupangilia mipango ya mambo ya kufanya. Kama wazazi na hasa kwa wanawake, tuna haja ya kujifunza zaidi kuhusu mwanamke wa Mithali 31 kwa undani. Maswali haya na majibu ni kwa mjadala na mabinti zetu. Tuendele kuwaongoza na kuwathathmini, nasi wenyewe tutazidi kukua katika safari ya kwenda mbinguni.

Mama Pam Foster wa doorpost.org amemzungumzia mwanamke huyu kwa undani. Tumechukua maswali yake, nawe utachukua nafasi kila siku kujadili na binti yako, na kumfundisha yanayohusu maswali haya ya Mithali hii 31. Ni vyema msome pamoja kitabu chote cha Mithali, Mhubiri, na Zaburi. Chukua muda kusoma Neno la Mungu lote kila jioni kwa miaka mitatu, mkisoma sura moja moja na kutafakari na kuwa na maswali mtajifunza mengi ya kulea tabia ya kufaa kwa mtoto. Hakuna kitabu bora kwa kukuza mtoto kama Neno la Mungu.

Je, anaelewa kwamba uumbaji kwa siku sita na mapumziko ni mhimili kwenye mafundisho ya Neno la Mungu? Siku hizi nadharia za kuibuka (evolution) zimezuka na kufanya mabinti zetu wasijithamini, kwamba wameumbwa na Mungu! Siku za Mwanzo moja ni siku halisi za masaa 24 na si mamilioni ya siku.

Somo la kwanza kwa watoto wetu ni utii. Twarudia “Utii” ndiyo somo la kwanza!”. Kutii maagizo ya Mungu na wazazi.

Tunakumbushia tu kwamba maneno haya yalizungumzwa na mama yake Sulemani, akimwambia kijana wake jinsi ya kuona mwanamke bora! Kinyume cha mwanamke bora ni mwanamke wa Mithali 7, ambaye ni ‘mwanamke mgeni’ (strange woman).

Lazima sisi wanawake tuwe watu wa kusali kwa kukesha na kuwa na mipango/magoli kamili ya kulea, na kuyaweka kwenye karatasi. Kama tunataka tuwe na mabinti wa mithali 31 lazima nasi waone mifano yetu . Hivyo tumwombe Mungu atupe nguvu, tufunge mikanda ili tusaidiane na mabinti zetu. Mabinti wajifunze utii, mipangilio, kujikana nafsi, ustadi, usafi, na kazi.

Wote tungependa tuwe na mabinti waliokomaa kiroho, kiakili, kijamii, , kiuchumi na kimwili pia.

Mwanamke huyu anazungumziwa kwa undani sana. Twaona anatayarisha chakula, anashona nguo zake na za familia, anafanya ujasiliamali, ananunua mashamba

na kulima, ananunua nyumba, anapanda mizabibu, anasaidia wenye mahitaji. Ni mwanamke wakupendeka (admired).

Wanaume pia wangependa kuwa na dada, mama, binti au mke kama huyu.. Hata kama mume ni mtu asiyeamini, aweza kubadilika kwa mwanamke kama huyu. Wanawake wana sehemu kubwa katika malezi, twaona Timotheo, mhubiri mkubwa alipata imani toka kwa bibi yake Lois, na kisha mama yake Yunisi. Tusichoke kutenda wema maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho.

Wanawake wengine wamekata tamaa kutokana na maisha magumu ya mateso, mwingine alisema "Nimekinywea kikombe." Ni kweli wengine wameangukia pagumu, hata hivyo tusichoke, tusipozimia roho, hata kama binadamu na wale wa familia yetu ya karibu wasitusifu (appreciate) au kutupenda, wito wetu kwa neema za Mungu, ni kuishi maisha ya mwanamke wa Mithali 31.

Mambo haya ni ya kufanya na mabinti zetu wakikua. Pengine yapasa tuwe na vitu vichache ili tuwekeze kwa watoto wetu hazina mbinguni badala ya duniani. Tusifikiri masomo ya shule tu, bali hata nyumbani. Ni vyema kuwa na mpangilio (syllabus) ya kusaidia watoto tabia na taaluma; maana hata hekima ya dunia tunayoikazania sana yaweza kuwa upumbavu kwa Mungu; 1 Kor 3:19. Waweza kuleta topic kwenye maombi, kuhoji watu, kutenda vitu (practical), kujadili, mafungu ya kukariri kutokana na topic, kuuliza maswali, kusoma vitabu vingine vihusuvyo tabia tunazozijadili na mwishowe kutathmini, ili wakue kiroho katika ile nyanja mnayotaka kuijenga.

"Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili, bali mwanamke amchaye Bwana ndiye atakayesifiwa. Mke mwema ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani" (rubies); Mithali 31:10. Fungu hili linatuambia tuombee mabinti zetu kuwa na roho za unyenyekevu, na upole mbele ya Mungu, kuwa tayari kusikia na kulitii Neno lake.

Wape nafasi wamhoji bibi au mama mwenye mvuto wa kumpenda Mungu na kuomba ushauri wake. Wape nafasi mabinti/binti zetu ya kuzungumza na baba, au wajomba zao na kuuliza ni sifa gani iliyowavutia kuoa yule waliyeoa. Je, katika Neno la Bwana wanawake kama hawa ni kina nani? Toa mifano ya hadithi za wanawake kama Debora, Esta, Hulda, Elizabeti, mke wa Ayubu, Ruth, binti za Lutu, Tamari, Safira, Goma, Prisila, Abigaili, Jezebel, Bathsheba, Raheli, na Rebeka.

Soma Tito 2 na andika orodha ya mwanamke amchaye Mungu. Soma 1 Tim 5:3-10 inayofanya mjane athaminiwe na kusaidiwa. Jiulize maswali kuhusu binti yako kama anampenda Mungu, na kama wokovu wake ni muhimu kwake. Je, anapenda kusoma Biblia, au anafurahi akisomewa kama ni mdogo? Je, anaelewa Neno la Mungu? Je, anapenda kumtii Mungu? Je, ana mahusiano na Mungu? Je, akifanya makosa, anajutia dhambi na kuomba msamaha kwa Mungu na wale aliowakosea? Je, anapenda kuwa kama wasichana wa dunia kwa mavazi, michezo na mwelekeo? Je, ana udhaifu fulani wa tabia? Je, anafanya jambo gani kuondokana na udhaifu huo. Je, lile tunda la Roho la Wagalatia 5:22-23 linaonekana katika maisha yake? Je, wawezaje kumsaidia katika nyanja hizi za tunda? Je, anakua akiendana na Mithali 31 na Tito 2? Je, ana magoli ya kumtukuza Mungu na kuwa mhudumu kwa Mungu na familia yake, au anajipenda na kutafuta anasa zake za kuinufaisha tu?

"Moyo wa mume wake humwamini, wala hatakosa kupata mapato," fungu la 11. Mume wake anaona kwamba ni mke anayechukua majukumu yake kwa makini. Lazima tuwatayarishe mabinti zetu kwa hili, kwa kuwafundisha (train). Elimu ya binti yako ni muhimu, na inafanywa nyumbani. Ajue kazi za nyumbani, mpeleke kwa mwanamke

ambaye ana bidii ya kufanya majukumu yake vizuri, amhoji kwa nini anafanya shughuli zake kwa uaminifu? Kwa nini awe mwaminifu katika kazi? Jadili naye mifano ya uaminifu kwenye Biblia toka udogoni kama vile Ibrahimu, Yusufu, Daniel, binti mtumwa wa Naamani, Delila, Mikali, mke wa Potifa, mke wa Hamani, Herodias, Hawa, au Tabitha. Umepita wakati wa jando na unyago, mabinti walifundishwa haya, leo hii mfundishe binti wewe na waumini wenzako. Usiseme 'shangazi'vvff ndiyo amfundishe hili.

Mara nyingi wasichana wana majaribu ya kuzungumza mno ubaya wa wengine na kusifia (flattery). Kama wazazi tuepuke kutia chumvi, uongo, umbeya, manung'uniko, wivu, hasira, kiburi na unafiki kwa maneno, matendo na mwelekeo. Mpeleke amhoji mtu kanisani "Kwa nini unamwamini fulani na si Fulani?" Je, waweza kumwamini binti akisema kitu au anasema nusu ukweli na nusu uongo akitoa udhuru? Je, anasema uongo kwa matendo yake na kutunga hadithi, au kupunguza kweli? Je, anatunza ahadi zake? Je, akisema uongo anajaribu kuufunika uongo huo kwa uongo mwingine? Je, anazungumza watu vibaya wasipokuwepo? Je, anarudisha vitu alivyoazima? Je, ana uaminifu katika mahusiano, magoli, malengo au mipango yake au anajidanganya hata yeyé mwenyewe? Je, anapenda kutoa rushwa au kujipendekeza ili afanyiwe kila anachotaka? Je, anasema kwamba alikuwa 'anatania tu' akikutwa amefanya uovu? Je, mara nyingine anazungumza bila kufikiri na kukosoa wengine bila kujali au kuwa na upole? Je, yupo huru kuja kwako na kukueleza mambo yasipokuwa mazuri na hasa yale nyeti?

Jadili naye maswali kama 'Kwa nini si vizuri mke kumsema vibaya mume, wazazi au hata wenzake kwa watu? Kwanini mwanafunzi hapaswi kumzungumza vibaya mwalimu wake?' Uaminifu ni muhimu utotoni na hata ukubwani. Jadilini ubaya wa talaka na aandike insha.

Je, yupo tayari kumsaidia rafiki endapo amekosea kwa upendo na unyenyekevu, na siyo tu kumsema mbele ya watu na kumwacha aendelee na tabia mbovu? Je, anakasirika haraka na kufuta urafiki kirahisi. Je, anapenda wote wasiwe na urafiki na yule ambaye yeye ameacha kuwa rafiki naye? Je, anasamehe haraka akiwa amekosewa? Je, anathamini mawazo ya marafiki zake au wadogo zake, na kuwasimamia naye pia aweza kuwapa ushauri mzuri?. Je, anakuwa na wivu au chuki rafiki yake au ndugu akifanikiwa? Je, yuko tayari marafiki zake wawe marafiki wa wengine, au anataka wawe marafiki zake tu? Je, anapenda kuwazomea, kuwashushua au kuwabeza wengine akiwa na marafiki zake? Je, anathamini uongozi wa wazazi na magoli ya familia. Je, anakosa adabu kwa wazazi wake mbele ya marafiki zake?. Je, ana uaminifu kwa mume wake wa siku za usoni kwa kujitunza au huingilia urafiki wa kimapenzi na wavulana/wanaume? Je, anajua kwamba ndoa ni jukumu la maisha yote (lifetime commitment)?

Kama msichana, usikivu ni jambo jema, hata kwa mume atakapoolewa. Kuwa msikivu bila kuingilia kati, kubishana au kupayuka payuka liwe lengo lake. Anapaswa kujua mke anamsikiliza mumewe kama kiongozi, akitoa majukumu au kujadili mambo ya familia. Watoto wake pia watahitaji kusikilizwa, hii ni karama anayopaswa kujifunza kuwa nayo. Wanawake wengi twahitaji tusikilize zaidi ya kuzungumza.

Dhambi zinazotuzinga kwa upesi kama vile umbeya, kukosoa, na kutona tona (nagging) zinatokana na kuzungumza sana badala ya kusikiliza. Twapaswa kufundisha mabinti zetu kusikiliza. Kitabu cha Mithali, Mhubiri, Zaburi na barua za Paulo vina mengi kuhusu haya. Angalia watu ambao unafikiri wana hekima, kisha waangalie wakizungumza na watu. Je, wanazungumzaje, wanasikilizaje? Je, wanaulizaje maswali? Je, waweza kujifunza nini toka kwao? Umbeya na kutosikiliza vizuri vina undugu. Je kwa nini ni

muhimu mke kumsikiliza mume au mtoto kabla ya kurukia? Mwambie aandike insha ya kumsikiliza mume au mtoto. chukua tangazo la biashara la uongo umpe alitoe kasoro.

Maswali ya kujiuliza kama mzazi ni: Je, anasikiliza sauti ya Mungu na kumtii Roho wa Mungu anapozungumza na moyo wake? Je, anasikiliza mahubiri kwenye nyumba ya ibada? Je, anaweza akarudia yaliyozungumzwa ibadani au anasema mahubiri yalikuwa mazuri, bali hawezi kukumbuka kitu? Je, anakusikiliza wewe au baba yake mkizungumza naye? Je, anaonyesha adabu ukizungumza naye, Je, anajifanya hakusikia? Je, anapoteza mawazo kwingine watu wakizungumza naye? Je, hana simile ukizungumza naye na anataka aendelee na shughuli zake, na mara nyingine anaondoka ukiendelea kuzungumza? Je, anasikiliza kwa umakini unachomwambia na kukifanya sawa? Je, anakumbuka alichoambiwa? Je, anapenda kuingilia kati mazungumzo na kufikiria atakachosema badala ya kusikiliza? Je, anatoa ushauri wake haraka wakati bado mwenzake anamwambia tatizo lake, Je anapenda kutawala mazungumzo yote?

Kama msichana anatakiwa awe na sifa ya upendo, asiwe mtu wakujifikiria na; na akariri fungu la1 Korintho13: 4-8, na baada ya wiki mbili hivi amalize kukariri yote. Je, akipenda watu ni matendo gani atatenda? Je, akimpenda Mungu na kutaka kufanya mapenzi yake ni matendo gani yataonekana kwake? Je, awezaje kuwaonyesha upendo ndugu zake, baba na mama yake, babu na bibi, Wajomba na shangazi? Je, apaswaje kuwatendea “maadui” zake, kutokana na Neno la Mungu?

Tito mbili yahimiza wanawake wajane wazee kufundisha wanawake vijana kupenda waume zao. Upendo unafundishwa pia, na ni vyema tuwafundishe binti zetu, hasa katika ulimwengu wa leo uliojaa ubinafsi au umimi (me, myself, and I). Wengi wanasema nafanya hili kwa ajili yangu, au “kila mara nawafanyia watu vitu, nimechoka sasa nataka nami nijifanyie!”. Wanawake wajane, wanathamini sana waume zao, hasa wakiwakumbuka, wanasema 'ningejua'.

Someni pamoja na kujadili upendo wa aina tatu (Phileo yaani wa ndugu, Agape yaani wa Mungu na Eros yaani wa mapenzi kati ya mume na mke). Je hizi aina za upendo zinatofautianaje?. Je, ana uvumilivu wengine wanapokosea au anapata hasira haraka? Je anaonyesha upendo wa Mungu kwa wengine hata kama haafikiani nao? Je, yupo tayari kusahau makosa madogo madogo ya watu aliyofanyiwa? Je, anapatana na kushirikiana na wengine, na wengine wanapenda awe rafiki yao? Je, anapenda kusaidia mahitaji ya wengine kabla yake au anajitafutia yeye kwanza kabla ya ndugu zake au marafiki? Je, anakimbilia kiti kizuri au andazi kubwa au mwanasesere mzuri ili wengine wasipate? Je, anaangalia mapungufu ya watu na udhaifu wao kupita kiasi? Je, anawakosoa marafiki zake kwenye kadamnasi? Je anapenda kujenga wengine au anapenda kujipigia filimbi yake na kujisifu? Je, anakumbuka makosa ya wengine mara kwa mara? Je, anacheka na kufurahi wengine wakipata adhabu? Je, anatafuta nafasi ya kuhudumia wengine au anataka yeye tu ndiye ahudumiwe? Je, anaonyesha upendo kwa wale wanaotaka kumdhuru au kumwangusha?

Utii na kuwa na adabu ni muhimu sana kwa msichana. Binti zetu tuwatayarishe wamtii Mungu. Ili kuishi maisha ya amani na furaha, ni muhimu kumtii mume endapo Mungu amewapangia kuolewa. Mabishano, kukunja nyuso saa yote, manung’uniko, kuzira, na kutaka kuburuza wengine si tabia njema. Wote tumeanguka na kupungukiwa na utukufu wa Mungu ila turudi.

Mama yetu Hawa kwa kutotii na kukaa karibu na mume wake, alikuwa mtenda dhambi kwa kwanza duniani. Mara nyingi tunafikiri wanaume wana vituko vingi na dhambi

nyingi kama vile kuua, ujambazi, uongo, na mengineyo; bali tukumbuke ni mwanamke ndiye aliyetufikisha hapa kwa kutotii! Mwanamume naye amepewa sehemu yake, ya kumpenda mke wake kama Kristo alivyolipenda kanisa na kulifia. Hii ni kazi kubwa mno pengine kuliko ya mwanamke akiitenda inavyopaswa.

Nilimsikia mama mmoja akisema wanaume wana ukarimu mkubwa kuliko wanawake, na hivyo tunapokuza watoto wa kiume tusisahau hili. Nilishangaa baadaye nikagundua ni kweli kwani mipango yote ya serikali ya kutoa misaada aidha ya ustawi wa jamii au kwa mataifa mengine, wanaume ndiyo wahusika mara nyingi! Hivyo wakina mama, tufundishe mabinti zetu ukarimu na karama tofauti za jinsia na fundisho litafika kwa wajukuu zetu pia! Kwa upande mwingine hasi, wanawake wanagombana na watu hapa na pale au majirani bali wanaume wanaenda vitani na kugombana na wengi! Haya yote mwanamke wa mithali 31 apaswa ajue ili asaidie watoto wake wote. Wanasema Barbra mke wa Bush yule mzee aliyekuwa raisi, alisema haya wakati mtoto wake aliposhika uraisi wa Marekani, nchi yenye nguvu duniani 'nimetawala dunia mara mbili, kwanza mume wangu alikuwa raisi, kisha mtoto wangu wa kiume sasa ni raisi!'. Mama huyu alijua kama mama ana nafasi fulani, si lazima ile mwanamume alipewa, ila ana fungu lake.

Katika kielelezo alichotupa Mungu, si kazi kumtii mume, kwani yaonekana yeye ndiye mwenye jukumu kubwa katika ndoa nasi ni wasaidizi. Kumtii mume ni furaha kubwa na ni amri toka kwa Mungu, na kama huamini, basi mwulize mama mwenye mkamwana (mke wa kijana wake) asiyemheshimu akueleze jinsi serikali hiyo ilivyo na masikitiko yake.

Mtoto wa kike anapaswa kujua agizo la Mungu la waefeso sita “Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana maana hii ndiyo haki”. Je, ni njia gani binti aweza kuonyesha utii kwa wazazi wake? Je, mamlaka gani mengine zaidi ya wazazi anapaswa kutii? Kanisa, serikali, kazi n.k. Someni Neno la Mungu la wale waliotii na wale wasiotii kama Akani, Kaini, Nuhu, au Yakobo. Soma kumbukumbu la Torati 28.

Je, kwa nini jina la Mungu linaweza kutukwana kwa mtoto asiyemtii mzazi au mke asiyemtii mume? Je, anatii bila kusita, kubishana au kulalamika? Je, anafanya unachomwambia kwa furaha au anaweka sura mbaya? Je, uso wake waonyesha roho ya unyenyekevu mbele ya Mungu na mamlaka Mungu aliyoweka kwa ajili ya maisha yake? Je, matendo yake yanaonyesha utii? Je, anatii mamlaka uliyompa mwingine kama yaya, shangazi au mwalimu? Je, anajua kwamba Mungu Ndiye mamlaka ya mwisho? Je, anathamini maamuzi yako hata kama mara nyingine hayaleti maana kwake? Je, anajua jinsi ya kukata rufaa kwako kwa adabu endapo anataka asikilizwe tena? Je, anaonyesha adabu kwa polisi, walimu na mamlaka ya serikali? Je, anatumia muda kujua Neno la Mungu na kulitii? Je, anakutii ukiwa karibu au hata mbali ambako humuoni? Je, anatii kwa furaha au kwa moyo mzito?

Kutunza amani nyumbani ni muhimu kwa msichana. Usichana ni maabara ya vile atakavyofanya duniani. Mahusiano mema ni zawadi toka kwa Mungu na kuyatunza na kuyapalilia ni jukumu. Tuwaepushe mabinti zetu na kuzira, kuweka visasi kwa wazazi au ndugu zao. Kuwa na chuki au hila si kitu Chema. Twapaswa tusamehe ili kuleta uponyaji na kukua na hata kukomaa kiroho. Soma kuhusu upatanishi, magomvi, kuonywa, na mwanamke mgomvi kwenye kitabu cha Mithali.

Je adui atendewaje? Mpe binti aandike kuhusu kusamehe wengine na kusamehewa. Soma Neno la Mungu na kuona mifano ya kusamehe na kusamehehwa. Twaweza kujua Neno la Mungu, bali tusipojua kusamehe tutapata maumivu mengi, mahusiano yaliyovunjika na hata kwenda Jehanamu tusipotilia makini. Mahusiano ya

binti akiwa mdogo katika familia yanamtayarisha kuwa na mahusiano mema na familia yake atakapokuwa mtu mzima.

Je, wazazi ni watu wa kupatanisha wengine, Je, wanasamehe watu, au wanapenda malumbano? Wewe kama mama angalia pale unapaswa kusahihisha. Jadilini kuhusu mwanamke mgomvi kwenye kitabu cha Mithali. Soma pale wanawake waligombana kwenye Biblia kama vile Sara/Hajiri, Raheli/Lea/Yakobo, Penina/Hana, Mikali/Daudi. Miriamu/Musa, Ayubu/Mkewe uodia/sintike. Waligombania nini? Matokeo yake yalikuwa yapi? Je, tunajifunza nini?

Soma Waebrania 12:15-16 na Jadili na binti. Jadilini kuhusu hasira, visasi, kusamehe na uvumilivu.

Je, anachukuliana vizuri na ndugu zake au kila mara wanagombana akijitetea kwamba anatunza haki yake? Je, ana haraka ya kuzungumza au anasikiliza anapoonywa? Je, anapogombana, anachunguza moyo wake kama ni yeye ana makosa? Je, anasamehe wengine, akijua hata yeye ana makosa pia?

Je, yupo tayari kumfuata aliyemkosea na kumwomba msamaha? Je, anapenda upatanisho au anakaa na kisasi? Je, anajua jinsi ya kutafuta suluhisho kwa njia ambayo haitaleta ugomvi? Je, anasali kwanza kabla ya kuzungumzia upatanisho? Je, yupo tayari kusuluhishwa hata ikibidi zaidi ya mara moja na mtu huyo huyo? Je, anajaribu apatane na waliyekosana mapema au anakaa na hasira muda mrefu? Je, anaamini Mungu atampigania au anapenda kuchukua sheria au kisasi mkono mwake? Je, anaangalia mazuri ya wangine au anaangalia mabaya yao tu? Je, ni mwepesi kukosoa na kukaa na chuki? Je, anasamehe na kusonga mbele au anapenda kuyaleta yale aliyokosewa zamani tena na tena?

Haya ni muhimu kwani binti akiwa na nyumba yake atakosewa na mume au watoto, naye atawakosea pia. Hivyo aanze kujifunza mahusiano ya kutunza amani anapokua.

Lazima ajue unyenyekevu ni jambo muhimu. Kunyenyekea kwa uongozi wa Mungu ili kila siku umimi upungue kusudi Roho wa Mungu aweze kufanya kazi ya kumsaidia kwa tabia njema. Awe tayari kukosolewa bila kubishana. Je, yuko tayari kusema alilokosea bila kuficha? Je, maneno yake yanaonyesha kiburi na anafikiri wakati wote yeye ndiyo yuko sawa? Je, hakati tamaa akifanya dhambi bali yupo tayari kuomba msahama si kwa kuepuka adhabu bali kwa kumpenda Mungu. Je, anajua hawezi akafanya vizuri bila uongozi wa Mungu? Je, anajua kwamba Mungu ndiyo mtawala na amempatia wewe mzazi, umsaidie katika maisha yake? Je, anajua sheria za Mungu ni kwa ajili ya mema kwetu?

Kuishi maisha ya usafi ni muhimu kwa binti, na mji wake atakapokuwa mtu mzima. Usafi wa mawazo, maneno na matendo. Mfundishe kuomba kila siku ili aweze kumtii Mungu na kuepuka majaribu.

Je, majaribu ni nini? Kwa nini tunafanya dhambi, matokeo ya dhambi ni nini? Someni pamoja kwenye Neno kuhusu dhambi na maisha ya giza au mahusiano ya dhambi. Je, wangapi wamefanya dhambi? Mshahara wa dhambi ni nini? Je, ni kina nani walishinda majaribu? Na ni kina nani waliepuka? Someni pamoja Mithali saba na jinsi ya kuepuka tabia ya mwanamke mgeni? Je,anajua kwamba kuna mapambano kati ya Shetani na Mungu na kwamba yeye anahusika? Je, anajua shetani alitoka wapi? Je, anajua akiwa na shida hapaswi kwenda kwa waganga au wachawi bali kwa wacha Mungu? Je, anajua yeye yuko hapa duniani kwa sababu gani?, Je, anajua jinsi atakavyopata ushindi? Je, anajua kulitumua Neno la Mungu kupata ushindi kwa majaribu? Je, anaepuka mahali

kwenye mitego ya majaribu au anajipeleka? Je, anachagua marafiki wanaompenda Mungu au wale wanaompeleka kwenye uovu? Je anajua kukimbia majaribu? Je, anakubali mashauri kuhusiana na marafiki wabaya? Je, anakutii katika mambo yote kama vile muda wa kurudi nyumbani au shughuli za za kufanya?

Je, ana tabia ya kutongoza wavulana au kusema vimaneno vyenye walakini vinavyowafanya watu wamshuku mambo maovu? Je, anamwomba Mungu kumsaidia kuepuka dhambi, Je, anaepuka marafiki wa kiume 'boyfriend' na kujua mpango huo wa dating si wa usafi bali ule wa uchumba (courtship)? Je, anatumia muda wake vizuri au anasoma vitabu vichafu au kuangalia picha mbaya? Je anatumia muda wake kuwa na ndoto za mchana zisizo na faida? Je, anakuja kwako kwa maswali ambayo ni nyeti na ya rika yake au anakuogopa (ya uchumba, marafiki wabaya n.k)?

Ni vyema kufundisha mabinti wetu uvumilivu na kuwa na tabia ya mbinguni. Twawafundisha haya wakiwa wadogo kabla ya kupevuka. Wawe na uvumilivu katika mambo mengi, mfano ya kutoanza kuwa na marafiki wa kiume mapema bali kufuata mpango a uchumba. Hatushauri kuanza uchumba mpaka kupevuka, hii ni kuanzia miaka 18, ila ni vyema waweze kujitegemea ili wasiwe mzigo. Marafiki wa kawaida (general friends) ndiyo wale ambao mara nyingi ataolewa nao.

Aepuke kuzungumza na wavulana mafichoni, akiwapa matumaini fulani ya urafiki usio mzuri. Ni vyema awe wazi ya yale yanayoendelea kwa vile wazazi wana uzoefu mkubwa, hasa maisha ya leo katika kuwasadiia mabinti ili wasiingie katika ndoa zenye huzuni. Mama uwe tayari kujadili; mtoto wako hawezi kujifunza kwa mwingine sawa, ila kwako. Ni vyema mama amsaidie binti kuweka viwango vya mume anayetaka kuolea naye, akiwa tayari kutii na kumheshimu mume huyo. Angalia mifano ya Isaka/Rebeka, David/Mikali, Esau, Samson, Solomon, .

Soma vitabu kama, "I Kissed Dating goodbye;" by Joshua Harris na mjadiliane hatari za Dating (urafiki na wavulana) na uzuri wa Courtship (uchumba). Je,yupo tayari kusikiliza mashauri yako kuhusu kuchagua mwenzi wa maisha, Je, anaamimi kwamba Mungu atamsaidia kupata mchumba au anataka kuharakisha? Je, yupo tayari kukua kiroho ili kuwa na nyumba bora au anakimbilia aolewe? Je, anasoma hadithi za mapenzi ambazo zote zina mafundisho mengi ya uongo kuhusu upendo na ndoa?

Je, yupo tayari kujitunza kwa kuepuka majaribu ya ngono yaliyo katika miziki, vitabu, picha, marafiki na filamu? Je, amekuja kwako na kuuliza maswali kuhusu ngono kwa mpango wa Mungu na ngono safi? Je anajua mpango wa Mungu kuhusu ngono? Je, ameelewa kukomaa kwa msichana kwa kuvunja uongo na jinsi ya kujitunza? Chukua muda kuzungumza nayo haya, si mara moja tu, ila hapa na pale. Je, yupo tayari kuishi peke yake maisha yake yote kama ni mwito ambao Mungu amemwitia?

Kujitoa kikamilifu ni muhimu kwa msichana. Twaona maisha ya Ruthu jinsi alivyojitoa kwa mume wake, na kisha kwa familia ya mume wake na kubarikiwa. Binti anapaswa aheshimu wazazi wake akiwa mdogo nyumbani kwao. Awaheshimu ndugu na jamaa kama kaka, dada, mama, baba, babu bibi, mjomba na shangazi. Angaliwe na mfundishe kwa makini, kisha ujiulize haya. Je, anaheshimu wakubwa wake? Je, anawakejeli, au kuwapuuzia wakubwa wake? Je, , anataka bibi na babu wamsaidie yeye bali yeye hataki kuwafanyia kitu? Je,anasikiliza kwa adabu wajomba, baba wadogo, au shangazi zake? Je, anatawaita bibi na babu nakuomba mashauri yao? Je, kwa kawaida anawasiliana na babu na bibi? Hapa wazazi ni lazima tuonyeshe mfano wa kupenda na kuheshimu wazazi wetu. Je, anawasaidia wazee kijijini mwake kwa furaha? Je, anawashukuru ndugu na jamaa wanapomsaidia au anaona ni haki yake?

“Hutafuta sufu za kitani, hufanya kazi yake ya mikono ka moyo” Fungu la13. Twapaswa kuwafunza mabinti zetu kuwa na ujasiliamali au bidii ya kazi. “Asiyefanya kazi na asile.” Wanapaswa wafanye kazi, wakijisia au wasipojisikia! Wajifunze kufanya kazi kwa furaha, kazi ni amri toka kwa Mwenyezi Mungu kabla hata ya maanguko ya binadamu. Mfanyakazi awepo au asiwepo, binti ajue kufanya kazi zote na azifanye.

Binti afanye kazi za mikono, kazi za shule, lazima tuwe na orodha ya vitu vyakufanya kila siku. Kama ni kulisha kuku, kutandika kitanda, kufua, kufagia, kudeki, kulisha wanyama. Twajifunza toka kwa nyuki, siafu na wanyama wengine kuhusu kutokuwa na uvivu. Chukua muda kuona wadudu hawa na binti. Aangalie unavyofanya kazi, naye afanye akijali wakati atakapojifunza kuzifanya asifanye kivivu. Mpe kazi zingine kwa malipo madogo ambazo si za kila siku kama una uwezo kumpa motisha. Aweza hata kufungua akaunti yake kama familia inaweza kufanya hilo na kujifunza kutunza akiba/kutumia pesa kwa hekima. Someni kuhusu kulala kupita kiasi na hasara zake. Chunguza maisha ya Yusufu, Nehemia, Daniel , Ruth au Tabitha. Angalia maisha ya Raheli na Rebeka wakifanya kazi kabla ya kuchumbiwa. Mkatie sehemu ya bustani ashughulikie. Angalia maisha ya wanariadha, wanasayansi, waandishi, wavumbuzi na masaa waliyotumia. Angalieni wanawake wenye biidii mnaowajua, wanafanya mambo gani? Je, uvivu una shida gani?

Jiulize, Je, anafanya vizuri anavyoweza? Je, anafanya kazi pale watu wanapomwangalia, Je, analalamika na kuweka sura mbaya akitaka apewe zawadi au kulipwa? Je, anangojea mwingine afanye kazi, aking’unung’unika au kutoa vijisababu? Je, anauliza maswali kana kwamba hajui kufanya kazi uliyompa, au inakuwa sababu kwake ya uvivu? Je, anafanya kazi za kila siku bila kukumbushwa? Je, anamaliza kazi au anapotea au kupeleka mawazo pengine? Je, waweza kumweleza jinsi kazi inavyofanywa na akaifanya? Je, anafanya kazi nusu nusu? Je, anatunza vitu vyake? Je, anarudisha vitu vyake baada ya kutuvimia? Je, anacheki kazi yake kabla ya kuripoti au anaparaza paraza tu? anapoteza muda, au kusema nitafanya kesho? Je, anakata tamaa na kuacha kufanya kazi inapokuwa ngumu?

“Afanana na merikebu za biashara, huleta chakula chake kutoka mbali, tena huamka kabla haujaisha usiku;” fungu la 14. Tabia ya uzalishaji mali, bidii ya kazi na utunzaji wa mali ni muhimu sana. Mtoto wa kike afundishwe bidii ya kazi za mikono, jinsi ya kutunza pesa, jinsi ya kufanya bajeti, jinsi ya kununua vitu sokoni au dukani. Kama kuna uwezekano alinganishe bei kadhaa au masoko tofauti kabala ya kununua. Afunzwe ubaya wa ubaradhifu au utumiaji mbaya wa vitu kwa kufuja. Ajue jinsi ya kununua chakula chenye lishe bali chenye bei nafuu. Afundishwe uchuuzi, kuona thamani ya kitu na kuweza kuzungumza apunguziwe kama inawezekana (bargain). Je, akinunua vitu kwa jumla, au vingi bei inakuwa ndogo au kubwa? Je, akipika chakula kingi akigawe mara mbili kwa kutumia siku moja, inasaidia matumizi ya pesa?

Mfundishe jinsi ya kununua , afanyeje ili aweze kuweka akiba? Afundishwe kufanya bustani ili kupunguza makali ya kununua kila kitu, hasa mboga. Je, anajua kutafuta nguo za mitumba zilizo nzuri na za kuzimachisa vizuri zipendeze, aidha kwake au kwa wadogo zake? Familia nyingi zinaingia gharama kwa burudani (recreation) ambazo ni ghali, je anajua burudani za kufaa na zisizo na gharama?

Niliona pale Dar es Salaam familia za wahindi wanaenda baharini kupunga upepo, na kula chips za mihogo au madafu kwa bei nzuri. Wakati familia nyingine zinaenda kwenye burudani ambazo ni ghali mno wakila kuku wa kukaanga kwenye hoteli kubwa

soda, pizza, icecream na vyakula vingine Ghali, na ambavyo siyo vya afya. Haya yote ni muhimu kuwafundisha watoto wetu.

Je, chakula kinachobakia anaweza kukitunza na kukitengeneza vizuri kifae? Mabaki ya mboga, na maharage machache, aweza kutengeneza supu na kuongeza vitu vingine. Je, wageni wakitokezea ghafla anajua jinsi ya kuongeza chakula kidogo kitoshe wengi? Afundishwe kufuga kuku wa mayai au ng'ombe wa maziwa kama kuna uwezekano. Msichana afundishwe kutunza chakula kwa wakati wa kiangazi.

Zamani makabila mengi yalikausha mboga za majani, viazi vitamu n.k. siku hizi hatufahamu haya. Wakati wa mvua tuna mboga nyingi, ila wakati wa kiangazi tunapata shida. Angalia kama ananunua visivyohitajika bila kufikiri. Je, anakubali matangazo ya biashara ya kununua vitu kirahisi? Je, yupo tayari kununua vitu ambavyo vimeshuka bei, au ana uvumilivu wa kungoja? Je, anajifunza kushona, kufuma na ustadi mwingine kupunguza matumizi? Je, ukimtuma sokoni, anaweza kulinganisha bei na kuleta vitu vya nafuu na vizuri. Je ukimwandikia orodha ya vitu vya kununua dukani, anavifuata, au ananunua usivyomtuma? Je, akiingia sokoni anajua tofauti kati ya vyakula vya lishe bora na vyakula visivyo na lishe (junk food)? Je, anaweza kufuata bajeti na kuitumia? Je, anaacha acha vitu vyake bila kujali viharibike?

Msichana afundishwe jinsi ya kutumia muda vizuri. Muda ni talanta ya ajabu, ambayo kila mtu amepewa. Mtoto afundishwe jinsi ya kumudu muda na kukomboa wakati ili aweze kumsaidia mume wake, watoto, jumuiya na kanisa. Mfundishe jinsi ya kupanga muda katika kufanya kazi za nyumbani. Mpe mradi wenye muda wa kumaliza (deadline). Tengeneza naye list ya mambo ambayo mnayoweza kumaliza kwa dakika tano, kumi na kumi na tano. Talanta ya muda ina thamani kubwa.

Atembee na kitabu anapokuwa anangojea basi, afume au afanye jambo fulani. Vitabu vya kumsaidia kimaisha (long life learning). Angalia jinsi muda ulivyoikuwa muhimu katika uumbaji kwenye Mwanzo moja. Tengezeni ratiba ya kutumia kwa siku nzima, mfano kuamka, kupiga mswaki na kuoga, kusoma Neno la Mungu. Mpatie muda awahoji watu wazima kwamba wangerudi nyumba ujanani ni nini wangefanya tofauti.

Je, majuto gani ya kupoteza muda au kutofanya jambo? Je, ni short cut gani zatakiwa ukipika, ukisafisha nyumba au ukishona? Je, ni jinsi gani mtu abajeti muda wake? Je, wafuatao walitumiaje mida yao kwa hekima? Daudi, Josiah? Kristo? Daniel, Miriam, Yusufu, Musa, Samueli. List shughuli ambazo zinafanyika kwa kipindi fulani tu katika maisha ya msichana mfano elimu, kuzaa watoto, ndoa, uzeeni. Mwulize kama anafanya yanayotakiwa kwa wakati wake.

Nunua daftari la kupanga muda na kalenda ya mwezi mirejee kila wiki. Jiulize kama anatumia muda wake vizuri kupanga maisha ya baadaye au ni kucheza na kupoteza muda. Je, anatumia muda kuwekeza kwenye umilele kwa kusoma Neno la Mungu na kuomba. Je, ana ratiba ya kila siku au anakaa na kuwaza ndoto za mchana. Je, muda wake wa mapumziko anatumia vizuri? Je, apoteza muda kwenye simu, tv na computer? Je, akipewa kazi anapoteza muda au anatunza muda? Je, anachukua muda mwingi kujirembesha? Je, analala, ana ratiba anayoifuata. Je, anawahi kanisani na shuleni au appointment nyingine? Je, anapenda kusema nitafanya kesho au kungoja kufanya mambo dakika ya mwisho? Je, anaweza kufanya shughuli mbili au tatu kwa wakati mmoja au akingojea maharage yaive, anakaa hapo hapo kisha ndiyo anainjika mboga? Je, angaalia njia za faida za kutumia muda wake kwa hekima?

Kama msichana na baadaye mama mwenye kushugulikia mume na watoto, ni vyema ajue kufua nguo, kujitunza kwa usafi katika mambo yote ya kike, kupika, kukomaa

na shughuli zote za nyumbani. Je, anaweza kugawa majukumu kwa wadogo zake, na hatimaye hata akiwa na msaidizi wa kazi aweza kumwambia cha kufanya bila kupoteza muda? Aangalie jinsi ufanyavyo kazi na kuzigawa kwa wengine wakusaidie. Angalia vifaa ambavyo unafanyia kazi na mwelimishe, naye aanze kununua pole pole anapopata visenti. Vifaa hivi ni kama cherehani, sindano, jembe, masufuria n.k.

Je, anajua kutumia cherehani, na hata kukarabati nguo zake? Je, anajua kutumia sindano, kukarabati nguo, kushona vifungo, au kufuma vitambaa. Je, anaweza kusoma pattern ya sweta, kitambaa cha kufuma, au nguo ya kushona?

Chukua pamoja na binti yako project fulani mfano kupamba ukumbi wa harusi na andikeni jinsi mtakavyofanya shughuli hatua kwa hatua na kuimaliza.

Angalia maisha ya Yusufu, Debora na Daniel. Je, Mungu aliwatayarishaje ili waweze kuwa watawala? Mungu anatayarisha wasichana wetu kuchukua majukumu ya kutunza familia zao na mengineyo. Angalia kama anamaliza shughuli unazompa. Je, aweza kuivunja project kubwa kwenye kazi ndogo ndogo na kuwapa wengine wamsaidie? (delegation), Je, anafundisha wadogo zake kwa uvumilivu?, Je, anapopewa kazi ya kusaidiana na wengine, anataka aifanye yeye mwenyewe? Je, anaweza kuelewa maelekezo ukimpa (directions). Je, aweza kukagua kazi ya wengine ambao wako chini yake? Je, anaongoza wengine kwa unyenyekevu au anawakandamiza na kuonyesha kwamba yeye ndiye bosi? Je, anasaidiana na wadogo zake kufanya kazi au anawatazama tu? Je, wengine wanapenda kufanya kazi naye au wanamuepa?

Mwanamke anaweza kupika milo 1000 kwa mwaka, wengi wanakumbuka vyakula vya mama zao. Ni muhimu tuwafundishe watoto wetu kupika vizuri. Tujifunze hata na mapishi mengine ya makabila tofauti na kupanga vya kupika, kutoka kwa vile tunavyolima na vile ambavyo ni rahisi kwa msimu ule. Je, anajua kiasi gani kila mtu katika familia anapaswa kula? Siku hizi za utandawazi aweza kupata mapishi toka sehemu mbali mbali kama vitabu, tovuti na mengineyo. Je, mwaweza na yeye mwandike kitabu chenu cha mapishi rahisi cha kutumia na kanisa lenu?

Wataalam wanasema kwamba mapishi yoyote yakiwa na zaidi ya vitu saba si mema kwa afya. Mfundishe kupika,si kwa vikolezo vingi ila kwa afya, kisha ladha na baadaye mwonekano. Kuna mapishi yayonachukua muda mfupi kupika, mengine yanachukua pesa chache. Ulizia marafiki, makanisani na ndugu mapishi mapya, na yakusanye muyaandike. Mwaweza kujitolea kanisa lenu kuwa na darasa la upishi kila mwezi mara moja kwa masaa matatu hivi.

Je,vifaa gani vyahitajika kwa pishi. Je, mwaweza kujifunza kupika mikate, kutengeneza jam au peanut butter? Angalieni magazeti ya upishi. Hoji wakina mama “Kwa nini wakati wa kula ni muhimu?” Je, anajua kuoka? Kukaanga? Kuchemsha? Je, anaweza kutumia vifaa vya jikoni kwa ustadi, usalama, na kuvitunza vizuri? Je, anaweza kufuata maelekezo ya mapishi (recipe) fulani? Je, anaweza kupikia watu wakiongezeka mara mbili? (Mfano ugali wa watu sita badala ya watatu). Je, aweza kupika kwa wakati na kutenga chakula mezani? Je, anajuaje chakula kimeiva? Je, anasafisha vyombo alivyotumia baada ya mapishi?

Je, mama akiumwa anaweza kumudu mambo yote mwenyewe? Je, anaweza kutengeneza chakula kitamu na cha kupendeza? Je, wale anaowapikia ni muhimu kuliko chakula anachotengeneza? Je, anapenda vyakula ghali vya mapambo mengi badala ya kubana matumizi na kupika vyakula vyenye lishe? Je, anaweza kubajeti chakula cha mwezi. Je, anakusanya mapishi mazuri na kujifunza yale yanayowezekana? Je, anajua kuwapikia watu wenye shida maalumu za afya kama kisukari, allergy, moyo au presha? Je,

anapenda kuendeleza talanta ya kupika na kuuza chakula? Kama mama je, upo tayari kumsaidia muanze genge dogo (restaurant)? Je, mambo gani ni muhimu yahusuyo chakula mbali na kwamba kina lishe nzuri na kina ladha tamu?

Mambo mengine ya kuangalia ni kupangilia mambo. Fungu la 15. Kupanga nyumba vizuri, kunaleta mawazo kutulia, na pia kunaakisi tabia ya Mungu ambaye ni wa mipango na uzuri (beauty). Tunaowaalika wanapenda waje zaidi kama nyumba zetu zina utulivu na mipangilio. Binti aliyejifunza kupanga vitu akiwa mdogo atakuwa msaada kwenye familia yake na hata atakapofanyia kazi.

Watu wengine wanazaliwa na talanta ya kupanga vitu vizuri, kama wanawake wa mashariki ya mbali, wanapangilia maua vizuri bila kutoka jasho sana; ila wengi wetu tunahitaji kufundishwa na kuhimizwa tena na tena. Kama wewe mama si mpangiliaji mzuri wa mambo, kama mimi, tafuta msaada kwa kusoma na kwa wengine.

Sheria ya kwanza mbinguni ni mpangilio (order). 1Kor:14:40 yasema kila kitu kifanyike kwa mipango. Mabinti wadogo wakicheza warudishe vitu vyao. Wajifunze kutandika vitanda vyao. Asubuhi mpange siku yenu na hata kuandika, mnavyotaka kufanya, la sivyo siku itaisha bila kufanya mengine. Jifunzeni jinsi ya kupangilia mipango yenu kwenye kalenda, au daftari. Wafundishe watoto kupanga vitabu vyao, picha, wanasesere, meza za kusomea, barua, kazi za shuleni, n.k. Wafundishe kupanga magoli, ya muda mrefu na mfupi.

Panga nao jiko, makabati yao, makabati ya vitabu. Pangeni pamoja na kuwafundisha jinsi ya kutoa kipaumbele (priority) katika mipango. Mkitaka kwenda mahali, kama safari pangeni pamoja, vitu vya kuchukua, ramani, kubook hoteli, simu zinazohitajika, tarehe za kwenda, mahali pa kupita, na vitu vya kufanya. Panga na mtoto ratiba ya siku ya kukaribisha wageni au karamu ndogo. Wekeni bajeti na jinsi ya kuifuata. Pangeni michezo, mapambo, na jinsi ya kupata pesa za kufanya hii karamu. Mkiweza someni vitabu vya Don Aslets “Clutter’s Last Stand” au “Clutter free”.

Tembeleeni nyumba za wanawake waliopanga vitu vizuri na kwa idhini yao tazameni jinsi wanavyopanga jiko, makabati, au sebule. Pangeni pamoja rekodi za nyumbani za afya, kama chanjo, huduma ya kwanza, na mihadi (appointments) ya kumwona daktari. Pia vyeti, kama vya kuzaliwa (birth certificate), ripoti zao za shule, viweke mahali maalum.

Chukueni faili jipya na kugawanya sehemu na kuandika namba za simu na address za watu, appointment za kalenda kama michezo/matukio, maelekezo kwa yaya, size za nguo za watoto wa nyumbani. Kila moja kwenye ukurasa wake. Weka hichi kitabu mahali mnapoweza kukipata na kukirejea (refer). Angalieni mahali nyumbani ambapo hapa mipangilio na kufanya pamoja baada ya kupanga la kufanya.

Mpe binti kazi ya kuweka picha vizuri na kuzilabel kwenye photo album. Pangeni pamoja risiti, marakaratasi ya bima au picha za kufundishia kanisani. saidiana na binti kupanga chumba chake na kukipamba kwa bei isiyokuwa kubwa. Soma www.Titus2.com wameandika kuhusu kumudu nyumba (managers of their home). Mwambie binti aandike insha ya “Thamani ya nyumba yenye mpangilio.”

Je, anaweka kila kitu kinapotakiwa, hata akivua nguo zake usiku haziachi kwenye sakafu? Je, anarundika vitu badala ya kupanga. Je kabati, pochi, begi la shule, lina mpangilio? Je, aweza kupanga mizigo yake vyema akienda likizo toka shuleni. Je, anavitupa tupa popote? Je, ana shida kupata vitu anapotafuta kama vile sindano, uzi, kazi ya shule au viatu vyake? Je, aweza kupanga mahali palipovurugika? Je, anaweza kutoa kipaumbele kipi aanze kufanya? Je, anapenda kukusanya vitu hata visivyo vya

maana “junk” na hataki kuviachia? Je, anaweza kutunza mihadi (appointments), anuani, na namba za simu bila kupoteza? Je, ni mtu wa mipangilio sana kichwani kiasi kwamba anapata hasira mipango ikibadilika? Je, unaweza ukamwachia nyumba ukaenda kwa siku moja? Je, anaandika mipango yake ya muda mrefu?

“Huangalia shamba, akalinunua, kwa mapato ya mikono yake hupada mizabibu;” fungu la 16. Fungu hili laonyesha mipangilio ya kununua vitu, kupangilia kutunza mbegu na kupanga jinsi shamba litakavyokuwa kwa mfumbo wa ufanisi na mazao bora. Hata kama ni mdogo, aweza kazi ndogo, kama -kuosha vyombo, kufua, kusafisha nyumba, kutunza wadogo zake, kwenda sokoni, kubadilisha nepi watoto. Kufanya kazi kutamsaidia kupanga mambo makubwa.

Wengi wanakazania shule, na hilo ni zuri, ila watoto wanasoma ili wapate kazi hatimaye. Kila anachofanya kina maana kwa Mfalme wa mbinguni kupata utukufu, na pia kinajenga tabia ambayo ndiyo pekee atakwenda nayo mbinguni.Tusidharau mianzo midogo, ndiyo inajenga watoto wetu kuwa mwanamke hodari na shujaa. Aanze kuweka magoli ya vikazi vya kufanya kabla ya kucheza. Mkatie kazi ndogo ndogo afanya na upange naye kadiri anavyozidi kukua.

Aweza kuanza kupanga magoli ya vitu vya kufanya vidogo vidogo hata vya ujasiliamali kama amefika miaka zaidi ya 14 hivi. Je, ana magoli gani ya kiroho siku za usoni kama kuonyesha upendo wa Mungu? Magoli ya mwanamke lazima yaendane na mume wake, jadilini kwa nini? Je, kuna kitu ambacho ni kigumu ambacho Mungu anataka ufanye katika maisha yako? Je, anapenda kumpendeza Mungu na kumpa utukufu na hilo ndiyo lengo lake kuangalia ya milele badala ya ya muda? Je, malengo yake ya baadaye yanaendana na maandiko ya Mungu au ni ya anasa? Je, ana mipango ya anayotaka kufanya kila siku, na magoli ya baadaye, na anayaandika? Je,anaafikiana na malengo yenu ya familia na kuwaunga mkono kihali na mali? Je, yupo tayari kukosa raha za muda akilenga magoli yake? (mfano kusomea mitihani, badala ya kucheza). Je, ana shauku ya kujifunza mambo mapya, na kutumia ustani huu? Je, anajua Yesu anakuja na ni muhimu kujitayarisha kwa tukio hilo kubwa kupita yote?

Twaona bustani inasaida mambo mengi katika maisha ya mwanamke. Kwa kawaida inabariki anayelima na wengine pia. Bustani inaweza ikaleta uzuri, mazoezi, na hata mahali pa mtu kupumzika na kubarizi. Bustani si lazima iwe kubwa, nimeona wengi marafiki wa mjini wameweza kuweka maua au nyanya kwenye makopo, wakala mpaka wakagawa. Furaha ya kupanda mbegu na kuona zinakua ni muhimu. Kila msichana ajifunze kupanda mboga, na maua pia! Apate mafunzo ya kulima bustani kwa ufanisi, maana ni huduma nzuri kwa wale wenye mahitaji.

Wengi tulio na bustani tumetoa mazao kwa watu ambao ni wahitaji, na kubarikiwa. Ni vyema binti aandike insha ya faida za kuwa na bustani. Je, anajua tofauti ya magugu na mimea? Ukiwa unafanya kazi bustanini unafanya naye? Je, anajua kutayarisha udongo kwa ajli ya kupanda na jinsi na mahali pa kupata maarifa ya kilimo? Je, anajua jinsi ya kukabiliana na wadudu waharibuo mazao? Je ,anauliza ushauri kwa watu wengine maarifa ya kilimo? Je umempa kipande chake cha bustani alime? Je, anaweza kupangilia jinsi ya kuendesha bustani, na kufanya hivyo kwa msimu mmoja?

Mwanamke huyu wa mithali anapofanya mipango ya kununua na kulima, anakuwa ni mjasiliamali na mwenye kujua jinsi ya kupanga matumizi ya pesa vyema. Kwa vile mabinti zetu watakuwa wakubwa na kuwa na majukumu ya kutunza pesa zao, za waume zao na kusaidia watoto katika mipango mbali mbali; kumfundisha mipangilio ya fedha ni muhimu (financial training). Mtoto afundishwe kugawa pesa zake apewapo, kutoa fungu

la kumi, na kuliweka kwenye bahasha au mahali tofauti. Kisha fungu la akiba, na fungu la matumizi. Ni vyema kusoma visa vya Marko 12: Mjane wa senti mbili; Mathayo 25 kwa mafundisho ya talanta na Luka 12 kuhusu tajiri aliyekuwa na mali nyingi.

Binti aulize watu mbali mbali, na hata wazazi kumsimulia mibaraka ya Mungu kwa wale waliorudisha zaka. Masomo ya tamaa ya pesa, kutumainia utajiri, kukopa na ubaradhifu wa pesa, ni muhimu. Mtoto afundishwe magoli ya fedha ya muda mfupi na muda mrefu. Je, atapataje pesa ya kununua kitu anachotaka? Wazazi wajadili, na kama kuna njia ya kumsaidia kufanya biashara ndogo ndogo, basi ni vyema kufanya hivi. Mtoto afundishwe kwamba kutoa ni bora kuliko kupokea, na Mungu hutubariki tunapotoa bila kunung'unika. Panapo nafasi mtoto afunguliwe akaunti.

Je, ni kanuni gani zitumike tunapokopa vitu? Je, aweza kulinganisha bei za vitu kabla ya kununua?Angalieni mifano ya Ibrahimu, Ayubu, Sulemani, Zakayo, Safira na Hezekia. Wekeni kumbukumbuku ya matumizi pamoja kwa mwezi. Fanyeni bajeti ya nguo kwa mwaka. Angalieni kanuni njema za kumkopesha mtu pesa. Awahoji wanawake wachache jinsi wanavyotunza pesa au kuweka akiba.

Je, kuna tofauti gani kati ya sadaka na zaka? Je, anatoa zaka na sadaka kwa ucheshi? Je, mke anawezaje kumsaidia mume wake kwa kuwa wakili mwema wa mali? Unapofanya bajeti ya nyumbani mshirikishe aone matumizi ya nyumbani ya kila mwezi. Ni yapi tunayotumia pesa kila mara tunayoweza kuyakata au kupunguza? Je, kuna uzuri gani wa mke kukaa nyumbani au kuwa na kibarua nje ya nyumbani? Je, anajua kwamba yote aliyo nayo amepewa na Baba wa mbinguni? Je, ana shukurani kwa Mungu aliyempa?

Je, anajua kuweka akiba au anatumia pesa bila kufikiri? Je, ni bahili au yupo tayari kukirimia wengine kwa vile alivyobarikiwa na Mungu? Je, anatumia pesa kwa fujo? Je, anapenda kukopa kopa, au kutumia zaidi ya alivyo navyo? Je, anapenda kutumia pesa kwa anasa za muda badala ya kutunza? Je, anaweza kubajeti kutokana na pesa alizo nazo?

"Hujifunga nguvu viunoni kama mshipi; hutia mikono yake kwa nguvu;" Fungu la `17. Kama vile mwanajeshi aendavyo vitani kwenye Waefeso 6:17, anavyokuwa, ndivyo tunavyotakiwa na mabinti zetu. Ili mabinti zetu waelewe neno vizuri twapasa kujifunza nao kwa mfumo na mpangilio ili waelewe mafundisho makuu ya imani (doctrines).

Kila mtoto awe na biblia yake na akifika miaka saba hivi apaswa kuwa na muda wake wa kusoma Biblia, japo kwa dakika kumi. Pengine itakuwa vyema apate Biblia yenye lugha rahisi kwa kuanzia. Tumekuwa tukitumia Clear word Bible au International Children Bible.. Ila hatuna Biblia za watoto za Kiswahili. Kwa sasa tumeanza kuandika Biblia ya watoto au hadithi za Biblia za watoto, tuombeeni ili tuweze kumaliza kazi hii.

Hatuwezi kumjua au kumpenda Mungu bila kusoma Neno lake. Na Uzima wa Milele ni kumjua Mungu, kumtegemea, kumtumiani na kutembea naye siku kwa siku; Yohana 17:3. Kuomba ni sisi tunazungumza na Mungu na kusoma Neno la Mungu, ni Mungu anazungumza na sisi.

Mama kama mzazi, lazima awe mfano. Je, watoto wanakuona unasoma Neno la Mungu kila siku? Mtoto aanze kuvikariri vitabu vya biblia 66 kwa mpangilio, au pengine kwa kutumia wimbo. Anakili vipande vya Neno la Mungu na kukariri. Kila siku mwaweza kusoma Mithali moja. Kusoma Neno la Mungu ni kitu cha kila siku, kama tunavyokula. Endapo tunaona tu busy sana, dawa ni kutokula chakula mpaka tumesoma Neno la Mungu. Tutajikuta tunasikia njaa na tutasoma. Mtoto anapojua kusoma tu, aanze kusoma

Neno la Mungu. Muwe na chati ya kusoma kila siku, pengine kurasa moja, kwa siku au sura moja kwa siku.

Someni historia jinsi Neno la Mungu lilivyotufikia na mambo machache ya Biblia; mfano lugha iliyotumika, vitabu vya torati, historia, mashairi, zaburi. ilichapishwa mara ya kwanza 1456 na mashine ya Gutenberg, imebadilisha maisha ya wengi, iliandikiwa kwa miaka 1700 na watu kama 40. ina sura 1189 si kitabu cha mashauri bora au mawazo mazuri tu bali ni sauti ya Mungu na mamlaka ya mwisho duniani na mbinguni!

Binti asome Biblia na kuweka jina lake mfano 1 Kor 13. Pale penye Neno upendo aweke kwanza jina la Mungu kisha asome mara ya pili na kuweka jina lake. Kariri ujumbe (theme) muhimu katika kila kitabu cha Biblia. Mpeleke binti ahudhurie masomo ya Biblia kanisani (Bible study). Someni pamoja Zaburi 119 na jadilini. Angalieni njia mbali mbali za kusoma Biblia na kuomba neema ya kutenda yaliyoandikwa. Mwandikishe binti kwenye masomo ya Biblia ya Posta au ya online, kama amazingdiscovery.org, na amazingfacts.org, secretunsealed au voiceofprophecy bible study. Akisoma fungu ni vyema aandike yafuatayo: Fungu hili linasema nini? Je, lina maana gani? Linawezaje kutumika maishani mwangu? Je, nifanyeje na hili fungu? Baada ya wiki aangalie kama kuna kilichobadilika kwa katika maisha yake kwa sababu ya lile fungu.

Je, anasoma Neno la Mungu kila siku bila kukumbushwa? Je, ana shauku ya kulisoma? Je, linabadilisha maisha yake na kuleta maana? Je, anaweza kutoa mifano, pale Neno la Mungu linaweza kutumika katika maisha yake? (application). Je, anauliza maswali akilisoma? Je, anashare na wengine? Je, anatafuta majibu kwa maswali yake kwenye Biblia? Je, anaweza akapata fungu kirahisi? Je, anajua angalau kwa mbali historia ya Biblia? Je, anajua jinsi ya kutumia mbinu za kusomea biblia kama kamusi, na marejeo mengine

Ni vyema mno kukariri Neno. Katika majaribu utamshinda mwovu kwa ahadi unazokumbuka tu! “Imeandikwa”. Neno la Mungu tukiliweka moyoni kwetu ndiyo silaha kubwa ya kutotenda uovu; Zaburi 119:10. Roho wa Mungu atatukumbusha pahali pa kutoa upanga kwa jaribu Fulani. Aanze kukariri fungu moja kila wiki. Watoto wadogo wana kumbukumbu nzuri, na kwa vile hawana mengi kichwani, itasaidia. Hakuna jambo linaloleta akili kupanuka na kuwa na wingi wa maarifa kama kukariri Neno la Mungu. Jadilini anapoendelea kukariri ili aelewe maana ya mafungu haya. sura za kuanzia kukariri ni kama Zaburi 23, au 91. 1Kor 13; Amri kumi za Mungu au hata kitabu cha waefeso cha mahusiano, ni kizuri sana. Waweza kurekodi vile alivyokariri. Ni vyema kuwa na daftari la kuandika yale mnayosoma. Je, anaweza kukariri mafungu 20?

Kumfundisha binti mazoea ya kuomba kila siku ni muhimu, kwa vile hata atakapokuwa mtu mzima atajua kumletea Mungu shida zake, na katika shida atakazokuwa na familia yake itamsaidia kutatua matatizo kwa maombi. Daima tufundishe wote tunaowashauri kumpa Mungu shida zao. Ombeni pamoja asubuhi na jioni, aombe mwenyewe pia. Jadilini pamoja sala kuu ya Bwana katika Mathayo sita. Kila mara anapojaribiwa kumzungumzia mtu vibaya, aombe. Awe na daftari dogo la kuandika anayoombea na tarehe. Itamsaidia kurudi na kumshukuru Mungu. Aombee wenye shida, serikali, familia, shule, wazee, kanisa, waliokata tamaa, wagonjwa. Ajifunze kuombea wanaomuudhi. Kumsifu Mungu, kuungama dhambi, kumshukuru Mungu na kuleta haja zenu iwe sehemu ya kila ombi.

Awahoji watu wa imani, wamishonari au wahubiri jinsi maombi yalivyofungua njia, au jinsi Mungu alivyojibu maombi yao. Je, wanawake gani walienda kwa Kristo kumwomba jambo fulani? Andikeni ahadi za Mungu na jinsi ya kuziomba? (zipo zaidi ya 3500). Aanze kuombea mume atakayemwoa japo ana miaka kumi na, tu.

Asome visa vya imani kama cha Hana, Musa, Sulemani, Nehemia au Daudi. Someni maisha ya Agustine, John Newton na wengine wanaoshukuru maombi ya mama Zao yaliyoleta tofauti katika maisha yao. Jifunzeni kanuni za maombi ya kufunga jinsi binti anavyokua. Je, anafumba macho akiomba? Je, maombi ni kitu halisi kwake, yaani mawasiliano halisi na Mungu au ni mapokeo tu? Je, anaomba uongozi wa Mungu kabla ya kufanya maamuzi? Je, anafikiri kuomba akiwa na shida? Je, anaonyesha kicho kwenye maombi, au anazungumza na kuchezacheza? Je, anaamini Mungu anajibu maombi? Je, unamwambia maombi yako yaliyojibiwa kupitia kwake? Je, anatoa shukurani kwenye maombi yake, au anaomba vitu wakati wote?

Ni vyema kuwafundisha mabinti zetu kutawala nafsi. Kukabili miili yao au hisia zao. Ni muhimu sana kujikana nafasi, kwenda kulala kwa wakati na kuamka kwa wakati. Kusoma Neno na kuomba mara baada ya kuamka. Kula kwa wakati na kujifunza kanuni nzuri za kutunza mwili (kupiga mswaki, kuchana nywele, kukata kucha, kuoga, kufua nguo) bila kukumbushwa.

Ajifunze kula akiwa na njaa, si kwa sababu hana kitu cha kufanya hivyo chakula kinakuwa rafiki. Asile mlo mpaka masaa manne au matano yapite. Uvivu, ulafi, kuvaa nguo zisizo na heshima, maisha ya uovu, marafiki wabaya ni mambo ya kuyakana.

Je, anasikiliza muziki wa aina gani? Aulize wengine wamwambie vitabia alivyo navyo ambavyo vinawachukiza wengine ili aviache kwa neema ya Mungu. Je, anajua chakula cha afya na kufanya mazoezi, au anakula chochote bora anakifurahia? Je, anajua Neno la Mungu lataka tuleje?

Asome maisha ya watu waliojikana nafsi ili kufanya mambo makuu katika maisha, mfano Daniel, Esta, Yusufu. Aandike insha ya 'Ulafi'.

Mkae mahali barabarani watu wanapopita muangalie watu. Je, wanavyotembea, macho yao, nguo zao au mtembeo wao unaleta mawasiliano fulani? Je, yupi atakuwa anajiamini, anajikana nafsi, au mvivu? Neno la Mungu linaitaje miili yetu? Soma hasara za kula mno au kula kidogo? Soma hasara za kula chakula kisicho na afya (junk food) au kile Mungu anasema tusile.

Kuna dhambi zinaathiri miili yetu kama vile hasira na zinginezo, zichambueni hizi. Soma sheria za afya na ulaji kwenye agano la kale kama toka wakati wa Nuhu kabla ya wayahudi. Angalia kama anajitahidi kuishi maisha ya afya,na usafi bila kukumbushwa, anapiga mswaki? Anafua nguo zake za ndani kila siku? Anaoga kila siku bila kukumbushwa? Je, anafanya mazoezi, na kujikana nafsi katika ulaji wake? Je, anajua kwamba mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu?

Je, mwonekano wake unaonyesha kujikana nafsi na kujiheshimu? Je, anatawala mwili wake ili asiwakere wengine? Je mara zote anaonekana amechoka? Je, mara nyingi ni mgonjwa? Je, anakaa kwa adabu? Je, kuna mambo ya kumsaidia ili awe na afya na nguvu? Je, anatabia za wasiwasi (nervous) kama vile kula kucha zake? Je, anajali anavyoonekana kwa watu? Je, anajali kupita kiasi mwonekano wake kwa watu?

Ni muhimu kuwafundisha mabinti zetu kupata ushauri unaofaa. Mungu ndiye mshauri mkubwa, ila ameweka watu pia watusaidie. Aweza kuwauliza wanawake watu wazima wacha Mungu. Atakapokuwa mtu mzima mara kadhaa atahitaji mashauri ya watu. Ni vyema kuwa wanyenyekevu kuuliza ushauri kuliko kuharibu mambo pale tunapokwama. Neno la Mungu katika Yakobo moja, lasema yoyote kati yetu asiye na hekima aulize, na Mungu atampa. Awaulize wazazi mahali ambapo katika maisha yenu mmeomba ushauri na kufanikiwa.

Kitabu cha Mithali ni kizuri kukisoma na kila mara asema “Mwanangu sikiliza mausia yangu....”. Je, atafutaje mshauri bora wa mambo ya kiroho, mambo ya nyumba, mambo ya jamii au mambo ya fedha? Tito 2 yasema wanawake wazee wawe washauri. Soma watu waliopokea ushauri mbaya au mzuri kwenye Neno Mungu.

Je, Hekima ni nini? Someni Efeso 5 :22-24 na kujadiliana: Kumtii mume kuna maana gani katika kupata ushauri wa wengine? Je, mke afanyeje mume wake anapompa ushauri usio na hekima kama Abigaili?

Nakumbuka ushauri alionipa mama yangu kabla ya kumaliza darasa la 12 alipoona watu wanakuja kuulizia posa au uchumba. Hata niliposoma kwenye seminari kwa vile nilikuwa msichana peke yangu, na hata chuoni kwenye kitivo cha kemia nilikuwa ni msichana pekee. Na huu ulikuwa ni umri wa watu kutafuta wasichana wa kuoa. Wavulana waliokuja mama alinishauri: “Unaona watu wanavyokuja wengi sasa angalia usiwe na majibu ya dharau au jeuri, hata kama sasa unasoma na hutaki kuolewa, wajibu vizuri na kwa heshima, hata wale unaofikiri hawastahili kwa vile wana tabia mbovu. Waambie wakupe muda kufikiria jambo hili, na baada ya siku chache waambie kwamba upo shuleni bado, au una mambo fulani ya kukamilisha hivyo waendelee tu kwani haitawezekana.” Akasema pengine baada ya miaka michache utakuwa umebadili mawazo, na kwa vile ulikuwa umewajibu kwa wema tu wanaweza kurudi na ukapata mtu mzuri wa kukuoa. Na hata isipokuwa wao, watakuzungumza vizuri kwa watu, na wale watu wataamini unajali watu.

Dunia inabadilika, leo wanataka kuoa, wewe hauko tayari, kesho utataka kuolewa nao watakuwa hawako tayari kwa sababu ya dharau au majibu yako. Kisha akasema si kazi ya msichana kumkimbiza mwanaume kama mke wa Potifa, wanaume wakufuate wewe, wale wanaokufuata ndio unamchagua mmoja kati ya hao. Ni aibu kumfuata fuata mwanamume, hata ukiwa unampenda, mwache akufuate. ingawa siku hizi wasichana ndo wanakazana sana kutafuta!'. Mwanaume aliumbwa ili atafute, na anajisikia vizuri akiona amempata, msichana au ametia bidii.. Zaidi ya yote, kuombea kupata mume bora hata zaidi ya mara tatu kwa siku ni muhimu maana hakuna ajuaye anayefaa. Wale walionekana wa kihasara, wamekuwa waume bora, na wale walioonekana wema, wamekuwa makatili kwa wake zao, moyo ni mdanganyifu, una magonjwa ya kuficha, ni nani aujuaye isipokuwa Mungu tu? Basi msichana ajue mume bora ni Bwana anayetoa, na si yeye kwa maarifa yake atampata.

Watu hubadilika, wale walioolewa na watu wa kufaa au ‘stable,’ wale watu walibadilika wakawa wabaya kwa wake zao, na wale tulifikiri walipata watu wasiofaa, wamebadilika. Mwenzi wa mtu aweza kufanya tabia yake ibadilike kwa kumpa nafasi ya kukua. Angalia zaidi kwenye Biblia wazazi walipotoa ushauri.

Je, binti anakufuata umpe ushauri kwenye mambo ya kawaida na nyeti? Je anakubali ushauri wako kuhusu marafiki zake au anabishana? Je, anafikiri mara zote yupo sawa? Je, anaomba ushauri wa mambo ya kiroho? Je, anatafuta kujua mapenzi ya Mungu kwa kusoma Neno lake? Je, anafurahia mashauri ya Mungu na wale wanaompenda Mungu, au anataka njia zake tu?

Kwa vile tuko katika jumuiya ya waumini, ni vyema tutiane nguvu na wale ambao tunaamini sawa. Tuwahusishe mabinti zetu na kanisa na kujadili mahuribi, na Neno la Mungu pamoja. Mabinti zetu waone thamani ya kusaidia shughuli za kanisa. Waweze kusaidiana na shemashi kusafisha kanisa. Wawashukuru walimu wao wanaowafundisha kanisani na viongozi. Kuna huduma nyingi kanisani, za kusaidia wenye mahitaji; mabinti zetu waweza kujumuika

Mabinti zetu wajifunze jinsi ya kukaa kwa utulivu kanisani na kutunza siku ya Bwana kwa mpango wa Biblia ulioagizwa. Je, wanawake wa Agano la kale na jipya walikuwa na sehemu gani katika kanisa?

Je,analalamika kwenda kanisani na kuepuka? Je, anatokatoka kanisani kwenda chooni au kunywa maji kila mara? Je anatumia yaliyofundishwa kanisani? Je anaomba akila tu, bali haombei maisha yake ? Je, marafiki zake wa karibu ni wa kanisani? Je, anafurahia kuwa katika nyumba ya Bwana? Je, anaweza kusema alichofundishwa leo? Je, anahudumia wengine na talanta alizopewa? Je, anasikiliza kwa makini? Je, anaombea mahitaji ya mwili wa Kristo? Je anajua karama zake za Roho? Je, anawapenda (admire) wanawake wa kanisa lake au viongozi au anawapenda watu wa dunia (celebrity)?

“Huona kama bidhaa yake ina faida; taa yake haizimiki usiku;” fungu la 18 . Mwanamke wa huyu ni mvumilivu, (perseverance). Kama wazazi tuepuke majaribu ya kuwakinga watoto wetu wasipate shida au mambo magumu. Watoto wasipate kuona toka kwetu kwamba Mungu anawatendea visivyo haki. Tuwasaidie wamrudie Mungu na Neno lake. Tusiwapunje watoto wetu nafasi ya kuona ukuu na uaminifu wa Mungu katika shida zao ili wakue na kusafishwa kuwa vito safi. Vitabu kama Pilgrims progress ni vizuri kuona hili. Wawaulize wazee wa imani uaminifu wa Mungu katika maisha yao. Waebrania 11 ni sura ya kusoma na kujadili watu hawa jinsi walivyotatua shida zao wakisaidiwa na Mungu. Tunapokuwa na wakati mgumu, ni nini kibaya kitatokea? Ni nani anashika hatamu za mambo yote? Kutii na kuamini kunasaidaje kuwajulisha wengine kwamba Mungu ndiye Mweza.

Soma maisha ya watu mashuhuri ambao hawakukata tamaa wakati wa dhiki kuu au kufeli. Someni zaburi, na magazeti kama 'Voice of matyr' kwenye computer ya watu waliokufa kwaajili ya imani siku za karibuni. Someni Isaya 53. Je, ni watu gani kwenye Biblia walistahimili mpaka mwisho? Je tunawezaje kushukuru kwa kila jambo? Jadilini ukuu na uwezo wa Mungu pamoja. Je kwanini Mungu anaruhusu majaribu na mateso? (1Petro). Je, ni kwa jinsi gani mke anaweza kuwa mvumilivu na mtiifu kwa mume ambaye ni mgumu kuishi naye? Je, Biblia inasemaje kuhusu talaka? Talaka na uvumilivu zinahusianaje?

Je, anakata tamaa haraka na hataki kujaribu tena kama alishindwa? Je, analalamika na kujihurumia kama mambo hayaendi anavyotaka au mtu amemkosea? Je, anaweka akili yake kwenye matatizo tu? Je, anaweza kutalawa hisia zake wakati wa shida au akiwa ana matatizo bila kuwa na chuki? Je, anajionyesha kwamba ni yeye tu mwenye matatizo duniani? Je, anapata faraja ya maandiko akijaribiwa au akiwa na shida? Je, anajihoji kwa dhambi zake akiwa na shida, ili aone pengine Bwana ataka kumrudi? Je,anajua kwamba Mungu anataka ajifunze katika shida zake? Je, anampa utukufu Mungu kwa jinsi anavyokabiliana na shida? Je,anamtumaini Mungu, na kuona majaribu yanamsaidia akomae?

”Hutia mikono yake katika kusokokota. Na mikono yake huishika pia. Huwakunjulia masikini mikono yake; naam huwanyoshea wahitaji mikono yake;” fungu la 19-20. Mungu ametukarimu na anatualika nasi tukarimu wale tusiwaowajua, na kuonyesha upendo kwao. Mwanamke anajifunza ukarimu kwao, anapokuwa mdogo. Nyumba inayokaribisha wale wanaohitaji faraja, ushirika, msaada, na upendo ni nyumba ya mfano bora. Mama ataleta hali ya furaha katika kushiriki kusaidia wengine. Wengi twaambiwa wamekaribisha malaika bila kujua (Waebrania 13).

Tufundishe watoto kuwa wakarimu, kwa kupeleka chakula kwa wagonjwa, kusaidia wenye mahitaji kama wazee na wagonjwa, kualika watu nyumbani mwetu. Wafundishe

watoto jinsi ya kumsalimu mgeni akija, kumtambulisha, kupokea mizigo yake, kuzungumza naye, kumhudumia chakula, na kumfanya ajisikie huru (ease). Jadilini, yeye kama mwenyeji afanye nini? Je, awezaje kusaidia familia kwa mgeni asiyetegemewa? Je, awezaje kusaidia watoto wa mgeni waliokuja kuwatembea na mama yao? Fikiria mtu ambaye mkienda kwake anawakaribisha kwa furaha na jaribu kumwiga.

Je, wageni wanaokuja kanisani awezaje kuwakaribisha wasikie wamependwa? Someni mifano ya waliokaribisha wageni kwenye Neno la Mungu. Je ni nani alikaribisha malaika? Angalia mifano ya Martha na Mary kwenye Liuka 10 na Yohana 12. Je, anaweza kupika chakula rahisi kwa upesi na kuwapa wageni? Je, anajua chakula wanachopenda watoto? Kwa wageni wanaolala, aweza kusaidia? Je, kuna tofauti gani kati ya mke na mume kwenye kukaribisha wageni? Je, anakaa na wageni au anajitenga

Je, yupo tayari wageni watumie vitu vyake? Je, anaingilia mazungumzo ya watu wazima kwa adabu? Je, anajitahidi kuanzisha mazungumzo na mgeni? Je anajaribu kuwa mkarimu kwa wageni hata wasio wa umri wake. Je, anasaidia wageni wajisikie wapo 'nyumbani"? Je, marafiki zake wakija anachukua jukumu la kuwakaribisha na kuwahudumia? Je!, ana adabu akikaa kwenye meza kuzungumza na wageni? Je, anawakirimu wageni wa kanisani na kuwasalimia? Je, anachukia wageni wakija kwa vile atakuwa na kazi nyingi? Je, anajua kwamba ukarimu wake ni jinsi ya kumhudumia Mungu? Je, anaona nyumba yao ni gurudumu la kufikia watu wamjue Mungu?

Kwa upande mwingine ajue jinsi ya kuwa mgeni bora, anapotembelea wengine. ucheshi, na kuwa na adabu pale alipo. Kuvaa nguo kwa heshima, hata kama ni wakati wa kwenda kulala. Jinsi ya kujibu watu au kufanya mambo kwa hekima. Mfano akisikia wenyeji wake wanagombana afanyeje? Shughuli gani aweza kumsaidia mwenyeji wake

Kuwa mwanamke mwenye rehema ni muhimu. Kusaidia masikini, kutia watu matumaini kiroho na kimwilli ni muhimu. Amhurumiaye Masikini, humkopesha Bwana, na Bwana hulipa bila kupunja. Watoto wa Mungu si mabahili bali hutoa. Mfundishe kutoa vitu vyake vya michezo, nguo zake n.k.

Pangeni jinsi ya kusaidia wajane, wagonjwa, vilema, wapweke, yatima, au wazee kanisani mwenu. Jinsi ya kuweka kando pesa za kusaidia wenye mahitaji; mfano walio jela, wamishonari, wanaotunza wagonjwa, wajawazito, watu wenye maradhi ya akili, watu waliodhulumiwa n.k. Je, mnaweza kuwasaidiaje? Je mafungu ganiya Neno la Mungu yatakuwa faraja kwao? Angalia www.persecution.com.

Soma vitabu vya injili na angalia jinsi Kristo alivyosaidia wenye mahitaji . Alisaidiaje masikini, wagonjwa, wajane au yatima. Soma gazeti au sikiliza taarifa ya habari na kuona mtasaidiaje waliopata maafa. Je, waweza kusaidia majirani zako ambao ni masikini bali hawatakiwi kupewa vitu bali ajira? Huruma au rehema in maana gani?
Je anaona watu wanapoteseka, au wanapokuwa na mahitaji? Je, ana huruma na mahitaji yao? Je, anapata huzuni na kuonyesha rehema kwa wahitaji? Je, anajua kusema maneno ya faraja kwa wale wenye maumivu? Je, anatoa muda na mali yake kwa kumpenda Mungu au atoa ili watu wamwone? Je, ana shauku ya kumfuata Kristo kwa kuhudumia watu? Je, anafurahi kuhudumu? Je, anajitoa kwenye huduma za kujitolea?

Twapasa kuhusika kwenye kusaidia mahitaji ya watu ya kiroho pia. Kama wanawake twahusika na haya kila siku. Tumeamriwa kwenda dunia yote na kuwaambia watu habari njema. Ni vyema aelewe kwa ufupi jinsi ya kutoa ushuhuda. Je, alikuwaje mkristo; n? Mungu amebadilishaje maisha yake. Ajue kisa cha msalaba hata kwa ufupi; kwamba wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu Warumi 3:23 na

6:23. Mshahara wa dhambi ni mauti, tunaokolewa kwa neema tu. Mungu anatupa neema tukiamini; ni lazima tuungame dhambi zetu na kuwa na toba ya kweli, tumwamini Kirsto kama Mwokozi wetu na tuna uhakika na Wokovu.

Je, aweza kumsimulia rafiki wokovu maana yake nini? Je, aweza kuomba na mtu na kumsaidia kuomba toba ya kwel? Aweza kuwa na klabu ya Bibia kwa watoto wa jirani? Watu walisaidia mahitaji ya kimwili ili kumsaidia mtu kiroho. Je, aweza kuchangisha pesa kwa mradiya kusaidia mahitaji ya kanisa,kama ujenzi?

Je, anaamini kuwa Yesu alikufa na kufufuka ili alipie dhambi zake? Je, amemkubali Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wake? Je, anaumia kwa wale wanaopotea bila kumjua Mungu? Je, anawaombea wasiomjua Mungu? Je, anajua mafungu ya kumwongoza mtu kumwamini Mungu? Je, anaona aibu kumkiri Kriso kwa wengine? Je, anapenda kumtii Mungu? Je, maisha yake yaendana na Neno? Je, anaombea watenda kazi wanaomtumikia Mungu na kuwatia moyo? Je, anatoa alicho kusupport kazi ya Mungu au anafikiria maisha hapa hapa tu?

Kuwa mtu wa haki ni moja wapo ya tabia ya mwanamke bora. Ni vyema ajue mambo yahusuyo sheria za nchi. Kupiga kura na kuheshimu viongozi. Ajue viongozi wanawekwa na Mungu na ni muhimu watende haki. Je, amchague nani anapopiga kura? Kuna ajenda nyingi mkristo anazopaswa kufikiria: Kama kutoa mimba, kuua wagonjwa (euthanasia), kuhukumu kunyonga, ushoga, ponografia, kutoza kodi, uasherati au uongo. Je, mtu anayempenda Mungu ahusikaje na hizi? Je, anapopiga kura ampigie kura viongozi anayeunga mkono haya? Je, kuna viongozi wanaompenda Mungu walioleta baraka kwa watu? Soma maisha ya Daniel, Nuhu, au Rehoboamu.

Je anajua viongozi wake, na anajua mamlaka yana maana gani? Je, anaweza kutoa hoja yake kupeleka kwenye uongozi wa ngazi za chini na hata juu? Je, anajua jinsi mswaada unavyokuwa sheria? Anajua mambo yanayoendelea nchini sasa hivi? Je, anaweza kugundua maneno ya yanayoposha ya “mawazo ya binadamu” kwenye vyombo vya habari? Je, anaonyesha heshima inayoakiwa kwa viongozi wa serikali, hata wale wanye ubinafi na uovu? Je, pale alipo anajitahidi kubadili sheria mbovu kwa kuzungumza na viongozi mahalia? Je, anahudumia majeruhi waliokosewa haki? Je, anajua kwamba mamlaka youte imewekwa na Mungu?

“ Hawahofii theluji watu wa nyumbani mwake, maana wote wa nyumbani mwake huvikwa nguo nyekundu;” fungu la 21.

Mwanamke hodari hujihami na wakati ujao. Ni vyema binti ajue simu za kupiga za dharura, kama vile ndugu wa kuomba msaada, polisi au zima moto. Yusufu alitayarisha Misri kwa wakati wa shida (Mwanzo 41). Nasi pia tuwafundishe watoto wetu kufanya hivyo. Tuwafundishe kujua cha kufanya moto ukianza kutokea, pa kukimbia na jinsi ya kusaidia wadogo zao. Ajue tochi, vibiriti au mishumaa vilipo.

Ukimwachia alee watoto wadogo, mfundshe vizuri jinsi ya kuwachunga na hatari zinazoweza kutokea na anavyoweza kuzikabili. Je, kuna majani au maua ya sumu karibu? Je, mtoto akinywa mafuta ya taa au akizama kwenye mto afanyeje? Mhoji mama ambaye amekutana na matatizo ya hatari za watoto nyumbani, alifanyeje? Mfundishe binti hatari za maji, umeme na gesi, na jinsi ya kuzima inavyotakikana.

Huduma ya kwanza ni muhimu; kila mtoto afundishwe kwa uwezo wa umri. Je, mtoto akiugua ghafla anajua cha kufanya, na mtu wa kumwuliza na kisha ampeleke mtoto hospitali? Je, sehemu mnayoishi ina hatari za aina gani, ni yapi mfanye mkiishi hapa? Je, anaweza kujua chakula kimeharibika na cha kutupa kisije kikasumisha watu? Je, mabaki ya chakula ni ya kutupa? Je, nyama, Mayai au samaki zinatunzwaje?

Je, mshikio wa sufuria hugeukia upande gani?, unapompa mtu kisu ushike upande gani? Je, anajua jinsi ya kutumia presha cooker kwa usalama? Mfundishe jinsi ya kutunza mboga kwa usalama, kwa kukausha au kuweka kwenye chupa. Ajifunze machache ya usalama kwa vyombo vya usafiri kama vile baiskeli, pikipiki au gari. Je, aweza kubadilisha matairi? Je, anajua jinsi ya kupata chanjo bila kudhurika? Mfanye utafiti wa pande zote.

Kitabu kama "Mahali pasipo na Daktari" ni kizuri, kuwa nacho. Ni wakati gani huduma ya kwanza ya nyumbani haisaiidii na lazima mtu apelekwe hospitalli? Jifunze na binti tiba mbadala na kukuza mimea ya tiba (herbs for medicine kama vile echinecia, tangawizi, vitunguu saumu) .Chukueni madarasa ya kuokoa mtu majini, kujilinda (self defence class). Jifunzeni usalama wa kuwa/kutokuwa na silaha mbali mbali nyumbani, kama mishale, rungu, mitego ya panya au sumu za panya au bunduki.

Je, anajua wakati wa tahadhari kama haupo? Je, anajua kuogelea? Je, anaweza kuwa na upeo wa kuona hatari inayokuja? Je, anakuwa mwangalifu ili asiwe hatari au kuumiza wengine? Mfano kuacha maji bila kudeki, kurusha vitu, n.k. Je, akiharibikiwa na chombo cha usafiri anaweza akawa msaada? Je, anajua jinsi ya kukabiliana na dharura ya nyumbani? Je, anashughulika na chakula kwa usafi na usalama? Je, anajua cha kufanya endapo tetemeko, au dhoruba ikitokea? Anaweza akatumia vyombo vya kazi kwa usalama? Je, anajua kujikinga na maradhi? Je, anajua kujikinga na mtu anayetaka kumpiga? (self defence moves), Je, anamtumaini Mungu kama kinga yake kuu na mpaji?

"Hujifanyia mazulia ya urembo, mavazi yake ni kitani safi na urujuani;" fungu la 22.

Mwanamke anayemcha Mungu anapenda vitu vya kupendeza pia, anajitahidi ashone na kujua ustadi fulani. Anajitahidi katika kuvaa vizuri hata nyumbani, asiwe kama yule anayekimbiza ndege shambani, avaaye vizuri akitoka nje ya nyumba. Ajifunze kutandika kitanda chake na kuacha chumba chake katika hali nzuri akiamka. Chumba kinabadilika kabisa, kwa kutandika tu kitanda! Aweza kusaidia kufuma vitambaa vya viti na meza. Kupanda maua na kuweka nyumbani, kusaidia ndugu zake kushona vifungo. Mungu ametuumba tupende ustadi na nakshi. Mfundishe kushona, kukarabati nguo , kama huwezi mtafute mtu amsaidie. Ajifunze kuweka zipu, kushona begi, kushona kitambaa cha mkononi, nguo ya mtoto, sketi, apron. Mwaweza hata kushona na kusaidia wenye mahitaji. Kuhudhuria madarasa ya ushonaji, upambaji, ufumaji kupata maarifa zaidi. Kina mama waweza kufundisha haya kwa wasichana kwenye nyumba za ibada au jumuiya. Vitabu kama "Simple secrets to a beautiful Home;" by Emilie. Barnes, ni vyema kuwapa wasichana wetu wavisoma

Je, chumba chake kina mpangilio? Je, anajaribu kukifanya chumba chake kuwa safi na maridadi? Je, meza, viti , nguo na matandiko yake yamekaa sawa? Je, anachukua muda kujifunza kupamba, kwa maua na vitu rahisi chumba, nyumba au hata kushirikiana na wengine kulipamba kanisa la Mungu? Je, mapambo yake ya kuta ni ya picha za watu wa dunia na celebrity na magazeti ya watu wa anasa, au ni mambo ya kumsaidia?

Yaonekana mwanamke huyu anavaa kitani na zambarau, hizi ni nguo za kifalme, ni binti wa mfalme huyu! Nafikiri kama tuna uwezo tuwe na nguo chache nzuri, na pia kusaidia wenye mahitaji. Kuwa mtoto wa mfalme ni pamoja na tabia ya kifalme. Mabinti zetu wajifunze tabia za adabu na upole za kifalme. Kusema asante, tafadhali, samahani, pole ni maneno ya dhahabu au kifalme. Wajue jinsi ya kuwa watulivu kanisani na kwingineko; na si kupayuka payuka na kuongea kwa sauti ya juu, au kubishana. Wajue jinsi ya kumwita mtu au kuzungumza na mtu. Wajue sheria (rules) wanapotembelea watu wengine. Gary na Cathy Maldaner wameandika kitabu "Visiting other families in polite

moments". Jaribu kuona ni mambo gani ya kufundisha watoto wajue mnapotembelea mtu (ugenini).

Je, mnapoenda kwenye hoteli au mgahawa mfanyeje (polite manners). Jinsi ya kuserve chakula, jinsi ya kuomba menu, kutumia kijiko au uma, au napkin (karatasi ya kujifuta mdomo). Andikeni sheria hizi mahali na kujifunza pamoja. Mfano ni nani anaanza kuserve chakula mkiwa wageni mahali? Vitabu kama Manners made easy by June Hines Moore ni msaada.

Jinsi ya kujibu simu, na kujitambulisha unapokutana na watu. Jinsi ya kumsifia mtu au kumtia moyo (compliment/praise), jinsi ya kumlaki mgeni mlangoni mwako, jinsi ya kushukuru ukisifiwa, jinsi ya kushukuru ukimaliza ukaribisho, jinsi ya kupenga makamasi, kupiga chafya au kukohoa mbele ya watu. Jinsi ya kutoa hudhuru ukienda chooni, jinsi ya kupanga meza na kupakua watu wale, jinsi ya kufanya mtu akusikilize anayefanya kazi Fulani (interrupting). Jinsi ya kuwa mgeni bora ukialikwa mahali, jinsi ya kutokuwa mchoyo na kutojifikiria, au jinsi ya kuandika shukurani kwa waliokualika ukirudi.

Je, msichana ajifunzeje jinsi ya kufanya mambo kwa tanashati (a girls guide to etiquette)? Someni vitabu vya injili, Je, unajifunza nini kuhusu Kristo kama mgeni, rafiki, mwalimu. Aliwasalimuje watu, alizungumzaje nao, aliaganaje nao, Soma jinsi Nabali 1Sam 25 na Hanuni 2 Sam 10; walivyokuwa na adabu mbaya. Je, wafilipi 2:2-4 inatusaidiaje kuhusu mahusiano na watu?

Andika list ya vile vitu vinavyowasinya watu (annoy) au ambavyo havionyeshi tabia njema (bad manners). Andika jinsi binti anaweza akabadili tabia hizi mbovu. Andika watu ambao ungependa kuwa nao, angalia tabia zao, Je, wana tabia gani za kiungwana (polite habits)? Je, wanaheshimu wengine kuliko wenyewe, linganisha na tabia yako. Angalia mfano wa mwanamke mwenye tabia njema muulize anafanyaje haya (graciousness and good manners/etiquette). Je, tunda la roho linahusikaje na tabia zetu Gal 5:22-23.

Alika mgeni kisha panga binti apange meza, aweke maua , apike na kuwa mwenyeji (gracious hostess). Angalia kwenye Neno la Mungu wale walioonyesha tabia njema, walifanya nini? Je, wapi biblia yatuambia tuwe na upole na utu wema (politeness/kindness); kama kujali wazee au kuhudumu wengine kabla yetu. Je, kwa nini si vizuri kuzungumza ukitafuna chakula mdomoni?

Je, anawafanyia wengine vile anavyopenda kufanyiwa? Je, ana tabia njema akiwa mezani (manners), Je, anazungumza kwa kujali watu (politely)? Je,anajua kutoa udhuru anapotakiwa, Je, anapenda watu na ana tabia njema (good etiquette) akifuata sheria zake kwa unyenyekevu na upendo kwa wengine. Je, wengine wapenda kuwa kuzungumza naye au kumtembelea? Je, mara nyingi unapata aibu ukiwa na wageni wako kwa tabia au jinsi anavyozungumza na watu? Je, anaonyesha adabu kwa wazee? Je, anajua kutoa shukurani, na anaheshimu vitu vya watu?

Ni vyema kuwafundisha watoto kuwa na kiasi. Tuwafundishe kwamba wanavyovaa au kuzungumza waweza kukwaza watu. Tuwaambie jukumu lao kuwa na hekima katika kuvaa, na kuzungumza na watu. Lazima wajue wao ni watoto wa Mfalme, na kufundishwa tangia wakiwa wadogo. Tuwavalishe kwa style zinazofaa toka udogoni.

Mara nyingi watoto wa kike wadogo wanavalishwa nguo za wazi, kama vikaputura vifupi, na mtoto akifika miaka 12 tunaanza kumwambia hiyo haifai na ameivaa toka udogo! Watoto wadogo ni vizuri wavalishwe kaptura wakiwa na magauni, maana

wakicheza nguo za ndani (chupi) zaonekana. Mtoto asitembee amefunga kanga iliyoacha mabega siku nzima, bali aongeze na nyingine ya kufunika mabega/kifua.

Tuwafundishe pia kuwa wanyenyekevu wenye kiasi, na wasiojisikia kwamba wao ndiyo muhimu kuliko wengine. 1Tim 2;9, yaeleza mwanamke anayempenda Mungu. Je,mavazi gani au fashion ambazo hazina kiasi? Lazima kuwe na jinsi ya kuvaa (dress code). Je, wanavaa suruali (trousers) za aina gani? Je, zinabana hasa kwenye sehemu za siri? Je, nguo zinaonyesha kifua na matiti? Je, magauni yako juu ya magoti? Mwambie binti azungumze na baba yake kuhusu nguo ambazo hazileti majaribu kwa vijana wa kiume au hata wanaume watu wazima.

Chukueni Catalog ya nguo za wanawake zenye picha na kuijadili. Kaeni mahali na kuona watu wanaopita na kujadili nguo ipi ni ya kiasi na ipi haina adabu (immodest). Je, unapima nguo hizi kutokana na kiwango gani? Andikeni sheria ya nguo za msichana anayemwakilisha Mungu, na jinsi ya kutengeneza nywele, kucha au uso kwa kumwakilisha Mungu. Je, mwonekano wa nje unajalisha au bora mioyo yetu ni safi hivyo inatosha? Ni kwa nini Mungu alitupa nguo bustanini mwa Edeni? Kwa nini hakuwaachia wakae na majani yale ya mikuyu waliojitengenezea yaliyowafunika kidogo tu na kuacha utupu mwingine? Kama Mungu alitupa nguo, ya kufunika mwili na si majani, hii ina maana gani kwetu?

Angalia fasheni ya nguo ya nchi mbali mbali, kisha angalieni miaka 50 hata mia ya nyuma watu walivyovaa. Je, hizi fasheni zinawakilisha maadili na utamaduni wa watu hao? Binti ajadili na wazazi kwamba goli lake ni lipi katika uvaaji wake? Anavaa kumpendeza Mungu au wanadamu; na anataka watu wamwone au amletee Mungu utukufu?

Nchi nyingi siku hizi wana sehemu ambazo familia yote inaenda bila nguo kabisa (nude beaches, or recreation); kwa nini hili ni kosa? Kwa nini Nuhu alimlaani mwana wake aliyemwona uchi? Wakati Kristo yupo duniani watu walivaaje? Je, uchi ni nini?Je! Ni kutokuwa na nguo kabisa au kuvaa nusu nusu, sehemu zingine zikiwa wazi?.

Neno la Mungu liko wazi kuhusu sehemu za mwili za kuacha wazi na za kufunika. Mwambie binti aende na baba yake kununua nguo zake, na baba atoe mawazo kwenye uchaguzi, kisha aseme kwa nini amechagua nguo hiyo. Mwambie baba yake naye waangalie nguo zake kabatini na wazithathmini na kutoa sababu kwanini zinafaa au hazifai.

Soma mwanamke mgeni kama wa Mithali saba. Je, anafanya nini kuwavuta wanaume? Linganisha wanawake wawili wa ufunuo, yule aliyevikwa jua na mwezi na yule aliyedanganya mataifa. Tofauti yao ni nini? Wanaume wa namna gani waenda kwa wanawake wageni? Mwulize baba amweleze binti jinsi vijana wa kiume wanavyoona mwanamke akiwa na nguo imebana, au inaacha sehemu nyeti za mwili (flirtatious). Someni kitabu “For Young women only;” kilichoandikwa na Shaunti Feldhahn na jadilini wote nyumbani mwenu.

Someni Mathayo 5:27-28. binti anapovaa afikiri kuhusu wanaume watakaomwangalia na yale watakayofikiri. Fikiria mwanamke mwenye adabu na roho ya kicho (modesty in spirit and dress).Angalia tabia yake, matendo, na jinsi anavyozungumza na wanaume, au anavyovaa. Soma wanawake wasio na kicho na jinsi walivyovaa. Walifanya nini?, matokeo yake yalikuwaje? Je, kutovaa vizuri kwawezaje kuwa kukosa uaminifu kwa yule utakayeolewa naye? Je, inasaidiaje wavulana wengine

kukosa uaminifu kwa wake zao watakaoa? Mtayarishe binti kwa uchumba atakapofikia miaka kama 18 hivi. Jadilini Jinsi ya kutokuwa mtu wa 'sheria' (legalistic) na uvaaji kwa adabu kikawa kimungu chetu.

Yasemekana wanaume wanajaribiwa kumtamani mwanamke na mwanamke anajaribiwa kumjaribu mwanamume amtamani. Jadilini hili. (Man is tempted to lust after a woman, and a woman lusts to be lusted after).

Je, anapenda ampendeze Mungu kwa uvaaji wake au anapenda ajiletee utukufu na watu wamwangalie? Je!, anapokea mashauri kwenye uvaaji au anajivalia chochote kinachomfurahisha? Je, anajua jinsi macho ya wanaume yanavyotazama mavazi na wanavyofikiri wanapoona mwanamke amevaa kwa namna fulani? Je, anawalinda wanaume wasiwe na mawazo ya dhambi kwa uvaaji wake? Je, anavaa nguo zinazomfunika au anapenda kujionyesha mwili wake? (expose body

Je, anavaa kama msichana au anapenda avae kama mvulana? Je, anapenda kutongoza wanaume kwa uvaaji wake, tabia na maneno? Je, anazidisha kuvaa kwa adabu mpaka anaonekana vibaya na kama si msichana? (overdo modesty). Je, ana kiburi kwamba anavaa kwa adabu na anamjaji kila mtu anayevaa vibaya? Je, anakuwa mtu wa sheria 'legalistic' kwenye uvaaji wake, akishikilia mambo ya nje, bali ndani ya moyo wake kuna roho ya uasi? Je anaweka sheria zake za uvaaji mzuri kwa wengine? (impose legalistic starndards of dress o others).

"Mume wake hujulikana malangoni, aketipo pamoja na wazee wa nchi;" fungu la 23. Huyu mwanamume anayeheshimiwa malangoni, lazima awe anaheshimiwa nyumbani pia. Mithali 12:4. Mwanamke mwenye hekima anayemheshimu, anamsaidia mume kukomaa na kukua katika uongozi na kuchukua majukumu.

Kumheshimu mume, kunaanza msichana akiwa mdogo, kwa kumheshimu baba yake. Kutona tona (nagging) ni tabia ya kuepuka. Lazima ajifunze kuheshimu, na kuona baba na mama yake ni mamlaka yaliyowekwa na Mungu katika maisha yake. Ajifunze kuitika kwa adabu anapoitwa na baba yake, amsaidie baba yake kumpokea mlangoni, kuchukua koti lake, kumpikia chakula chake na kumtengea. Ajifunze kumshukuru baba yake, na kujua vile vitu vinavyomfurahisha, kama vile gazeti, muziki, au vitabu. Andika orodha ya vile vinavyomchukiza na kumpendeza baba yako.

Someni kitabu cha Mithali na kuona uhusiano katika ya mzazi na mtoto. Pia someni Efeso 5:33.

Je, ni kitu gani kinaonyesha heshima kwa baba yako? Je,mama anamweheshimuje baba? Hapa sisi wanawake lazima tujitahidi ili watoto wetu waone. Je, tunawasaidiaje waume zetu kama wasaidizi? Je, anawezaje kuonyesha heshima kwa babu yake au kaka zake? Je, mwaweza kuandika list ya vitu vinavyoonyesha kukosa adabu? Kama binti ana shida ya kuheshimu wazazi aandike sababu za kutowaheshimu, na kuona Biblia inasemaje kuhusu hizi sababu.

Soma yahusuyo mke wa Ayubu, Mikali, na Vashti, walikosaje heshima kwa waume zao? Soma Sara, na Esta waliheshimuje waume zao? Chunguza watoto au wanawake wanaokosa heshima kwa waume au wazazi wao. Je, watoto wanapata mfano gani kutoka kwa wanawake wanaokosa adabu kwa waume zao? Je, mamlaka ya mwanamume yanakuaje katika nyumba hii? Je, mamlaka ya Mungu yanakuwaje katika nyumba hii?

Binti ajadili na baba yake umuhimu wa kumheshimu mume. Je, mfanyakazi, raia, mtoto au mke afanyeje endapo mamlaka haijiheshimu? (unworthy of respect). Je, yuko huru kutiii mamlaka, hata inapofanya dhambi?

Je, anazungumza kwako na kwa baba yake kwa adabu? Je, anazungumza kwa maneno ya adabu kwa wazazi na kwa mamlaka? Je, unapozungumza naye au kumwita anaitikia na kugeuza uso wake akusikilize? Je, uso wake na mwonekano anaonyesha anatii? (expressions, gestures, and posture). Je, anakuheshimu mbele ya watu na hata mkiwa peke yenu? Je, anasema madhaifu yako mbele ya watu wengine? Je, anakukosoa mbele ya watu? Je, anaheshimu watu wazima polisi na viongozi wa serikali? Je, anajitahidi akupendeze? Je, anakuona wewe kama mamlaka ambayo Mungu amemwekea katika maisha yake? Je, anaheshimu maoni yako? Je, anajua jinsi ya kukueleza pale anapotofautiana nawe? Je, anakukosea adabu na kuonyesha kwamba anaona aibu wewe kuwa mzazi wake? Je, anapenda kukukebehi au kukucheka mbele ya watu?

Kumsupport mume ni muhimu sana, hebu wasichana wafundishwe. Hii inafanya waume zetu kufanya shughuli yao ya uongozi waliyopewa na Mungu kwa ubora zaidi. Mwanamke ni msaidizi, wa mume wake, anapaswa kumtii na kutumia muda na uwezo wake kumheshimu mume wake. Akifanya hivi vyema aweza kuwa taji kwa mume wake. Pengine inabidi aweke kando matakwa yao ili kuwahudumia waume zao, na hili wajifunza wakiwa wadogo.

Pengine wanawake wengine hawafikiri hili, kwa vile wameolewa na wanaume wasiomcha Mungu, ila hata hao wanahitaji kuheshimiwa; Math 20:28. Hata mwana wa Adamu alikuja kutumikia watu. Hebu ajue jinsi ya kutumikia wadogo zake, dada au kaka zake. Amuulize mama yake au mama wengine kwamba “Magoli yako leo ni nini?” Ataona magoli ya mama wengi ni ya kuhudumu, na kutumikia nyumba zao.

Ajifunze jinsi ya kupendeza kaka zake, au dada zake kwa siku moja. Awaombee wazazi wake. Jadilini njia za kumsupport baba kwenye shughuli zake. Je, anajua kuacha anayopenda (interest) ili kusaidia wengine? Amwangalie mama yake aone anayofanya kumsupport baba yake. Msichana amhoji baba yake ni kwa njia ipi mama alimtia moyo katika mwito wake aliopewa na Mungu. Je, amemsaidiaje katika maisha yake? Angalia jinsi mabinti wanaowasaidia baba zao. Wahoji wanaume wawili jinsi wake zao walivyowasaidia kufanikiwa kimaisha? Ni jinsi gani wamewatia moyo kukomaa katika shughuli zao za uongozi?

Soma maisha ya watu mashuhuri na viongozi wa historia na nafasi ambayo wake, au mama zao walichukua kusaidia haya? 1Tim 3:1-13.

Je, mwanamke ana jukumu kumsaidia mume wake kwa namna gani? 1Tim3 na Tito 1 zinaonyesha kwamba mwanamume anahitaji mke kumsaidia kwa mambo mengi. Angalia mfano wa Yesu kama mtumishi, alitumikiaje watu?

Angalia wanawake kwenye Biblia kama Sarah na Priscscilla walivyosaidia waume zao? Soma maisha ya wake kama wa Lutu, Haman, Yezebeli au Herodias; Je, walisaidiaje waume zao? Angalia familia ambayo mke hataki kumsaidia mume wake, je, matokeo ni nini? Je, kwa wale wake wanaotaka kuwa na taaluma na kuiendeleza badala ya kusupport waume wao, jiulize jinsi itakavyowasaidia watoto au waume zao.

Je, familia yawezaje kufanya dhambi kama timu? Je, mke anawezaje kuwa msaada kwa mume wake kwa maneno yake, kwa kumsifia yale mema yake, kwa kuwa mnyenyekevu na kuwa mwenye heshima, au kuwa maombi? Andikeni njia 15 za kumheshimu mume. Je, Jukumu lako kama mke lawezaje kuwa kama kanisa, msaidizi wa Kristo kwa mume wako?

Fungu la 24 latuonyesha ujasiliamali ambao mabinti zetu wanatakiwa wajifunze. Tufundishe mabinti zetu jinsi wanavyoweza kujiajiri wenyewe majumbani ili kuwa na kipato na ustadi. Baba au mama waweza kubuni mradi wa kusaidia, pengine kuuza vitu vidogo vidogo kama maji, vitu vya kushona au vya kupika. Kama kuna kazi anazoweza kuzifanya na kulipwa afanye vile.

Wanawake kama wale wa Matendo 16-15 wanatuonyesha kwamba wanaweza kuuza vitu vya nakshi. Jadilini faida za mwanamke kuwa na kazi za kumletea kipato nyumbani badala ya kufanya kazi nje ya nyumba. Jifunzeni yahusuyo leseni ya biashara na kodi ya serikali. Hoji wanawake wenye biashara zao, Je, wanafanya nini? Fikiria biashara inayohitaji mtaji mdogo na muanze. Je mwanamke atumiaje mapato yake anayopata kwenye kazi zake?

Je akifanya kazi ina ubora? Je anapenda Mungu afurahi na kazi yake? Je, anaongeza ustadi wa ufundi alio nao? Je, ana ustadi wa kumwezesha kupata kipato? Je, wengine wanajua ni mfanyakazi bora? Je, watu wanapenda bidhaa zake au ustadi wake? Je, ana mbinu za ujasiliamali? Je, anapenda kufanya kazi nje na nyumbani? Je, akiona hitaji anajaribu kulitatua? Je, anapenda apate pesa kwa mahitaji yake binafsi tu au kusaidia familia na wengine pia?

"Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake, anaucheka wakati ujao;" fungu la 25. Mwanamke huyu anajua maisha ya imani, kuridhika na kumshukuru Mungu. Anajua Mungu ameshika hatamu ya wakati ujao. Twahitaji kuwasaidia mabinti kuridhika na yale ambayo Mungu, na sisi wazazi tumewapa. Twaweza kujadili na kuandika pamoja yale ambayo tunashukuru kwayo. Je, anawashukuru wazazi wake kwa yapi? Kuna tofauti gani kati ya kuomba na kushukuru? Filipi 4:6-7 na 1 Thes 5:16-18. Je, wivu, chuki,

Soma watu ambao hawakuridhika kwenye Biblia. Kila mara unapojaribiwa kulalamika, soma Wafilipi 2 na Isaya 53. Je, binti ya Mfalme anapaswa kuishi maisha ya kutoridhika? Zungumza na mwanamke mtu mzima kuhusu kuridhika. Jadili neno kutamani (covet) lina maana gani? Andikeni orodha ya vitu ambayo hamridhiki navyo (discontent); kwa mwonekano wako, unapoishi, familia yako, kisha andika shina la kutoridhika na hivi vitu kwenye moyo wako. Kisha ungama kwa Mungu. Angalia Waebrania 11, na jinsi kila mtu aliyeandikwa alivyoridhika.

Je, anamshukuru Mungu kwa anayompa? Je anadai kununuliwa vitu mkiwa dukani? Je, anajali kama mwingine atapata sehemu kubwa kuliko yeye? Je, anataka kuwa na vitu vile anaona wengine wanavyo? Je, anaweza aishi maisha magumu na kuona mafundisho Mungu anampa?

Je, anamtegemea Mungu kama mtoaji? Je, anakazania mambo ya kupita au ya milele? Je, anaridhika na alivyonavyo au anataka zaidi? Je, ana roho ya shukurani kwa wazazi na upendo wenu? Je, anatoa shukurani kwa huduma au anavyofanyiwa? Je, anapenda kulalamika na kulialia? Je, anajitahidi na wengine kupata anachotaka? Je, anapenda kutetea haki zake mara zote? Je, anajihurumia kupita kiasi; (self pity)? Je, anatamani vitu vya wengine na kupata wivu? Je, anatamani talanta au kufanikiwa kwa wengine? Je, anatamani baraka za wengine na zinamtia uchungu?

Mungu hutoa mahitaji yetu sasa na ya wakati ujao. Ni nani alimpa Adamu mke wake? Je, Mungu ataka tuwe watu wa namna gani? Mika 6:6-8. Angalia wanawake wote waliosaidia kazi Yesu au mahitaji yake, wangapi walikuwa hawajaolewa? Wajue wanawake ambao hawajaolewa kwenye ushirika wao na kuwatembelea. Je, binti anaweza

kuifanya miaka ya kutoolewa iwe bora (shule, kusoma Bibia, huduma, kukariri mafungu, ustadi). Je! Anajua dhambi iliyoingia ya wanawake kuolewa na wanawake na wanaume kuolewa na wanaume? Jadili naye.

Biblia yataja watu kama vile Miriamu, Rahabu, Delila, Mariamu, Martha, Esta, Ana, mjane wa Serepta, binti za Zelofehadi. Je, kutoolewa kwao kuliwasaidiaje kutumika walivyotumika? Je, Mungu aliwasaidiaje kupata riziki? Makosa gani walifanya? Na adhabu gani waliyoipata? 1 Kor 7:34-35.

Andika jinsi ambavyo mwanamke asiyeolewa na asiyekuwa na jukumu la kumpendeza mume anaweza kuhudumu kwa ufanisi mkubwa. Angalia jinsi uhuru wake unavyoweza kumsaidia kuwa wa huduma kwa kazi ya Mungu. Ni mambo gani ambayo waweza kusaidia kanisa sasa ikiwa haujaolewa? Je, ukiitwa na Mungu kutoolewa (single) waweza kumtumaini Yeye?

Zungumza na wazazi kuhusu kuitwa kumtumikia Mungu pasipo kuolewa. Kwa nini Mungu, wakati mwingine huita watu ambao hawajaolewa? Je, watu hawa wanajisaidiaje kupata riziki? Je, usipoolewa utaishi kwenye mji wako mwenyewe? Je, ni wapi utaomba ushauri ukiwa mwenyewe (single)? Soma Biblia inapozungumzia: “Mwito wa kuishi maisha ya usela/solemba; (single). Soma kitabu; ‘Did I Kiss Marriage Goodbye;’ cha Caroly MCCulley. Je, maisha ya kuishi mwenyewe yanaweza kuwa bora na kamili? Jadilini kuhusu upweke.

Je, anamtumaini Mungu kwa kila jambo na anaridhika (fulfillment) na uhusiano wake na Mungu? Je, anajua adui anakuja kwa njia nyingi zaidi ya ile ya kutenda dhambi? Kukata tamaa, unafiki, marafiki wabaya, kuchoka; n.k. Je, amejitoa kwa Mungu kutumikia wengine, na anatumia nafasi hiyo kuanzia nyumbani? Je, ana nafasi nyumbani kujifunza kuwa mke na mama? Je, anamtumaini Mungu kumchagulia mume na anayefaa kwa wakati unaofaa, kama ndio mpango wake? Je, anajali mawazo yako kuhusu wavulana wanaokuja kwake? Je, anajali mambo ya kuolewa kuliko utii kwa Mungu? Je, ana ndoto za mchana kuhusu ndoa? Je, ana mawazo ya mahaba yasiyofaa?

Je, kipi ni muhimu kwake, kuwa mcha Mungu aliyekomaa au kuolewa na mtu yoyote? Je, anaona wivu rika zake wakiolewa? Je, anapata hofu akijua hataolewa? Je, anajua kwamba Mungu anaweza kuwa amempa wito wa useja na kumtumikia badala ya kuolewa? Je, anajua kwamba Mungu ana mipango maalumu naye, endapo akiolewa au asipoolewa? Je, anatumia miaka ya kutoolewa ni ya kujitayarisha kwa wito mkuu wa Mungu? Je, anazungumza na wanawake wasioolewa kanisani kwa njia nzuri na upendo? Je, ana upendo wa kutaka kushugulikia mahitaji ya wale wapweke?

Tufundishe mabinti zetu kutoishi maisha ya hofu, bali nguvu na ujasiri. Watambue kuomba ni muhimu. Wanapopata hofu wamtegemee Yeye. Someni kuhusu ahadi za Mungu na ulinzi wake. Angalia wanawake hawa walimtumainije Mungu, mke wa Nuhu, mke wa Lutu, Sara, Esta, Yokebedi, Debora au za Ruth. Chagua Zaburi za kusoma pale unapokuwa na woga. Angalia pale wana wa Israeli walipopata hofu kwenye kitabu cha Kutoka. Je, wale wa Waebrania 11 walionyeshaje ujasiri?

Wahoji wanawake kadhaa pale walipojaribiwa kuwa na hofu na ilikuwaje walipoogoa na ilikuwaje walipomtegemea Mungu? Soma maisha ya Sara, mazuri na

madhaifu yake yalikuwa yapi? Je, alifanyaje alipojaribiwa? Je, kwa nini ametolewa mfano kwa wale wenye imani?

Je, anahofu ya kumtumaini Mungu kumtunza? Je, ana imani ya Warumi 8:28? Je, anajua mafungu ya kusoma akiwa na woga? Je, akiwa na woga anaomba? Je, anaogopa kujaribu chochote kipya? Je, anaogopa watu wanavyomfikiria? Je, anaogopa kufanya makosa? Je, anaogopa wakati ujao (future)? Je, anaweza kusema 'hapana' watu wakimwambia atende uovu? Je, anaogopa kujeruhiwa? Je, anaogopa kuzungumza na watu? Je, ana wasiwasi, na kuona kwamba atashindwa, na kuona matatizo tu?

Je, ana ujasiri wakutatua magomvi au kutoelewana na marafiki, ndugu, walimu au wazazi? Je, ana ujasiri kusema alikosea? Je, yupo tayari kuomba msamaha akimkosea mtu? Je, anamwogopa Mungu zaidi ya binadamu? Je, anaweza kumwambia rafiki akifanya dhambi? Je, anakata tamaa afanyapo dhambi? Je, anapokea maonyo na kukosolewa kwa hali chanya? Je, anaogopa kutoa mawazo yake? Je, anaogopa kumshuhudia Kristo mbele ya watu? Je, ana hofu kuelezea hisia zake?

"Hufumbua kinywa chake kwa hekima; na sheria ya wema i katika ulimi wake." Ulimi hauwezi ukafungwa, una uovu usiotulia. Umejaa sumu iletayo mauti. Kama wazazi twapaswa tuwasaidie watoto 'kufuga' ulimi mapema ili wawe mibaraka kwa waume zao, watoto, kanisa na jumuiya. Daudi anamwomba Mungu atie kufuli ulimi wake. Ni vizuri tuwaambie mabinti zetu pale wanapozungumza isivyo, na marafiki zao waweza kuwa walinzi wao pia. Twapasa tusirudishe ubaya kwa ubaya. Twawezaje kufanya hivi? Mwambie binti amuulize mtu amwangalilie yale maneno yote yasiyo na sababu (idle words ya Mathayo 12:36-37).

Someni Yakobo 3 pamoja na kujadili. Soma watu ambao wamewasaidiwa kwa maneno mazuri, na wale ambao maneno mabaya yamewaharibia. Angalia maneno kama magomvi, malamiko, umbeya, uongo, kutia chumvi, kushuhudia uongo, na kukufuru.. Je, mwanamke anawezaje akajitawala kwa maneno yake? Soma kisa cha Abigaili au mke wa Pilato. Je, mwanamke awezaje kuwa na maneno ya kutia moyo au ushauri mwema? Twawezaje kutawala nafsi tunapozungumza? Twawezaje kufanya mazungumzo yetu yakawa mbaraka (improving speech)?

Je, anapenda kuwabandika watu majina? Je, anazungumza kwa ujinga, kwa sauti inayokera? Je, anatania wengine(mock)? Je, anapenda kulialia na kulalamika? Je anapenda kusengenya wengine? Je, sauti yake inakuwa kali wakati wote? Je, anapiga mayowe akigombana na nduguze? Je, anapenda kuripoti makosa ya wengine? Je, anatumia maneno yasiyo na upendo (unkind) kwa nduguze? Je, anapenda kusema maneno ya kuchokoza wenzake? Je, anapenda kukosoa watu na kuwakejeli (sarcastic)?

Je, anapenda kulitaja jina la Mungu bure? Je, anaonyesha heshima kwako na baba yake kwa maneno yake? Je, maneno yake yanajenga wengine au yanawararua? Je ,anasema lolote limjialo kichwani au anachuja maneno? Je, anamsahihisha aliyekosea kwa unyenyekevu? Je, anatoa ushauri mwema kwa wengine? kufungua kinywa kwa hekima kwa mama au mke ni muhimu. Watoto wanabidi wafundishwe (training) kutii. Hapaswi kuwa mvivu kwa kazi . Twapaswa kufundisha binti zetu jinsi ya kuwa na urembo wa ndani zaidi ya wa nje.

Sura ya 43
HITIMISHO

Mpendwa msomaji kwa kumalizia, tumeona maswali ni mengi tuliyoulizwa katika semina za malezi, hivyo email address yetu ni masakamomadi@aol.com au jambomuhimubooks@gmail.com

Baada ya kutembea muda na kukosa vitabu vya Kiswahili vya malezi ya watoto. Tuliona tuandike kitabu, si kwa vile tuna utaalamu sana, la hasha bali kwa vile tuliona kwamba hakuna ambaye ni mtaalamu wa kulea. Kila mtu ana mizoga yake! Ni Mungu tu ambaye ndiye Mzazi mtaalamu na MWEZA. Zamani mashangazi, mabibi walisaidia, ila siku hizi hata wao waonyesha mmomonyoko wa malezi kwa vile hawajapata maarifa hayo yaliyotolewa kwenye jamii zetu za zamani. Uvumilivu wetu wazazi unazidi kupungua jinsi dunia inavyoendelea, wiki hii nilisoma gazeti na kuona mama aliyemwambia mtoto wake wa miaka saba asinywe maji kwa vile anakojoa kitandani! Mtoto huyu alikufa kwa kuishiwa maji, madaktari walipompima walikuta hana maji. Walimlinganisha na pacha wake wakakuta ni kweli. Wazazi tunajitia busy kweli kweli hata sijui tulizaa kwa ajili gani na tuko busy hivi, tukiwapa wengine kutunza watoto wetu. Kumfundisha mtoto kutawala nafsi, kujikana nafsi, huduma, utii na kazi ni mambo matano ya muhimu sana. Katika kitabu cha Nabii Musa kumbukumbu ya torati asema, “Mwana akiwa mlafi na asiyetii, waitwe wazee na apigwe mawe auawe. Yaonekana jambo hili ni zito sana mbele za Mungu, yaani kutokuwa na kiasi na kutotii.

Mara nyingi mtoto akiwa ni mbaraka si kwamba wazazi wamebahatisha! Bali mara nyingi ni neema za Mungu na kazi waliyoifanya. “Nawapenda wale wanaonipenda, na wale wanitafutao mapema wataniona.” Methali 8:17. Anza malezi mema mapema, mtoto akifika miaka mitatu tabia imejengeka, na miaka sita, tabia inakuwa imekamilika! Ila kama umekosea mahali, kama sisi, mwombe Mungu maana ni mwenye rehema akufanyie miujiza kubadilisha tabia mbovu. Pia usisite kuwaomba wengine msaada ambao wana upendo na wanamjali Mungu mara zingine mtoto amsikia mwingine kwa Njia zile anazotumia, ila katika yote Mwombe Mungu sana. Uzazi si kazi ndogo kwani nimegundua uzazi definition yake ni mwenye dhambi mmoja anamkuza na kumlea mwenye dhambi mwingine! Sote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Ila Mungu anatupenda sana, na anatasa tufanikiwe, na ana ahadi zaidi ya 3500 kwenye neno lake, na kati ya hizo 365 zasema “Usiogope”. Nina changamoto nyingi kama mzazi, nimeshakosea mengi sana ila

leo nasikia neno “usiogope”. Nashuka magotini saa hii na kumwomba Mungu anipe nguvu, nishinde siku moja nitakapoulizwa “wapi kundi lako dogo nililokupa” niseme ni hawa kwa Neema ya Mungu tu na si nguvu zangu masikini.

Kama mtume Paulo anavyosema, “Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii;” Warumi 8:7. Ni mapambano siku zote ya kuwa na tabia njema ya mbinguni! Mambo ya dunia yalivyojiset ni kukuharibia malezi ya mtoto. Kila siku omba Mungu na kuendelea na vita. Hakuna mbabe wa shule hii awe China, Tanzania au Mexico! Hata Kaini alimwua ndugu yake Abel kabla ya televisheni. Angalia maisha ya Nadab, Abihu, Absalom, na wengine ambao wazazi wao walikuwa wazee wa imani. Usiogope, hata sisi tungeogopa tusingeandika, kwani hatuna uzoefu wala ushindi wowote. Tumejitosa tu! Mama mmoja alimkatisha tamaa mwenzake “Watoto wako ni wabaya sana utawasaidiaje watu nawe yako yakushinda!”. Hii si kweli kwani uzoefu ni msaada au daraja la wengine kupitia pale tulipokosea, na pia kuna wajukuu Mungu akitujalia. Pale tulipokosea kwa watoto bado kuna watoto katika jumuiya tunaweza kusaidia tukipata maarifa mazuri ya malezi toka kwa Baba wa mbinguni. Tunadai lile Fungu la “kuangusha mawazo yetu “
1Kor 10:5.

Mtoto mchanga uliye naye mkononi si malaika ila mtenda dhambi kama binadamu wote. Ni wewe wa kumleta kwa Mungu na kumlea katika kicho cha Mungu. Usiwe na roho ya malalamiko na manung’uniko. Hayo yaliwafanya Waisrael wafie jangwani wote, kasoro wawili. Mungu hajibu manung’uniko, bali hujibu maombi. Neno kubwa ni kumfundisha mtoto wako aweze kuishi bila wewe. Aweze kumtegemea Mungu na kuwa mtii, endapo upo au haupo. Aweze kujikana nafsi, na kujitafutie riziki, na kumudu maisha yake endapo upo au haupo.

Jaribu kuepuka kukaa mijini, ni pabaya kulelea watoto. Yalimpata Lutu japo Petro alisema alikuwa mtu wa haki, kwa kukaa mjini alipoteza watoto na mke. Tusome ile ngazi Ambayo Petro anaisema.... nukuu. Pengine Nuhu alikaa mashambani, yeye aliokoa jamaa yake. Miji ina majaribu ni mengi, japo ina mashule, maduka na huduma, ina mengi mabaya zaidi. Vijiji vya ujamaa vilikuwa na shida hii ya kuleta vijana wengi pamoja wasio na shughuli, ila kupeana utalaam wa uovu. Wanasema kujenga tabia kijijini ni mara kumi bora kuliko mijini.

Twaona Isaka na utii wake, japo alikuwa kijana mwenye nguvu kumshinda baba alitii kutolewa dhabihu na baba yake Ibrahimu. Watoto wengi wakorofi wameharibu ndoa za wazazi wao na wale ambao wana tabia njema wamejenga ndoa za familia zao. Angalia maisha ya Yakobo na Esau yalivyotenganisha wazazi wao. Hata na wazazi walifanya kosa la kupendelea watoto, nayo ikawa sumu kubwa. Rebeka aliharibu mambo hapa. Kina mama, “Mvuto wa mama na maombi una nguvu nyingi.”

Angalia maombi na kazi ya mama Musa, na jinsi Musa alivyokuwa jemedari na kiongozi wa kiroho. Wakina mama tusijiachie, hakuna kazi ya muhimu kuliko hii ya kumsaidia mtoto kuwepo mbinguni siku moja.

Mama lazima awe na kiasi, kutawala nafsi na kujikana nafsi. Vita vikubwa ni vya kushindana na nafsi (battle of self). Nafsi ife, au yule mtu wa kale atokomee. Mama wote wa wanadhiri waliambiwa wafanye mambo fulani; kama kutokunywa pombe n.k. Tunaona Hana, mama ya Samuel alitaka kumtunza mtoto amtumikie Mungu. Wazazi wengi tunataka kumlea mtoto atutumikie sisi! Mungu anapendezwa na maombi yasiyo na uchoyo au ubinafsi. Anza kuomba hayo leo. Ombea na watoto wa wenzio na kuwasaidia mashauri bora ya uzima. Wokovu ni kazi ya Roho wa Mungu bali kuwaambia wengine habari Njema ni kazi ya kila kiumbe. Ondoa chuki, ili mtoto asione una uadui na mtu naye ajifunze kupenda na kuwa bora. Adui angalia mazuri yake ana mengi, hata ni kwa adui ndiyo utapata ukweli na kujikakamua kusonga mbele.

Ndoa ya Hana na Elkana na nyingine zaonyesha mitara ni mibaya mno kwa ndoa na matunzo ya mtoto! Katu, siyo mpango wa Mungu! Hana alilea mtoto kwa miaka pungufu ya sita na mtoto akakumbuka yale mafunzo, na kuwa jemedari wa kumtetea Mungu. Katika kitabu cha Danieli, tunaona Danieli, Mishael, Anania na Azaria walikuwa vijana wadogo, ila waliweza kushinda majaribu makubwa walipotekwa. Walijifunza haya wapi? Si utumwani, bali nyumbani walifunzwa kiasi, kujikana nafsi, na kuepuka tamaa. Mama zao waliwafundisha kutokula ovyo ovyo.

Hata Kristo, mwalimu wake wa kwanza aliyekuwa binadamu alikuwa mama yake. Hakwenda mashule ya marabi kujifunza! Mzazi ndiyo mwalimu wa kwanza. Alijifunza kwa kuishi maisha magumu, ya kufanya kazi, akijikana nafsi. Na ndiyo maana ni muhimu mtoto akae nyumbani na kufundishwa mpaka afike umri wa miaka minane hadi kumi hivi. Hata hivyo shule nyingi zina watoto wengi darasa moja, na nilitembea pengi ambapo watoto hata wa darasa la tatu hawajui kusoma. Shule moja mvomero, ilisemekana ina mwalimu mmoja na watoto mia saba! Mama asiyeenda shule ila anajua kusoma, atamfundisha mtoto wake kujua kusoma akiwa na kitabu kwa miezi michache tu! Atamshinda mwalimu mwenye watoto mia moja darasani, kwani yeye ana mmoja!

Twaona Mariamu na Yusuf kwa kutoangalia mtoto kwa siku moja, walipotelewa na mtoto Kristo, na ilichukua siku tano kumpata. Hata nasi wazazi kwa kupuuza, kupiga masoga na watu, au kutosali twaweza kupoteza watoto wetu na kumpoteza Mungu katika maisha yetu. Usiogope kazi ngumu ya kulea hata kumtelekeza mtoto kwa jamaa, ni bora kuwa na mtoto mmoja na kumshugulikia kuliko kupeleka watoto wako kwa wengine ambao hawathamini mambo unayothamini. Usiwekeshe watoto kwa ndugu na jamaa, labda iwe dharura. Ni wakati wa kupanga kuwa na watoto wachache tutakaomudu kuwalea.

Siku hizi ni ngumu, si za kuwekeza watoto kwa mjomba au shangazi. Mzazi mmoja alilalamika kwamba alimweka mtoto kwa mjomba na akamfundisha ulevi. Mababu na mabibi pia japo wanasaidia, ila usitoe uongozi wako kwao, maana wao wanadekeza watoto au hawana makini ya kutosha kushugulikia watoto. Tunarudia,Iwe dharura tu kumwekeza mtoto wako kwa watu hapa na pale.

Kuna wengine hawataki kutunza watoto, aidha, walipata mimba bila kutarajia. Kwa hawa nashauri watafute njia ya kuwapa wazazi ambao watamtunza mtoto huyu vizuri. Usifikirie kumwua mtoto kwa njia yoyote. Yeye ni kiumbe kamili, hata kutoa mimba iwe

mwiko. Mtoto si mnyoo ambao tunatoa ndani ya tumbo. Tabia hii imejengeka pengi. Nchi kama ya Marekani wanawake milioni nne hutoa mimba kila mwaka!

Wazazi tutaulizwa hukumuni tulivyolea watoto wetu. Watu wakikusaidia ni bonasi isiwe sehemu ya programu yako! Hata hivyo ukiwa mzee kama uliacha watoto wako walelewe na wengine muda wote itakuwa vigumu kukusaidia maana umekuwa kama mpita njia.

Wale wenye wasaidizi nyumbani muwe waangalifu, kwani tumesikia mengi. Mfano dreva aliyeingia katika uhusiano wa kimapenzi na binti aliyekuwa anampeleka shuleni. Yaya aliyemweka mtoto mchanga kwenye oven na kumwua kwa sababu tajiri alimgombeza. Mayaya wanaowafanya wavulana wadogo kuwa waume zao, au yaya aliyetumia mswaki wa mtoto na kumpa mtoto ukimwi na kadhalika.

Kuna wazazi wengi wanaotesa mayaya na watenda kazi pia na hiyo ni maada nyingine ya kuzungumzia. Kama unaona kwamba kazi yao haikuridhishi, kuliko kuwatesa, fanya mwenyewe majukumu yako ili usisigane na watu. Pale inapobidi uwe nao, lazima kuwafundisha vizuri (train) ili wajue cha kuwalea vizuri, si kuwapa Chakula na kufua nguo zao tu, bali kuwasaidia kihisia na kitabia na hata kiroho pia. Watathmini, na kuzungumza nao mara kwa mara kama mwajiri wa ofisini. Yaya asiyeweza kusoma na watoto neno la Mungu, ikiwa unaenda siku nzima, itakuwa ni shida. Wazungu wengi wakiajiri yaya wanauliza mambo mengi, kama vile anajua kusoma na kuandika, amefika darasa la kumi na mbili, anaweza kumsaidia mtoto kiafya akizidiwa, anaweza kuamua magomvi ya watoto, anaweza kuwafundisha watoto mambo ya taaluma n.k. kama una uwezo usichukue mtu tu, eti ni bei rahisi kumlipa, wakati Ambayo una uwezo wa kumlipa hata Yule aliyesomea ualimu na akakosa kazi akusaidie mengi zaidi. Au ukapata mwenye uzoefu wa kufundisha watoto mengi, na japo utamlipa zaidi watoto Wako watapata mengi zaidi.

Ni muhimu mzazi aseme na kueleweka asiache maswali fulani, ndiyo iwe ndiyo, na siyo, siyo (ambiguity). Lazima nyumba iwe na kanuni za kufuata, na mikutano ya familia na watoto pengine kila wiki au mwezi. Mzazi asiogope kufuata sheria akiona atamkasirisha mtoto. Eli kuhani alijua ubaya watoto wake. ila hakuwakataza kufanya kazi ya hekaluni, waliendelea kuifanya. Aliona atawakosea au aliwaogopa. Alisikia malalamiko ya watu, ila pengine alipenda watoto sana na kuona watu wanamsakama na watoto wake.

Kutoka udogo mtoto afundishwe kuheshimu neno la mzazi. Wazazi wengi wanafikiri mtoto ni mdogo sana hawezi kusikia maagizo! Muda ukishaenda unakuwa umepoteza mvuto. Mtoto aliyezaliwa tu anaanza kufundishwa, mfano, kutokula ovyo ovyo, ale baada ya masaa matatu n.k. Wazazi wengi waliokua katika hali ya umasikini au shida wanafikiri kwamba watawalea watoto wao' ili wasipate shida kama wao. Wanawaacha kufuja vitu, na kufanya watakavyo. Jambo la kusikitisha ni kwamba watoto hawa ambao hawajapata shida wanashindwa kuishi na watu au wanaingia magenge mabovu ya uvutaji au tabia nyingine za uovu.

Wazazi wanapaswa kujua kwamba utajiri wao waliupata kwa sababu ya nidhamu na kazi ngumu. Watoto waliokuta vitu tayari kama vile majumba, magari na mashamba

imekuwa si mbaraka kwao. Mara nyingi wanaingia majaribu ya shetani kwa namna moja au nyingine. Yaweza usione vizuri, ila ukiangalia kanuni za mbingu utaona mashimo. Chunguza maisha ya wale ambao wamekuwa mbaraka kwa wengine na kuwa majemedari kwa mambo fulani, utakuta maisha yao yalikuwa na kanuni, kujikana nafsi, na kazi nyingi ngumu kama kukamua ng'ombe au kulima saa kumi na moja asubuhi na kadhalika.

Watoto wengi pia wamelelewa bila baba. Nchi ya Marekani ni asilimia hamsini. Jambo hili ni gumu katika tabia na malezi ya mtoto. Ni masikitiko; kama Charles Spurgeon alivyosema kwamba wazazi wengi hata wanaompenda Mungu, wanafurahi tu pale mtoto wao anapokuwa na akili darasani hata kama hamjui Mungu. Je watoto wetu wana vitabu vya Neno la Mungu na wanavisoma?

Masomo ya darasani ni mazuri ila sijawahi kusikia mtu aliyesema, "Hesabu imenifanya nisiwe mwizi," au "Jiografia imenifanya nisiwe mwongo au mwasherati." Ni neno la Mungu tu, ndilo lina nguvu ya kubadilisha tabia. Tunakaza kwa kurudia, ni NENO TU LA MUNGU linasaidia tabia. Filosofia za watu hazifui dafu.

Wazazi wengi wanahakikisha watoto wana mabegi makubwa yenye vitabu vya shule wakienda asubuhi, ila hawajali kama watoto wana Neno la Mungu na wanalisoma au wanabadilishwa nalo katika maisha yao. watoto wetu waendapo ibadani wawe na penseli au peni na Neno la Mungu. Darasani wakienda bila vitabu itakuwaje? Tunakazana waende na nguo nzuri kwenye ibada ila bila Neno la Mungu itasaidia nini? Je, wanasoma masomo yao ya lesoni? Kama una pesa za vocha za simu na kujisumbua na "halo, halo;" siku nzima, basi una pesa ya kuwanunulia watoto wako neno la Mungu.

Tunaagiza jamaa zetu wa mijini watuletee vitu vingi, kwanini wasituletee Kitabu kikuu pia? Agiza vitabu vya nyimbo za kuabudu ili watoto waimbe, wakariri mafungu ya Neno la Mungu kila siku. Huo ndio urithi bora utakaowapa, si majumba na mashamba. Shughulika nao sasa, kuna siku watasikiliza marafiki zao kuliko wewe, na utakuwa umechelewa. Utaonekana kwamba umepitwa na wakati, (old fasheni). Ikiwa runinga ni shida itupe. Nilipata shida na watoto wangu walipokuwa wanaangalia runinga, wakakosa adabu kabisa! Ukiwaita hawaitiki, ukiwauliza swali hawajibu. Mawazo yao yametekwa kabisa, wanakodolea runinga macho na wanapigwa na butwaa kwa wanayoyaona na kuyasikia! Runinga amekuwa kimungu au msukule fulani (hyponotic).

Mtoto mmoja Nairobi, aliyekuwa na mikanda ya ponografia; alikuja nayo shuleni na kuwapa watoto wengine. Iliposhikwa, mama alikana, "Mnamsingizia mtoto wangu, hawezi kufanya vile nyumbani kwangu! Ni mtoto mwema." Mtoto akaitwa mbele ya mama, na kuulizwa, akakiri kwamba amekuwa akiangalia nyumbani mikanda hiyo nyumbani, wakati mama hayupo!

Kina mama msitetee watoto, tabia inajengwa wakati wowote na popote. Wakina mama wengi wamekuwa adui wa kwanza wa watoto wao kwa kutetea uovu. Uwe kibaruani usiku na mchana. Wafanye watoto wako wawe marafiki wa karibu ili mambo yakiharibika wakwambie. Mzazi ndiyo kiongozi si mtoto. angalia mtoto anayofanya na umwelekeze. Umpe uhuru pole pole kutokana na vile anavyokabili majukumu yake. Mtoto asikae kivivu bila kazi ya la kufanya. Kusali asubuhi na jioni na watoto ni muhimu.

Ni sehemu yetu kama waumini wa Mungu. Kukosa kutelekeleza wajibu ni dhambi. Lazima kuwe na kanuni ili kujenga tabia (regularity). Wakati wa kulala, kula, kuomba, kucheza, yahitaji uvumilivu na uendelevu (consistency). Kiasi na kujikana nafsi inatokana na maisha yenye mpangilio (order). Usifanye ratiba ya mtoto kuwa holela.

Mama mmoja na mume wake wenye watoto katika shule ya msingi na sekondari walijivinjari na marafiki na ndugu kila siku kuanzia saa kumi jioni, wakitoka kibaruani mpaka saa mbili usiku. Walifika kwetu karibu kila siku, wakifanya mazoezi pamoja na kutembelea majumba ya watu kwa minuso wakati wa chakula. Watoto wao walikuwa wakijikuza wenyewe. Mwanamke mmoja ambaye alikuwa hajawahi kuolewa au kuzaa, aliwaona akashangaa walipotoka. Akaniuliza, “Hivi huyu mwanamke anatembea na bwana saa zote akimchunga, badala ya kuchunga watoto!”

Usiache watoto wajikuze wenyewe. To a child is folly alisema Sulemani; (mtoto ana ujinga mwingi kwa tafsiri nyingine). Usiache mtoto kwa muda kila siku unaenda mahali.

Maisha ya Yohana mbatizaji yanaonyesha kwamba japo wazazi walimpata uzeeni kabisa hawakumdekeza. Aliishi mashambani na kufanya kazi mahali ambapo majaribu yalikuwa machache. Japo alikuwa wa ukoo wa kifalme na ukuhani, uvivu haukuwa sehemu yake!

Mara nyingi wazazi wengi tunakazana na matendo ya nje tunayoyaona, na si matengenezo ya moyo. Hili ni kosa kubwa. Watafanya ya kutufurahisha ili wasiadhibiwe, ila mioyo yao haijabadilika. Jaribu kufanya mabadiliko ya moyo, akili na nia ya ndani, yale matendo ya nje yatakuwa rahisi. Yusufu alifundishwa asiwe mzinzi akiwa mdogo. Yeye hakuwa jitu. Hata alipokuwa mwenyewe Misri alimkimbia mwanamke aliyemshika kwa nguvu, huku amefunga taulo, akasema “Nimfanyiaje Mungu ubaya kama huu?” Ila Samson aliyekuwa Raisi na jitu lenye nguvu nyingi alishindwa jaribu hili akaanguka kwenye uasherati. Ilikuwa rahisi yeye kutumia nguvu zake kumpiga konde mwanamke na kumtupa mbali hata kumzuia asimfuate! Hapa pia ni nafasi ya kufundisha watoto wetu wa kike katika ulimwengu wa leo, kuwa na kiasi na tabia bora. Watoto wetu wengine wasichana siku hizi wanakimbiza wanaume, na kupunguza hadhi yao kama mke wa Potifa badala ya wanaume kuwatafuta. Watoto wetu wapaswa kujistahi, na kuwa na uungwana hii itawasaidia kupata wachumba na waume bora, kuliko kujipeleka au kuonyesha tabia ya ukahaba. Sisemi kwamba wakati wote wachumba ndiyo waje kwao kutawatafuta, kwamba hawana usemi kabisa kwa yule wanayempenda, bali wafanye haya kwa hekima na kujistahi, bila ya kujionyesha “chema chajiuza, kibaya chajitembeza”. Na hata sisi wakina mama tulioolewa kama mke wa potifa, hebu na tujisitiri na kuepukana na uasherati, zamani wanaume ndiyo walijulikana kw.a tabia hii mbovu, siku hizi baada ya sisi kupata vibarua na kwenda shule tumeingia katika uovu huu pia, na haya ni mafundisho mabaya mno kwa binti zetu.

Kila siku wapanda mbegu bustani ya mtoto. Yeye haangalii sana vile unavyosema, maana hayo ni maneno tu, anangalia vile unavyoishi. Je, unajua? Unasema yale

unayowaza, ila unaishi yale unayoamini! Saidia watoto katika jumuiya yako pia wakiharibikiwa nawe umeharibikiwa. Watakuja kwako na kukuibia, au kukupiga.

Uwe tayari kadiri ya uwezo wako kunyoosha mkono wako kusaidia wengine, “Amhurumiaye masikini humkopesha Bwana naye atamlipa kwa tendo lake jema. Je, umeshawahi kumkopesha tajiri mkubwa kama vile Bill Gates? Au Rais wa nchi yako? Basi hapa unamkopesha MWENYEZI MUNGU mwenyewe! Nikisikia fungu hili natetemeka. Mimi Kinyangarika nimkopeshe BWANA WA MAJESHI WA MBINGUNI kweli? Mungu ambaye wataalamu sasa wanasema kuna sayari zaidi ya trilioni alizoumba! Mimi ndiye namkopesha? Nimepata mawazo mazito kila naposoma hili fungu.

Kwenye vituo vya ibada, wawepo mama na baba wa imani wa kusaidia watoto ambao hawana wa kuwaelekeza vizuri, watoto wengi wanazaliwa katika mazingira magumu, mfano, na wakina mama ambao ni watoto pia, wasiokuwa na maarifa n.k. wengine hata uvumilivu unakuwa mgumu katika kuwafundisha watoto.

Usifurahie moyoni mwako uonapo mtoto wa mwenzako anaharibikiwa; ni kama kufurahi wakati mgonjwa ni mahututi kwenye hospitali hata ICU (Intensive Care Unit). Mara nyingi tukiwa na mwenzetu mgonjwa tunasikitika na kwenda kumtazama hata kupelekea chakula. Je, umeshawahi kwenda kwa mgonjwa mahututi na kuanza kumcheka akiwa pale kitandani kwenye hospitali? Nafikiri utaonekana una wazimu. Nilimsikia mama mmoja akimng’akia mwenzake, alipomwambia shida ya mtoto wake, “Wewe unasema mtoto wako atakuwa mbaya zaidi ya wa kwangu?” Roho ya maneno ya jazba kama haya ni ya ibilisi. Omba msamaha na msaada ikutoke.

Tumeona Ibilisi aliua watoto wadogo wa kiume kwa kumtumia Herode na Farao kwenye Neno la Mungu. Na hata leo anataka aue watoto wa kiume. Baadhi ya Vijana wetu wa kiume wamekuwa wakijiunga kwenye makundi ya tabia mbovu. Wengine hawataki kwenda shule hata wale ambao wazazi wao wana uwezo wa kuwasomesha. Hawataki kwenda ibadani. Asilimia sabini ya walio katika nyumba za ibada ni wanawake. Wakina Baba mtusaidie na hili. Nimeona wakina baba wengi wanapenda watoto wao na wake waende ibadani ila wao wanakaa nyumbani!

Baba jitahidi jinsi ya kumsaidia mtoto wako wa kiume akue katika mazingira bora, apate ustadi ili aweze kukabiliana na mahitaji ya familia, na zaidi ya yote aweze kuwa kuhani nyumbani mwake ili siku moja aingie Paradiso. Hili ni jambo kubwa mno. Maisha yetu duniani yana maana tu kama tunajitayarisha kupata uzima wa milele mbinguni, zaidi ya hapo ni kupoteza muda, maana sidhani kama kuna mtu anapanga kuungua katika ziwa la moto, kupiga mayowe na kusaga meno. Japo neno la Mungu linazungumzia upendo wake, ila kuna siku ya hukumu Ufunuo 1:7. Na ni vizuri tuelewe hilo kwa undani kwamba ni Mwenye rehema ila pia ni Mwenye haki. Itakuwa mbaya sana endapo watu wabaya waende mbinguni. Je, ungependa kukaa karibu na mwizi asiyeacha hiyo tabia mbinguni? Ila Nahumu 1:9 yasema, “Atakomesha kabisa, mateso na dhambi haitainuka tena mara ya pili.”

Wazazi tuanze kuweka mkazo jinsi ya kuwasaidia watoto wetu wa kiume, wana majaribu mengi nje ya nyumbani, kama Samsoni Mnadhiri. Japo wazazi wake waliuliza, “Tumtunzaje huyu mtoto;” na wakaambiwa; Samson alizidiwa nguvu na msukumo wa rika na marafiki.

Baba wengi walio na mabinti watulivu waliosoma wanasema wanaogopa kwamba wanaume waungwana wa kuoa watoto wao wamepungua. Mmoja aliniambia, “Binti yangu anakutana na vijana wasio na ustadi wanaotaka mtu wa kuoa na akae kama kupe.” Uwe muwazi kwa mtoto wa kiume kuhusu majukumu yake, na upate maarifa ya hii shughuli. Hakuna karatasi walilokuja nalo tumboni la maarifa ya kuwatunza (parenting manual).

Tuwalete watoto wetu kwa Mungu kwa njia ya maombi, na kisha tuwatambulishe kwake. Tuwafundishe jinsi ya kutatua matatizo, hatuwezi tukawatatulia matatizo yao lazima wajifunze nyenzo za kutatua. Kwa kawaida baba anazungumza na mtoto wake dakika tisa Marekani na mama dakika ishirini na nne hivi. Nafikiri kwa vile hakuna mayaya, mababa wengi hutumia muda na watoto wao Marekani kuliko Afrika.

Wazazi tufundishe watoto watu kusamehe, na kujisamehe. Mungu anatusamehe kila siku. Katika Neno la Mungu tunaona dhambi iliingia duniani kupitia wazazi wetu Adamu na Hawa, waliambiwa wafanye kafara, ikiwa kama kielelezo cha Kafara yake Mungu kubwa ambayo ilikuwa inakuja. Kutosamehe kumeleta maumivu mengi kwenye familia nyingi, mtoto aelezwe somo la kusamehe, kufuta hasira na kutoa visasi. Kutosamehe ni kama kunywa sumu na kufikiri yule aliyetukosea atakufa. Kusamehe kunatufanya sisi tuwe huru na kuwa ukurasa mmoja na Mungu wetu. Tunaambiwa tusiposamehe wengine nasi hatutasamehewa. Mungu ndiye anayetuwezesha tusamehe watu, hivyo mtoto amwombe Mungu “ahadi zako za kweli, umesema tusamehe, ni vigumu kwangu, naomba unisaidie nisamehe”. Kujisamehe pia ni muhimu sana ili tuondokane na hatia, Mungu anatusamehe dhambi zetu zote, hata iwe ya aina gani, nasi tuwe tayari kujisamehe.

Kazi ni muhimu. Ijapokuwa mtoto anaona mfano wako hata katika kazi, ni lazima pia kumfundisha, kukagua kazi yake na kumtia moyo. Angalia website (401 ways to get your child working) na doorpost.com. Wazazi wengi hawatumii ‘kutia moyo’ kama nyenzo moja muhimu. Mtoto analaumiwa na kutukanwa bila mzazi kutambua alichofanya. Mzazi anaacha makovu ya huzuni kwa mtoto. wengine wanakejeli watoto wao. Mtu mzima unapokejeli watoto, inaonyesha kutopevuka (immaturity). Mtoto ni mtoto tu, usiwe kila mara unamkatisha tamaa.

Watu wa nchi za magharibi ambao wampenda Mungu wanasoma na kujifunza mbinu za kulea kwenye neno la Mungu toka kwa waandishi mbalimbali. Najua utamaduni wa kusoma ni mdogo nyumbani. Nilisoma gazeti fulani na kuona jinsi mwandishi mmoja akiwaandikia wamarekani weusi, naye alikuwa mmarekani mweusi; alisema “Ukitaka kuficha kitu kwa mtu mweusi, kiweke kwenye karatasi. Maana hasomi. Ukiweka hata dola mia moja kwenye kitabu, utaenda miaka kumi; ukirudi utaikuta. Wana mzio (allergy) wa kusoma!” Ni lazima tujikaze na kutafuta maarifa ya kulea watoto, si kuwapa chakula, nguo na malazi tu! Kuna zaidi ya hapo. Tabia na kujitegemea ni muhimu.

Zamani watu wengi waliacha wazazi wakajitegemea na kusaidia wazazi. Siku hizi watoto wazee wanakaa kwa wazazi na watoto wao, au hata wajukuu zao. Magomvi madogo madogo yanatokea walipooa au kuolewa na warudi nyumbani. Aidha tabia zao ni ngumu au hatukuwafundisha uvumilivu. Lazima uwe na ratiba na watoto wako, usiache wajikuze. Panga magoli au malengo ya unayotaka watoto wako wafanye! Sisi ndiyo tunaleta tofauti katika maisha ya watoto wetu. Ukimwona mtoto ana huruma, uchoyo, mchapa kazi, ana hekima, au msema kweli ujue mara nyingi hivi vinatokea nyumbani. Tunda halianguki mbali na mti.

Gazeti la Times la May 20, 2013 lilionyesha kwamba watoto wengi wapo nyumbani, na kushugulikia mambo yao mengi (kizazi cha mwaka 2000 au Millenium). Wanapenda kujipiga picha mpaka 85 kwa siku wakituma kwa face book “niangalie nakula, niangalie naendesha pikipiki” n.k. Tabia ya umimi imeanza kutapakaa, hivyo watoto wasaidiwe kujikana nafsi ili watakapoishi katika jumuiya na familia wawe raia bora kwenye falme hizi za dunia na ile ya paradiso.

Sulemani asema moyo wa mtoto una upumbavu, ila yabidi asahihishwe. Apewapo kazi usiachie hivyo ila uitathmini na kuisahihisha. Na pia aone matokeo ya kazi mbaya au tabia mbovu (natural consequence). Usipoteze muda wako kibaruani au masomoni kama mzazi wakati mtoto anakua. Sijasikia mtu aliyestaafu aliyesema, “Ninajuta, kwa nini sikukaa ofisini muda zaidi!”

Wazazi, adui wa roho anafanya kazi ovataimu kupotosha watoto wetu. Anawachukia ni ajabu. Ni kama simba angurumaye akitafuta awameze. Anajua ana muda mdogo. Macho yetu yamefungwa tusione hawa malaika walioanguka. Wana uzoefu wa miaka 6000 wapo kibaruani. Ila tujipe moyo kuna malaika wa Mungu pia wa kutusaidia endapo tunachagua upande wa Muumba. Tuko vitani, vita vya kiroho. Hebu tusiwe na upendo ulio na upofu kwa watoto wetu. Upendo huo potofu utafanya tusiwaadilishe jinsi tunavyotakiwa. Vifaa vya vita ni neno la Mungu, haki, imani, kiasi, kukesha na uvumilivu.

Usiache watoto wajifunze uovu eti wataweza mbeleni kuchagua mema au mabaya! Magugu ya uovu yataongezeka kwa kasi kuliko wema. Muda wa kulea unapita haraka, na ni mfupi. Hivyo usiweke magugu bila sababu eti ajue maovu pia, na kisha achague.

Linda kwa uangalifu milango ya macho, masikio, mionjo, hisia na harufu! Mtoto asisikilize muziki wowote. Miziki kama ya rap na Rock imeonekana kuleta mivuto mibaya ya tabia kama uharamia na ulevi. Jaribu kuangalia kwenye tovuti kwa vichwa kama “rap na tabia ya watoto”. Si siri, hata kwa wale wasiojali Mungu. Muziki ukoleapo unaacha fahamu za ubongo (frontal lobe) kutofanya kazi zinabaki hisia (feelings and emotions) na hii inamfanya mtu awe dhaifu kufanya maamuzi mema. Epuka miziki inayorudia rudia maneno hata kama ni maneno ya Mungu mfano “Nakusifu, nakusifu, nakusifu.” Baada ya muda hufikiri inakuwa kama ulevi. Unasahau hata unamsifu nani! Hata utungapo nyimbo maliza maneno mfano “nakusifu Mungu kwa vile umenijalia maisha n.k.”

Hata runinga ina tabia hii, mtoto akitazama baada ya muda hatumii ubongo atakuwa tayari kusikiliza chochote aambiwacho na kufanya (bypass the frontal lobe).

Siku hizi runinga ana dada yake anaitwa compyuta. Wengi tunanunua hivi vitu na dhamira nzuri kusikiliza taarifa, na historia (documentary) ila udhibiti inapungua na hata ukienda kulala watoto wanaendelea kuangalia wanachotaka.

Pia nimeona hata matangazo ya biashara yana watu waliovaa nusu uchi na kusema maneno ya ajabu. Mtoto hawezi kutofautisha maisha halisi na yale ya kwenye runinga.

Mtoto wa miaka minne alimkimbilia baba yake nje na kugumia, “Baba huyu mtu anataka kumwuua mama aliyekaa dukani.” Tumesikia watoto walioua, wakifikiria mtu huyo ataamka na kuwa katika kipindi kingine. Runinga inaonyesha watu wanaoishi pamoja bila kuoana. Hii ni dhambi kwa maagizo ya utamaduni wetu na Neno la Mungu.

Kwa nini runinga iwe mwalimu wa watoto wetu na maadili mageni? Watoto wa televisheni wana usikivu mdogo, wanatafuta mahaba mapema, wanapenda magomvi, makelele, na ghasi na hata ukatili . Runinga inakuwa mwalimu wake na hivyo hata kupoteza maadili na mambo ya kiroho si kitu kikubwa kwake. Na hata sisi watu wazima mengi ya uovu tunapoyaangalia tena na tena tunapunguza nguvu ya kujaji uovu na wema. Hata mayaya wakiangalia siku nzima na watoto wetu pia wanapata dozi.

Ni muhimu mtoto achaguliwe shule nzuri ambayo itamsaidia kumjenga kiroho, kimwili na kijamii. Usipeleke watoto watakapopata majaribu ambapo tabia na mambo ya kiroho ni duni. Vitabu na magazeti wanayosoma watoto viangaliwe. Watoto wasisome vitabu vya waandishi makafiri wasiojali tabia ya mtoto. Vitabu vingi vinapanda mbegu za uovu kwenye akili za watoto, na kupunguza thamani ya neno la Mungu na maadili mema. Vimekuja vitabu vingi vya watoto, vya uchawi vimekuja, kama vile vya Harry Potter, Pica n.k. Burudani ziangaliwe, nyingi siku hizi ni za anasa au zinazohusiana na uchawi.

Computer pia ni shida. Watu wamewasiliana kwenye mitandao ya facebook, na wengi wametoroshwa. Nimesikia watoto wadogo wakitoroshwa na wazee kwa sababu ya kuwasiliana nao kimapenzi na kupata hisia zisizo halisi kimaisha za kubuni au kuwazia hivi(fantasy) au kuishi maisha ya anasa. Mtoto anaathiriwa kwa mvuto mkubwa zaidi na uovu zaidi ya wema. Mtoto asiachiwe kwenda kokote, na saa yo yote anapotaka. Mtoto wa kike ni tofauti na mtoto wa kiume. Japo tunazungumza juu ya usawa, madhara kwa mtoto wa kike akitembea usiku peke yake ni tofauti kidogo na ni makubwa kuliko ya mtoto wa kiume.

Talaka pia ni athari kubwa kwa watoto. Watoto wameonekana kuwa na shida kubwa ya nidhamu wakijiunga na magenge ya ulevi, kuvuta sigara, uharamia, wizi, umalaya na mengineyo. Na ndiyo maana katika kitabu hiki tumezungumzia ndoa kwa muhtasari.

Adui shetani anafanya kazi na mtoto hata aliyezaliwa leo! Mama wapaswa ndiye awe mpiganaji wa mtoto huyu. Ni ukatili kuacha makucha ya shetani yakimnyangua mtoto. Mama usiwe adui wa mtoto kwa kuruhusu uovu uanze au uendelee. Usalama wa watoto unategemea mno mzazi kuwa macho na kukesha. Wadumu katika kumpenda Mungu nakuomba msaada toka kwake kila saa!

Kanuni ya upendo wa Mungu iwe dira. Soma 1Wakorintho 13 na Zaburi 91. Mafungu haya yanatueleza kwamba Mungu anatulinda na analinda watoto wetu. Nafikiri wote tunangoja ile sauti siku moja, “Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu kwa madogo, ingia katika raha ya milele.” Kwenye utafiti Marekani, asilimia themanini na mbili walisema kwamba wana imani wataenda mbinguni. Ni nadra sana mtu kusema anapanga kwenda ziwa la moto au jehanamu; hakuna anayejipangia mambo mabaya! Shida ni kufuata ile njia nyembamba ya mashimo isiyo na uzuri, ukilinganisha na pana ya lami iliyojaa maua na mapambo.

Sisi wenyewe hatujiwezi. Kuwa mzazi ni kazi kubwa na mara nyingi inakatisha tamaa. Maana kila binadamu mimba yake ilitungwa dhambini: “Tazama mimba yangu ilitungwa katika dhambi.” Zaburi 51 yatukumbusha tumezaliwa dhambini, na kila binadamu amefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Hebu Bwana Atutegemeze na kutusaidia katika kazi hii nzito ambayo mara nyingi imenitia hofu, imeniletea machozi na kunikimbiza magotini kutafuta uso wa Mungu. Hebu tushirikiane kutafuta uso wa Mungu maana Bwana anajua watoto wetu toka wakiwa tumboni na kuwatakasa. “Usiseme mimi ni mtoto, maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema neno nitakalokuamuru.” . tujipe moyo kwani Bwana anapenda watoto mno wetu kuliko hata sisi tunavyowapenda

Paulo anamwambia Timotheo kwamba, “Wewe umeyajua maandiko toka utotoni mwako, toka kwa bibi yako Lois na mama Yunisi!” Watoto wetu ni mbaraka kwa Mungu kufanya mapenzi yake, kwetu na kwenye jumuiya; hebu tuendelee kuwaombea.

MASWALI NA MAJIBU YA WAZAZI (**mifano**)

1. ***Mimi ni mama wa watoto wadogo watatu, nimesoma na ningepata kazi, ila wengi wananiambia kukaa na watoto ni vizuri.***

Mpango mzuri ambao watoto watafaidika kupita yote ni wa mama kukaa nyumbani. Na kama mna uwezo wa kuishi kwa mshahara mmoja jitahidini mama akae nyumbani. Watoto wanafurahi wakikaa na mtu mmoja anayewapenda na wa karibu kama mama. Hata kujifunza wanajifunza kwa urahisi zaidi. Hakuna mtu unayeweza kumlipa akatunza watoto wenu kama mama! Utafiti umeonyesha kwamba watoto wanaokaa na mama wana magonjwa machache kuliko wale wanaokaa na makundi ya watu wazima na watoto.

Nafikiri hii ni pamoja na magonjwa ya kuambukiza, ya kukosa jua, ya kukosa mazoezi n,k. Mahusiano yanajengeka zaidi na unakuwa na nafasi ya kumfundisha mtoto wako utii ukiwa naye kuliko akiwa na watu wengine. Kuna wakati inabidi mtoto wako akae na wengine, ila hakuna aliye bora kama mzazi. Jumuiya za kutunza watoto zisizomthamini Mungu hawafundishi watoto kuhusu Muumba, na watoto kunyanyaswa inakuwa rahisi.

Mama wengine wasema wanaboeka kukaa na watoto siku zima na wangependa wapate kazi iwachangamshe. Kusema kweli kazi nyingi zinaboa kwa namna fulani. Piga picha ya mtu wa maabara kwenye darubini siku nzima, au mwanariadha anayefanya mazoezi siku nzima. Nafikiri kitu ambacho huwa tunafikiria ni pesa, kwamba hulipwi. Jaribu kuangalia kama unaweza kutafuta biashara ukaifanya nyumbani kwako ili ukae na watoto wako. Pia utafute mama wengine na kuwa na mikutano nao, angalau mara moja kwa juma. Hii itasaidia kutoboeka kwako.

Hata hivyo mama ana kazi nyingi kuamka asubuhi, watoto wavae, awapikie, asali nao. Na akienda kibaruani akirudi mara nyingi anachoka hata watoto wakimwomba awahadithie hadithi anakuwa amechoka. Na mahusiano ya unyumba nayo yanavunjika siku hizi kwa vile kila mtu anakuwa amechoka na ugomvi kidogo ukitokea basi kila mtu yuko tayari kusambaratika aende kwake. Watoto wanahitaji wewe mama uwe nyumbani, kama haiwezekani basi itabidi uende kibaruani ukimwomba Mungu atoe nafasi siku moja utunze watoto nyumbani.

Mama mmoja rafiki yangu, tuliyesoma naye, aliamua kukaa na watoto wake nyumbani hadi walipofikia umri wa kwenda shule. Na walipoenda shule alifanya kazi asubuhi tu, na mchana alikuwepo nyumbani kuwapokea watoto walipotoka shuleni. Mama huyu alikuwa amesoma sana, alikuwa na PhD, lakini aliamua kutunza watoto kwanza. Watu walimcheka sana, wakamwita mjinga, hata kama ni msomi. Lakini leo, anavuna matunda hapa hapa duniani, make watoto wake ni tofauti, wana tabia nzuri, tofauti kabisa na wengine wa rika lao.

2. ***Tuna mtoto wa miaka miwili aitwa Baraka, ambaye anataka abebwe kila saa, na tukimkanya asifanye kitu, analia na kurusha vitu huku akijigaragaza (tantrums).***

Ukimwambia asishike vitu kama vile vyombo vya umeme hasikii. Je miaka miwili inatosha kumchulia hatua za nidhamu?

Katika nia nzuri ya kumfurahisha na kutaka muwe na amani mumemfanya awe kisultani. Haiwezekani kumbemba kila saa! Mwacheni alie wakati mwingine, hatakufa! Akiwa amekula, hana kiu na ameenda chooni, muwe huru mkiendelea kumwangalia mkifanya shughuli zenu. Akipiga kelele msimwangalie sana, angalieni mbali kana kwamba kuna hatari ila msimbebe.

Kama mmezima taa usiku acheni apige mayowe, kumfundisha tabia na nidhamu kunaanza toka anapozaliwa! Soma, ujue namna ya kumfundisha mtoto hata wa miezi michache nidhamu, itakuwa huyu wa miaka miwili anayetaka kuwapa shughuli! Anajua mnampenda kweli, naye mnamwona anapendeza ila hajikani nafsi. Anataka maisha yote yazunguke kwa matakwa yake. Lazima awe na wigo wa vitu ambavyo aweza kuvifanya, mkimwambia la, iwe la!

Adhabu za kuchukua vitu anavyovipenda zitumike (consequences). Kiboko kitumike kwa nadra sana. Baada ya kumwambia mara kadhaa. Kutokana na umri wa mtoto, mzazi awe mwangalifu ili asimwumize mtoto. Usipige ukiwa na hasira. Mtoto ni vyema ajue kosa lake kwa uwazi kabisa. Mzazi anahitaji uvumilivu mwingi. Mtoto mdogo wa umri huu ana udadisi, ila haina maana aharibu vitu. Mwachie aguse kile ambacho hakina hatari ukiwepo ila awekewe wigo wa vitu vinavyopaswa kufanywa na visivyopaswa kufanywa. Mfundishe kwamba, kumwaga vitu, kuharibu, kuangusha vitu, au kuua hata wadudu ni kosa kama wadudu hawa si wa madhara. Ni kweli miaka hii ya awali ni changamoto, ila mambo haya ni kwa watoto wote wanaoendelea kukua. Washugulikie wawe na utii bora na wakiwa wakubwa utafurahi kama umefanya kwa upendo na kuwasaidia kuwa raia bora.

3. ***Watoto wangu bado ni wadogo, ila napoona wale wenye watoto vijana kuanzia miaka kumi na mitatu (teenager), naona wana shida nyingi na watoto wao, kuliko mimi. Je, nifanyeje niepuke shida hizo za mbeleni?***

Mafikara uliyo nayo ni ya wazazi wengi! Tunakusahuri utumie muda mwingi kujenga mahusiano na watoto wako wakingali wadogo, kama tulivyoshauri katika kitabu hiki. Pia mkabidhi Mungu huu woga ulio nao maana Yeye anajua ya mbeleni, ili tusikope shida za kesho na kuwa na wasiwasi au kusononeka. Tuendelee kujifunza zaidi, na kuombea malezi.

4***. Kwa nini inakuwa kazi watoto kutii tukiwaagiza kitu? Kwa nini mpaka tuwape adhabu au tuwafokee? Kwa nini hawaonyeshi ushirikiano na kukubali yale mambo ya maana tunayowaambia ili wapunguze ugomvi?***

Changamoto wanayotupa inatokana na roho ya binadamu ya kutaka kuwa na upinzani wa vitu ambavyo ni vizuri, vya Mungu, na kuvutwa na sumaku ya viovu. Roho ya binadamu, toka mwanzo wa dunia, ina ushindani wa falme hizi mbili: Ubaya na wema.

Wanapenda kuonekana kama ni mashujaa na wanatawala ukumbi. Hata watoto wakiwa wenyewe kwa wenyewe wanataka kuonyesha ni nani ambaye ni bingwa au nyota! Hii inatokea shuleni, kwa wazazi na pengine. “Sidhani kama unaweza kunifanya nikusikilize au nifanye utakavyo.’ Roho hii ya ushindani ni lazima ishugulikiwe, mtoto ajue ni nani mwenye mamlaka mapema, maana hata watoto wengine wakisikia iwe darasani au nyumbani, nao pia wanataka kupinga mamlaka. Weka sheria na sema kile ambacho unatazamia, na fuatilia

5.***Nikiwa na miaka ishirini na mmoja nilipata mimba nje ya ndoa na sasa nina mtoto wa miaka mitatu. Najua si mbali mtoto atauliza baba yake ni nani. Nimwelezeje, na wakati gani?***

Wakati utafika, itabidi umweleze habari yote na uhusiano wenu na baba yake. Ila si sasa. Lazima awe amekomaa kidogo na hisia zake ziwe tayari kuchukuliana na jambo hili. Usifanye kitu hiki kuwa siri kubwa ambayo aidha wewe au yeye mnakuwa mnalifikiri wakati wote. Kina mama wengi wamefanya hili kuwa siri na ni makosa.

Jambo hili lapaswa uzungumze na mtoto na kuliweka wazi. Hasa akiwa mkubwa. Usimdanganye, utakapomweleza. Zungumza kwa faragha na kwa upendo kuhusu mzazi wake ukifika wakati wake. Anza kumpa habari chache kuhusu mzazi wake. Mfano, “Baba yako aliondoka kabla hujazaliwa. Hakutaka tuishi pamoja. Sijui kwa sababu gani. Pengine ilikuwa haiwezekani yeye kunioa. Sifahamu. Ila nina uhakika angekuona angekupenda na kukutunza, ila hakuwahi kukuona. Pengine tuanze kusali ili Mwenyezi Mungu Atupe mtu mwingine kuwa mume wangu na baba yako. Je, unapenda tufanye hivyo?”

6.***Nakasirika kwa vile mtoto wangu wa miaka miwili tukiwa ibadani hakai mahali pamoja. Anajua hapaswi kukimbiakimbia, ila anapiga makelele na kukimbia kimbia, nifanyeje?***

Kwa kweli watoto wa umri huu hawawezi kukaa mahali pamoja. Na kwa vile ibada nyingine hazitengi vipindi vya watoto kwenye chumba chao. Nafikiri hakuna haja ya kumwadhibu kwa hili ila lifanyie kazi kila mara. Mlete na vitu vya kushugulikia kama ni kuchora na rangi (crayons) apake rangi, au mwanasesere. Ila usimwache mtoto na yaya eti unaenda nyumba ya ibada. Mtoto huyu ni mkubwa na anajifunza kitu kanisani/msikitini, japo kidogo na anajenga tabia ya kicho kwa vitu vya Mungu.

Yeye anahitaji kumjua Mungu kuliko wewe maana ananza safari yake hivyo unafanya vizuri. Jaribu kuwa mvumilivu na kuendelea kuomba, ili kanisa lako liwe na sehemu ya watoto. Fanya mazoezi naye wakati wa siku za katikati ya wiki jinsi ya kukaa kanisani ili akifika awe amezoea. Watoto wakiwa na mwalimu wa watoto siku ya ibada, na ukimleta toka akiwa mdogo atazoea kukaa na kutulia, atakuwa anajua wakati huu ni wa kufanya nini? Usiende Ibadan bila mtoto ukimwachia mtu!

7.***Je, ni kwanini watoto ambao wanalelewa kwenye familia zenye wazazi wazuri wenye kila kitu wanatokea kuwa wabaya na wale wenye wazazi wabaya wenye hali ngumu ya maisha pia wana watoto wanaotokea kuwa wema?***

Si mazingira na urithi peke yake vinavyofanya watoto wawe kama walivyo! Wazazi wengi wanajipongeza hata kujitapa wakiwa na mtoto mwenye tabia nzuri na mafanikio, na kujilaumu wakiwa na tabia mbaya. Wanasema “Je, tulikosea wapi?’ Ni kweli kabisa

wazazi wana mvuto mkubwa wa tabia ya mtu ila siyo fomula yote. Mengine ni uzoefu wa mtoto, lishe ya mtoto, marafiki wa mtoto, uchaguzi wa mtoto maana Mungu ametuumba tuwe na uchaguzi.

Kwa kweli uzazi ni changamoto na zawadi pia. Unapofikiria unajua watoto wako na kwamba umewalea vizuri; unaweza kupigwa na butwaa kwa jambo usilolijua. Endelea kuishi magotini, hata watoto wako wakiwa wakubwa, usifikirie kwamba umechelewa. Bado wana muda wa kubadilika; na wasipobadilika utafanya tofauti hata kwa wajukuu zako. Hata kama kwa udhaifu wako ulifanya makosa ya wazi kwa watoto wako, una nafasi ya kusoma na kujua kwa ajili ya watoto wa jumuiya na ndugu na jamaa ili uwape uzoefu wako nao wanufaike.

7. ***Mtoto wangu alichanjwa na watu wengi wameniambia lazima niwe mwangalifu wa chanjo.***

Kwa kweli mambo ya chanjo ni topic ndefu sana. Kuna shirika linaitwa National vaccine information center (NIVC) lenye wanasayansi wengi wanaotoka dunia nzima wa biology, tiba, hisia za fahamu, bacteria, na wengineo. Wengi wanaozungumza wanaona kwamba wanarisk kazi zao kwa kusema haya. Toka 1997 hoja ya chanjo inaendelea kukua. Wazazi wanahitaji kujielimisha kwa hili ili kusudi utafiti wa kinga uendelee kufanywa. Hatuna shaka kwamba chanjo zimesaidia wengi. Na tunaamini kwamba kinga ya mwili ya asili itawezeshwa kwa ubora kama tutafuata yale masharti kumi ya afya kwa magonjwa mengi. Usalama wa chanjo wahitaji kuendelea kuwa na utafiti mwingi. Ni vizuri mteja ajue uzuri wake na ubaya wake na zisitolewe kwa mpigo. Watoto wengine wamedhurika ubongo kwa ajili ya chanjo.

Utajuaje kama mtoto ameathiriwa na chanjo? Nafikiri kama mtoto hakuwa mgonjwa kabla, na akapata hiyo shida kwa sababu ya chanjo, mzazi ajue reaction ya chanjo inakuwaje na ajue jinsi ya kuiripoti. Ni vizuri ajue mtengenezaji wa chanjo na namba za hizo chanjo. Kwenye gazeti namba 105 la Family Living la US Mar/Apr 2001; mzazi aliandika kwamba aliagiza chanjo ya tetanas ili ije pekee yake kwenye famasia kuepuka chanjo za mseto.

Kwa sababu nchi zetu ni changa na mambo mengine ni vigumu kufanyika, hebu wazazi tusome zaidi kwenye mtandao habari za kweli za madhara ya chanjo na jinsi ya kusaidia familia zetu. Iwe mteja unayejielimisha, ni kweli chanjo zimeua watu, zimeletea watu kisukari, kuletea watoto utindio wa ubongo (angalia kazi ya Dr Sptizer walter wa Mc Gill university Canada). Chanjo zinaandikwa kwenye chupa kama dawa zozote; madhara na faida zake. Chanjo zingine zinahifadhiwa kwenye zebaki ambayo ina madhara kwa mwili. Kina mama wajawazito, inapendekezwa ni vyema wasipate chanjo mpaka wakati huu upite. Usiwe unachukua matibabu kusoma vizuri. Siko hapa kukwambia la, au ndiyo, ila jitahidi upate habari zaidi.

8. ***Waweza kukata kondo na mtoto wako mtu mzima bila kuharibu mahusiano?***

Hii ni shida hasa ya mama wengi kwamba hisia zao zinakuwa bado kwa watoto wao (attached) na hasa kwa wale ambao wamelea watoto solemba, bila baba mtoto. Watoto wengine watu wazima bado wanaishi nyumbani, au mama anaenda kuishi na

watoto wake japokuwa hana kasoro yoyote ila kihisia anaona analiwazwa kwa namna fulani.

Mzazi ni lazima awaonyeshe watoto kwa matendo na kwa maneno kwamba wanaweza kuishi au kufanya lolote wanaloweza. Watoto wanajifunza kwa tabia zetu kwamba tumewaacha huru na si kwa maneno. Mzazi mmoja aliomba mtaji kwa mtoto wake ili ajitegemee, “Ili nikuache huru nisikufuate fuate hata ukioa na kukuharibia ndoa yako.” Ila aliendelea kumfuata mtoto wake hata alipooa na kukaa kwake kwa miaka. Kwa mazungumzo na matendo yake alikuwa anaharibu ndoa ya mtoto wake bila kunuia.

Ni kweli mtoto aweza kuwa na miaka kumi na minane ila ahitaji usaidizi wa shule na mengineyo. Mjue mtoto wako vizuri. Mtafutie njia ajitegemee ikiwa ni kibarua, elimu, rasilimali kama ardhi, au mtaji. Kwa mtoto aliyetoka na kurudirudi tena tafuteni shida iko wapi na kumsaidia. Mara nyingine hata mtoto aliye kwake, waweza kuwa haujakata kamba naye kuliko aliye nyumbani. Mambo haya yahusisha hisia sana na pengine mnalisha na kumvisha huko kwake! Zungumzeni kama wazazi msikae kimya na kulalamika lalamika tu hasa watoto wakiwa hawasaidii kazi wanazungumza tu, na hawasaidii mzigo wa maisha. Gazeti la May 20, 2013 Times limezungumzia shida hii, si yako peke yako! Mtoto wa namna hii aweza kuwa na upweke au hana uhalisi wa maisha, na hata kama ameoa au kuolewa yuko hatarini kuharibu ndoa yake wakati wowote. Wazazi pia wasiangalie tathmini za watu kwa kulazimisha binti yao aolewe maana watu wanawauliza kwa nini haolewi na awapatia wajukuu!

9. ***Je, kuna uzuri gani wa watoto wangu watu wazima kuishi nami nyumbani?***

Wazazi wengine wanapendelea kuendelea kukaa na watoto wao watu wazima kwa vile wanapatana katika mengi. Siku hizi hata kupatana mke au mume ni kazi! Tunaishi katika dunia ambayo watu wamekosa uvumilivu. Kila mtu anataka kuishi mwenyewe na akiishi mwenyewe anapata upweke, na kuwa kwenye simu saa yote, au kutembelea watu saa yote! Akipata mteja wa kuzungumza hamwachii. Ila akiwa na mtu kwenye nyumba, anatasa kugombana saa yote.

Watoto wanaoishi nyumbani ni msaada kwa majukumu, kumaliza shule vizuri na hata katika maisha ya jamii. Wasichana na wavulana wengi wamejiingiza kwenye hatari za ngono kwa sababu ya kukaa wenyewe; wanatembelewa na mtu wa jinsia tofauti na kuanza mahusiano mabaya ambayo walikuwa hawakupanga. Msichana akiolewa akiwa ametoka kwao shida hii inapungua sana, labda amfuate huyo mwanamume nyumbani kwake. Mtoto pia anakuwa hana upweke, na kupata mashauri toka kwa wazazi kuhusu yule anayeolewa naye kabla hajakaa naye au hajamtembelea anapoishi.

Mzazi pia aweza kupata nafasi ya kumwona vizuri huyu mkwe au mkamwana. Majaribu pia yanapungua ya kufanya vituko akiwa kwa wazazi maana ana mashahidi wengi. Mtoto pia anazidi kupevuka na kupata mawazo mazuri ya hekima akiwa na wazazi. Jambo jingine ni kwamba, wazazi wakiwa na mahusiano mazuri na mtoto wanaweza kujadili shida zao na kuona waendelee kukaa namna gani. Watoto wanaweza wakapunguza bili za kodi ya nyumba na matumizi mengine ili wasaidie familia kitu kingine.

10. ***Ukiwa na watoto watu wazima na wakawa wana uasi nyumbani kwako uchukue hatua gani?***

Huu ni wakati mgumu kwa mzazi kumwambia mtoto aondoke. Mara nyingi mzazi anaumwa na dhamira kwamba pengine hakufanya jambo lisilo sawa. Na mahusiano yanaharibika kwa miaka mingi na pengine kidonda hicho kisipone. Kama mtoto anazidi kufanya uasi na ukaidi nyumbani ni vyema aondoke, maana anawatia huzuni wale wazazi mle ndani kwa kutofuata sheria za kimsingi, ambazo kila nyumba inazo.

Tabia ya kuishi katika dhambi za wazi wazi mfano madawa ya kulevya au ulevi, kuleta kimada na kuishi naye, na kufanya fujo za ugomvi nyumbani ni mojawapo ya vitu ambavyo itakuwa vizuri kuzungumza, kisha vikiendelea kuna haja ya kutengana kwa upendo ili mwendelee kuwasiliana mkiwa mbali. Mama mmoja alisema kijana wake alikuwa akileta rafiki wa kike na wanalala kwenye kochi lao sebuleni wakikumbatiana. Alimkanya kuhusu jambo hili na hakusikia, ilibidi wamwambie aondoke.

Kama wazazi, mna jukumu kwa lile linaloendelea nyumbani kwenu. Je, jambo hili, katika kesi hii, linamtukuza Mungu kwa imani yenu? Je, ukiwa na mtoto aliye na matusi au anapangua kila kitu kwenye nyumba utamwacha tu? Je, akiwa kupe na hataki kufanya kazi? Ni vizuri kumpa muda kama mwaka mmoja aondoke nyumbani, utashangaa atapata kibarua haraka! Ila usimtupe mtoto kwenye uhalifu zaidi ya alio nao; kama kuolewa mapema bila kupanga au kuingilia ulevi.

Lazima nyumba iwe na sheria na mawasiliano. Kukaa pamoja na kujadili mambo ya familia na kuishi ni muhimu. Jaribu kufuatilia sheria hizo kwako. Kama mtoto wako anakuwa na shida za kisheria na amewekwa jela kwa madawa au wizi msaidie aondokane na tabia hii; ila baadaye mwachie achukue majukumu ya matendo yake na kupokea matunda kwa tabia yake hiyo. Kumbuka wewe siyo Mungu uchukue majukumu ya uhalifu wake, itabidi aende ili uokoe jahazi la familia!

11. ***Je, tufanyeje ili watoto wetu wazima watuheshimu?***

Mzazi awe na upole, ukaribu upendo. Mtoto wako aliyetoka kwako akirudi pengine kufua nguo au kufurahia chakula cha mama mpe hiyo nafasi. Pia maneno yako yasiwe ya ugomvi na kutaka kuonyesha mamlaka yako kwake na kumwamrisha kufanya vitu. “Nipe pesa ya kununulia baiskeli, fanya hivi au vile.”

Tujue wao ni binadamu na kuna mstari wa kuongea na mtu bila kumvaa au kumwingilia usoni. Ni vizuri kukaa pamoja na kujadili badala ya kumshtukiza. Je, atumie vitu vya familia kama vyake mfano gari, baiskeli, au lazima aombe ruhusa? Weka sheria ili mheshimiane.

Mara nyingi tunawazingira watoto wetu mno tukiogopa kuwapoteza, kwamba wataenda mbali na fimbo zetu hazitafika kule na bado tunahitaji kuwamiliki!

Tumeona mfano wa mwana mpotevu kwenye neno la Mungu: Aliishi akimlaumu baba yake na baba hakutaka atoke. Alipomwachia alirudi wakaheshimiana! Jadili haya tunaona mfano wa mwana mpotevu aliyebaki nyumbani akisema baba yake alimpendelea yule aliyeenda, baba alijibu; “Sikia mwanangu, wewe u pamoja nami siku zote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena kufanya furaha na shanngwe ilipata kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka, alikuwa amepotea naye amepatikana.”

Mchukue mtoto wako na mjadili hili, ili mweze kuheshimiana. Mambo mengine si ya kuepa epa na kuinamisha nyuso yako kwenye mchanga tukifikiri yatajitatua. Epuka kuhadithia wema wa huyu mtoto na ubaya wa yule ukiweka maksi utapoteza wote na heshima yako pia. Kila mtoto ataka apendwe zaidi, usijiunge na kundi fulani.

12,***Ufanyeje ikiwa watoto wako wanarudi rudi nyumbani baada ya kujitegemea kutaka wakae nawe tena?***

Sijui nchi yetu ina watoto watu wazima wangapi ambao wanaishi na wazazi. Ila nchi ya Marekani ina watoto milioni kumi na sita! Watoto wengi wanarudi nyumbani kwa sababu ya ugumu wa maisha, yaani kukosa pesa au kuwa na talaka. Wanaporudi wanakuwa na familia. Kuanza maisha tena ya kuwapikia na kushugulikia wajukuu yahitaji kukaa pamoja ili kutatua pale wanapofika tu, na si baadaye.

Mama mwingine alilalamikia binti yake aliyekuja na watoto wadogo, akawa anawaacha na kwenda kutafuta wanaume na kuja usiku! Wazazi wakawa wanaogopa kumwambia maana wakimwambia aondoke, wajukuu wao watapata shida na mama kama huyu.

Wengine wameona kwamba kazi za kupika, kufua n.k zigawanywe ili mama huyu mzee asipate kazi ya kupikia watu wengi, kufua, kusafisha nyumba na kuosha vyombo. Je, una watoto ambao wakirudi hawachukui majukumu? Kaa nao uwaeleze, kama moyo wakuuma waambie uko tayari kukaa na wajukuu ila si wao. Ila wengine wakiona kwamba unawapenda sana watoto wao. wanasema wataenda nao ili wakuumize moyo.

Mababu na mabibi wengine hawapendi wajukuu wa mtoto fulani. Wengine wanawapenda na kuwashughulikia sana wajukuu wa msichana zaidi ya wale wa mvulana. Hawa ni rahisi kusema nenda na watoto wako! ila usiwanyime watu mema yaliyo haki yao, ikiwa yako katika uwezo wa mkono wako kuyatenda. Ila mababu/bibi wengi wamechoka kifedha, kihisia na hawana nafasi za kuweka hawa wote. Jiulize, je, umechelewa? Au kuna uwezekano wa kukarabati daraja? Zungumza, sikiliza na heshimu. Usipate hofu. Siku ya hofu yako umtumaini Mungu.

13.***Je, mtoto afanye kazi kiasi gani kwa siku?***

Ni vyema mtoto afanye kazi ila kuwe na balansi, siyo siku nzima ya kazi na wala hamna mchezo. Mtoto wa miaka minane ajue kufua nguo zake vizuri na asimamiwe. Kuwapa wanyama chakula, kufagia, kusafisha chumba chake na shughuli chache za jikoni. Asikae kwenye Tv au kupiga tu gumzo. Lazima ujue mtoto wako yupo wapi.

Simamia au fuatilia kazi ulizotoa kama zimefanywa, usipofuatilia utakuwa umepoteza somo. Usiseme huna nafasi. Mtoto anajifunza kazi vizuri ukimsimamia. Hii itamfanya awe mfanyakazi mzuri akiwa na wenzake au mume/mke bora. Magomvi mengi yametokana ya kuishi kivivu. Asiyefanya kazi asile. Kwa habari zaidi, angalia doorposts.org pam Foster au Rb Bradley(nogreaterjoy)website

14.***Je, mtoto asipopenda kula alazimishwe?***
La! Usimlazimishe mtoto kula kama si mgonjwa! Mara nyingi shida hii ipo kwa wale wenye chakula kingi, na mtoto anakiona saa zote, na kula kula tu siku nzima! Mtoto asile vitu vya sukari na kupishanisha muda wa kula, ikifika wakati wa kula atakuwa na hamu ya chakula. Mara nyingi mtoto anaishiwa hamu ya kula wakati wa kipindi cha miaka ambayo hakui sana. Jaribu pia kujifunza mapishi na kile anachopenda ukiweza kama kinafuatana na milo ya afya tuliyozungumzia, mpe.

15. ***Je, wapaswa kumwomba mtoto wako msamaha ukimkosea?***
Ndiyo. Mara nyingi imebidi niwaombe watoto wangu msamaha kwa kuwa na haraka au hasira na kusema nisichopashwa, au kuwahahidi kitu nisifanye, au kuwalaumu kwa kosa ambalo hawakufanya. Nikifikiria baadaye au wakati wa kulala nikikumbuka na kuwaomba msamaha: “Jana nilifanya hivi kwa makosa, unajua mzazi ni binadamu tu naomba unisamehe.” Mara nyingi watoto wamesema, “Tunajua ulikuwa umekosea, ni vyema umeomba msamaha, tumekusamehe.” Na wote tunafurahi sana.

16. ***Je, nifanyeje kama mtoto wangu bado anakojoa kitandani na ni mkubwa?***
Kwanza usimwadhibu, hakuna anayetaka kukojoa kitandani kwa makusudi, utaleta shida zingine zaidi. Panga uwe unamwamsha usiku saa fulani. Waweza kutumia saa zenye kengele. Asinywe maji masaa kabla ya kulala. Dawa za asili kama pia zimetumika. Kumbuka ni shida ya watoto wengi hasa wa kiume, na mara caribú zote haihusiani na ukosefu wa nidhamu. Itakuja kuisha siku moja, ila utaona “ni siku nyingi mbona haiishi”

17. ***Tuna watoto watatu na tuko busy, tunajaribu kutafuta muda tunashindwa, je, tufanyeje?***
Mtoto anajaji upendo kwa muda mnaotumia kuwa nao. Kwa vile mlilewata watoto duniani, tafuteni muda. Ni vyema mama akae nyumbani kama imeshindikana kabisa. Tafuteni jinsi ya kuziba hili pengo. Mtu atakayepoteza ni mtoto maana anajenga tabia na ustadi. Watu wanaweka list ya vitu vya kufanya ila kushugulikia watoto kunachukuliwa kwamba si kitu cha kutiki, kwamba ni wajibu tu. Ni vyema kuwa na desturi ya vitu ambavyo mnafanya pamoja, kama kula pamoja, kuenda ibadani, kwenda kwenye sherehe au likizo. Familia ni zaidi ya kuishi chini ya paa moja! Ni vizuri kuweka vitu vizuri kwenye program kama mzazi ili uweke vizuri zaidi. Hii haina maana usiende ibadani ila angalia usiseme utafanya kila kitu kwa ndugu jamaa na rafiki na kusahau watoto wako. Twaambiwa kwamba tukiwakosesha watoto ni jambo kubwa “ imepaswa kufungiwa jiwe kwenye shingo na kutupwa majini”. Kumbe jukumu letu wazazi ni Kubwa mno.

Baba mmoja aliyekuwa busy sana, alikuwa hana wakati wa kukaa na watoto wake. Watoto walitamani sana wapate muda wa kubarizi na baba yao. Siku moja alipokuwa bafuni, wakachukua diary yake, wakaperuzi waone kama kuna siku moja free. Walipoipata wakajibukia appointment, wakaandika “Siku ya kutembeza watoto.” Ninadhani baba

alikuja kuiona baadaye, lakini hakusema cho chote. Basi watoto wakipata nafasi, kama hayupo, walikuwa wanacheki kuona kama appointment yao bado ipo. Wakawa wanafurahi na kujiandaa; hadi siku mbili kabla, walipoangalia walikuta baba amekata na kalamu nyekundu na juu yake ameweka appontiment nyingine! Watoto walivunjika moyo sana.

18. ***Mtoto wangu wa miaka kumi na minane alitoroka nyumbani na tabia yake si nzuri, nifanyeje?***

Ni vigumu kusema kitu utakachofanya kama jambo kama hili likitokea. Pengine bila ya kumgombeza na kuropoka ropoka maneno mabaya, mwite na ujaribu kumwelekeza na kumtembelea Kama akikataa, si vizuri kwa mzazi kuwa dikteta kwa mtu wa umri huu; itampa uasi zaidi moyoni. Kwa vile ni mtu mzima, akiwa na shida wazazi waweze kumsaidia alipo, jinsi wanavyoweza. Kaa naye umweleze matokeo ya tabia hii na matokeo ya tabia njema; yeye afanye uchaguzi.

Mwana mpotevu alitoka kwa baba yake na baba alimwachia nafasi apumue anavyopenda, alipozinduka toka kwenye tabia mbaya alirudi mwenyewe na kupokelewa kwa shangwe.

19. ***Mnavyoandika kitabu cha malezi; Je, nyumba na watoto wenu wako shwari?***

La, hasha! Ni vita vya kila siku, ila kuna haja ya mtu kuandika na sisi kama wazazi tusaidiane; lile unalolijua utuambie ili tufaidike na lile tunaliojua tutakwambia. Hakuna mzazi mkamilifu. Ila tunajaribu kwa neema ya Mungu.

Kila binadamu amefanya dhambi tunaokolewa kwa neema, naona siku nyingine kwangu ni kama kimbunga kimepita; tunakuwa kama bisi tukingona hapa na pale, na nakosa nguvu kwamba nitaendeleaje na shughuli ya uzazi? Mungu ndiye Atupate nguvu sisi wote. Endelea kujisomea ili ujue zaidi. watu wengine waweza kukufanya uone kama umeachwa na basi kwamba wanaendelea vizuri ila kila mtu ana mizoga yake. Wewe mwangalie Mungu na jifunze zaidi jinsi ya kufaulu, atakuwezesha kwa yote na kukutia nguvu. Mlilie, mwambie kama Yakobo kwamba, “Sitakuacha mpaka unibariki.”

20. ***Tuna shida ya pesa kwenye malezi ya watoto, tufanyeje?***

Kwa kweli mimi si mataalamu wa ujasiliamali au biashara, ila kuna haja ya kutafuta wataalamu na kujifunza, kisha mitaji. Na kama kuna uwezekano wa kurudi shule kuongeza nafasi za kupata kazi fanya vile. Kama una ardhi lima. Nimeona mahali pengi kama Tanzania, kuna ardhi; wengi wangelima na kukabiliana na maisha ila uvivu unakuwa mwingi. Shamba ni mali. Fanya kazi kwa bidii angalau masaa manane kwa siku, na endelea kuomba.”Kila aombaye hupewa, kila atafutaye hupata na kila abishaye hufunguliwa.”

Jihadhari na tamaa na ulafi. Je unataka uwe na vitu kama watu wengine, au ni mahitaji ya kawaida? Je, waweza kupunguza matumizi yako kwa kununua nguo za mitumba, kulima au kufanya vibarua vidogo vidogo? Je, wajua kupanga bajeti ya nyumbani? Jifunze. Je, kuna mashirika yanayotoa misaada fulani, kama kusomesha watoto? Peleleza utapata habari na maarifa ambayo hukuwa nayo.

Mkopo uje kama jambo la mwisho, labda kwa ajili ya mtaji. Epuka madeni kama ukoma, uwie watu upendo. Ila wakati mwingine waweza kupata mkopo au ruzuku ili uweze kuongeza kipato. Usizoee kutumia credit card! Ishi maisha rahisi, nimeona hata nchi maskini watu wakijenga majumba makubwa ya kutisha, yenye vyumba vingi, watoto wakienda mtu abaki kufuta vumbi. Hata wale wanaompenda Mungu wameingia ansa hii ya vitu (stuff).

20. ***Hivi kuna faida gani ya kuwa na watoto, maisha ya kulea siku hizi ni magumu?***

Ni kweli uzazi ni gharama na kifurushi chenye mengi magumu. Mwenyezi alitupa amri tuzae na kuongezeka. Tuliumbwa hivi. Mwulize yule anayetamani kuwa na mtoto, utakuwa na picha kamili. Ni kweli uzazi na kulea si kazi rahisi' ila katika jamii zinazopenda kuwa na watoto sana ni Waafrika; hata kufikia hatua ya kuachana kama mke hazai! (Si mume asipozaa!). Kwa walio na watoto wanaojuta ni wachache sana. Wengi mlipenda mzae na mmefurahia watoto wenu.

Jiulize, hivi Mungu Mwenyezi, alituumba kwa sababu gani? Ili tumsadie kazi? La. Ni kuonyesha upendo na utukufu Wake. Wengi wamepata faida kuwa na watoto. Angalia yale mema ambayo watoto wanakutendea hata kama hawakupi kitu. Watoto ni urithi toka kwa Bwana, anatupa kama zawadi kwetu. Wengi nchi zingine wameamua wasizae na hilo kwa nafasi chache ni sawa, zungumza na mwenzi Wako akikubali. Hata hivyo maisha ya Manabíi kama Henoka waliweza kumwelewa Mungu zaidi walipokuwa wazazi na kujua upendo wa Baba Mungu, kuna Vingi tunavyojifunza kama wazazi, mfano uvumilivu, kutojifikiria, upendo n.k. baada ya kuzaa tabia zangu mbovu zilijitokeza zaidi, naomba Mungu anisaidie niziungame na kuziacha.

22. ***Kuna haja ya kumfundisha mtoto mambo ya imani? Je, haitakuwa kama kumlazimisha?***

Ni muhimu sana mzazi kumfundisha mtoto hasa kwa muda unaofaa wa utoto. Mema na mabaya na amri za Mungu lazima zifundishwe, na mtoto akikua anakuwa na uchaguzi mwenyewe. Mtoto anazaliwa na uchoyo na kujifikiria anakuwa na mawazo ya kumfuata Mungu na kumfuata shetani. Mtoto anazaliwa katika pambano la wema na ubaya. Hazaliwi akiwa mzuri; ila pagani. Hivyo anafundishwa kumjua Mungu. Ni kumrithisha mtoto umasikini usipomweleza kuhusu muumba wake.

Miaka saba ya mwanzo mfundishe mtoto upendo wa Mungu, neno la Mungu, kuomba, nguzo za imani, furaha ya kumjua Mungu, imani na uzuri wa Mungu. Ampende Mungu na jirani, ajikane na kutawala nafsi pia kutii (submission). Asiwe mchoyo, asiwe msengenyaji na tabia zile mbovu. Atii wazazi. Amheshimu na kumtii Mungu katika mali yake, kusujudu, kutokuwa na kiburi, uaminifu, kutunza siku ya Bwana, kutokuwa na tamaa ya mali n.k.

23. ***Unaonaje kuhusu TV; Je, wazazi watawale mambo ambayo watoto wanatazam?.***

Asilimia kubwa ya TV ni mambo yasiyosaidia kabisa. Maoni yetu ni kwamba, kama utaweza kuitoa kwako itasaidia! Au uwe na mikanda ya kusikiliza maana hata matangazo ya biashara yanaanza kuwa na watu waliovaa nusu nusu, ujangili,ukatili, uovu au kukosa adabu.

Watu wameona kwamba ukatili mwingi unaongezwa na watu wengi kutojithamini. Historia ya Hitler wa Uerumani ni mfano mzuri, alitaka kuwabamiza wengine kutuliza hasira zake. Shetani amejiinua pembe zake akitaka ateke watoto wako na kuchukua muda wa familia yenu na pengine hata afya zenu. Kama unataka kushughulikia TV sana, chukua kalamu na karatasi uandike programu zote, unazotaka watoto waangalie, na uwepo kuona yametimika hayo matakwa yako.

Nchi nyingine zina channel mia tisa! Watoto wanaamka usiku wazazi wakiwa wamelala na kutazama mambo ya ajabu! Vikatuni vyasema maneno ya watu wazima na matusi. Pima haya kwa makini na zungumza nao. Pata ushauri pia. Usiwe dikteta.

24. ***Mimi ni kijana wa miaka kumi na mitano, nimeambiwa nitakuwa na mabadiliko ya kimwili ila siyaoni! Ni yapi hayo?***

Yatakuja tu, subiri. Mifumo mingine ya mwili yaweza kuwa na hitilafu hapa na pale ila mfumo wa uzazi ni nadra sana usifanye kazi. Kuna tezi yaitwa pitituary gland ndani ya ubongo wako, ambayo ina ukubwa kama harage. Hii ndiyo Bosi (master gland) ya tezi zote; inaongoza tezi zote na hata ile ya uzazi kufanya kazi. Mtoto asiyefahamu, kama msichana aweza kufikiri ni uvimbe. Mwili unajitayarisha kwa uzazi. Mwili utaanza kukua upesi (rapidly). Nywele kutokeza kwenye kwapa, na kwenye sehemu za siri. Nywele hizi, zinasaidia kupunguza unyevunyevu na harufu. Misuli kujengeka zaidi kwa wavulana, sauti kubadilika, ndoto nyevu na ndevu huota. Viungo vya uzazi vitakua.

Mara nyingine katika kupevuka uchovu unatokea kwa ajili ya mabadiliko mengi, pata usingizi vizuri angalau kwa masaa manane. Kula vyakula bora.

Kwa wasichana maziwa hukua, kuvunja ungo,, damu kutoka kila mwezi kupitia uke, kila baada ya wastani wa siku ishirini na nane. Hii ni kutayarisha mimba kutungwa na isipotungwa damu inatoka baada ya mishipa kubomoka na kutayarisha mfuko wa mtoto tena kwa mwezi ujao.
Mabadiliko mengi hutokea baada ya miaka kumi na miwili kwa wasichana, na kumi na minne kwa wavulana. Japokuwa nyama na maziwa siku hizi yana vichocheo vingi (hormones) ambavyo hufanya mwili kukua haraka na kuleta mabadiliko kwa watoto pungufu ya miaka kumi!

Usafi wa moyo na ngono ni muhimu (purity ya mawazo, matendo na maneno)Wengi wanaogopwa kuchekwa hasa wasichana wanakuwa na aibu, self conscious, la, hasha hautachekwa. Hakuna ambaye anafikiria mambo yako sana. Ila mzazi au mlezi, ni vyema kwa maarifa na vifaa, akupe pamba ili ujitayarishe kujitunza vizuri ili nguo zako zisichafuke. Pia akufundishe namna ya kuweka hiyo pamba, kubadilisha na mahali pa kuitupa na usafi kwa jumla. Usiitupe kwenye vyoo vya kuvuta. Kwa wavulana, wembe wa kukata ndevu na kadhalika.

Wengi waweuliza kama wanaweza kupata mimba bila ngono. Kamwe haiwezekani. Labda hospitali wanaochukua mbegu ya wanaume na kuipandikiza, kama inavyokuwa kwenye ngombe wa kisasa . Kuna hofu za kupevuka; hebu mzazi/mlezi ujadili jambo hili

kwa undani zaidi. Tawala tamaa zako, japo umepevuka si wakati wa kuwa na rafiki wa jinsia nyingine (boyfriend/girlfriend). Jihadhari na urafiki wa namna hii uwe wa wazi au siri. Tumia nguvu na mawazo yako zaidi kujifunza kazi, maarifa na ustadi na kumjua Mungu. Chagua marafiki vizuri, wanaomcha Mungu. Usisikie dhamira kukushitaki ukifikiri ngono 'hapa na pale' ni kawaida ila usiweke mawazo yako katika hayo. Ikifika wakati wake utakuwa wa kawaida tu na wala si rahisi kuwa na dilema wa nyanja hii.

Wengi wanaona aibu kutoa nguo kwenye ofisi ya tabibu, mara nyingi huna haja ya kuogopa na kama unataka mzazi wako aandaamane nawe fanya hivyo. Zawadi kubwa utakayompa atakayekuoa au utakayemwoa ni ubikira wako uwe mwanamume au mwanamke. Usafi wako wa mwili ni muhimu sana. Zaidi ya asilimia sabini ya vijana wamefikia siku ya ndoa wakiwa wamefanya ngono na watu wengine! Ila Mungu ni mwenye huruma sana anatusamehe pale tumekosa, ila tuanze safari mpya ya usafi/uaminifu wa moyo, matendo na maneno..

25. ***Nina mzazi ambaye anakuja kwangu na kutaka kuendesha nyumba yangu, na jinsi ninavyolea watoto wangu. amekuwa mzigo moyoni mwangu. Nifanyeje?***
Kila nyumba ina shida zake. Jaribu kumzungumzia, na muweke mipaka. Wewe na mume Wako mjadiliane na kumwambia kwa upendo, kama anakaa nanyi nyumba moja, basi ni bora mtafute jinsi ya kumsaidia ajitegemee,

26. ***Nina umri wa miaka 14, na napenda kuvaa kama wengine wa rika langu, ila wazazi wangu wanasema kwamba ni muhimu niangalie kama mavazi haya ni ya adabu, ya kumweshimu Mungu na watu. Naonekana kama nimeachwa na basi na fasheni hizi za kizee!***

Mara nyingi tunapungukiwa na kujithamini kwa kujifananisha na watu wengine. Unajali ukichekwa. Utakapokuwa mtu mzima, haya yatapotea kwa kujua kwamba hakuna anayetaka sana ufanane naye, na pia unahitaji kuwa na msimamo au uti wa mgongo kwa mambo mengi! Huwezi ukawa unakopi yale yasiyo mema kwa vile unataka kufanya kama wengine! "kila mtu anafanya hivyo." Acha 'everybody' afanye, wewe siyo 'everybody.'

Jifunze kujitegemea na kwa kutofurahisha watu kwa mabaya bali kwa mema. Pata maarifa ya kupata marafiki wema, sio lazima wale mashuhuri, ila wale wa tabia njema hata wakiwa wachache au bora kukosa rafiki kuliko kuwa na rafiki wabaya.

28. ***Nina binti wa miaka kumi na saba. Anataka kuvaa sidiria ila hana maziwa; je, nifanyeje?***
(jinsi ya kushugulika na matatizo yanayopata watoto).

Kwa vile anataka kufanana na wengine, au kuwa mtu mzima na anapata hofu kwa mabadiliko ambayo hayakuja kwake haraka kama inavyotazamiwa. Hamna ubaya kumnunulia avae. Wakati huu mtoto anakuwa hajiamini, au kujipunguza thamani. Wengine wanajiona wanyonge au kujiona amekataliwa na rafiki zao, na hukata tamaa.

Mzazi afundishe watoto kujithamini maana mara nyingi watoto wana ukatili wa maneno na kucheka wengine. Mfundishe jinsi ya kujitoa kwenye moyo uliopondeka, mwonyeshe kwamba anapendwa na kuthaminiwa nyumbani. Mtoto ajue pia kwamba hawezi kufuata wengine katika kuvunja amri au kutotii. Kumbuka, kama mzazi huwezi ukawatatulia matatizo yao yote. Wajifunze kutatua shida za mazingira yao. Mtoto anakuwa na magumu kiasi fulani ambayo anaweza kutatua. Hutamrukia viunga vyake vyote!

Miaka ya viunga inaleta mtoto kukomaa, kuwa mwenye uvumilivu, huruma, ushujaa, ushindi. Mti usio na mizizi unaanguka kirahisi upepo au mafuriko yakija. Watoto waliojifunza kutatua matatizo wanakuwa na ulinzi (security). Huko kutoa matatizo yao yote, ila kuwatia moyo, kuwakinga katika madhara makubwa, kuwapa nyenzo za kuruka viunga na kuwaonyesha uko upande wao.

29. ***Nitajuaje kama mtoto wangu atumia madawa ya kulevya?***

Ataonekana kuchoka na kukosa malengo (ambition), kuzorota kwa kazi ya shuleni, kutotilia makini vitu, kutowasiliana na familia au wenzake kwa ufanisi. Kutojali hisia za wengine, sura kubadilika, kama macho kuwa mekundu, au macho kucheza cheza, kutojali usafi wake, na kubwatika kwa kuonywa mambo madogo madogo. Pia atapendelea kukaa mwenyewe wakati wote, kuwa na marafiki ambao hataki wajulikane, kula mno, magomvi, na kuwa na harufu ya vileo. Maadili huvunjika, pia anakuwa na alama za sindano kwenye mwili, kuwa mtu wa siri kupita kiasi, kupotea kwa pesa au vitu vya thamani nyumbani na anaweza kuharisha.

Watoto wengi wameshajua madhara yake ila endelea kuwaambia tu na kuendelea kutafuta ufumbuzi. Zungumza nao kuhusu msukumo wa rika pia, na kuwa shujaa wa kusimama peke yake siku moja! Mzazi uwe mfano, ili nawe usiwe na msukumo wa rika, wa kuigaiga na kutaka kuwa na vitu kama au kuvaa kama watu wengine. Kuna watu wazima wengi ambao bado, wanataka kufanana na watu fulani. Hebu tuige mfano wa mashujaa waliosimama wenyewe, maana kuna wakati ambapo inabidi usiende na kadamnasi.

30***. Mtoto wangu anapenda kukusanya miti, mimea, wadudu na wanyama, nifanyeje?***

Akiviweka chumbani kwake, kwa unadhifu na bila kuleta madhara au harufu mwache aendelee, kwani huu ni umri wa kukusanya vitu. Ataokota kila kitu anachopata njiani, kama makopo, waya, vifuniko vya chupa, n.k. Mpe box awe anaviweka au mwelekeze mahali pa kuviweka. Kamwe, usivitupe.

31. ***Binti yangu wa miaka kumi na sita, ambaye hajaolewa, ameniambia ni mjamzito nifanyeje?***

Binti yako anakuhitaji sana sasa kuliko awali. Uwe mwenye upendo; kaa mzungumze. Siyo wakati wa kusema "Nilikwambia;" na kugomba ovyo ovyo. Mara nyingine mahusiano yenu yaweza kujengeka baada ya hii shida kuliko awali, mkashikana zaidi. Aliyekosea mara nyingi huwa mnyenyekevu. Msaidie na mwenzi Wako (mume/mke) mambo ya kutunza mtoto na arudi shule kama anaweza, ili aweze kuwa na riziki njema zaidi baadaye. Mkae na kuzungumza kwa undani, baada ya kujifungua; kwa maana tabia hii imeonekana kujirudia kwa wasichana wengi, hata wanapataa watoto kadhaa nyumbani kwao. Akiwa mtu mzima ana uchaguzi wa usafi na kutunza amri, ila achukue majukumu ya kutunza watoto wake. Baba wengi wamekuwa na magomvi na wake zao "unanificha mambo ya binti, mlifanya naye mipango ya kupokea mahari eh?" Jaribu kuyaweka wazi kwa mume Wako, na muwe na rehema.

32.***Umesema kupiga mtoto wa umri wa zaidi ya miaka kumi na miwili si vyema, apewe adhabu gani basi?***

Angalia kwenye mambo kama posho ya pesa (pocket money) na mengineyo ambayo waweza kuyapunguza. Pia unaweza kumground mahali kama kwenye chumba chake, au nyumbani, umwambie asitoke kwa muda fulani. Adhabu hii ni nzuri kwa watoto wa rika hili. Angalia hata wale wadogo sana inabidi kuwaadhibu bila kuponda roho zao (damage spirit). Elezea mipaka vizuri (define boundaries). Usifoke kwa kumwaibisha; "Mbona maksi zako mbaya kuliko za mdogo wako," au "mtoto mjinga hufai kitu."

www.ngj.org au soma gazeti la No Greater Joy.

33. ***Binti yetu amekuwa akiona aibu siku hizi; akivaa huwaambia dada zake watoke chumbani!***

Mabadiliko ya mwili yafanya atake faragha (peke yake) mpe nafasi, mara nyingi ni kitu cha muda mfupi tu.

34. ***Je, watoto wanapevuka mapema siku hizi?***

Ni kweli; kwa urefu na mabadiliko ya mwili. Katika nchi ya Marekani, miaka ya 1850, mtoto alivunja ungo akiwa na wasitani wa miaka kumi na saba. Miaka ya 1950 wastani ukawa miaka kumi na mitatu, na sasa ni wastani wa miaka kumi na miwili.

35. ***Mtoto wetu wa miaka kumi na mitatu anaona aibu kuonekana nami mzazi, nimemzaa na kumlea na kumtumikia maisha yote na sasa ananionea aibu hasa akiwa narafiki zake! Je, nikubali hili au nilipinge?***

Miaka kumi na mitatu hadi kumi na minne ndiyo migumu sana. Watoto wa umri huu wanapenda mno kuonekana kama ni watu wazima, na wanajitegemea na huona aibu

kuonekana na wazazi. Lione jambo hili kama la kawaida katika kipindi hiki; labda kuwe na harari. Mahusiano yako na mtoto yatarudi. Japokuwa si kama yale ya utoto udogo.

36. ***Je, nivae na kuzungumza kama mtoto wangu teenager ili aone kwamba namwelewa?***

Hakuna ujinga kama wa kujifananisha na mtoto ili uonekane unamwelewa. Je, mtoto wa miaka miwili akijiangusha, nasi tufanye vile? Waweza kuonyesha uelewaji wako kwa kumkubali kwa njia nyingi tofauti. Kwanza yeye anataka kutofautiana nawe, awe pekee. Ukianza kumfuata ataabadilisha staili! Usimwigize, bado anahitaji mamlaka yako, na wewe ndiwe mwenye kumwongoza! Hatufuati mfano wa watoto, ila watoto ndio waige mzazi ambaye naye amwige Mzazi MKUU yaani MUNGU. Hii inamaanisha maagizo, amri, mausia na shuhuda za MUNGU.

37. ***Mtoto wangu wa miaka kumi na minne ameanza kutuonyesha wazi wazi, kuvunja sheria na kuchukia familia. Anatuchukia tukimwadabisha. Anakuja amechelewa bila kuomba udhuru, tufanyeje?***

Ni vyema umchukue kando siku tofauti na anapoanza vituko. Nenda naye kutembea, mfano, kwenye kiwanja, mgahawa n.k. Mwambie kwamba una mambo dharua ya kuongea naye. “Naona mabadiliko yanatokea nyumbani, umekuwa na hasira, ujeuri, mimi na mama yako tunajikuta pia tunafadhaika na kukemea. Huu si mpango wa Mungu kwetu au kwako. Je, kuna njia bora ya kutatua haya matatizo?, Ndiyo maana tuko hapa leo.” Mweleze unajua mabadiliko ya mwili wa ujana, kuna misukumo. “Umeonja uhuru na unataka kula, kutembea, na kuvaa unavyotaka. Tunajua unataka kuwa bosi wako mwenyewe na watu wasikuingilie. Muda si mrefu utakua, utajitegemea na utaoa. Kwa sasa hujakua bado. Kwa miezi kadhaa umetaka kutuonyesha na mama yako, kwamba umekua, na hutaki kusoma, kufanya kazi au kuja wakati unaotakiwa. Ni rahisi kwetu kukuacha ufanye utakavyo, ila tunajua tutajuta nawe pia utajuta. Una wadogo zako wanaokungalia na kuiga mifano ambayo itaharibu maisha yao ikiwa tutaacha ufanye utakavyo. Sisi tu mawakili wa Mungu soma 1 Sam 12: 22, 25:27 –34. Mungu alimwadhibu Baba Eli na watoto wake kwa sababu ya tabia yao mbaya.” (Angalia kwenye neno mifano mingi mingine).

“Mungu hatatuhesabia kwamba hatuna hatia kukuachilia vile. Nataka utuahidi kwamba utakuwa mwangalifu kwa mambo haya; 1, 2, 3, nasi tuendelea kuwa waangalifu kujali maslahi yako. Utakapohitaji kitu na kutuuliza tutaangalia kama umekuwa mwangalifu kuyafuata haya. Tunajua wewe ni mtu mzima na kwamba hatuwezi kutumia kiboko, ila kuna mambo ambayo hatuwezi kuyaachilia; (cant be compromised); hata kama ukipiga kelele na kufanya ujeuri. Hutaki tukae usiku mzima tukipembua njia za kukufanya ukose raha, maana zipo!”

“ Nahitaji kufanya kazi yangu kwa umakini hii miaka michache ambayo upo nyumbani. Ni juu yako sasa. Twaweza kuwa na amani ukishirikiana nasi na kufanya miaka michache uliyobakiza kuishi nasi iwe ya amani. Yabidi urudi nyumbani mapema, kujituma kazi na kumweshimu mama yako na mimi. Tunakupenda kuliko unavyoweza kufikiri. Tunataka kudumisha urafiki kwenye dunia ya machungu mengi. Hayo machungu mengi hujayafikia ila kuna siku lazima utayaona, tunahitajiana (we need each other).

Tunakuhitaji, na hata nawe, amini usiamini watuhitaji hapa na pale. Tusaidie, tukusaidie tusidondoshe mpira." Kisha muulize;
"Je, una lolote la kutuambia?" Mpe mtoto muda afikiri. Hata kama kijana wako awe na hasira au asijibu, umemweleza hali ya hewa na mategemeo yako. Yawezekana kuwaelekeza vijana bila kuwazungumzia kwa ujeuri. Kuwa mwema kwake, na mwelezee wigo.

42. ***Kwenye mazishi ya mjomba wa watoto wangu watoto wameniuliza kuhusu mauti, niwajibuje?***
Neno la Mungu limetuonyesha kwamba mtu akifa analala kaburini kungojea ufufuo. Martha, dada yake Lazaro alisema, "najua siku ya mwisho lakini sasa ananuka yangu ". Jitahidi kumweleza mtoto ukweli , na kama hufahamu mwambie unapeleleza au hufahamu. Martha Akajibiwa na Bwana "MIMI ndiye ufufuo na uzima!" Bwana akija na parapanda ikilia, makaburi yatafunguliwa na wafu watatoka makaburini, na wala si mbinguni, kisha watapaa kumlaki YESU mawinguni. Neno la MUNGU halisemi YESU atakuja na jeshi la wale waliokufa na kuwa huko mbinguni, bali linasema atakuja na jeshi la malaika.

Bwana Anakuja afufue, kama wako mbinguni tayari, hakungekuwa haja ya kuja. Huu ni ufufuo wa watu wenye haki. Kuna ufufuo wa wale waovu ambao wataenda jehanam kwenye adhabu ya moto uchomao na kuwateketeza. Mungu hajaahidi uzima wa milele kwa waovu kwamba wataungua milele! La hasha, wataungua na kuteketea.

Ni vyema mtoto ajue kuna mshahara wa dhambi na wema. Mtoto apewe nafasi ya kulia, umtulize ila asiambiwe usilie uwe shujaa, kwani imeleta makovu au vidonda vya muda. Atalia kwa siku kadhaa au hata baada ya miezi, hapa na pale aruhusiwe kulia. Mtoto mdogo ni vigumu kumweleza kuhusu mauti, hata watu wengi wazima hawajui vizuri neno linasemaje kuhusu mauti. Ndiyo maana tumeamibiwa ni fumbo(mystery).

Ni vizuri mtoto aone maiti ya mzazi wake anapozikwa, japo watoto wadogo sana wanakuwa na hofu na kuota ndoto za kutisha usiku. Utapima kama mzazi. Mtoto akingwe na watu wengi wanaopiga mayowe makubwa kilioni kama inawezekana maana inajenga mfadhaiko mwingi. Mtoto aweza kuona yule aliyekufa amemtelekeza, au akasikia dhamiri inamshitaki kwamba yeye ndiye aliyemwua hasa kama alimkasirikia. Msaidie kumweleza mtoto yeye si sababisho la kifo. Mtoto ajue baada ya kifo hakuna nafasi ya kuungama ni mwisho wa maamuzi.

43. ***Mtoto wangu anakuja toka shuleni akilia kwamba amepigwa na watoto wengine. Je, nimwambie ajitetee kwa kuwapiga pia?***
Ni vyema umwambie mtoto wako asiwe na tabia ya kupigana katika mchezo. Watoto wana uchoyo na ukatili mara nyingine, kwa kuwatenga wenzao na kuwasema kwa wazi, kama wana kilema au maumbile tofauti. Watoto wanajipenda, wanalimbikiza vifaa vya kuchezea kwao. Kwa vile bado ni mdogo, mwambie vitu vingine ajihami. Na akipigwa au kuchukuliwa vitu vyake, amwambie mwalimu ili aliyefanya hilo ashugulikiwe. Watoto

wenye ukatili kama wale “bullies” angalia website breakingsilencenow; ni vizuri washugulikiwe ili wasizidi kuhangaisha wengine!

Ikiwezekana watoto hawa wapigwe au kuchapwa na wanafunzi wenzao ili wakomeshe tabia hii! Na kisha mwalimu aishugulikie. Mtoto anayependa kupigana atakoma ujinga! Cha muhimu mzazi asisitize ubaya na ujinga wa kupigana ila asimwache mtoto mdogo akipigwa bila kujitetea au kutafuta haki. Watoto wengine wenye nguvu, kwa ajili ya “bullies,” wamejifunza karate na mengine ili kuondoa unyanyasaji huu.

43. ***Unafikiri watoto wa miaka mitano waachwe wasikilize muziki wa rap na rock?***
Kwa kweli muziki huu ni mbaya sana kwa ye yote, hata mtu mzima asisikilize. Angalia sura ya muziki na tabia. Tabia mbovu zimezaana kutokana na rap na miziki na sampuli zake. Kwa vile shetani alikuwa mwanamuziki mbinguni, ameshugulikia binadamu wapende muziki wake wa uovu. Miziki hii hatukuwa nayo kwenye tamaduni zetu za kiafrika. Hata mambo ya dansi mengi yanakita kwenye uasherati. Hata ngoma za kiafrika zilikuwa za heshima na si za kudansi mwanamke na mwanaume wakiwa wamekumbatiana 'milimita moja'. Je kuna mtu angependa mume wake au mke washikane na mtu namna hii?

44. ***Baada ya mambo yaliyotokea Rwanda ya ukabila ya watusi na wahutu na makabila yetu mengine, nifanyeje ili mtoto wangu asiwe na ubaguzi?***
Hakuna litakalosaidia watoto kama mfano wako unavyowatendea wa makabila mengine. Kuwabagua au kuwajali wale walioumbwa kwa mfano wa Mungu. Ubaguzi karibu wote duniani, uwe wa rangi au wa kabila unarithiwa kutoka kwa wazazi, na mara zingine unahusiana na mali, yaani kubagua masikini. Watoto wetu wanatutazama kwa makini, na kufuata nyayo zetu. Mama mmoja wa kizungu aliniambia kwamba siku moja walipoenda kuogelea kwenye bwawa, na waliporudi nyumbani, alimwuliza mtoto wake “mmeonaje kuogelea na watoto weusi” watoto walijibu “kulikuwa na watoto weusi pale?”. Kwa maana nyingine watoto hawakujali rangi waliona ni marafiki tu na wakaendelea na michezo. Kwa upande mwingine watu weusi nao wanawashuku wazungu kwamba wana ubaguzi hata kama hawajakaa na mtu au kufahamu nia yake. Ni dhambi kushuku watu kwa yale usiyo hakika nayo. Mama huyu alisema alipata fundísho. Watoto wadogo waweza kuonyesha dharau kwa kutojibu watu wakiwasalimu au kuonyesha ubaguzi kutokana na wanayoona nyumbani. Hata ubaguzi wa jinsia “dada zako watakuoshea nguo zako na kusafisha vyombo, wewe ni mwanamume hapa” anaambiwa mtoto wa miaka nane. Kuna ubaguzi wa dini pia wa kuona sisi ndiyo tuna ukweli wote au wengine wanahitaji kufa sisi ndiyo tuishi maana wao ni waovu. Kuna ubaguzi kwa wazee kwa kuwasononesha na kuwatupia maneno. Moyo umejaa mengi na tunayaleta kwa matendo na maneno yetu. Tusifikiri ubaguzi wa rangi tu bali hata makabila, je tunatenga makabila fulani? Je tunawasema vibaya? Fundisho la Rwanda lilikuwa zito, na limetokea zaidi ya mara moja, hebu tujifunze kujua, tu familia ya Mungu. Somo hili ni refu,ila anzia kufuta ubaguzi nyumbani mwako maana mbali huko utafika baadaye.

45. Nakuza watoto wawili wa kiume mwenyewe kama mama je watu wa imani yangu wawezaje kunisaidia?
Kwa kweli kila anayempenda Mungu ni baba au mama wa kiroho. Wanaume waweza kusaidia watoto hawa kujifunza kazi, michezo na mambo ya kiume. Watoto hawa wakiwa na wajomba, baba wadogo au wakubwa pia waweza kuwa msaada. Ni wajibu wa kila mtu

kwenye jumuiya ya wampendao Mungu kusaidia malezi “yachukua kijiji kulea mtoto”. Mtoto si wa mtu mmoja, hata faida ya mtoto ni taifa , jumuiya na nyumba za ibada pia.

46 Mtoto anamjuaje Mungu ?,sehemu yangu mimi mzazi ni ipi ya kumtambulisha MUNGU kwake?

mtoto anazaliwa kama kafiri asiyejua Mungu. Nabii Yeremia anasema “ moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha nani awezaye kujua? Mimi, Bwana nauchunguza moyo’. Mtoto wa chini ya miaka saba anafundishwa kwa urahisi kuhusu Mungu Muumbaji. Kule Ghana na pengi afrika ni rahisi hata mtoto kumjua Mungu. jina “Mungu” ni Onyame kwame ikimaanisha “Mungu Mwumbaji” mtoto anaanza kumjua Mungu akifundishwa na wazazi toka utoto. 75% wanamjua na kumwamini Mungu kabla ya kufika miaka 10! Na 3% baada ya miaka 50. Nabii Musa alisema Mungu Bwana ni mmoja nasi tumpende kwa mioyo, nguvu, roho na akili zetu zote. Na maneno anayotuamuru kama wazazi ni kwamba tuwafundishe watoto wetu kwa bidii na kuyanena tutembeapo njiani, tulalapo na tuondokapo, tuyafunge kwenye mkono na yawe utepe wa macho, tena tuyaandike kwenye miimo ya nyumba na malango yetu. Ni muhimu kufundisha watoto amri za Mungu na waone kama tunaishi hizo amri na kukazia kwenye mazungumzo na maisha yetu ya kila siku. Maisha yetu ndiyo mahubiri makubwa kwa watoto wetu. Tusiwe kama mafarisayo ambao waliambiwa “wanayowaambieni yote mafarisayo fuateni, maana wajua sheria mpaka takarakimu ya mwisho ila matendo yao msifuate, maana ni wanafiki”. Mtoto mdogo anajua mnafiki mapema tena hata pengine kuliko sisi watu wazima. Watoto wadogo wanachoka haraka, fanya ibada na maombi yawe ya kufurahisha. Kwa vijana leta changamoto, mijadala na maswali. Mtoto akiwa miaka 9 hivi apaswa kujua kusoma neno la Mungu kila siku na kusali mwenyewe mbali na wazazi. Aifanye imani iwe yake na si wazazi . safari ya maili 1000 huanza na moja, endelea kuomba Mungu mtoto apende vitu vya kiroho na toa Tv haisaidi katu ibada ya nyumbani. Mtoto ajue Mungu ni baba yake. Wakatoliki wamesema “tupe mtoto kabla ya miaka sabaa atakuwa wetu”. Miaka saba ya mwanzo ni muhimu mtoto ajue “amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu. Yeye amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha Bwana, maana atakuwa kama fukara nyikani. Hataona yatakapotokea mema..Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana Ambaye Bwana ni tumaini lake, maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; na hautaona hofu wakati wa hari ijapo

ni muhimu pia mtoto ahudhurie nyumba ya ibada regulary na ajue kusaidia yatima , masikini na wajane au watu wenye mahitaji ndiyo dini ya kweli, kumpenda Mungu na Jirani. Mpe mtoto majukumu ya kuongoza ibada anapoendelea kukua, mpeleke kwenye makambi ya mafundisho au semina za vijana/watoto.

47. Napenda mke wangu akae shambani na kuishi na watoto nami nifanye kibarua mjini ili aangalie mashamba na watoto wanakua mashambani vizuri

mke wako siyo mama yako. Ulipotaka kumwoa ilikuwa kwa kuishi naye si kibarua wa shamba kwanini nawe usilime hili shamba? . Kaeni mjini wote au shambani wote ili mfundishe watoto wenu kazi. Shamba ndiyo mwanzo wa alfabeti za Elimu. Matayarisho ya tabia njema ni rahisi mara kumi zaidi mashambani kuliko mijini. Hata kama kila mwisho wa wiki waenda haitoshi. Mtoto anasaidiwa malezi kila siku. Baba anasaidia kuboresha sana nidhamu ya watoto. Hata hivyo kuishi mwenyewe ina nafasi kubwa sana kukuingiza kwenye uasherati , kutokula vyakula bora, kuwa na maamuzi yasiyojali familia,

au kuwa na marafiki wabaya au kwenda sehemu zinazofanya watu waulize maswali. “Mtu atamwacha baba yake na mama yake na kuambatana na kazi au shamba?” si sehemu ya Amri tuliyopewa na Mungu. Kwanini kuoa kama mnakaa mbali? Wengine wasema “sili silali kwa kukufikiri, nakuota”, ila wakioa wanataka mke awe bibi majivu tena akae mbali nao, hivi hii ni haki kweli yeye akae mashambani na wazazi wako nawe ukae mjini?

48. Mimi na mke wangu tunatofautiana, yeye ataka kuwanunulia watoto kila kitu, mimi nasema ni kuharibu watoto wajali vitu na mali kuliko vile muhimu, Mume wangu ataka kuwanunulia michezo ya kompyuta nami sitaki, sasa imekuwa mvutano.

kwa kweli hata mimi naona watoto wasipewe kila kitu. Wajifunze kujali watu na Mungu na si vitu. Wapunguzie majaribu ya kupenda vitu na kutumia watu ili wapende watu na kutumia vitu. Mara zingine wazazi wananunua vitu kwa vile dhamira zao zinawashitaki kwamba hawakai na watoto ila kila mara wapo barabarani. Hata hivyo dunia yabadilika siku zikija za shida watoto waliodekeshwa na vitu watakuwa na mfadhaiko mkubwa. Matangazo ya biashara yamewekwa kuwatega watoto wetu. Wao hupata pesa ila watoto wetu hupata vitu ambavyo baadaye vyaleta tamaa na huzuni. Wazazi nao wapunguze kununua vitu ili mtoto wenu asiwafuatilize. Ukiwa na ulevi wa kununua vitu utashindwa kusema la kwa watoto wakiomba vitu. Watu wachache sana wamejenga tabia nzuri utotoni wakiwa na vitu, tabia inajengeka vyema ukiwa na vitu vichache na kukana nafsi na kufikiria kuwasaidia wengine pia. Hata babu akimpa zawadi mara zingine Ancona ni haki yake na hawashukuru. Vitu vingi vinapunguza ubunifu wa mtoto pia, apaswa ajue kutengeneza gari, mwanasesere au vitu vingine vya kucheza atafurahia muda mrefu ila kama ameletewa baada ya muda anavichoka na kuvitupa huko na kule na kufanya wewe uwe bibi majivu wa kufagia mabaki au makaratasi yaliyofungiwa toys.. Kwa upande wa chakula peremende na vingine vyafanya akose hamu ya chakula wakati ukifika. Vitu vingine mtoto anyimwe ili aweze kuvithamini! Na vingine anapokuwa mkubwa avifanyie kazi , akitoka jasho hataviomba omba kila mara

49 Nimeambiwa kuwanunulia watoto michezo ya bunduki au mikuki ni kufanya wawe makatili

Kwa kweli ukatili mwingi unatoka na kuangalia Tv na vitendo vyetu wazazi au walezi, unyanyasaji au mtoto kuchagua kuongozwa na uovu. Wakati ukatili unaonyeshwa kwenye runinga unafanya moyo, uende mbio, macho yacheze cheze, midomo kukauka na viganja kutoa jasho. Watoto wadogo wakicheza mchezo wa vita ni sehemu tu ya maisha ya kuonyesha yanayoendelea kila siku. Mchezo kwa watoto ni “sehemu ya maisha ya kila siku yakiigizwa”. Mara nyingi haina madhara labda mtoto huyo awe na nia ya kushugulikia hizi silaha(toys) kupita kiasi kwa hisia zisizo za kawaida.

50 Nasikia vibaya kutoa adhabu kwa mtoto najiona kama nitakuwa dikteta au mtu mkatili.

Ni kweli kama wazazi mara zingine tunatoa adhabu bila haki. Ila bado kama wazazi tumepewa ili jukumu na Mungu na tuna uzoefu kwani kule wanakokwenda sisi tumepitia. Ni kweli kwamba sina hekima zote wakati wote ila nina upendo mtoto wangu awe na tabia njema. Upendo wetu na adhabu zetu zapasa zitoshane. Kama una lita moja ya upendo basi na adhabu iwe lita moja. Usimpe adhabu mtoto ambaye humpendi! Labda

iwe katika mazingira Fulani tofauti. Ukiwa mkali na kutoa adhabu kupita kiasi, mtoto aweza kuwa na hofu na asiwe mwenye kujitegemea kwa fikira zake na ukimwachia awe kisultani kidogo waweza kuona aibu kwenda naye mahali maana atakuaibisha. Usiruke mipaka kwa adhabu nyingi au kudekesha kwingi. Mtoto anakuwa na wigo akiwa na sheria na adhabu, na anajisikia salama. Angalia babu/bibi wasimwache mtoto wako kufanya yale ambayo yataharibu nidhamu. Mweleze mtoto tendo lake baya na kutotii kwake ndipo umpe adhabu. Usitoe adhabu au usiadilishe kwa hasira. Kama mtoto ana hasira msaidie jinsi ya kutoa hasira yake kwa njia ambayo haina madhara. Mtoto mara zingine anatingisha kibiriti kuchunguza ni nani mwenye mamlaka! Jielimishe ili utumie mamlaka yako kwa hekima na upendo

adhabu mara zingine inamwokoa mtoto wako ili mbeleni asipate adhabu mbaya zaidi, wengi wamesikia kisa cha mtoto aliyekuwa na tabia ya kuiba akimletea mama yake alichoiba. Alipokuwa mtu mzima aliiba na kuhukumiwa kifungo cha miaka mingi, alipoulizwa kama anataka kusema kitu, alisema naombeni mumlete mama yangu hapa nizungumze naye. Mama yake alipoletwa alimwuma sikio na kusema 'mama yote haya yamenipata kwaajili yako, nilikuwa naiba nakukuletea ila hukunikanya, leo naenda jela, wewe huendi, ni haki hii?@.

51. Je! kumpiga mtoto kiboko ni kumnyanyasa na kumponda roho kwa kumkatisha tamaa na kumfanya apungue thamani machoni pake?.

La hasha, watoto wanatofautiana kuna wengine ukimkazia jicho tu atapata hofu, atalia na kujisahihisha na hatarudia kosa. Ila wengine ni lazima wapate kiboko. Narudia upendo wako na viboko vyako vitoshane! Moja isipite nyingine. Usipige na hasira. Kama huna upendo usifanye biashara ya kupiga mtoto! Kumpiga mtoto ni kumsaidia awe bora ni tendo la upendo si la kumalizia hasira zako. Watoto wengi wameumizwa hata kuuwawa kwa viboko. Wengine wana makovu mengi kwaajili ya watu waliowapiga kumaliza hasira zao. Watoto wengine wameulizwa “kazi ya mwalimu ni nini?” wakajibu “kupiga watu viboko, hata mimi siku moja nitakuwa mwalimu nicharaze watu”.

Mtoto awe zaidi ya mwaka mmoja, na asipigwe kwa nguvu umri huu mdogo mkononi. Tabia ya kupiga watoto matakoni ni ya nadra na soma zaidi kabla hujafanya hivi. Mtoto mkubwa kuanzia miaka 12 awe na adhabu zingine na si kupigwa. Watoto wapewe nafasi ya kupumua na kukua kwa upendo. wazazi wengi wamesema usipige mtoto na mkono maana mkono wa mzazi ni wa upendo, upige na kiboko na kisiwe kikubwa. Kupiga makofi ni hatari kwa viungo vya mwili usoni au makonde ni hatari kwa kichwa. Makofi kwenye mikoni ni tofauti. Lazima vipigo vilete maumivu ili kuleta tofauti, ila maumivu yasiwe makubwa ya madhara. Mpige mtoto baada ya tukio na mweleze sababu na umpige bila hasira. Kwa wazazi wengine imewasaidia kuomba na mtoto baada ya adhabu. Mtoto mdogo aruhusiwe kulia kwa dakika chache. Mweleze unampenda hata umkumbatie ila tabia ile siyo nzuri. Neno la Mungu linasema ,”mwanangu usiyadharau mausia ya Bwana wala usizimie moyo ukikemewa naye. Maana Yeye ambaye Bwana ampenda humrudi Naye humpiga kila mwana akubaliye.. mwana yupi asiyerudiwa na babaye? Msiporudiwa mmekuwa wana haramu wala si wana halali. Kila adhabu kwa wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha bali huzuni, lakina baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani”. Basi mzazi anachukua nafasi ya Mungu hapa duniani kumwadili mtoto.

52 Hakuna kinachoniudhi kama watoto wangu wawili wa kiume kugombana kila mara, je nifanyeje na magomvi yao

Ni kweli inachukiza wakina mama wengi hasa kugombana gombana, kuamua. Watoto wadogo hawachukiani kwa siri, wanafanya vyote wazi wanakuwa kama wapo vitani. Waweza kuchukua chochote na kumpiga mwingine wanamnyanganya mwingine kitu. Watoto wengine wameendelea na magomvi ukubwani. Mzazi ujue jinsi ya kuamua, Kain na Abel waligombana kabla ya runinga! Haikuchukua raundi baada ya uumbaji. Wivu ndiyo kitu kikubwa. Mzazi aweza kuipunguza hii kwa kutowalinganisha watoto. Usilinganishe talanta, michezo,maumbile ,ustadi au kitu chochote."mfano huyu hana akili darasani, hajui kupika, hajui kutunza vitu vyake, hajui kuvaa vizuri, au hapangi vitu vyake vizuri nk. Kila mtoto aheshimiwe na kama ana talanta Fulani ikisemwa, sema na ya mwingine pia, maana kila mtoto ana jambo Fulani zuri. Mara zingine watoto wanagombana ili kutaka attention (umakini wako) na kama hushuguliki nao wanaacha. Jaribu kusema "kama mnataka kuondoa furaha yenu kwa kugombana hapa kila siku nendeni kule nje mkaonyeshe ubingwa wenu siyo hapa mbele yangu. Mara nyingi wataacha. Mama asirushe mikono na kuonekana hajiwezi "magomvi yamenichosha mie, hata sijuie nifanyeje, wacha baba yao aje". Mama jifunze kuamua hata ukiwa peke yako, nawe pia una mamlaka ya uzazi. Baba akija atilie mkazo na muwe mraba mmoja. Mara zingine toa adhabu kwa magomvi haya.Weka sheria mfano: hakuna kuitana majina, kila mtu akae kwake, mkubwa asimtanie mdogo, lazima uweke mipaka. Zaidi lipeleke kwa Mungu maana likiendelea ukubwani lina madhara zaidi. Nina mama ambaye ana watoto wa kiume waliofunga ndoa na wanagombana, wala hawataki kuzungumza pamoja. Imefanya watoto na wake zao wasifahamiane kabisa. Adui ana Njia nyingi za kutuibia furaha Ambayo Mungu anataka tuwe nayo asipotuweza kwa hili anatafuta lile.

53 Tunataka kuwa na watoto na tunajiuliza wapishane miaka mingapi ili waweze kucheza vizuri

Kawaida watoto wanaopishana miaka 2 hushindana sana ila wanaweza kuwa na urafiki na ushirika kuliko wengine. Watoto wanaopishana zaidi yamiaka 4 huwa hawagombani sana ni jambo la nadra na laweza kutokana na mmoja kupenda kuburuza mwingine. Ila kupanga kuwa na watoto haitokani sana na hili ila afya ya mama , hali ya maisha na nia yakuwa na mtoto mwingine.

54 Mtoto wetu ana wivu na mdogo wake aliyezaliwa na tunaona pengine aweza kumdhuru

Mtoto attention kwake inapopungua anakuwa na wivu. Kaa uzungumze na mtoto wako kuhusu mtoto mpya mwambie hata yeye alipokuwa mdogo alipakatwa na kusherekewa vile alipozaliwa. Mwonyeshe kwamba upendo wako kwake haujapungua. Watoto wengi hawawezi kueleza wivu wao ila wale wakubwa zaidi ya miaka 5 wamesema " hivi sijui huyu mtoto amekuja hapa kufanya nini? Kwanini asiende akakae na watu wengine". Mwachie muda azungumze mawazo yake, maana mashuguli ni mengi baada ya mtoto kuja na kila mtu anamwacha mkubwa na kumshugulikia mzazi na mtoto. Fanya mengine anayopenda kama kutembea kwenda mjini mwambie "mtoto hawezi kwenda mjini. Mwache akus aidie kufanya vitu vidogo kwa mtoto kujenga mahusiano. Mtoto baada ya

muda atagundua maisha duniani hayana kitovu kwake tu bali watu wengine ni wa muhimu pia. Jaribu kumlinda mtoto mchanga asidhuriwe pia.

55 Mtoto wangu hakosi adabu wazi wazi ila hachukui majukumu nifanyeje?
Tabia za utoto kama vile kusahau vitu, kupoteza vitu, kuharibu vitu, kutotandika kitanda, kutopiga mswaki, kutopanga vitu vyake si njema.
Jaribu kutafuta vitu vya kusisitiza hivi vitu kufanywa. Usimwite majina kama “mjinga, mvivu au mpoteza vitu”. Hautasaidia tabia. Najua hii ni ngumu hata mimi limenishinda mara nyingi, lakini siwezi nikakwambia ikitushinda basi tufanye lile ambalo ni ovu! Msifu mtoto akikumbuka kitu kama kutandika kitanda. Mweleze tabia yake ina matokeo. Mfano; Asipoenda na begi la shule atashindwa kusoma na atarudishwa nyumbani au akichelewa kibarua atafukuzwa kazi, akipoteza nauli ya basi atatembea kwa mguu. Tabia kama hivi zinapojirudia mfano anamwaga maji kwenye sakafu kila mara, je ni uasi au ni mchezo tu. Tabia inafunzwa mengi ili mtoto asisahau,yaandike kwenye ukuta, mfano chukua ufuto, kalamu na peni ukienda shule nk

56 Nina mtoto wa miaka 4 ana tabia yakulalamika lalamika tu kila saa. Hazungumzi kwa sauti ya kawaida ni malalamishi tu (whining).
Mwambie mtoto akifanya hili. Pengine amelizoea sana na haoni tofauti. Pengine ameona sauti hii tofauti ndiyo inayoweza kumfanya asikilizwe. Mwambie unashindwa kumwelewa kwaajili ya sauti ya kulalama. Mwambie azungumze sauti ya kawaida. Rudia hili ukisikia sauti hii na utaona matokeo mazuri. Waambie na wengine wa familia wafuate nyayo zako

57 Je, kusema asante, ni muhimu?.
Ndiyo mtoto atakiwa ajenge tabia ya shukurani. anayofanyiwa si haki yake ila ni rehema! Hii itamfanya aweze kuwa na shukrani. Pole , asante, naomba, tafadhali, samahani na maneno ya tunu au dhahabu. Ataishi na watu vyema, kama akioa/kuolewa au akiwa na watoto, watabarikiwa na tabia njema, na aweza kuwafundisha wengine kwa mfano wake.

58 Nina mtoto anayeogopa giza nifanyeje
Ni kweli watoto wanaogopa giza kutokana na sisi wakubwa au kutokana na hadithi zetu. Matani yasiwe yanahusu giza, mnatembea kwenye giza na kusema “zimwi anakuja huyo” . mwambie mtoto kwamba unaenda kwenye giza ila Mungu yupo pamoja naye kama anaogopa kwamba uovu hufanyika gizani.

59 Je, mtoto wa miaka 4 aweza kusoma.
Ndiyo kama ni akili nyepesi kushika, aweza kusoma kwanza kiswahili ni rahisi kusoma maana a e I o u hazibadili ila wazazi wachache wako tayari kushugulika na hawa watoto bila kuonyesha hasira. Kama hautakuwa na uvumilivu acha mtoto akue kwanza ni vizuri kwa macho yake na ubongo kungoja. Usikimbizane na watu wenye mashindano “mtoto wangu asoma na miaka 3” hata akisoma na miaka 3 ataenda wapi? Mfundishe kazi, zile njia za ubongo zihusuzo kazi zinakuza mafikara kuliko masomo . Mfundishe kuvuka barabara, kwenda chooni na kujifuta vizuri, kufunga viatu vyake, kuhesabu mpaka 20 au kujibu simu. Mpatie vitabu au mpeleke maktaba na msomee. Akiwa tayari ataanza kusoma

***60 Watoto wadogo wa darasa la kwanza na la pili wapewe maksi kwenye darasa*?**
Kutoa maksi ni kitu ambacho kinasaidia mtoto ila kwa mtoto mdogo wa madarasa hayo, msisitizo uwe kwenye kujitahidi kwake, hata kama kazi yake si nzuri sana ili umtie moyo. Maksi zitumiwe kujenga motisha na wala si kubomoa, na pengine ni nzuri kwa watoto wakubwa kidogo.

61 Nimeona watoto wengi wanapenda walimu strict au "wakoloni".
ni kweli walimu wale ambao wanaleta mpango kwenye darasa wanapendwa maana una uhakika wa mipango au kinachofuata. Haitakuwa mshangao. Mwalimu anayependa watoto na kuwa strict watoto wanajifunza zaidi. Darasa likiwa na fujo watoto wanaogopa usalama wao na watoto wengine waweza kuonea wengine. Watoto wengine hawana haki kwa wenzao na wasipokuwa na mwalimu ambaye anasimamia mambo kwa umakini wanaweza kuumizwa. Watoto wanapenda kutendewa haki wakiwa na mwalimu anayefuata sheria watatendewa haki badala ya uharamia, makelele na uonevu. Mwalimu ambaye anachia uovu uendelee bila kukemea, au taaluma isitiliwe mkazo si mbaraka kwa watoto. Mtoto asiyefanya kazi yake, mwalimu lazima afuatilie na ikiwa zaidi ya mara moja, adhabu itolewe.

62 Nina watoto ambao hawaleti kalamu wala karatasi wakija kusoma na nikiwaazima hawarudishi
Nafikiri lazima utoe adhabu kwa hili. Mfano waambie kwamba wakija safari ijayo na wamechukua penseli zako wasimame kwa saa moja wakiandika. Baada ya muda kila mtu atakuja na penseli yake. Kama kuna yule anafanya hili akionekana anasimama, ataona aibu

63 Kuna umuhimu gani kwenda shule na watoto wanasahau waliyofundishwa?
Mbali na hesabu, mwandiko na kujua kusoma, shule ina faidi zaidi ya hapo.Ni kweli kuna kusahau ila shule inaleta nidhamu na kujikana nafsi, kukaa kwa muda na kufuata masharti, kufanya kazi, kushirikiana na wengine, kutoka jasho. Hata nyumbani mtoto apewe kazi za kujifunza. Yanayofundishwa yanabadilisha mwenendo, hisia na pia ustadi wa kujitafutia riziki. Kama asipoenda shule, mfundishe nyumbani ukitumia syllabus inayokubaliwa (homeschooling).

64. Mimi ni kijana wa miaka 21 nataka kuoa, niko mwaka wa pili chuo kikuu wa shahada ya kwanza na mchumba wangu tukimaliza tu twataka kuingia shahada ya pili, na kutafuta vibarua na tuanze kutafuta kiwanja kujenga nyumba
Vijana wengi wanapigana vita vingi kwa wakati mmoja (battle with many fronts). Mama, watoto na baba wasoma. Kisha mnataka muwe na vitu vingi. Vibarua mwende na pia mtoto aweza akaja saa yoyote, ni nani atakuwa na muda na watoto? Kila mtu yuko katika high ambition ya kuwa na hiki na kila. Ningeshauri pengine mfanye harusi baada ya kumaliza shule au mkioana msiwe na watoto kwanza. Hata mahusiano ya ndoa yanaharibika kwa tamaa za kuwa na kila kitu na watu hawana muda na mwenzi wake na mwishowe kuachana. Nilitembelea mji Fulani mkubwa hapa kwetu afrika nikakuta bwana Fulani na mke wake wameachana na mama anakaa na watoto. Bwana na mke, ni

madaktari wafani mbalimbali. Wamehenya kumaliza shule na nyumba nzuri, magari na vitu, ila wanagombana kwa ukatili mwingi na kuchapana mpaka kila mtu ametokwa hamu na vitu. Walichukua muda kuvipata vitu ila havina maana tena. Wote wana huzuni, kila mtu anakaa kwake, wanagombania watoto, wanafika shuleni na kumwambia mwalimu “akija mume wangu usimpe mtoto! Ningoje mimi”. Mtoto akawa mgonjwa nao wanaendelea na ugomvi. Usitake ujaze vitu vyote duniani kwenye mkono wako! kuwa na furaha ni zaidi ya elimu na vitu, ishi kwa hekima za mbingu ,usitegemee akili zao maana vitu vyote vitakuwa siku moja ubatili. Wazungu wasema “less Is more” yaanni kuwa na vichache ni kuwa na vingi. Vingi ni kama amani, uvumilivu, furaha, kuridhika nk Fikiri hili. Waweza kuonekana umeshinda kwa moja au mawili na kushindwa kwa mengi ya thamani zaidi.

65. ***Tuna kijana wa miaka 21 bado anaishi nyumbani ila hakubali mamlaka yetu na hatueshimu. Anavunja sheria zetu nyumbani, anasikiliza miziki ya ajabu kwa sauti ya juu, anarudi baada ya saa saba usiku. Nahofia wadogo zake ambao ni wadogo wanaanza kumfuata na kuvunja sheria pia***

kijana huyu ni mkubwa na kwa vile ana shingo ngumu, hali hii itazidi kuwa mbaya mwaka hata mwaka. Mwiteni na mzungumze naye matakwa yenu na kutaka kwake uhuru . Kutoheshimu sheria kwake kwaonyesha amekua na inabidi mmsaidie akaishi mwenyewe kwa kupanga chumba, kumnunulia vitu vya kuanzia maisha nk. Inakuwa vigumu kumbadilisha mtu mzima au kumlazimisha. Watu wa dini ya Amish marekani mtoto wanakuwa kwenye mamlaka ya mzazi sana na kwa nguvu zote ila akifika 16 anaambiwa uko huru kunywa, kuhama na kufanya chochote unachotaka. Ila ukikaa lazima uendelee kutunza kanuni za maisha. Wanapewa fedha kwenda mjini waanze maisha yao, wanapoenda huko, Wachache sana wanatumia huo uhuru, wengi wanapenda kuendelea na urithi waliopata na wanarudi kwao (Amish wanajali maisha rahisi ya kumcha Mungu. Waishi bila umeme, magari, au vifaa vyovyote vya kisasa, wanatumia farasi, na kulima kwa plau, wanashona nguo zao na kujenga majengo yao wenyewe, wale wa mijini wanaitwa Mennonite). Sisemi kwako ufanye haraka, ila kwa waamish wamekuwa wakifunza watoto na kufanya nao mazoezi ya kuwaachia huru na kuwajengea ustadi toka utoto. Usimfuge mtoto sana unaalika uasi, labda uone mtoto mwenyewe anapenda kushirikiana nanyi vizuri

66 Kuna watoto wa nyumba nzuri wanakuwa waovu wakikua na wengine waovu kutoka nyumba ngumu ila wakikua wanakuwa wema sana

kweli hata mama mwingine nilimsikia akiomba “ulimbadilisha Sauli kwa nguvu kuwa Paulo na tabia yake ovu akawa mtu mwema kwanini usimlazimishe kijana wangu kama ulivyomlazimisha Sauli”. Hili ni fumbo, kama wazazi tunafanya sehemu yetu, kwa nguvu zote. Kama vile maharamia walivyovunja majengo ya New York World trade center, kwa nia ovu, ndivyo ambavyo wazazi tunapaswa kuwa na nia yenye nguvu na kina ya kunuia katika malezi bora ya watoto wetu. Kama wao walinuia uovu na kuweza, je sisi tunaonuia wema ili watoto wetu wamjali Mwenyezi Mungu na watu, Mungu hatajibu dua zetu? Usikate tamaa mwombe Roho wa Mungu akusaidia mtoto ampende Mungu sana, na kupenda watu, hata wakiwa na shida omba huruma na kuwasaidia. Mungu naye atampa njozi mtoto, na misheni ya vitu vya kufanya maishani na kisha usongo na nyenzo (Vision, Mission, Passion and Provision).

67 Vyuo vikuu vya siku hizi, vijana wetu wa kike na kiume wanakaa vyumba vya karibu , hamna masaa ya kuwatembelea kwenye bweni, unaonaje hii tabia kwa adabu za watoto wetu

Jambo hili linaleta shida za watoto wetu kuwa na maisha yasiyokuwa na usafi. Hasa katika enzi ya mambo ya ushoga, kumekuwa na kuchanganyakiwa, na kusema vyoo vya wasichana na wavulana viwe pamoja na hadithi za ajabu ambazo toka enzi za mababu hatukuzisikia. Siku moja tulitembelea chuo kikuu Nairobi kama chuo na tulipelekwa kwa vyumba vya wasichana tuliowafahamu. Chumba kimoja kidogo sana kama wasichana wawili wana pazia linatenganisha. Msichana wa upande wa kushoto alikuwa amelala na mwanamume wanazungumza nasi tumemtembelea msichana mwingine upande wa kulia! Na usiku wanalala vile pia. Binadamu anakuwa kama mnyama, kulala na mwanamume hapa, na wengine kando hapo. Bafu na choo wanashare . vyumba vya wasichana na wavulana vipo pamoja. Kwa kweli hata tamaduni zetu za kiafrika watoto walilindwa. Hii ni njia ya kuleta ukahaba na uovu. Karibu 70% ya wanafunzi watakuwa wameshugulika na ngono nje ya ndoa kabla ya kumaliza shule. Je unapinga msemo wa wazee “sitaki binti yangu aende chuoni atakuwa malaya, nitakosa ngombe wa mahari?!”. Jambo hili limeathiri uaminifu kwa Mungu, kwa watu na hasa mume/mke. Nguvu za ashiki kwa vijana ni kubwa na tena unawaweka vyumba vya pamoja wanatembeleana, na kujamiiana na wengine na kuishi kule.. Kwa kweli ni kufanya jamii ivunjike. Huu ni uovu wa wazi. Kama tumeiga magharibi inabidi tuachane nao. Pengine maisha ya usafi si muhimu katika vitivo vya elimu ila tutavuna tunavyopanda. Napenda kusema kwamba masomo yameingiza wengi kwenye uasheratina dhambi ya ushoga. Ni vyema watu waoane kabla ya kwenda chuoni kama hawawezi kuzitawala tamaa zao. Wengine wanasema sitaoa mapema mpaka nifike miaka 30, kumbe anafanya ngono na hata kuzaa . tofauti ni nini? Kwamba huna ruksa au cheti na maana unafanya yote tayari. Uasherati umeleta mmomonyoko wa mengi katika jamii. Oa au olewa usiseme unaenda chuoni na unashugulika na maisha uasherati/uzinzi.

67 Je,Mtoto afundishwa kuhusu ashiki(sex) akiwa na umri gani?

Mtoto mdogo kawaida anaanza kujiuliza maumbile yake akijitazama na jinsia nyingine na kukuuliza maswali. Usishtuke. Jaribu kupembua anachojua na uongezee hapo. Mfano mtoto wa miaka 6 alimwuliza mama yake tumetoka wapi? Mama alitumia muda kumpa semina kueleza mambo ya uzazi nk kwa muda wa dakika 15. alipomaliza mtoto alisema “nilikuwa nauliza sisi ni watu wa kabila gani, tumetoka mji gani? Wazazi ni vizuri wamjibu mtoto, si vizuri aambiwe na watoto wenzake, au vitabu akienda shule. Usipende kuficha ficha, maana shetani afanya ashiki ionekane ni kitu cha aibu wakati ilipewa kama zawadi. Anza kuzungumza na mtoto pengine uzazi kwa mimea kisha wanyama kama kuku, mbuzi. Pengine ameona haya kwa mimea hivyo uanzie pale. Kuwa wazi na mkweli. Unaanza kueleza pole mambo ya maumbile na unaendelea na somo siku zinavyoenda. Sisitiza usafi wa ngono (purity), mawazo, nia na maneno ya mdomoni. Ngono kama zawadi toka kwa Mungu kwa kuendeleza kizazi, nk. Mtoto wako asiende shule ya bweni kusikia haya kabla hujamwambia atapata hadithi zingine ambazo pengine hazitakufurahisha, labda awe na walimu wanaomcha Mungu na wenye uzoefu na jinsi ya kujibu maswali haya inavyotakiwa. Kwa maoni yangu Mtoto akifika miaka 10 ni vizuri ajue maana hata mashule ya serikali watakuwa wamejifunza mengi! Mfundishe kwa hatua. Somo hili uliendeleze, wengine wamefundisha watoto baada ya kuvunja ungo au kubalehe wakaishia pale, wakashtuka mambo mengi yametokea baada ya watoto kufika miaka 16, kumbe masomo haya yahitaji kuendelezwa kila siku zinapokwenda. Mtoto wakati wa karibu na kupevuka pia

unaendelea na somo. Na kumwomba Mungu akusaidie maana siku hizi vimezuka vitu vya uchafu wa moyo vya amalaya wa mapicha na hata punyeto (masturbation) vyote hivi si dhambi tu bali hata vyaweza kuharibu akili za mtoto asiwe wa kufaa kwa jumuia au familia yake, yote haya yasome na kuyaelewa vizuri, zaidi ya yote Mwombe Mungu.

68 Unafikiriaje kuhusu jezi au unifom mashuleni

Inasaidia kujenga nidhamu, na watoto wote kulingana. Lazima mtoto awekewe viwango, usipoweka viwango kufeli ni rahisi hasa katika ulimwengu wa mitumba na fasheni. Angalia timu za mpira, wanariadha au wanakwaya ili wafanikiwe jambo la muhimi ni nidhamu. Kuwa na nidhamu na kujikana nafsi ni kupunguza kufanya mambo kiholela. Viwango na masharti ambayo si ya kunyanyasa ni muhimu.

70 Nina watoto wa darasa la tano ambao saba hawana nidhamu nifanyeje

Kwanza angalia vile vitabia yao na motisha yake, mara nyingi watoto wanapenda kujionyesha. Waweke katika mazingira ambayo hawatajionyesha. Wengine hata wanapenda wawe nyota kwa kupigwa viboko watoto wote wawangalie! Kutafuta attention, mweke nyuma ya kabati ili asionekane dawati lake likae pale. Akitoka hapo baada ya mwezi atagundua kwamba ile atensheni hapati. Waambie wazazi wafanye kazi nao pia na kutoa au kupunguza runinga. Unapoona hata badiliko dogo wapongeze na msonge mbele. Runinga ni mwalimu wa mengi pia yasiyofaa, kwamba wanafanya watu wa magharibi aina maana ni jambo zuri.

71 Watoto wakati wa ibada yao wanafanya fujo, na walimu hawawashugulikii inavyopasa

Walimu wa ibada ni wa kujitolea na pengine hawajasomea saikologia na jinsi ya kushugulika watoto. Wengine wanafikiri wawafundishe kuhusu Neno la Mungu tu na sio adabu au nidhamu. Watoto waweza kufundishwa na walimu wapate semina. Haiwezekani kufundisha masomo na vurugu bila nidhamu!Hilo si shamba la wanyama (zoo). Ni sehemu ya mafunzo. Pia ni kulikejeli Jina la Mungu kuleta vurugu kwenye nyumba yake “nyumba ya Mungu itaitwa nyumba ya Sala na siyo pango lao wenye vurugu”. Utaratibu ni muhimu. Hata adhabu mara zingine inabidi itolewe! Ila kabla ya adhabu jiulize je umewaeleza sheria na wamekuelewa? Je unawapenda kiasi ya kutosha? Je maisha yangu ni mfano mzuri kwao? Je upevu wa umri wao ni upi? Omba na kuzungumza na wazazi wakusaidie, maana hutaki adhabu iwe kali wakimbie nyumba ya Bwana!

72. Tuna mtoto wa mwaka mmoja, tumesikia kwamba tunaweza kuisisimua (stimulate) akili yake na kuongeza uwezo wake wa kuelewa vitu (intelligence).

Utafiti wa Dr burton white wa Harvard kwa watoto ulionyesha haya. Miezi 8 mpaka 18 mtoto anaweza akaongeza uwezo wake wa akili kutokana na uzoefu anaopata. Mama ndiye mwalimu mkubwa wa kuleta mazingira haya. Lugha inayozungumza ni muhimu sana. Lugha hii si ya runinga! Watoto wenye mazingira makubwa na kusogea hapa na pale wanajifunza zaidi umri huu. Toka na mtoto nje, shambani, hapa na pale nk . mawasiliano ya familia ni muhimu sana hivyo mnapozunguza nyumbani na maelewano yenu ni mali sana! Mambo matatu yalionekana kwenye utafiti kama muhimu a. Mzazi aliye na

mpangilio mzuri wa mazingira, b. anayeruhusu watoto kuwauliza maswali hapa na pale na kuwaletea kuelewa, ucheshi, maarifa na faraja b. wanasimamia nidhamu dede (firm discplinarian) huku wakionyesha upendo mkubwa kwa watoto!

73 Mtoto wangu wa miaka sita ana nishati za kuruka hapa na pale, mawazo hayako makini dakika moja yapo hapa dakika nyingine pale nilimpeleka kwa tabibu watoto akaniambia nimpe dawa za kumtuliza(hyperactive child) nifanyeje?

Shida hizi za watoto kupewa dawa za kuwatuliza ziko magharibi zaidi ila zinakuja kwetu afrika. Mtoto aliumbwa acheze na kufurahia, na kukimbia. Ila wakina mama wengi wapo vibaruani na wanakosa uvumilivu wa kukimbia na mtoto na kucheza naye wakija toka vibarua maana wamemaliza kazi moja na wanaingia nyingine. Kazi ya mama ni full time ila haina malipo hata kwa wale wenye watoto wa miaka 10+ wanafurahi wakija nyumbani na kumkuta mama na kumweleza yaliyoendelea shuleni au katika maisha yao. Mtoto wa miaka sita pengine hajakua haraka kama wengine na bado anapenda mchezo sana, waweza hata umrudishe darasa moja nyuma au akae nyumbani akicheza apevuke vizuri. Soma kitabu cha Dr Raymond and Dorothy Moore cha homegrown kids. Mtoto aweza kusubiri asiende shule mapema ukimfundisha kazi ndogo ndogo, na atakapoanza kusoma tarakimu hata akiwa na miaka tisa atazitambua haraka na bila masumbufu. Mara nyingi watoto wakiwa shule wanachuliwa kama kikundi ila ukiwa naye nyumbani kama shule ya nyumbani uko naye peke yenu. Thomas Edison aliyegundua taa ya bulb alikuwa na uwezo mkubwa wa akili ila alionekana hatulii na msumbufu. Mwalimu alishindwa, mama yake alimchukua na kumfundisha hata jinsi ya kufanya majaribio ya sayansi nyumbani akawa mwanasayansi mkubwa anayejulikana duniani

Kuhusu watoto wenye mahitaji maalumu (special needs) pata msaada zaidi kutoka kwa walimu wake, wakuambie vizuri siku inavyokwenda darasani, na ukifika nyumbani nawe ushugulike naye, maana walimu wana watoto wengi. Usikate tama watoto wengi wamepiga hatua kwa kushugulikiwa mmoja mmoja na wazazi wao, hata wakaenda vyuoni. Watoto ambao watu walisema hawatajua hata kusoma. Endelea kumwomba Mungu, ndiye aliyeumba macho, ulimi, masikio, ubongo, na vyote. Kwa wale wenye watoto viziwi, vipofu au bubu. Siku hizi kuna shule na msaada zaidi. Mengi waweza kuyapata kwenye tovuti pia.

73. Tuna mtoto wa miaka sita na mzito kujifunza vitu darasani tufanyeje.

Ubaya ni kwamba shule zinaweka miaka na tunafikiri kila mtoto umri Fulani awe darasa Fulani na ajue list ya mambo haya! Kutumia miaka kupima mtoto amefika hapa, ni kurahisisha (convenient) kazi ya mzazi, au mwalimu katika shule ila haisaidii mtoto. Watu hutofautiana na atafika tu pale unapotaka, mpe nafasi. Ni kosa kubwa kumwonyesha au kumwambia mtoto ni “mjinga, hawezi au mpumbavu”. Mpe muda, mfundishe vitu rahisi, na mpe uhuru kiasi Fulani. Usijiunge kwenye maonyesho “mtoto wangu ndiyo ana akili, amejua kusoma na miaka 4!”. Aweza kujua kusoma mapema ila yule asiyejua kusoma wakifika darasa la saba akampita. Nafikiri mmeona mashambani vitu vingine vinakua tofauti vya kupandwa wakati mmoja! Shule mara nyingi zina paa moja kwa watoto wote, fanya kazi na mtoto wako na umpe nafasi ya kupumua. Ukisoma zaidi kuhusu ubongo unavyokua tumboni na mtoto akitoka una hatua Fulani na mara zingine watoto wengine kuna ucheleweshe Fulani. Na kama mtoto ana shida ya kweli ya utindio wa ubongo (mentaly retarded) ambayo yaweza kupimwa na watalaam basi usimweke kwenye

mashindano ya kawaida.. Endelea kusisimua akili ya mtoto. Urithi wako, mazingira na maumbile ndiyo yanachangia. Mtoto awekwe kwenye mazingira ya kujifunza, mfano atembelee uwanja wa ndege, kituo cha basi, maktaba, mbuga za wanyama au kuwa na wanyama wa kufugwa n.k. kawaida mtoto akiwa na uzito kiasi kikubwa usimweke kwenye darasa la wale watoto wanaojifunza kwa kawaida. Utamfanya awe na mifadhaiko, shida za nidhamu kama kupiga watoto wengine, na kuropoka kwa sauti kubwa au kufanya fujo. Shule za watoto wenye mahitaji tofauti na watoto wengine kwa kuwa na uzito au wepesi mno kujifunza ni adimu kwetu. Kama una uwezo peleleza hizo shule

74. Tufanyeje na watoto wasiojiweza darasani kama walimu, niliye naye ana IQ ya 120 hawa ni watoto ambao japo wanasoma wanafeli. Na wale wana IQ (urithi wa akili) wa kutosha (zaidi ya 70)?

Kuna pengi wanafundisha jinsi ya kufanya mitihani (how to take a test) ili kama ana woga wa mitihani umtoke. Pia mtoto afundishwe ufanisi na kasi ya kusoma. Aonyeshwe jinsi ya kusoma kwa ufanisi. Mfano asubuhi sana na si usiku. Usimkejeli mtoto, kumuumiza, na kumkimbiza kama anajitahidi. Mwalimu wa kawaida ni vigumu na watoto 100 darasani. Zungumza na mzazi pia akusaidie. Mwambie kila siku ulichofundisha ili apokee mwenge huu na kuleta nuru kwa mtoto kesho yake. Mzazi akae na mtoto na kusaidia kazi za shule (homework). Zawadi ndogo ndogo zitolewe mfano sh 50 kwa kumaliza hesabu. Mzazi inabidi awe na nidhamu na ratiba, maana mbinu za kushugulika na mtoto ni vizuri zibadilike au ziwe tofauti tofauti. Gari laenda rahisi lenyewe kuliko unapolisukumu. Tafuta motisha kwa mtoto

75 Mtoto wangu ana shida ya macho na masikio na akisoma anaelewa vitu tofauti

Mtoto huyu ni vizuri apelekwe kwa tabibu ili ijulikane kama shida yake yaweza kupata muafaka. Watoto wengi hawaoni au hawasikii vizuri wahitaji mawani au msaada wa afya. Kisha umweke kwenye “mstari” tofauti na watoto wa kawaida. Kama mzazi fanya naye kazi nyumbani. Mfundishe na mshugulikie. Hichi ndiyo nimeona wenzetu wa magharibi waliozaa watoto wenye udhaifu Fulani wazazi wanawashugulikia kwa nguvu hata kwenda kubadili katiba za nchi ili watoto kama hawa wapate msaada kwenye wizara ya elimu. Najua nchi zetu ni changa ila wengi wanaendelea kusoma vizuri, wana magari na nyumba kama magharibi, je tukisimamia haya mengine dede yatatushinda? La tukiwa na kipaumbele na kumwomba Mungu ataondoa viunga hivi. Mtoto wako akiwa kiwete huwezi kumwambia ukimbie na watoto wenye miguu miwili na uwe sawa na wao. Ila akiwa na shida ya kujifunza tunataka akimbie na watoto wengine kwa usawa!. Pengine wazazi hawagundui kwa urahisi au ukamili kama ni shida ya ulema au ni uvivu na ukaidi wa mtoto. Naamini na kuthamini elimu ya shule, na kwamba imeleta tofauti kwetu Afrika, tumeona kazi na maisha wanayoishi wale walioenda shule zamani. Nathamini nidhamu kwa watoto na kutii. Ila mtoto kujithamini ni muhimu usimvunje mtoto moyo, kwa mambo ya shule akakosa kujithamini baadaye ukashindwa kukarabati shida hiyo. Siyo kila mtoto atashamiri na kufanya vizuri darasani kama kawaida ya wengi ilivyo. Kuna kesi chache tofauti. Hapo mzazi wataka upime wako ujue. Mtoto ana haki na utu wa binadamu akiwa ana uwezo wa darasani mkubwa au mdogo. Yeye bado ni mtoto wa Mungu. Ikiwa masomo ya darasani hayawezekani ni vizuri kumtafutia ustadi aweze kukabili mazingira yake. Si kila mtu duniani atafit kwenye mfumo huu. Shahada kisiwe kimungu kidogo. Bora ajue kutafuta riziki na kuwa na tabia ya Mungu.

76 Mtoto wangu amefukuzwa shule na sijui la kufanya. Mimi mzazi ni mwalimu na nimeomba wanisaidie ili amalize shule, miezi 2 angemaliza, wamekataa. Siku ya kumchukuwa wakaniambia "mwalimu gani wewe unashindwa kumwadabisha mtoto wako" kwa kweli tumejitahidi mno na tunaogopa kuendelea kutumia nguvu mno na kumdhuru. Tunaona aibu kwa marafiki zetu na wakituuliza watoto wenu wanaendeleaje mawazo yetu yanafikiri kwamba wanatucheka. Mke wangu anafanya kwenye picha za xray hospital na ameona watoto wengi wamevunjwa mifupa kwa adhabu na wazazi, sasa naanza kuelewa hawa wazazi walipopitia. Tuna watoto wengine 3 wanatabia nzuri wamemaliza shule, wameolewa na wameenda kwenye miji yao

Kuna pande mbili za sarafu ya hili. Pengine mzazi alikuwa na shida ndiyo maana walimu walisema vile. Hakumwambia mtoto na kuwaambia "nataka ufuate haya masharti". Au hawakuwa na muda wa mtoto walikuwa kwenye mashuguli, uovu kama pombe, uasherati au kujipenda na ubinafsi badala ya kushuguulikia watoto. Au hawakushika usukani wa malezi vizuri wakati wa udogo.

ila sidhani kesi hii ni shida ya wazazi bali maneno waliyosema walimu hawakudhamiria waliropoka au kutouwa na upendo. Wazazi wengi wamekuwa wepesi kujilaumu siku hizi kuliko zamani! Zamani mtoto akiwa na nidhamu mbaya watu walisema ni mtoto mbaya, na mzazi hakujilaumu sana.

Mawazo mengi yamekuja kwa wazazi hawa, kutoweza kutatua matatizo la mtoto huyu, dhamira kuwashitaki, kutojiamini kwamba wanaweza (lost confidence), kuona wamemwangusha mtoto, au hawakuweka mfano mzuri, kuona wamechelewa , kuona majukumu ni mengi mno (overwhelmed), kumchukia mtoto na kutotaka kumpa usalama na mwisho Kufikiri pengine kwenye utoto wao walifanya hivi na tabia inajirudia kwenye kioo, au wanalipwa walivyosumbua wazazi wao.

Mzazi huyu asijilaumu na kujihukumu sana. Wazazi tumetwika na kulaumiwa hata na watoto wetu walio na mvi makwao! Mtoto akiwa na akili, mwanamichezo, mwasi, ana sura nzuri, mrefu, kilema, mgonjwa, mnene, mrefu, mvivu tunafikiri au wanatuambia wazazi ndiyo sababishi. Hakuna mtu ataelewa aibu hii ya mzazi aliye na mtoto mwovu! Ila Hata mtoto ana uchaguzi hasa mkubwa wa miaka 17 kama huyu. Wakati neno la Mungu linaandikwa mtoto wa miaka 12 alianza utu uzima. Wazazi hawa wasichukue kama wao ndiyo wanafanya hili mfano (mchungaji mmoja alisikitika kijana wake alipompa mimba msichana kanisani, akaandika barua ya kuacha kazi, kama ndiye yeye alizini akisema kwamba hakusimamia nyumba yake vizuri kama Tito 1:6 ilivyosema. Nafikiri fungu hili ni kwa watoto wadogo. Nafikiri hata Adam na Eva walichagua dhambi na haikuwa shida ya Mungu. Muda umeenda usiendelee kujilaumu, mwombee kwa matumaini. Watoto wengine wanaonyesha uasi waweza kubadilika na kuwa wema tu baadaye na wale walionza vizuri wakamaliza vibaya. Soma kitabu parents in pain by Dr John White au angalia website.

77. Nilimzaa mtoto nje ya ndoa, mume wangu alipoenda vitani. Mume wangu anamchukia mtoto huyu na hii imenifanya hata mimi nimchukie

Ukifanya uamuzi wa kumpenda mtoto utampenda ingawa umepitia hapo. Mtoto hana kosa, ni wewe ambaye ulikuwa na uamuzi zaidi ya mtoto. Kama mtoto huyu utashindwa kumpa upendo ni vizuri utafute mtu wa kukusaidia. Mara nyingi wazazi wako waweza kukusaidia ila usipotee kabisa, tuma kwa mtoto zawadi,piga simu na kujua maendeleo yake. Neno la Mungu linazungumza bibi Lois akimlea Timotheo. Ila lazima uwe na uhusiano mzuri na wazazi wako ili mtoto asaidike zaidi. mahusiano mabaya na wazazi

yatamuumiza mtoto zaidi. Watoto wakisikia wazazi wako wanakusema vibaya inapunguza nafasi ya ufanisi wa kukuza tabia ya mtoto. Waambie washugulikie nidhamu. Endelea kujenga mahusiano mazuri na kama ni wale wanaokusema vibaya kwa mtoto hawatakusaidia mtoto bali kumwaribu. Angalia wazazi wako kama ni wale wanaopenda kufuata imani yako au vitu unavithamini au dada zako ndiyo mnafanana kwa maadili yenu .Ni nani ajuaye hata huyu mume aweza kukuchoka hasa baada ya kuona hata damu yako unaitelekeza na huyu mtoto akawa msaada kwako siku moja. Angalia pia kama wazazi wako wanakidhi mahitaji yake. Kuna mabibi/babu wengi hawapendi kulea watoto, wanataka kuwa huru au hawana uwezo wa kukabiliana na suala lako. Hili pia ni fundisho la kutoshiriki kwenye uasherati au uzinzi. Mwombe Mungu Msamaha akusaidie. Usilinganishe watoto pia, wapende wote kwa usawa. Usiwe na wivu wa watoto wengine ukiwaona unasema “watoto wa wengine wazuri, ningekuwa na mtoto wa aina vile, aidha kwa maumbile, visomo, mali au chochote! Huyo ndiyo aliyekupa Mungu mtunze vizuri. Hakuna mkamilifu, na hata hivyo mambo ya dunia hugeuka na kuchuja, hebu chuki yako uiondoe, utafute ufumbuzi, Mungu ni wa rehema anasemehe, na ni fundisho kwetu kwamba dhambi inaumiza. Endapo Daudi angejua kumchukua mke wa Uria ni dhambi ambayo watu wangeisoma miaka 3000 asingeifanya,maana kwa miaka hii yote ametoa mwanya kwa adui za Mungu kulitukana Jina la Mungu.

78 Inakuwaje watoto wadogo wanajifunza kuzungumza lugha na lafudhi wakati watu wazima twaweza kujifunza lugha ila si lafudhi?

Wazungu waita hii phoneme contraction au kuanguka kwa sauti. Koo la mtoto mdogo linachukua shepu Fulani ya lafudhi kwa urahisi na shepu hiyo anajengeka na kuwa ngumu kubadilika. Hii inafanya kubadilika shepu ya koo kuwa ngumu na kufanya lafudhi isiweze kubadilika. Hata mamlaka ya mzazi kwa mtoto ni vile, kuna dirisha la mtoto la muda utotoni la kumthamini na kumheshimu mzazi linajengeka. Dirisha hili ni la muda mfupi, baada ya hapo inakuwa ngumu. Wazazi wengi wanatenda kosa la viwango tofauti kwa watoto tofauti. Wa kwanza akizaliwa wazazi wanaweka viwango vikubwa, baadaye wanachoka na kulipua kazi. Wana mashuguli mengi pengine, kila mtoto ana viwango vyake na wa mwisho anakuzwa vibaya kupita wote viwango vikiendelea hivi.

77. Nilisafiri kwenye basi na mama mmoja, mtoto wake wa miaka 3 anasumbuka na kupiga makelele, kila abiria alichoka nao. Je mtoto kama huyu asaidiwaje?

mtoto kama huyu kama ameonekana haumwi, hana njaa wala haitaji kujisaidia, ni vyema atolewe mkazo wa jambo. Mzazi asiwe na tabia ya kurudia rudia , akisema mara moja tu ifanyike, ya pili adhabu itolewe. Mfano toa mguu wako kwenye bomba la maji. Mwambie unahesabu mpaka 3 na kama haujatoka ni adhabu. Mara nyingi wazazi tunapenda kurudia rudia, na mtoto anaona kwamba utarudia rudia ndiyo afanye. Hata hivyo mtoto wa miaka 3 mama huyu angesafiri na vitu vya kuchezea, kuandika au kuchora ili awe na kitu cha kujishugulisha kwa safari ndefu

79. Tulilea watoto tukiishi gizani na tabia za ulevi, wizi, uasherati, uongo na mengineyo. Sasa tumerudi kwa Mungu na tunampenda Mungu, ila watoto wetu tuliowalea gizani zile tabia wanaendelea nazo na zinapita hata zile mbaya zetu, tukiwaambia hawataki kusikia kama vile sisi tulivyokuwa. Hatutaki wapate shida tulizopata hivi kwanini watu hawajifunzi

kutokana na uzoefu wa wengine? Wanatuambia "mnataka tuwe ambavyo hamkuwa?" tunasikitika ila tufanyeje. Tunashindwa kujisamehe

Hali hii ni ngumu na ni fundisho kwa wengi wetu kwamba Mungu Atusaidie tuishi maisha ya mfano bora kwa watoto, maana mara zingine mzazi aweza kuacha uovu ila mtoto akamzidi kwa ule umaarufu mbaya. Ila tukumbuke Binadamu anapenda uovu hata kama angekuwa na wazazi wema namna gani! Kwa kweli hakuna mzazi ambaye hajutii jambo Fulani alilofanya kwa watoto! Hakuna mzazi mkamilifu. Hata baada ya muda tukiangalia nyuma wote tuna makosa tele. Muhimu kumkabidhi Mungu Atuongoze. Jifunze kujisamehe, na pia mfundishe mtoto kujisamehe na kukusamehe. Dunia ina mazito mno. Mkutano mmoja nilikwenda baba mmoja Steve Chapman alisema alirudisha gari nyuma akamgonga mtoto wake kwa bahati mbaya". Dunia ni ngumu. Jifunze kusahau yaliyopita si ndwele."Natenda neno moja tu, nayasahau yaliyo nyuma nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo niifikilie ile medali ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu"umkabidhi mwombe Mungu msamaha maana YeYe ni mwenye rehema " binadamu wote tumefanya dhambi, tumeoza hakuna mwema". Zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni. Chukua muda kufanya tofauti kwa wajukuu wako au watoto wa jumuiya kwa yale mema unayojua ya kusaidia watoto. Kile kilicholiwa na mchwa Mungu Atakurudishia kwa mapenzi yake maana anasikia kilio chako "nitakurudishia watoto wako". Ila usiwe mtu mwenye wivu, malumbano au jazba. Nimeona wazazi wengi waliopata shida hii wakiona watu wengine wenye watoto ambao wamesoma vizuri na tabia njema wanafurahi sana wakianguka na kusema "tumelingana", huu ni uovu. Maana hata wao wakiwa "wabaya" haitasaidia wako wawe "wazuri" bali kuongeza mbegu za uovu duniani. watu wakizungumza watoto wako usiwe na haraka kujibu "wananicheka na watoto wangu, hata wao watakuwa kama wangu tena wabaya zaidi", hii ni roho ya adui na si ya Mungu ya kutaka watoto wa wengine waharibikiwe kwasababu wako waliharibikiwa. Ili Mungu asikie sauti yako kuwa mnyenyekevu anayewaombea watu mema ! "Ukae kimya mbele za Bwana Nawe umngojee kwa saburi usimkasirikie yeye afanikiwaye". ". Mungu ni mwenye huruma, haki na rehema hata Samson mnadhiri alipoteza muda kwa uovu, au mfalme Manase saa ya mwisho walipata kubadilika, ila angalia bahati ya mwenzako usilalie mlango wazi , leo ndiyo nafasi ya kumwamini Mungu ukipata nafasi, na pia ukimwamini toka ujanani utafanya usiwapeleke wengi Jehanam.

80. Je, waweza kumruhusu kijana wako kiume na rafiki yake wa kike wasiyefunga ndoa waje kulala kwako?

La. Itakuwa kumvunjia Mungu heshima na kanuni ambazo mimi na mke wangu tumeziwekea msingi. Nitachukuliana na watoto ila si kiasi hicho cha kumhuzunisha Mungu wangu. Pengine naweza kuwatafutia mahali pa kulala kama nyumba ya wageni.

81. Je kuna wakati wazazi hawapendi watoto wao ?

Ndiyo ni kama maisha ya ndoa, tabia na vitu vingine vinafanya upendo wetu upungue. Kuna wakati mwingine mtoto anafanya vituko vikubwa, mama mmoja aliniita akasema nifanyeje "sina upendo na mtoto tena". Alikuwa ni mtoto wa miaka 10, aligundulia amefanya vituko vikubwa shuleni. Ila upendo ni kanuni si hisia zinazokuja na kutoka. Angalia jinsi ya kufanya mahusiano yawe mazuri. Mshauri kwa mambo, inategemea na shida yenyewe. Siku za mbeleni tabia zingine huondoka. Uwe na uvumilivu wanapokua, utashumshukuru Mungu kwa uvumilivu huo

82. Tuna mtoto wa miaka 2 ana dada wa miaka 4, 6 na 8 anawapiga na kuwafanyia fujo mpaka wanalia tufanyeje?

Mwambie vizuri na aelewe kwa vile mtoto wa miaka anajua vyema maumivu na kupigwa waambie dada zake kwamba akiwapiga nao wampige miguuni au mapaja. Hii inaitwa nidhamu ya upendo (loving discpline)

83 Ni matatizo gani yanatokea wazazi wanapoachana na watoto wao waliokuwa watu wazima?

Watu wengi walifikiri ni matatizo ya wakwe! Kumbe siyo, ni matatizo ya mahusiano na wazazi! Hata wengine wanafikiri kwamba wanaishi na wakwe vizuri kuzidi wazazi wao. Tatizo ambalo limechukua karibu nusu ya zote ni wazazi kutopenda watoto waende "mama hakupenda niwe huru, hakugundua kwamba sikumhitaji kwa namna ile tena. Alitaka niwe chini yake na anitawale kwenye maisha yangu". Wengine wamesema wazazi wanawaona kama watoto na wanataka yale waliyokuwa wanawafanyia wakiwa wadogo waendelee, hawafurahi tukisaidia wengine au kufanya vitu vya jumuiya. Mwingine alisema nina miaka 54 na bado nikimtembelea mama yangu haniruhusu nimenye viazi au kupika, anasema sifanyi vitu anavyotaka. Kila mara ananikosoa kosoa tu hata akija kunitembelea kwangu. Kila saa anataka kunishushua, hata kwa vitu vidogo vidogo. Mwingine alisema "nilikuwa kitinda mimba wa watoto 5 na msichana peke yangu, na nikirudi kutembelea wazazi mama anasema ingekuwa heri ningekuza watoto wa kiume 4 kuliko binti mmoja, na naomba Mungu anisaidie na kunipa nguvu za kumsamehe mdogo wake ni malumbano kila saa, "hata najiwazia kuna haja ya kumtembelea kweli? Yaonekana haridhiki na kila kitu japo amebarikiwa sana ni mtu wa kunikosoa kosoa tu. Nampenda na kumheshimu ila nataka aache sumu zake". Mwingine alisema mama yangu ana wivu na kujilinganisha nami kila mara kwa nguo , kwa uzuri wa uso "nywele zako siyo kama zangu, nashangaa mzazi kujilinganisha vile kama mke mwenza, hivi kwani tuna mashindano gani!?".

84 Mtoto mtu mzima au mzazi akiwa na maneno ya kashifa, malumbano, kukosoa na ya kuumiza ufanyeje? (toxic people)au watu wenye sumu wanaitwa kwa kingereza

hili ni jambo la kutia huzuni, ila kuna watu wa namna hii hawana furaha na wanapenda kutia wengine huzuni. Wengi wanapenda kucontrol watu na wanataka vitu viende watakavyo, yote ni kuhusu wao (it is about them). Nafikiri umekutana nao wengi au wewe ni mmoja wao! Nilihudhuria mkutano wa "women of faith" na kuna washauri wanaoependa Mungu wengi (counselors) wao walitoa ushauri wakiwa kwenye panel (jopo) ambalo Sandi Pati alikuwa mwenyekiti. Mmoja alisema wakimbie watu kama hao! Ila utawakimbiaje wakija kukutembelea nyumbani pako, kukupigia simu na kukuandikia barua mara kwa mara? Watu wenye sumu "toxic people" wamo duniani hata nyumba za ibada tunapata mioshi yao. Jaribu kufanya wema na kuwasamehe, maana usipowasamehe ni wewe ndiye unapata shida, wao wenyewe mara nyingi hawajijui, ni hodari, wana nguvu, hawana kazi ya kufanya (idle) na wengine wana maradhi ya hisia. Kuwafikiria mno ni kama kunywa sumu, ukitegemea wao ndiyo watakufa. Yabidi uwasamehe, kisha usonge mbele. Nabii mwenye hekima Ibrahim alikuwa na hii shida na mpwa wake aliyeishi naye kama mtoto wake baada ya kaka yake kufa. Kulikuwepo magomvi na malumbano 'basi usiwepo ugomvi nakusihi kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako maana sisi tu ndugu.. Je nchi hii yote haiko mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume, ukienda

upande wa kuume nitakwenda upande wa kushoto". Mwanzo 18 yaelezea Ibrahim alijua kutawala watoto wake vyema.
Tujitahidi tuwe wapatanishi, kwa watu wanaopiga simu kugombana au kuandika mabarua ya sumu ni rahisi usijibu! Nilijifunza hili baada ya miaka mingi, kwa vishawishi vya kujibu nyaraka za watu kama hawa, haikusaidia!. Hautawaridhisha na majibu yako bali utaongeza mafuta kwenye moto. Pengine uwashauri waandike kitabu kusitransfer hizi nguvu zao kwenye jambo la manufaa! Wanaweza kuandika mpaka peni au computer ikatoa moshi!. Ila kwa yule anayekuja kwenye nyumba mwambie vizuri tu kama Ibrahim. Hakuna atakayemwona Mungu Anayependa kulumbana lumbana, ni tabia ya mwovu si ya Mungu. Akiendelea kukufuata fuata niandikie!. kwa wanawake angalia kwenye computer huduma za mama Beth Moore usikie mashauri, na washauri wengine kama vile au Reviveourhearts Internet radio au blog ya one without words.
Dr Dobson anazungumzkia Tough love principles (kanuni za upendo mgumu?) zisome. Phyllis and David York, wanasema wazazi kuna wakati wa kumwonyesha mtoto awe mahali pake. Mama mmoja alipigwa kisu na mtoto wake na bado anatolea udhuru kwamba "hakudhamiria kufanya vile" na bado wanaendelea kuishi nyumba moja na mtoto wa miaka 19. Jaribu kuondoka na mahusiano ya ya sumu (toxic). Kumsamhe, mwelewe, ila anapovuka mipaka mwambie mfano, hutatumia hii simu, hauruhusiwi kutumia baiskeli yangu. Wazazi hawa wa tough love wana chama chao cha kusaidiana mawazo. Yaweza mbinu zisifanye kazi mara zote ila zitafanya mara nyingi. Yawezekana wewe mzazi ndiyo sumu kwa watoto! Kama ni vile, omba Mungu akusaidie uache jazba hiyo yenye sumu.

85 Namwonea wivu jirani yangu ana mtoto anayetii, anashika sheria na kufanya anayoambiwa

Ni kweli mara nyingi sote tunapenda tuwe na mtoto kama huyu (compliant child). Ila mara zingine watoto kama hawa wanategemea wazazi mno kiasi kwamba hawafikiri kwa mawazo yao (long dependence relationship). Mtoto akipevuka yatakiwa awe huru na kufikiria na kujitegemea. Watoto wale wanaopenda na nia yao ni ngumu kubadili (strong willed) wanakuwa tayari wakati wowote kuondoka na kuwa huru.
Mtoto wa kupendeza wakati wote, mara nyingi hawezi kueleza hasira yake na anakuwa na hasira ya ndani ambayo anaitoa kwa njia nyingine yenye madhara zaidi. Mara nyingi inakuwa kazi kushirikiana na ndugu zake na kuwa na chuki, hadithi ya mwana mpotevu yatufundisha zaidi kwamba yule aliyebaki na kufuata sheria alikuwa ndani ya moyo wake amechukia. Yawezekana si mara zote ila ni mfano kwamba anayeshika sheria anaona wengine wanaachiwa tu hata wakifanya mabaya au ndiyo wanaishi (mfano wa kaini na Abel). Mtoto wa namna hivi akiwa mkubwa aweza kuugua vidonda vya tumbo, vichwa au shinikizo la damu. Watoto wa namna hii wanahitaji tuwajali na kuwauliza maswali wazungumze ya moyoni, na kuwafanyia haki ukilinganisha na wengine. Wape uamuzi wa kuchagua nguo au shule n.k washikilie ila waache pia waende wasikutegemee sana. Hakuna kitu kama mtoto rahisi, kulea kila sample ya tabia ina shida yake. Maana akiwa rahisi kupendeza marafiki wabaya aweza kuigiza vile Ambavyo ni vibovu kirahisi ili atunze amani nao. Kwa kifupi, hata akiwa ni rahisi kulea, awe na uti wa mgongo (back bone) na mabadiliko ya moyo na si matendo tu.

86 Je, mtoto kurudia darasa ni kitu kizuri?.

Mara zingine mtoto ni vizuri arudie darasa si kwaajili ya taaluma tu bali kupevuka kiakili na kijamii. Mtoto akiwa mgonjwa kwa muda mrefu ni vizuri arudie, ila mtoto ambaye

anakuwa mzito sana kujifunza haitasaidia sana. Wazazi wengine wanaona kwamba wakati wa likizo mtoto afanye tuition imsaidie ili aweze kuwa na wengine na hii pengine ikawa msaada au isiwe. Mtoto atafaidika zaidi kama nyumbani atasaidiwa hasa kwa vile unamsaidia mmoja kwa wakati mmoja. Ni vizuri mtoto afundishwe kujua kusoma akiwa nyumbani, maana shuleni kuna watoto wengi ili awafikie wenzake. Wazazi fanyeni kazi na watoto wenu

87 Je! watoto ambao wamezaliwa na uzito wa kujifunza wana mahitaji kama wengine?
Ndiyo! wote wanahitaji kupendwa na kuthaminiwa. Mara nyingi kuwatenganisha madarasa na kuwaitia majina imeleta huzuni na makovu mengi. Mwalimu aangalie atawezaje kuwa wa upendo na msaada kwa watoto hawa. Ila mzazi ajibidishe naye kuendeleza kazi ya mwalimu nyumbani, apate maarifa kwa wataalamu na hata kwenye tovuti siku hizi kuna mengi ya watoto wenye mahitaji maalumu (special needs children). Watoto wengi wamemaliza sekondari na kwenda hata vyuoni, ambao wengi walifikiri hawataenda kokote. Si wanaoenda kwa kazi tu wanaowezea maisha bali hata wale waendao pole pole, wamekuwa mbaraka kwa wengi, angalia mengine kwenye tovuti na kwa watalaamu kuhusu watoto wenye mahitaji maalumu na jinsi ya kushugulikia hilo.

88 Nina mtoto anayetaka kuonyesha mamlaka yake na kukataa kila anachomwambia afanye. Ana miaka 7
Shida hii ipo kwa binadamu wote, toka mtoto anazaliwa anataka awe anatawala (manipulate). Watu wazima wameandika vitabu vingi kuhusu hii tabia mfano emotional tafsiri“blackmail, do what I want, shut up and do what I tell you, do what I want and I will be nice to your sweet mother, don’t upset me, can’t you see I am sick?, do what I want or I wont pay the bills”.
Have a new Kid by Friday na Dr Lehman, ni kitabu kizuri cha kuonyesha kwamba mtoto ajue kwamba kuna matokeo ya tabia mbovu au kuwa mtawala. Mfano akija nyumbani na kusema “mama mbona saa saba na chakula sijala”. Mama aseme “ni kweli ila nilipokwambia ufagie ulisema kwamba hutaki, hata mama hajisikii kupika leo”
Mtoto mdogo wa mwaka anaanza kukataa kulala akiwekwa kitandani, anakataa chakula anachopewa anataka kingine, hataki nguo aliyonunuliwa, hataki kuosha vyombo au shuguli za nyumbani, hata kukaa kwenye gari kila mtu anagombania dirisha n.k
tabia hizi zakutaka utawala zanaendelea ukubwani na kufanya mtu asijitawale nafsi. Mtoto akiwa mdogo anakuwa chini ya mamlaka ila anapokuwa mkubwa akiwa na tabia ya kutojitawala nafsi ataingia pabaya sana mfano: Sulemani kama mfalme alishindwa kuwa na uzio, akaoa anavyotaka, kula anavyotaka na kwenda anakotaka. Hitler na Stalin walikuwa na mamlaka haya na kutumia vibaya. Mfano Stalin alisemekana aliua 25 milioni. Siku moja alisema polisi waende kwa walimu wake waliomfundisha msingi na sekondari kuwaua
Je mtoto aweza kufanya anavyotaka? Je ni nani mwenye mamlaka katika nyumba? mzazi akiondolewa mamlaka ya kuadhibu mtoto mara zingine madhara mengi zaidi yanafanyika kwa mtoto. Mzazi asikubali mtoto amwite majina yoyote ya kashfa hata akiwa mdogo ni njia ya mtoto kukalia kiti cha mamlaka. Akisema kitu cha kukasirisha, ukakarisirika ameshinda mchezo wa kuwa mtawala
Mamlaka na kusifiwa mno, yamefanya wengi wajenge kiburi na kuwa watu ambao wana udikteta. Na hata si madikteta wa uongozi wa chi tu, ila hata madaktari ,wanamuziki, wachungaji, mashehe, marabi, wanasheria, wanajeshi waliopata kuonyesha utawala au

kusifiwa wamekuwa watu wasiojikana nafsi na kujifikiria wao kuliko wengine. Ni kweli mtu hujaribiwa na sifa zake. Ila anapoanguka akajinyenyekeza huweza kufanya huduma nzuri kwa watu. “Ambaye ni mdogo kwenu ndiye mkuu katika ufalme wa Mungu”. Chuck Colson aliyekuwa kwenye wizara ya ulinzi wa marekani wakati wa kashifa ya Watergate na kwenda jela. Alipenda mamlaka na kuyatumia vibaya. Ila alipofika jela ilimfanya aweze kuishi maisha ya huduma na kusaidia watu waliokuwa jela. Mtoto akipata mamlaka mapema ana risk ya uasi, kutoheshimu mamlaka (mzazi, mwalimu, polisi na hata Mungu). Mzazi asimpe mamlaka mtoto akiwa mdogo ayatoe pole pole mtoto akiwa anakua na kumwacha awe huru akienda kujitegemea

89 Tufanye nini kama wazazi kwa kweli tumechoka na hii kazi ya kulea?

kuna kitabu kilichaondikwa na Dr Joseph Procaccini “parent burnout”.Wazazi wanaochoka sana ni wale wanaojali watoto wao na kujitahidi kutafuta kila njia ya kuwasaidia maana hakuna kuungua kama hakuna moto. Wanakuwa kafara kwa watoto, wanaacha mambo mengine yote kama marafiki na muda wao kama mke na mume wa kuongea na kufurahiana. Kila “mwali” wa jua unaenda kwa watoto. Hawawezi kupeleka hata watoto kwa mtu awangalilie watoto hata kama ni mother Teresa!. Kila mara wanakuwa na watoto. Hawaamini hata wazazi wao kwamba japo wana uzoefu zaidi ya wao, na wanaweza kuwasadia wakati mwingine. Wanajiweka katika hali ya upweke.

pengine bibi na babu waishi mbali au hawajali kusaidia wajukuu zao ila wamejiingiza kwenye kazi nyingi, kufanya mazoezi, kutalii na rika zao, nk. Ni kweli mabibi mababu wengi si msaada siku hizi. mke pia aweza kuchukulia kulea watoto ni muhimu hata kumsahau mume wake. Mume naye akachukia watoto kwamba yeye hajaliwi. Hatukatai usiwe mzazi bora (superparenting). Ila usiwe mtu ambaye unashugulikia watoto mno na kujisahau au akafikiri ni wewe tu waweza uzazi mzuri kiasi cha kuchoka na kuungua.

Nguvu za mwanadamu ni muhimu na zina kipimo zinafikia, na mtu huanza kuchoka. Wazazi wanaotaka kuwasaidia watoto waangalie nguvu zao zisiende kwa yasiyo muhimu. Hata Yesu alichukua muda na kwenda mbali kupumzika na kuomba. Angalia mwili wako utunze vizuri. Najua makanisa, mashule, marafiki, ukoo, misikiti, na jumuiya pia zataka tufanye vitu Fulani na tunachoka kabisa maana tuna shuguli zetu pia. Watoto wanapata shida tukiwa tumechoka hivi. Maana kuchoka baadaye kunajileta kwa magonjwa mwilini, kama vile shingo, presha au sonona n.k

Mara zingine wazazi walifikiri wakizaa itasaidia mahitaji yao ya upendo ila kuchoka, hasira na kuchukia kumeibuka. Wazazi watambue hii shida. Mzazi aweza kujitoa kwenye jukumu la kulea kihisia au kusema “nimechoka na hawa watoto siwezi kulea sasa hivi, ni kama waniondokee usoni mwangu. “ I just can’t deal with the kids right now”. Mzazi na hasa mama wa namna hii anaweza kujisikia vibaya ila hajui jinsi ya kupata msaada. Mara nyingi anakuwa mpweke na hana wa kumshauri. Anafikiria ila anachanganyikiwa, na mahusiano yake ya ndoa yanaharibika. Baadaye watoto wanaharibikiwa.

Si wengi wanafikia hatua hizi Ila wapo na anza kuangalia dalili hizi

Ufanyeje ili maisha yako ya kulea yawe mazuri bila kufoka foka, kugomba gomba, kutishia , kukosoa kosoa, kuchoka. Lazima kuna njia nzuri. Usipende kufanya vitu vingi kwa wakati mmoja. Kusoma. Kuolewa, kupata mtoto, kufanya kibarua, kujenga nyumba nk. Mara nyingi hata ni vyema mngoje angalau miaka 2 baada ya ndoa ndiyo mpate watoto. Kuna mengi ya kuadjust kwanza. Mwili wa binadamu hauhitaji presha nyingi hivi. Mwili ukichoka na hisia pia zinafyatuka. Mwili, akili na roho zafanya kazi pamoja. Utajiletea huzuni kama si wazimu. Lazima uwe na balansi ya hizi ili usibomoke! Tumia

mwili wako vizuri kama kukimbia marathon, usimalize nguvu zote mara moja kama mkimbiaji wa mbio fupi na ukifika wakati watoto wanaanza kupevuka nguvu inapungua kumaliza mbio. Uzazi ni mbio za marathon kimbia pole pole ni miaka mingi pengine 20 hata 30, ndiyo siri ya ushindi. Ishi maisha yenye balance na kumlilia Mungu ni wa rehema maana binadamu hatujiwezi

90. Wazazi wengi wanashitakiwa na dhamira zao kwaajili ya matunzo ya watoto, tufanyeje?

Ni kweli kila mzazi anadhamiri inamshitaki kwaajili ya malezi, hata mtoto akiwa mdogo, mfano "unasikitika kwamba tunamwachia yaya badala ya kushugulikia watoto wetu". Dhamira kutushitaki ni kufikiri kwamba kuna kitu tunakifanya kibaya. Kama ni kitu cha kuomba msamaha tuombe msamaha na kuamini tumesamehewa. Ila kama kiko nje ya uwezo wetu hakuna haja ya kujichapa viboko. Ila ni vizuri kuzijua hisia hizi, usizifungie kwenye chupa mwishowe zilipuke kama bomu. Angalia pale pa kusahihisha. Usifanye dhamira kukushitaki na kukuharibia malezi. Wazazi wengi wamedeka watoto kwa dhamira kuwashitaki kwamba wanaenda vibaruani au mtoto anaumwa naye yupo kazini. Wengine watoa mazawadi kwa watoto kupita mpaka, wanafanya kazi zote nyumbani na kuacha watoto wawe huru, hawakemei tabia Fulani, au wampa mtoto chochote atakacho,kwa vile wanaona kwamba hawako na watoto wakati wote, au wanataka watoto wampende yeye kuliko mwenzi wake.

Toa dhamira kukushitaki na jaribu kuishi kwa furaha na maisha ya imani na matumaini. Huwezi kuwa mkamilifu na tambua hivyo. Angalia kama kuna njia zingine za kufanya mambo kuwa mazuri, omba msamaha pale wa panapotakiwa na songa mbele.

91 Nina watoto wakambo nifanyeje?.

Kulea watoto wakambo ina changamoto zake nyingi hasa wakiwa wakubwa. Ulipomwoa au olewa na huyu mtu ulijua hali hii na ulikubali kwamba utaishi na watoto wake kwa upendo. Watoto wengi wana ndoto kwamba wazazi wao watarudiana na mtu anapooa, yafanya wale watoto wamchukie yule mke au mume mgeni.. ni vyema kabla ya ndoa, kuweka wazi na kuzungumza na watoto pia mategemeo yao ni yapi. Wazazi solemba wanakuwa karibu na watoto wao hata pengine kulala chumba kimoja, zungumza na mtoto kile ambacho kitaenda kutokea. Mfano " tumekuwa karibu nawe ila sasa naenda kuolewa. Kama ndoa yangu itakuwa kama Mungu anavyotaka, napaswa kuwa kitu kimoja na mume wangu. nampenda mume wangu ila upendo wangu kwako hautabadilika.

'Mara zingine utafikiri kwamba "uko nje"nikiwa nimeolewa, sipendi udhanie hivi kwani nakupenda na unahitajika katika maisha yangu. Endapo mawazo haya yatakuja "hawanihitaji nami siwahitaji" naomba uniambie ili tuzungumze. Watoto wengi hufikiri hivi na si jambo linalosaidia familia kuwa na upendo na furaha. Lazima uniambie ukiwa na lolote moyoni tuzungumze pale kwenye maumivu na kujaribu kutatua'.

Mara zingine watoto hawapendi kushirikiana vyumba au vifaa na watoto wa yule mume/mke. Ni vizuri mzungumze na kuafikiana mambo Fulani, ili msilete vurugu na ugomvi. Jaribu kuwa mwema na mwenye upendo pande zote. Jaribu kuwa wa haki pande zote, hata upande wa mtoto wako usipende kuwafurahisha sana wale wa mume wako waliokuja ili kununua upendo wao na kumtelekeza wako nayo pia ni shida yabidi kubalance. Watoto wengi husema "usiniambie kufanya lolote wewe si mzazi wangu". Yabidi mzungumze na mzazi wake ili muafikiane kwenye mambo ya nidhamu na kazi za nyumbani mtafanyeje. Muwe timu moja. Mara zingine watoto wakubwa wa jinsia tofauti

wana hofu kuishi karibu au kutumia vyoo pamoja. Pengine ni vizuri milango ifungwe na angalia hali kwamba ni watoto wa namna gani, waweza kuingia katika shida katika nyanja hii. Watoto wengine dhamira zao zinawashitaki wakipenda mama wakambo au baba wakambo wanafikiri wamewatelekeza wazazi wao. Na wazazi wengine ambao wako nje waleta ugomvi kule waliko kuharibu ndoa hii mpya.
Watoto wengine wanalinganisha wazazi wao na wale wakambo mbele yako “mama yangu ana mapishi mazuri si kama yako” “ baba yangu ana kazi nzuri siyo kubeba magunia kama wewe” n.k. Jaribu usirudishe maneno ya kulipizia. Watoto wana hasira kwamba nafasi ya mzazi wao imechukuliwa, zungumza nao na kuwaambia kwamba “najua kwamba ni vigumu kuwa na mzazi mwingine, na mngependa muwe na baba au mama yenu mzazi na si mgeni kama mimi ila najitahidi tuishi kwa furaha na kuwa timu moja ya kupata ushindi”. kisha waambie “ hata mimi moyoni mwangu naumizwa na kupata huzuni mkinipakazia vitu, nami nataka tuishi kwa urafiki na kusaidiana pamoja”. Ukiona kwamba magomvi yanakuwa makubwa zaidi ni vyema ujitoe na kwenda mahali kimya si wakati wa kufokeana na kupaza sauti,na kusoma zaburi 37.
Japo uzazi wa kambo si rahisi waweza kufanikiwa kwa kuzungumza nao na kuwa na mikutano ya familia ya kutatua matatizo. Je mnataka mwendelee kuishi pamoja na kusaidiana maishani kama kusoma na mengineyo au kuna njia zingine pengine za kuishi kumudu ili tatizo. Endapo kila mmoja ataka kutuma mikuki kwa mwingine hamtafika mbali. Niliona familia moja mama mmoja alipenda kurusha mikuki , hata yule mtoto akisema yametosha tuache na kwenda chumbani mwake, yule mama alimfuata yule mtoto na kufungua mlango na kuendelea. Endapo mmeamua kuishi pamoja kama mke na mume muwe timu moja ya upendo kwenu na watoto. Muwe tayari kupenda watoto wote na kuwahudumia bila ubaguzi.
Mara zingine watoto, au jamaa au wageni wenu wanaweza kuwa na wivu na kutaka mwachane mwahitaji kuzungumza nao na kuelewa nia zao na kuja na suluhu ili uhusiano wenu uendelee. Je ni kwenda shule ya bweni? Je ni kutafuta wakae na mama yao au jamaa mwingine wa karibu na kuwasaidia huko. Kumbuka kwamba hata mkiachana na kuoa/olewa mwingine haya yatalipuka tena. Watoto wanakaa muda mfupi na mzazi, ila mtu na mke wanakaa mpaka kifo kiwatenganishe
Ingawa shida za watoto wakambo ni nyingi nimekutana na wengi walioshukuru kwa kulelewana na mama au baba wakambo vyema na wana urafiki na wanathamini mzazi huyo. Hata mama mmoja wa mombasa aliniambia “mama yangu mzazi alikuwa mbaya kwangu kuliko mama wakambo alikimbia kwenda kwa wanaume mbali mbali mara nyingi! Hata hakutujali”. Mungu bado ana watu wake japo wakambo wazuri sana kwa watoto. Najua mara nyigi kuwa mama wa kambo ni ngumu zaidi kuliko baba wakambo. Pengine ni kwasababu mama ndiye anayekaa na watoto, anawapa Chakula na mahitaji mengine. Kama una changamoto hii mwambie Mungu akupe msaada wa siku kwa siku

92 watoto wengi wakizungumzia ndugu zao wanasema maneno ya kufurahisha marafiki mfano “nina dada mkoloni sana na kaka yangu kila mara vitu vyake akiviweka nataka nivipige teke” je hii ni hali ya kawaida?
Inaonekana kitu cha kawaida kwa watoto wengi wa umri wa teenage 12+ kuwasema ndugu zao hivi ili wapate kuwa timu moja na marafiki au rika zao, ni msukumo Fulani wa rika. Pengine ni kutaka kuiga wenzao au ni wivu kwa ndugu zao. Nafikiri tabia hii si nzuri maana kila mtu ni “mlinzi wa ndugu yake”. Waeleze watoto wako kwamba mko timu moja na msifikiri watu wa nje watawapenda sana kwa kuonekana hamko timu moja. Jenga

tabia ya kutozungumza mambo mabaya kwa wenzako shuleni, nyumba ya ibada au katika jumuiya. Ukimshika mtoto akizungumza mabaya kuhusu Fulani mwambie akwambie mawili mazuri ya mtu huyo. Usizungumze mume, mke au watoto wako vibaya kwa watu wengine. Jaribuni kufanya vitu vyenu pamoja. Fundisha watoto kumshukuru mwenzao au kumpongeza akifanya jema. Mtu akifanya kosa angalia jinsi ya kumsaidia kama ndugu na si kumlaumu laumu. Kuwa mwanatimu wa familia inasaidia kuwa mwanatimu kwenye familia ya Mungu pia katika jumuiya. Wote tunajisikia na nguvu tukiwa na timu inatusapoti na kuwa na mategemeo mazuri nasi.

Nasi wazazi tujaze vikombe vya upendo vya watoto wetu, chukua muda kuwasikiliza na kujenga timu bora. Wapende bila kamba yoyote au vizuizi (unconditionally). Itawasaidia kuwa wanajumuiya bora.

93 Nawezaje kusaidia watoto watii mamlaka

'na sasa Bwana Mungu wako anataka nini kwako? Ila umche BwanaMungu wako na kewnda katika njia zake zote na kumpenda na kumtumikia Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kuzishika amri za Bwana na sheria zake ninazokuamuru"

wazazi wana jukumu la kuwafundisha watoto wao wampende Mungu na mamlaka yake. Kujifunza kumpenda Mungu mzazi wetu mkuu na mamlaka ya juu ni muhimu na hii mtoto atajifunza toka kwako. Mtoto aweza kuogopa mamlaka au kupenda na kuheshimu. Mamlaka ya dunia kama polisi, jaji, mwalimu. Wafundishe watoto wako kukuheshimu na kukupenda. Mwambie mtoto kwamba usingependa kuishi pale pasipo na mfumo au mamlaka "je ingekuwaje kama tusingekuwa na polisi au jeshi?". Mwulize mtoto. Waeleze watoto mamlaka ya dunia kwa kawaida yamewekwa kututumikia sisi , au kwa faida yetu.

Usipokuwa mwangalifu utafundisha watoto wako kuogopa mamlaka ya dunia au kukuogopa na kumtumikia Mungu kwa woga wa adhabu au kuasi wazi wazi na kutelekeza karama ya Mungu ya wokovu.

Usipende kutumia nguvu au udikteta "sijali unafikiri nini fanya hili nalokwambia" watoto wakiwa wanapigwa, fokewa, laumiwa, kosolewa kila mara na kunyimwa uchaguzi au uhuru kabisa wanajenga hari mbaya na mamlaka. Wazazi wengine wanaweka sheria nyingi ambazo wenyewe hawazifuati mfano " usiangalie runinga zaidi ya saa moja". Ikija soka wanaangalia kwa saa tatu.

mzazi awe na mamlaka ya serikali ya nyumbani ila atumie demokrasia hii itafanya watoto wafuate ambazo wanajua sababu au wamesaidia kutunga. Mfano hakuna kuvuka barabara –waulize sababu kisha watoe na uandike wajue sababu. Kwa mtoto mdogo waweza kuweka sheria bila kueleza vitu vingi. Ila mzazi jifunze kufurahi na watoto wako hata kucheza nao siyo kila saa unatafuta mbinu za kuwakimbia na kufanya vitu vyako. Waongoze watoto kutii mamlaka yako. Mara zinginei onyesha rehema, si kila kosa lahitaji adhabu kali, mara zingine watoto hufanya kitu kwa bahati mbaya. Mfano kumwaga maji, siyo kila kitu unatoa adhabu. Utafanya watoto wasikwambie ukweli wote na kuwa waongo , dhamira kuwashitaki na kutaka usikae karibu nao

94 Nilikwenda kutembea kwa rafiki na watoto wangu. wakaanza kufuatisha watoto wa ile nyumba kupiga makelele na kuzomea nifanyeje na mama yao hawagombezi wale watoto.

Napotembelea familia nyngine najaribu kuangalia watoto wangu wasikose adabu "usiguse hiki au kile, angalia miguu yako usikanyage hiki au kile" ila mara zingine yule mzazi wa ile

nyumba anasema “ni sawa tu wacha waguse au wakanyage!”. Nafikiri ingekuwa rahisi mwenyeji kuweka viwango “tukiwa tunatembelea hapa hii itafanya nisiwe na tashishwi wakati nafanya ugeni hapa”. Nikiwaambia watoto wangu sheria au watoto wa mwenyeji yaonekana mimi ndiyo “mzazi mbaya” . napenda watoto wangu wajue yule mwenyeji wetu hapendi hizi ghasia pia ila anataka asitukoseshe raha. Wazazi wengi hawapendi watoto wao kuambiwa wakiwa wanakosa, wanaona ni kama wamekosolewa mbinu zao za kulea.

Endapo kwenye jumuiya tungekuwa tunasapoti mzazi mwingine akiwa anatusaidia na watoto wetu tungepiga hatua kubwa kwa malezi ya watoto. Wazazi wajifunze kuona kwamba wazazi wengi tu wana nia njema kwa tabia ya watoto wao. Mtu anayependa watoto akiwaambia watoto wetu, wanaweza kujifunza toka kwake vizuri tu, na tukawa timu moja na mzazi huyo. Mfano mzazi aweza kusema “tawi la mti huu laonekana dogo ni hatari kwenu wote kupanda huu mti, labda mmoja mmoja”. Badala ya kusema “shukeni haraka kwenye mti wangu mtajutia mkipanda”. Mtoto anajifunza kumpenda na kumheshimu mlezi mwingine ambaye si mzazi kutokana na upendo wake. Mtoto anajua si mzee mbaya tu ila ni mtu anayejali mema yao. Mfano ukimwona mtoto anapiga kelele kanisani badala ya kumngoja mzazi wake baada ya ibada umwambie, mwambie mtoto ukitabasamu “ sisikii mahubiri mkizungumza kwa sauti kubwa” au ukisikia mtoto mmoja anamzungumzia mwenzake vibaya “maneno hayo yatamhuzunisha mwenzako, jambo la upendo ni kumwomba msamaha”. Ukiona watoto wangu wanaharibu vifaa, usingoje mpaka vimeharibika uniambie baadaye waambie “ hili si jambo jema la kufanya litawaweka kwenye tatizo kubwa”. Napenda watoto wangu wampende na kumweshimu Mungu na kupenda watu, na siwezi kuwa kila mahali, au mara zingine waweza kumsikiliza mwingine vyema zaidi, naomba kwa kujali waambie ili uwasaidie. Nami nafanya vile kwa watoto wa wengine

95 nitamsaidiaje mtoto wangu ajue talanta zake?

kila mtoto ana talanta spesheli na akizitumia vizuri zinazidi kujengeka kwa kumtumika Mungu na kuhudumia watu. Mwambie mtoto hakupewa talanta ajivune au ajisifu, ila kwa utukufu wa Mungu. msaidie mtoto kujenga talanta kwa kumpa ujasiri, uhuru , kujiamini ili zitokeze. Mungu anatoa talanta na mtoto anakuwa na shauku ya kuitumia. Unamjua mtoto kuliko yoyote, je anapenda nini, ana maumbile gani. Usifanye kosa la kuendeleza talanta yako kwa mtoto kwa vile uliizika (hasa kama mtoto hana hiyo). Mwonyeshe mtoto mambo mbali mbali yatakayofanya talanta yake kutokeza, kama vyombo vya muziki, fasihi, michezo, taaluma. Mfano waweza kununua darubini telescope na kuona kama mtoto apenda kusoma mambo ya fizikia yahusuyo nyota. Vingine hata si ghali mfano filimbi yawesa isifikie dola 10, ila mtoto aweza kujifundisha mwenyewe nyimbo ukashangaa. Ukuze udadisi na shauku ya mtoto katika vile vizuri anavyovipenda. Itamsaidia pia matatizo ya kuingia kwenye ukorofi!. Lazima uwe na magoli na hata watoto waishi kwa magoli. Mambo mengine yaonekana hayawezekani ila kama Mungu ametoa talanta itashamiri tu. Beethoven wa ujerumani alikuwa kiziwi akatunga nyimbo nzuri sana na kucheza piano, ni nani angetegemea hayo? Mungu ametoa vipaji, hataki tuvipoteze au tuwe wavivu. Umashuhuri si lazima kujulikana au kuwa na cheo ila kutumia talanta Mungu ametupa. Edison alisema kuwa na akili nyingi au intelligence ni “2% ubongo na 98% mitulinga”. Kingereza twasema 2% brains na 98% hard work. Kuweka magoli ni muhimu, mwambie mtoto wako aweke magoli na kuanza kuyatekeleza kama kuranda na kutengeneza viti kila siku, kufanyia mazoezi mashine ya kushona au vyombo vya muziki

kwa dakika 20 kila siku nk. Msimulie mtoto wako watu mashuhuri waliotumia talanta zao kama vile Mzee Morris na ngoma zake kumi, Kambarage Nyerere, Jomo Kenyata, Patrick Lumumba, Mandela n.k. Mwambie azifikie nyota au vito juu. Fikia nyota moja kwa wakati mmoja, na zile za karibu na endelea kufikia zingine. Mpongeze akifikia nyota, na kuna zingine pengine asifikie ila asikate tamaa na aendelee kufikia zile zinazoweka kushikika. Kuna maswali dodoso (questioneer) zaweza kuwa msaada kudadisi pia, nilituma kwa watoto wangu nikapata mwanga kidogo.

96 nawezaje kuwapa watoto wangu motisha?.

Kuwatia watoto moyo ni muhimu sana. Mara zingine tukimwona mtoto anachezea tiara au pia (kite or top) tunamgombeza ila watu wengine kama Benjamin Franklini wamevumbua mambo ya umeme kwenye michezo ya aina hii. Majaribio mengi ya sayansi na ugudunzi yalianza watoto wakiwa wadogo na wazazi wao wakiwatia moyo kufanya majaribio, kukuza talanta au kucheza michezo Fulani. Pengine kwaajili ya umasikini waweza kufoka “usitumie cherehani yangu au msumeno”. Hili ni kosa ambalo wengi tunafanya. Mtoto wako anakupima namna gani katika kipimo cha kumtia moyo? Jaribu kumwuliza! Kukosoa, kutaka mtoto awe mkamilifu katika ustadi au kuwa na mawazo chanya kunafanya mtoto akate tamaa na kujifikiria hawezi au ni duni. Ujasiri wako wa kumtia moyo unajenga mtoto kujiamini kwamba anaweza (confidence). Mwahikikishie mtoto wako ana talanta kumi au zaidi! utamweka kwenye mahali pa kufanya mengi ukimwongoza. Kuna mtu anaitwa Barnabas ambaye maana yake ni mwana wa matumaini –encourager. Ni tabia nzuri Ambato wote tumlilie Mungu tuwe nayo. Jifunze tabia hii kwa watoto hata kwa wengine ukiwatia moyo. Kwa wale wenye maofisi au biashara mweke mtoto wako katika shuguli, hata wa miaka 8 utashangaa anavyojifunza na siku hizi mambo ya computa marafiki wameniambia watoto wao baada ya kufundishwa wamewasaidia mengi na kujiamini kufanya mengi ya kusaidia wengine. Akikosea mpe moyo “jaribu tena”.. tia moyo, tia moyo tia moyo. Kamwe usiseme “najua ungeshindwa”.watoto wana udadisi na kuuliza maswali ya “kwanini”. Mahali pa usalama usiogope watoto kuchafuka wakijifunza. Wakitengeneza vitu kwa kuvumbua wanavithamini zaidi ya kununua. waache watoto wagundue, watajifunza zaidi ya kuwaambia. Kuza udadisi wao

97 Nitawasaidiaje watoto wangu kutofautisha baya au jema?

Mtoto akiwa mdogo ni rahisi unamwambia hili baya hapana usifanye na hili zuri. Ila anapokua inakuwa kazi. Yaani nyeusi na nyeupe inakuwa rahisi kutofautisha, ila kijivu ni ngumu kidogo. “inabidi tufundishe watoto wetu toka udogo, wakiamka, wakitembea na kwenda kulala” neno la Mungu.. ila watoto mara nyingi wana nia ya kufanya mema ila wanajikuta wamefanya makosa. Je inakutokea nawe pia? Mtume Paulo kwenye matendo saba alisema anapata shida hii. Ikiwa wameiona, waeleze kuhusu tatizo la dhambi lilivyoingia duniani. Watoto wanajitahidi kuwa wema wakifanya makosa wanaomba msamaha na kusema hawatafanya ikifika usiku wameshafanya na kukata tamaa. Shetani ana nguvu na ujanja, watoto kwa nguvu zao wenyewe hawawezi pambano hili. Ila Mungu ameshatupa ushindi kwa Mwana wake.wafundishe wamwombe Mungu aingie mioyoni mwao na kuwasaidia kushinda hii vita. Tunaokolewa kwa neema na Haki ya Mungu. “ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa” wape ahadi hii waidai. Mtoto akiwa mdogo anaona ubaya na wema kwa rangi nyeusi na nyeupe tu ila anapokua anaanza kuona mambo mengine kama nia (will) iko kwenye ubaya uliotokea

au kama ni bahati mbaya na si kudhamiria. Watoto hawajajua kanuni na nia (principles na motives) vyema. Waambie kwamba kutii bila kujua sababu unavyozidi kukua haisaidii sana. Mara zingine waweza kufikiri akipewa adhabu sana kwenye jambo Fulani, basi ndiyo kosa kubwa na si kweli. Wazazi wamsaidie mtoto kufikiri baya na zuri anapoendelea kukua, isiwe ni udikteta wa wazazi ila moyo na nia yake isiwe na uasi. Jadiliana nao kuhusu kanuni. Hata wasipoonyesha wanajali maadili yako waweza kushangaa wakiwa na wengine wanasimamia kile ulichowaambia, na Kutoa ushuhuda wa maagizo yako! Hautaki wawe wanafiki au mafarisayo, ila waweke sheria hizi kwenye mioyo yao. Mfano kudansi au kuangalia filamu mbaya kuna ubaya gani? Kwa kifupi haileti mahusiano mazuri na muumba kwani itakuingiza kwenye uharamia au uzinzi n.k waulize je kwenda mbinguni na kuishi milele na Mungu ndiyo safari yao? Basi lazima wapange na kuishi kutokana na mahali wanataka kufika, magoli yao yawe pale.

98. Je ni muhimu watoto waende ibada?"

Daudi katika Zaburi amesema "njooni tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele ya Mungu aliyetuumba. Kwa maana ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake". Kuabudu kunapaswa kuwa kitu cha kuleta furaha. "mtumikieni Mungu kwa furaha , njoni mbele zake kwa kuimba". Ukiwa katika nyumba ya ibada chunguza watoto wako, je wanajifunza kuabudu? Je wanampenda Mungu na kuwa kwenye nyumba yake? Au wanazungumza, kulala ,kusoma na kucheza? Je watu wazima wanatoa mfano mzuri. Je wanakuwa na mawazo gani kuhusu kuabudu? Kuabudu yapasa kutoke kwenye mioyo yetu na kububujika bila kulazimishwa. Ni kupenda kuwa karibu na Muumba wetu. Kile ambacho watoto wako wanaona watu wengine wakifanya kanisani kisiwe ndiyo viwango watoto wako wanapenda wawe navyo. Jaribuni kufanya kiwe kitu ambacho mtoto wako hapendi kukosa kwa 'kina' ya thamani yake.. Endapo una watoto wadogo na wanashindwa kutia makini waweza kwenda nao nje na kuwasomea kitabu au mambo ya asili yahusianayo na kuabudu. Fanya nyumba ya kuabudu kiwe kitu cha furaha na si mahali pa kufoka na adhabu. Jinsi watoto wanavyokua, washirikishe katika kuchagua nyimbo, mafungu, kuandika. Weka viwango vyako vya kuabudu, la sivyo utaona wanakopi watoto wengine kanisani na kuanza kufanya yasiyo ya kuabudu. Kabla ya kwenda kanisani chukua muda msiende mkiwa na kukosoana, kukasirika na kuharakishana!. Watayarishe watoto kimawazo, fikeni mapema. Hata waweza kutoka mapema na kuchukua muda na kuzungumza hata kula kifungua kinywa kwenye viwanja kabla ya kuja kanisani (picnic). Pengine hata kabla ya mahubiri watoe watoto nje mzungumze na kutembea kidogo ili mawazo yao yawe tulivu. Mkitoka waulize pia kwamba wamejifunza nini?: na wanawezaje kutumia kwa maisha ya kila siku?. Kama ibada haipangwi kwa kujali mahitaji ya watoto waambie viongozi. Programu ziwe na hadithi za watoto, mafungu, ushuhuda, kwaya ya watoto, wakaribishaji watoto, maswali kwa watoto, ibada ya watoto mara moja kwa mwezi, au watoto wawe na huduma yao, au watoto wakubwa kuhubiri mara moja kwa miezi miwili n.k

kuimba nyimbo, kukariri maandiko na, kusali, hata kusoma ni elimu kubwa kupita zote dunani, hivi vyamsaidia mtu kuliko kitu kingine.

99 kazi gani nimpe mtoto wangu napata shida kuamaa, ana miaka 6?

kazi ni muhimu kwa tabia ya mtoto sana. Inafanya mzazi atawale nia ya mtoto (willful transgression not to be overlooked)-" kutotii kwa kunuia kusiachwe kiholela " alisema

Susan Wesley mama wa watoto 19 kutoka Uingereza. Tumia adhabu kama mtoto analeta uasi wa wazi wazi au anapiga mamlaka ya mzazi. Angalia list kwenye sura ya kazi na website ya "401 ways to get your kids to work at home by Mc cullough". Njia 401 za kufanya watoto wako wafanye kazi za nyumbani. Nimetoa muhtasari wake kidogo. Kando na kumweheshimu Mungu kama Mwenye Enzi, linalofuatia ni kujua na kupenda kazi. Watu husoma ili wapate kazi. Mtoto apasa afundishe ustadi, Nimepata shida kufundisha watoto, ila mara zingine nikiwapeleka kwa mtu mwingine wafanye kazi kwake hufanya. Fanya juu chini, na kuomba hekima, mtoto asiyejua na kuthamini kazi ni mzigo kwake, jumuiya na kwa yule atakayemwoa au atakayeolea naye. Uvivu si tabia ya mbinguni. Biblia inasema asiyefanya kazi asile! Agizo zito. Je waweza kusema asipokula itakuwaje? Hebu tuangalie chungu chungu na siafu walivyo na bidii!

100. kubariki nyumba au mtoto kuna maana gani?

Watu wengi mtoto akizaliwa wanaita watu wanaompenda Mungu na kumtoa wakfu mtoto ili aweze kumtumikia Mungu na kuhudumia watu. Jambo hili ni la muhimu sana. Na ni vizuri sadaka itolewe. Watu wengi wametumia pesa nyingi kufanya sherehe za siku ya kuzaliwa ila wamesahau kutoa sadaka kwa masikini, wajane au yatima. Ni vizuri kwenye sherehe hii ya kumkakabidhi Mungu mtoto wetu, tupate kufikiria wengine wenye mahitaji. Waumini wengine pia watoe ahadi za kusaidia watoto katika jumuiya hiyo. Inachukua kijiji kulea mtoto awe mwadilifu. Watu wengine pia hutoa nyumba zao wakfu. Mungu ana kusudi maalum kwa kila nyumba. Familia yaweza kufanya vingi vizuri kwa watu na kwa Mungu, na shetani anawasukuma kwenye mengi maovu hivyo ni muhimu kuwa na maombi maalum ya kuweka wafku nyumba ili mfanye kazi pamoja kwa furaha na upendo. Familia moja iliamua kuiweka nyumba yao wakfu kumtumikia Bwana na kuita mchungaji wao na wageni kufanya karamu ndogo. Waliandika kwenye ukuta "Nyumba hii ya Masaka Momadi imewekwa wakfu tarehe 20/11/2001 ili kumtumikia Bwana na kuhudumia watu". Unaonaje leo uanze kupanga karamu hii na kuandika ukutani mwako maneno haya ambayo yatakuwa ushuhuda kwa wageni wako na kwako, na utaposahau magoli yako ya maisha utajikumbusha ukiyaangalia tena na tena na kupata tochi kumulika hata siku ile ya asubuhi njema.

Au waweza kuandika "chagueni leo ni nani mtakayemtumikia, ila mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana"

chukua muda kuwabariki watoto wako kila siku, upatapo nafasi wawekee mikono vichwani na wape baraka.

101. nifanyeje mtoto wangu ajue anamhitaji Mungu na inabidi amfahamu

kujua sheria za mpira haziwezi kumfanya awe mchezaji bora. Ila maarifa anayopata ya sheria ayatumie yeye mwenyewe. Kujua kuhusu Mungu ni muhimu , ila uzoefu wa kuwa na mahusiano naye wahitaji mazoezi. Waambie watoto ushuhuda wako na waulize maswali katika hatua zote za ibada ya familia. Maombi yenu yaandikeni na yaliyojibiwa shukuruni mkiwa wote. Mtoto wako ajue unaomba na kujaribu kuishi maisha ya kumtegemea Mungu. Wape nafasi watoto kwa mzunguko kuongoza ibada. Personal responsibility ni muhimu, kila mtoto hata wa miaka 4 afundishwe kuomba mwenyewe na kujenga imani yake, maana ukiwa haupo nani atamsaidia? Mtoto hatafika mbinguni kwa wewe kumpenda Mungu. Mungu hana wajukuu ni watoto tu. Imani yabidi itoke kwake mwenyewe si mtumba wa imani yako!. Amtegemee, amwamini na kumtumaini Mungu. Aone uzuri na upendo wa Mungu upitao kina, marefu na mapana kwake. Kwamba hata wewe au yeye

humependi vile kama Mungu wa mbinguni. Mwambie twamwitaji Mungu ila hatujui mpaka tusipojiweza na njia zote zimefungwa kama Naamani aliyekuwa na ukoma! Mtoto asifikiri kwamba anaweza bila Mungu. Nadharia zingine mtoto hawezi kuelewa ila ya upendo wa Mungu, watoto wengi wanaelewa vyema kuzidi watu wazima na ndiyo maana 75% ya watoto humpokea Mungu mioyoni mwao kabla ya kufika miaka 10. tuonyeshe watoto kwamba Mungu ni halisi katika maisha yetu. Toka mtoto anapozaliwa usikazanie hadithi zisizo halisi kama za superman, zimwi. Mwambie wokovu ni bure ukiupokea, toa mifano mfano chukua hii sh 100 ni zawadi, je yabidi urudishe au ulipie? La. Hitaji kubwa la mtoto ni kuokolewa, na Mungu anasema "Niangalie mimi mkaokolewe,enyi ncha zote za dunia, maana mimi ni Mungu na hapana mwingine". Kila mtoto anazaliwa pagani au kafiri, mpaka afundishwe imani, na kisha aipokee na kuifanya kuwa yake mwenyewe.

102. tunafundishaje watoto wetu kusali?

Tunaambiwa kuomba bila kukoma. Mara nyingi watoto wetu wanasali kama desturi bila kufikiri, wakila au wakienda kulala. Walisema maajabu 7 ya wanaompenda Mungu ni kama "kuombea chakula kupita maisha yao, kuangalia TV kwa muda mkubwa kuliko kusoma Neno la Mungu nk). Sidhani kama tungekuwa na marafiki kama tungezungumza nao wakati mambo yameenda vibaya tu. Ili kujenga mahusiano yapasa tujadili, tuambiane habari, kuhusu yanayotokea katika maisha yetu ya kila siku. Mfundishe mtoto wako azungumze na Mungu kama rafiki, amweleze yale ambayo yanaendelea maishani mwake " leo asubuhi nilicheza mdako au , mama alinipiga viboko bila haki nami nilishangaa je Baba wa mbinguni nawe ulionaje pale ? nafikiri rafiki yangu alifunga goli zuri leo' . Wafundishe watoto wako kuwaombea wengine pia, wakiona matokeo mazuri imani yao itajengekea na kupenda kuomba zaidi. kusali ni kuzungumza na Mungu kama rafiki, kunaleta faraja na matokeo ambayo yanatufanya tukaribie na Mungu na kuwa na furaha. Kama mzazi nimejikuta napenda kuongea mno, na marafiki na watoto n.k. Bali sina muda wa kuomba, na wakati kuomba ni kuongea na Mungu. Nimejiuliza inakuwaje nina maneno mengi ya kuongea, blah blah ila ikija kuomba au kuongea na Muumba wangu, maneno yanakauka?!! Je hili limekutokea wewe pia? Tuombe Mungu atuhurumie kwani mambo yote ya kimbingu ni mpando, lazima tukiamka twende magotini, asubuhi mchana na usiku, na zaidi ya hapo. Tujifunze 'kupiga porojo na Mungu" kama vile marafiki zetu.

102. Twawezaje kuwamotisha watoto wetu kuona kwamba mbinguni ni mahali ambapo ni muhimu kuliko kote kufika?

maandiko matakatifu yanaonyesha mbingu, ahera au paradiso ni mahali pazuri sana. Uzuri wake wameshindwa kusimulia binadamu "macho hayajaona, wala masikio hayajasikia, wala hayajaingia katika masikio ya binadamu mambo ambayo Mungu ametayarishia watu wake". Baadhi ya mambo yaliyosemwa ni hakuna maumivu, vilio wala kifo. Majengo ya vito, barabara za dhahabu, vyakula vya kupendeza macho na ladha vya pekee. Mito ya kupendeza, moyo kupata raha na kuridhika , urafiki, kucheza na wanyama kama simba na amani ipitayo akili yote. Ni sehemu ya lazima kufika! Mahali pa ajabu. Mbinguni ni mahali, si hali, mahali panapofurahisha watoto. kutakuwa na michezo na mengine mengi. Usimfanye mtoto afikiri mbinguni ni kuishi kwenye majumba makubwa bila anaowapenda au kiupweke, au mbinguni kutakuwa na watu tu na si wanyama au utakuwa unaelea mawinguni ukipiga vinanda masaa 24! Ila jipe moyo katika ulezi, usihofu wala usiogope kwani pambano ni la Bwana.

Mbinguni ni mahali kila mtoto au mtu ataridhika kwani kila mmoja atakuwa na uhuru anaoupenda usiokuwa na dhambi.
Endelea kuzungumza na watoto wako kuhusu mbingu, ni tumaini la baraka hautajuta kuwa kule na kila mtu atapata vitu vya kufanya na kufurahia au kufurahiana na wengine! Onyesha mbingu kuwa nzuuri sana kulinganisha na dunia yetu ambayo imekuwa kama tambara bovu lililochoka. Wewe na watoto wako njozi zenu mziweke kule, na mnuie na kufanya matayarisho kwamba siku moja mtakutana kule kwenye kiti cha enzi cha Mungu! Jambo la kufurahia kukutana kwenye mto wa uzima au mti wa uzima. Tukilenga mbingu tutapata mbingu, ila tukilenga sifuri tutapata sifuri. Hivi kuna cha kulinganisha hapa duniani kweli. Basi utii wetu na watoto wetu unaanza hapa maana mbinguni Dhambi haitainua kichwa chake tena Nah 1:9. Maana hakuna anayetaka kustarehe mbinguni kisha mtu akaja kumpiga konde, au akamwibia kiatu chake!

103. Nimpeleke mtoto wangu wa miaka 6 shule gani kusoma?

Zamani tulipeleka watoto wetu shule za serikali bila kujali sana. Ila tabia za jumuiya yanazidi kupotoka. Ni muhimu sana uamue kwamba jambo muhimu katika maisha yako ni nini? Kwa upande wangu kama mtoto atasoma nyumbani na kukaa na mama mpaka darasa la nne, itakuwa kitu chema sana. Vitabu vyaweza kununuliwa na mtoto akajifunza nyumbani na kuwa na mwalimu mmoja mwanafunzi mmoja, kwa kawaida mtoto anajifunza vizuri kuliko mazingira mengine! Ila kwa sababu wakina mama wengi wameingia vibaruani, na wengine hawajapata fununu kumfundisha mtoto wao nyumbani, hapo ndiyo shule za kuchagua zinakuja. Kwangu ni muhimu mtoto afunidishwe imani, kusoma na kulitii neno la Mungu aamkapo na aendapo kulala. Hivyo, kama familia ina uwezo ipeleke mtoto kwenye shule inayofundisha imani ya kumpenda Mungu. Sipendi kupeleka mtoto wangu shule yoyote. Najua shule nyingi zenye ushindani ni nzuri mtoto asiwe mvivu. Mtoto anapasa kujali matokeo yake ya mtihani. Mzazi apeleleze vizuri kwenye wizara ya elimu, kwa wazazi wengine na kadhalika kujua shule nzuri kwa tabia na taaluma. Kuna wengi ambao itabidi wapeleke mtoto wao kwenye shule ya jumuiya kwa vile hawana uwezo ila mzazi mfundishe mtoto wako nyumbani pia. Niliona watoto 100 kwenye darasa moja. Na pia kuna shule mama Fulani aliniambia mvomero miaka ya nyuma, ilikuwa na watoto kama 700 na mwalimu mmoja!. Je mzazi aweza kununua vitabu na kuanza kufundisha mtoto wake hesabu na kusoma darasa la kwanza na la Pili? Wazazi wengi wajua kusoma. Kitabu cha kujifunza kusoma mwaka huu nimeona ni kama dola mbili au tatu. Watu wengi wanapesa ya kununua vocha/credit za simu , je vitabu si muhimu zaidi? mtoto wako asifike darasa la pili hajui kusoma na kufanya hesabu rahisi, mtoto anayekumbuka kwa wepesi huchukua miezi 3 tu kujua kusoma!

105 Watoto wangu wanagombana mno nifanyeje?

Wanandugu kugombana imekuwapo toka wakati wa Kaini na Habili hata kabla ya runinga! Chanzo kikubwa ni mashindano na wivu, kwa kifupi ni mimi . mimi, mimi (me, myself and I). Kitu kikubwa usiwalinganishe, kwa na kuwa na upendeleo. Usilinganishe tabia, maumbile, taaluma au talanta. Hili limekwaza wazazi wengi. Endelea kufuwafundisha tabia au kanuni ya kuishi pamoja, wengi wanapokua tabia hii hupungua, na kupendana sana. Wanasema watoto wanaofuatana ndiyo wanaoneana wivu sana. Kitabu cha Warumi saba kinaeleza msingi wetu wa kufanya maovu “kile tupendacho kufanya hatufanyi, bali

tusichopenda cha dhambi twajikuta tumefanya! Ole wangu mimi, ni nani atakayeniokoa katika mwili huu". Mkumbushe mtoto kwamba ibilisi apenda awe analumbana na kuwa kama bisi, ajitahidi kumpinga, ni mafundisho ya kila siku, na kuomba Mwenyezi rehema zake. Nimeona maombi tu ndiyo silaha. Spurgeon Mhubiri alieyeanza kuhubiri akiwa na miaka 16, na akiwa na miaka 20 alikuwa na kanisa la zaidi ya watu 2000 alisema "Ni afadhali nifundishe mtu mmoja kuomba kuliko kumi kuhubiri". Maombi ni nguvu nyingi katika maisha ya ulezi, waombee watoto.

106. Nina mtoto ambaye ana uzuri wa uso, ana miaka 8 na kila mtu anamsifia, je hili ni jambo zuri.

Kwenye dunia yaleo ambayo watoto wengi wanaanza kutojiamini na kutojithamini, itamsaidia kujikubali. Uzuri imekuwa kama nguvu (power) hasa kwaajili ya runinga na mambo ya maonyesho mengine. Ila hili laweza kuwa hatari, kwa mfano kwa msichana wa miaka 14 ambaye ana uzuri wa uso na shepu nzuri, aweza kupata attention ya wavulana nyingi na kumwingiza kwenye majaribu ya ukahaba na kuharibu maisha yake. Hivyo mzazi ni vyema amwambie japo kuna macho yanakutazama, wewe ni nani na malengo yako duniani ni gani. Kushugulikia usafi wa moyo, taaluma aambiwe ni muhimu. Maana hayo hayatakimbia, yana siku zake yanakuja tu. Utafiti ulifanywa wa wasichana na wavulana wazuri baada ya miaka 25 waliona kwamba wengi walikuwa na ndoa zisizo na furaha. Hii ilitokana pengine na mashindano ya watu wa tabia mbovu kuwakimbilia. Wa wastani au mtu mwenye sura ya kawaida anapata wale watu wanaompenda kwaajili yake na si sura au talanta. Na pia uzuri unapoisha uzeeni, kwa wale wanaoingiza uzuri kichwani kupita kipimo wanachanganyikiwa kwamba sasa hakuna anayewatazama au kuwathamini sana. Wamekuwa wa kawaida na hili laweza kuwaletea shida. Kazania tabia ya kicho kwa Mungu, ndiyo Uzuri bora lupita wote. Mcheza filamu Marilyn Monroe ni mfano wa watu waliopata hiyo shida. Mara nyingi ukiweka uzuri kwanza kuharibikiwa ni kwingi. Kupima mtu kutokana na uzuri wa sura au talanta ni makosa. Mmeona hili limetokea kwa wacheza muziki wakikimbiliwa na watu ila maisha yanalemea pande moja. Wazazi hapa epukeni kulinganisha watoto, na kusema maneno bila kufikiri kwa watoto wengine "nywele zako mbaya, kipilipili cha kutisha" ni nani alikuambia kwamba nywele fulani ni mbaya au nzuri? Muumba wetu hajaandika hayo kwenye Neno lake?.

Mtoto anathamini tathmini yako. Usimfanye apondeke moyo bila sababu. Watoto wanahitaji kupendwa na kukukubaliwa. Kaka Restrapo alisema kwamba shangazi yake mmoja alipendwa kuliko wengine kwasababu alikuwa na rangi ya kahawia, na nywele zilizonyooka, na akaruhusiwa kufanya vile ndugu zake hawakuruhusiwa, hii ilimfanya asikomae (immaturity), hata leo ana miaka 70 bali ana mazungumzo ya kitoto na kila alipoolewa aliachika kwa kutoheshimu watu kule. Hichi ni kilema kibaya Kumpa mtoto

106. ***Madoli ya kampuni ya Barbie yana wanasesere watu wazima warembo sana wenye maziwa, wengine hata wana mimba. Watu wengi wamesema si mazuri unafikiriaje***?

Kwa upande wangu hata mimi madoli ya namna hii sipendi mtoto wangu awe nayo. Kwa namna fulani yanakuza uzuri wa sura, uasherati na pesa. Mtoto anaanza kujipima na madoli hayo. Mtoto anapocheza anahitaji sanamu za watoto wadogo si watu wazima. Watoto hawa ni wadogo, wasikuzwe kushugulikia mambo ya watu wazima hata upevu wao wa mambo ya kiutu uzima utakuja mapema bila kupanga. Chagua wanasesere wako vizuri, chunguza. Wengine wana majitu ya kutisha tisha ya mazimwi kama Ninja, ndiyo

wanasesere. Macho kama ya nyoka n.k. Unajenga mvuto wa aina fulani pia na hayo. Watoto wadogo wachezee vitu vya kawaida visipeleke mawazo yao pale ambapo haisaidii kimaadili, kijamii au kiroho. Wasipende kufanana kwa nguo, rangi, miziki au maneno na hawa wanasesere. Mtoto wa kike aliyekuwa na sura ya kawaida akijilinganisha na hawa ataona kama ameachwa na basi na si kweli. Thamani yake si kuonekana kama hawa wanasesere. Mungu anamthamini kama yeye. Mungu ameumba watu tofauti kwa utukufu wake.

104. ***Nimesikia mtoto wa katikati ana shida ya kujiona hana nafasi maalum kwenye familia*** ?

Nni kweli , mtoto wa kwanza au wa mwisho, au mtoto wa kwanza wa kike au wa mwisho wa kiume wanaona wana sehemu maalumu katika familia kuliko mfano msichana wa tatu na wane katika familia ya watoto 5. Anakuwa amezaliwa pia wakati amekuta wengine. Na wengine baadaye wanamfuata anakuwa katikati. Wazazi wachukue muda wa kuwaonyesha watoto wao kwamba wanawathamini, na hasa watoto wa katikati. Mama na baba wachukue muda wa kutembea na mtoto mmoja mmoja, kwenda mahali hata kama ni karibu sokoni, ili wajue wao si namba tu. Au wapewe nafasi ya kuchagua mahali au kitu mara ya kwanza ili wajue wanathaminiwa kama wao. Dr Lehman ameandika mengi kuhusu nafasi hizi, ila si kanuni ambazo hazibadiliki, ni general information.

Nnawaachiaje watoto wangu uhuru waende makwao wakiwa watu wazima?

Hili ni jambo gumu sana maana kwanza tunafikiri hawako tayari na watapata shida ulimwenguni na watu hawatawafanyia mema kama sisi. Pengine tunaona wapo hatarini kiasi Fulani. Jambo jema kupita yote kwa mtoto wako ni kumfundisha aishi bila wewe! Kuwa tayari kuwa huru ni kwamba umewafundisha majukumu! Tumefanya kazi ya upendo, na sasa imeisha! Tuko ukingoni hatujui kama tulie, tufurahi au tuendanaje na upweke. Tuna tiara mkononi tuiachie? Ila mara zingine tunaona ugumu kuwaachia kwa vile thamani yetu ya maisha ilikuwa imeganda kwa watoto hawa, na tunaogopa watakuwa huru na hatutakuwa na nguvu nao tena. Au tulikuwa hatutajenga mahusiano na wake au waume zetu, na sasa hatuna cha kuzungumza pamoja (empty nest syndrome). Kuna wakati kwa kila kitu, wakati wa kutupa jiwe na wakati wa kuokota. Umefika wakati wa kuiachia tiara iende, umeshafanya kazi yako. Iachie tiara iende ili muwe na mahusiano ya urafiki mapya yenye zawadi zake. Tiara itajiachia kwenda yenyewe hata usipoaichia ila wewe iachie wakati ufikapo ili iende kwa namna nzuri. Msiachene kwa magomvi na malumbano achaneni kwa upendo mkifurahiana

105. Je niwalipe watoto wangu kufanya kazi za nyumbani?

La hasha! Watandike vitanda vyao, maana ni wao wanavilalia. Wasafishe vyombo maana ni wao wanakula! Usizoeshe kulipa watoto kwa kazi. Waweza kuwalipa kwa kuwapa motisha kazi chache mno. Mfano kusafisha baiskeli ya baba, kulima bustani zaidi ya mpango wa kulima wa kila siku n.k wakumbushe, matumizi ya pesa ni mahitaji na si matakwa. Watoto wanapenda wanunuliwe hiki na kile kama sisi watu wazima tu. Pesa yenyewe ni ndogo hata kwa mume na mke sasa watoto wakitaka itakuwa ngumu. Ukiwa na uwezo kuwapa pesa ya posho kidogo mara moja kwa mwezi si vibaya , ila wabuni miradi yao. Waweza kuuza mayai ya kuchemsha, au magazeti au maji. Wasaidie kubuni na wape mtaji wafanye masaa Fulani kwa wiki. Zaidi wapaswa kuwasaidia kwenda chuoni, kupata ardhi, mitaji au ustadi wajitegemee. Huo ndiyo urithi wao. Ila wasitegemee

kwamba utawapa mali. Jaribu mali usaidie watu wenye mahitaji kama yatima, wajane, masikini na kazi ya kuongeza ufalme wa Mungu. Hata kwenye hati ya mirathi usisahau ukiwapa watoto wako kitu kumega fungu la kusaidia kazi ya Mwenyezi Mungu. Ni haki hata mimbo mingi ya taifa yaomba Baraka toka kwa Mungu hivyo najua waafrika wengi Mungu ni ngao na baraka kubwa.

106. Nitajuaje watoto walio kata tamaa, wasiojithamini au walio na huzuni? Discouraged or depressed

Dalili za watoto hawa ni kutotulia mahali pamoja, kujitenga pembeni na wengine (withdraw), wanakuwa wazito na kutofautiana na ratiba ya watoto wenzao, wanakuwa wakaidi, wenye uvumilivu mdogo, wanafikiri wanahitaji hiki au kile kama marafiki zao. Wanakuwa wakali na wana tabia ya kuvunja sheria. Vya kuangalia hapa ni kama tabia yako! kwanza je unafoka foka, na kumkejeli bidii zake? Unazungumza na mke au mume wako kwa adabu mbele ya mtoto?. Mara zingine ni kumpeleka kwa tabibu aende kumwangalia kama kuna shida ya afya kama matezi n.k. mtoto mshugulishe na kumfundisha nyumbani kwa mpango na ratiba na pia asiwe anakula vitu vya sukari, mafuta, kukobolewa au chumvi nyingi. Mtoto afundishwe kujikana nafsi na kuhudumia wengine nyumbani, kwenye jumuiya au kwa wagonjwa. Angalia kama ana lishe bora, na mazingira ya kufaa, waombe wataalamu pia wakusaidie.

Nitatoa mfano mmoja wa Ninapoishi: waligundua wavulana wadogo weusi (Black americans) walikuwa na shida za hisia kuliko wengine. Mwalimu mmoja alisema ilitokana na kuishi na mama tu bila baba, na mama wengine walikuwa wana tabia ya kuleta marafiki wa kiume nyumbani, na kumkemea kemea mtoto. Mtoto alijiona ametengwa, na kuishi kwa hofu. Watoto hawa walizaliwa na urithi mkubwa wa akili, ila baadaye hisia zao zilikawa nzito na kuwafanya wasijisomee, na kujiachia kimasomo

107. ***Nina mtoto kilema je nifanyeje naye ili aweze kujenga ustadi?***

Watoto wengi vilema wanaachiwa wajifunze na kupata maarifa wenyewe hasa kwenye nchi zetu za kiafrika. Upendo ndiyo hitaji lao kubwa na kisha peleleza habari za watoto kama hawa na jinsi ya kuwasaidia. Wawe vipofu, viwete, viziwi, bubu, wanaojifunza pole pole n.k. wanaweza kuwa na upungufu kwenye hiyo nyanja moja ya maumbile ila wana talanta nyingine tu. Mungu anawapenda kuliko sisi. Mzazi anza kuzifanyia kazi hizo kwa mpangilio na ratiba. Wengine wameweza kutumia vyombo vya muziki. Usiruhusu mtoto kuitwa majina nawe au wengine. Mpatie nafasi ya mazingira mbali mbali ya viasili, miti au maua. Wengi waweza kufundishwa bustani, kusuka vikapu, au kusoma kwa tarakimu tofauti za kugusa na vidole (braille). Fanya nao kazi na kuwashugulisha, usikae tu na kuwaonea huruma na kuwalemaza maana wengi wanaishi maisha ya kawaida hata kuwa na miji yao. Wale wanaosikia wasomee kila siku. Hata kama una kitabu kimoja tu cha neno la Mungu kinatosha. Uwe na utajiri wa uvumilivu, upendo na uelewaji. Kwa wale wenye shida ya viungo, uliza ushauri wa mazoezi ya viungo. Wafundishe thamani ya huruma, kupewa majukumu, uaminifu n.k, Zaidi omba nao na kuimba nao toka wakiwa wadogo wamwelewe Mungu kama rafiki, na wajifunze kumtukuza. Naomba uangalia maisha ya kijana Nick vujevic kijana aliyezaliwa Australia bila mikono, miguu, ila alikuwa anaona hana tabú au hakutahayari (Google tovuti -no hands, no legs, no worries). Huyu alitaka hata kujiua maana watoto walimcheka sana akiwa shule toka utoto. Mungu alimsaidia kupata wazazi wanaompenda Mungu na kumpa faraja ya Mungu, hii ilimfanya ajithamini. Amezungumza kwa watu milioni 4, ameoa na ana mke na mtoto. Anatembea dunia nzima

kutia watu wazima na watoto moyo. Amekutana na vile wengi sana. Anasema hata hawezi kumkumbatia mkewe au mtoto wake, ila mbinguni ataweza kufanya vile, hata kuweka mikono mifukoni. Hebu mzazi apeleke kutindikiwa kwake kwa Mwenyezi Mungu atafarijiwa siku kwa siku na kushinda.

111 Sipendi kurudia rudia mambo na kuonekana kama nafuatilia sana mtoto, nataka niwe Mwema (sweet) kwa mtoto.
mtoto anahitaji kufuatiliwa, na kuambiwa mambo Fulani akifanya vibaya inabidi uzoee hili akilini mwako. Ukiacha kufuatilia ufanisi unakuwa mdogo. Jitahidi kutawala sauti yako isiwe ya kufoka, uwe na uvumilivu, na mtoto aone uko upande wake (best interest). Ukisema uachilie tu, na hasa wakati ukiona mambo yameharibika utakuwa na hasira kali zisizoweza kutawaliwa (lose control). Hiki nimekiona kimetokea, hasa kwa wakina baba. Wakina mama wanaonekana wanambana mtoto na hawamwachii nafasi, mpaka mtoto anaona kwamba baba ni afadhali, baadaye baba ambaye amejiziuka akiona mambo yameharibika na alikuwa hana hata fununu, anapoteza uthibiti, na kuanza kugomba na kutoa adhabu nzito nzito, pahali ambapo angekuwa amefuatilia asingefikia stage ya kufanya kitu ambacho hata baadaye akajutia.
Zaidi ya yote, mtoto ajue kila kitu kina matokeo (consequence), mfano usipotoa magugu kwenye bustani leo, basi sitakuchukua kwenda mjini na wewe. Saa ikifika ya kwenda mjini mwage uende. Jaribu Kutna matokeo (consequence) zile anazozipenda. Mfano maliza kupiga deki, ndipo utakula Chakula cha mchana. Sipendi Kutoa adhabu na Chakula, ila ukiona mtoto ameshakula kifungua kinywa, basi aweza kuvumilia, adeki ndiyo ale Chakula cha mchana. Marafiki zangu wanaofundisha watoto vyombo vya muziki, watoto wanaochukia mazoezi, waliona ni vyema wabadilishane na mama wengine, ili waendelee kuwa na urafiki na watoto. Mungu atakapa hekima. Nami sijafuzu nipo bado msituni kwa hili, tuombeane!
Ila Narudia, kwaajili yang una kwako, upendo Wako kwa mtoto ulingane na adhabu, kama unamchukia mtoto, usimpe adhabu,

108. mtoto alitishia kujiua nikaona ni maneno tu na akajiua, nasikia dhamira inanishitaki pengine ningefanya kitu Fulani angekuwapo leo

kwa kweli swali hili ni gumu na hakuna anayeweza kulijibu maana sisi hatujui mtoto anafikiri nini, ameumia au kuumizwa kiasi gani, anasoma au kushirikiana na nani au kwa kifupi ni nini kimetendeka?. Mzazi mmoja mtu mzima alienda Marekani na mke wake kusomea uchungaji, akasema akamwacha mtoto wake wa form 3 boarding na walezi pia wa kuangalia mambo. Mtoto alitishia kujiua wasipokwenda naye Marekani. Baba alimwita mtoto akasema “ukijiua sisi tutasikitika sana, kwani tunakupenda mno. Ila wewe una uamuzi. Sisi tunaenda kwa muda wa miaka 3 na mama yako na tunatafuta njia mpate visa mjiunge nasi, ila sasa bado mambo hayajulikana kwani hata sisi tumechangiwa tiketi na watu. Wewe vumilia. Mtoto aliendelea kutishia, walikwenda shule marekani mwaka wakarudi kuhubiri nyumbani Tanzania mtoto akiendelea kutishia . walimwita wakamwambia wewe sasa ni mkubwa wa miaka 17, tunakupenda mno. Wakamweleza kwa undani zaidi thamani yake kwao na kwa Mungu “ila kama unataka kujiua, sisi hatuna uwezo wa kukubadilisha usifanye. Ila tutamwomba askofu x afanye mazishi yako maana tunaenda na hatuna uwezo, tuko mbali kuja tena, tutalia sana kwa uchungu, ila wewe

ndiye mwenye usukani wa uhai wako". Mtoto huyu hakujiua alingoja wazazi wakamaliza ile miaka 3. ila chunga sana! watoto wengine huwezi kuwaaambia haya, wataendelea mbele na kujiumiza. Ila soma masomo ya afya kidogo wanasema, mtu akitishia uichukulie maanani, uliza maswali kama, watatumia njia gani, na sababu gani, na utafute msaada wa kisaikologia kushauri, Maana jambo hili ni zito, na huliwezi mwenyewe. Na zaidi ya yote mwombe Mungu Akusaidie, maana hata wao wa saikologia wanaweza chembe ndogo na wao makubwa na mazito yamewatokea wakashindwa kuyahimili. Ni Mungu tu, ndiyo Atakutoa kwenye shimo hilo. Uwe mtu wa kusali ukikikesha

113. ***Jitahidi kumkumbusha mtoto wangu kila mara na sasa ana miaka 11 "piga mswaki, paka mafuta, kumbuka daftari la kwaya " n.k. ni lini nitapumzika nisiongee onge***e. Ana adabu ila ni mvivu na ni goigoi wa mambo fulani.

kwa kweli watoto wengi wahitaji kukumbushwa! Ila yaonekana yale wanayopenda hawayasahau!. Niliuliza watoto wangu mbona mnasahau kupiga mswaki ila hamsahau kula? Kwa kweli uzazi ni kazi ya kujifunza na pata potea nyakati fulani! (guess work) unajaribu kinachofaa kwa watoto kisipowezekana unajaribu kingine alimradi wakumbuke. Watoto wa zamani kwenye neno la Mungu akifika miaka 12 alihesabika kupewa majukumu mengi. Ila Mtoto akiishi kwako bado una jukumu kumkumbusha meno. Andika na ratiba kwenye chumba chao. Mwambie anawakilisha familia yako, hivyo akitoka na chakula kimemwagika kwenye nguo ni wewe unapata aibu. Mara zingine mwambie lazima uache demokrasi na kuamrisha kitu Fulani kifanyike! Kuna haja ya kutii sheria za nyumba. Watoto wanajifunza kuwa watu wazima. Hawajaota mizizi. Tukisoma maisha ya Ezekiel na hata ya Yesu alitoka nyumbani na miaka 30. Mara nyingi kabla ya hapo makosa mengi yafanyika. Uzoefu waja mtu akifika 30 hivi! Pengine mapema kidogo kwa wasichana. Na ndiyo maana wengi waliofanya ndoa baada ya miaka 30 wanavumilia kidogo kuliko waliooa mapema.

Lakini mtoto ajue matokeo ya kutochukua majukumu, mfano hatutakula Chamula cha usiku mpaka nguo zako zimefuliwa, hutapata posho yako ya mwezi huu mpaka umepanda ile miche ya maembe niliyoleta.

114. Mtoto alale masaa mangapi?

mtoto aliyezaliwa kuanzia masaa 18 hivi, mtoto wa miaka miwili masaa 12-13, mtoto wa miaka miwili mpaka sita masaa 12 hivi, mtoto wa darasa la kwanza mpaka la tano masaa kumi mpaka kumi na moja, mtoto wa miaka 12 na kuendelea masaa tisa mpaka kumi. Watoto wale wa miaka kumi na wanachelewa kulala waambiwe walale mapema na wasilale zaidi ya saa nne asubuhi. Watu wazima hata watoto wanaolala sana pia ni shida. Mfano mtu mzima anayelala zaidi ya masaa 9 kila siku aweza kupata magonjwa Fulani. Angalia umri wako na masaa ya kulala iwe masaa 2 kabla ya saa sita ya usiku. Watoto wadogo wa wakilala baada ya saa tatu wanaongeza riski ya kuugua kisukari. upungufu wa saa moja la usingizi kila siku kwa wiki moja ni sawa na kukosa usingizi kwa siku moja nzima, na kuongeza rsiki za ajali. Na deni la usingizi halilipiki! Linauchosha mwili.

116. nilipeleka watoto wakiwa wadogo Amerika kusoma na wananiita niende kuwatembelea ila sina nafasi. Mzee ni mtumishi wa serikali nami nafuga ng'ombe na hakuna wa kumwachia.

Ni muhimu kutembelea watoto. Watoto wanakuwa na ukiwa hasa wale walienda kusoma wakiwa wadogo wa miaka kumi na, mpaka ishirini na. Hawana uongozi, mashauri na marafiki wanaowajali kama wazazi. Wengi hawamalizi shule na wazazi wangejua

wangewatembelea mara kwa mara bila kujali pesa. Watoto wengi wameachia shule katikati. Hata baada ya miaka 10 hawana shahada, na mara zingine wazazi wanaendelea kutoa msaada. Nachoelewa hapa kwamba shida si pesa ila muda. Wengine hata hawawezi kuhudhuria arusi za watoto au kuwapa mashauri ya wachumba. hii imefanya watoto wengi waishi na watu tu bila ndoa. Na kujiletea maumivu mengi. Mara zingine waoe mtu mkatili ili kupata makaratasi (uraia).
Watoto wamekosa watu wa kuwashauri na kupima watu hawa. Wengi ya watu ni wale ambao hawajulikani walipozaliwa, makuzi yao au kama hata waliacha wake/waume nchi walizotoka. Mtoto anakutana na milima, wakati wazazi wanajali ngombe au kibarua!. Nafikiri ni vyema watoto wetu tuwalete wakiwa wamepevuka kidogo, kama shahada ya pili, Marekani si mbinguni, mtoto anahitaji msaada wa mzazi bado ili akabili maisha. Watoto wengi wameacha kumwabudu Mungu, kuingia kwenye ulevi, au maisha ya anasa ambayo familia haiafikiani nayo. Kuna wengi saana wanaokabili maisha vizuri bila kuja kusoma magharibi, fanya utafiti na kuona lile linalokuwa msada kwako na kumpa Mungu utukufu.
Kuna wazazi pia wanaoenda nje ya nchi kwa muda mrefu kwa kusoma au kibarua na kutelekeza watoto. Wengine huandika barua, hupiga simu na kutuma vitu ila hili si mbadala wa kuwa na mtoto. Watoto wengi wamepata hasira na kuchukia wazazi, wengine wamefanya maamuzi mabovu kwa kutokuwa na uongozi. Baba fulani wa malawi aliyekuja Tanzania kwa vibarua, nilikutana na binti yake Marekani, aliyeniambia kwa hasira baba alivyowatelekeza akiwa na miaka 6. Nilijaribu kumtafuta mzazi huyu Dar na kumpata, alikuwa na hali nzuri, makanika mwenye gereji yake, ila hakuwasiliana na watoto na mke kwa miaka zaidi ya 30. Mama mwingine wa Botswana (daktari) aliyetelekezwa na mume (daktari wa meno), alimwachia mtoto dada yake amtunze mpaka alipokuwa na miaka 16, alienda kumwona, mtoto ili amlete. Mtoto alikuwa na jazba, alimleta mtoto na kuishi naye Washington, na mtoto alimhuzunisha mama kila mara kwa kusema kwamba ametelekezwa mpaka mama alijinyonga mwaka huu. Hii ni habarí ya kweli, maana rafiki yangu ambaye alikuwa dada wa huyu mama aliniambia siku moja kwamba anaenda kwenye mazishi ya mdogo wake aliyepatwa na huzuni hii, mpaka hakujua jinsi ya kusonga mbele. Niliwaza, baba na mama walikuwa na uwezo na makazi makubwa makubwa waliyopokea angalau dola 20,000 kwa mwezi, ila mtoto hawakuchukua hatua nzuri na akawa msumari wa moto kwao. Walikuwa na mtoto mmoja tu! Mara zingine sidhani kama kuna nafasi bora kuishi na watoto! Kama ni Wako, ishi nao tu, kwa shida na furaha.

117. huwa nachukia sana mtoto akiropoka kwangu maneno mabaya. Mfano "sikupendi, mzazi gani wewe", au "nakuchukia sana mama"
Kwa kweli maneno haya ni mazito kwa mzazi, na hakuna mzazi ambaye anaweza kuyastahimili. wasemavyo wahenga, ni kweli "mzazi ni jalala" ni kweli. Angalia maneno haya mtoto anayatoa wapi, na ana maana gani nayo. Jaribu kutafuta moyo wake "mwanangu nipe moyo Wako" zungumza na mtoto sababu ya hasira hizi , na kusema maneno bila ya kufikiri, maneno haya yaweza kuendelea ukubwani kwa walimu, mabosi, mke au hata watoto wake. Mtoto afundishwe jinsi ya kuzungumza hata kama hakupendezwa na kile anachokanywa. Mzazi pia asichokoze, au kumkasirisha mtoto bila sababu. Mzazi aepuke hasira na harara ya kumjibisha mtoto akizungumza haya. Atulie kabla ya kuzumza na mtoto, maana aweza kumdhuru mtoto kwa kauli zake au laana.

Mtoto ni mtoto, na tembo hachoki mkonga wake, mwombe Mungu na kujua sasa una wakati wa kumkunja samaki akiwa mbichi.
Wazazi hapa nasi ni wakati mzuri wa kujua kwamba hasira ni dhambi na si msaada kwa tabia ya mtoto. Hasira ni Pepo, kama tulivyoona wakati Yakobo na Yohana wana wa Ngurumo wakiomba wapewe mamlaka ya kuleta moto uangamize sehemu Kubwa kwa vile walikataa kuamini au kuwakaribisha Luka 9:51-56. Hasira ni chukizo, na ni roho ya chukizo. Twakataza watoto wetu wasiangalie vipindi vibaya, wasiabudu sanamu au wasiseme uongo au kufanya uasherati bali tunaingiza ndani ya nyumba hasira.
Mzazi mmoja alijisifu kwamba yeye hana vipindi vibaya vya TV nyumbani, watoto anawasimamia vizuri, ila alikuwa akipatwa na hasira watoto wanakimbia. Aliposema kwa mshauri kwamba anashangaa watoto wake wana tabia mbovu, aliulizwa “je una hasira?”, alijibu
“mara moja kwa miezi miwili”, Yule mshauri alimwuliza, je ukiwa unaishi karibú na volcano ambayo inalipuka kila miezi miwili utakaa hapo?” au “ukiwa na mbwa anayeuma watu mara moja baada ya miezi miwili, utaendelea kumfuga?”. Hasira na lugha mbaya, wizi, uongo, uchawi na dhambi zingine, ni sawa. Hakuna binadamu ambaye ana hasira akayafanya mapenzi ya Mungu sawa. Yalimkuta Musa, kwa hasira yake alijikuta kwenye shida nyingi.wengine wamefikiri kwamba kuna hasira takatifu (righteous indignation). Nafikiri hii ni Mungu tu Ambaye anaiweza, sisi hatuwezi kuwa na utakatifu na hasira.
Neno la Mungu limetaja hasira mara 585, na mara 470 inazungumzia hasira ya Mungu, mfano kwa Akani, Uza, Joram, Manase n.k. Wazazi tumwombe Mungu tuache hasira, nimeingia mara nyingi kwenye mtego huu na ninamwomba Mungu. Hasira inahusiana sana na kisasi, ukiwa na hasira kwa mtoto, chukua muda kupoza hasira ili hata ukitoa adhabu usifanye kwa kisasi, na mtoto asirithi hasira yako, maana nimeona kwa mifano halisi ikienda kizazi hadi kizazi. Kuna tofauti kati ya hasira na kukazia, wahubiri wengi wamehubiri kwa hasira wakifikiri ni mkazo au ni maadili ya kumsahihisha mtu ila ni hasira.
Basi mtoto anayelipuka na hasira nakusema ovyo ovyo, anabidi asaidiwe, maana Pepo la hasira limeleta maovu au madhara mengi.

maswali haya yamejibiwa kwa fikara au maoni ya mwandishi ambaye anaamini kumcha Mungu ndiyo chanzo cha maarifa. Mwandishi anaamini kwamba kulea mtoto bila msaada wa Mungu ni kitu kisichowezekana. hatuwezi kuishi bila Mwenyezi Mungu na ni lazima tuwaeleze watoto wetu ili wamwabudu na kumjali katika maisha yao ndipo mema yatakaowajia. Watoto bora na wazazi au walimu bora ni wale wanaochukua muda kumtafuta Mungu. Yote yatapita ila Yeye ni wa milele. Yeye ndiye anayetatua matatizo yetu siku kwa siku. Binadamu atakusaidia kidogo tu, ila mkabidhi Mungu atakutatulia yote na Atakupa faraja na kisha uzima wa Milele.

118. Je kuna tofauti gani kati ya malezi ya magharibi na kwetu afrika?

Mengi yanategemea na nyumba au familia, ila magharibi mtoto akifanya kitu anaachwa, hakanywi na majirani au yoyote. Pengine tofauti ni maisha ya kileo na zamani. Kijiji hakihusishwi. Sheria zingine za serikali zinamlinda mtoto mpaka, mzazi anakosa la kufanya, ila akiharibu mambo akifika miaka 18 polisi aweza kumchukua.

Ila mfumo wa elimu unasaidia watoto vizuri magharibi, hata wenye uwezo mdogo wa D wanaweza kumaliza polepole kutokana na kasi yao hata kama ni miaka kumi wamalize shahada. Elimu ya magharibi ina project na vitendo, vitu vinavyohusu maisha ya kila siku, ila elimu yetu haikuwa na project, ila kukariri na nadharia.
Mahali pengine watoto wengine wengine ukiwakanya wanasema wananyanyaswa. Kuadabishwa magharibi mara nyingi kiboko kinapungua kuliko kwetu afrika. Na kule afrika huwezi kumwambia mtoto utachukua michezo yake au wanasesele, kwa vile anatengeneza mwenyewe. Pia kumwambia mtoto adhabu ya 'kakae kwenye kona' haina maana maana, hata hiyo nyumba haina kona vile. Watoto hawaulizwi unataka kula nini, bali twawapa tulicho nacho, mambo ya kulala kwa watu wasio jamaa hayapo. Pia kusifia watoto mpaka kuwapa zawadi wenzetu wanatuzidi.
Watoto afrika wanajiunga kucheza pamoja bila ya kusema 'Je mimi ni rafiki yako au nicheze na wewe' mnacheza pamoja bila sheria au urasmi. Afrika watoto wakiwa wanacheza pamoja, mzazi ukienda dukani unaenda nao, ila hapa unawaambia waende nyumbani kwao, na mara nyingi wakati wa chakula wanaenda kwao. Kuwafundisha watoto maumbile na ngono si wazi, ni kama siri na hayafundishwi wazi labda kwenye jando na unyago. Watoto huambiwa shangazi atawafundisha. Sehemu za siri kwa kingereza ni darasa la sayansi ila lugha zingine za afrika inachukuliwa kama matusi.
Ukiishi na watoto wa kike wa jamaa wanakusaidia kazi za nyumbani, na wanapaswa kuja mapema nyumbani. Kweli mambo ya kileo yana upungufu mwingi wa kiroho ila unene wa miili.
Ila watoto wote ni sawa kwa kucheza, kuchora kwenye udongo, yaani ulimwengu wa mtoto ni sawa kote.

119. kwanini watoto hawaalikwi arusini siku hizi wakati arusi kilikuwa kitu cha wote? Watoto wanaona kwa matendo, kama hawaendi arusini watafanya arusi kweli? Ni kama mahafali ni muhimu kuhudhuria ili waone ni kizuri nao wafanye

(wamechangia watu watatu (Ndugu Essaba, Lima, Mavanza na Odunga)

Kwanza tuanze kwa kuelezea aina zenyewe za Arusi. Kwa arusi za siku hizi hata za wampendao Mungu twaona afadhali watoto wabaki majumbani na wasiyaone hayo yanayofanyika.

Arusi zetu siku hizi zinaisha usiku wa manane sio tena kama enzi hizo arusi inafungwa asubihi na ikifika saa 12 jioni kila mtu anaelekezea au anakaribia kuelekea nyumbani. Maarusi mengi yameondoa sura ya arusi na imebaki sura ya sherehe, mashindano, kujionyesha, fahari na hata uovu mara zingine.

> Kumbi zinazotumika nyingi ni kumbi za starehe zisizoruhusu watoto kuingia kutokana na umri wao hata kwa siku za kawaida. Wakiingizwa kwenye arusi watagundua makubwa. Utukufu wa arusi unaachwa ibadani,na ukumbini ni sherehe, nderemo, Yesu nibebe nibembeleze nibebe . . . . .na nyimbo kama kwaito

watoto pia hawaachwi wacheze au wakae kwao na kufurahia bali wanagombezwa wakikimbia kumbini na kukoseshwa raha kwa muda mrefu wagande mahali fulani kuangalia watu wanaozungumza.
watoto wengi wamesoma kadi 'watoto tunawapenda ila usiwalete' wakashangaa tunawapenda nini?.
Mida yapotea kwa ngoma za kila kabila, babu seya,

Arusi tunamaliza muda mfupi kabla ya asubuhi, haina maana yoyote kwa watoto bali usumbufu.

Arusi zetu tumewakabidhi watu wanaitwa ma-MC, wengine wanawaita "Msema Chochote". Ni kweli hawa watu wanasema chochote. Wakianza kumsifia bibi arusi sisi wakubwa tunashangilia lakini watoto wanaona tusivyo wakweli. Bibi arusi anaambiwa ana macho ya aina fulani mara hivi mara vile, lakini watoto hawaoni hayo anayosema MC! Sisi tunaonekama kama waongo mbele ya watoto.
hata watu wanaokuja kushugulikia wanashangaa mbona arusi hii imejaa uovu?

Leo arusi ni kama deni! Usipo changia hata wewe mwenyewe hualikwi, na kipo kiwango cha fedha ambacho usipofikisha hualikwi achilia mbali na mtoto wako. Ikitokea hujamchangia mtu hata salamu zinapungua, yani kwa ujumla arusi zimechukuwa sura tofauti kabisa na ilivyokuwa. Hayo sio duniani tu, hata kanisani. Arusi hazina kiasi na sura yake inabadilika kutoka kanisani kwenye ukumbini.

Tuwaache watoto wawe salama majumbani au tubadilike kwanza turudi kwenye arusi za asubuhi, zisizo na mbembwe nyingi, MC awe mwongozaji wa arusi mwenye maadili, ukumbi utangaze utukufu wa Mungu na watu wote wajue hivyo.
hebu turudie mapito ya zamani arusi kama ile ya Kana mwujiza wa kwanza ulipotokea. Japo tunawabagua watoto wetu watakuwa madada na makaka mbinguni na si watoto wetu tena. Binafsi sisi tunaona ni jambo baya kutoalika watoto kwenye arusi, na tunashauri turudi mapito ya zamani. Mambo kama ni mabaya japo ya kileo, basi yamepitwa na wakati

1. Katika familia nyingi watoto wengi huwekwa mwishoni kwa kila jambo linalotaka kufanyika unaweza kuona mzazi anavaa suti nzuri sana na ya gharama kubwa lakini watoto wanavaa nguo za mitumba.
2. Sherehe za siku hizi ni biashara kamili kwa hiyo watoto wengi hawana kitu cha kulipia ili wawe na uwezo kushiriki katika biashara hiyo.
3. Sherehe za siku hizi ni sherehe za kidhambi:
Lazima pawe na muziki wa isiyo na minuto ya kusaidia au unaosisimua watu.

Lazima pawe na pombe.
Lazima ifanyike usiku wa manane ili watu wasiwe na aibu.
Lazima ifanyikie kwenye kumbi za starehe ili watu wa kila namna wahudhurie.

4. Wazazi wengi kwa sababu ni waovu hasa uzinzi wanawaona watoto ni wasumbufu sana na wanawanyima uhuru wa kufanya kile wanachotaka kufanya.
5. Siku hizi watoto wanathamani sana wanapokosekana lakini wakipatikana hawana thamani ndiyo maana leo utakuta watoto wanaitwa majina ya ajabu mfano Sikutumaini, Matatizo, Shida, Masumbuko, majina kama haya tayari yanaondoa thamani ya watoto hata mzazi ukimwuliza kwa nini ulimwita mwanao jina hilo anakujibu nilimzaa kwa bahati mbaya!

Maswali haya yamejibiwa kwa mafikara au maoni ya mwandishi ambaye anaamini kumcha Mungu ndiyo chanzo cha maarifa. Mwandishi anaamini kwamba kulea mtoto bila msaada wa Mungu ni kitu kisichowezekana. hatuwezi kuishi bila Mwenyezi Mungu na ni lazima tuwaeleze watoto wetu ili wamwabudu na kumjali katika maisha yao ndipo mema yatakaowajia. Watoto bora na wazazi au walimu bora ni wale wanaochukua muda kumtafuta Mungu. Yote yatapita ila Yeye ni wa milele. Yeye ndiye anayetatua matatizo yetu siku kwa siku. Binadamu atakusaidia kidogo tu, ila mkabidhi Mungu atakutatulia yote na Atakupa faraja na kisha uzima wa Milele.

120. Napenda kupata mwangaza kuhusu teknolojia kwenye nyumba zetu za ibada leo. Pale naishi watoto hata wa miaka 6 wanakuja na vyombo vya teknolojia kama tablet, smart phone, I pod, Nintendo. Wanaleta hivi vyombo kanisa na kusikiilza muziki hata wakati huduma inaendelea, au mhubiri anatoa somo. Kitu kizuri ni kwamba kinawafanya wawe kimya au inapunguza fujo. Ila sijui kama hili ni sawa. Wengi wao wana ukarimu sana wa kushirikia hivi vyombo na wenzao. Utashangaa hata mtoto wa miaka miwili anayoweza kufanya kwenye vyombo hivyo. naelewa wakati wa kuwapa watoto kalamu, rangi na karatasi umepita. Mabadiliko haya yamekuwa haraka mno. Nami kama mama wa watoto wawili, ningependa wakue wakielewa utukufu wa nyumba ya ibda kwa macho yao, hata zaidi yakuwambiwa. Mawazo yamegawanyika sehemu mbili, kuja na Biblia kanisani na vitu vichache vya watoto kasha kuwaambia wasikilize mhubiri au kuwapa vyombo vya kisasa wajishugulishe navyo.
(majibu toka kwa watu kadhaa).

(a)Nafikiri hii ni shida yetu sote wenye watoto. Kama kuna pa kusaidiana ni hapa kwa mashauri ya upendo. msukumo wa rika, na matengenezo ya moyo ndiyo shida. wewe kama mzazi ndiyo unafanya maamuzi. Mambo yakikuharibikia hakuna atakusaidia. hivyo ni vyema kuamua vizuri. Technology ni udhuru tu ila matengenezo ya moyo na kutokuwa na shauku ya vitu vya kiroho ni kwetu wote binadamu, 24/7 tunaandamwa na hili. mzee wetu wa kanisa alisema kama mama watu wazima 5 tu kati ya 100 wataenda mbinguni kwenye nyumba ya ibada, basi ni 5 tu kati ya watoto 1000 wataenda mbinguni. Hata Nuhu alinishangaza kweli hakuwa na wajukuu? Vijana wote watatu hamna mtoto! Sulemani asema mtoto ana ujinga mwingi. Watoto wana majaribu ya kuzama mengi mnooo.

na sasa imekuja kama ulevi hii I pod. Na sisi ndiyo tunanunua! Naona wazungu wengi wa matengenezo wanakiepa hichi kifaa. Tukimwona mlevi na pombe ibadani tutastuka na kuanza kumshambulia, ila sisi watu wazima na watoto, hatujiwezik tu hoi bin taabani. Tunatembea na hivi vitu saa yote, hata kukosa adabu. Siku hizi ukizungumza na mtu mara simu yake imelia hata kama si ya maana, hasemi hata samahani anakuacha kwenye mataa. mtoto wangu wa miaka sita sita aliniambia 'mama unaiependa hii simu kuliko vyote duniani, hata nyumba ikiungua moto tukikuita utakuwa kwenye halo halo tu'. ni ulevi, hakuna ambaye ataangamia nisipopokea simu ibadani, eti mimi ndiyo najidai namwokoa au nashika zamu niko kwenye simu au gadget Fulani saa zote, najidanganya tu. Mungu wake na watu wa karibu ndiyo watamsadia; au mtu akiwa na dharura hiyo ataita ambulance apelekwe hospitali. Hata watu wazima hawaji na Biblia kanisani bali na simu ya mkononi, na wanatuma sms wao kwa wao humo humo nyumba ya ibada.
Nafikiri vyombo hivi watoto siku ya ibada waviache kutumia . Au itafanya wachukie ibada? Hata kila siku watoto wengi hasa wa shule ya msingi wawe wanatumia labda kwa saa moja tu, chini ya uangalizi, maana sasa tunavitumia kama yaya, ila mara nyingi hatujui wanaangalia nini. hata kama si vibaya wanavyoangaliaadui anawatoa kwa mema, wanasema adui wa mazuri sana mazuri kidogo. Adui aona bora awashugulishe wao nasi tu saa yote nikiamika kabla hata ya kusoma Neno la Mungu nipo kwenye mtandao, ni sawa hiyo kweli? Ni ulevi! .Sasa mimi mama mzee nikifanya vile mtoto ambaye mimi ndiye nimempa I pod ataweza kusoma neno la Mungu kweli? mtoto akiwa kwenye I pod nikimwita maombi, anachukia, na mawazo hayawi hapo. tumestruggle na hilo, jamani kumbe wale 144,000 kwenye neno la Mungu ufunuo 7/14 ni wengi mno Ee?
Lazima tuombe usiku na mchana. maana mapigano yetu si ya nyama na damu..... bali hayo hayo tunayoyajua ambayo yako kwenye 'kipaji cha uso ;frontal lobe ' 24/7
kama kuna watoto wanajishugulisha na I pod na vitu vya kuwasaidia kiroho basi watakuwa 1% ,punguza hicho chombo sana.ninajikaza kwangu maana sikuona sababu ya kuwa na hicho chombo, ila mtu mwingine alikileta na mtoto wangu mdogo wa msingi nikasikia anacheka saa nane ya usiku, kumbe yuko kwenye I pod. siku nyingine aliamka asubuhi kama anaumwa, baba yake akasema aende hospitali , kumbe alikuwa kwenye ipod mpaka kunakucha 11 yr old. wapendwa, hivi vifaa kama vina mazuri, nangoja kuona. maana mimi ni mtu wa zamani na ushamba wangu ni mwingi. nachojua tumlilie Mungu. mtoto hutampa kazi anachukia ataka awe kwenye chombo. washiriki wengi naowatembelea ni vile vile. tufanyeje na hivi vyombo? wazazi waweza kuonekana ni waumini, ila wote hakuna anamiliki hivi vyombo kwa hekima, labda tusiwe navyo, ila tukiwa navyo, nani anajua wanachoona kweli?
hata sodoma na gomora ilikuwa nchi ya kisasa na kileo, ila watu waliangamia. tusifikiri sisi ndiyo tofauti na tunajua sana kuliko wale wa Sodoma. Walikuwa majitu yenye akili na nguvu kupita sisi. dhambi yao ilikuwa hawakusaidia masikini, waliishi kwa ubatili, chakula kilikuwa kingi, hawakuwa na la kufanya hivyo vitu vya ovyo ovyo vikawashugulisha. Nasi watoto wetu hawana kazi za

kutosha, tunawakinga na kazi za kulima, kupika na kufua, hivyo watafanya nini kam si vyombo hivi?
tusaidiane mawazo na maombi

- (b) Mzee Mukangara: Ni hakika sisi sote tunahitaji kueliemishwa. '*Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia; basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru'.* Warumi 13:12
- **Technology** iletwayo makanisani leo ni utimilifu wa unabii katika Daniel 12:4 isemwapo kuwa "Maarifa yataongezeka." Linatimia machoni petu.
- Kila baada ya miezi mitatu kuna mabadiliko. Tutafikia ambapo kila baada ya nusu saa ni technolojia mpya!
- **"Kuongezeka kwa Maarifa"** **ni ishara** kwamba, ule mwisho umekaribia. Ni kusema, kaeni 'chonjo'. Kaeni tayari.
- **Kwa wana wa nuru**, maarifa hayo kuongezeka, **ni kwa utukufu wa Mungu**. Habakuki 2:14 *"Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikayo bahari."*
- **Tusiiogope technolojia.** Ndiyo imetuletea **vitabu** na **simu** tuzitumiazo, na **ndege** tupandazo, na **viwanda** vya uchapishaji vinavyochapisha **Biblia** **zetu**, **nguo** tuvaazo, **magari** tuyatumiayo kwendea ibadani na kazini, majengo ya nyumba zetu, **fedha zetu, ATM nk** name it.
- **Walio wa nuru** hawababaiki juu ya tekinolojia.
- **Yale Shetani** ayawekayo humo, wana wa nuru hujiepusha nayo.
- **Shetani ataleta ponografia (umalaya wa picha)**, walio wa nuru hawatajishughulisha nayo. Ataleta kila aina na udanganyifu, lakini Roho wa Mungu atawawezesha kutambua hila na mitego ya Shetani.
- **Shetani asipewe utukufu wa Technolojia.** Si ya kwake. Utukufu huo ni wa Mungu Mwenyezi. Yeye ni 'mkwazaji' tu mwenye hila, akijua muda wake uliosalia **kuswekwa jehanum**, ni mchache. Anatafuta aende na vitoto vyetu na wazazi wao jehanum.
- **Shetani asipewe utukufu** wa mwanadamu kumtii kumwasi Mungu. Mwanadamu huyo ameumbwa na Mungu. Shetani hakuumba hata nzi. Yeye si muumbaji, bali kiumbe. Kazi yake - according to Jesus - ni muuaji tangu mwanzo, na baba wa uongo. Yohana 8:44
- **Tuyapinge na kuyazuia yaliyo ya Shetani** ndani ya technolojia, lakini tusiipinge technolojia. Ni utukufu wa Mungu.

- Watoto hao hununuliwa gadgets hizo na wazazi wao.
- Pale ambapo Shetani atakwaza akili za watoto hao, athari zake ni kubwa. Watoto watajifunza kuwa na miungu mingine.
- Wazazi wao "watalipa" mbele ya Atakayewahukumu wote wenye mwili.

. kuleta vitu hivi ibadani ndiyo twaita

- Hicho twaita mitego ya shetani "the snares of Satan."
- Watoto hufuata wapewacho na wazazi wao.. Wakikatazwa, wataacha. Wakipewa, watapokea.
- Wazazi wa watoto hao hawataiepuka ghadhabu ya Mungu iwapo hawatalitambua hili mapema na kuchukua hatua.
- Siku ibada ni ya Mungu wako!!!!! Tii, uishi, asi ufe. Si siku ya michezo na miziki ya duniani. Kama ni lazima, ni siku ya kutumia gadgets zote kujifunza Biblia ili watoto hao wamjue Mungu na Makusudi yake kuwaleta ulimwenguni. Mwisho wa siku wazazi wanao wajibu wa kuwauliza watoto: leo umejifunza nini? Leo umekariri nini?

Hata kama wanatulia eti hawapigi kelele bado kuna shida maana hawafanyi wanayotakiwa katika mahali pale/

1.. Mtoto akililia wembe, na ukampa, utakuwa umemtuliza. Nakumbuka sheria za Mungunilizozikia kwa baba wa taifa, Mwalimu Nyerere, wakati wa uhai wake. Alisema, "Sheria za Mwenyezi Mungu ziko hivi: Mtoto akichezea moto, utamchoma palepale. Akichezea utelezi, ataanguka palepale. Akichezea wembe, utamkata palepale." Nini kimetokea? Wazazi wa mtoto waliona njia ya kumtuliza huyu kiumbe aombaye shari kana kwamba anaomba heri ni kumkubalia, ili awe 'calmed'. Is that positive wakati mtoto ameungua moto, au amekatwa na wembe, au ameanguka katika utelezi na kuvunjika mkono au mguu?

2.. Nabii **Habakuki** anauambia ulimwengu wote akisema, "*Lakini BWANA yumo ndani ya Hekalu lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele zake."* Habakuki 2:20 SWALI: Ni kwa vipi wakati BWANA yumo katika hekalu lake, wazazi peke yao ndiyo wawe humo, badala ya kuwa na watoto wao, wakafundishwa kuwa kimya mbele za BWANA? (2) Ikiwa Wazazi wamo katika hekalu na watoto wamo katika "Gadgets", je, gadgets hizo ndilo hekalu la Mungu? (3) Kama ndivyo, ni kwa nini wazazi nao wasiwe katika hekalu hilo? (4) Kama sivyo, ni mungu gani aliye katikagadgets hizo? These are rhetorical questions. Kila mmoja ajijibu mwenyewe moyoni mwake.

Kwamba wana ukarimu wa kuwapa wengine:

- Kuna Neno hili la kuaminika kutoka kwenye kinywa cha Yesu katika Mathayo 5:46-47 lisemalo hivi: *"Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo? Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo?"*
- "ukarimu" wafanya watu wanaotafuta haki ya Mungu na wale wanaompenda adui. Waulize wavuta- bangi: watakwambia wanavyosaidiana 'misokoto'. Waulize wavuta-sigara: watakwambia wanavyoisaidiana hata 'vichungi'. Waulize wanywaji wa "Chibuku" wakwambie 'wanavyotikisa' jug na kunywa kwa kushirikiana - mmoja baada ya mwingine.

• Ndivyo Shetani awezavyo kuwatumia watoto wetu, na ukarimu kwa vitu ambavyo si vya msingi "vyema'

• (c) Profesa Bisanda: shida si watoto bali wazazi wanaonunua vitu hivyo. kumbukeni kwamba tunashugulika na kizazi cha Y (generation Y, ambacho ni digital, na wazazi ni Analogue! Teknologia tunayoiona hapa huwezi kulinganisha na vile ambavyo tutavikuta mbinguni. Hebu fikiria Mwenyezi Mungu atapitia rekodi za matendo ya watu wote bilioni nne, walioishi zamani na waliopo leo kwa sekunde au pungufu ya hapo. Je archive yake itakuwa kubwa kiasi gani? Naamini rekodi kule zitakuwa superior (BORA MNO?) kuliko hizi za DVD, USB, n.k

124. Nawezaje kumsaidia mtoto wangu awe na mapungufu mengi!-bonasi!

KANUNI 12 ZA KULEA WATOTO ILI WAWE WATUKUTU

1. Anza tangu utotoni kumpa mtoto kila kitu akitakacho. Kwa njia hii atakuwa akiamini kuwa anapaswa kuishi duniani.

2. Anapojifunza maneno machafu mchekee. Hivyo atajidhania yu mwerevu.
3. Usimpe mafunzo yoyote ya kiroho. Subiri hadi awe na umri wa miaka 21 halafu mwache “ajiamlie mambo yake mwenyewe”.
4. Epuka matumizi ya “hilo ni kosa”, atajisikia hatia. Hili litamfanya aamini baadae kuwa, atakapotiwa mbaroni, jamii haimpendi na anateswa.

5. Okota kila kitu anachoacha ovyo. Mfanyie kila kitu ili azoee kuwatupia wengine kila wajibu.
6. Mtetee dhidi ya majirani, walimu na Polisi. Hao wote wanamchukia mwanao.
7. Gombaneni mara kwa mara mbele ya watoto wenu. Hivyo hawatastuka nyumba itakapovunjika baadae.

8. Mpatie mtoto fedha zote za matumizi anazotaka. Usimwache azalishe za kwake mwenyewe. 3
9. Timiza haja yake ya kila anachotamani, chakula,vinywaji na raha. Hakikisha kila jambo mwili wake unalotamani

linapatikana.

10. Mwache asome kila kilichochapishwa, na asikilize kila wimbo ambao mikono yake itaufikia. Uwe mwangalifu kuhakikisha kuwa vyombo vya chakula na bilauri zote ni safi isipokuwa ubongo wake ulishwe
takataka.

11. Anapokuwa ameingia matatani, jifariji kuwa "nisingeweza kumsaidia lolote".
12. Jiandae kwa maisha ya huzuni. Hakika utayapata.

Yametwaliwa kutoka jarida linaloitwa, '*Kanuni 12 za kulea mtoto awe mtukutu'* linalosambazwa na Polisi wa Houston Texas

125. Mume wangu husafiri safari sana, hii linatuwia vigumu na watoto.

Ni changamoto kubwa, mzazi anaposafiri safari, iwe ni baba au mama. WAtoto wetu tunao muda mfupi, ikiwezekana basi mzazi atafute kazi ya karibu, japo hailipi sana. Ila kuna kazi fulani lazima zifanywe. Basi mzazi aweza kupata maarifa ya kuboresha wakati anaokuwa na watoto. Mfano akirudi watoto waweze kumpokea kwenye kituo cha basi au uwanja wa ndege na kuchukua muda kuzungumza naye. Awapigie simu mara kwa mara, na kuwaandikia barua. Ajitahidi kuwaona walimu wa watoto wake hata kama ni mara chache kwa mwaka. Apate muda wa likizo na kupanga na watoto waende mahali pamoja.

Kwa kweli ni mengi mzazi aweza kufanya akiwa mbali, na kuna vitabu vimeandikwa kwa haya. Na Tovuti itakusaidia mawazo zaidi toka kwa wazazi wengine ambao wanakabiliana na changamoto hii.

126. Njia gani ni nzuri kujenga mahusiano na watoto wangu?

Njia nyepesi 13 za kujenga uhusiano na watoto wako.

1. **Mchukue mtoto pamoja nawe kila mara unapokwenda mahali Fulani kwa gari**. Hii itakupa muda wa kuongea pamoja. Watoto wako watajifunza kutoka kwako wakati unaponunua, unapohudumu, unapoendesha, na watajifunza kutumika pamoja nawe.

2. **Fanya kazi pamoja**. Katika bustani, jikoni na nyumbani. Siyo tu kwamba hii itakupa muda zaidi wa kuongea na kuwafundisha watoto wako katika kazi unazozifanya, lakini pia itaokoa muda wako na kukuachia muda zaidi wa kuwa pamoja nao katika mambo mengine.

3. **Soma vitabu na kuangalia picha pamoja kama familia.** Hata mtoto mdogo kabisa anaweza kufurahia kuangalia picha za kitabuni na kukusikiliza unaposoma kwa sauti. Mbali na kuweka kumbukumbu za pamoja utakuza upendo wa wakujifunza na kujenga fursa kubwa za majadiliano, kuangalia na kujadili picha zinazofaa pamoja pia husaidia watoto wako kukuza stadi muhimu za kufikiri na utambuzi wa kiroho.

4. **Ongea nao - na usikilize!** Chukua muda unapowaingiza kitandani, na waulize siku ilivyoenda au wasimlie hadithi fupi. Wasikilize kwa uvumilivu wanapotaka kukuelezea jambo fulani. Anza hili mapema, na watoto wako wanaopenda kuongea nawe watakapopevuka bado watapenda kuongea nawe.

5. **Onyesha ukarimu na mjumuike pamoja kama familia.** Punguza muda ambao wanao wanautumia na wenzao wa rika moja, na tumieni muda zaidi pamoja kama familia, katika shughuli pamoja, katika kukaribisha familia nyingine nyumbani kwenu, na kuwakaribisha marafiki wa watoto wako nyumbani kwako.

6. **Tafuta miradi ya kufanya kama familia.** Kushiriki malengo ya pamoja mnapoendelea kufanya kazi na kutoa huduma pamoja vitaivuta familia yenu pamoja. Tafuta njia ya kutoa huduma pamoja kupitia kanisa lako, kuwahudumia waliozuiwa na mazingira au katika nyumba za wazee kwa pamoja, anzisheni biashara ndogondogo pamoja, iweni wenyeji wa matukio ya familia nyingine, wasaidieni bibi na babu, anzisheni mifugo, pigeni chombo cha muziki pamoja! Imetolewa bure na Pam Forster, © Doorposts-www.doorposts.com

7. **Onyesha kuvutiwa na vitu vinavyowavutia wanao.** Baba yangu aliliweza sana hili. Usalama nilioupata katika upendo wake na mwelekeo wa maisha yangu vyote vimepata msingi mkubwa kutoka katika karama hii kubwa ambayo ni baba yangu peke yake angeweza kunipa! Kaa usikilize binti yako anapopiga kinanda, nenda kwenye mchezo wa mpira, wewe na kijana wako, jengeni nyumba ya kuchezea pamoja, choreni picha pamoja, furahieni ujenzi wa jengo kubwa, wasikilize hasa.

8. **Waonyeshe watoto wako upendo wa kimwili.** Washike mikono,wakumbatie, sema,"Ninakupenda," na kuwakumbatia tena! Ulimwengu umebadilika eti usipowaleta karibu mwingine atawaleta karibu!

9. **Panga ratiba ya kukutana na mtoto mmoja mmoja.** Ombeni pamoja! Shughulikieni mambo yanayohusu majaribu na dhambi, waambie kuwa uko upande wao, ombeaneni. Jifunze Biblia pamoja. Wafundishe wanao jinsi ya kujifunza Biblia mnapojifunza mada zinazofaa pamoja. Soma vitabu na kujadili pamoja (Mazungumzo kwa msichana, Mungu kazini, Watu wa baadae, Kuvunja ngome na Mawazo kwa vijana ni mifano michache ya vitabu tulivyokwisha soma. Pia tulisoma pamoja vitabu kwa ajili tu ya burudani). Tokeni nje kwa ajili ya matembezi pamoja. Hili tumeligundua kuwa jema hasa kwa vijana wetu wa kiume! Wakiwa njiani huongea zaidi kuliko tukiwa tumekaa nao kwenye viti vya sofa. Tokeni nje mkale pamoja. Si lazima kiwe chakula cha kupendeza

sana. Hata koni tu inaweza kuwapatia muda mzuri kama vile chakula cha gharama. Nendeni nje mkapige kambi! Kila mmoja alipokuwa mdogo, sote "tulipiga kambi nje" pamoja sebuleni kila Ijumaa jioni! Pia tulipiga kambi nje usiku sakafuni pamoja na watoto na makambi ya dharura wakati wa kiangazi juu ya sitaha. Inashangaza ni kiasi gani zaidi watoto wanavyoongea tunapokuwa tumelala pale gizani! Iweni na "kutoka alasiri kwa wasichana" kila mwezi au "kutoka alasiri kwa wavulana". Hili ni wazo ambalo nilitiwa shime kulitekeleza baada ya kusoma kitabu bora kabisa cha Carolyn Mahaney's, Maongezi ya Msichana. Mara moja kila mwezi wasichana pamoja nami tulitoka tu alasiri (au wakati mwingine kwa siku nzima) tukafurahi pamoja. Tulitembelea bustani za maua ya Tulip, Iris, bustani za Mawaridi, migahawa ya chai, maduka ya vitabu, maegesho, na zaidi, na kila mara tulikuwa na wakati mzuri sana. Kila mara iweni na wakati wa kujadili na kuweka malengo. Tulijaribu kulifanya hili angalau mara moja kila mwaka. Ilionekana kuwa ni utaratibu wa msaada mkubwa, na siku zote tulitiwa moyo, tulipoangalia nyuma na kuona ni malengo mangapi yaliyotimizwa mwishoni mwa mwaka uliopita. Angalia ibara ya Pam Foster, © Doorposts – www.doorposts.com

10. **Waadhibu wanao.** Mojawapo ya njia bora kabisa za kuwasilisha upendo kwa watoto wetu ni kuwaadhibu kwa dhati, kwa upendo na pasipo kukoma. Mithali 13:24 inasema, " Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe, Bali yeye ampendaye humrudi mapema". Mtoto aliye huru kufanya lolote apendalo hatajisikia salama katika pendo la wazazi wake. Akiachiwa peke yake, pia atakuwa mtoto mgumu kuonyesha upendo. Karibisha mazingira ya adhabu kama fursa za kuwa karibu zaidi na wanao. Kwa unyenyekevu tukiikabili mioyo yetu yenye dhambi, tukifurahi katika neema ya Mungu na Injili ifunikayo dhambi yetu, tukiomba msamaha nasi tukisamehe – haya yote yatawavuta watoto na wazazi pamoja kama kaka na dada katika Bwana. Karibisha mazingira ya adhabu kama fursa za mafundisho. Tuna mengi ya kuwafundisha watoto wetu katika miaka michache tuliyo nao majumbani mwetu. Kila tabia mbaya, kila dhambi, ni fursa ya ziada ya kuwafundisha toka neno la Mungu.

11. **Sema wazi wazi kazi unayoiona Bwana akiifanya katika maisha ya watoto wako.** Wakia moja ya neno zuri la kutia shime ni bora kuliko ratili ya matengenezo. Tazamia ukuwaji na uwaaambie wanao unavyoona Bwana akitenda katika maisha yao. Unaweza usitambue hili litawatia moyo kiasi gani.

12. **Usijiondoe kupita kiasi.** Wanao wanapohitimu chuo au kufikia umri wa miaka 18, inawezekana kujiengua sana pale ambapo watoto wanafikia umri wa kufanya mabadiliko makubwa maishani (kazi, mwenzi wa maisha, n.k.). Baki ukiwa umeungana na watoto wako ambao sasa wanafikia utu uzima. Fahamu juu ya marafiki zao. Wahamasishe kukaa nyumbani hadi Mungu atakapowaongoza kufikia ndoa. Endelea kutoa miongozo na ushauri, ukitambua kuwa mahusiano yanabadilika wanao wanapofikia utu uzima. Baada ya umri wa kupevuka, tunapasa kubadili majukumu yetu kutoka wenye mamlaka na badala yake kuwa walezi nwashauri wanaotumainiwa.

13. **Mshukuru Mungu kwa ajili ya watoto wako na waombee kila siku.**

131. Ungemshauri mtoto wako nini ambaye amemaliza shule naye anaenda kujitegemea?
Mpendwa Mwanangu Daudi. Sasa unamaliza shule, na hili linatuletea furaha na barka kwetu wazazi. Ni wachache wanamaliza shule ya sekondari na ni asilimia moja tu wanamaliza shahada ya.Kitu kikubwa katika maisha ni kujitambua wewe ni nani, uko hapa duniani kwaajili gani, na unakwenda wapi? Jiulize swali hili mara kwa mara! Mfano wake ni Mimi ni Daudi, Nipo hapa duniani kwa vile niliumbwa na Mungu ila mambo yaliharibika Edeni kwaajili ya dhambi na sasa ukarabati unaendelea ila Naenda mbinguni. Hii itakupa dira katika mambo ya maisha mengi ili usipoteze nafasi nzuri ya kufanya yale yatakayoleta tofauti.
Maisha na uwakili ni kitu kimoja! (Uwakili ni jinsi tunavyotumia maisha yetu) Hebu YEYE Mweza akupe njozi, utume, usongo na nyenzo (vision, Mission, Passion and provision) unapoendelea kufanya kazi. Wachina wasema ukitaka kufanya tofauti kwa siku moja kula chakula kwenye hoteli nzuri. Ukitaka kufanya tofauti kwa mwezi mmoja oa/olewa (mfano mbaya). Ukitaka kufanya tofauti kwa mwaka mmoja panda bustani. Na ukitaka kufanya tofauti maishani 'panda mtu;' yaani saidia watoto kupata elimu, au peleka watoto shule. Utakuwa umemkwamua mtu.

Nilipofika Marekani zaidi ya miaka 26 iliyopita nilimwomba Mungu nikisema akinisaidia kupata kazi nitatoa asilimia fulani baada ya zaka, ya kufanya tofauti katika maisha ya watu nilio na undugu nao na wale ambao sina undugu nao. kwa vile niliona shida daima zinakuja, na pesa inaingia mikononi na kutoka, ila kama unaomba Mungu akuwezeshe kufanya hili baada ya miaka mingi italeta tofauti. Ni vyema unapoanza kazi kufanya hivi, maana sasa utakuwa na mshahara wa kila mwezi usipopanga mambo mengi yatakuja na yatafanya yale ya muhimu yasifanyike (Differentiate between the urgent and the important). Ndugu wengine wa upande wa baba na mama pia usiwasahau. Hata bibi, babu, baba wakubwa/wadogo, binamu au mama wakubwa/wadogo kutuma pesa au zawadi, hata ikiwa ni dola 30 kwa miezi sita, atakukumbuka na kukuombea. Angalial jinsi ya kuinua maisha yao. Ila sisemi wewe mwenyewe ujisahau, La! Panga mambo kama haya na nunua daftari uyaandike, na baada ya miaka mingi ukisoma utatabasamu mwenyewe. Watoto wengi waliozaliwa hapa Marekani na kukua hawajui jamaa na huo ni umasikini wa aina fulani kwa vile hawawezi kufanya tofauti kwa jamaa. Wewe una bahati kwa vile unawajua wengi wa nyumbani. Hebu katika maisha yako uwakumbuke, si kwamba unawiwa ila kwaajili ya upendo kama jina lako linavyosema "aliyependwa" ili ubarikiwe na pia uwasaidie kimaisha. Albert Schweizer mmishonari alisema daima tukumbuke duniani hatuishi wenyewe bali tuna kaka na dada wakiwemo watu wa nchi hii wanaohitaji msaada wetu wa hali au hata mali yaani si waafrika peke yao wenye mahitaji. Naomba Mungu atakuonyesha kipaumbele.
Wachina wasema ukitaka kufanya tofauti kwa siku moja kula chakula kwenye hoteli nzuri. Ukitaka kufanya tofauti kwa mwezi mmoja oa/olewa (mfano mbaya). Ukitaka kufanya tofauti kwa mwaka mmoja panda bustani. Na ukitaka kufanya tofauti maishani 'panda mtu;' yaani saidia watu kupata elimu, au peleka watoto shule. Utakuwa umemkwamua mtu. Maisha ni vita kubwa, kila siku ina pambano lake, ila kumbuka kwamba katika njia zako zote umkiri naye atakuwezesha katika mapito yako yote. Mhubiri alikuwa akikumbuka ujana wake kwamba alijaribu kutafuta furaha katika vitu, wanyama, bustani, wake, chakula, na fahari zote alihitimisha kwa kusema "Mche Mungu na kumtukuza ndiyo

jumla ya mambo yote". Akizungumzia mara 38 kwamba mengine ni kujilisha upepo chini ya jua. Mizania yake inahitaji hekima, hebu omba akupe hekima katika kila hatua.
Ukipata kitabu cha do Hard things na Harris or I kissed dating goodbye ni vitabu vizuri kwa young man, hata hivyo anza na messages to young people. Tofauti ya Daudi na Yusufu ni Yusufu alikimbia, na Daudi alikodoa macho, si anayekimbia ni mwoga ila shetani huwezi ukaanza kujadiliana naye. Kuna vitu vinavyofanya mtu wa Mungu aanguke navyo ni wanawake, mamlala, na pes. Kama kuna mtu anayefikiri hawezi kuangushwa basi atakuwa na hekima kuzidi sulemani, atakuwa na nguvu kuliko Samsoni au atakuwa anampenda Mungu kuliko Daudi.
Maisha yetu duniani tukizaliwa tunasema wacha ngoja niende shule nitakuwa na raha na kuridhika, kisha tunasema wacha nipate kibarua au nichume hela nitakuwa na raha, kisha wacha ngoja nioe/niolewe na kuwa na watoto nitakuwa na raha, kisha wacha nistaafu nitakuwa na raha, kisha wacha nipate wajukuu nitakuwa na raha, kisha wacha watoto wajitegemee basi nitakuwa na raha, mwishowe uzee unaingia na tunasema mimi sina raha na siku hizi mara magonjwa na udhaifu, kisha kuwategemea watu kunaingia. Bibi yangu mzaa mama mwaka wa 1969 alikuja kututembelea tukiwa Arusha, alikuwa na miaka 48, nilimwona ni mzee sana, nikasema bibi wewe ni mzee hivi. Alinijibu 'Grace nilitazama tu upande huu nikigeuka nikajikuta ni mzee!, haikuchukua muda, hata wewe utazeeka na utashangaa miaka imeenda wapi! Mwombe Mungu uwe wakili mwema najua siku moja atakwambia "vyema mtumishi mwema ulikuwa mwaminifu kwa madogo, ingia katika raha yangu ya milele".

Vitu vya dunia vinapungua thamani, leo ***nanunua kitu kipya na kesho huwa najiuliza***. "kwa nini nilipoteza pesa zangu na kitu ***hiki*** kibaya au kibovu, mbona hakivutii". Ila vile vya milele vinavyoleta tofauti hautasikitika.
Kumbuka mambo matano muhimu kwa kila binadamu

1. Mwamini Mungu, na ungama dhambi zako, na Mpende sana
2. Soma Neno la Mungu kila siku
3. Omba bila kukoma kila siku
4. Tafuta ushirika utakaokusaidia kukua na kuishi katika kweli
5. Waambie watu wengine kuhusu habari njema na hukumu inayoujia ulimwengu kwa uhakika
6. Ishi mtindo wa maisha unaoendana na Maandiko
7. Huduma za jamii, yatima, wajane, wazee, wapweke, masikini

Mungu anatupenda sana kuliko tunavyojipenda, naye anataka tukae naye milele kuliko shauku yetu ilivyo
ubarikiwe sana na angalia hatua hizi 7 katika maisha yako ya kila siku
Mama yako

<u>Hatua saba za kuelekea kileleni:</u>

Hatua ya 1:Amka masaa mawili au moja! kabla ya miadi yako ya kwanza au kabla ya kufika kazini. Wekeza masaa ya mwanzo kwa kusoma vitabu vya kiroho, Elimu na vya kutia hamasa. " Masaa ya kwanza ndio gurudumu la kuendesha siku" Unapoamka, jiongezee mwenyewe maarifa ya kiakili ili uwe na siku njema. Utakuwa na mtazamo sahihi, makini, mbunifu na mwenye tija kazini kwa siku yote kama utafanya hivi. Kama

utawekeza katika fani yako saa moja tu kwa siku, hiyo itakuwa ni sawa na kusoma kitabu kimoja kwa juma, na vitabu hamsini kwa mwaka. Mtu mzima kwa kawaida anasoma kitabu kimoja kisicho cha hadithi kwa mwaka. Endapo unasoma kitabu kimoja kwa juma unafikiri utakuwa mkuu katika taaluma yako na kusonga mbele katika hekima dhidi ya watu wengine wote kwenye biashara yako? Ni hakika ndivyo itakavyokuwa! Hiyo itakuwa ni sawa na vitabu 500 kwa mwaka, utahitaji nyumba kubwa ya kuhifadhi vitabu vyako! Hii itakufanya uwe mtu mwenye mamlaka katika taifa lako kuhusiana na taaluma yako kwa miaka mitatu hadi mitano.

Hatua ya 2: Andika tena malengo yako makuu kila siku katika daftari katika wakati uliopo kila asubuhi kabla ya kuondoka, bila kuangalia kile ulichoandika jana. Kitendo cha kuandika na kurudia ni cha kuunda kanuni ya uundwaji wa taarifa katika mfumo wa kuongoza akili yako. Unaporudia kuandika malengo kumi kila asubuhi unataendelea kuona na kufikiri juu ya fursa za kufikia malengo hayo hatimaye. Utakuwa makini, mwenye mwelekeo sahihi na usiyeyumbishwa, utakuwa mtu mwenye malengo na nia thabiti. Na utafanikiwa katika malengo yako kwa haraka zaidi kuliko kama yangekuwa ni mawazo tu yanayoelea katika akili yako.

Hatua ya 3: Kila siku weka mipango mapema. Andaa orodha na panga vipaumbele katika kazi yako kabla ya kuondoka nyumbani. Uwezo wako wa kuona vipaumbele na kuchagua kile ambacho ni cha muhimu zaidi ambacho utakuwa ukifanya kila wakati ni ufunguo wa kupangilia maisha yako na kuzidisha matokeo yake.

Hatua ya 4: Jenga nidhamu ya kushughulisha akili yako yote katika jambo MOJA. Chagua kitu ambacho ni cha muhimu kuliko vyote ambacho unaweza kufanya kila siku. Halafu anza nacho kwanza na kifanyie kazi mpaka kimekamilika kwa 100%. Uwezo wako wa kuwa makini na kufanya kazi, wakati unaendelea na na zoezi la kujijengea hiyo kuwa tabia, yenyewe, itakuwezesha kukuza uzalishaji wako, ufanisi, na matokeo mazuri katika mwezi unaofuata.

Hatua ya 5: Sikiliza vipindi vya kuelimisha katika gari lako: mfanyabiashara wa kawaida anayeendesha gari anatumia masaa 500 – 1000 kwa mwaka akiwa katika usukani wa gari. Unapogeuza gari lako kuwa jingo la chuo kikuu ama darasa la simu ya mkononi unapata elimu sawasawa na kuhudhuria mihula miwili ya masomo ya chuo kikuu wakati unapokuwa unaendesha gari. Watu wengi wamebadilika toka katika ufukara hadi kuwa matajiri kwa kusikiliza vipindi mbalimbali vya sauti kwenye magari yao.

Hatua 6: Uliza maswali mawili ya tafakuri kila baada ya kupiga simu, kuhudhuria sherehe au kukutana na mtu fulani: swali la kwanza ni “Je ni jambo gani nimefanya vyema?” swali la pili “ni kitu gani naweza kufanya tofauti?” Swali la kwanza linakulazimisha kufikiri kwa kina na kukumbuka mambo yote sahihi uliyoyafanya mara ya mwisho ulipokutana na mtu fulani, katika mkutano, ulipofanya uwasilishaji ama sherehe: hata kama haikufanikiwa. Swali la pili linakulazimisha kufikiri juu ya njia mbalimbali tofauti unazoweza kutumia kuongeza ufanisi katika mazingira yaleyale. Andika mawazo haya mahali fulani pia. Njia hii ndiyo ya haraka na zoezi la muhimu zaidi katika ukuaji binafsi na kuendelea kwa mtu.

Hatua ya 7: Mchukulie kila mtu unayekutana naye kama lulu ama thamani kubwa ya fedha: kote nyumbani na ofisini, unapotembelea watu nyumbani kwao na kila unayekutana naye. Unapowachukulia watu kuwa wa muhimu na wa thamani, watarejesha fadhila kwa kukuchukulia kama mtu wa thamani pia. Watatamani kuhusiana nawe, kufanya kazi nawe, na kununua vitu kutoka kwako na kukutambulisha kwa marafiki zao. Anza kwa watu wa nyumbani kwako unapoamka asubuhi, washukuru, kuwa na mtizamo sahihi utajikuta una amani na furaha siku nzima. 85% ya mafanikio yako yanategemea mahusiano yako na watu, usiwe mtu wa kukasirika kasirika.

Contents

1.Sijatafuta title ya kitabu ila pengine: 1

2.–ALFABETI ZA MALEZI YA WATOTO au mzazi wa karne ya 21 au nini? Najaribu kutoa penye Yesu niweke Mungu iwe universal hata kwa waislamu 1

3.(The main thing, is to keep the main thing, the main thing) 1

5.Eli alikuwa amekosa mawasiliano muda mrefu hakujua kinachoendelea. Alishakuwa mzee nno na kukosa kueleweka na watoto ambao ni kizazi tofauti. Alikuwa amepoteza mamlaka yake juu ya wanawe. Watoto wake walikuwa wameharibika sana kitabia kusaidika. 43

1.Mbingu na dunia ndiyo vitabu vya mtoto wa kiume, kabla hajaanza kujua kusoma au kuandika, kama Zaburi 19 inavyosema. Zaburi 144: 12-15 yasema, 'Wana wetu na wawe kama miche waliokua ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni zilizonakishiwa kwa kupamba hekalu. Ghala zetu na zijae akiba za jinsi zote. Kondoo zetu na wazae elfu na makumi elfu, mashambani mwetu ngombe zetu na wachukue mizigo, kusiwe kushambuliwa. Wala kusiwe kuhamishwa. Wala malalamiko katika njia zetu. Heri watu wenye hali hiyo. Heri watu wenye Bwana kuwa Mungu wao.” 94

The Eagle does not fight the snake on the ground. It picks it up into the sky and changes the battle ground, and then it releases the snake into the sky.
The snake has no stamina, no power and no balance in the air. It is useless, weak and vulnerable unlike on the ground where it is powerful wise and deadly.
Take your fight into the spiritual realm by praying and when you are in the spiritual realm God takes over your battles.
Don't fight the enemy in his comfort zone, change the battle grounds like the Eagle and let God take charge through your earnest prayer. You'll be assured of clean victory.
Pray without ceasing. The Eagle does not fight the snake on the ground. It picks it up into the sky and changes the battle ground, and then it releases the snake into the sky.
The snake has no stamina, no power and no balance in the air. It is useless, weak and vulnerable unlike on the ground where it is powerful wise and deadly.
Take your fight into the spiritual realm by praying and when you are in the spiritual realm God takes over your battles.
Don't fight the enemy in his comfort zone, change the battle grounds like the Eagle and let God take charge through your earnest prayer. You'll be assured of clean victory.
Pray without ceasing. 132

Contents 132

7.ASSIGN 05
========== 132

8.ASSIGN 06
==========.....133
9.ASSIGN 07
==========.....135
10.ASSIGN 09
==========.....135
11.ASSIGN 10
==========.....137
12.ASSIGN 11
==========.....137
13.
ASSIGN 12
==========
KANUNI 12 ZA KULEA WATOTO ILI WAWE WATUKUTU.....138
14.
ASSIGN 13
==========
2. KANUNI 11 KWA AJILI YA MARAFIKI ZA WATOTO WETU.....138
15.ASSIGN 14
==========.....139
16.
==========.....139
17.
==========
2.0 KANUNI 11 KWA AJILI YA MARAFIKI YA WATOTO WETU.....140
18.ASSIGN 18
==========.....140
C,INDEX 144
Lisa Jacobson 144
C:\E:Mwalimu Marwa.docx

5.BIBLIA NI RAMANI – Biblia inasema, Ninaamini, na tatizo linaisha.

Kitabu hiki kimebeba fikra ya Mungu, Hali ya mwanadamu, Njia ya wokovu, Hatima ya wadhambi, na furaha ya wenye haki. Mafundisho yake ni Matakatifu, kanuni zake zadumu milele, historia yake ni ya kweli na Suluhisho lake ni la kuaminika, Kisome upate hekima, kiamini ili uwe salama na kijaribu ili uwe Mtakatifu.

Kina nuru ya kukuongoza, chakula cha kukuwezesha, na faraja itakayokujaza furaha. Ni ramani kwa msafiri, Fimbo kwa mahujaji, dira ya rubani, upanga wa askari, na Mkataba kwa Mkristo. Hapa Paradiso hur.ejeshwa, Mbingu hufunuliwa, na milango ya kuzimu hufungwa. Kristo ndiye muhusika mkuu: Wema wetu, muundo wake, utukufu wa Mungu, na mwisho wake. Kitabu hiki hakina budi kujaza akili, kutawala moyo, na kuongoza mapito yetu.

Kisome taratibu, mara kwa mara na kwa maombi. Ni madini ya utajiri, paradiso ya utukufu na mto wa furaha. Kimetolewa kwako maishani, kitafunguliwa wakati wa hukumu, na daima kitakumbukwa milele. Kinatoa kiwango cha juu cha uwajibikaji, Kitatoa ujira kwa kila mtenda kazi bora na kitawahukumu wote waliochezea mambo matakatifu. Kamwe hakuna kitabu kingine kinachoinua akili na kuongeza uwezo wa kufikiri kama Biblia.

Iamini upate hekima, isome uwe salama, Ijaribu uwe mtakatifu.Biblia si kitabu cha kukupatia taarifa bali kitabu cha kukubadilisha. Ni Sauti ya Mungu ikizungumza, tena yenye Mamlaka kuu Mbinguni na Duniani. Bwana amelikuza Neno lake juu ya Jina lake. Mbingu na nchi zitapita lakini si Biblia. Biblia imeshinda kila aina ya changamoto za nyakati zote.

<u>6.Shughuhuli nyingi ni adui MKUBWA WA MAOMBI.</u>

“SHETANI ALIITISHA MKUTANO WA ULIMWENGU: Kuwa na shughuli nyingi Hii ni kanuni ambayo shetani anaipenda kuitumia.
Muovu daima yupo kwa ajili ya kutafuta, kuua na kuharibu. Anahitaji kupora amani yetu na kutajaza na maovu yote yasiyotokana na Mungu. Kadri ambavyo nilitafakari na kugundua katika amani yangu leo, nilikumbushwa jinsi ambavyo shetani hufanya kazi katika maisha ya watu wengi kwa kuwapatia shughuli nyingi na hivyo kuhamisha tafakari yao mbali na Mungu na kuwapeleka katika masuala mengine yasiyo na tija.

Kadri unavyosoma habari hii, hebu na ikusaidie kwa kurejesha mawazo yako kwa mambo ya Kiroho na kuondoa macho yako katika mambo ya dunia hii ambayo kwanza si nyumbani kwetu na muda m,fupi ujao itapita isiwepo tena. Nakutakia Mibaraka na Amani ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Shetani aliitisha mkutano wa roho chafu (mapepo) ulimwenguni kote. Katika hotuba yake ya ufunguzi alisema,
"Mnajua kuwa hatuwezi kuwazuia wakristo wasiende kanisani"
"Hatuwezi kuwazuia wasisome Biblia na kuutambua ukweli"
Na wala kamwe hatuwezi kuwazuai wasiwe na mahusiano ya karibu na Mwokozi wao"
"Punde wanapopata muunganiko huo na Yesu, nguvu yetu ya kuwatawala inavunjika."
" Hivyo waache tu wahudhuria ibada makanisani mwao; waache wapate chakula kizuri kilichofunikwa, LAKINI tuhakikishe kuwa tunapora muda wao, ili kwamba wasipate muda wa kuunganika na Yesu Kristo."

"Hiki ndicho ninachowataka mfanye," Shetani akaawaagiza:
" Muwapumbaze kiasi kwamba wasimfikirie tena Mwokozi wao na kuwa na huo muunganiko wa muhimu kwa siku nzima!"

"Tutawezaje kufanikisha hili?" Mapepo yakauliza.

" Wapeni shughuli nyingi katika mambo yasiyo na umuhimu katika maisha na vumbueni program nyingi za kushika akili zao, mambo ambayo yatawafanya waone fahari kuyatenda, tamaa ya pesa, visasi, wivu, hasira, kutosamehe, na kila aina ya hila" Akajibu
"Wajaribuni katika matumizi, matumizi, matumizi na kukopa, kukopa, kukopa."

"Washawishini wanawake waliolewa kutafuta kazi za kuajiriwa na waume zao kufanya kazi kati ya siku 6-7 kwa juma, masaa 10-12 kwa siku, ili kwamba waweze kupata pesa ya kukidhi mfumo wao wa maisha uliojaa matumizi."
" Wafanye wasipate muda wa kutulia na watoto wao." Kadri familia zao zinavyoparaganyika, ndivyo na nyumba zao hazitaweza kuwaokoa na misongo ya kazini."

"Sisimueni akili zao kiasi kwamba wawe hawawezi kuisikia ile sauti ndogo nyembamba."
" Warubuni kusikiliza miziki ya kidunia, ama kutuma meseji zisizo na umuhimu, wakati wakiwa wanaendesha magari, ama wanapokuwa katika Ibada. Badala ya kufanya Ibada ya maombi wafanye washughulike na vifaa vya teknohama kama IPOD, IPhone, IPAD, CDs, TV n.k. Majumbani Makanisani na hakikisheni kuwa kila duka la kuuza CD na DvD na kwenye kila kumbi za starehe zimejaa program za kupiga miziki ya kidunia tu.

"Hili litajaza akili zao na kuvunja ule muunganiko na Kristo."
"Hakikisheni kwenye kila meza za kahawa mnaweka magazeti ya udaku na umbea"
"Shindilia kwenye akili zao taarifa zisizo na uhalisia kwa masaa 24 kwa siku"
" Wafanye waduae wakati wanaendesha magari yao kwa kuona mabango ya matangazo ya bidhaa yanavyobadilika badilika pembezoni mwa barabara."

“Gharikisheni barua pepe zao kwa jumbe za kitapeli, matangazo ya biashara, michezo ya bahati nasibu, na kila aina ya gazeti la kujaribu bahati, promosheni za kupata bidhaa, huduma za bure na matumaini ya uongo...”

“Wawekeni wasichana wembamba, warembo kwenye magazeti na TV ili kwamba waume zao waamini kuwa uzuri wa nje ndilo jambo la msingi na wao wataanza kutoridhika na wake zao”

“ Wafanyeni wanawake walioolewa wakate tamaa na kuchoka kuendelea kuwapenda waume zao. Endapo hawataweza kuwajali waume zao vyema, wataanza kutafuta wanawake wengine mahali kwingine.”

“Hilo litaharibu familia zao kwa haraka!”
“ Mleteni Father Chrismas mfanye awe mkarimu kwao ili kuwapumbaza wasiwafundishe watoto wao maana halisi ya Kuzaliwa kwa Kristo.”

“Kadhalika wafanyeni wafikiri juu ya vyakula na sherehe za siku za shukrani na Chrismas, ili kwamba wasiwe na muda wa kuomba kwa ajili ya roho mtakatifu kwa ajili ya wokovu wao na wa wengine.”

“ Wapeni mkate wa Pasaka ili kwamba wasizungumze kuhusu UFUFUO Wake na Nguvu kushinda dhambi na mauti au Nguvu ya kuwawezesha KUJISALIMISHA kwa KRISTO kwa hali zote.”

“Hata katika maburudisho yao, yafanyeni yasiwe na maana. Wafanyeni wakitoka katika maburudisho hayo wawe wamepumbuaa na kuchoshwa zaidi, wafanyeni waendelee kutazama picha na kutafuta watu wa kusikiliza visa vya hadithi zao wenyewe.”

“ Msiwape muda wa kwenda kutazama viumbe asili na kutafakari Uumbaji wa Mungu. Wapelekeni katika maeneo ya maburudisho, Michezo, Matamasha na kutazama movie”

“Wapeni shughuli, shughuli, shughuli! Na watakapokutana kwa ajili ya ushirika wa Kiroho, wafanye wapige umbea na vijembe ili watakapoondoka waondoke na dhamira zilizochafuliwa. Bila shaka hili litawafanya wasahau Dhima na Dhamira yao ya kutanganza Injili.”

“ Punde watakuwa wakijitaabisha, kutoa kafara ya afya na familia zao kwa kujaribu, kuunganisha program nyingi pasipo kuhusianisha maombi. Kwa njia hii wataendelea kuwa na shughuli nyingi, bila kugundua tofauti ya kuwa Roho Mtakatifu hayupo katika wingi wa shughuli zao kwani KUTENDA na KUWA ni mambo mawili yasiyofanana.”

“Inawezekana!”
“Inawezekana!”
“Inawezekana!”

Ulikuwa mkakati mzuri!

Mapepo yaliondoka kwa shauku kutekeleza wajibu wao kuwafanya Wakristo mahali popote wawe watu wa shughuli nyingi, usiku na mchana wakitoka hapa na kuelekea kule., huku wakiwa na muda kidogo sana kwa ajili ya Mungu na familia zao.

Hawakupata kabisa muda wa kuwaambia wengine juu ya nguvu ya Kristo kubadili maisha yao, wala hawakuwa na muda wa kuhudhuria ibada kanisani.

Nadhani swali kwa sasa laweza kuwa, je shetani ameweza kufanikiwa katika mkakati wake?
Je umewahi kusikia sauti nyingi zikikuelekeza kutimiza majukumu mengi na kwahiyo unaomba kidogo ambapo ulihitajika kutulia,kwa muda kiasi na ukaendelea kujenga mahusiano na Yesu? Hebu na uwe Hakimu!!!!

"ACRONYM"
UFUPISHO WA NENO LA KIINGEREZA
"B.U.S.Y." is "B-eing U-nder S-atan's Y-oke"?
(Kuwa chini ya kongwa la Shetani?)

7.**Kwanini tuombe? MAOMBI NI JIBU**
" Maombi ni jibu la kila tatizo maishani. Mara nyingi hatuombi kwa mazingira Fulani maishani, kwasababu kutoka sehemu tulipo, tunaonekana kupoteza tumaini, lakini hakuna jambo lisilowezekana kwa Mungu.
Hakuna jambo lililofungika kiasi kwamba haliwezi kupata tiba. Hakuna mahusiano ya wanadamu ambayo yameharibika kiasi kwamba Mungu hawezi kurejesha suluhu na maelewano.
Hakuna mazoea ambayo yamekita mizizi kiasi cha kushindikana kutibika.
Hakuna aliye mdhaifu kiasi kwamba hawezi kupata nguvu tena.
Hakuna aliye mgonjwa kiasi kwamba hawezi kutibiwa tena
Hakuna aliye mjinga kiasi kwamba hawezi kuwa na akili tena
Chochote tunachohitaji ama kustahili, kama tunamwamini Mungu, Atatupatia.

Kama kuna jambo lolote la kututia hofu na mashaka, hebu na tuache kuutazama ugumu wake na tumwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji, Upendo na nguvu Herald OCT 7, 1865.

Kama unahitaji kufanya jambo Fulani kwa ajili ya Mungu, unda kamati, na endapo unahitaji Mungu afanye jambo fulani kwa ajili yako omba...

9.**Kanuni zinazohusiana na MAMLAKA katika familia yetu...**

1. Tunampenda na kumtii Bwana wetu, Mungu kwa unyenyekevu wa moyo wote
2. Tunasoma Biblia na kuomba kila jambo kwa Mungu kwa moyo mnyoofu
3. Tunawajali na kuwatii wazazi wetu katika Bwana bila kuonesha hali ya dharau
4. Tunakubali kukosolewa na kuonywa kwa moyo wa unyenyekevu.

Kuhusiana na masuala ya MAHUSIANO katika familia yetu....

5. Tunapendana, kwa kuchukuliana kwa huruma, utu na staha
6. Tunasaidiana, kwa upole tunatanguliza mahitaji ya wenzetu kabla ya mahitaji yetu.
7. Tunatiana moyo, kwa kutumia maneno yale tu yanayojenga tabia njema na kubariki wengine.
8. Tunasameheana, kwa kufunika kosa kwa upendo pale tunapokosea ama kuwakosea wengine.

Kuhusiana na UMILIKI WA MALI katika familia yetu.....

9. Tunashukuru Mungu kwa kile tulicho nacho, kwamba kiwe kidogo ama kingi.
10. Tunaridhika kwa kile tulicho nacho, na sio kutamani vingine wengine walivyo navyo.
11. Tu wakarimu kwa vile tulivyo navyo, kwa kushiriki kwa uwazi na wengine.
12. Tunajali vile tulivyo navyo, kwa kuvitumia kwa busara na kwa umakini.

Kuhusiana na KAZI katika familia yetu.....

13. Tunabidii kukamilisha kazi kwa uaminifu na kwa umakini tunapoombwa kufanya hivyo.
14. Tunachukua juhudi binafsi kufanya kazi zetu zote pasipo kuhitaji kuambiwa
15. Tunafanya kazi kwa roho ya ushirikiano, kwa uwazi tunatoa na kupokea msaada.
16. Tunafanya juhudi binafsi kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani yanadumu kuwa masafi muda wote.

Kuhusiana na TABIA katika familia yetu.....

17. Tunachagua kuwa na furaha, hata pale ambapo tunahhisi tulitakiwa kulalamika
18. Tunachagua kuwa wapatanishi, hata pale tunapojihisi kupisana kauli.

19. Tunaamua kuwa watulivu, hata pale tunapojihisi kama tunashindwa kutulia
20. Tunaamua kuwa wapole, hata kama tunahisi hatukutakiwa kuwa hivyo.

.

Kuhusiana na CHAGUZI katika maisha yetu…..

21. Tunafanya kile tunachojua kuwa ni sahihi, bila kujali wengine watasema nini.
22. Tunauliza kabla ya kutenda, pale ambapo hatujui nini sahihi cha kufanya
23. Tunajaribu kujizuia mar azote na kwa kila hali.
24. Daima tunasema ukweli na kamwe hatujaribu kusema uongo wa aina yeyote.

10 JINSI YA KUTOKUWA NA FURAHA MAISHANI

Jifikirie Mwenyewe
Jizungumzie mwenyewe muda wote
Tumia kiwakilishi "mimi" mara nyingi iwezekanavyo
Jipime muda wote kwa kutumia mawazo na maoni ya wengine
Sikiliza kwa shauku kuhusu kile wengine wanasema kukuhusu wewe
Kuwa na mashaka
Tarajia watu wakukubali
Kuwa na wivu na tamaa
Kasirika kwa kila anayekutukana
Kamwe usisahau kukosoa wengine
Usimwamini mtu yeyote isipokuwa wewe mwenyewe
Sisitiza watu wakukumbuke na kukuheshimu.
Lazimisha mawazo yako juu ya kila jambo yaheshimiwe.
Kasirika endapo watu hawakukumbuki na kukupa fadhila.
Usisahau huduma uliyowahi kutoa.
Daima tegemea nyakati njema kwa ajili yako.
Jaribu kukwepa majukumu yako kama utaweza.
Wajali watu wengine kwa kiwango kidogo sana kadri inavyowezekana.
Jipende mwenyewe kupita kiasi.
Kuwa mbinafsi.
Kanuni hizi zitakuhakikishia kutokuwa na furaha maishani.

Njia nyepesi 11 za kujenga uhusiano na watoto wako.

1. **Mchukue mtoto pamoja nawe kila mara unapokwenda mahali Fulani kwa gari.** Hii itakupa muda wa kuongea pamoja. Watoto wako watajifunza kutoka kwako wakati unaponunua, unapohudumu, unapoendesha, na watajifunza kutumika pamoja nawe.

2. **Fanya kazi pamoja.** Katika bustani, jikoni na nyumbani. Siyo tu kwamba hii itakupa muda zaidi wa kuongea na kuwafundisha watoto wako katika kazi unazozifanya,

lakini pia itaokoa muda wako na kukuachia muda zaidi wa kuwa pamoja nao katika mambo mengine.

3. **Soma vitabu na kuangalia picha pamoja kama familia.** Hata mtoto mdogo kabisa anaweza kufurahia kuangalia picha za kitabuni na kukusikiliza unaposoma kwa sauti. Mbali na kuweka kumbukumbu za pamoja utakuza upendo wa wakujifunza na kujenga fursa kubwa za majadiliano, kuangalia na kujadili picha zinazofaa pamoja pia husaidia watoto wako kukuza stadi muhimu za kufikiri na utambuzi wa kiroho.

4. **Ongea nao - na usikilize!** Chukua muda unapowaingiza kitandani, na waulize siku ilivyoenda au wasimlie hadithi fupi. Wasikilize kwa uvumilivu wanapotaka kukuelezea jambo fulani. Anza hili mapema, na watoto wako wanaopenda kuongea nawe watakapopevuka bado watapenda kuongea nawe.

5. **Onyesha ukarimu na mjumuike pamoja kama familia.** Punguza muda ambao wanao wanautumia na wenzao wa rika moja, na tumieni muda zaidi pamoja kama familia, katika shughuli pamoja, katika kukaribisha familia nyingine nyumbani kwenu, na kuwakaribisha marafiki wa watoto wako nyumbani kwako.

6. **Tafuta miradi ya kufanya kama familia.** Kushiriki malengo ya pamoja mnapoendelea kufanya kazi na kutoa huduma pamoja vitaivuta familia yenu pamoja. Tafuta njia ya kutoa huduma pamoja kupitia kanisa lako, kuwahudumia waliozuiwa na mazingira au katika nyumba za wazee kwa pamoja, anzisheni biashara ndogondogo pamoja, iweni wenyeji wa matukio ya familia nyingine, wasaidieni bibi na babu, anzisheni mifugo, pigeni chombo cha muziki pamoja! Imetolewa bure na Pam Forster, © Doorposts- www.doorposts.com

2. 12. KANUNI 12 ZA KULEA WATOTO ILI WAWE WATUKUTU

3.1 Anza tangu utotoni kumpa mtoto kila kitu akitakacho. Kwa njia hii atakuwa akiamini kuwa anapaswa kuishi duniani.

3.2 Anapojifunza maneno machafu mchekee. Hivyo atajidhania yu mwerevu.

3.3 Usimpe mafunzo yoyote ya kiroho. Subiri hadi awe na umri wa miaka 21 halafu mwache "ajiamlie mambo yake mwenyewe".

3.4 Epuka matumizi ya "hilo ni kosa", atajisikia hatia. Hili litamfanya aamini baadae kuwa, atakapotiwa mbaroni, jamii haimpendi na anateswa.

3.5 Okota kila kitu anachoacha ovyo. Mfanyie kila kitu ili azoee kuwatupia wengine kila wajibu.

3.6 Mtetee dhidi ya majirani, walimu na Polisi. Hao wote wanamchukia mwanao.

3.7 Gombaneni mara kwa mara mbele ya watoto wenu. Hivyo hawatastuka nyumba itakapovunjika
baadae.

3.8 Mpatie mtoto fedha zote za matumizi anazotaka. Usimwache azalishe za kwake mwenyewe.
3.9 Timiza haja yake ya kila anachotamani, chakula,vinywaji na raha. Hakikisha kila jambo mwili wake unalotamani linapatikana.

3.10 Mwache asome kila kilichochapishwa, na asikilize kila wimbo ambao mikono yake itaufikia. Uwe mwangalifu kuhakikisha kuwa vyombo vya chakula na bilauri zote ni safi isipokuwa ubongo wake ulishwe takataka.

3.11 Anapokuwa ameingia matatani, jifariji kuwa " nisingeweza kumsaidia lolote".

3.12 Jiandae kwa maisha ya huzuni. Hakika utayapata.

Yametwaliwa kutoka jarida linaloitwa, *Kanuni 12 za kulea mtoto awe mtukutu* linalosambazwa na Houston Police.

2. KANUNI 11 KWA AJILI YA MARAFIKI ZA WATOTO WETU

2.1 Wazazi huamua lini, wapi na akina nani watoto wao wanaweza kucheza nao.
2.2 Marafiki hawaruhusiwi kwenda nyumbani kwao mtu yeyote, au kwenda popote, hapo wazazi wao wameruhusu kufanya hivyo.

2.3 Marafiki hawana budi kuheshimu sheria za nyumba za wenzao na viwango vyao wakati wote na mahali popote
.
2.4 Marafiki hawana budi kuwa wema kwa watu wote wa familia za wenzao.
2.5 Marafiki wanaweza tu kuchezea vitu vya michezo vya wenzao endapo wapo tayari kuviomba kwanza, kuwa waangalifu na kuvirudisha pale walipovitoa kabla hawajaondoka.

2.6 Marafiki wanaweza kugawa au kuazimishana vitu endapo tu wamepata idhini kwanza kufanya hivyo kutoka kwa wazazi wa wenzi wao.

2.7 Marafiki hawawezi kuondoana wasimalize kwa furaha shughuli za kifamilia pamoja na kazi za shule.

2.8 Marafiki wasisababishe wenzao kukosa huduma za kanisani au shughuli nyingine muhimu za kifamilia.

2.9 Wanafamilia ndio marafiki zetu walio muhimu zaidi. Hivyo kaka na dada hawana budi kuwa waaminifu kila mmoja kwa mwenziwe.

2.10 Watoto ambao wanasababisha au wanasema vitu vinavyosababisha wenzao wasiwe watiifu hawataruhusiwa kucheza pamoja tena hadi hapo watakapoomba msamaha kila mmoja kwa wazazi wa mwenzake.

2.11 Marafiki wanaweza kuingizwa na kuwa miongoni mwa shughuli maalum za wenzao endapo wameonyesha kuwa wanaweza kucheza pamoja vizuri katika matukio mengine.

na Greg na Josh Harris

5.Tabia za mwanamke mkali anayeburuza wengine

1. Husimama mwenyewe kama mamlaka binafsi. Utambulisho wake umejengeka katika mtizamo potofu ya kuwa maisha yake ni jukumu lake binafsi na uhuru wake ndilo jambo la thamani kubwa
2. Daima anavutwa na tamaa ya kutaka Zaidi, tamaa zake kamwe si rahisi kuzitosheleza
3. Hatambui kuwa kutokuwa na shukrani, majivuno, na mashaka ndio vichocheo vya maisha yake.
4. Huhamasika na vitu vilivyo na umuhimu kwake, anaishi na dhana ya ubinafsi
5. Anatamani kupendwa na kubembelezwa, lakini anaweza kuumia sana anapohisi kukataliwa
6. Anaingia kwenye magomvi mara kwa mara, akichanganya tabia ya ukatili na ushujaa
7. Ana shauku ya madaraka na hakuna mtu ama chochote cha kumzuia katika kufanikisha hilo
8. Anatumia uwezo wake kumnyanyasa mumewe na wengine, anaweza asijulikane kama mnyanyasaji ila kitendo chake cha ukosoaji, mtizamo hasi na uzungumzaji wa sauti kali ni kama tindikali
9. Ni mkali na si muwazi na huona fahari kufanya hivyo
10. Mara nyingi huingia katika migogoro na wengine
11. Anaweza kudai kuwa Neno la Mungu ndiyo mamlaka yake kuu, lakini kusoma kwake ni kama kitabu cha kitaaluma, haimsaidii kurekebisha mahusiano yake na wenzake.
12. Mara nyingi haoni shida kuzozana, lakini nia yake ni kwa ajili ya manufaa binafsi ama faraja na mwenendo wake waweza kuwa wenye kudharau wengine.

Hutembea kwa kiburi na jeuri lakini ni kipofu kwa kukosa unyenyekevu. Anaona tabia ya unyenyekevu kama ishara ya udhaifu. Anaamini kwa dhati kuwa tabia ya kutofautiana na wenzake inatokana na wao kuwa na uwezo mdogo, kutokuwa watu wa kiroho, ama tabia ya kutojiamini.

13. Anataka kuwa mtawala wa wengine na amefanikiwa kukuza uwezo wa kuwa juu yaw engine kwa kutumia hila na mbinu za ujanja ujanja

14. Hata kama hawezi kukubali, maisha yake yamejengeka katika ubinafsi. Anaridhika tu pale anapopata mambo yanayomhusu;

Hatua saba za kuelekea kileleni:
Hizi ni hatua saba katika kanuni ya asilimia 1.000 ambazo zitakushangaza endapo utazifanyia mazoezi kama mzazi

Hatua ya 1:Amka masaa mawili kabla ya miadi yako ya kwanza au kabla ya kufika kazini. Wekeza masaa ya mwanzo kwa kusoma vitabu vya kiroho, Elimu na vya kutia hamasa. "Masaa ya kwanza ndio gurudumu la kuendesha siku" Unapoamka, jiongezee mwenyewe maarifa ya kiakili ili uwe na siku njema. Utakuwa na mtazamo sahihi, makini, mbunifu na mwenye tija kazini kwa siku yote kama utafanya hivi. Kama utawekeza katika fani yako saa moja tu kwa siku, hiyo itakuwa ni sawa na kusoma kitabu kimoja kwa juma, na vitabu hamsini kwa mwaka. Mtu mzima kwa kawaida anasoma kitabu kimoja kisicho cha hadithi kwa mwaka. Endapo unasoma kitabu kimoja kwa juma unafikiri utakuwa mkuu katika taaluma yako na kusonga mbele katika hekima dhidi ya watu wengine wote kwenye biashara yako? Ni hakika ndivyo itakavyokuwa! Hiyo itakuwa ni sawa na vitabu 500 kwa mwaka, utahitaji nyumba kubwa ya kuhifadhi vitabu vyako! Hii itakufanya uwe mtu mwenye mamlaka katika taifa lako kuhusiana na taaluma yako kwa miaka mitatu hadi mitano.

Hatua ya 2: Andika tena malengo yako makuu kila siku katika daftari katika wakati uliopo kila asubuhi kabla ya kuondoka, bila kuangalia kile ulichoandika jana. Kitendo cha kuandika na kurudia ni cha kuunda kanuni ya uundwaji wa taarifa katika mfumo wa kuongoza akili yako. Unaporudia kuandika malengo kumi kila asubuhi unataendelea kuona na kufikiri juu ya fursa za kufikia malengo hayo hatimaye. Utakuwa makini, mwenye mwelekeo sahihi na usiyeyumbishwa, utakuwa mtu mwenye malengo na nia thabiti. Na utafanikiwa katika malengo yako kwa haraka zaidi kuliko kama yangekuwa ni mawazo tu yanayoelea katika akili yako.

Hatua ya 3: Kila siku weka mipango mapema. Andaa orodha na panga vipaumbele katika kazi yako kabla ya kuondoka nyumbani. Uwezo wako wa kuona vipaumbele na kuchagua kile ambacho ni cha muhimu zaidi ambacho utakuwa ukifanya kila wakati ni ufunguo wa kupangilia maisha yako na kuzidisha matokeo yake.

Hatua ya 4: Jenga nidhamu ya kushughulisha akili yako yote katika jambo MOJA. Chagua kitu ambacho ni cha muhimu kuliko vyote ambacho unaweza kufanya kila siku. Halafu anza nacho kwanza na kifanyie kazi mpaka kimekamilika kwa 100%. Uwezo wako wa kuwa makini na kufanya kazi, wakati unaendelea na na zoezi la kujijengea hiyo kuwa tabia, yenyewe, itakuwezesha kukuza uzalishaji wako, ufanisi, na matokeo mazuri katika mwezi unaofuata.

Hatua ya 5: Sikiliza vipindi vya kuelimisha katika gari lako: mfanyabiashara wa kawaida anayeendesha gari anatumia masaa 500 – 1000 kwa mwaka akiwa katika usukani wa gari. Unapogeuza gari lako kuwa jingo la chuo kikuu ama darasa la simu ya mkononi unapata elimu sawasawa na kuhudhuria mihula miwili ya masomo ya chuo kikuu wakati unapokuwa unaendesha gari. Watu wengi wamebadilika toka katika ufukara hadi kuwa matajiri kwa kusikiliza vipindi mbalimbali vya sauti kwenye magari yao.

Hatua 6: Uliza maswali mawili ya tafakuri kila baada ya kupiga simu, kuhudhuria sherehe au kukutana na mtu fulani: swali la kwanza ni "Je ni jambo gani nimefanya vyema?" swali la pili "ni kitu gani naweza kufanya tofauti?" Swali la kwanza linakulazimisha kufikiri kwa kina na kukumbuka mambo yote sahihi uliyoyafanya mara ya mwisho ulipokutana na mtu fulani, katika mkutano, ulipofanya uwasilishaji ama sherehe: hata kama haikufanikiwa. Swali la pili linakulazimisha kufikiri juu ya njia mbalimbali tofauti unazoweza kutumia kuongeza ufanisi katika mazingira yaleyale. Andika mawazo haya mahali fulani pia. Njia hii ndiyo ya haraka na zoezi la muhimu zaidi katika ukuaji binafsi na kuendelea kwa mtu.

Hatua ya 7: Mchukulie kila mtu unayekutana naye kama lulu ama thamani kubwa ya fedha: kote nyumbani na ofisini, unapotembelea watu nyumbani kwao na kila unayekutana naye. Unapowachukulia watu kuwa wa muhimu na wa thamani, watarejesha fadhila kwa kukuchukulia kama mtu wa thamani pia. Watatamani kuhusiana nawe, kufanya kazi nawe, na kununua vitu kutoka kwako na kukutambulisha kwa marafiki zao. Anza kwa watu wa nyumbani kwako unapoamka asubuhi, washukuru, kuwa na mtizamo sahihi utajikuta una amani na furaha siku nzima. 85% ya mafanikio yako yanategemea mahusiano yako na watu, usiwe mtu wa kukasirika kasirika.
te:

Ubongo wako ulivyoumbwa yapasa uyafanye haya.

1. Fikiria kama ambavyo mazoezi ya viungo humsaidia yeye afanyae, ndivyo nawe inavyokuwa unapoizoesha sehemu ya mbele ya ubongo wako kufikiri, uwezo wako wa kufikiri unaongezeka.

2. Kuwa mtu anayependa ukweli, kuwa na shauku nao, tunashindwa kuufikia ukweli kwa sababu Mungu hana ukomo, Naye huudhihirisha upendo wake kwetu kila siku (Maandiko, Sayansi na uzoefu)

a. Jifunze na ufurahie Amri za Mungu na kanuni zake. Sheria ya Upendo, Sheria ya uhuru.

3. zithibitishe nadharia zote kuhusu Mungu kwa kutumia maandiko

4. kwa kulingana na ushahidi wa tabia ya Mungu Uaminifu wa kiwango cha juu na tabia ya upendo, jisalimishe kwake. Anza kila siku kwa kumualika Roho wake.

5. tafakari kila siku kuhusiana na tabia ya Mungu ya upendo na ufahamu, Ukweli uliojazwa na shukrani, na tafakari juu ya Mungu na ufalme wake wa upendo na kazi ya uumbaji.
6. Mwamini Mungu katika maisha yako, siku za usoni na matokeo yake baada ya kuelewa uaminifu wake na kupitia uzoefu wake.

7. Fanya mazoezi ya kanuni za Mungu. Ishi bila choyo, kwa kuwapatia wengine, jitolee na tafuta kuwashirikisha wengine kile Mungu alichokupa. Kadri unavyotoa ndivyo utakavyopokea.

8. Tafuta namna ya kushiriki ukweli kuhusiana na ufalme wa Mungu na upendo kwa wengine, jiunge na taasisi zinazojishughulisha na kudhihirisha upendo wa Mungu ulimwenguni. Anzisha huduma, ongoza masomo ya biblia, shirikiana na waumini mlio na mtizamo sawa wa kiimani. Ushirika hukuza uwezo na maarifa, hudhihirisha upendo wa Mungu katika kuponya na kuhuisha.
9. Ishi kwa kulingana na mpango wa Mungu wa maisha ya kimwili. Jiepushe na sumu zinazoweza kudhuru mwili na roho kama vile, tumbaku, pombe, madawa ya kulevya, viburudisho, michezo ya kupigana, kusoma vitabu vya kidunia, ama mambo yanayohafifisha tabia ya Mungu.

10. Fanya mazoezi ya mara kwa mara ya viungo na ukuaji wa mishipa ya fahamu, pamoja na chembechembe za kusawilisha kiwango cha hasira.
11. Pata muda wa kutosha wa kupumzika, kunywa maji, vuta hewa, kula vizuri na kulala ili kwamba ubongo wako usije ukaathirika katika uwezo wake wa kufanya kazi.
12. Ishi kwa kulingana na kanunu ya Mungu ya Asili. Kula vyakula vyenye afya, hakikisha unatoa uchafu mwilini, pata mwanga wa jua, utapunguza magonjwa mengi.
13. Samehe: usishikilie jambo kifuani, Kutunza hasira kifuani kunakufanya kuwa mtu wa hofu na mashaka na hatimaye hupunguza Amani na afya kwako
14. Usiwe na hatia: inapunguza Amani, na kuongeza mashaka, na inawathiri wengine wasio na hatia, ungama dhambi zako na endelea na maisha.
15. Kama hofu na mashaka imekujaribu ili kutenda kinyume na dhamiri yako ili kwamba upate ukubali wa wenzio, kumbuka kujiweka pembeni na kujiuliza.

a. Ukweli ni nini? Kipi ni sahihi? Kipi kina afya? Na kipi kinastahili? Je nifanyeje?

b. Jiulize mwenyewe endapo mtu fulani amekukataa ama amekukasirikia kwa kufanya kile unachoamini kuwa ni sahihi je huyu aweza kweli kuwa ni rafiki yako, je unahitaji ukubali wao?

c. Kuwa tayari kuwaweka watu wengine huru kufikiri ama kuhisi kadri watakavyo kuhusiana na wewe. Endapo unafikiri " kama nikifanya kile wanachohitaji, basi hawatanikasirikia". Basi jaribu kuwaacha huru wafikiri kadiri wanavyochagua kufikiri juu yako na utakuwa huru kutokana na misongo ya kutaka kuridhisha matakwa yao.

d. Kumbuka upendo hufanya kile kilicho sahihi kiafya na kimantiki, kwakuwa ndivyo, si kwakuwa inasikika vizuri wakati huo. Tazama ng'ambo na utumie kanuni hizi za Mungu hata kama zinaonekana kuwa ngumu kwa wakati huo.

e. Daima MTAZAME YESU, ishi kwa ujasiri katika uzuri wa MUNGU, ukijua ukweli wa SHERIA YAKE ya upendo, mpango wa maisha, kwa moyo wako wote itazamie siku ya YA MAREJEO YAKE.

Sheria 21 za nyumba yetu

by Gregg Harris

1. We obey God.
Tunamcha, Tunampenda na kumtii Mungu
2. We love, honor and pray for one another.
Tunapendana, tunaheshimiana, na tunaombeana
3. We tell the truth.
Tunasema kweli bila kuleta ulaghai
4. We consider one another's interests ahead of our own.
Tunatanguliza mbele maitaji ya wenzetu kisha yetu
5. We speak quietly and respectfully with one another.
Tunazungumza zizokuwa za kufoka, na kwa heshima
6. We do not hurt one another with unkind words or deeds.
Hatuumizani na maneno makali
7. When someone needs correction, we correct him in love.
Pale mtu anapohitaji masahihisho, tunamsahisha kwa upendo
8. When someone is sorry, we forgive him.
Akiomba msamaha tunamsamehe
9. When someone is sad, we comfort him.
Mwenzetu akiwa na huzuni tunamfariji
10. When someone is happy, we rejoice with him.
Mwenzetu akiwa na furaha, tunafurahi naye
11. When we have something nice to share, we share it.
Tukiwa na kitu cha kushiriki pamoja tunashirikiana
12. When we have work to do, we do it without complaining.
Tukiwa na kazi ya kufanya, tunafanya bila malalamiko
13. We take good care of everything that God has given us.
Tunatunza alivyotupa Mungu kwa uwakili aliotuusia
14. We do not create unnecessary work for others.
Hatufanyi kazi ya wengine kuwa ngumu
15. When we open something, we close it.
Tukifungua kitu tunakifunga tena (e.g begi, bomba)
16. When we take something out, we put it away.
Tukitoa kitu nje tunakirudisha tulipokikuta
17. We read the Bible and pray every day
Tunasoma Neno la Mungu, tunaomba kwa moyo ulio tayari kujifunza na kutenda hata yaliyo mapya
18. When we make a mess, we clean it up.
Tukichafua mahali, tunasafisha vizuri
19. When we do not know what to do, we ask.

Tusipojua la kufanya kitu tunauliza
20. When we go out, we act just as if we were in this house.

Kanuni za familia yetu

Sally Clarkson

Kuhusu mamlaka ya nyumba yetu

.

Tunampenda na kumtii Mungu, kwa mioyo yetu yote
Tunasoma Neno la Mungu na kuomba kila siku na moyo mkunjufu
Tunawaheshimu na kuwatii wazazi wetu na ari njema
Tunasikiliza mausia na kukubali adhabu kwa roho ya unyenyekevu

Kuhusu mahusiano kwenye familia yetu

Tunapendana na kuchuliana kwa wema, upole na adhabu
Tunahudumiana kwa unyenyekevu, tukifikiria mahitaji ya mwenzetu kwanza
Tunatiana moyo, kwa kutumia maneno ya kujenga na kubariki.
Tunasameheana, na kuyasahau hayo kwa upendo hata pale tulipoumizwa na kukwazwa

Kuhusu umilikaji wa familia yetu

Tunamshkuru Mungu kwa vyote tulivyonavyo, vidogo au vikubwa
Tunaridhika na tulivyonavyo, hatutamani walivyonavyo wengine
11. We are generous with what we have, sharing freely with others.
Tu wakarimu kwa tulivyanavyo, tunashirikiana na wengine kwa moyo mkunjufu.Tunasaidiana kwa tulivyo navyo, tukivitumia kwa hekima na kuwajibika

Kuhusu Kazi katika familia yetu

Tunanuia kumaliza kazi tuliyopewa kwa uaminifu na kwa muda wake.
Tunanuia kumaliza kazi tuliyopewa, bila ya kukumbushwa kumbushwa
Tunafanya kazi kwa moyo mkunjufu, tunasaidiwa na kusaidia wengine bila kinyongo
Tunachukua jukumu la kuweka nyumba yetu nadhifu na safi wakati wote

Kuhusu mtazamo wa familia yetu

Tunachagua kuwa wacheshi, hata pale tunapojaribiwa kunung'unika
Tunachagua kuwa wapatanishi, hata tupatapo majaribu ya kubishana bishana
Tunachagua kuwa wavumilivu, kinyume cha nia zetu
Tunachagua kuwa watu wa shukrani, kinyume cha vishawishi vya kibinadamu

Kuhusu uchaguzi wa familia yetu

Tunafanya yale ambayo yanapasa haki, hata wengine wakitushawishi mengine
Tunauliza kabla ya kutenda, pale ambapo hatujui lile jema kulifanya
Tunatawala nafsi kwa hali na mali wakati wote
Tunasema kweli daima, na tunaepuka ulaghai wa aina yoyote

Tukienda popote kwa wengine, tunafanya haya 21 mema kama vile tu tupo kwetu

Tukikiuka au kusahau sheria 21 za Nyumba hii, tunakubali hatua za nidhamu na maagizo toka kwa Mungu

Kuweka kwenye index za nyuma

Lisa Jacobson

Njia za kumwandaa mvulana awe Mwanamume bora

1. **Mche Mungu ndiyo chanzo cha hekima.** Mithali 1:7
2. **Sikiliza kwa makini.** Mwanamume mwenye hekima husikiliza na kujifunza mengi, Mithali 1:5
3. **Tilia maanani maagizo ya baba yako.** Utafurahi kwa hilo. Mithali 1:8
4. **Usiyasahau mafundisho ya mama yako.** Ana hekima kwako. Mithali 1:8
5. **Tawala hasira.** Yeye anayetawala hasira ni bora kuliko shujaa, ni zaidi ya anayeteka mji. Mithali 16:32
6. **Tunza ahadi zako.** Mwanamume anasema na kufanya aliyosema.
7. **Usishikamane na wale wasiomjali Mungu.** Mwatu waovu wanaharibu tabia njema 1 Kor 15:33
8. **Wekeza kwenye urafiki mzuri na bora.** Marafiki ambao ni msaada zaidi ya ndugu wa damu. Mithali 18:24
9. **Fanya yanayohitajika bila kuambiwa.** Usingoje kuambiwa wakati unajua unachopaswa kufanya.
10. **Uwe mtanashati.** Usivae ovyo, uonekana nadhifu na msafi.
11. **Mtegemee Mungu, na siyo akili zako.** Mithali 3:3-5
12. **Usipuuzie masahihisho.** Chukulia kama nafasi ya kujifunza na kukua. Mitahli 3:11
13. **Julikana kama Mfanyakazi bora.** Jifunze kufurahi kazi yako na fanya lolote jema linalotakiwa kulifanya.

15. **Uwe na usafi moyo, mawazo na matendo . Kuna nguvu kwenye usafi**

16. **Uwe mwungana.** Uungwana ni kipimo cha mwanamume kama vile ujasiri ulivyo.

17. **Fanya mazoezi, usijiachie mwili wako utepete tepete.** Kijana anapashwa kuwa na nguvu, na aliye tayari kufanya yanayobidi kufanywa/

18. **Uwe wakili wa wa watoto na wanyonge kwako.** Usiwe mtu wa juu sana kwa walio chini.

19. **Hudumu kwa unyenyekevu kama Mwanamume bora.** Usiache mtu akutoe kwenye ubora, Fuata mfano wa Mungu kwenye Wafilipi 2

20. **Wasaidie wanawake/wadada.** Wafungulie mlango, wapishe kiti, wasaidie kubeba mizigo. Walinde na kuwatetea,

21. **Jitoe kujifunza masomo mengi unavyoweza.** Soma vitabu, fanya utafiti, chunguza na uliza maswali.

22. **Wape heshima wale waliokuzidi umri.** Wasalimu kwa salaam zinazotakiwa, wape mkono, na sikiliza yale wanayosema.

23. **Kimbia dhambi, Toroka mara kwa haraka kama Yusufu unapokumbana na majaribu.** 1Tim 6:11

24. .

25. **Uwe jasiri kama simba.** Mtu mwenye haki hana haja ya kuona aibu kuhusu yale yasiyo ya haki. Mithali 28:1.

26. **Mpende Mungu sana na Neno lake.** Amebarikiwa mwanamume ambaye anafurahia sheria ya BWANA. Zaburi 1

e. Njia za kumtayarisha msichana awe bora
f. Lisa jacobson

.

1. **uwe mpole na maneno, hata matendo yako.** HEbu uzuri wako uonekana kwa upole wako na roho iliyotulia. 1 Petro 3).

2. **Uwe jasiri.** Kama mwanamke utakabiliana na mambo ambayo yatahitaji uwe imara na mwenye akili bora zilizotulia. Mithali 31:25

3. **Ishi maisha ya usafi wa moyo, mawazo na matendo.** Kuna uzuri wa kuishi maisha safi.

4. **Chagua furaha.** Utabariki wote wanaokuzunguka na uso wenye ucheshi. Isitoshe ndiyo njia nzuri ya kuishi

5. **Chagua furaha.** Utabariki wale wanaokuzunguka na uso wenye ucheshi. Isitoshe ndiyo njia bora ya kuishi.

6. **Itafute hekima.** Hekima ya kweli yatoka mbinguni tu. Yakobo 3

7. **Uwe huru kucheka.** Itakufanya uburudike na wale waliokuzunguka utaondoa kiwingu kwao.

8. **Shugulikia afya yako. Hakikisha unakula vyakula bora, unafanya mazoezi, na kupata wasaa wa kupumzika. Jitunze vizuri, ndivyo utakavyoweza kusaidia wengine pia.**

9. **Zungumza maneno ya matamu.** Watu wataweza kukuzikiliza ukifanya vile, kuliko kuwasuta na kuwakosoa kosoa.

10. **Uwe tayari kufanya kazi kwa bidii.** Jifunze kufurahia kazi, na kushugulikia lolote linalobidi kufanya.

11. **Imba kwa sauti.** Nyimbo za kumtukuza Mungu hubadilisha mtazamo (mood) humpa Mungu utukufu, HEbu imba kwa sauti kubwa! Zaburi 98:4.

12. **Soma mambo mbali mbali.** Amua kuwa mwanafunzi wa kudumu. Jifunze yanayohusu bustani, Historia, kuoka mikate, lugha mpya, tiba mbadala, jiografia, na mengine mazuri yanayokupendeza moyo

13. **Angalia wale wenye mahitaji.** Uwe na huruma kwa wengine, na tumia talanta zako kuwabariki

14. **Leta uzuri katika maisha yako nay a wengine.** Iwe ni maua, usanii, mashairi, kazi za mikono, au rangi zinazovutia

15. **Tembea kwenye matatizo na changamoto ukiishika imani.** Usitembee kwa nguvu zako mwenyewe bali mtumaini BWANA MWEZA naye atakubeba

16. **Vaa kwa adabu, Utapendenza na utafurahia 1 Tim 2:**9

17. **Wekeza kupata marafiki wazuri.** Chukua muda kupata marafiki wema watakaokutia moyo, kuhuisha na kukupa changamoto kukubariki

18. **Tayarisha vyakula vitamu vitamu.** Wabariki wanaokuzunguka na talanta zako za upishi.

19. **Tumia muda ukiwa peke yako kusoma Neno la Mungu na kulitafkari .** Kamwe usiwe mwenye shuguli nyingi wakati wa Muda wako na Mungu

20. **Uwe mwema kwa wengine.** Wema si ghali kutenda, ila unaleta mvuto mkubwa kwa wale wanaokuzunguka. Mithali 31:26

21. **Serve cheerfully.** Look to Christ as your example, not what the world says about service. Nothing begrudging or stingy there (Phil. 2).

22. **Hudumu kwa ucheshi.** Mwangalie Kristo mfano wetu, na siyo dunia inavyohudumu watu. Usiwe mlalamika au bahili. Wafilipi 2

23. **Ombea mambo yote.** Usitatue mambo mwenyewe, nenda kwa BABA yako wa mbinguni na furaha zako, huzuni zako na shida zako. Efeso 6:18.

24. **Chunga unayosema.** Maneno au ulimi una nguvu kujenga au kubomoa, hivyo yatumie vizuri

25. **Wapende watu saana.** 1 Wakorintho 13

Vitabu, CD au DVD zilizotumika kunukuliwa au kupata mawazo

1. Misingi ya huduma ya mtoto. Learn and Share publishers. Arusha Tanzania. Dr Emmanuel Mbennah, 2008

2. How to Have Kids With Characters Even if Your Kids are Characters by Nadine Brown . Tyndale House Publishers in, Wheaton, Illinois. USA, 1990.

3. It is Your Money Isn't It?. Practical Money Management for Christians. Review and Herald. 1993. Edward Reid. Hagerstown M.D.

4. Morris. The Blessed life. DVD

5. Successful Parenting. Ann and John Murphy. St Pauls Edition. 1983. Boston MA, USA.

6. Parenting Your Child by the Spirit. By Sally hohnberger. Pacific Press Publishing Association, Nampa Idaho, USA. 2005

7. Uponyaji wa Mungu. By Dr Ann Mc Neilus and Moses Mwalumbili. African Herald Publishing House. Kendu Bay , Kenya.

8. Balanced Living by Vicki Griffin. Balancedlivingliterature.com

9. You Never stop being a parent: The Myth of Empty Nest . Helen Hosier.

10. Biblia takatifu. The Bible Societies of Tanzania. Dodoma 1994.

11. Adult children. The secrets of Dysfunctional families, John and Linda Friel. Health Communication Inc, Deerfield beach. Fla, USA. 1988

12. Ministry of healing. Pacific Press. Idaho, USA. Ellen G White.

13 Child Guidance. Pacific Press. USA. Ellen G White

14. Nusuru Ndoa Yako. Pastor David makoye, Morogoro Tanzania.

15 The Medical Missionary. Harvestime books.2004

16. Bringing up Your Child. A Homegrown Perspective. Jane Kaibiria. 2009. Aura creations. Nairobi Kenya

17. Dr James Dobson. Answers your Questions About Raising Children. And Parenting is not for Cowards. 1974. Tyndale House. Wheaton IL, USA.

18. Successful Parenting. Ann and John Murphy. St Paul.1983. Boston Ma.

19. Huduma ya Doorpost.org. USA

20.Mr and Mrs Nyantika. Raising Children for eternity, Kenya.

21. Dr Lehman. Have a New Child by Friday. USA

22. Changing the Heart of a Rebel , Freedom From Anger, Dating and what to Expect when a Child is 12 years old by Dr Davis. Solvefamilyproblems.com USA

23 Visit these websites for more: Revivingourhearts.org, fly.com (finallyloveyourself), onewithoutwords, doorpost.org, 21rules in this house, Breakingsilencenow.org, aboverubies.

24 On line bible school (www.bibleschools.com/1416)

25 James Dobson. Preparing for Adolescence. Straight talk to teens and Parents. Regal books, Ca, USA

26 Dorothy Moore. Home grown Kids CD.

27 Anger. Dr Davis. CD.

28. Difference between Dating and Courtship. Dr Davis

29 websites : Reviveourhearts.com, aboverubies.com, amazingdiscoveries, fly.com, doorpost.org